

# USUFI

Njia ya kuelekea kwenye kuiingiza imani moyoni (Ihsan)



Othman Nuuri Topbash





Dar Es Saalam - 2014

As-Salaam Islamic Center  
Plot 354 Mbezi Beach, Makonde, Dar Es Salaam - Tanzania  
Cell: +255 254 734 362,  
Email: aic2013@gmail.com

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kutolesha sehemu yoyote ya toleo hili, kuitunza katika mfumo utakaowezesha kunakiliwa au kukisambaza katika aina au namna yoyote ile, iwe elektroniki, kuchapa, kunakilisha, kurekodi au vinginevyo bila kupata ruhusa kutoka kwa mwenye haki miliki.

**ISBN:** 978-9944-83-684-5

Mwandishi:	Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu:	Abdi Mohamed Adam
Mfasiri:	Hemedi Dhuli Hemedi
Mhariri:	Ibrahimu H. Kabuga
Msanifu jalada:	Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na:	Sarkhan Isgandarov Nijat Garibov

# **USUFI**

**NJIA YA KUELEKEA KWENYE  
KUIINGIZA IMANI MOYONI  
(IHSAN)**

**Othman Nuri TOPBASH**



بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

وَاللَّهُ  
أَعْلَمُ  
بِذَاتِ  
الْعَرْشِ  
الْعَظِيمِ

وَاللَّهُ  
أَعْلَمُ  
بِذَاتِ  
الْعَرْشِ  
الْعَظِيمِ

اِنْسِرُوا نَافْسِكُمْ  
اَلْاَرْضَ وَالسَّمَاوَاتِ  
اَلْاَرْضَ وَالسَّمَاوَاتِ  
اَلْاَرْضَ وَالسَّمَاوَاتِ  
اَلْاَرْضَ وَالسَّمَاوَاتِ

قَدْ اَفْلَحَ مَنْ كَتَبَهَا \* وَقَدْ خَابَ مَنْ رَدَّتْهَا \* كَذَّبَتْ ثَمُودُ بِطَغْوَاهَا \* اِذِ ابْتِغَتْ  
اَشْقَاهَا \* فَاَتَاهُ رَسُوْلُ اللهِ نَاقَهُ اللهُ وَسُقِيَهَا \* فَكَذَّبُوهُ فَعَقَرُوْهَا \* فَدَمَّرَهَا  
عَلَيْهِمْ رَبُّهُمْ بِدِيْنِهِمْ فَيَسُوْا \* وَلَا يَخْفَى عَقْبُهَا \* كَتَبَ الْاِنجَالِ عَلَيْهِمْ حُفُوْاهَا

*“Kwa jina la mwenyezi mungu mwingi wa rehema mwenye kurehemu.*

*Naapa kwa jua na mwangaza wake! Na kwa mwezi unapo lifuatia! Na kwa mchana unapo lidhihirisha! Na kwa usiku unapo lifunika!*

*Na kwa mbingu na kwa aliyeijenga! Na kwa ardhi na kwa aliyeitandaza! Na kwa nafsi na kwa aliyeitengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake!*

*Hakika amefanikiwa aliyeitakasa, Na hakika amekhasiri aliyeiviza.”  
(Ash-Shams, 1-10)*

Vitu anavyoviapia Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an vina umuhimu wa kipekee katika istilahi za kidini, lakini mafunzo yanayofuatia vitu hivi yana maana kubwa zaidi. Hivi ndivyo ilivyo katika aya za Qur'an zilizotangulia, lakini kuna tofauti kidogo: Katika aya hizi Mwenyezi Mungu ametoa viapo saba kwa mfuatano kabla ya kutaja somo halisi ambalo ni nafsi, anasema, “Hakika amefanikiwa aliyeitakasa, Na hakika amekhasiri aliyeiviza.” (Ash-Shams, 9-10)

Ni jambo la kuvutia kwamba hakuna mada nyingine ndani ya Qur'an iliyofuatishwa kwa viapo vitakatifu kama hivi tofauti na kuitakasa nafsi, imeletwa baada ya viapo saba. Jambo hili linatosha kuashiria umuhimu na ulazima wa kuitakasa nafsi kwa ajili ya uongofu wa mwanadamu. Hivyo kitabu hiki chenye kichwa habari “Kutoka kwenye imani (iman) mpaka kwenye kuingiza imani ndani ya moyo (ihsan)”, ni mkusanyiko wa maelezo mengi kuhusiana na mada hii muhimu kama ilivyothibitika kupitia kwenye maneno ya watakatifu wa Mola pamoja na matendo yao.







## Dibaji

Shukurani zote njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye amempulizia mwanadamu roho itokanayo na Yeye na kumjaalia tafakari ya kimetafizikia na tafakari kubwa zaidi; na amani iwe juu ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake - ambaye kama mfano wa kuigwa na wanadamu amefurahia zaidi kupewa kwake zawadi hizi takatifu.

Hapana shaka kwamba usufi unawakilisha moyo, kiini na mwelekeo wa kiroho wa uislamu. Uislamu unasifu tabia za kibinadamu za kiroho na mapenzi yaliyo ndani ya nyoyo za waumini mpaka kufikia kileleni, hasa pale ambapo kiini hiki na imani ya kiislamu vinapokuwa katika namna ya matendo yaliyo katika vitendo vya watu wanaojiweza. Hii inamaanisha kwamba usufi umebeba miongoni mwa miti yenye matunda mengi ya elimu ndani ya bustani la uislamu. Kulingana na mlengwa, Usufi umeelezewa katika miundo mikuu mitatu:

1. Kwanza kabisa kwa ajili ya wasomi.
2. Kwa ajili ya wasomi na watu wa kawaida.
3. Kwanza kabisa kwa ajili ya watu wa kawaida.

Baadhi ya kazi za kisufi zimeandikwa hasa kwa ajili ya watu waliendelea zaidi kielimu katika mwendo wa kisufi. Katika kipengele hiki tunaweza kutaja *Fusus al-Hikam* iliyoandikwa na Ibn Arabi (aliyefariki 1240) na *al-Insan al-Kamil* iliyoandikwa na Abdulkarim al-Jili (aliyefariki 1403). Kazi nyingine kama vile *Mathnawif* ya Jalaladdin Rumi (aliyefariki 1273) zimeandikwa kwa ajili ya wote watu wenye elimu za juu na watu wa kawaida; hapa watu wa kawaida wataweza kunufaika na kazi hizo kulingana na kiwango cha uelewa wao. Aina hii ya pili ya kazi hizi huwasaidia wale waliojifunza sayansi za dhahiria ili kuweza kutambua lengo kuu la elimu zao, elimu ambazo ni za Mola. Bado baadhi ya kazi kama vile *Anvar ul-Ashiqiriy Muhammediye* iliyoandikwa na Ahmed Bican (katika karne ya 15) na Yazicioglu Mehmet (aliyefariki 1451), na *Nafakhat al-Uns* iliyoan-





dikwa na Abdurrahman Jami (aliyefariki 1492), zote hizi zimeandikwa kwa ajili ya watu wa kawaida. Kazi hizi zinalenga kuchangia katika kujenga misingi imara ya kinadharia na kivitendo kwa watu wa kawaida ambao tayari wana uelewa wa misingi ya dini na hivyo kuweza kuboresha imani zao.

Utofauti huo wa kazi za kisufi unatokana na juhudi za kutaka kuwezesha jamii za madaraja yote ziweze kuelewa uislamu kulingana na uwezo wao wa akili. Hivyo watu wenye elimu zaidi na watu wa kawaida huweza kuutekeleza uislamu vilivyo, ndio maana mababu zetu wakafikia kuuita utaratibu huu wa pande mbili za elimu kuwa ni wenye “bwawa mbili”.

Kwa kuzingatia mgawanyo huo Usufi huweza kuifikia jamii ya mwanadamu ya kila daraja. Kwa upande mmoja unaifanya jamii iwe macho dhidi ya nyakati za furaha kiuchumi na kiutulivu, wakati kwa upande mwingine unawatuliza watu kwa kuwapa njia za kutokea kwenye matukio ya hatari wakati wa shida. Kwa upande mmoja usufi unawaweka waumini wenye kutenda mema mbali na hisia za usalama na uhakika kuhusiana na mwisho wao wakati upande mwingine unawapa matumaini waovu kwa kupitia rehema na msamaha wa Mola usio na mipaka. Hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Anatolia wakati wa uvamizi wa Mongolia, tukio ambalo lilileta ukatili na mahangaiko katika ardhi. Lakini kilikuwa ni kipindi hicho ambapo sufi wengi wasomi na taasisi zake mbalimbali zilienda kwenye tukio kwa ajili ya kuwahenga wakazi wa Anatolia na kutuliza maumivu yao makali.

Leo hii ambapo mwanadamu amezungukwa na matatizo na tabu kama hizo, bila shaka usufi unaweza kuwasaidia wanadamu waweze kuyakabili matatizo hayo, kwa kutoa suluhisho la kinadharia na kivitendo. Kwa hakika ndugu zetu wengi ambao ndio wametoka kutoroka kwenye nira ya ushirikina wanahitaji na kutafuta tiba ya kiroho, kama ndege waliojeruhiwa. Vivyo hivyo watu wengi wa mashariki na magharibi ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakitaabika kutokana na dhana ya wayakinifu sasa hivi wamekuwa na ari ya kutaka kuufahamu uislamu kama ulivyofundishwa na sufi wa mwanzo. Kukua kwa mapenzi yao juu ya kile wanachokiona kutoka kwenye mifano dhahiri ya watu hao kumewapelekea kuishia kuukubali uislamu kwa moyo wao wote.

Nukta zote hizi zinaashiria kwamba Usufi unawakilisha ubainifu wa wazi wa uislamu na bila kusahau zawadi kubwa ya baraka na ubora mikononi mwa waumini. Kwa hiyo Usufi unachukua nafasi kubwa katika





kuwasaidia waislamu ili waweze kuboresha hali yao kidini, na wakati huo kuwapelekea wasio waislamu mafunzo sahihi ya uislamu na hatimae kuwavuta katika uislamu na kuwatengenezea njia ya kuweza kuipenda dini. Ili kuwa na uhakika na mafunzo yake usufi umekuwa kioo chenye kuakisi mwenendo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kuuhamisha kwa vizazi vilivyofuata mpaka siku ya mwisho. Kwa sababu hiyo ndio maana msukumo na mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mjumbe wake – rehema na amani ziwe juu yake – vimekuwa vikisimumua nyoyo za waumini wakati wote tokea mwanzo wa uislamu, dini ambayo itabakia mpaka siku ya mwisho. Ndio maana uislamu unaendeleza uwepo wake na ushawishi wake licha ya udhaifu wa waislamu wengi kulingana na mazingira ya sasa ya dunia.

Maadui wa uislamu wanaojidhihirisha na waliojificha wamekuwa wakijaribu kuutenganisha usufi na uislamu, vitu ambavyo kiuhalisia vinakwenda pamoja kama mwili na roho. Wanadai kwamba usufi unaleta mtazamo tofauti na uislamu. Uelewaji wake mbaya juu ya usufi unawaingizia mkanganyiko wale wenye ari ya usufi na kuwafanya wasielewe uhalisia wa mambo. Hivyo maelezo sahihi juu ya usufi ni suala muhimu katika ulimwengu wa leo. Licha ya kurekebisha mkanganyiko kuhusiana na usufi, lakini pia kitabu hiki kimeleza kubainisha uzuri wa dhana hii kama tulivyokwisha elezea kwa ufupi, haya yote ni kwa ajili ya zile nyoyo na akili zenye ari juu ya usufi. Kwa msingi huu dhana ya usufi ni kama bahari isiyo na mipaka; inatawanyika pamoja na kazi za wanachuoni ambazo zinaelezea fikra na matendo sahihi yanayoendana na njia hiyo.

Kulingana na mwenendo huu wa wanachuoni tumejaribu kutoa mchango mdogo, licha ya kwamba juhudi zetu ni kama tone moja ndani ya bahari. Kwa mtunzi kufikia kwenye thamani ya tone moja kunatosha hali ya kuwa kitabu hiki kinafanya kazi kama daraja la kuziunganisha nyoyo na Mola wao; hata hivyo kimsingi usufi ni hali ya akili (*hal*) zaidi kuliko maneno yanayotolewa (*qal*).

Katika kitabu hiki kwanza kabisa kinatoa maudhui ya ujumla ya Usufi, na baada ya hapo kinaendelea kwa kuelezea nukta muhimu za itikadi hii ya kiislamu kama vile elimu juu ya Mola (*marifatullah*), kumpenda Mola (*mahabbatullah*), kuitakasa nafsi (*tazkiyatun-nafs*), kuutakasa moyo (*tasfiyatu'l-qalb*), mwenendo wa kisufi wa kuigwa katika utekelezaji wa mambo (*ushub*), na nyingine kama hizo. Kwa kawaida mifano tunayoitoa inatoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, na





kufuatiwa na wanachuoni wakubwa katika uislamu ambao si wengine bali warithi wa Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake. Tumekuwa tukiyafanyia kazi baadhi ya mambo yenye kutatanisha yahasuyo nukta muhimu katika usufi, lakini ni kulingana na hoja za ujumla na si kulingana na hoja za mtu mmoja mmoja. Pia tumegusia kwa umakini baadhi ya mambo yanayotekelezwa na baadhi ya wasomi kimakosa, mambo ambayo yapo mbali na mwenendo wa kisufi. Kama ambavyo tutaona, tumesema kwamba mambo haya hutokea ama kwa sababu ya ujinga au upuuziaji wa wahusika.

Kwa ufupi ni kwamba ingawa kazi hii imeandikwa rasmi na mtunzi lakini kilichopo ndani yake si kingine bali mkusanyiko wa kazi za watakatifu wa Mola. Msukumo na uzuri wote unaopatikana katika kazi hii ni kioo chenye kuakisi ulimwengu wa kiroho wa watakatifu hao kuelekea kwetu. Kazi yetu imekuwa ni kukusanya na kuziweka pamoja taswira hizi kulingana na mahitaji na mazingira yaliyopo. Matokeo yake tumefaidika sana kutokana na kazi zilizotangulia za usufi, vile vile kutoka kwa marafiki zetu wengi ambao kwetu ni kama “vitabu vinavyoishi”. Ni heshima na furaha kwetu kulitaja jambo hili.

Na kwa kumalizia tu ni kwamba hatuna budi kusema kwamba dua zetu za dhati ziwaendee wale watu ambao Mola amewataja katika kazi hii na marafiki zetu kutoka chuoni ambao wametusaikia katika kufanikisha kazi hii.

***Ewe Mola! Licha ya udhaifu na upungufu wetu katika kuelezea dhana za mwenendo wa kisufi, tupatie baraka zako na jaalia maneno yetu yawanufaishe wasomaji wetu! Ewe Mola! Tujaalie sisi na wasomaji wetu fadhila zako zisizo na mipaka kutokana na jitihada hii iliyofanywa kwa moyo safi na unyenyekevu!***

***Amin!***

**Othman Nuuri TOPBAS**

Uskudar, Istanbul, 2002





---

# SURA YA KWANZA

---



## USUFI NI NINI?

### A- ASILI YA USUFI

#### B- MAANA YA USUFI

- 1- Mwenendo wa kisufi unawakilisha mfano wa maaadili (*akhlaq*) na adabu (*adab*).
- 2- Mwenendo wa kisufi unahusiana na kuutakasa moyo na nafsi.
- 3- Mwenendo wa kisufi ni mapambano ya kiroho yasiyoisha.
- 4- Usufi unamaanisha usafi wa moyo (*ikhlas*)
- 5- Usufi unamaanisha kusimama kwa ushupavu katika njia iliyonyooka (*istiqama*)
- 6- Mwenendo wa kisufi ni (*rida*) na kujisalimisha (*taslimiyyah*)

#### C- MADA YA USUFI

#### D- LENGU LA USUFI

#### E- ULAZIMA WA KUFUATA USUFI

#### F- UHUSIANO WA USUFI NA MADHEHEBU MENGINE

- 1- Fani za kiislamu
  - a- Thiolojia (*Kalam*)
  - b- Ufafanuzi wa Qur'an (*Tafsir*)
  - c- Maneno na mwenendo wa Mtume Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake – (*Hadith - Siyar*)
  - d- Sheria (*Fiqh*)
- 2- Sayansi asilia
- 3- Fasihi
- 4- Sanaa
  - a- Muziki
  - b- Usanifu majengo
  - c- Kaligrafia
- 5- Falsafa

#### G- ELIMU YENYE MANUFAA





“Sema, nimemuamini Mwenyezi Mungu na kisha uwe na msimamo.”

(قل آمنّا بالله ثم استقم) (Muslim, Iman 62)



# Usufi ni nini?

## A. ASILI YA USUFI

Zaidi ya baraka Zake zisizohesabika, Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia mwanadamu kuwa na ubora wa kipekee, ubora wenye thamani kubwa. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameutaja ukweli huu ndani ya Qur'an pale aliposema, “**Na Nikampulizia roho inayotokana na mimi**” (al-Hijr, 29) Kutokana na hayo Mwenyezi Mungu anawataka waja wake wampende na kumuabudu ili wapate sehemu ya elimu yake na kuwa karibu yake.

Pia Mwenyezi Mungu mtukufu amewajaalia wanadamu kuwa na ubora wa kipekee ili waongozwe katika muelekeo huu. Licha ya ubora huu wa ujumla pia amewajaalia ubora maalum baadhi ya waja wake ambao amewapatia kazi ya utume. Huu ni ubora wa ziada kwa wanadamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika kipindi ambacho hakukuwa na Mitume miongoni mwa wanadamu, Mola wetu aliendelea kuwabariki wanadamu wa kawaida kwa kuwachagua baadhi ya waja wake ambao walifuata nyayo za Mitume ili wawaongoze watu katika njia iliyonyooka.

Taasisi ya utume inawakilisha baraka za Mwenyezi Mungu kwa mwanadamu. Katika kuwapa wanadamu utume, Mwenyezi Mungu mtukufu alifungua taasisi hii kwa kumuweka Adam - amani iwe juu yake, ambaye alikuwa mwanadamu wa kwanza na wakati huo huo alikuwa ndiye Mtume wa kwanza. Baada ya kufuatiwa na Mitume wengine laki moja na ishirini na nne elfu, njia hii tukufu ya uongofu imekuwa ikipitia maboresho na kuendana na mabadiliko ya kijamii ya mwanadamu. Na mnyororo huu wa uongofu ulifikia ukamilifu wake katika kipindi cha utume wa Mtume wa mwisho, Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake.

Mtume Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake, ana sifa mbili zinazomtofautisha yeye na Mitume wengine. Kwanza kabisa nuru yake





iliumbwa hata kabla ya kuumbwa nabii Adam- amani iwe juu yake, sifa ya pili ni kwamba yeye alikuwa Mtume wa mwisho kuletwa hapa duniani. Hivyo Mtume Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake - anawakilisha kurasa za mwanzo na za mwisho katika kitabu cha utume. Kwa maneno mengine, taasisi ya utume ilizinduliwa na nuru ya Muhammad (*Nur-i Muhammadi*), kiumbe wa kwanza kuwepo, na ilifungwa na kiwiliwili cha Muhammad (*Cisman-i Muhammadi*); alikuwepo kabla na baada ya dunia. Sifa hizi mbili za kipekee zinamfanya awe Mtume wa mwisho hapa duniani, lakini pia wa kwanza katika asili ya uumbaji.

Kwa kuwa sababu ya kuwepo viumbe wengine wote ni nuru ya Muhammad, Mwenyezi Mungu mtukufu alimuumba Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kwa ubora wa kipekee, kiasi kwamba akaitwa “kipenzi” (*habibi*) cha Mola wetu. Ili kumfanya kiumbe apate mafunzo ya nje na ndani yake, Mwenyezi Mungu mtukufu alimtuma Mtume Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake- kwa wanadamu kama zawadi.

Mwenendo wa kuigwa wa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anawakilisha kilele cha sifa za kibinadamu, zikiwemo zile ambazo hazizewezi kueleweka kutokana na utambuzi wa kawaida wa mwanadamu. Sababu ya hili ni ukweli kuwa Mwenyezi Mungu mtukufu amemfanya yeye kuwa mfano wa kuigwa (*uswa hasana*), mfano wa ukamilifu kwa wanadamu wote. Kutokana na kuwa kwake mfano wa kuigwa kwa wanadamu wote, hivyo Mwenyezi Mungu mtukufu amemfanya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, apitie kila hali inayoweza kufikirika katika maisha ya mwanadamu, ikiwemo kuzaliwa kwake yatima, mpaka baadae kufikia kwenye utawala wa kisiasa na kidini katika jamii yake. Hivyo kila mtu katika ngazi yoyote ya maisha anaweza kupata mfano mzuri wa kuigwa katika maisha ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, na kujifunza katika mfano huo.

Ndani ya Qur’an, Mwenyezi Mungu mtukufu anasema kuwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anawakilisha mfano bora kwa wanadamu wote, kwa kila mtu, kuanzia mwanzo wa utume wake mpaka siku ya mwisho.







لَقَدْ كَانَ لَكُمْ فِي رَسُولِ اللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ  
 لِمَن كَانَ يَرْجُوا اللَّهَ وَالْيَوْمَ الْآخِرَ وَذَكَرَ اللَّهَ كَثِيرًا

“Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana.” (al-Ahzab, 21).

Hii inamaanisha kwamba wanadamu wote wanahitaji kujifunza sifa za Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, ili kwa kupitia ramani iliyowekwa na maisha yake na matendo yake, waweze kupata ukamilifu wa dini na maadili. Kwa maana pana zaidi ukamilifu huo unapatikana katika asili ya mwenendo wa kisufi. Kila mtu hana budi kukifanyia kazi kile alichojifunza kulingana na uwezo wake. Jambo hili huanza kwa kuiga (*taqlid*) na huishia kwa kujitambua (*tahqiq*), kitu ambacho hutokea kulingana na kiwango alichonacho mtu juu ya mapenzi yake kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Kutapatikana baraka na ufunuo mbalimbali kwa kushikamana na Mtume- rehema na amani ziwe juu yake. Pale tutakapoweza kumfuata Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, katika matendo, kiroho na mwenendo wake kwa kadiri tunavyoweza itapelekea kupata heshima kubwa hapa duniani na kesho akhera. Mwenyezi Mungu ambaye utukufu ni wake alimuumba Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, katika silika bora (*fitra*), nje na ndani yake na kisha akamfunza vilivyo. Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, anasisitiza suala hili pale anaposema, “Mola wangu amenielimisha, na uzuri ulioje kwa namna alivyonielimisha!”<sup>1</sup>

Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, aliishi kwa miaka arobaini katika jamii iliyokuwa na vurugu na iliyokuwa katika ujinga kabla ya kupata utume. Lakini yeye alikuwa katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu na kukulia katika elimu kutoka kwake. Kamwe hakushiriki katika matendo yoyote ya upuuzi ambayo yaliigubika jamii yake kabla ya uislam. Na ili kuandaliwa kwa ajili ya majukumu mazito ya utume, kifua chake kilipasuliwa na moyo wake kusafishwa na kujazwa baraka na nuru.

Hata kabla ya utume wake, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu- rehema

1. Suyuti, Jamii's-Saghir, 1,12





na amani ziwe juu yake, aliishi katika maisha ya kuheshimika na aliamini kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja. Hasa kabla ya kupata utume alikuwa ameongeza uaminifu wake kwa Mwenyezi Mungu kiasi kwamba alijitenga kwa kwenda pangoni katika mlima Hira na kukaa kwa kipindi kirefu kwa ajili ya kutafakari maswali mbalimbali yamhusuyo mwanadamu. Sababu ya nje ya kufanya vile ilikuwa ni kutokana na namna alivyokuwa anaona mahangaiko, dhulma na tabu katika jamii aliyokuwa akiishi, fikra zilizosababishwa na moyo wake wa huruma juu ya viumbe vyote. Lakini sababu ya ndani ilikuwa ni maandalizi kwa ajili ya kupokea ujumbe mtukufu ambao ni Qur'an, kutoka kwa Mwenyezi Mungu mpaka kwenye moyo safi wa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Ufunuo na msukumo alioupata ndani ya moyo wake katika kipindi hiki cha maisha yake viliuongoza moyo wake kuelekea kwenye utwahirifu wa kiroho na kufanya uwe tayari kupokea ufunuo mtakatifu. Baada ya kuwa tayari kupokea ufunuo, moyo wake uliobarikiwa ulianza kupokea ishara za kiroho na msukumo kwa kupitia maono ya kweli kwa muda wa miezi sita. Kisha pazia lililokuwa limeficha siri za kiroho likafunuliwa kwa ajili ya Mtume-rehema na amani ziwe juu yake. Hatua hizi zilimsaidia kuboresha uwezo wake aliozaliwa nao kwa ajili ya kupokea ufunuo na kumuwezesha kuhimili mzigo mkubwa ambao hauwezi kustahimiliwa na watu wa kawaida; sawa na namna chuma kinavyogeuka na kuwa chuma cha pua kutokana na sifa zilizoko ndani yake.

Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake - alikusanya mamlaka na majukumu waliyokuwa nayo Mitume wote waliomtangulia na kuyaweka katika jukumu lake. Heshima ya Mitume waliotangulia, uzuri wa maadili yao na silika yao vilifikia kilele kwa Mtume. Aliasisi misingi ya sheria. Alifundisha namna ya kutwahirisha moyo na nafsi, mambo ambayo ndiyo kiini cha usufi. Pia alifundisha njia sahihi ya kumuabudu na kumuomba Mwenyezi Mungu kwa moyo safi. Kwa kupitia mwenendo wa maisha yake alionyesha namna ya ukamilifu wa maadili. Umri wake wa miaka arobaini ulikuwa ni wa mabadiliko makubwa si kwake binafsi bali wanadamu wote.

Kiini cha ufusi kinahusika na kupandisha imani zetu kwa kiasi cha ukomavu na kuweza kupokea ufahamu na mapenzi ya Mola wetu, na hivyo kutengeneza mchanganyiko kamili unaohitajika kabla ya kukutana na maisha halisi. Mchanganyiko huo kamili ndio utakaotuokoa; mchanganyiko





yiko ambao ni urithi mtukufu kutoka kwenye mapango ya Hira na Thawr. Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alipitia katika mafunzo mazito ya kiroho katika nyakati mbalimbali na sehemu mbalimbali na sio katika mapango ya Hira na Thawr peke yake, hasa kwa kumuandaa kwa ajili ya uzito wa ufunuo wa Qur'an; na mafunzo haya ndiyo yaliyozaa matunda ya kuutakasa moyo wake na kuisafisha nafsi yake.

Kabla ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- kupokea ufunuo wa Qur'an alikuwa tayari ameshafikia katika kiwango cha ukomavu wa kiimani na ukamilifu wa maadili. Hata hivyo baada ya kurudi kwake kutoka kwenye pango la Hira ambako kwa mara ya kwanza alipata maelekezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa uwazi, Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alifikia kwenye ukamilifu wa juu zaidi ambao hauwezi kulinganishwa na sifa nzuri alizokuwa nazo kabla ya kupata utume. Hapo Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa ameingia kwenye muunganiko wa kiroho na Mwenyezi Mungu; alikuwa ameonjeshwa ladha ya nuru ya upweke na ujuzi wa Mwenyezi Mungu, na hivyo kufikia kwenye kilele cha hali ya kiroho ya kumtambua Mola, na kupandikiza uchamungu katika kila sehemu yake ya mwili. Yote haya yalimpelekea afanye matendo ya ibada wakati wa usiku mpaka alfajiri na kupelekea miguu yake kuvimba. Hata wakati macho yake yamefunga, moyo wake ulikuwa haulali na daima ulikuwa katika hali ya kumkumbuka Mola mtukufu.



Ukweli ni kwamba kwa kupitia ufunuo wa Qur'an tukufu iliyojaa elimu na hekima, Muhammad aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- aliwaacha wenzake katika hamasa; na kwa kupitia maisha yake binafsi na matendo yake, alikuwa bahari ya wema yenye kustaajabisha, na hivyo alikuwa mbora hapa duniani na kesho akhera. Mpaka siku ya mwisho hakutakuja kuwa na ugunduzi ambao utamkanusha Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, wala hakuna msomi yeyote atakayekuja kufikia kiwango chake.

Ukomavu huu wa kiimani wa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- ulikuwa ukiendelea kuongezeka mpaka kufikia kilele chake; na kwa kupitia kupanda kwake mbinguni (*Miraj*), ambako ni zawadi ya kipekee kutoka kwa kipenzi (*Mahbub*) mpaka kwa (*Habib*), ilimpelekea





kuwa “msafiri wa milele”. Katika usiku ule, akiwa mgeni maalum wa Mola wake, Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, alienda na kupita mipaka ya muda na nafasi ya dunia ambayo wanadamu hawawezi kuipita, na hivyo akapata ukweli wa siri iliyotajwa ndani ya Qur’an tukufu kwa kusema “Baina ya mipinde miwili, au karibu zaidi” (An- Najm, 9)<sup>2</sup>.

Zawadi hii tukufu iliyoitwa *Isra* na *Miraj*, ilikuwa ni zawadi kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, na matukio haya yalitokea kutokana na kuondolewa kwa muda mipaka yote iliyowekewa wanadamu. Katika suala hili utambuzi wa kidunia wa muda na nafasi ulitoweka, na safari na maono ambayo yangeliweza kuchukua umri wa mabilioni ya wanadamu, yalitokea katika kipindi cha muda mfupi mno. Mtume-rehema na amani ziwe juu yake- alisafiri na kupita mipaka ya “Ulimwengu”, “Kiti cha Enzi”, na “Mkunazi” na kupata nafasi ya kipekee ya kumuona Mola na kuongea naye moja kwa moja bila ya kiumbe wa kati.

Huo ndio ukomavu wa kiroho na ukamilifu ambao Mwenyezi Mungu mtukufu alimjaalia Mtume aliyebarikiwa-rehema na amani ziwe juu yake. Sifa hizi kutoka kwa Mwenyezi Mungu mtukufu ziliendelea kumuongoza katika kazi kipindi chote cha jukumu lake la kusambaza ujumbe mtukufu kwa wanadamu na kuwaongoza katika njia iliyonyooka. Mategemeo na shauku aliyokuwa nayo Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- katika kutimiza jukumu alilopewa, vilimpelekea kwenye kilele cha ubora wa kibinadamu. Katika harakati zake alikataa zawadi zote za kidunia alizoahidiwa ili aache kutangaza ujumbe huu. Machoni mwake aliona kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa usahihi ndio jambo la muhimu kwake kuliko kitu kingine chochote.

Tukio lililotokea katika masiku ya mwanzo ya utume wake linaelezea vipaumbele vya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Washirikina wa Makka walimtuma baba yake mdogo ambaye ni Abu

2. *Qaba qawsayni aw adna:*

Wakati wa usiku wa *miraj* Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – peke yake ndiye aliyeruhusiwa kupita zaidi ya mti wa mkunazi (*Sidrat al-Muntaha*). Hakuna kiumbe mwingine akiwemo Jibril – amani iwe juu yake – ambaye aliruhusiwa kusogea kwa Mwenyezi Mungu kwa ukaribu kiasi kile. Maneno ya Qur’an yasemayo “urefu wa pinde mbili, au karibu zaidi”, yanaashiria mkutano wa siri kati ya Mwenyezi Mungu na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Uelewa juu ya uhalisia wa mkutano huu upo nje ya uwezo wa uelewa wa kawaida.





Twalib aende akamuambie Mtume aachane na shughuli zake za kiutume. Katika kujibu ombi hili Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- alimuambia baba yake mdogo kwa sauti ya upole, “Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, baba yangu mdogo, kwamba hata kama wangeliweka jua upande wangu wa kulia na mwezi upande wangu wa kushoto, kamwe nisingeliacha kuutangaza ujumbe huu. Ama Mwenyezi Mungu Mtukufu ajaalie ujumbe huu usambae duniani kote na hivyo niwe nimekamilisha jukumu langu, au nivute pumzi yangu ya mwisho katika njia hii”<sup>3</sup>.

Kutokana na kushindwa kwao, washirikina huku wakichukia kuza-liwa kwa uislamu na kukua kwake, walienda mbali zaidi katika ombi lao. Wakati huu walikuja kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- na kusema, “Kama unataka utajiri tutakupatia mali za dunia nzima na wewe utakuwa tajiri mkubwa kupita wote miongoni mwa makabila yote ya waarabu. Kama unataka madaraka basi tutakufanya uwe kiongozi wetu, na uwe mtawala wa Makka. Kama unataka mwanamke mwenye hadhi kubwa basi tutakuoza mwanamke mwenye hadhi kubwa na mzuri kupita wan-awake wote wa kiyuraysh...tutakuruhusu umchague mwenyewe na kum-chukua. Tuko tayari kufanya chochote unachotaka...ili mradi tu uachane na haya yote”.

Jibu la mwisho la Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- juu ya maombi ya kipumbavu kutoka kwa washirikina lilikuwa, “Sitarajii cho-chote kutoka kwenu; utajiri, mali, mamlaka, uongozi wala wanawake. Kitu ninachokitaka ni kwa nyinyi kuacha kuabudia hayo masanamu ambayo hayana uwezo wowote na kuanza kumuabudia Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee”<sup>4</sup>.

Bila shaka maneno haya na vitendo vinaonyesha mifano mizuri kwa wanadamu wote, hasa katika kuwa na msimamo katika imani na kutambua jukumu lako, na pia kuwa katika hali ya kumtumikia Mwenyezi Mungu kwa moyo safi. Maombi hayo yalikuwa yameegemea katika kupata raha za kidunia badala ya zile za kesho akhera. Historia ya mwanadamu imejawa na mifano mingi ya wale wanaoiuza akhera yao kwa thamani ndogo ya mafanikio wanayotarajia kuyapata hapa duniani.

Qur’an tukufu pamoja na mwenendo wa Mtume aliyebanikiwa- rehe-

3. Ibnu’l-Athir, *al-Kamilfi ‘l-Tarikh*, II, 64.

4. Ibn Hisham, *as-Sirah*, 1,236.





ma na amani ziwe juu yake- vinajumuisha misingi muhimu ya uislamu. Kutokana na Qur'an kuwa ndio sababu ya uongofu mpaka siku ya mwisho, huanza kwa kumtukuza Mola wa walimwengu wote na kuishia kwenye kuutakasa moyo dhidi ya sifa zote hasi na kumfanya mtu atafute ulinzi kwa Mola wake, kwa kujisalimisha kwake bila ya kushurutishwa. Mwenendo wa Mtume unawakilisha uongofu wa kivitendo kwa wanadamu; kumfuata Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- ndio njia ya pekee ya kupata furaha ya kweli hapa duniani na kesho akhera. Hakuna chochote hapa duniani kinachoweza kulinganishwa na uongofu huu hata kama kitaonekana kuwa na thamani kiasi gani, uongofu huu ni wa milele na hauwezi kukaliwa na chochote kingine.

Kwanza Qur'an tukufu ilishushwa kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- na baada ya hapo ikawafikia wanadamu wote kwa kupitia kwake. Qur'an ni maneno matakatifu ambayo yanamuita mwanadamu katika kumtambua Mola wake na kumfikia kwa kufuata misingi ya utambuzi wa kiasili wa kumfikia mzalishaji kwa kupitia kwenye zao, sababu kwa kupitia kwenye madhara, msanii kwa kupitia kwenye sanaa, na Muumbaji kwa kupitia kwenye kiumbe. Matokeo yake Qur'an inafundisha njia bora na nyepesi ya kumkumbuka Mola mara kwa mara na kuishi katika maisha ya umakini na uchamungu, katika maisha ambayo mtu anayazingatia maamrisha matakatifu kana kwamba anamuona Mola wake mbele yake, na hivyo kupata mapenzi na radhi za Mwenyezi Mungu.

Kila mtu hana budi kufahamu kuwa chanzo cha pekee cha mapenzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake; kwani kumpenda Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- ni sawa na kumpenda Mola, na Vivyo hivyo kumtii au kutomtii Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- ni sawa kumtii au kutomtii Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa ilivyotajwa hapo juu, sababu ya kuwepo kwa viumbe ilikuwa ni mapenzi ya Muumba juu ya nuru ya Muhammad, kitu cha kwanza kuumbwa. Kwa hiyo viumbe vyote vingine viliumbwa kwa sababu ya nuru ya Muhammad. Mwanadamu anawakilisha nafasi ya kipekee juu ya viumbe vyote katika kupokea zawadi takatifu. Na ubora juu ya viumbe vyote upo kwenye uwepo wa Muhammad, kwa maneno mengine uwepo wa Mtume aliyebarikiwa-rehema na amani ziwe juu yake- hapa duni-





ani. Mtu anajumuisha sifa za viumbe vyote, ndio maana akaitwa “dunia ndogo” au “ulimwengu mdogo”. Hivyo mwanadamu ni kiumbe wa kipekee ambaye ana sifa za wema na ubaya, wa viumbe vyote. Wakati huo huo mwanadamu anawakilisha chaguo safi juu ya viumbe vyote, kwani yeye ni kama mbegu ambayo ina mti mpana ndani yake. Au kwa usawa huo huo, ni kama mtu ambaye ana jamii nzima ndani yake. Kwa kuzingatia sifa hizo za kipekee mwanadamu amebeba cheo cha “lulu ya viumbe” (*ashraf-i makhlūqat*); lakini bado uwepo wa Muhammad unaenda mbali zaidi ya hapa. Wale waliokutana na Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kwa dhahiri waliweza ama kutambua undani wake au kuupuu- zia, kwa kutegemeana utambuzi wao au ukosefu wao wa maadili. Kwa kumuangalia tu baadhi yao waliweza kutambua na kukubaliana na wema wake; wakati wengine walishindwa haya na kumuona ni mtu mbaya. Abu Bakr na Ali ibn Abi Twalib- Mwenyezi Mungu awe radhi nao- mwanzoni walimtambua kama alivyomtambua Abu Jahl, lakini baadae waliona vitu tofauti mno ukiwalinganisha na Abu Jahl. Hivyo hawa wawili wakawa na mapenzi makubwa juu ya Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kiasi kwamba wakawa ni kiungo cha kwanza katika mnyororo wa njia ya Kisufi.

Usufi unalenga kumkubali Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kiroho na kimwili; hali ya kumkubali inayotokana na mapenzi yasiyo na mipaka. Kwa hiyo usufi unajikita katika kumfuata Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- kiroho na kimwili, na unawa- ongoza waumini katika kupokea sehemu ya imani yake na kumuwezesha mtu kufuata mwenendo wa Mtume kikamilifu. Kwa maneno mengine mwenendo wa kisufi unalenga katika kusambaza imani kwa upendo na moyo safi na kukamilisha matendo ya ibada kwa unyenyekevu mkubwa na kuishi katika maisha ya utii. Haya yanatokana na msukumo wa zawadi nzuri iliyoanza kwa “Pumzi takatifu” aliyopuliziwa kwa mara ya kwanza baba yetu Adam- rehema na amani ziwe juu yake, na ambayo ilifikia uka- milifu wake kwa Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Ili kuweza kutambua ukweli wa kiroho na maamrishi ambayo ndio kiini cha *tasawwuf*, ni muhimu kupata ufahamu mkubwa juu ya maisha ya Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake.

Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anawakilisha mfano bora kwa wanadamu katika kila kipengele cha maisha, ukiwemo





uwerevu wake katika kuwafundisha watu na kutwaharisha nyoyo zake. Kama Mtume, alipewa dhamana ya majukumu mengi ambayo kwayo alitekeleza maagizo mbalimbali. Miongoni mwa majukumu hayo, kuna aina nne zinazopatikana:

**1. Kupokea ufunuo mtakatifu (wahy):** Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- alipokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kupitia mkuu wa malaika Jibril – rehema na amani ziwe juu yake. Upokeaji huu wa ufunuo mtakatifu, ambao ulitokea kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, ulifikia mwisho kutokana na kuondoka kwa Mtume-rehema na amani ziwe juu yake- katika dunia hii.

**2. Kuelezea mafunzo ya Qur'an:** Qur'an tukufu imebeba hukumu na mambo mbalimbali kwa ufupi, mambo ambayo Mtume aliyebarikiwa-rehema na amani ziwe juu yake- aliyaelezea na kuyafafanua katika miaka yake ya jukumu la utume. Wanachuoni wa kiislamu (mujtahid) wameli-chukua jukumu hili baada ya kufariki kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake. Lengo la kuifafanua mafundisho ya Qur'an ni kuyafanya yaweze kueleweka na hivyo kuweza kutumika katika maisha. Jukumu hili limechukuliwa na wanachuoni wa kiislamu walioidhinishwa, juhudi hii inaitwa “kutafakari kunakojitegemea” (*ijtihad*). Kimsingi *ijtihad* ni suala la kuendelea katika jamii ya waislamu, lakini utekelezaji wake unategemea uwepo wa wanachuoni wakufunzi katika muda fulani. Kwa namna yoyote ile jukumu hili linawahusu wanachuoni wa kiislamu wenye ujuzi ambao wamefikia kiwango kinachohitajika katika *ijtihad*.

**3. Kutekeleza majukumu ya kiutawala:** Ili kuwafanya watu wafuate maamrisha na kuacha makatazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mambo mengine kwa ujumla, uanzishwaji wa muundo wa kiutawala ulikuwa wa lazima kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Hivyo serikali ya kiislamu aliyoianzisha iliendelezwa na watu wema waliomfutia au makhalifa.

**4. Kutwaharisha nafsi za wanadamu:** Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- aliweza kuzigusa nyoyo za watu na kuwashawishi, kwa kupitia uwezo wa kiroho aliopewa. Baada ya kuiaga kwake dunia, vizazi vya waislamu vilivyofuata vilichukua majukumu yote vyenyewe, isipokuwa hawakuweza kupokea ufunuo mtakatifu. Jukumu hili la mwisho la kuzifikia nyoyo za watu na kuzitakasa lilikuwa ni miongoni mwa maju-







kumu yake muhimu sana, na ni jambo la kawaida kutegemea kuendelea mpaka saa ya mwisho; kwani uwiano sawa wa maisha ya kidini unategemea utulivu wa kiroho na kimwili. Hasa jukumu hili limetekelezwa na kuendelezwa na wasufi, juu ya misingi ambayo inatokana na utekelezaji wa maelekezo ya Qur'an kutoka kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake-moja kwa moja. Wasufi wameweka msisitizo maalum katika mafundisho ya dini ya kiroho ili kuwasaidia watu wawe wanadamu bora na waislamu wakomavu katika uislamu wao. Bila shaka uislamu utaendelea mpaka siku ya mwisho, pamoja na safari yake isiyo na mwisho ambayo inahusiana na masuala ya kiroho. Kwa mujibu huu kuendelea kuwepo kwa usufi na wawakilishi wake wa kiutawala unatengeneza sehemu nyeti katika safari hii.



Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anawakilisha ubora wa hali ya juu katika wanadamu kwa kuwa na sifa ya utambuzi wa hali ya juu katika utumishi, ibada, mahusiano ya kijamii na maadili. Kwa miaka kumi na tatu akiwa ndani ya Makka, Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- amepitia katika mafunzo ya maandalizi; na pindi alipokuwa anahamia Madina alipata mafunzo ya kiroho zaidi ndani ya pango la Thawr, ambako alishuhudia mambo matakatifu. Pango hili lilikuwa sehemu maalum ya kupata ushuhuda wa hekima kutoka kwa Mwenyezi Mungu na mambo makubwa zaidi ya kiroho. Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alikaa kwenye pango lile kwa siku tatu. Mwenzake alikuwa ni Abu Bakr- Mwenyezi Mungu awe radhi naye, mtu mwema zaidi baada ya Mitume. Kuanzia mwanzo mpaka mwisho uswahaba huu ulikuwa hes-hima kubwa na nafasi ya kipekee kwa Abu Bakr, huku akitajwa na Qur'an kama “wa pili katika wawili” ndani ya pango (at-Tawbah, 40). Pia Qur'an ametaja namna Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alivyomtuliza Abu Bakr- Mwenyezi Mungu awe radhi naye:

لَا تَحْزَنُ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا

“Usihuzunike; Kwa hakika Mwenyezi Mungu yupo pamoja na sisi” (at-Tawbah, 40). Maneno haya ya Qur'an yanaashiria ukweli kuwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alimfundisha Abu Bakr maana ya siri





za ndani za kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutokana na uelewa wa kisufi, tukio hili lilikuwa ni mfano wa mwanzo wa kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu kimya kimya (*dhikr-i khafil*) na kiashirio cha namna ambavyo kuwa pamoja na Mwenyezi Mungu katika hali ile kunavyoleta utulivu katika moyo. Wasufi wanasisitiza zaidi ukweli kuwa kihistoria pango la Thawr lilikuwa ndio chanzo cha kuhamishwa kwa siri za kiroho kutoka kwenye moyo mmoja kwenda kwenye mwingine katika desturi za kiislamu. Hivyo, Abu Bakr- Mwenyezi Mungu awe radhi naye- ndiye aliyekuwa muislamu wa kwanza katika kupokea mafunzo ya kiroho moja kwa moja kutoka kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, ndio maana akachukuliwa kuwa ndiye aliyestahili kushika mamlaka baada ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake katika desturi za mwenendo wa kisufi wa kupokezana madaraka. Hivyo pango la Thawr likawa sehemu maalum ambayo mja angeliweza kumfikia Mola wake, Ambaye yuko juu ya vitu vyote.

Wasufi wanaelezea zaidi kuwa licha ya mafunzo yake ya misingi ya kumdhukuru Mwenyezi Mungu kimya kimya (*dhikr-i khafil*) kwa Abu Bakr- Mwenyezi Mungu awe radhi naye- lakini pia Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alimuelekeza Ali ibn Abi Twalib- Mwenyezi Mungu awe radhi naye- kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa sauti (*dhikr-i jahri*). Kwa kuzingatia misingi hiyo ya kihistoria, maelekezo ya kumkumbuka Mola, jambo ambalo ni la umuhimu wa kwanza katika mafunzo ya kisufi, yana asili kutoka kwenye mafundisho ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, maelekezo ambayo yaliendelezwa na viongozi wa mwanzo na watukufu katika uislamu.

Kwa kuzingatia kiini cha dini, ukweli ni kwamba usufi ulikuwepo tokea kipindi cha nabii Adam- amani iwe juu yake- mpaka kwa Mtume Muhammad- rehema na amani ziwe juu yake. Misingi mingi ya usufi inajidhihirisha yenyewe katika maisha ya kila Mtume. Kujitokeza kwake kinadharia na kivitendo kama inavyooneka hivi leo kunatokana na kuwekwa katika mfumo mzuri kwa mara ya kwanza katika karne ya pili baada ya Hijra; yani kuhama kwa Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- kuto- ka Makka na kwenda Madina katika mwaka wa 622 A.D.





huo Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa akitoa kanuni za kithiolojia na kisheria kwa maswahaba ili wazifanye ziwe bora zaidi katika masuala mbalimbali yaliyohusu uislamu. Maelekezo haya hayakuandikwa mahali popote wakati wa uhai wake, lakini wanafunzi wa wanachuoni wakubwa, kwa mfano wa sheria, walianza kukusanya mawazo ya walimu wao na kuyaweka pamoja. Hatua hii ndio iliyokuwa mwanzo wa kuibuka kwa madhehebu mbalimbali, na mawazo ya wanachuoni wakubwa kukusanywa chini ya jina lake, hivyo kila hiba ya mwanachuoni ikaja kufahamika kama vile madhehebu ya Hanafi, Shafii, Maliki na Hambali. Kutokana na kuoekana kwake kuwa yanafaa katika maisha ya kawaida, madhehebu haya yakapendwa na watu wengi.

Kama ilivyo fikra nyingine za kiislamu, tasawwuf inawahamasisha watu kuiga uvumilivu na uchamungu wa vizazi vya waislamu vya mwanzo, ambavyo vilitekeleza misingi ya usufi. Kadiri muda ulivyokuwa unaenda waislamu wengi walijikuta wakikimbilia kwenye mambo ya kidunia, hivyo wale waliobakia na msimamo wakabaki wachache ndani ya jamii. Kundi hili la mwisho lilichukua jukumu la kuwaonya watu dhidi ya starehe za dunia zenye kudanganya na kuwapa ushauri mzuri ili kuwaongoza katika njia ya haki. Hawakulenga kuanzisha fikra mpya au utaratibu mpya wa kiroho. Lengo lao la pekee lilikuwa ni kuishi katika maisha ya kawaida kulingana na maelekezo ya Qur'an na *hadith* za Mtume. Kutokana na kukubalika kwake, watu wa kizazi kilichokuwepo na vizazi vilivyokuja vilipenda mawazo yake, na vikawa vinahudhuria kwenye mafundisho yake na kuyafanyia kazi kivitendo. Hatua hii iliwafanya watu hawa wema watambulike kama viongozi na walimu wa kiroho. Watu waliokubali mafunzo yale ya dini walianza kukusanya maneno na maelekezo ya walimu wao na kuyaweka katika mfumo mzuri wa somo la kiroho. Baadae fikra za kisufi zikawekwa chini ya majina ya walimu wao kama vile Qadiriyya, Mawlawiyya, Naqshbandiyya na mengine kama haya.

Neno *tariqah* linamaanisha njia ambayo kila tawi la usufi linaitumia ili kumfikia Mola kwa kusaidia kustawisha sifa za kimaadili na kidini walizonazo wanadamu. Kwa kutegemeana na itikadi zao, kuna aina tatu za *tariqah*:

**1. Njia kwa ajili ya matendo mema (*tariq-i akhyar*):** Hizi ni *tariqah* zinazozingatia matendo ya ibada na uchamungu.





**2. Njia kwa ajili ya watu wema (*tariq-i ebrar*):** Hizi ni *tariqah* zinazozingatia kuitakasa roho ya mwanadamu kwa kupitia mazoezi ya kiroho na huduma.

**3. Njia kwa ajili ya wapenzi (*tariq-i shuttar*):** Hizi ni *tariqah* zinazolenga kufikia malengo ya aina moja kwa kupitia upendo.

Kila moja katika aina hizi tatu za *tariqah* zinawakaribisha watu kulingana na wasifu wao. Kila mtu anajiunga katika *tariqah* ambayo inaendana na utakaso wake na ukamilifu wa kiroho. Kwa kuwa watu wana tabia tofauti, ni jambo la kawaida kuwa na *tariqah* tofauti. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an:

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَ مِنْهَا جَاءَ

“Kila mmoja katika nyinyi tumemwekea sharia yake na njia yake.” (al-Maida, 48) .

Neno minhaj kutoka kwenye aya ya Qur'an limetafsiriwa kama “njia iliyomulikwa”, hasa ikamaanisha njia ya utumishi ambayo haina budi kufuatwa ili kumkaribia Mola kiroho. Methali maarufu ya kisufi inasema kuwa “Idadi ya njia za kumfikia Mola ni kubwa sawa na idadi ya pumzi zinazotolewa na kila kiumbe”.

Kwa upande mwingine hukumu za Qur'an ziko katika aina tatu:

1. Itikadi (Kanuni za imani)
2. Sheria au hukumu
  - a) za ibada
  - b) za mahusiano ya kijamii
  - c) za adhabu
3. Maadili au utambuzi wa moyo (*fiqh-i kalbi*)

*Fiqh-i kalbi* inamaanisha ubora wa moyo wa mtu au maadili yake, kwa ushirikiano wa itikadi na kanuni za kivitendo. *Fiqh-i kalbi* inalenga kukomaza matendo ya mtu kiasi cha kuzalisha matendo mema (*amali salih*). Kutokana na Qur'an, uchamungu (*taqwa*), uvumilivu (*zuhd*), na kupendezesha au kuiingiza imani moyoni (*ihsan*) vinawakilisha sifa





muhimu za thamani ya moyo.

Uchamungu (*taqwa*), kumtumikia Mwenyezi Mungu wakati wote, kunamaanisha kuulinda moyo kwa kutekeleza maamrishi ya Mwenyezi Mungu na kuacha makatazo yake katika hali ya kuufahamu wajibu wako wenye kuendelea mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Uvumilivu (*zuhd*) ni kuondoa moyoni kila kitu isipokuwa Mwenyezi Mungu.

Kupendezesha au kuiingiza imani moyoni (*ihsan*) ni kuanza kumtafuta Mwenyezi Mungu bila kuchoka huku unatambua kuwa upo chini ya uangalizi wake wakati wote.

(الْإِحْسَانُ) أَنْ تَعْبُدَ اللَّهَ كَأَنَّكَ تَرَاهُ فَإِنْ لَمْ تَكُنْ تَرَاهُ فَإِنَّهُ يَرَاكَ

Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- amesema, “*Ihsan* ni kumuabudu Mwenyezi Mungu kana kwamba unamuona; kwani hata kama humuoni, Yeye anakuona” (Bukhari , iman, 37, Muslim, iman 1). Kwa maneno mengine *ihsan* inamaanisha kuuzoesha moyo mpaka ifikie hatua mtu anahisi na anaona kuwa anaangaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kila hatua anayopiga. Hali hiyo ya kisaikolojia inaboresha hali ya moyo na inamuwezesha muumini kuishi kulingana na maamrishi ya Mwenyezi Mungu katika kipindi chote cha maisha yake. Ni kwa kupitia hatua hii ndipo ambapo moyo unakuja kuwa umetakasika; na hivyo kuto-ka na kuyafahamu haya tunagundua kuwa usufi unahusiana na kuuelekeza moyo kwenye utakaso.



Kwa upande mwingine, kwa waja wema, *ihsan* inawakilisha miraj ya kiroho au kupanda kiroho mpaka kwa Mola wao, kama ambavyo neno lenyewe linavyomaanisha, katika kumfanya mtu kisaikolojia ajihisi yuko karibu na Mola wake wakati wote. Msingi wa hii fikra ya *ihsan* umejikita katika maana iliyokwisha kutolewa na Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, ambapo *ihsan* inaelezewa kama fikra za kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu kana kwamba mtu anamuona mbele ya macho





yake; na ingawa yeye hamuoni Mola, lakini kwa hakika Yeye anaona kila kitu, akiwemo yeye. Wale wanaozingatia umuhimu huu wa *ihsan* huweza kuyaendesha maisha yao kama inavyotakiwa, hivyo hutoa nafasi kwa ajili ya *ihsan* ndani kabisa ya nyoyo zao.

Kutokana na haya, ihsan ni ukweli wa kiroho ambao wasufi wanautafuta. Katika kufanya juhudi ili kuwa na ihsan kunamuwezesha mtu kuwa karibu na Mola wake, na yeyote atakayejenga huo ukaribu huwa ‘Rafiki Yake’, mwenye tabia njema ambaye anaziadhimisha sifa za Mola wake kana kwamba ni zake mwenyewe. Mja ambaye hataweza kufikia hatua hii atakuwa amekwama katika sehemu ya chini ya kuielewa dini na hivyo anabakia katika hali ya kuiga tu. Haiishii hapo, bali sifa za kimaadili na kiroho za Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- hazikuwekwa kwenye vitendo na maswahaba pekee bali pia zilipelekwa mpaka kwenye vizazi vilivyokuja baadae. Hivyo kila muislamu anafurahia kupata nafasi ya kuonja utamu wa imani ya kiislamu; na maana hiyo hakuna utabaka katika desturi za dini ya kiislamu.

Kutokana na maelezo yaliyotolewa mpaka sasa, tunaweza kutoa mukhtasari wa uelewa wa usufi katika mizunguko ya mila za kiislamu kama ifuatavyo: Kutokana na kuwa msingi wake ni Qur’an na hivyo kuwa na asili katika uislamu, Usufi kipengele muhimu katika mila za dini ya kiislamu. Kinyume na usahihi wa ukweli huu juu ya usufi, baadhi ya watu wanaangalia chanzo au vyanzo vya usufi nje ya uislamu. Wanaangalia katika vyanzo mbalimbali vinavyozingatia etimolojia au historia ya asili ya maneno. Kwa mfano wanasema kuwa neno usufi limepatikana kutokana na neno la kigiriki “*sophia*”, neno linalosemekana kutokana na neno la kiarabu “*tasawwuf*”. Kwa namna hiyo hiyo kuna wengine wanaojaribu kuchambua asili ya usufi kutokana mila za kabla ya uislamu, za kikiristo na kiyahudi; na bado kuna wengine wanadai kuwa mwenendo wa kisufi umetokana na mizizi ya dini ya kihindu. Kwa ujumla nadharia zote hizi zimeshindwa kutoa uelewa wa kweli juu ya kiini cha usufi.

Wanachuoni wa kiislamu nao wametoa maneno mengi na yenye kushawishi katika kuelezea asili ya neno “*tasawwuf*” kama linavyopatikana katika vyanzo mbalimbali vya uislamu. Kwa mfano, maoni yametolewa kuwa kulingana na historia ya asili ya maneno, neno “*tasawwuf*” lime-nyambuliwa kutoka kwenye maneno ya kiarabu “*safa*”, “*safwah*” na “*istafa*”,





ambapo maneno yote yanamaanisha ‘utakaso’ katika maeneo mbalimbali. Baadhi ya wanachuoni wa kiislamu wanatoa uhusiano wa kihistoria kati ya neno “*tasawwuf*” na sehemu ya jamii ya waislamu wa mwanzo, ambayo watu wake walijitolea kufanya matendo ya ibada na uvumilivu wakati wote, watu ambao waliitwa “*ahlu’-suffa*”, yani “watu wa utakaso”. Inasemekana kuwa walikuwa wakivalia majoho ya sufi; kwa maneno mengine, majoho yaliyotengenezwa kwa “*suf*”, neno la kiarabu la sufi. Hivyo “*sufi*” au “*muta-sawwif*”, ni mtu anayevaa nguo iliyotengenezwa kwa sufi, kutoka na msingi kuwa kihistoria “*ahlu’-suffa*” walikuwa wakipendelea mavazi hayo hayo, kutokana na uvumilivu na unyenyekevu waliokuwa nao.

Kama ilivyo kanuni ya msingi, wanachuoni wa kiislamu wanategemeza ufafanuzi wao binafsi wa masuala ya dini katika Qur’an na *Sunnah*. Hivyo kama ilivyo kwa mwanasheria wa kiislamu ambaye hatoki kwenye Qur’an na *Sunnah* wakati anapotoa hukumu mbalimbali katika masuala ya kisheria kwa kupitia fikra zisizo tegemezi (ijtihad), Sufi nao wanategemeza ufafanuzi wao juu ya masuala ya dini katika Qur’an na *Sunnah*. Kwa msingi huu Sufi hawatofautiani na wanasheria wengine wa kiislamu, kwa kuwa wote wanatarajiwa kutekeleza majukumu yao kwa hisia za uchamungu na hofu juu ya Mola wao (*taqwa*) na wanatetea hoja zao kwa ushahidi wa Qur’an na *Sunnah*.

Hata hivyo wakati mwingine baadhi ya waandishi wa kisufi ambao hawana ufahamu wa kutosha juu ya misingi ya dini na huku wakisukumwa na utamu wa raha ya kiroho, wanaweza kukosea katika kuhukumu kwao mambo au kutoa maneno yenye kuchanganya. Masheikh wa itikadi ya kisufi ambao walikuwa wanachuoni wenye ufahamu mkubwa na ambao walikuwa wakifahamu sayansi za mambo mengi, waliweza kukingwa na makosa hayo. Naqshbandiyya na sufi wengine sawa na hawa ambao wana-jipamba na kanuni za wazi za Qur’an na *Sunnah* wametoa kanuni maarufu juu ya jambo hili kwa kusema “Kitako imara cha dira ni Shariah (Sheria)”. Pia Rumi naye anaelezea:

*“Sisi ni kama dira. Vitako vyetu imara vimesimama juu ya Shariah, na tunasafiri katikati ya mataifa sabini na saba kwenye dunia. Shariah ni kama mshumaa; inamulika na kuonyesha njia. Mtu hawezi kusogea mbele kwa kushikilia mshumaa mkononi peke yake, lakini pia mtu hawezi kusonga mbele kwa kuushikilia mkononi. Pindi unapoanza kufanikiwa chini ya nuru ya Shariah...hii ndiyo tunayoiita tariqah”.*





Usufi ni juhudi ya kuishi katika maisha ya utulivu kwa dhati ya dini, na huku ukiji-takasa kutokana na kasoro za kimaadili na nafasi yake kupandikiza mwenendo mzuri wa kimaadili.



## B. TAFSIRI YA USUFI

Usufi ni shauku au hali ya akili, na sio maneno matupu; suala la uhalisia wa maisha na sio kufahamu tu. Kadiri mtu anavyoridhika na kufuata mwenendo wa kisufi, ndivyo anavyozama zaidi katika ufahamu wa ukweli wa kiroho. Kinyume chake haiwezekani kutoa maelezo ya kutosha kuhusu ukweli wa usufi kwa kupitia maneno pekee. Kwa hiyo watu wengi wema wenye ufahamu na utamaduni tofauti tofauti wametoa maana mbalimbali za mwenendo wa kisufi, huku wakizingatia hali zao za kiroho kwa wakati ule; jambo ambalo linaufanya usufi kuwa fikra pana.

Watu wema na wafuasi wao wanasonga mbele katika njia yao ya kiroho kulingana na uwezo wao, na kulingana na msukumo wa uzoefu wa nyoyo zao. Kutokana na mtazamo huu mtu anaweza kukutana na maelezo tofauti tofauti katika masuala ya dini ya aina moja, yaliyotolewa na watu wema mbalimbali, kiasi kwamba maelezo haya yakatokana na hali zao za kiimani na pia kutokana na hali maalum wanayoipokea katika nyoyo zao. Zaidi ni kwamba, kila moja kati ya tafsiri hizi juu ya usufi zilizotolewa na watu wema mbalimbali ni sahihi kulingana na ujuzi wao binafsi wa kuchambua mambo. Na kutokana na utambuzi wa kiini cha usufi leo hii, mtu anaweza kupata maana pana, pia kulingana na maana mbalimbali walizozitoa watu wema waliotangulia.



Kwa kuzingatia vipengele vinavyolingana katika maana mbalimbali za mwenendo wa kisufi, tunaweza kusema kuwa usufi ni fikra ambayo inamuelekeza muumini kwenye ukamilifu wa maadili kwa kuboresha nyoyo zao, hali zao za kiimani na kuwasaidia kuiga mifano mizuri ya maadili na mwenendo mwema, na hivyo kuwaongoza kuelekea kwenye kumfahamu Mwenyezi Mungu.







Zifuatazo ni baadhi ya tafsiri za usufi zilizotolewa na watu wema kulingana na uwezo wao wa kiroho walijaaliwa:

### 1. Mwenendo wa kisufi unawakilisha mfano wa maaadili (*akhlaq*) na adabu (*adab*).

Kumuokoa muumini kutokana na uigaji bila ya ujuzi wowote (*taqlid*) katika masuala ya dini, ambayo ndio mwenendo wa kuigwa huzalisha ihsan ndani ya mtu, ihsan ambayo huleta msimamo na maadili mema ndani ya fikra za mwanadamu. Ihsan haina budi kuweka fikra njema ndani ya moyo wa muumini, na pia kumsababishia kumkumbuka Mola wake wakati wote, kana kwamba anamuona. Mwishowe ihsan inakuwa nguvu muhimu ya kuongoza matendo na tabia ya muumini katika maisha yake yote. Abul-Husayn an-Nuri anaelezea usufi kwa uzuri zaidi pale anaposema, “Usufi haujabeba taratibu na ujuzi lakini umebeba maadili mema (*akhlaq*). Kama ingelikuwa ni kuhusu taratibu, mtu angelizipata kwa kupitia juhudi zake binafsi lakini kama ingelikuwa ni kuhusu maadili mema, mtu angelijifunza kwa kupitia elimu ya kawaida. Kwa sababu hii si taratibu wala maadili mema pekee ndiyo yanaweza kumfikisha mtu kwenye lengo. Usufi ni kufanikiwa katika kumpa Mwenyezi Mungu haki zake”. Hivyo msisitizo unaopatikana katika tafsiri ya An-Nuri ni muunganiko kati ya mwenendo wa kisufi na kujipamba na sifa zake nzuri.

Ingawa mtu anaweza akashindwa kuona neno *tasawwuf* limetajwa katika kipindi cha maisha ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, kiini chake na ukweli wake ulikuwepo chini ya maneno kama “mfano wa maadili bora” sifa aliyokuwa nayo Mtume- rehema na amani ziwe juu yake; sifa ambazo muumini hana budi kujipamba nazo. Maadili ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- yamethibitishwa na Qur’an kama ifuatavyo:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ

“Na hakika wewe una tabia tukufu.” (al-Qalam, 4)

Vivyo hivyo pindi Aisha- Mwenyezi Mungu awe radhi naye- alipoulizwa kuhusu maadili ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- alijibu kwa kusema, “Maadili yake ni yale ya Qur’an” (Muslim, Musafirin, 139). Pindi mja anapojipamba na sifa za kimaadili zilizotajwa





ndani ya Qur'an na akashikamana na misingi ya Qur'an, atafikia mahali Qur'an itakuwa ndio muongozo wa maisha yake. Kutafakari maana ya Qur'an, kuisoma kwa unyenyekevu na kutekeleza maagizo yake, kunapelekea kuwa katika kilele cha maadili mema.

Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alitumwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kuja kuungoa ulimwengu mzima, katika upeo wake wote, tokea mwanzo wa utume wake mpaka saa ya mwisho. Hatuna budi kushukuru kuwepo kwa kumbukumbu za kihistoria na za wanachuoni zenye kuaminika, kiasi kwamba leo hii tumeweza kuwa na maelezo ya kutosha juu ya maisha ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake. Pindi mtu atakapochungulia kumbukumbu hizi atakutana na vipengele vyenye kustaa-jabisha katika maisha yake; kutokana na kuwakilisha kwake ukamilifu wa maadili ya mwanadamu. Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- yeye mwenyewe anagusia jukumu lake pale anaposema, "Sikutumwa bali kuja kukamilisha maadili mema" (imam Malik, Muwatta, Husnu'l-Khuiq 8). Qur'an nayo inalithibitisha hili katika aya inayomtaja Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- kama "kiigizo chema" (*uswatun hasa-nah*): "Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana." (al-Ahzab, 21).

Hata baada ya kuondoka kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, Mwenyezi Mungu ataendelea daima kuwatukuza wanachuoni wema miongoni mwa watu, kama zawadi kwa wanadamu na cha muhimu zaidi kuendeleza utekelezaji wa maadili mema. Katika *hadith* wanachuoni hawa wanatajwa kama "warithi wa Mitume" (*warathatu'l-anbiya*)<sup>5</sup>. Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anatoa maelezo zaidi juu ya wanachuoni kama hao kwa kusema, "Muumini wa kweli ni yule mwenye tabia njema kabisa" (Ahmad ibn Hanbai Musnad, II, 250). Maneno haya yanadhihirisha ukweli kuwa tabia njema ni matunda ya imani na dalili za ukamilifu wake. Hivyo watu wema ni viongozi wa kiroho ambao wamependelewa kutokana na kushikamana kwao na tabia njema ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Abu Muhammad

5. Neno "*warathatu'l-anbiya*" linaashiria wanachuoni wa kweli ambao kwa nje na ndani ya nyoyo zao wameiga mwenendo wa kiutume na hasa maadili ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na wanafuata kiigizo hicho katika kila kipengele cha maisha yao kinadharia na kivitendo; kama ambavyo *hadith* inasomeka, "...wanachuoni wa kweli ni warithi wa Mitume". *Abu Dawud*, IIm, 1.





al-Jariri ametoa tafsiri ya mwenendo wa kisufi inayoendana na haya kwa kusema, "...kujipamba na tabia njema na kujizuia na maovu".

Kila mtu hana budi kuupamba moyo wake kwa maadili mema na kuutakasa kutokana na maovu, kufanya hivi ni muhimu ili kupata furaha ya milele na uongofu. Katika kuisitiza jambo hili, Abu Hashim as-Sufi anasema, "Kufuta kiburi kilichoko ndani ya moyo ni vigumu zaidi kuliko kuchimba mlima kwa sindano". Vivyo hivyo Abu Bakr al-Kattani amesema: Usufi unahusu maadili mema. Mtu ambaye ni mbora kimaadili zaidi yako pia ni msafi kiimani zaidi yako".

Historia ya mwanadamu imejawa na udhihirisho wa mienendo ya kuigwa ya Mitume. Kwa mfano nabii Yusuf-amani iwe juu yake- amonyesha moja ya mifano mizuri ya maadili mema katika historia. Kama ilivyosimuliwa katika Qur'an, Yusuf-amani iwe juu yake-si kwamba aliacha kulipiza kisasi kwa ndugu zake ambao miaka kadhaa iliyopita walitenda uhalifu mkubwa kwa kumtumbukiza ndani ya kisima mahali ambapo hakukuwa na watu, bali alionyesha huruma ya hali ya juu na kuwasamehe pindi alipokutana nao miaka kadhaa baadae, na kuwahakikishia kuwa "Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusamehe- ni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu" (Yusuf, 92).

Lengo kuu la Sufi ni kujitahidi kumuiga Ibrahim- rehema na amani ziwe juu yake- katika kuondoa moyoni kila kitu cha kidunia na kuujaza utii juu ya maamrisho matakatifu; Ismail-amani iwe juu yake-katika kujisalimisha kwake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuridhika na qadari takatifu; na Ayyub- amani iwe juu yake-katika kuugubika moyo wake kwa subira ya hali ya juu. Pia ni muhimu kujipamba na huzuni ya Daud-amani iwe juu yake- na kujizuia kwa Isa-amani iwe juu yake.

Moyo wa sufi unapaswa kuiga moyo wa Musa - amani iwe juu yake, kutokana na kuzama kwake kwenye furaha ya kiroho na kumfikiria Mola wake wakati wote, na juu ya hayo yote, moyo wa Mtume aliyebarikiwa-rehema na amani ziwe juu yake,

*Ewe bwana! Fahamu kwamba adab ni roho ndani ya mwili wako;*

*Adab ni jicho la watu wa Mwenyezi Mungu na ni nuru ya nyoyo zao.*

*Kama unataka kuponda kichwa cha shetani , fungua macho yako Uan- galie!*

*Adab ndiyo inayomkandamiza shetani.*





*Kama huwezi kuona adab kwa mtu , basi yeye si mwanadabu.*

*Adab ndiyo inayowatofautisha wanadamu na wanyama.*

Katika mada hii hii Rumi naye anasema,

*Fikra zangu zilivutia moyo wangu,*

*“Imani ni nini?”*

*Moyo wangu ukanong'oneza sikio la fikra zangu,*

*“Imani si kingine bali ni adabu (adab)”*

Mshairi mwingine anasimulia,

*Adab ni taji lililoteremshwa ardhini kutoka kwenye nuru ya Mwenyezi Mungu!*

*Liweke juu ya kichwa chako na ujiweke mbali na mandhari za aina zote.*

Kwa hiyo kwa muda mrefu sasa kumekuwa na desturi ya kuweka kibao cha tahadhari kinachosomeka “Adab Ya-Hu” katika mahoteli ya kisufi! Wito huu ni wenye maana nyingi. Huku ukimkumbusha msomaji juu ya umuhimu wa kuishi katika maisha ya *adab*, wakati huo huo ni dua yenye kumaanisha “Ewe mola, tujaalie *adab!*”

## **2. Mwenendo wa kisufi unahusiana na kuutakasa moyo na nafsi**

Kwa kuwa mwanadamu amekuja hapa duniani kwa ajili ya kujaribiwa, ataendelea kupata mitihani mpaka afikwe na mauti, haya ni kutokana na uwepo wa nafsi ambayo imebeba mabaya mengi. Hata kama mtu atakuwa amefikia kwenye daraja la utakatifu, lakini bado atakuwa anakabiliwa na tishio la vikwazo vikuu vitatu: Dunia yenye kupita, nafsi na shetani. Wakati wote ataendelea kuwa katika tishio la kudanganywa na kuhadaiwa na hila na mitego ya vitu hivi vitatu. Manufaa ya utumishi huanza kupatikana pale tu muumini anapougeuzia moyo wake kwa Mola, na kujiepusha na hatari ya hivyo vitu vitatu vilivyotajwa, matokeo yake atakuwa amejinusu dhidi ya ulaghai wa raha za dunia.

Kuutakasa moyo na nafsi ni muhimu katika kurekebisha maovu yaliyopo kwa mwanadamu na hivyo kupandikiza mbegu za uchamungu (*taqwa*) ndani yake. Kwa sababu hii ni jukumu la kila mwanadamu kumfa-





hamu Mwenyezi Mungu Mtukufu kulingana na uwezo wake. Jukumu hili linaenda mbali zaidi ya kumfahamu kwa kawaida bali kumfahamu kikweli kweli, na matokeo yake kufanya amali njema. Hiyo ndiyo maana halisi ya “utumishi”. Ili kuuhuisha utumishi wa namna hii mtu hana budi kujitahidi kuutakasa moyo na nafsi; na jambo hili linapelekea kuviruka vikwazo vyote vya dunia. Hiyo ndiyo njia ya pekee ya kumfikia Mwenyezi Mungu hapa duniani na kesho akhera.

Asili ya moyo ni kwamba umefunikwa na utukufu wa Mwenyezi Mungu; kwa maneno mengine, ni sehemu ambayo Mola wetu anapatazama wakati wote, na hivyo moyo uko wazi kupokea maamrishi matakatifu kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sharti kuwa uwe umesafishwa dhidi ya matamano ya kidunia na ubinafsi. Moyo ambao umegubikwa na matamano haya unakuwa hauko safi kiimani na hivyo hauwezi kupokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Katika kusimamia kwenye kanuni hii si lazima mtu aache kuwapenda watu wengine kinyume na Mwenyezi Mungu; ingawa tumesema hivi, wale waliofanikiwa kuwa na moyo safi mwishoni mwa safari hii wanakuwa wamejizua kukipenda kitu kingine chochote tofauti na Mwenyezi Mungu (*masiwa*). Kutokana na ukweli kwamba wanadamu hawawezi kufuta kabisa nyoyoni mwao mapenzi yao kwa ‘vitu’ vya kidunia, ni matumaini kuwa watanufaika kutokana na mapenzi haya ikiwa hawataegemea zaidi kwenye mapenzi hayo kama ilivyo kwenye mapenzi ya kweli kwa Mola wao.

Kwa kukumbuka kazi na hadhi ya moyo kimwili na kiroho kutatuwezesha kuona umuhimu wa kuutakasa. Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anasema, “Kuna pande la nyama katika mwili wa mwanadamu...likisalimika basi mwili wote utasalimika, na likiharibika basi mwili wote utaharibika. Kuweni makini...kwani pande hili (la nyama) ni moyo”. (Bukhari , Iman, 39).

Rumi anatoa maelezo ya mfano juu ya ukweli huo huo kwa kusema kuwa pindi mtu anapojaribu kujaza kiroba kitupu, hana budi kuhakikisha kuwa kiroba hicho hakina tundu lolote; kinyume chake juhudi yake itakuwa ni bure. Vivyo hivyo Rumi anaendelea kwa kusema kuwa matendo ya mwanadamu yatakuwa na maana na yatampelekea uongofu ikiwa yatafanywa kwa moyo uliotakasika; kwani malipo ya matendo yanategemea nia, na nia nayo ni amali ambayo inategemeana na moyo. Kutokana na muunganiko huu imara mtu hana budi kusahihisha nia yake na kuipamba kwa moyo safi; lakini hili si jambo rahisi. Walimu waliofuzu ndio pekee





wanaoweza kumuongoza mtu katika mchakato huu wa kuutakasa moyo, mwishoni mtu huyu atakuwa amefikia hali inayotakiwa. Walimu wema huwafundisha wafuasi wao wauelimishe moyo katika kuwasaidia katika kufikia kwenye *ihsan*, ambapo hufikia kwenye hali ya kiroho ambayo hufanya moyo uhisi uwepo wa Mwenyezi Mungu wakati wote.

Ili kufikia katika daraja hili la ukamilifu wa kiimani kunahitaji kuutakasa moyo dhidi ya matamano ya aina zote na vitu vingine kinyume na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Moyo uliofikia katika ubora huu huanza kutambua siri za ndani na huwa chanzo za udhahirisho wa majina matakatifu na siri za kiroho, siri ambazo undani wake unategemea na kina cha ukomavu wa kiroho wa moyo husika. Kumtambua Mwenyezi Mungu (marifatullah), ambako ni kumfahamu Mola ndani ya moyo, hujitokeza kwenye moyo wa mtu husika, na kujitokeza huku huashiria mwanzo wa mabadiliko ya ufahamu wa kawaida (*ilm*) kwenda kwenye ufahamu wa kweli au hekima (*irfan*).



Qur'an inatueleza kuwa wale tu watakaoende mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa moyo safi ndio watakaoweza kupata uongofu:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَلَا بَنُونَ إِلَّا مَنْ أَتَى اللَّهَ بِقَلْبٍ سَلِيمٍ

“Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi.” (as-Shuara, 88-89). Kinyume chake, nyoyo ambazo zitakuwa zimechafuliwa kwa maovu na zimekuwa mbali na Mwenyezi Mungu hazitafaulu, kama tunavyofahishwa katika Qur'an, “Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, Hakika amefanikiwa aliye itakasa, Na hakika amekhasiri aliye iviza.” (as-Shams, 7-10). Pia Qur'an inadhihirisha, “Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri.” (az-Zumar, 22). Kutokana na msukumo wa maneno haya ya Qur'an, Abu Said al-Kharraz alitoa maneno ambayo yalitoa mwangaza mkubwa katika mjadala wetu huu: “Mbora ni yule ambaye Mwenyezi Mungu ameutakasa moyo wake na kuujaza nuru ya imani”.





### 3. Mwenendo wa kisufi ni mapambano ya kiroho yasiyoisha.

Kutoka kwa Junayd al-Baghdadi, tafsiri hii inaonyesha ukweli kuwa usufi ni juhudi ya maisha yote (*jihad*) katika kupambana na matamania ya nafsi. Mapambano haya yanalenga katika kuweza kuendesha matamania ya mtu. Kwa kawaida vita hudumu kwa muda maalum; lakini vita dhidi ya nafsi havina cha kuvimaliza mpaka mauti yakufike. Qur'an inaelekeza, "Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini." (al-Hijr,99). Mwenyezi Mungu Mtukufu anawatahadharisha waja wake dhidi ya kutojali, kwani kunafungua milango ya moyo na kuruhu kuingiwa na hila za nafsi na kuuweka katika hatari wakati wote.

وَ اذْكُرْ رَبَّكَ فِي نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَ خِيفَةً وَ دُونَ الْجَهْرِ  
مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَ الْأَصَالِ وَ لَا تَكُنْ مِنَ الْغَافِلِينَ

Katika suala hili hili Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- hutumia maneno "*jihad* kubwa" pale anapoonyesha juhudi kubwa inayotakiwa kuchukuliwa katika kupambana na nafsi. Pindi waliporejea kutoka katika vita vya Tabuk, vita vilivyoitwa "Vita vigumu" kutokana na asili yake magumu yaliyopatikana ndani yake, Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- aliwageukiwa maswahaba zake na kuwaambia, "Sasa hivi tumetoka kwenye *jihad* ndogo na tunaelekea kwenye *jihad* kubwa". Maswahaba walistaajabishwa na hivyo wakamuuliza Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, "Je *jihad* ipi kubwa zaidi ya hii?", Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- akajibu, "Kwa hakika kwa sasa tumetoka kwenye *jihad* ndogo na tunaelekea kwenye *jihad* kubwa...*jihad* dhidi ya nafsi"<sup>6</sup>.

Katika kutoa fikra zake juu ya namna ambavyo uislamu unaweka uwasa mdogo kati ya *jihad* kubwa na ndogo, msomi wa zama zetu Roger Garaudy anasema, "Usufi ni elimu kamili ya kiroho katika uislamu, kwani inahusiana na mapambano ya ndani dhidi ya matamania yote ya asili ambayo yanamuweka mtu mbali na lengo la kuumbwa kwake na kumfanya awe mtumwa wa nafsi yake. Katika maneno ya kiislamu, juhudi hii inaitwa "*jihad* kubwa". Kwani *jihad* ndogo inahusiana na kupambana dhidi ya mamlaka, utajiri na elimu ya uongo ambayo inawaweka waislamu mbali

6. Suyuti, *Jamii 'Saghir*, II, 73





na njia ya Mola wao; waislamu wanatekeleza *jihad* ndogo ili kudhihirisha umoja na utulivu katika njia ya Mola wao. Hii inaweka usawa kati ya aina hizi mbili za *jihad* (Kubwa na ndogo), jambo ambalo linaleta furaha na msimamo katika maisha ya mtu binafsi na ya kijamii<sup>7</sup>.

#### 4. Usufi unamaanisha usafi wa moyo (*ikhlas*)

Usufi unamaanisha usafi wa moyo mbele ya Mola. Kimaana usafi wa moyo unamaanisha kufanya matendo yote ya ibada kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee, bila ya kuwa na matumaini mengine moyoni. Jambo la kufuta aina zote za matamano ya kidunia kutoka moyoni mwako na kuzingatia kwenye radhi za Mola wako ni jambo muhimu katika uislamu. Lengo la wazi la matendo yote ya ibada ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu; na kama mtu atakengeuka na kuruhusu lengo la pili, yani maslahi ya kidunia, neno zuri la kupewa kitendo hiki litakuwa ni uovu wa moyo au maneno matupu. Matendo yaliyofanywa kwa mazoea hayana thamani mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo usafi wa moyo sifa muhimu katika kuwezesha matendo ya ibada yakubaliwe na Mwenyezi Mungu.

Usafi wa moyo ni kuulinda moyo dhidi ya aina zote za matamano ya kidunia na kuukurubisha kwa Mwenyezi Mungu, jambo lenye kufanya moyo uwajibike. Cha zaidi ni kwamba usafi wa moyo unapelekea kupata radhi za Mwenyezi Mungu, jambo kubwa la wema ambalo anaweza kulipata. Katika sehemu nyingi ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu ametaja umuhimu mkubwa wa usafi wa moyo katika matendo ya ibada yanayotekelezwa na waja wake, kwa kusema, "Hakika Sisi tumekuteremshia Kitabu hiki kwa Haki. Basi muabudu Mwenyezi Mungu ukimsafia Dini Yeye tu." (az-Zumar, 2) na pia amesema, "Sema: Hakika mimi nimeamrisha nimuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumsafishia Dini Yeye tu." (az-Zumar, 11). Aya za Qur'an zinatutarifu zaidi kuwa baada ya shetani kufukuzwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu alisema, "Akasema: Mola wangu Mlezi! Iliyoy kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote, Ila waja wako walio safika." (al-Hijr, 39-40).

Usufi ni kujiokoa mwenyewe kutoka kwenye mikono ya nafsi kwa kufanya kila kitendo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kwa kufahamu kuwa baraka zote na utukufu unatoka kwake pekee. Licha ya kiwango chako cha imani, huna budi kuchoshwa na ubinafsi na kujiona, mazoea ambayo







yanatukumbusha ufunuo mtakatifu alioukata Mtume aliyebanikiwa- re-  
ma na amani ziwe juu yake- wakati anarejea Madina kutoka kwenye ush-  
indi wa Badr:

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ وَمَا رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَ لَكِنَّ اللَّهَ رَمَى

“Akasema: Mola wangu Mlezi! Iliyoy kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote, Ila waja wako walio safika.” (Al-Anfal, 17)<sup>8</sup>. Kwa hiyo mja hana budi kuchukua tahadhahri wakati wote juu ya kutokuwa kwake salama na juu ya hali yake ya kuwa yeye ni kiumbe, na atambua kuwa kila baraka, ushindi na mafanikio yanatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kama zawadi. Kufikiria kinyume chake kutasababisha kupungukiwa kwa malipo ya amali, kama si kufuta kabisa.



Kushindwa kutekeleza matendo ya ibada kwa moyo safi na kuruhusu nafsi kukuendesha kutaleta madhara makubwa, kama ilivyotajwa katika *hadith* iliyosimuliwa na Abu Hurayra- Mwenyezi Mungu awe radhi naye, kwamba Mtume aliyebanikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- amesema, “Mtu wa kwanza kuhesabiwa siku ya kiyama ni mtu aliyekufa shahidi. Ataletwa (mbele ya kiti cha hukumu). Mwenyezi Mungu Mtukufu atamfanya ahesabu neema zote alizompa katika uhai wake na yeye atazihesabu kila moja na huku yuko radhi nazo. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu atamuuliza, ‘Je ulifanya nini kama shukurani?’ Atajibu, ‘Nilipigana kwa ajili yako mpaka nikafa shahidi’. Hapo Mwenyezi Mungu atajibu, “Unasema uongo. Ulipigana kwa ajili ya kuitwa ‘shujaa hodari’; na hivyo ndivyo ulivyoitwa’. Kisha Mwenyezi Mungu atamhukumu na kisha mtu yule ataburuzwa kwa uso wake na kutupwa motoni. Kisha ataitwa mtu ambaye alikuwa na elimu, akawafundisha wengine na alikuwa ni mwenye kuisoma Qur’an. Baada ya kuletwa Mwenyezi Mungu atamfanya azihesabu neema zake kwake na hivyo mtu yule atazihesabu na huku yuko radhi nazo. Kisha

8. Kulingana na mapokeo ni kwamba pindi vita vilipoanza Mtume aliyebanikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliomba na kuwarushia maadui vumbi, vumbi ambalo liliyapata macho yao na kuwachanganya. Aya hiyo ilishushwa baada ya tukio hilo.





Mwenyezi Mungu Mtukufu atamuuliza, ‘Je ulifanya nini kama shukurani?’. Atasema, ‘Nilitafuta elimu na kuisambaza kwa wengine na kusoma Qur’an kwa ajili ya kutafuta radhi zako’. Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema, ‘Unasema uongo. Ulitafuta elimu ili uje kuitwa mwanachuoni, na ulisoma Qur’an ili uitwe msomaji; na hivyo ndivyo ulivyoitwa’. Kisha hukumu itapitishwa dhidi yake na kisha atachukuliwa na kuburuzwa huku uso wake umeelekea chini na kutupwa ndani ya moto. Kisha ataletwa mtu ambaye Mwenyezi Mungu alimfanya kuwa tajiri mkubwa na kumjaalia kila aina ya mali. Baada ya kuletwa Mwenyezi Mungu atamfanya azihesabu neema zake kwake na hivyo mtu yule atazihesabu na huku yuko radhi nazo. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu atamuuliza, ‘Je ulifanya nini kama shukurani?’. Atasema, ‘Nilitumia fedha katika kila namna ambayo wewe unairidhia’. Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema, ‘Unasema uongo. Ulifanya hivyo ili uonekane ni mtu mkarimu; na hivyo ndivyo ulivyoitwa’. Kisha hukumu itapitishwa dhidi yake na kisha atachukuliwa na kuburuzwa huku uso wake umeelekea chini na kutupwa ndani ya moto”. (Muslim, ‘imara, 152).

Katika mada hii hii, Rumi naye anasema, “Ewe mwenye kudharau! Ninatamani lau ungelielekeza uso wako kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huku ukiwa na moyo safi pindi unaposujudu ndani ya ibada na kufahamu vizuri zaidi maana na kusema, “Utukufu ni wako Ewe Mola wangu, ambaye umetakasika na aina zote za upungufu, kama kweli ulikuwa ume-sujudu kwa moyo wako, na si kwa mwili wako pekee!”

Matendo ya ibada yasiyotekelezwa kwa moyo safi yanakuwa na upungufu na yanakuwa yamechanganyika na ushirikina. Ufunguo wa kuyasafishwa matendo ya ibada ni usafi wa moyo. Amali yoyote iliyofanywa nje ya moyo safi inakuwa haina manufaa kwa mtekelezaji. Baada ya kukiri imani ya kweli, jambo linalosisitizwa na Qur’an baada ya hili ni kutekeleza swala za faradhi; na wale wanaotekeleza swala hizo za faradhi bila ya kuwa na moyo safi wanatahadharishwa kama ifuatavyo: “Basi, ole wao wanao sali, Ambao wanapuuza Sala zao” (al-Maun, 4-5). Kutokana na ukweli wa jambo hili Junayd al-Baghdadi anasema, “Usafi wa moyo unamaanisha kuyatakasa matendo yako dhidi ya uchafuzi”. Mtu mwema mwingine anaangaza katika usawa unaotakiwa kuchukuliwa katika tendo lolote la kiibada pale anaposema, “Kujidai na kujipongeza kwa kuwa kwako na moyo safi moja wapo ya kutokuwa na moyo safi”. Katika kuzingatia katika usafi wa moyo, hatari kubwa inapatikana pale mja anapoanza kujihukumu juu ya uchamungu wake mwenyewe. Kutokana na hili, Mjumbe wa





Mwenyezi Mungu- rehema na amani ziwe juu yake- anasema, “Kuweni na moyo safi katika dini. Kama mtafanya hivyo, basi hata kiasi kidogo cha amali kitakutosha”. (Hakim, Mustadrak, IV, 341). Katika *hadith* nyingine Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- anasisitiza kanuni hiyo hiyo pale aliposema, “Kwa hakika Mwenyezi Mungu haangalii nyuso zenu na mali zenu, bali anaangalia nyoyo zenu na amali zenu” (Muslim, Birr, 34).

### 5. Usufi unamaanisha kusimama kwa ushupavu katika njia iliyoonyooka (*istiqamah*)

Katika istilahi za kisufi, *istiqamah* ni kushikamana kisawa sawa na Qur’an na *Sunnah*. Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu anamuamrisha Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake- pamoja na wau-mini wawe na *istiqamah*, pale aliposema:

فَاسْتَقِمُّ كَمَا أُمِرْتَ وَ مَنْ تَابَ مَعَكَ وَ لَا تَطْغَوْا

“Basi, simama sawa sawa kama ulivyo amrisha, wewe na wale wanao elekea kwa Mwenyezi Mungu pamoja nawe; wala msikiuke mipaka. Hakika Yeye anayaona yote myatendayo.” (Hud, 112).

Imepokewa kuwa kutokana na sura hii Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- alisema, “Surat Hud imenizeesha” (Tirmidhi, Tafsir Surah, 56/6). Washereheshaji wameyaelezea maamrisha haya yaliyompelekea Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kuwa na mzungu mzito<sup>9</sup> wa kiroho kama ifuatavyo, “Ewe Mtume, huna budi kufanya mambo yako kulingana na maadili na masharti ya Qur’an na kuwakilisha mfano hai wa msimamo, kiasi kwamba kusiwe na shaka na kasoro katika mwenendo wako. Usiyafikirie maneno yenye kuumiza kutoka kwa washirikina na wanafiki na badala yake muachie Mwenyezi Mungu awashughulikie. Simama imara katika njia iliyonyooka katika wajibu wako binafsi na wa kijamii, kama ulivyoamrisha na usikengeuke katika njia iliyonyooka. Usihofie aina yoyote ya ugumu ambayo inaweza kukufanya ufikirie kuwa inaweza kukuzuia usikamilishe jukumu lako la kiutumeme. Hata kama utakutana na vikwazo vya namna gani, na Mola wako pekee ndiye msaidizi wako”<sup>10</sup>.

9. Qurtubi, *al-Jami*, IX, 107

10. Elmalih M. Hamdi Yazir, *Hak Dini Kur'an Dili*, IV, 2829-2830.





Kutokana na aya hii ya Qur'an, Abdullah ibn Abbas- radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- anasherehesha kwa kusema, "Kulingana na uzito wa aya hii juu ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- hakuna maneno mengine ya Qur'an yenye uzito na yenye kutoa changamoto kama haya" (Nawawi, Sharh-i Sahih Muslim, II, 9) Ingawa maneno haya kwa juu yanaonekana kumlenga Mtume- rehema na amani ziwe juu yake- mwenyewe, lakini changamoto yanayoitoa inawaenea waumini wote, na kwa maana hiyo, aya hii haikuhusu ustawi wa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- pekee, bali ilihusu ustawi wa wafuasi wake wote katika kusimama imara katika njia iliyonyooka. Kwa namna yoyote ile msimamo wa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- tayari umeshathibitishwa na Qur'an, pale inapomuongelea kuwa yupo "...katika njia iliyonyooka" (Yasin, 4) Kwa hiyo kilichompelekea Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- kuzeeka ilikuwa ni huruma aliyokuwa nayo juu ya uongofu wa wafuasi wake.



Kwa kuwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- alifanywa kuwa Mtume wa mwisho kwa wanadamu, ujumbe huu utabakia hai milele, kama muongozo wa kuwaonyesha wanadamu namna ya kuelekea katika njia iliyonyooka, njia ambayo itawafikisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Qur'an inakiri kuwa mapenzi na huruma ya Mola wetu juu ya wanadamu inategemeana na utii wao kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, kama ilivyotajwa katika aya ifuatayo:

قُلْ إِنْ كُنْتُمْ تُحِبُّونَ اللَّهَ فَاتَّبِعُونِي يُحْبِبْكُمُ اللَّهُ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ذُنُوبَكُمْ

وَ اللَّهُ غَفُورٌ رَحِيمٌ

"Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuatani mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu." (Al- i Imran, 31)

"Sema: Mt'iini Mwenyezi Mungu, na mt'iini Mtume. Na mkigeuka, basi yaliyo juu yake ni aliyo bebishwa, na yaliyo juu yenu ni mliyo bebishwa nyinyi. Na mkimt'ii yeye mtaongoka. Na hapana juu ya Mtume ila kufikisha Ujumbe wazi wazi." (an-Nur, 54)





Katika suala hili Dhunnun-i Misri anasema, “Yeyote anayefuata *Sunnah* ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, anakuwa amethibitisha mapenzi yake kwa Mwenyezi Mungu kivitendo”. Pia maneno ya Bayazid Bistami yanafanana na haya: “Hata kama utamuona mtu yuko angani na huku amekunja miguu yake, angalia ikiwa mtu huyu anatekeleza maamrisha ya Mwenyezi Mungu au la, je anafuata *Sunnah* na kuchunga mipaka aliyowekewa na Mwenyezi Mungu. Ikiwa utashindwa kuyaona haya, basi usije ukatangaza utukufu wake, licha ya kitendo chake kisicho cha kawaida”. Kiini na mafanikio ya kubakia kwenye msimamo katika “njia iliyonyooka” yametajwa ndani ya Qur’an ambayo inathibitisha kuwa “...Na wenye kumt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!” (an-Nisa, 69). Kama ambavyo aya hii ya Qur’an inavyoonyesha, njia iliyonyooka ambayo kuifuata kwake kunatokana na kumtii Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, ni njia wanayoifuata ‘waliochaguliwa’. Kiini cha kusimama imara kwenye njia iliyonyooka ni imani na uchamungu ambao unatamfanya mtu amkumbuke Mola wake wakati

wote, na vitu hivi vinakaa katika moyo pekee. Hivyo kusimama imara katika njia iliyonyooka kunaashiria mchakato wa kuunganisha moyo na mwili. Imani, usafi wa moyo na kiasi ndani ya moyo vinamfanya mtu abakie katika njia iliyonyooka wakati wote.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake- amesema, “Ikiwa ulimi hausimami imara katika njia iliyonyooka basi moyo hauwezi kufanya hivyo; na ikiwa moyo hausimami imara katika njia iliyonyooka basi imani haiwezi kuwa imara” (Ahmad Ibn Hanbal, Musnad, III, 198). Siku moja swahaba aliomba ushauri kwa Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, kisha Mtume akamshauri aseme, “...Ninathibitisha imani yangu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kisha kuwa na msimamo katika hilo” (Muslim, iman, 62).

Hakuna hali ya kiroho ya juu zaidi ya kusimama imara kwenye njia iliyonyooka katika hali zote, na pia hakuna amri iliyo ngumu kama hii. Kusimama imara katika njia iliyonyooka ni kushikamana na njia kiasi katika matendo yote ya ibada bila ya kuvuka mipaka, na kutopumzika katika njia ya Mwenyezi Mungu, ambaye utukufu ni wake. Pia kunahusiana na kutekeleza maamrisha matakatifu kadiri ya uwezo wako. Kutokana na ugumu wa jambo hili, kusimama imara katika njia iliyonyooka kumechu-





kuliwa kuwa kitendo (*karamah*) kikubwa ambacho watu wema wanaweza kukihimili. Watu wema wameweka umuhimu mkubwa katika suala la kubakia kwenye msimamo; kwa maneno mengine kuendelea kuifuata njia ya heri ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- huku ukiwa na subira katika msimamo huu. Rumi analielezea suala hili vizuri zaidi pale anaposema:

*Hali ya kuwa roho yangu ipo ndani ya mwili wangu,  
Mimi ni mtumishi wa Qur'an na ni vumbi chini ya unyayo wa  
Mtume aliyebarikiwa,*

*Kama mtu yeyote anasimulia kitu kingine kinyume  
na hiki kutokana na maneno yangu,  
Mimi niko mbali na maneno yake na yeye mwenyewe,*

*Kama mtu ataenda kukaa katika meza nyingine tofauti  
na meza ya Mtume,  
Afahamu kuwa shetani atakula naye sahani moja;*

*Kwani chakula kilicholiwa katika meza nyingine tofauti  
na meza ya hekima,  
Hukwama katika koo la mlaji...na hufikia hata kulitoboa.*

## **6. Mwenendo wa kisufi ni (*rida*) na kujisalimisha (*taslimiyyah*)**

Neno *taslimiyyah* linamaanisha kujisalimisha, utii na kukubali kitu bila ya kubisha. Neno uislamu linatokana na mzizi mmoja. Usufi unajitahidi kujenga hisia za kuridhika na kujisalimisha kwa Mola ndani ya moyo, ili kufungua njia kwa mja kumkurubia Mola wake na kuhisi kuwa anaangaliwa na Mwenyezi Mungu wakati wote. Maisha ya duniani yamejawa na maumivu, wasiwasi na madhara, bila kusahau ukweli kuwa mtu hana budi kupambana na mitego ya aina mbalimbali iliyowekwa na nafsi. Vyote hivi vinaweza kupungua pale mja atakaposhikamana na kukinai na kujisalimisha kwa Mola wake; kwani maumivu ya matatizo yataanza kupungua pale mja atakapoanza kutambua kuwa tabu zote hizi ni baraka zilizojificha kutoka kwa Mola wake. Hapo ndipo maumivu yanapokuwa sababu ya kusherehekea badala ya kulalamika.

Cha zaidi ni kwamba *taslimiyyah* inaashiria kukubali kwa moyo wa mja juu ya kila kitu alichokadiriwa; nahitajika kukubaliana na kila kitu ulichokadiriwa baada ya kuchukua tahadhari ya lazima. Mfano wa dhahiri





juu ya *taslimiyyah* unaweza kupatikana kwa nabii Ibrahim- amani iwe juu yake- na mwanae Ismail- amani iwe juu yake. Baada ya kuagizwa na Mwenyezi Mungu amtoe kafara mwanae, Ibrahim- amani iwe juu yake- alikubali amri hii yenye kuogopesha bila kusita, wakati mwanae ismail- amani iwe juu yake- naye alikubaliana na amri hii tukufu ya kutolewa kwake kafara. Qur'an tukufu inaonyesha heshima juu ya tabia yao ya mfano, hivyo wote wawili wanatukuzwa kwa "...Basi wote wawili walipo jisalimisha, na akamlaza juu ya kipaji." (As-Saffat, 103).

Mja hana budi kujisalimisha kwenye maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu na kuridhika na kila kitu alichopangiwa na Mwenyezi Mungu. Kufikwa na magumu na mitihani huku ukiwa na subira na kumua- chia mambo yote Mola wako ni jambo la lazima. Na ukweli ni kwamba njia ya kuelekea kwenye ukamilifu wa imani imejawa na mitihani. Kutokana na haya Shaiq al-Balkhi anasema, "Lau mtu angelijua malipo ya tabu, asingelitamani tabu hiyo imuondoke". Baada ya kulitambua hili watu wema wameweka huzuni na raha katika mtazamo mmoja. Kwa kuwa kuzidisha kukazia katika huzuni na kupitiliza katika furaha si chochote bali ni mitego ya nafsi, ni muhimu kuyapokea yote haya kwa kuridhika na kujisalimisha na huku ukifahamu kuwa daima kile ulichopangiwa kitakufika tu.

Huruma na upendo ni mambo mengine yanayoendana na taslimiyyah, kwa kiasi ambacho mpenzi anakubali kila kitu kiwe kizuri au kibaya, kitu ambacho kinatoka kwa kipenzi chake, na anakichukulia kuwa ni fursa yake ya kuonyesha ukweli wa mapenzi yake. Hii ndio sababu iliyompelekea Abu Ali Rudbari kusema, "Usufi unamaanisha kupiga magoti kwenye mlango wa kipenzi chako na kusubiri kwa unyenyekevu na kujisalimisha, hata kama inafahamika kuwa kipenzi atamuambia mpenzi aondoke". Mja ambaye moyo wake umejaa mapenzi anakubaliana na kila kitu kinachotoka kwa Mola wake; kukubaliana kunakoendana na uzito wa mapenzi yake kwake. Kujisalimisha kwa kweli kwa Ibrahim- amani iwe juu yake- kulipelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu akaugeza moto mkali kuwa bustani ya mawaridi ndani ya sekunde. Kukinai na kujisalimisha juu ya qadari kulikofanywa na Yaqub- amani iwe juu yake- kulipelekea maumivu makubwa yenye kuumiza ya kutengana na mwanae mpendwa Yusuf- amani iwe juu yakae- aseme, "Lakini subira ni njema" (Yusuf, 18).

Sufi wamefanya kujisalimisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa jambo la lazima katika maisha yao, kama tunavyoweza kuona katika maneno ya Rabia al-Adawiyya, "Mpenzi humtii kipenzi chake bila ya





kushurutishwa”. Hii inamaanisha kuwa *taslimiyyah* inahusiana na kutii kwa mapenzi. Maswahaba walisafisha madaraja yao ya wema kwa kupitia kwenye mapenzi, utii na imani yao juu ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, jambo lililowapelekea kuwa mifano ya kuigwa katika kuviongoza vizazi vya waislamu vilivyofuata.

Kutokana na maana ya usufi iliyokwishatolewa tunaweza kumaliza kwa kusema kuwa mwenendo wa kisufi unamuhitaji muumini afanye juhudi ya kuiweka dini katika matendo kwa kujitakasa dhidi ya uchafu wa kiwiliwili na kiroho na kujipamba na tabia njema. Kwa njia hii muumini atafikia kwenye ufahamu mkubwa wa mambo yote ya kimwili na kiroho yanayotokea na ataweza kufahamu siri ambazo haziwezi kufahamika kwa kutumia uwezo wa kimantiki pekee. Usufi unahusiana na kujitahidi kuishinda nafsi na kuufanya moyo ufurahie raha zisizo na kikomo. Kwa mtazamo mwingine pia mwenendo wa kisufi ni aina ya fikra ya kielimu inayofafanua namna ambavyo mwili unavyoifunga minyororo roho ndani ya gereza na kufunga milango, ili kuizuia isitambue ukweli na hekima ili-yopo kwenye matukio yanayotokea. Katika kumpatia mwanadamu funguo ya kufungulia milango ya mwili, mwenendo wa kisufi unaipelekea roho kutoka kwenye gereza hilo na kuiwezesha kuyafahamu masomo na hekima zilizojificha kwenye aina zote za matukio yanayoweza kuonekana, na kufundisha njia sahihi ya kuyathaminisha kutokana na ufahamu wa kiroho.

Ibrahim Effendi ambaye ni Sheikh maarufu wa nyumba ya kisufi ili-yopo Aksaray, anaelezea maana ya usufi katika mistari ifuatayo:

*Kuwa sufi mwanzoni, ni kuwekwa huru na uwepo wa kimwili,  
Mwishoni, ni kupanda katika kiti cha enzi cha moyo.*

*Kuwa sufi mwanzoni, ni kujivua mwili,  
Mwishoni, ni kuingia kwenye kasri la Mola la siri.*

*Kuwa sufi, ni kuondoa vazi la mwili lililochakaa,  
Kwa malipo ya uwepo uliotakasika, na nuru ya Mola...*

*Kuwa sufi, ni kuwasha mshumaa wa moyo kwa mwangaza mtukufu,  
Na hivyo kuurusha kwenye moto wa upendo, kwa ajili ya kuungua milele...*

*Kuwa sufi ni kujiokoa kutoka kwenye mikono ya nafsi,  
Na hivyo kufuata sheria na kufikia kwenye imani ya kweli.*

*Kuwa sufi ni kuendana na misingi ya Mola,  
Na hivyo kupata msaada na tiba ya shida.*







*Kuwa sufi ni kuufungua mwili kwa ufunguo wa jina la Mola,  
Na kuingiza kwenye milango ya udhalili.*

*Kuwa sufi ni kuyaingiza maneno ya kisufi kwenye vitendo,  
Kiasi kwamba kila neno linalotolewa linakuwa ni sehemu ya maisha.*

*Kuwa sufi ni kuweza kutafsiri ndoto na maneno,  
Kuwa siri katika upande wa kulia wa kiti cha maisha.*

*Kuwa sufi ni kuwa na furaha na kutatizwa mbele ya Mwenyezi Mungu,  
Kustaajabu mbele ya siri kutoka kwa Mwenyezi Mungu.*

*Kuwa sufi ni kuondoa moyo kila kitu kinyume na Mola,  
Kuuelekeza moyo kwenye kiti chake cha enzi kwa kupitia kwenye imani.*

*Kuwa sufi ni kufika mashariki na magharibi kwa mpepeso wa macho,  
Hivyo kuwajali watu wote na kuwapa hifadhi.*

*Kuwa sufi ni kushuhudia uwepo wa Mola katika kila kitu,  
Hivyo kuwa jua lenye kumulika viumbe vyote.*

*Kuwa sufi ni kuzielewa lugha za viumbe vyote,  
Kujihisi una jukumu la Suleiman katika ulimwengu wa akili.*

*Kuwa sufi ni kukamata kishiko imara, kujibebesha jukumu zito,  
Hivyo kuitafakari Qur'an na kusambaza habari za neema takatifu.*

*Kuwa sufi ni kukaa na viumbe vyote kwa kupitia jina la siri la Mola,  
Uwezo wa kushikamana na maamrishi ya Qur'an.*

*Kuwa sufi ni kumtafuta Mola kila unapopatupia jicho lako,  
Hivyo kugeuza uzito kuwa wepesi kwa mwanadamu mwenzako.*

*Kuwa sufi ni kuuelekeza moyo kwenye hifadhi ya elimu takatifu,  
Kulipeleka tone, ambalo ni mwanadamu, kwenda kwenye bahari pana.*

*Kuwa sufi ni kuunguza uwepo wetu sote kwenye moto wa maangamizi;  
Na kisha kufufuka kwa kupitia kwenye nuru ya uthibitisho.*

*Kuwa sufi ni kuita katika njia, kwa kusema "Mwenyezi Mungu anato-  
sha" (ar-Rad, 43),*

*Kutoa matumaini ya furaha kwa ajili "kurejea" kusikoepukika. (al-  
Ghashiyah, 28)*

*Kuwa sufi ni kufufuka baada ya kufa mara elfu moja kila siku,  
Kuwa kama mfufuaji wa maiti za viumbe vyote.*





*Kuwa sufi ni kuangamiza uwepo kuelekea kwenye uwepo mtakatifu,  
Kujificha kwenye ukaribu ulio "karibu zaidi". (an-Najm, 9).*

*Kuwa sufi ni kuisalimisha roho kwa kipenzi chako na kuwa huru;  
Kuwa pamoja na kipenzi milele.*

*Kuwa sufi ni kwa Ibrahim kuwa mja wa kweli wa Mola,  
Kushikamana na kutii sheria ya Muhammad.*





**M**ada ya usufi ni pana na yenye kina kirefu kama bahari; kwani inajumuisha kila kitu kinachohusiana na roho na nafsi ya mwanadamu.



### C. MADA YA USUFI

Maana na tafsiri mbalimbali zilizotolewa kuhusiana na usufi zinaashiria upana wa mada yake. Ndio maana tunaweza kusema kwamba mada ya usufi ni pana na yenye kina kirefu kama bahari; kwani inajumuisha kila kitu kinachohusiana na roho na nafsi ya mwanadamu. Kimsingi umegusia hali za kiroho zinazopitiwa na msafiri katika safari yake ya kiroho, pamoja na watu anaokutana nao njiani, pamoja na mambo anayokutana nayo, vitu anavyovifahamu, na namna anavyomuabudu Mola wake; ingawa haya ni machache katika upana wa mada zilizopo kwenye usufi. Kama si kukata kwetu mada fupi yenye kueleweka tungeliendelea kutambaa ndani zaidi kwenye mada ya usufi.

Zaidi ya hayo mwenendo wa kisufi unajihusisha na hali za kiroho na vituo ambavyo anapitia mwanafunzi katika mchakato wa kuboresha roho yake kutoka kwenye ubichi na kuelekea kwenye kuiva, kwa kuutakasa moyo na roho na yake. Kwa maneno mengine tunaweza kusema usufi unajihusisha na njia sahihi za kuweza kuutakasa moyo na roho na kupata utambuzi wa ndani na nje, na hivyo kupelekea matendo ya sufi yawe yanaendana na maamrishi ya Mola na matokeo yake kupata furaha kesho akhera. Matokeo ya haya yote ni kujipamba na mwenendo bora na kuyafahamu mambo mbalimbali ya kiroho. Na kiini cha yote haya ni kuhakikisha mtu anaonja ladha ya *ihsan*, yani kuingiza imani moyoni, na kufurahia raha yake isiyoelezeka.

Kwa maelezo mengine ni kwamba mwenendo wa kisufi unahusiana na kanuni na njia za kukuwezesha kuzielewa hekima za Mola, siri na malengo yaliyofichwa kwenye majina na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu, pamoja na ubainifu wake mkubwa ulioenea ulimwengu kote. Katika suala hili usufi unazungumzia fikra zinazohusiana na vitu visivyoonekana, roho, moyo na nafsi; pamoja na hali za kiroho kama vile utambuzi (*kashf*), ufunuo (*ilham*),





ushuhuda wa kiroho (*mushahada*), raha (*wajid*), na mapenzi (*'ishq*), na pia hali za kiroho zinazopatikana kwa kupitia hali hizi.

Kwa ufupi usufi unahusiana na kutoa uwezo wa kiroho wa kuona na kushuhudia majina na sifa za Mola na kuwezesha kupatikana kwa elimu takatifu (*marifatullah*), na kumpatia mwanadamu utambuzi halisi juu ya ulimwengu, Qur'an pamoja na yeye mwenyewe, kwa kumpitisha kwenye safari ambayo mwisho wake hupatikana ukomavu wa imani.





**L**engo la mwenendo wa kisufi ni kuingiza ladha ya maadili ndani ya moyo wa muumini; ladha ya huruma, upendo, ukarimu, msamaha na shukurani.



## D. LENGU LA USUFI

Kwa kuangalia tu tafsiri na somo la usufi, ni rahisi kuona kuwa umebeba lengo muhimu na tukufu kwa wanadamu. Utekelezaji wa lengo hili ulianza tokea kwa Mtume wa kwanza na lilitokelezwa na Mitume wote waliofuata mpaka Mtume wa mwisho, na baada yake walifuatia watu wema. Mtu anaweza kulisema lengo hili kuwa ni 'kushikamana na jukumu la utumishi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika namna bora uwezekanavyo'. Tukihukumu kwa namna hii utaona kwamba usufi unawakilisha lengo kuu la wanadamu; lengo la kumtoa kila mwanadamu katika maadili mabovu na kumpamba kwa sifa za kimaadili anazoziridhia Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake- rehema na amani ziwe juu yake- na hivyo kuwawezesha kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hii inamaanisha kuwa nafsi haina budi kuwekwa chini ya mamlaka ya dini na kujitahidi kutekeleza matendo ya ibada kwa moyo safi, kama *ihsan* inavyotaka. Jambo hili linautakasa moyo na kuuelekeza kwenye ukweli wa kiroho na mwishoni kwenye radhi za Mwenyezi Mungu, ambaye utukufu ni wake.

Tukizingatia dhati ya asili, mwanadamu ameumbwa na kufanywa mbora juu ya viumbe vyote na ameumbwa 'katika umbile bora' (at-Tin, 4); Lakini katika kujitenga na lengo lake la asili, mtu amekuwa na tabia ya kujiharibia mwenyewe asili yake na kufikia kuwa mtata zaidi ya wanyama. Kwa hiyo, jambo la pekee la kuonyesha heshima na thamani ya mwanadamu ni imani (*iman*), na baada ya hapo maadili mema (*akhlaq*). Jukumu la Mitume lilikuwa ni kuutakasa moyo na roho na kuzijaza imani na maadili mema. Kutokana na kuwa kwao warithi wa Mitume, watu wema nao wanaendelea kutekeleza jukumu hili tukufu na hivyo kuonyesha mifano hai ya mafundisho ya Mitume kwa kufundisha na kuifanyia kazi elimu iliyopo nyoyoni mwao katika jamii zao.

Sufi wanajaribu kumfuata Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani





ziwe juu yake- katika kila jambo, ndani na nje. Katika jamii zao, wanatekeleza majukumu yaliyotekelezwa na Mitume kinadharia na kivitendo. Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anadokeza ukweli wa jukumu lao pale anaposema, “Wanachuoni wa kweli ni warithi wa Mitume” (Abu Dawud, ‘ilm, 1). Hivyo usufi umelichukua lengo la Mitume; lengo la kuwaongoza watu kuelekea kwenye ukomavu wa kiimani kwa kuwaepusha na matamania ya nafsi na utovu wa maadili.

Katika *hadith al-qudsi*, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema, “Dini hii ni dini ninayoithibitisha. Mambo muhimu yanayofaa katika dini hii ni ukarimu na maadili mema...kwa hiyo ziendelezeni sifa hizi mbili kama mnaifuata dini hii” (Haythami, Majma’u al-Zawa’id, vill, 20). Ili kuendana na amri hii, mwenendo wa kisufi unalenga kuingiza ladha ya maadili ndani ya moyo wa muumini; ladha ya huruma, upendo, ukarimu, msamaha na shukurani.

Lengo jingine la usufi ni kuwasaidia wale waliozaliwa na uwezo mkubwa wa kiroho wajiboreshe wenyewe katika njia ya kujizuilia na machafu na kuwa wachamungu. Mafundisho ya kisufi yanawaongoza watu kama hao katika kuboresha imani zao, kwa kuwawezesha kukandamiza matamania ya nafsi zao na kujikurubisha kwa Mola wao; na hivyo kuwaongoza katika njia ya kumtambua Mola wao. Katika suala hili sufi wanasukumwa na aya ya Qur’an isemayo:

إِنَّا عَرَضْنَا الْأَمَانَةَ عَلَى السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَالْجِبَالِ فَأَبَيْنَ أَنْ يَحْمِلْنَهَا  
وَ أَشْفَقْنَ مِنْهَا وَ حَمَلَهَا الْإِنْسَانُ إِنَّهُ كَانَ ظَلُومًا جَهُولًا

“Kwa hakika Sisi tulikadimisha amana kwa mbingu na ardhi na milima; na vyote hivyo vikakataa kuichukua na vikaogopa. Lakini mwanaadamu akaichukua. Hakika yeye amekuwa dhaalimu mjinga.” (al-Ahzab, 72) Vivyo hivyo lengo la mwenendo wa kisufi ni kuwaokoa watu kutokana na dhulma, dhidi yao wenyewe na watu wengine, na ujinga, na kuwapamba na sifa za wema. Kinyume cha dhulma (*zulm*) ni haki (*adl*), vitu ambavyo vinaonyesha uhalali na usawa wa matendo yaliyotekelezwa na mja. Wakati kinyume cha ujinga (*jahl*) ni ujuzi (*ilm*). Ili kuwa mtu mwenye ujuzi huna budi kuzikamata sayansi za wazi na za kificho. Kuhusiana na suala hili Ghazzali anasema, “Warithi wa Mitume ni wale wenye elimu za sayansi za wazi na kificho”.





Ukombozi wa mtu unategemeana na kujitenga na sifa mbaya zinazosababishwa na nafsi na kutekeleza mambo kulingana na masharti yaliyowekwa kwa ajili ya amali njema (*amal salih*), na bila kusahau kuiweka elimu katika matendo, kwa kufanya hivi kutampelekea mtu kuwa mwanaadamu mwema. Katika istilahi za kisufi, haya yanamaanisha kuigeuza elimu ya kawaida na kuwa *irfan*, yani utambuzi mkubwa au hekima. Katika upembuzi wa mwisho usufi unajihusisha na maelekezo ya kinadharia na kivitendo katika kuhuisha jambo hili. Watu wema ni wale wanaolitambua lengo hili na hivyo kurekebisha ubora na uzito wa imani na uchamungu wao; ingawa wako wachache kiidadi. Ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu amewataja watu hawa pale aliposema:

أَلَا إِنَّ أَوْلِيَاءَ اللَّهِ لَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ  
وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا وَكَانُوا يَتَّقُونَ

“Jueni kuwa vipenzi vya Mwenyezi Mungu hawatakuwa na khofu wala hawatahuzunika. Hao ni ambao wameamini na wakawa wanamcha Mungu.” (Yunus , 62-63)

Pale imani itakapojikita ndani ya moyo wa muumini itamuokoa kutokana na kila namna ya uchawi na itamuweka karibu na Mola wake. Kwa upande mwingine uchamungu ambao unamaanisha kumkumbuka Mola wako wakati wote, huutakasa moyo kutokana na vitu vyote kinyume na Mola. Kwa namna hii, moyo wa muumini unafikia ubora wa kuwa “mpaka wa jicho takatifu” na hivyo kuwa mpokeaji wa ufunuo na hekima kutoka kwa Mwenyezi Mungu.





**S**iku ambayo mali haitofaa kitu wala wana. Isipokuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi (as-Shuara, 88-89).



## E. ULAZIMA WA KUFUATA USUFI

Usufi unawakilisha kiini cha imani ya kiislamu; kama ilivyo kokwa ya tunda inavyolipa tunda ladha yake. Ni jambo la wazi kwamba kimsingi mtu ana vitu viwili: mwili na roho. Kila moja wapo ya vitu hivi ina mahitaji na matakwa ya kiasili. Uislamu hauvikatai vitu hivi, kwa kuwa ndivyo tulivyoubwa navyo na kuzaliwa navyo; badala yake unavitambua kama vitu vya kiasili. Uislamu unalenga kuboresha yake matakwa chanya na kupunguza matakwa na vishawishi hasi kwa kiwango kidogo kadiri iwezekanavyo na kuyaelekeza kwenye mwisho chanya. Na ili kuendana na lengo hili, uislamu umeweka kanuni kadhaa.

Kama mtu atapuuzia mahitaji yake ya kiroho na kuyajenga maisha yake yote kulingana na mahitaji na matarajio ya kimwili, hawezi kupata furaha na utulivu, kwa kuwa anatakiwa afanye jambo litakalotosheleza mahitaji ya kiroho yasiyozuilika. Dini inatoa utaratibu wa uwiano sawa kati ya ulimwengu wa kiroho na kimwili. Upande mmoja inamuongoza mwanadamu kwenye ulimwengu wa kimwili, lakini kwa upande mwingine haikatai wala kupuuzia mahitaji ya lazima ya ulimwengu wa kiroho. Dini hufafanua matakwa ya kimwili na kuyawekea maana inayokubalika mbinguni. Pale mtu atakapoanza kukitazama kila kitu kwa mtazamo wa kimwili, atianza kutambua kila kitu, hata vile vitu visivyoonekana kwa mtazamo wa kimwili. Atashindwa kuona ukweli wa kiroho kwa kupitia mtazamo wa kimwili. Hii ni sababu moja wapo miongoni mwa sababu kuu zinazowapelekea watu wengi waupinge mwenendo wa kisufi.

Katika hali yake ya asili, na isiyoharibiwa, utambuzi wa mwanadamu umeegemea kwenye siri za kiroho na ukweli wa kidhahania, na vile vile kwenye uwepo imara wa kiroho. Jambo la msingi ni je mwanadamu anaitosheleza roho yake au la, kama alivyo tayari kutosheleza mahitaji ya kimwili. Leo hii wamagharibi wengi wanahangaika kupambana na







mmomonyoko wa maadili licha ya kufikia kilele cha kujiridhisha kimwili, hivyo wamejikuta wameingizwa kwenye mashimo ya upagani. Hata ndani ya Roma ambako ndio kitovu cha ukatoliki, wapagani wapo kwa idadi kubwa katika jamii, haya kwa kuwa wameshindwa kutosheleza mahitaji ya kiroho na kimwili. Sababu ya msingi inayopelekea kuwepo kwa tatizo hili ni ukweli kuwa wamepoteza muungano kati ya asili takatifu na nyoyo zao. Kwa kuwa dini yao ya sasa imepotoshwa kutokana na kuingiliwa na mwanadamu, imepoteza utukufu wake na hivyo haiwezi tena kutosheleza matakwa ya asili ya mwanadamu. Na kwa sababu hii wamagharibi wengi hawahisi raha ya ndani katika dini yao; wala hawafikii furaha na utulivu wa kweli.

Mtu asiye na raha ya kiroho inayopatikana katika dini, anakiangalia kila kitu, hata vile vitu dhahania, katika mtazamo wa kimwili na kuvichambua katika namna mbaya kabisa. Matokeo yake uelewa wa dini yake unakuwa mdogo au unapotea kabisa.

Lakini kwa upande wa usufi, unamuongoza mtu kuelekea kwenye roho. Hufungua njia inayofaa kwa ajili ya kutosheleza uwezo wa kiroho. Kama tutapuuzia upande wa kiroho wa dini, upande ambao unamfanya mwanadamu atosheke, tutakuwa tumempunja huyu mwanadamu kwa kiwango kikubwa. Kwa njia tutakuwa tunahamasisha manufaa ya nje na ya kidunia katika matendo ya ibada na utumishi, haya yatakuwa ni gharama ya kupuuzia lengo kuu ambalo litauridhisha moyo. Hivyo kwa mfano swala za kila siku, kufunga na kutoa sadaka kutachukuliwa kama mazoezi ya viungo, taratibu nzuri ya mlo na msaada wa kijamii. Uelewa na matendo ya namna hii katika dini yatachukuliwa kuwa ni kwa ajili ya maslahi fulani. Lakini hatutakiwi kuzipuuzia faida hizi moja kwa moja bali hatuna budi kutambua kuwa haya si malengo makuu ya ibada hizi, bali ni matunda yake tu.

Kama tutaweka mazingatio yetu kwenye manufaa ya nje pekee, tutakuwa tumepoteza maana halisi ya kutekeleza matendo ya ibada; na kwa kuwa mtazamo huu mbovu ungelitupeleka mbali na kiini cha uislamu, uelewa wetu usingelikuwa wa kiislamu. Kiini cha dini kinahusiana na kukamilisha mahitaji ya mwanadamu kiroho na kutosheleza silika yake kwa upande wa dini.

Kabla ya Mtume-rehema na amani ziwe juu yake- hajapandishwa mbinguni alipewa ufahamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu juu ya siri





iliyopo kwenye sura ya Qur'an *Inshirah* (Upanuzi). Kifua chake kilifunguliwa na kisha moyo wake ukasafishwa na kujazwa elimu na hekima, kama maandalizi ya kushuhudia mambo ya ajabu na siri kubwa na undani wa kiroho, mambo ambayo yako nje ya uwezo wa kibinadamu.

Mtume aliyebarikiwa-rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa na moyo safi na mwema kuliko wanadamu wengine, ukweli uliohibitishwa na hata makafiri wakubwa wa wakati ule. Licha ya haya yote lakini alitakiwa kufanyiwa upasuaji wa kiroho ili ajazwe uwezo wa kuweza kupokea siri nzito alizokuwa anatarajiwa kuzipokea kutoka kwa Mola wake, hivyo alipitia kwenye upasuaji ulioitwa *Shaqq-i Sadr* (Upanuzi wa kifua)<sup>11</sup>. Upasuaji huu unasisitiza juu ya umuhimu wa ulimwengu wa kiroho. Hivyo hata Mitume ambao walipendelewa kwa sifa ya kutotenda maovu (*isma*) lakini pia walipitia kwenye mchakato wa kusafishwa nyoyo zao kabla ya kwenda mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ikiwa Mitume ambao ni waja wa Mwenyezi Mungu waliochaguliwa iliwabidi kupitia katika mchakato wa usafi wa ndani, basi tunaweza kuona ni namna gani ilivyo muhimu kwa watu wa kawaida kupitia hatua hii, kwani mtu hawezi kuusogelea upambanuzi (*Latij*) huku akiwa na moyo muovu na katili. Jambo hili linaweza kulinganisha na hali ya mtu ambaye amepoteza milango ya fahamu ya kuona na kunusa na ambaye hawezi kufurahia harufu nzuri ya ua la waridi; au kutokuwa na uwezo wa kuona mandhari nzuri kwa kupitia dirisha lenye ukungu. Kwa hiyo ili kuweza kupokea siri takatifu na hekima, moyo hauna budi kusafishwa dhidi ya uchafu aina yoyote ile, kama tunavyokumbushwa na Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'an kwa maneno yanayosema, "Siku ambayo kwamba mali haiato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi." (as-Shuara, 88-89). Na moyo utatakasika kwa kupitia elimu ya kiroho pekee.

Wakati ukipita pembezoni mwa ufukwe unaweza kuona idadi kubwa

11. *Shaqq-i Sadr* au pia *Sharh-i Sadr* ni neno lenye kuelezea upasuaji walioufanya malaika juu ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake. Wakati wa upasuaji huu malaika walipasua kifua cha Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na kukijaza nuru takatifu na utulivu ili kuweza kumuongezea imani zaidi. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alifanyiwa upasuaji huu mara mbili katika maisha yake; mara ya kwanza ni wakati wa utotoni na mara ya pili ni kabla ya kupanda kwake mbinguni. Qur'an inalieleza suala hili kwa kusema, "Je hatukupanua kifua chako (ewe Muhammad)" (*Inshirah*, 1)





ya mawe, mawe ambayo yamezama ndani ya mchanga na yamesawazishwa kwa nguvu ya mawimbi, na mawimbi haya si tu yameondoa kasoro zote za mawe haya bali yameyaongezea uimara kama wa matale. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa kipande cha almasi. Baada ya kukatwa kwa mapigo maalum na fundistadi ndipo inapofikia hali yake nzuri ya kung'aa na kuwa kama kioo. Pia ili mtu apate kiasi kidogo cha dhahabu, hana budi kuchekecha kiasi kikubwa cha udongo. Tunachomaanisha hapa ni kwamba kila kitu hapa duniani hupitia aina fulani ya mchakato wa kusafishwa. Moyo nao hauna tofauti; kwani ili ufikie ubora wa usafi wa Qur'an hauna budi kupata elimu ya kiroho.

Moyo usio na elimu ya kiroho ni kama chuma ghafi na baridi. Ili kukiweka katika umbo fulani huna budi kukiweka kwenye moto ili kuondoa kutu yake, na kisha kukigonga kwa ustadi ili kugeuza ugumu wake kuwa ulaini. Ni kwa kupitia hatua hizi tu ndipo utaweza kukipa umbo unalokusudia. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa moyo; ili kuipa ubora unaohitajika unahitaji kuingizwa katika mafunzo ya kiroho, mafunzo ambayo yataufanya moyo uanze kushuhudia ukweli ambao hauwezi kuonekana kwa uoni wa kawaida na ambao hauwezi kutambuliwa na uwezo wa kimantiki. Uoni au ushuhuda huu wa kipekee unahusiana na hisia na utambuzi wa kiroho pekee.

Ili kufikia hatua hii ya ubora, mtu hana budi kuimarisha na kukomaza uwezo wa moyo wake. Kwa namna hii hii kama mtu wa kawaida ambaye hana mafunzo yoyote atakapojaribu kufanya kitendo ambacho kinahitaji mazoezi ya muda mrefu, anaweza akaishia kuvunja mifupa yake; lakini kitendo hicho hicho kinaweza kufanywa na mwanariadha aliye na mafunzo bila ya madhara yoyote. Uwezo wowote wa kimwili unaweza kupatikana kwa kukusanya nguvu zote za mwili na kulenga sehemu moja. Vivyo hivyo, ili moyo upate uwezo stahili wa kiroho, hauna budi kukusanya nguvu zote katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu, ambaye utukufu ni wake, na katika kumpenda Mjumbe wake- rehema na amani ziwe juu yake. Qur'an imegusia sharti hili pale iliposema:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ  
وَ إِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَىٰ رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُونَ





“Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi.” (Al-Anfa1, 2)

Ili kuupeleka moyo juu ya ubora huu kunahitajika kuusafisha na kuuweka mbali na dhambi na kisha kuukomaza kiroho; kwani moyo mgumu na usio na mafunzo yoyote hauwezi kuangaliwa na Mola kama inavyostahiki. Mwanafunzi wa shule ya awali hawezi kuelewa yaliyomo kwenye vitabu vilivyotumiwa na wanafunzi wa shule ya sheria, haya ni kwa kuwa akili yake yaijafikia ukomavu unaohitajika ili kuyapambanua mambo. Atakuwa bado anakabiliwa na miaka mingi ya elimu mbele yake. Vile vile moyo ambao haujakomaa unahitaji namna fulani ya elimu na mafunzo kabla ya kuweza kupambanua mambo katika njia ya Mwenyezi Mungu. Elimu na mafunzo haya ndiyo uthibitisho muhimu katika njia ya kisufi.

Hivyo kitu cha kuzingatia mno ni moyo ambao ubora wake ndio Mola anaouzingatia katika matendo yote ya ibada, kama ambavyo imethibitishwa na maneno ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake: “Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu hatazami miili yenu na muonekano wenu, bali anatazama nyoyo zenu” (Muslim, Birr, 33). Hili linaenea kwenye mambo yote. Kama mja atakula kwa lengo la kupata nguvu kwa ajili ya kutekeleza matendo yake ya ibada, basi kula kwake huku kutakuwa ni aina ya ibada. Kufanya kazi kwa ajili ya kupata kipato cha halali kwa ajili ya familia yako ni ibada; na kila hatua iliyopigwa kwa malengo hayo italipwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kuwa nia yake ambayo inapatikana moyoni ni nzuri.

Sawa na hili ni vazi. Kwa mfano kuvaa imamah ni sehemu ya *Sunnah* au mwenendo sahihi wa Mtume-rehema na amani ziwe juu yake. Mtu anayevaa imamah hana budi kulenga kukomaza imani yake na kufanya *sunnah* hii kuwa ndio utaratibu wake, na kwa mfano, kumpelekea kuwapenda na kuwahurumia wengine. Ukitekeleza *sunnah* hii kwa namna hii inaweza kumpelekea mtu kujivuna. Yunus Emre anauelezea ukweli huu vizuri zaidi pale anaposema, “Kama kuwa daruwesh ilikuwa ni kuvaa kilemba na johu, tungelivinunua vitu hivi kwa bei ndogo”.

Katika namna hii hii, kujifunika kwa mwanamke ni sharti katika uislamu. Hivyo mwanamke wa kiislamu hana budi kujifunika kwa nje tu, budi kwa ndani na kiroho. Wakati amejifunika mwili wake anaweza kuwa uchi katika maadili. Ikiwa mwanamke ni mjinga na hana aibu, anaweza





kuweka pembeni hijabu yake katika kipindi cha ugumu au pindi nafsi yake inapopata nafasi ya kumtawala. Wakati amejihifadhi mwili wake hana budi kutunza heshima yake, kwani yeye amekabidhiwa jukumu la kuwalea watoto wake na kutunza nyumba. Kwa sababu hii anahitajika kuwa na maadili ya hali ya juu katika kila kipengele cha maisha yake. Bila shaka maadili yake hayana budi kwenda sambamba na kujihifadhi kwake, jambo ambalo ni lazima alitekeleze bila ya kuvuka mipaka iliyowekwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kama ambavyo tumekwishasema mpaka sasa, kwa kuzingatia maamrishi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kujihifadhi sio mwisho wa safari bali ni sehemu tu au mwanzo wake.

Mfano mwingine ni kwamba, kujenga msikiti kunachukuliwa kuwa sadaka kubwa katika uislamu, lakini ikiwa mtoaji fedha hafanyi hivyo kutokana na ukomavu wake wa kimaadili bali kwa kuiridhisha nafsi yake kwa ajili ya kupongezwa tu, Mwenyezi Mungu atuepushie hilo, lakini thamani ya sadaka yake itakuwa ndogo mno na itakuwa kana kwamba hakufanya chochote. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu huwashusha na kuwadhalilisha wale ambao katika matendo yao wanajifurahisha wao wenyewe na wakati wote wanasema ‘Mimi’; na wakati Yeye anawatukuza wale wanaosema, “Ewe Mola! Haya si chochote bali ni fadhila na wema wako”. Hivyo sharti pekee la kufanya matendo yote ya mwanadamu yakubaliwe mbele ya Mwenyezi Mungu ni nia yao na maadili yao bora.

Kutokana na mambo yote yaliyotajwa, tunaweza kufikia kwenye majumuisho kuwa usufi unachukua nafasi muhimu katika dini ndani ya maisha ya mwanadamu; kwani huu ni mfumo wa kiroho wa elimu wenye malengo ya kufundisha kwa ubora namna ambavyo kila jambo linatakiwa kufanywa katika hali ya kiibada, na namna ambavyo kila tendo la ibada linatakiwa lifanywe katika njia ya kiroho iliyo safi. Hivyo kuna mambo mawili katika kila kitendo cha ibada; utaratibu na kiini. Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu Mtukufu hatoi maelezo ya kina juu ya taratibu za swala, kama vile ni mara ngapi tunatakiwa kurukuu na kusujudu katika swala moja. Lakini ametufahamisha kuhusu hali ya kiroho tunayotakiwa kuwa nayo wakati tunatekeleza vitendo hivi, na kuacha utaratibu wake uchukuliwe kwenye matendo ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake.

Hata mnafiki anaweza kukamilisha utaratibu wa kawaida au sharti la nje la kitendo fulani cha ibada. Kwa mfano mnafiki mkuu Abdullah ibn Ubayy ibn Salul, mara kwa mara alikuwa akihudhuria swala za faradhi katika msikiti wa Madina nyuma ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na





amani ziwe juu yake; lakini kitendo hiki kilikuwa si kitu bali ilikuwa ni utaratibu wake ambao haukuwa na dhati ya kweli. Matendo ya ibada yali-yofanywa kwa ajili ya kukamilisha utaratibu pekee hayana malipo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kukubalika kwake kutategemea muunganiko wa utaratibu na kiini chake.

Upembuzi wa makini katika aya za Qur'an na maneno ya Mtume juu ya nguzo za uislamu kama vile swala tano, kufunga, kutoa zaka na kuhiji, unaonyesha kuwa ni jambo la msingi kwa mja kuunganisha masharti ya kivitendo na kimwili katika matendo yake. Kwa mfano kuhusiana na swala tano Qur'an inasema, "Soma uliyofunuliwa katika Kitabu, na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda." (al-Ankabut, 45). Mtu ambaye hawezi kujizuia na maovu licha ya kuswali swala tano anakuwa hana usafi wa moyo katika matendo yake. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawachukia wale wanaoswali swala tano bila ya kuwa na ikhlas, "Basi, ole wao wanao sali, Ambao wanapuuza Sala zao" (al-Maun, 4-5). Pia na aya ifuatayo ya Qur'an inatoa habari kama hizo, "Hakika wamefanikiwa Waumini, Ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao" (al-Muminun, 1-2)

Kwa kuingia na kusafiri nje ya maana yake ya nje, Rumi anatoa tafsiri ya ndani kabisa ya aya iliyotajwa hapo juu na kusema, "Wanaendeleza hali zao wakati wa swala na hata baada ya swala. Swala za kila siku, ambazo hutuonesha njia iliyonyooka na kutuzuia na maovu, hufanywa mara tano kila siku. Lakini wale waliozama katika upendo wa kumpenda Mwenyezi Mungu, muda wote huwa katika swala, kwa sababu ya shauku ya upendo wa Mwenyezi Mungu unaowasha moto ndani ya nyoyo zao kiu yao haiwezi kutoshelezwa na kuswali mara tano; wala haiwezi kuondoka hata kwa kuswali mara laki tano." Kadhalika, Yunus Emre anazielezea swala za wale waliozinduka katika mghafala katika ubeti ufuatao:

*Imam wetu ni upendo, jamaah yetu ipo ndani ya moyo;  
Qiblah chetu ni Mpendwa wetu, swala ndio manukato yetu.*

Muda wa swala hudumu kwa takriban dakika kumi au kumi na tano. Lakini, mja anatarajiwa kuendelea kumakinika kwenye masuala yake ya kidini hata baada ya kumaliza kuswali, ili moyo wake usikumbwe na uasi wa fikra mbovu ambazo humvuta kidogo kidogo kwenye mghafala, utovu wa maadili na hata kuingia kwenye ukafiri. Kwa sababu hii, mja anatakiwa





kuushughulisha moyo wake na kumdhukuru Mwenyezi Mungu na daima kuwa katika hali ya kumkumbuka.

Kwa upande mwingine mtu asiyejali anakuwa hana moyo wenye sifa ya kujisalimisha na kumfikiria Mwenyezi Mungu Mtukufu hata wakati wa swala za faradhi, licha ya nje. Kisa kifuatacho kina maana kubwa kuhusiana na swala hili.

Daruwesh mmoja ambaye alikuwa katika harakati za kujikomaza kiroho alikuwa akiswali swala ya faradhi ndani ya msikiti usiku wa manane. Mara mvua ikaanza kunyesha na kutokana na matone ya maji yaliyokuwa yakidondoka kutoka darani, moyo wake ulianza kutamani kwenda nyumbani. Wakati ule sauti ya tahadhari kutoka ndani yake ikasema, “Swala yako hii haina ubora kwetu kwa sababu umeipeleka sehemu yako nzuri (moyo) nyumbani na hapa ukaacha mwili tu”. Hili linatukumbusha maneno ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake, “Kuna watu wengi wanaosimama usiku wa manane kuswali lakini wanachopata pekee ni kutolala usiku” (Ahmad ibn Hanbal, Musnad, II, 373). Hivyo yote haya yanaturudisha katika ukomavu wa kiroho na maadili.

Ukilinganisha na hili ni swala la kufunga, kufunga kunahusiana na nje na ndani ya mtu, mambo ambayo hayana budi kuzingatiwa wakati wa kufunga. Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anatahakikishia kuwa ufungaji wa namna hiyo utapelekea kufutiwa madhambi yote yaliyopita: “Yeyote atakayefunga ndani ya mwezi wa Ramadhani, kwa kutegemea malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, atasamehewa madhambi yake yaliyopita” (Bukhari, Sawm, 6). Kinyume chake njaa itakuwa ni mazoezi ya kukaa na njaa. Lengo la kufunga ni kufikia uchamungu; kuwa katika hali ya kumkumbuka Mola wakati wote (*taqwa*). Jambo hili linathibitishwa na Qur’an yenyewe: “Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamungu.” (al-Baqarah, 183).

Kutokana na mtazamo huu, funga si ya kutekelezwa kwa tumbo pekee, bali kwa viungo vyote vya mwili, na cha msingi zaidi ni moyo. Pindi tutakapofikiria juu ya umuhimu wa neema zilizotolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu, moyo unatarajiwa kufikia katika daraja la juu la imani kwa kupitia funga. Funga ni aina ya mafunzo ya kuweza kustawisha sifa za maadili kwa mtu, kama vile huruma na upendo. Kama mtu aliyefunga hataonyesha sifa hizo basi kufunga kwake kutakuwa ni kutekeleza wajibu. Kusengeny





na kulamba kisogo wakati umefunga ni mambo ambayo yanazuia kupata malipo ya funga yako au kupunguza fadhila zake. Mtume aliyebarikwa-rehema na amani ziwe juu yake- anathibitisha ukweli wa jambo hili kwa kusema, “Kuna wengi miongoni mwenu wanaofunga, lakini matokeo yake ni kushinda na njaa na kiu” (Ahmad ibn Hanbal, Musnad, II, 373 ). Hadithi hii ni kiashirio kingine cha umuhimu wa kufunga kimwili na kiroho.

Umuhimu wa kufanya matendo ya ibada kimwili na kiroho unaweza kuonekana pia katika utoaji wa zaka, kitendo chenye kudhihirisha na kuthibitisha namna muumini anavyowajali wengine. Pindi Mwenyezi Mungu Mtukufu anapoongelea sifa za muumini ndani ya Qur’an husema, “Anageuzwa kutokana na haki mwenye kugeuzwa.” (Adharyat, 9).

Kama muumini ni mwenye imani ya juu, pindi anapotoa zaka kutokana na mali yake hufanya hivyo kwa kufahamu kuwa anarudisha haki za wahitaji na si kana kwamba anawasaidia, na cha zaidi anawafurahia na kuwashukuru kwa kumpa fursa ya kutwahirisha mali zake. Pindi muumini atakaposhikamana na ufahamu huu ndipo atakapokuwa amepata maana halisi na ubora wa kutoa zaka. Ni jambo la uhakika kwamba mpokeaji anamsaidia mtoaji katika kupata nafasi ya kutekeleza kitendo cha ibada cha faradhi na pia kumlinda dhidi ya mikosi na matatizo mbalimbali, na pia kupata malipo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Pindi muumini aliyekomaa anapotoa sadaka yoyote huzingatia *hadith* isemayo, “Sadaka hufikia mkono wa Mwenyezi Mungu (wa uweza) kabla haijafikia mkono wa mhitaji” (Tabarani, Mujam al-Kabir, ix, 109)<sup>12</sup>. Ili kuweza kupata siri ya *hadith* hii, muumini hutoa huku akitambua na kufahamu kuwa kiukweli kila anachotoa huenda kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na huo ndio msingi wa kuthibitisha ubora wa kutoa zaka, jambo linalopatikana kwa kupitia ukomavu wa kimaadili na kiroho.

Wakati watu wema waliopita walipokuwa wanatoa sadaka, walikuwa wakiifunga vizuri na kuitoa kwa siri kwa kufahamu kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ataipokea kabla ya wahitaji. Huo ni baadhi ya udhihirisho na ubora wa maadili na wema unaotokana na uislamu. Katika kuonyesha ubora wa kutoa zaka, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasisitiza nukta hii hii ndani ya Qur’an kwa kusema, “...na (Yeye Mwenyezi Mungu) anazikubali sadaka...” (at-Tawbah, 104).

Kinyume na haya, kama mtu atatoa sadaka bila ya kutambua ubora







wake, atakuwa kana kwamba amejifutia malipo yake, kwani uislamu unakemea kufanya mambo kwa kujivuna. Wakati wote muislamu hana budi kuwa mfano wa kuigwa katika wema na umakini; hata hivyo sifa hizi zinategemeana na kiwango cha mtu cha maadili na imani.

Maadili ya hali ya juu na mwenendo wa kiroho unaweza kupatikana kwa urahisi wakati wa hija. Ukiangalia hija kwa juu unaweza kuona kuwa ni kitendo cha ibada kilichotawaliwa na matendo ya kimwili zaidi, kama vile kuvaa vazi maalum la hija (*ihram*), kuizunguka Al-Kaaba (*tawaf*), kusimama katika mlima Arafa, kuchinja, kwenda Muzdalifa, na kadhalika. Hata hivyo haya yote yanajumuisha vipengele vya nje vya hija. Lakini tukiingalia ibada hii kwa upande wa kiroho, na kushiriki, tutagundua kuwa hija inatukumbusha juu ya saa ya mwisho na siku ya kiama, ambapo kwa kupitia hija tunahitajika kuikumbuka siku ya hesabu na kutafakari na kuyahesabu masiku yaliyokwishapita katika maisha yetu.

Vivyo hivyo kumchinja mnyama kwa nia ya kutafuta ukaribu na Mola pia kuna masharti ya ndani na nje, kama ilivyo kwa matendo mengine yote ya ibada. Ingawa wakati kumchinja mnyama lazima ufuata utaratibu fulani, lakini cha msingi zaidi ni nia ya mchinjaji, nia ambayo mahala pake ni moyoni. Nia yako ndio itakayoonyesha ikiwa kuchinja kwako kutakubaliwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu au la. Maelekezo juu ya jambo hili yako wazi:

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَاءَ وُهَا وَ لَكِنَّ يَنَالُهُ التَّقْوَى مِنْكُمْ

“Nyama zao hazimfikii Mwenyezi Mungu wala damu zao, lakini unamfikia uchamngu wenu. Namna hivi tumewadhalilisha kwenu ili mumtukuze Mwenyezi Mungu kwa alivyo kuongoeni. Na wabashirie wafanyao mema.” (Al-Hajj, 37).

Kutokana na aya hapo juu tunaweza kusema kuwa kama mtu atachinja mnyama kutokana na vitisho katika jamii, yani wasiwasi juu ya upinzani dhidi ya uislamu, basi kitendo chake hicho hakitapata radhi za Mwenyezi Mungu. Mfano wa wazi juu ya jambo hili umetajwa katika Qur'an kuhusiana na watoto wawili wa nabii Adam- rehema na amani ziwe juu yake. Kabil alitoa kafara mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu bila ya kuwa na moyo safi, alifanya hivyo ili kutekeleza sheria pekee. Na bila shaka kafara yake ikakataliwa. Kwa upande mwingine ndugu yake Habil alitoa kafara





mbele ya Mwenyezi Mungu kwa moyo safi na kwa usahihi, matokeo yake kafara yake ikakubaliwa. Aya ya Qur'an inayolizungumzia suala hili inasema, "Na wasomee khabari za wana wawili wa Adam kwa kweli. Walipo toa mhanga, ukakubaliwa wa mmoja wao, na wa mwengine haukukubaliwa. Akasema: Nitakuuwa. Akasema mwengine: Mwenyezi Mungu huwapokelea wachamngu." (Al-Maida, 27).



Vitu vyote vilivyotajwa hapo juu vinaashiria kuwa kukubalika na usahihi wa matendo yote ya ibada vinategemea maadili, ukomavu wa kiroho na utambuzi wa mtendaji. Haya yanathibitisha ulazima wa elimu ya kiroho na umuhimu wa kuutakasa moyo.

Pia katika suala hili tunaweza kupata nukta nyingine muhimu. Ni kweli kwamba matendo yote ya ibada yanapaswa kutekelezwa kwa moyo safi na uchamungu, na kuwa mbali na kuingiliwa na aina yoyote ya majivuno. Lakini ni jambo la ajabu kwa muumini akaacha kutekeleza mambo ya faradhi kwa kuhofia kuwa hatayatekeleza katika viwango vinavyohitajika na hivyo kupelekea kutopata kitu. Mtu yeyote hatarajiwi kuacha jukumu lake la kutekeleza ibada; na anachotakiwa zaidi ni kujitahidi kukuza ubora wake kadiri iwezekanavyo kwa kurekebisha nafsi yake kwa kuongeza kiwango chake cha usafi wa moyo na uchamungu. Njia ya kuelekea kwenye mafanikio ya kiroho imejaa mitihani na hivyo inahitajika juhudi kubwa katika kupambana na matamano ya nafsi. Haiwezekani kufikia daraja la juu la uchamungu kwa haraka na kwa wepesi. Usafi wa moyo ni daraja la juu katika ukuaji wa kiroho na kuliendea daraja hili kunahitaji kwenda hatua kwa hatua. Na kama ilivyo muhimu kutumia juhudi binafsi katika njia hii, lakini ni muhimu zaidi kuomba msaada na uongofu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kutokana na ukweli kwamba ubora wa matendo ya mtu unategemea hali yake ya kimaadili na kiroho, mwenendo wa kisufi unatoa msaada muhimu wa kuuongoza moyo kwenye uelekeo sahihi na kutafakari juu ya uumbaji. Hivyo si jambo la kushangaza kuona kuwa watu wanaupinga mwenendo wa kisufi licha ya kanuni zake nzuri zilizowekwa juu ya uislamu. Maamuzi ya namna hiyo ni matokeo ya uwezo mdogo wa kutafakari.

Makosa, upotoshaji na maelezo yasiyo sahihi katika fikra zote za kielimu ni jambo lisilo la kuuliza. Fikra za kidini pia zimekumbwa na masuala





haya haya, ukiwemo usufi ambao ni kiini cha mafunzo ya kiroho katika uislamu. Dhehebu lolote linaweza kutofautisha haki na batili katika suala tunaloliongelea. Kwa maana hiyo, mtazamo wowote usio wa haki unaojaribu kuonyesha kuwa makosa na kasoro fulani ni za sufi pekee, itakuwa ni jambo la kushangaza. Watu husika kuwa na ustadi au kutokuwa nao ni jambo linaloweza kuonekana katika nyanja zote za elimu; na hakuna sababu ya msingi ya kuutenga usufi na kuushutumu kwa kutokuwa sahihi katika nyanja za fikra za dini ya kiislamu.

Kunaweza kuwa na watu wasio na ustadi na wakajiita kuwa ni Sufi na kufanya mambo chini ya nembo ya usufi ingawa kiukweli wakawa wanauchafua tu. Hakuna sababu ya kuwajumuisha watu hawa pamoja na sufi walio na ustadi ambao wanatekeleza mambo kulingana na mwenendo wa dini ya kiislamu. Hivyo kuukataa usufi kuwa ni nyanja ya kiislamu kutokana na msimamo huu ni jambo linalotia mashaka. Kuukataa mwenendo wa kisufi kutokana na baadhi ya upotoshaji ni sawa na kukataa fani nzima ya udaktari kutokana na baadhi ya makosa katika matibabu; ni kweli kwamba kunaweza kuwepo watu katika fani hii ambao watakuwa wanaitumia vibaya na kuichafua. Hivyo kinadharia na kivitendo si jambo jema kuukana usufi kwa madai kuwa hauna msingi katika mafunzo ya kiislamu.

Mwenendo wa kisufi hauwezi kueleweka kutokana na matendo ya watu wanaojiita sufi lakini wakawa hawana ustadi wa kutosha na ambao wana nia mbaya, na ambao wanadai kuwa ni wawakilishi halali wa mwenendo huu. Ukweli ni kwamba usufi unaweza kueleweka kutokana na wale wenye imani thabiti, kwani hata akili ya kawaida inaweza kutofautisha mwenendo sahihi wa kisufi na usio sahihi kwa kuangalia utofauti wa ubora wa matendo yao.

Na pia usufi hauwezi kueleweka kwa kuzingatia majumuisho ya kawaida, kwani ni jambo linalohusiana na moyo, ni kitu kilicho jengwa juu ya misingi ya huruma na upendo. Kuufafanua usufi kwa haki kwa wale wasio na upendo hata kidogo ni jitihada ya bure; ni sawa na kuzifanua rangi kwa mtu ambaye alizaliwa kipofu.

Kadiri mtu anavyojisogeza mbali na kutafakari kiroho ndivyo anavyokuwa muigaji dhaifu. Hatoweza kujielewa mwenyewe wala hatoweza kuzama kwenye vina vya roho yake. Atakachoweza kufanya ni kuwaiga wale waliomzunguka. Hatoweza hata kufurahia uzuri uliolala katika moyo wake, atakuwa mbali na kuweza kuwa mfano bora katika jamii yake. Ili





kuweza kuwa karibu na Mola na kumfikia kutawezekana kwa kuboresha maadili yako ambayo ndiyo yanayoweza kukana kila aina ya matamaniao ya dunia.

Katika kiini chake, usufi ni sayansi inayowahusu wanadamu. Pindi mwanadamu atakapojiweka mbali na masuala ya kidunia na kuzingatia moyo wake na nafsi yake, atajikuta yuko mbele ya milango ya kasri la hekima na ukweli. Sufi wa kweli ni wale wanaoielewa Qur'an na kuifanya kuwa ndio muongozo wao katika kuthibitisha imani yao ya kweli. Sufi ni mtu anayejihisi kuwajibika mbele ya Mwenyezi Mungu kutokana na ustawi wa jamii anayoishi.

Siku moja mtu mwema Najmaddin Kubra aliungana na wafuasi wake kwa ajili ya kuswalia maiti ya mtu mwema mmoja ambaye alikuwa amefariki muda si mrefu. Walipokuwa wanakaribia mwisho wa swala kwa kumkumbusha maiti maelezo yanayohitajika kaburini, Kubra alitabasamu. Wafuasi wake walishangazwa kutokana kumuona Kubra anatabasamu katika sehemu kama ile na hivyo wakashindwa kujizuia na kumuuliza sababu. Mara ya kwanza hakutaka kuwaambia sababu lakini waliposisitiza zaidi Kubra aliwaambia, “Moyo wa mtu anayemkumbusha maiti juu ya maelezo yanayohitajika ulikuwa umekufa na hauna mazingatio, wakati moyo wa maiti ulikuwa uko macho na wenye kuzingatia. Nilistaajabishwa kutokana na kuona kuwa Mtu asiye na mazingatio alikuwa anajaribu kumsaidia mtu mwenye kuzingatia mambo na ambaye moyo wake uko macho”.

Kwa namna hii, moyo wa wale wanaoupinga usufi kwa ajili ya kuthibitisha usahihi wa ufahamu wao wanashangaza kama ilivyo kwa moyo uliokufa ukijaribu kuufufua moyo ambao tayari uko hai. Tayari yameshakwisha kuthibitishwa mafanikio ya sufi katika karne nyingi kutokana na kuhuisha kwao maisha ya kidini, kuyahamisha kwenye vizazi vinavyofuatia, kuiongoza jamii kwa ujumla na kuusambaza ujumbe wa uislamu. Mwanachuoni mkumbwa wa kiislamu analithibitisha jambo hili na kukiri, “Nilikulia katika namna ya kutumia mantiki katika mambo yangu. Kutokana na kuji-funza kwangu sheria na chunguzi mbalimbali nilizozifanya vilinipelekea kukataa kila kitu ambacho hakikuelezewa na kuthibitishwa kwa namna yenye kuingia akilini. Bila shaka mpaka leo hii ninatekeleza wajibu wangu wa kidini kama vile kuswali swala tano na kufunga, si kutokana na ushawishi wa kisufi bali kutokana na wajibu wa kisheria. Huwa ninajiambia mwenyewe, “Mwenyezi Mungu ndie Mola wangu, mlinzi wangu. Ameniamrisha kuyafanya haya na hivyo ni lazima niyafanye. Kinyume na hayo





haki na wajibu vyote vinategemeana. Mwenyezi Mungu Mtukufu ameyapanga haya kwa ajili yangu ili ninufaike kwayo, inamaanisha nina wajibu wa kumshukuru”.

Lakini tokea nianze kuishi magharibi, Paris, nilishangazwa kuona kuwa maneno ya sufi kama vile Ibn Arabi na Rumi ndiyo yanayoongoza kwa kuwafanya wakiristo waupende uislamu; na si maoni ya wanashe-ria wa kiislamu au wanathiolojia. Nimeyashuhudia haya katika maeneo mengi. Nilipokuwa nikiulizwa swali lolote linalohusu mada fulani ya kiislamu jibu langu lilikuwa si lenye kushawishi pindi nilipokuwa naliegemeza kwenye uthibitisho wa kimantiki na kiakili. Lakini kwa kutoa ufafanuzi wa kisufi kulipelekea uthibitisho wake kukubaliwa wakati wote; ingawa baada ya muda nilipoteza ufanisi wangu juu ya hili. Haitoshi, niligundua kuwa huduma kubwa katika uislamu hasa katika Ulaya na Afrika ya leo vilitegemea si katika upanga au akili bali katika moyo, yani Usufi; kama ilivyokuwa katika kipindi cha Ghazan Khan kufuatia uharibifu mkubwa wa ardhi za waislamu mikononi mwa Hulagu.

Kutokana na kuligundua hili nikaanza kuchunguza baadhi ya kazi za usufi; na jambo hili likafungua macho ya moyo wangu. Niligundua kuwa mwenendo wa kisufi katika kipindi cha Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- na katika mifano ya kuigwa ya sufi wakubwa, haukuhusu maneno na taratibu fulani za wanachuoni, bali ulihusiana na kumuongoza mwanadamu katika njia bora ambayo itampeleka kwa Mola na kutafuta njia za kuboresha mwenendo wa mwanadamu. Mwanadamu hutafuta sababu za wajibu aliobebeshwa. Ufafanuzi wa kimantiki na kiakili kuhusiana na ulimwengu wa metafizikia hutuweka mbali na lengo. Ufafanuzi wa kimetafizikia na kiroho pekee ndio utakaoweza kuwatosheleza wanadamu<sup>13</sup>.

Kutokana na maneno haya tunaweza kuhitimisha kwa kusema kuwa hatua yoyote ya kuupinga usufi, ambao makubaliano yake na Qur'an na *Sunnah* si ya kuuliza, ni sawa na kuukata mti uliojaa matunda, jambo ambalo ni dhambi kubwa. Kuna maneno ya Rumi yasomekayo, “Ulilil-aumu waridi kama pua yako haiwezi kunusa”.

13. M. Aziz Lahhab, *Islam Sahsiyetciligi*, tafsiri ya I. Hakki Akin, uk. 114-115, tanbihi ya 8, Istanbul, 1972. Tanbihi hii ipo katika barua iliyoandikwa na Muhammad Hamidullah kwenda kwa mfasiri, tarehe 7 Septemba, 1967. (Imechu-kuiliwa kwa Mustafa Kara, *Metinlerle Gunumuz Tasavvuf Hareketleri*, uk. 542-543)





Kipengele kingine muhimu katika usufi ndani ya dunia hii tunayoishi kipo katika njia unazozitumia katika kurekebisha tabia na mwenendo wa kibinadamu, njia zinazoweza kumbadilisha mtu na kuwa mwanadamu bora. *Shariah* yetu tukufu inalenga kuwaongoza wanadamu kwa kuwafahamisha malipo na adhabu zinazowasubiri hapa duniani na kesho akhera. Kwa upande wa Usufi huba na upendo ndivyo vinavyotumika. Mwanadamu wa kawaida anakabiliwa na mfidhaiko wa kiroho wa kuwekwa mbali na dini na mzigo wenye kuumiza wa madhambi. Ni jambo lililopingika kuwa kuwaelekezea upendo, msamaha na huruma kutasaidi kwa kiasi kikubwa kuwasahihisha na kuwaokoa watu hawa. Kwa mtazamo huu dunia ya leo hii ina uhitaji mkubwa wa mwenendo wa kisufi, kinadharia na kivitendo, zaidi ya inavyohitaji ukweli wa kiroho. Kuwaelimisha na kuwaongoza watu chini ya kivuli cha huruma, uvumilivu na upendo bila shaka kutapelekea kwenye manufaa ya ulimwengu mzima. Kuziendea nyoyo hizi zilizo katika shida ya kutafakari na matamania katika namna ya kiislamu na kutumia uhamasishaji chanya na kuwaongoza katika uelekeo bora, kutapelekea manufaa zaidi kuliko kuwatisha kwa adhabu kadhaa.

Kwa kuwa usufi unachukulia kutokuwa na maadili na kuvuka mipaka kwa wanadamu kama athari za ukosefu wa upendo, hivyo njia zake zinazingatia misingi chanya ambayo ndiyo inayotumika kutoa ujumbe wa kiislamu. Kiasili, wanadamu wakati wote wanahitaji upendo; hivyo wanazipenda njia zilizotumiwa kwa karne nyingi na watu wema kama vile Abdulqadir Jilani, Yunus Emre, Bahauddin Naqshbandi and Rumi.

Kisa kifuatacho kina mguso mkubwa pale tunapotafakari namna mwanadamu alivyo na shauku na upendo juu ya watu wema waliotangulia. Muhammad Iqbal, ambaye alikuwa muislamu mwenye uwezo mkubwa wa kufikiri na alikuwa mpenzi wa Rumi, alikuwa katika ndege akielekea Uturuki. Pindi ndege ilipoingia kwenye anga ya Uturuki mtu huyu aliyekuwa na uwezo mkubwa wa kutafakari alisimama na kubakia vile kwa kitambo. Pindi watu waliomzunguka walipomuuliza sababu iliyompelekea kufanya vile, Iqbal alijibu kwa hisia kubwa, “Hizi ni ardhi zenye kaburi la Rumi na

wale watu wema waliojitwika mzigo wa jukumu la kuulinda uislamu dhidi ya maadui zake. Kama ingelikuwa si waturuki, uislamu ungelikuwa umerudi kwenye rasi ya uarabuni. Kutokana na heshima kubwa niliyonayo ndani ya moyo wangu juu ya mwanachuoni huyu mkubwa na watu wa hapa nilijihisi sina budi kusimama kwa heshima”.





Mfano uliopita unaonyesha namna ambavyo sufi wa kweli anaweza kupata msukumo wa jambo licha ya kupita karne nyingi. Karne nyingi baada ya kifo cha Rumi, ambaye alikuwa muwakilishi mkubwa wa mwenendo wa kisufi, mwenendo wake ulitokea kupendwa mno na Iqbal. Kutokana na ukweli kuwa mafundisho ya Rumi yalikuwa sababu ya kumsaidia Iqbal kuwa na mwenendo bora na kujipamba kwa upendo, huruma, umakini na elimu, kiasi cha kupelekea mwenendo wa kisufi uhitajike katika zama zetu. Usufi unaziunganisha nyoyo kutokea mashariki mpaka magharibi, na kuzikomaza na kuzitukuza ndani mchakato huo; na huu ni ukweli usiopingika katika miaka na karne zote.





***K**uwa sufi ni kujipamba na sayansi na uhalisia wa wazi na hivyo kuvuka mipaka ya moyo.*



## **E. UHUSIANO KATI YA USUFI NA FIKRA NYINGINE ZA KIELIMU**

Fikra za kielimu zimekuja kutokana na kupenda kuuliza alikozaliwa nako mwanadamu. Kila moja miongoni mwa fikra hizi inachunguza sheria na kanuni zinazohusu uhalisia katika eneo husika. Ndani ya uchunguzi wake kila fikra hufikia katika nukta ambazo zinaendana na usufi, ama kwa makusudi au bila ya kutarajia, hufikia usufi ambao wenyewe hugusia nukta hizo kwa mtazamo mpana; mtazamo ambao hutokana na hekima. Mwendano huu haupatikani katika sayansi za kidini pekee, bali pia katika sayansi zote, kinadharia na kivitendo, kuanzia kwenye sanaa mpaka kwenye falsafa. Kutokana na uhusiano huu sasa tutaangalia kwa ufupi uhusiano uliopo kati ya usufi na fikra nyingine za kielimu chini ya vipengele vitano.

### **1. USUFI NA FIKRA NYINGINE ZA KIISLAMU**

Lengo la dini ni kumfanya mwanadamu amtambue Muumba wake, kumfahamisha wajibu na majukumu aliyonayo mbele ya Mwenyezi Mungu na kumuongoza namna ya kuishi na watu katika jamii kulingana na matakwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kinachoendana na hili ni lengo la usufi; kumuongoza muumini kwenye uelekeo huu na kumpatia nguvu za kiroho na kimaadili ili kumsaidia kuyatekeleza haya malengo ya kidini. Pia usufi unatoa misingi ya kiroho na ufafanuzi juu ya mtazamo wa nje wa maamrishi ya kidini na humhamasisha kiroho muumini ili atekeleze majukumu yake kwa moyo safi na uchamungu. Hivyo kama ilivyotarajiwa, bila shaka mwenendo wa kisufi unaendana na matawi yote mengine ya elimu za kiislamu. Upembuzi juu ya uhusiano wa ndani kati ya usufi na fikra nyingine za kiislamu utatosha katika kuangaza zaidi juu ya ukweli huu.







### a. Usufi na Thiolojia

Masuala ya thiolojia ya kiislamu kimsingi yanahusu dhati, sifa na upweke wa Mwenyezi Mungu. Kwa kuwa kimsingi inahusiana na mada za kiitikadi, thiolojia inachukuliwa kuwa fikra ya kiislamu muhimu kuliko zote (*ashrafu'l-ulum*). Moja ya malengo ya msingi ya thiolojia ni kuweka misingi imara katika kukubali imani za kweli na kukataa zile za uongo. Kwa hivyo kazi muhimu ya thiolojia ya kiislamu ni kuzirudi zile hoja za kuupinga uislamu na kuwashawishi watu kuwa uislamu ndio dini sahihi na ya kweli kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lengo la usufi ni hili hili; unalenga katika kumfahamu Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenyezi Mungu ambaye ana sifa kamilifu na ambaye yuko mbali na aina zote za udhaifu, lakini kumfahamu huku ni ndani ya moyo.

Thiolojia inajaribu kutafuta suluhisho la matatizo ya kiitikadi kwa kuzin gatia Qur'an na *Sunnah* na kwa kutumia uwezo wa kibinadamu kimantiki. Kwa namna hii nafasi ya wanathiolojia inaweza kulinganishwa na ya wanafalsafa. Lakini kinyume na wanafalsafa, wanathiolojia hawatenyanishi akili ya kibinadamu na dini; badala yake wanaitumia akili katika kuihudumia dini. Hata hivyo kutokana na kuhama kwake kimantiki kutoka kwenye sababu mpaka kwenye athari, uwezo wa mwanadamu wa kimantiki hautoshi wenyewe kama wenyewe, katika kumpelekea mtu kufikia ukweli. Hii ni safari ya kielimu ambayo inahitaji kutumia vitu vingine, cha kwanza na cha mbele ni moyo.

Itakapofikia mahali ambapo akili haiwezi tena kuendelea ili kupata suluhisho, moyo huchukua nafasi yake na kuhakikisha mwanadamu anasonga mbele katika safari yake ya kupata suluhisho yeye mwenyewe. Katika usufi suluhu hizi hujidhihirisha ndani ya moyo katika hali ya msukumo wa kiroho; na huendelea bila ya kusema kuwa suluhu hizi ni lazima ziendane na Qur'an na *Sunnah*. Mwishoni mwa mchakato huu wa kiepistemolojia, usufi unakuwa umemuongoza mja mpaka kwenye mwisho wenye kuridhisha.

Kwa uhakika zaidi, pia wanathiolojia wa kiislamu wameonyesha umuhimu wa moyo kama chombo sahihi cha ufahamu. Kwa namna hii kama ambavyo tumekwisha sema kuwa wao wanatofautiana na wanafalsafa, wengi miongoni mwao wanatambua nyanja ya akili kama chombo cha ufahamu. Tukiangalia historia tutakuta kuna wanathiolojia wengi ambao kinadharia wanatambua usahihi wa ufafanuzi wa kiroho, bila ya kusahau





wengine wengi ambao wao binafsi walifuata mwenendo wa kisufi.

Hivyo akili ya mwanadamu, kutafakari kwake na maamuzi yake wakati wote vinatokana na hisia zinazotokana na ulimwengu wa kimwili. Hivyo hujaribu kutafuta ukweli kwa njia ya kubainisha usawa na utofauti wa mambo. Hivyo ni vigumu kuweza kupata uhalisia wa vitu vya kimetafizikia, vitu ambavyo si rahisi kufahamika na mwanadamu wa kawaida. Kwa hiyo utambuzi wa mwanadamu hauwezi kutosheleza mategemeo aliyozaliwa nayo mwanadamu ya kufikia kwenye uhalisia wa mambo. Ukilinganisha na uhalisia wa kimetafizikia, uhalisia ambao fikra za mwanadamu wa kawaida haziwezi kuufikia, mtu anaweza kuboresha kiwango chake cha ufahamu kwa kupitia ufunuo wa kiroho na udhihirisho utokao moyoni. Hapa ndipo inapokuja kazi ya usufi, kwani unatoa huduma muhimu mno kwa mwanadamu katika kumuwezesha kufikia uhalisia wa asili, jambo ambalo lisingewezekana kwa akili ya kawaida ya mwanadamu. Usufi huliwezesha jambo hili kwa kumpa mwanadamu nguvu kwa kupitia kumkumbuka Mwenyezi Mungu na hivyo kupelekea moyo uwe tayari kupokea ufunuo wa kiroho. Kwa kuyazingatia haya, kutokana na sifa za Mwenyezi Mungu za utendaji wake, Usufi haujaungana kwa ukaribu na thiolojia ya kiislamu pekee; bali huboresha ufafanuzi wa kithiolojia na hatimae kumridhisha mwanadamu, hasa katika masuala ya kimetafizikia ambayo akili ya kawaida ya mwanadamu haiwezi kutoa majibu.

Sufi huwaelekeza watu kulingana na akili zao na hutoa hoja za kithiolojia kwa ajili ya kuwatosheleza watu wenye uwezo mkubwa wa kufikiria. Huimarisha imani za watu juu ya kuwepo kwa Mwenyezi Mungu mmoja. Fakhruddin Razi, ambaye alikuwa mwanathiolojia wa kiislamu mkubwa na mshehereshaji, anafafanua uhusiano kati ya usufi na thiolojia ya kiislamu kwa kusema, “Ingawa njia za wanathiolojia hazitoshi kufikia kwenye uhalisia, lakini bado ni hatua muhimu za mwanzo za kuendewa kama kitangulizi cha usufi. Ukamilifu wa dini unaweza kupatikana kwa kupitia uhamisho kutoka kwenye sayansi zenye kufahamika na watu wote na kwenda kwenye sayansi za siri; na hizi zimeegemea kwenye ufahamu wa uhalisia wa ndani wa vitu”<sup>14</sup>.

14. Muhammad Salih al-Zarqan, *Fakhr al-Din al-Razi wa-ara'uhu al-kalamiyya wa-alfalsafiyya*, uk. 76 (Imechukuliwa kwa Muhammad Abid al-Jabiri, *Arab-Islam Kulturiinun AktiYapist*, uk. 626.)





### **b. Usufi na ufafanuzi wa Qur'an (Tafsir)**

Sayansi ya ufafanuzi wa Qur'an hutafuta maana za ufunuo wa Qur'an na kuusherehesha. Qur'an tukufu ni muongozo mtakatifu kwa wanadamu na maneno yake yamebeba maana pana. Kutokana na mtazamo huu, tafsir inafanya kazi kama famasia ya usufi. Usufi unalenga kuutakasa na kuusafisha moyo wa mwanadamu, lengo ambalo nyanja ya tafsir inasaidia kwa kutoa maelezo husika na dawa. Kimsingi Usufi unategemea Qur'an katika uchambuzi wake wa mada mbalimbali.

Kutokana na kutoa maelekezo katika kila kipengele cha maisha, Qur'an tukufu humpelekea mwanadamu kupata radhi za Mola. Humfahamisha mtu namna halisi ya kuongoza maisha yake huku akiwa na hisia za kuwajibuka mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutekeleza matendo ya ibada kwa moyo safi kadiri iwezekanavyo na kuishi katika maisha ya kiuchamungu, maisha ambayo yamezungukwa na kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Mambo haya ni ya msingi mno katika mwenendo wa kisufi.

Kama ambavyo tumeona, lengo la kwanza la usufi ni kumfikia Mola kwa kupitia moyo. Na dhana sahihi wa usufi ni kuitambua Qur'an tukufu kama mhimili wa mwanadamu, mhimili ambao aya zake zinawataka watu watafakari kiundani kama njia muhimu ya kumuongoza katika njia iliyo-nyooka. Kuisoma Qur'an ni sehemu muhimu katika maisha ya sufi; hili ni jambo la kwanza analotakiwa kulifanya katika masaa ya mwanzo wa asubuhi. Hata hivyo kuelewa ujumbe unaopatikana katika aya za Qur'an kunahitaji moyo safi.

Kwa kuwa mwenendo wa Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake- ulikuwa sawa na Qur'an, watu wema ambao walitakiwa kuwa na maadili mema walipigania kukiendea kila kipengele cha maisha yao kulingana na mwenendo alioonyesha Mtume- rehema na amani ziwe juu yake. Kutokana na kuifanyia kazi Qur'an katika kipengele cha maisha yao waliweza kuwa Qur'an iliyo hai.

Kwa kuwa Qur'an tukufu ndio chanzo chao cha baraka na ufunuo, sufi wametoa mchango mkubwa katika fasihi za *tafsir*, huku wakitoa huduma kubwa kwa ajili ya kuboresha fasihi kwa kuziangaza aya za Qur'an zenye visa. Washereheshaji wa Qur'an wa kisufi wamefanya kazi kubwa kwa umakini kwa ajili ya kuchimbua maana na hekima za ndani ya maneno ya Qur'an. Bila shaka jukumu lao lisichanganywe na kutaka kwao kuyafungia maneno matakatifu ndani ya mipaka ya uwezo wa kibinadamu; hii haiku-





wa nia yao, kwani sufi wasingelithubutu hata kidogo kudhoofisha maneno yenye thamani kubwa ya Qur'an. Cha zaidi ni kwamba sufi hawakubaliani na tafsiri zisizo na misingi yenye kueleweka. Kanuni za ujumla kwa ajili ya sherehe za kiroho kama zilivyowekwa na walimu wa kisufi ni kama ifuatavyo:

- 1) Maana ya ndani ya maneno ya Qur'an isigongane na ujumbe wa nje wa aya husika.
- 2) Maana iliyopendekezwa haina budi kuendana na yaliyomo katika Qur'an na *Sunnah*.
- 3) Maana na muktadha wa aya husika ya Qur'an lazima iwe inafaa kupelelelwa maana ya kiistiari iliyopendekezwa.

Katika baadhi ya mifano ya sherehe za Qur'an za kisufi tunaweza kutaja *Haqaiqu't-Tafsir* ya Abu Abdullah Rahman as-Sulami, *Lataifu'l-Isharat* ya Qushayri na *Ruhu'l-Bayan* ya Ismail Hakki wa Bursa. Katika kuongezea katika sherehe hizi kamili za Qur'an tukufu, kuna nyingine nyingi ambazo zimebeba maana za kiistilahi katika aya maalum za Qur'an, kama vile kazi za Ibn Arabi na Rumi. Bila shaka ni kweli kwamba Qur'an ni maneno ya Mwenyezi Mungu yasiyoigizika, maneno ambayo yamekuja moja kwa moja kutokana na sifa yake ya kuongea (*kalam*). Kwa hiyo, kadiri atakavyokuwa mahiri mshereheshaji, katika hukumu ya mwisho maneno yake yatabakia kuwa sherehe; mazingatio na maneno ya mwanadamu ambayo hayawezi kulingana na ulimwengu wa Qur'an.

Kama wanadamu hatuwezi kuelewa kwa ukamilifu uhalisia wa dhati na sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo katika kuielewa Qur'an. Kutokana na kuwa zao la sifa ya kipekee ya Mwenyezi Mungu ya kuongea, Qur'an haiwezi kumakinishwa na akili ya yeyote na haiwezi kugeuzwa na ulimi wa yeyote, hata kama atakuwa na vipawa vya namna gani. Uelewa wetu wa Qur'an tukufu ni sawa na kuchukua tone kutoka kwenye bahari pana; na hili limegusiwa na Qur'an yenyewe:

“Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, maneno ya Mwenyezi Mungu yasingeli kwisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (Luqman, 27).

Tunaweza kusema kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hutumia mwenzo wa hali ya juu kwa wanadamu zaidi ya uwezo wao wa kawaida ili





yawapelekee kutafakari juu ya maneno ya Mwenyezi Mungu yasiyochuja wala kupitwa na wakati na kuyakubali kulingana na kiwango chao cha uelewa. Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake- anauelezea upekee huu wa muundo wa Qur'an kwa kusema, "Hakuna mwisho katika maana za Qur'an" (Tirmidhu Fadailu'l-Quran, 14 ). Rumi naye anasema, "Inawezekana kuyatafsiri maneno ya Qur'an kwa kiasi kidogo cha wino; lakini tutakapotaka kuzielezea siri zote zilizomo ndani yake tutahitaji kiasi kikubwa mno cha wino kiasi kwamba hata kama kingefikia bahari kis-ingelitosha; na pia hata kama miti yote duniani ingelitumika kama kalamu isingelitosha".

Maneno ya Qur'an na ya Mtume yaliyotajwa hapo juu yanaashiria kwamba Qur'an imebeba uhalisia na ukweli katika umbile la nyuklia. Kama undani huu wa Qur'an ungelitajwa wazi basi kiwango chake kingelivuka mipaka yote. Kwa sababu hii Qur'an hutaja baadhi ya mambo kwa uwazi na mengine kwa mafumbo. Wale tu walio na elimu ya kutosha ndio watakaoweza kufumbua siri hizi; hawa ni wale ambao wana utambuzi wa ndani katika kuelewa uhalisia uliofichikana ndani ya tungo za Qur'an na ambao wanatekeleza maamrisha yake kwa umakini na moyo safi.

Katika kutaja vigezo vya kielimu vinavyohitajika ili kuitafsiri Qur'an, wanachuoni katika fani ya *tafsir* wameweka tawi linaloitwa 'ufahamu kutoka kwa Mungu (*wahyi*)', utaalumu ambao wamepewa waja maalum wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Taaluma ya namna hii hupatikana kwa njia ya kujipamba na uchamungu, staha na uvumilivu, na kuendeleza mapambano dhidi ya nafsi bila kuchoka. Jambo hili limeashiriwa katika *hadith* inayosema, "Yeyote atakayekifanyia kazi kile anachokifahamu basi Mwenyezi Mungu Mtukufu atamfundisha kile asichokifahamu" (Abu Nuaym, Hilya, x, 15). Hii inamaanisha kwa uwazi kuwa mtu hawezi kupata sehemu ya siri za Qur'an kama hajajitahidi kujisafisha kutokana na tabia mbaya kama vile kujivuna, wivu, kuipenda dunia na kadhhalika. Kwani Qur'an inasema, "Nitawatenga na Ishara zangu wale wanao fanya kiburi katika nchi bila ya haki. Na wao wakiona kila Ishara hawaiamini. Wakiiona njia ya uwongofu hawaiishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu wamezikanusha Ishara zetu, na wameghafilika nazo." (al-Araf, 146).





**c. Usufi na maneno na matendo ya Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake - (*Hadith-Siyar*)**

Sayansi ya *hadith* huzingatia maneno, matendo, uthibitisho katika mambo mbalimbali, sifa za kimwili na kimaadili kutoka kwa Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake. Kama ambavyo inakubalika katika fani zote nyingine za taaluma ya kiislamu, *hadith* inachukua nafasi ya pili kama chanzo muhimu cha taaluma kwa Sufi baada ya Qur'an. *Hadith* kwa ujumla wake zimebeba matukio sahihi katika kila kipengele cha maisha ya Mtume- rehema na amani ziwe juu yake, yakiwa ni ya kimwili, kimaadili au kiroho. Kutokana na mtazamo huu si jambo la kushangaza kufikia kwenye hitimisho kuwa *hadith* zinachukua nafasi kubwa katika kuanzishwa na kuendelezwa kwa usufi. *Hadith* ambazo zinaashiria sifa njema kama vile kujizuia (*zuhd*), maadili mema (*wara*), kuiingiza imani moyoni (*ihsan*), staha (*tawaddu*), kuwajali wengine (*ithar*), subira (*sabr*), kushukuru (*shukr*) na kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu (*tawakkul*) zimebeba misingi mizito ya nadharia na vitendo. Hizi zote zinaendana kwa karibu na usufi kutokana na kuonyesha kwake maneno na matendo ya Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake. Haya yanadhiri-hisha namna ilivyo vigumu kutenganisha kati ya usufi na sayansi ya *hadith*.

Kama ambavyo ilitajwa wakati wa mjadala juu ya uhusiano kati ya usufi na tafsiri ya Qur'an, lengo la kwanza la usufi ni kutafuta ukaribu na Mola na mwishowe kumfikia Yeye. Wanafahamu kuwa safari ya upendo mtakatifu haiwezi kufanikiwa ila kwa kufuata nyayo za Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake. Kwa hiyo sufi humfuata Mtume aliyebarikwa- rehema na amani ziwe juu yake - katika mambo yote na hufurahia kutumia kumbukumbu za *hadith* ambazo ndizo zinazotoa muongozo katika maneno na matendo yake ya mfano.

Kumfuata Mtume aliyebarikwa - rehema na amani ziwe juu yake – ni kuhisi upendo wa hali ya juu kwake na kumuweka mbele katika kila kitu. Kuna aya nyingi ndani ya Qur'an ambazo zinagusia wajibu wa kumpenda na kumtii Mtume - rehema na amani ziwe juu yake. Mifano madhubuti inayohusu wajibu wa mtu kumpenda na kumtii Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – inaweza kupatikana katika vyanzo vya *hadith* na wasifu wa Mitume. Si tu kutekeleza matendo ya ibada na kuishi na watu vizuri bali pia kunahusiana na kuwa na tabia njema, Mtume aliyebarikwa - rehema na amani ziwe juu yake – ndiye mwanadamu aliyekuwa na maadili mema kuliko wote katika umma huu. Katika kufafanua na kuthibitisha mwenen-





do huu wa Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – juhudi za *hadith* na wasifu wa Mitume ni vitu visivyokwepeka.

Kumbukumbu ya maneno ya Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – yaliyohifadhiwa kwa umakini mkubwa yapo mpaka leo kwa msaa-da wa masimulizi sahihi ya vizazi vya waislamu. Zaidi ya haya maneno matukufu pia matendo na tabia za Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – zilisimuliwa na maswahaba zake kwa upana zaidi, na kupitishwa kwenye vizazi vilivyofuatia mpaka leo hii. Ubora ulioshuhudiwa kwa sufi wakubwa wa mwanzo ulikuwa unaendana na mwenendo mwema wa Mtume aliyebarikiwa - rehema na amani ziwe juu yake; mwenendo ambao kila muislamu hana budi kujipamba nao kadiri ya uwezo wake, kwani Mtume aliyebarikiwa - rehema na amani ziwe juu yake- alitumwa kuja kuwa mfano bora wa kuigwa na wanadamu wote. Wale ambao wataweza kujipamba na mwenendo wake watakuwa ni watu wa kipekee kutokana na kuyaelewa kwao maelekezo ya Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – na kuyafanyia kazi kwa umakini mkubwa katika maisha yao yote. Ukweli kwamba sufi wanajitahidi kuwaongoza watu katika uelekeo huu wa Mtume kutokana na mafundisho yao ya kinadharia na kivitendo unatosha kuthibitisha kuwa wao wakati wote wanafanya mambo kulingana na *Sunnah*.

Mwenendo bora wa sufi ni taswira ya mwenendo na tabia za Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kama zilivyowafikia katika kumbukumbu za *hadith*. Ukizingatia haya utaona kwamba matendo na mwenendo wa sufi wa kuigwa ni udhihirisho wa maneno na mwenendo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba kutokana na kujipamba kwao na mafundisho yaliyopo katika *hadith*, sufi wanakuwa ni wenye kueneza mafundisho ya Mtume katika nyakati na sehemu mbalimbali.

Hata kabla ya usufi kujitokeza kama fikra ya kielimu sufi na wanachuoni wa *hadith* walikusanya vitabu vilivyopewa jina la *kitabuz-Zuhd* (Kitabu cha kujizuia), kitabu ambacho ni kama daraja lenye kuunganisha usufi na sayansi ya *hadith*.

Kwa upande mwingine wachaji mungu wa kiislamu waliikuza fani ya *hadith* kwa kuweka ufafanuzi wa *hadith* mbalimbali kulingana na maana za kiroho. Na ingawa wanachuoni kwa ujumla wanakataa uwezekano wa ufafanuzi wa namna hii lakini baadhi ya sufi wanatoa hoja kwamba iliwezekana kwa mtu kupokea *hadith* kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa





– rehema na amani ziwe juu yake – kutokana na msukumo na amri yake ya kiroho. Kutokana na mtazamo huu hayo yote yanaweza kutokea kwa kupitia ufunuo wa kiroho.

Katika historia ya elimu ya kiislamu tunawakuta wanachuoni wengi wa kisufi kama vile Hakim Tirmidhi na Kalabadhi, watu ambao walitoa kazi zao katika fani ya *hadith* na usufi. Pia kuna wapokezi wengi wa *hadith* ambao walikusanya kazi zao kulingana na dhana ya usufi. Kwa mfano Imam mkubwa kama Bukhari – rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye alikusanya *hadith* nyingi na ambaye kazi zake zinachukuliwa kama maandiko muhimu ya kiislamu baada ya Qur’an tukufu, alikuwa na kawaida ya kuiandika kila *hadith* aliyokuwa ameiweka kichwani. Kabla ya kuiandika *hadith* hiyo alikuwa akiswali raka mbili kwa ajili ya kumuomba Mola ampe ilham juu ya usahihi wa *hadith* ambaye anataka kuiandika. Ni baada ya dua nzito na ufunuo wa kiroho ndipo alipokuwa akiingiza kwenye kazi zake *hadith* aliyokuwa ameipata<sup>15</sup>. Pia inasemekana kwamba Ahmad Ibn Hambal ambaye ni mwanachuoni mwingine mkubwa wa *hadith* alichukua *hadith* tatu moja kwa moja kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akiwa ndani ya ndoto.<sup>16</sup>

#### d. Usufi na sheria ya kiislamu (*fiqh*)

Kwa kawaida neno *fiqh* linamaanisha kufahamu, kuelewa na kutambua. Katika nyakati za mwanzo za uislamu neno *fiqh* lilikuwa likijumuisha aina zote za elimu, za kidunia na kiroho, na mtu ambaye alikuwa amebobea katika elimu alikuwa akiitwa *faqih*, wakimaanisha *alim* au mwanachuoni. Kwa maana hii *faqih* alikuwa ni mtu aliyekuwa na utambuzi juu ya hekima mbalimbali zinazomhusu kiumbe na vitu vingine, pia aliyekuwa na uwezo wa kutambua na kufahamu haki na wajibu wake katika dini. Kwa namna hii Imam Abu Hanifa anaitafsiri *fiqh* kama “...ufahamu wa mtu juu ya vitu vinavyomnufaisha na kumduru kwa kuzingatia misingi ya dini”.

Lengo la elimu hii ilikuwa ni ‘kumfahamu Mola’ ufahamu ulio muhimu kwa ajili ya furaha ya mwanadamu. Hivyo baadae kazi za Abu Hanifa juu ya mada za itikadi zilikusanywa na wanafunzi wake chini ya kichwa cha habari “*al-Fiqhu’l-Akbar*”, au *fiqh* kubwa kuliko zote. Katika

15. Angalia Ibn Hajar, *Hady al-Sari Muqaddima Fathul-Bari*, uk. 489; Ibn Hajar, *Taghliq al-Taliq*, Toleo la 421.

16. Angalia *Majmu al-Hadith*, manuscript 110a-112b.







siku za mwanzo za uislamu neno *fiqh* lilikuwa linamaanisha hivyo. Kadiri siku zilivyokuwa zinaenda wakati elimu ya kiislamu ilipokuwa ikipanuka, neno *fiqh* lilipata maana yake ya kiistilahi na wanachuoni wa kifiqh wakaanza kuweka pembeni mijadala ya kiitikadi na kimaadili kutoka katika *fiqh* na kubakiza matumizi yake katika masuala ya kivitendo na kisheria. Na leo hii maana hii ndio inayotumika katika kutafsiri *fiqh*.

Usufi huhusisha elimu ya vitu vinavyowanufaisha na kuwadhuru wanadamu. Kwa kuongezea katika uhusiano wake na nyanja ya epistemolojia katika *fiqh*, elimu ya kisufi inahusiana na masuala ya kidini ya ndani na nje. *Fiqh* inatufahamisha juu ya mahitaji ya nje na ndani katika mada za dini za kivitendo kama vile udhu, swala za faradhi, kufunga na kadhalika. Kwa upande wa usufi, unatoa elimu kwa kuzingatia mahitaji ya ndani; yani kuusafisha na kuutakasa moyo ili kumuandaa mtu kuweza kuishika elimu na ufunuo unaohusiana na utekelezaji wa matendo haya. Hivyo mwenendo wa kisufi unafanya kazi kama mahala pakuzingatia usafi wa moyo wakati wa kuyatekeleza matendo haya. Kutokana na hili pia usufi umeitwa “*fiqh* ya ndani” (*al-fiqh al-batin*) au “*fiqh* ya utambuzi” (*al-fiqh al-wijdani*), haya ni kutokana na kubeba kwake misingi ya kiroho na kiini cha *fiqh*.

Hakuna shaka kwamba lengo kuu la sayansi ya *fiqh* ni kuhakikisha kuwa matendo yote ya ibada yanatekelezwa katika ubora fulani ambao utapelekea yakubalike mbele ya Mwenyezi Mungu. Ubora huu utaweza kupatikana kwa kutokana ukomavu ya kiroho unaopiganiwa katika usufi. Kwa msingi huu *fiqh* na usufi ni vitu vinavyotegemeana; kwani malengo makuu ya usufi ni kumfanya muumini afikie katika uhalisia wa kimetafizikia na kiroho kwa kupitia matendo na tabia za nje ambazo *fiqh* imezielezea kuwa ni wajibu. Kuyaweka katika matendo masharti ya *fiqh* hakuwezi kuzaa matunda yanayotarajiwa bila ya kufikia kwenye ukomavu wa kiroho na kimaadili ulioelekezwa na usufi.

Kwa mfano katika swala za kila siku sayansi ya *fiqh* inaelezea masharti yake ya nje kama vile twahara na kuswali kwa kufuata utaratibu unaokubalika. Cha zaidi ni kwamba *fiqh* inaonyesha ulazima wa nia ambayo yenyewe ni sharti la ndani. Lakini wakati inafanya hayo haijishughulishi mno na kutoa ufafanuzi juu ya masharti ya kiroho ya swala kama vile kuutakasa moyo dhidi ya kujiona na wivu, hata kama haya yatakuwa muhimu katika ukamilifu wa swala na masharti yake ya nje. Usufi hupangilia masharti ya ndani ya swala na kujaribu kuyaunganisha na masharti ya nje. Kwa kuwa *fiqh* ni tawi la Shariah na ni muhimu kwa waumini wote kuifuata, kimsingi





hudhibiti vipengele vya nje vya dini, vipengele ambavyo ni wajibu kwa wanadamu. Vyovyote iwayo usafi wa moyo wakati wa kutekeleza wajibu huu ndio utakaopelekea kukubalika kwake mbele ya Mola.

Wanachuoni wa *fiqh* wametoa hukumu za kidini ambazo zinadhibiti matendo yote ya ibada na mahusiano ya kijamii kama vile ndoa, talaka, biashara na adhabu. Wao huzifanyia uchunguzi na kuzipangilia hukumu hizi. Na sufi nao hutoa nafasi ya kimaadili na kiroho juu ya hukumu hizi na husisitiza juu ya umuhimu wa hali ya kiroho anayotakiwa kuwa nayo mtu wakati wa kuzitekeleza. Na si chochote kingine tofauti na Qur'an tukufu kinachowasukuma sufi katika suala hili; kwani Qur'an ndio na kwanza na ya mbele katika kutoa msisitizo juu ya vipengele vya kiroho vya matendo ya ibada.

Bila shaka yote haya hayamaanishi kuwa sufi hawaipi umuhimu sayansi ya *fiqh*; wala haimaanishi kuwa wao hawapendi kujishughulisha katika masomo ya hukumu za kiislamu. Kinyume chake watu wakubwa katika usufi pia walikuwa ni wanachuoni wakubwa katika fani za masomo ya kivitendo likiwemo hili la *fiqh*. Kwa mfano katika suala hili tunaweza kutaja majina ya Ghazzali, Ibn Arabi, Rumi, Imam Rabbani, and Khalid Baghdadi.

Wale wanaoshindwa kutambua ukweli uliomo katika hukumu za kidini na uhalisia wa kiroho wanadai kuwa kuna tofauti kubwa kati ya sayansi ya *fiqh* na usufi. Ukweli ni kwamba kuna mifano dhahiri juu ya suala hili katika historia ya dini. Tukizingatia uhusiano kati ya wanachuoni wa kweli wa *fiqh* na sufi wakubwa tutaona kuna mambo mengi yanayot-hibitisha uhusiano wake. Huwa kunatokea kutofautiana na mabishano kati ya wajinga ambao wanajiona kuwa wana elimu kubwa katika *fiqh* na wale sufi wasio waaminifu ambao wanajichukulia kuwa wako katika ukamilifu wa kiimani.





**T**utawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali  
na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie  
kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba  
Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?"  
(Fussilat, 53).



## 2. USUFI NA SAYANSI ASILIA

Sayansi asilia ambayo mafunzo yake ya msingi yanashikilia kuwa utambuzi wa milango ya fahamu ndio unaokubalika katika kumpatia mwanadamu elimu na taarifa zake za kisayansi zinazalishwa katika maz-ingira ya maabara, kwa juu inawezekana kuonekana kuwa haihusiani na usufi. Lakini uhalisia wa mambo si hivyo.

Shughuli yoyote ya kisayansi ambayo inalenga katika kuelewa hekima na uhalisia wa viumbe na uwepo wa asili hufikia mahali ambapo ndipo metafizikia inapoanzia; na hapa ndipo ambapo sayansi asilia na usufi vinakutana. Usufi huzama na kuvumbua siri na hekima za viumbe vyote na ulimwengu wa kimetafizikia kwa ujumla. Huwaongoza wanadamu katika kufikia daraja la kumfahamu Mwenyezi Mungu na ulimwengu kwa namna yenye kushawishi, kuaminika na bora zaidi. Kwa kifupi usufi humpeleka mtu kwenye ulimwengu wa uhalisia.

Sayansi asilia huzingatia ulimwengu wa kimwili na unaoonekana. Vitu vilivyogunduliwa kwa kupitia elimu ya sayansi asilia huwa ni ubora ulio-wekwa katika vitu hivyo na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Haya yanamaani-sha kuwa kila kinachogunduliwa katika ulimwengu huu wa kimwili huja kama ushahidi juu ya nguvu na utukufu wa Muumba. Kutokana na nukta hii tunaweza kusema kuwa sayansi asilia hutusaidia kutambua vyema miu-jiza ya uumbaji wake.

Kwa upande mwingine uislamu huchunguza mambo pamoja na vipengele vyake vya kiroho na kimetafizikia. Sayansi asilia ya leo imet-hibitisha ukweli huu. Kila uvumbuzi katika dunia hii hufungua mlango wa kimetafizikia kuelekea kwenye mambo mapya yasiyofahamika na hui-pelekea akili ya mwanadamu kufikia kwenye ulimwengu usio na mwisho. Mwanadamu huanza kwa milango yake ya fahamu na mwishoni hupeleka kwenye uhalisia wa ndani wa kimetafizikia. Haya hasa yanahusika katika





zama zetu; sayansi imeleta maendeleo ya hali ya juu kiasi cha kukutana uso kwa uso na metafizikia. Kwa sababu hii nadharia za wayakinifu wa zamani ambao walijaribu kuficha uhalisia kwa sasa zimepoteza nafasi yake. Kwa mfano nadharia ya Lavoisier juu ya uhifadhi wa molekuli/maada, ambayo ilichukuliwa kuwa mwiko katika karne iliyopita, kwa sasa imepoteza mashiko kwa wanachuoni wengi. Vile vile 'kanuni ya umilele wa maada' ambayo ilikuwa miongoni mwa mambo yaliyokuwa yakileta uhasama kati ya wanafalsafa na dini, haikuweza kupata tena watu walioiunga mkono. Kwa sasa hata sayansi inapendekeza nadharia kuwa maada si kitu cha muhimu bali ni kitu cha bahati mbaya. Na suala kwamba maada ni nishati kandamizo limetokana na kuvunjwa kwa atomi na kupata chembe chembe ndogo, na imefahamika kuwa tunachokiita 'maada' kiuhalisia ni nishati ambayo imewekwa katika namna fulani. Kwa kuongezea ni kwamba gunduzi nyingi za kisayansi hasa katika nyanja za fizikia, kemia, baiolojia na falaki, zinathibitisha mambo mbalimbali yahasuyo asili ya vitu, mambo ambayo tayari yamekwisha tajwa katika maandiko ya dini, ya kwanza na ya mbele yakiwa ni Qur'an tukufu.

Ugunduzi mpya katika jeni za mwanadamu unaashiria kuwa kila mwanadamu ana aina fulani ya mfumo wa kipekee; huu ni mfano mmoja miongoni mwa mingine mingi yenye kuthibitisha asili ya uumbaji mtakatifu. Katika kutoa shukurani juu ya hili msomi na mshairi wa dola wa uthmainiyya wa karne ya 19 aliyetwa Ziya Pasha alisema:

*Ninamtukuza Yeye ambaye ustadi wake huvifanya vichwa viwe sikivu,  
Na ambaye utukufu wake humfanya mwenye hekima kuwa dhalili...*

Tokea mwanzo wa uislamu waislamu walikuwa wakifundishwa na walikuwa wakifahamu udhaifu wa ndani wa uwezo wa mwanadamu ukilinganisha na maajabu ya ustadi mtakatifu. Na pia uwezekano kuwa mwishoni mwa dunia gunduzi hizo za kisayansi zitaweza kukaribia daraja la miujiza si siri kwao. Kwani kila ugunduzi mpya wa kiislamu unamsukuma mwanadamu kutambua uwezo wake mbele ya ustadi mtakatifu wa Mwenyezi Mungu ambaye hekima yake ya hali ya juu ndiyo inayompelekea kuafahamu mambo. Udhaifu huu ndio ambao Ziya Pasha analeta mbele pale anaposema:

*Akili ndogo haziwezi kuelewa hekima hizi takatifu;  
Kwani mizani yake haiwezi kupima uzito mkubwa kiasi hiki.*





Usufi hutafakari juu ya viumbe vyote ili kutambua siri za kimetafizikia zilizojificha katika uwezo wao; Upeo wa sayansi asilia huweza kujibu maswali yao. Muunganiko huu unapelekea kuonyesha uhusiano chanya usiopingika kati ya usufi na sayansi asilia.

Ukweli ni kwamba Qur'an tukufu inatutaka tutafakari juu ya siri nyingi na hekima katika uumbaji. Kwa mfano aya ya Qur'an ifuatayo inaligusia suala hili kwa kusema:

سُنُّرِبِهِمْ آيَاتِنَا فِي الْأَفَاقِ وَ فِي أَنفُسِهِمْ حَتَّىٰ يَتَبَيَّنَ لَهُمْ  
أَنَّهُ الْحَقُّ أَوَلَمْ يَكْفِ بِرَبِّكَ أَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ

“Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao wenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?” (Fussilat, 53).

Neno “upeo” katika aya hii linaashiria ulimwengu huu ambao anaishi mwanadamu. Na maneno “miongoni mwao wenyewe”, yanaashiria hekima, mafunzo na siri zilizomo kwenye vipengele vya kibaiolojia na kiroho ndani ya mwanadamu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Qur'an yake tukufu anagusia umuhimu wa kuuchunguza ulimwengu huu na hivyo kutafakari juu ya dalili zake zilizopo kwenye viumbe vyake. Katika suala hili tunaweza kutaja baadhi ya aya zifuatazo:

“Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.” (al-Hajj, 46).

“Na hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo. Hatukuviumba hivyo ila kwa Haki, lakini wengi wao hawajui.” (ad-Dukhan, 38-39).

Na tukizingatia uumbaji wa mwanadamu, Qur'an tukufu inagusia kwamba kama ilivyo kwa viumbe wengine uumbaji wa mwanadamu umejikita katika malengo maalum na utafikia kikomo kama ilivyotajwa katika tamko lifuatalo:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا وَأَنَّكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ





“Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?” (al-Muminun, 115).

Tokea kwenye hatua ya chini mpaka ya juu katika uumbaji kuna udhihirisho wa wazi juu ya ustadi mtakatifu katika kila chembe. Usufi unalenga kuwafahamisha watu juu uhalisia wote huu, uhalisia ambao mwanadamu ndiye kitovu chake. Katika kuongezea kwenye kipengele hiki cha kinadharia, pia usufi unalenga katika kumkomaza muumini kidini na kiroho kwa kupitia mafunzo kadhaa kama vile kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu na tafakuri nyingine za kiroho. Hivyo usufi umebeba maelekezo ya kinadharia na kivitendo.

Katika maandiko ya Qur’an kuna aya ambazo zinaita katika kuzingatia hekima zilizopo kwenye ulimwengu wa kimwili na kila wakati Qur’an inauliza maswali ili kuonyesha msisitizo. Ingawa msisitizo huu unaweza kuonekana unahusiana na hali ya kimwili juu ya maswali hayo, lakini hayahusiani na hayo pekee. Kwa sababu hiyo katika maswali yetu ili tufahamu hekima juu ya vitu vinavyoonekana tunahitaji methodolojia ya hali ya juu zaidi ya yanayopatikana katika sayansi asilia. Ukweli huu unadhihirisha hitajio la mtu juu ya kuboresha hali yake ya kiroho katika moyo wake ili kuweza kupokea hali hii ya kiroho. Katika kutoa uwezekano huo kwa wanadamu, hapo ndipo usufi unapochukua nafasi yake. Kama ilivyogusiwa hapo kabla, kanuni maarufu ya kisufi inauchukulia ulimwengu huu kama udhihirisho wa majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo kila kiumbe katika dunia hii ni muujiza wa ustadi. Tunaweza kuendelea na kujaribu kuandika vitabu vingi ili kuelezea asili na uhalisia wa mambo yanayoonekana ni ya kawaida katika maisha ya kila siku; lakini bado tutashindwa kutoa picha kamili. Kwa mfano pindi swala anapokula jani la forosadi ili kuzalisha maski, na nondo wa hariri naye hula jani hilo hilo ili kuzalisha hariri. Ulimwengu unaotuzunguka unaingia kwenye miujiza na dalili za Mwenyezi Mungu Mtukufu; vyote vikiwa kwenye upeo wetu ingawa sisi hatutengi muda wa kutosha ili kuweza kutafakari vizuri mambo hayo. Pindi mtu atakapotazama kwa lengo la kupata funzo katika majani yenye ukijani, maua yaliyochanua na mti wenye kutoa matunda, na pia atakapotafakari juu ya namna ambavyo mimea hii inapata rangi, harufu na ladha yake kutoka kwenye ardhi, basi mtu huyo hawezi kukosa kustaajabu juu ya utukufu na nguvu ya ustadi mtakatifu. Usufi unawahamasisha watu kuutazama uumbaji mzima kwa macho yao ili kupata mazingatio. Matokeo yake sufi wanaamini kuwa hakuna kilichoumbwa hapa dunia bila sababu,





bila malengo, hukumu wanayoithibitisha kwa kuzipeleka nyoyo zao kwenye malengo hayo hayo.

Kama ilivyo kwa Qur'an tukufu na mwanadamu, ulimwengu ume-kuja ili kudhihirisha majina matukufu ya Mwenyezi Mungu. Mtu anaweza kusema kuwa sayansi zote asilia zinalenga katika kudhihirisha hekima ya Mwenyezi Mungu na kanuni zinazouongoza ulimwengu mzima, mambo ambayo kimsingi ni udhihirisho wa majina matukufu ya Mwenyezi Mungu, kama ambavyo imekwishaelezewa. Cha kushangaza ni kwamba sayansi zote asilia na wanasayansi wengi wameshindwa kutambua na kutafakari juu ya mambo haya; kama ambavyo wale waliokomaa kiroho na kimaadili wangeliveza kupata siri na hekima za uumbaji nyoyoni mwao, jambo ambalo kiufahamu linazidi upeo wa sayansi asilia. Usufi umeweza kuvuka mipaka hii ambayo sayansi asilia imeshindwa kuvuka na hapa ndipo vitu hivi viwili vinaposhikamana.





*U*sufi ndio ulioifanya fasihi ya waturuki  
iwepo na kisha kuikuza na kuikomaza.



### 3. USUFI NA FASIHI

Usufi unaendesha mafunzo yake ya kiroho ndani ya moyo na sufi nayo huyaweka mambo haya mazito na utambuzi unaoingizwa nyoyoni mwao katika namna mbalimbali za kifasihi, ikiwemo ushairi na nathari. Katika kuzihuisha tafakuri na mafunzo haya kwa njia ya maneno, sufi wamekuwa wakizishughulisha akili zao kwa karne nyingi na kuacha kazi nyingi za sanaa zisizo za kawaida na zenye manufaa makubwa. Mchango mkubwa wa sufi umemsaidia mwanadamu kidogo kidogo kufikia hali nzuri kwa kupaza sauti zao ili kutoa hisia zenye kuvutia zilizopo ndani yao.

Katika historia ya fasihi ya kituruki kuna desturi iitwayo 'Fasihi ya *tekke*', fasihi ambayo ina asili ya kidini na ambayo ilianza kwenye majumba (*tekkes*) of kanuni za kisufi. Mtindo wa lugha katika fasihi ya *Tekke* unatofautiana kuanzia kwenye wepesi na moja kwa moja mpaka kwenye kusisimua na hata kufundisha. Alama za kidini na kiroho zimeingizwa katika zao la desturi hii. *Munacat* na *Nat* ni aina mbili maarufu za mashairi katika fasihi ya *Tekke*. Suala la msingi katika *Nat* ni upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu (*tawhid*) na kujikinga kwake, wakati *Munacat* ni neno lenye kuwakilisha upendo na shauku juu ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake. Licha ya jambo hili kuonekana tofauti lakini aina zote za fasihi ya *Tekke* zinawahamasisha watu kuboresha viwango vyao vya uchamungu, kuzibembeleza na kuzituliza nyoyo zao zenye shauku; na pia zinalenga katika kuzisafisha dhidi ya madhambi na kupuuzia mambo, na hivyo kujenga mapenzi, mshikamano na amani ndani ya jamii.

Tokea nyakati za msukosuko wa uvamizi wa Mongol, Mashairi ya Yunus Emre yalikuwa yakiwaongoza na kuwatuliza watu mpaka leo hii. Kwa kupitia mashairi yao na aina nyingine za fasihi, Sufi wametoa huduma kubwa katika kuisambaza dini katika vizazi vilivyokuja na kuhuisha sifa za kiroho na kimaadili. Khoja Ahmed Yesevi, Hacı Bayram Veli, Eshrefoglu Rumi na Aziz Mahmud Hudayi ni baadhi ya watunzi wa kisufi ambao si







tu walichangia katika kuiendeleza fasihi ya kiislamu ya Uturuki, bali pia waliwaongoza waumini kutokana na zao la fasihi yao.

Kutokana na desturi ya zamani au fasihi ya *Diwan* ilikuwa imebeba kazi za mashairi yaliyokuwa yameandikwa katika mfumo wa mizani iliyoitwa *aruz*, na yalikuwa katika mtindo wa kisanaa wa hali ya juu. Licha ya ukweli kwamba imebeba vipande vizuri vya sanaa ya mashairi, lakini sehemu kubwa ya fasihi ya *Diwan* imebeba ushairi wa vina uliozama katika mawazo ya kisufi. Mawazo ya ushawishi wa kisufi juu ya fasihi ya *Diwan* si ya kushangaza, kwani mtu anaweza kukuta ndani yake mifano mingi ya uwakilishi wa kiroho wa kiislamu, huku ukiwa umewekwa katika mtindo mzuri.

Kila aina ya shairi katika fasihi ya *Diwan* hugusia kipengele maalum cha dini. Kwa mfano *Munacat zinahusiana* na upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu; na hasa zile zilizoandikwa na washairi wa kisufi zimejawa na shauku ya kiroho. Vile vile kwa upande wa *Nat ambayo mada yake kuu ni kuhusu Mtume aliyebarikiwa* - rehema na amani ziwe juu yake, hapa huwa mtu anajawa na mapenzi juu ya Mtume. Kwa mfano *Fuzuli anaonyesha shauku yake kubwa juu ya Mtume* - rehema na amani ziwe juu yake - katika mistari ifuatayo kutoka katika kazi yake maarufu ya *Su Kasidesi (Shairi la maji)*, ambapo anagusia njia ya maji yatiririkayo:

*Maisha yao yote, wakigonga vichwa vyao kwenye jabali moja baada ya jingine,  
Ili kufikia kwenye ardhi aliyotembelea, kama mzururaji, maji yakitiririka.*

Matokeo yake chini ya ushawishi na msukumo mkubwa uliotokana na usufi, sufi wengi wakubwa kama vile Rumi, Fuzuli, Naili, Nabi, Nahifi and Sheikh Galib, waliweza kutoa kazi za sanaa zenye kuvutia.



Yote haya yanaonyesha maendeleo ya kiroho kutokana na aina zote za sanaa. Vipengele vya kisufi vya kiroho na kimaadili vilivyopo kwenye kazi za fasihi vimewezesha ladha ya sanaa ya mashairi ifikie nyoyo za jamii. Katika kuthibitisha suala hili mwanachuoni mkubwa wa Kituruki aitwae Nihad Sami Banarli anasema, “Usufi ndio ulioifanya fasihi ya Kituruki iwepo na kisha kuikuza na kuikomaza”. Ushawishi mkubwa ulioletwa na usufi katika kazi za fasihi pia unaweza kuonekana katika kazi za washairi ambao hawakuwa na uhusiano na usufi. Kwa mfano Nabi alikuwa mshairi





ambaye mara nyingi aliandika kuhusiana na mada zisizokuwa za kidini, ingawa hakuweza kujizuia kuandika kuhusiana na *nat*. Shairi la kwanza lililompelekea Tevfik Fikret kuwa maarufu lilikuwa katika *munacat*.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – binafsi aliwashawishi waumini waboreshe ujuzi wao katika sanaa na aliwata watafakari juu ya uwepo wa mwanadamu. Hasa alifahamisha juu ya ushawishi wa ushairi katika moyo na ubongo. Kutokana na *hadith* iliyosimuliwa na Aisha - Mwenyezi Mungu awe radhi naye, Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaagiza maswahaba zake wajenge mimbar maalum kwa ajili ya mshairi aliyeitwa Hassan ibn Thabit ndani ya msikiti wake. Hassan alikuwa akikaa katika mimbar hii na kutoa majibu ya kiushairi dhidi ya mashairi yaliyoandikwa juu ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kuhusiana na Hassan Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alisema, “Mwenyezi Mungu anamuunga mkono Hassan kwa kupitia Roho takatifu hali ya kuwa Hassan anamlinda Mjumbe wake” (Tirmidhi , Adab, 70; Abu Dawud, Adab, 87). Kutokana na ukweli kwamba Jibril – amani iwe juu yake – yuko pamoja na mshairi Hassan hili linaashiria kuwa kama msanii huyu ataamua kuandika kitu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu basi atapokea ufunuo mtakatifu na ithibati juu ya kile anachokifanya.





**V**itu muhimu katika sanaa ya wanadamu vimefinyangwa na usufi; vinawakilisha taswira ya usafi wa wanadamu, umakini na ufahamu wao katika hali mbalimbali. Kama ambavyo inaonekana katika historia, sanaa ya wanadamu ina nafasi kubwa katika kujenga ustaarabu.



#### 4. USUFI NA SANAA

Kazi za sanaa na mifano dhahiri juu ya uzito wa kiroho na umakini katika mambo mazito. Mwishoni kila sanaa ya mwanadamu itakuwa ni picha ya fikra na hisia zilizo ndani ya mwanadamu. Usafi wa kisanaa na kisanifu wakati wote huenda sambamba na undani wa kiroho.

Vitu muhimu katika sanaa ya wanadamu vimefinyangwa na usufi; vinawakilisha taswira ya usafi wa wanadamu, umakini na ufahamu wao katika hali mbalimbali. Kama ambavyo inaonekana katika historia, sanaa ya wanadamu ina nafasi kubwa katika kujenga ustaarabu. Matokeo yake mataifa yaliyokuwa yameendelea kiustaarabu katika kipindi kilichopita yalikamilisha mafanikio haya si tu kutokana na siasa, uchumi na jeshi, bali pia yalitokana na sayansi na sanaa. Historia ya uislamu imejawa na mifano ya maendeleo kama haya. Hapa hatuwezi kuelezea kwa kina juu ya mambo ya kiroho yaliyopatikana katika aina nyingi za sanaa. Badala yake tutasimamia katika maelezo kwa ufupi juu ya mambo ya kiroho yanayoonekana katika aina kadhaa za sanaa.

##### a. Musiki

Uislamu haukafazi uendeleu wa sifa zilizo ndani ya mwanadamu; badala yake huziweka katika utaratibu mzuri. Kama ilivyo kwa aina nyingine za sanaa zenye kuvutia; muziki nao ni moja wapo ya aina hizo ambayo kwa kupitia kwayo tunaweza kudhihirisha baadhi ya sifa zilizomo ndani ya mwanadamu. Kama ilivyo kwa aina nyingine za sanaa mtu hawezi kuukubali wala kuukataa muziki bila ya masharti yoyote.

Sufi wanatambua ushawishi mkubwa wa muziki juu ya mwanadamu na hivyo wanaitumia sanaa hii kwa ajili ya utukuzo, kama ambavyo imegusiwa katika kanuni za msingi za uislamu. Wanaoendesha muziki kwa maslahi ya akhera na wanafanya maudhui yake na maagizo yake





yafikie roho ya mwanadamu na si nafsi yake. Hivyo sufi wanakubali na kutumia aina ya muziki ambao unakubaliana na kanuni hizi za msingi, na wanakataa na kukataza aina zote za muziki ambazo zinachochea katika kumpoteza mwanadamu.

Kwa hakika pindi utakapoendeshwa kwa nia njema, ama ukiwa katika aina ya utumiaji wa ala za muziki au ukiongozwa na mashairi ya vina yenye vionjo vya *gazel*, *kaside* na *ilahi*, hapa muziki utakuwa umechukua nafasi kubwa katika kupandisha imani ya mwanadamu, kwani utakuwa unamuingizia fikra na ladha ya akhera. Kwa utaratibu huu muziki huleta manufaa makubwa. Kwa mfano, utaongeza utii kwa msikilizaji, utamfanya amkumbuke Mwenyezi Mungu Mtukufu, utamfanya awe makini na madhambi, utamuingizia moyoni mwake fikra safi na baraka, nakadhalika. Hasa pale muziki utakapokuwa umewekwa katika muda muafaka, wakati ambapo mtu atakuwa katika hali ya kiroho itasaidia kumuweka mtu katika hali nzuri ya kiroho. Kutokana na manufaa yake katika akili ya mwanadamu Sufi wamekuwa wakiutumia muziki kwa miaka mingi pamoja na njia nyingine chanya. Kutokana na athari yake katika dini sufi waliuweka muziki katika tawi la muziki wa kiislamu na zaidi ukaitwa ‘muziki wa kisufi’.

Pia hatuna budi kusema kuwa hakuna makubaliano ya moja kwa moja ya kuukubali au kuukataa muziki kwa sufi. Wakati kuna baadhi ya sufi wanaokataa moja kwa moja matumizi ya muziki kama njia moja wapo katika mafunzo ya kiroho, kuna wengine ambao wanasema kuwa muziki unaweza kutumika kwa nia hii pale ambapo masharti kadhaa yatafuatwa. Kwa mfano wanakataza matumizi ya ala za muziki zenye nyuzi lakini wanaruhusu matumizi ya madufu ambayo uhalali wake umepatikana katika historia kuwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaruhusu maswahaba zake watumie ala hizo katika baadhi ya sehemu kama vile katika vita ili kuwaamsha askari wa kiislamu.

Ili kujizuia na majadiliano yasiyoisha juu ya suala hili itatosha kuhitimisha kuwa matumizi ya sauti nzuri ya mwanadamu yanakubalika ndani ya mipaka ya uhalali katika dini. Inaweza hata kusemwa kuwa kuukubali muziki wa namna hii kunapendekezwa na waislamu wengi. Ni kweli kwamba adhana ya *muadhdhin* iliyotolewa kwa sauti nzuri ina mguso mkubwa kwa wasikilizaji. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alizingatia jambo hili wakati wa kumchagua mtu kwa ajili ya kuwaita waumini katika swala. Wakati waislamu walipokuwa wanajadiliana juu ya njia sahihi ya kuwaita waumini katika swala za faradhi Mtume aliyebarikiwa – rehema





na amani ziwe juu yake – aliota ndoto ambayop ndani yake aliambiwa maneno ya adhana. Ingawa kwanza aliwataarifu Abdullah ibn Zayd na Omar ibn Khattab – Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – juu ya adhana, lakini hakuwapa maswahaba hawa wakubwa jukumu la kuisoma. Kinyume chake Bilal – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ndiye aliyepewa jukumu hili, jambo ambalo mtu anaweza kusema kuwa sauti yake imara na nzuri ilichukua nafasi kubwa katika uteuzi wake; jukumu hili alilitekeleza katika kipindi chake chote alichokuwa hai.

Baada ya kuyasema hayo, hatuwezi kusema kuwa muziki unasababisha ushawishi chanya pekee kwa wanadamu. Pia isingelikuwa sahihi kuu-kataa muziki moja kwa moja wakati ukweli ni kwamba unatumika mno katika zama zetu katika kuwapotosha watu.

Kisa kifuatacho kinatupatia mbinu ya ujumla ya uislamu katika kuendea muziki kwa njia bora. Khoja Misafir ambaye ni mfuasi wa Bahauddin Naqshbandi anasema, “Nilikuwa mhudumu wa Bahauddin na pia nilikuwa nikipenda sana muziki kwa wakati huo. Wakati fulani nilikusanyika pamoja na wafuasi wake wengine huku tumeshikilia mikononi baadhi ya ala za muziki, tuliamua kupiga muziki mbele ya mwalimu wetu ili tuweze kufahamu namna anavyolichukulia suala hili. Hivyo tukatekeleza mpango wetu mbele yake. Mwalimu wetu hakutuzuia kufanya vile alisema, “Hatufanyi hivi...lakini pia hatukatazi”.

Mtazamo wa Naqshbandi unamaanisha kuwa waumini hawana budi kuelewa na kuwa makini juu ya muziki; kwani unaweza kutumika vibaya na kumpelekea mwanadamu kupotea. Tukirudi kwenye usufi ni kwamba hakuna budi kuchukua hatua madhubuti wakati wa kuuendea muziki, hasa katika zama hizi. Kama ambavyo tunaweza kuona katika baadhi ya makundi yanayojinasibisha na usufi, maudhui ya usufi yasiopotoshwe kwa kuimba.

## **b. Usanifu majengo**

Kwa hakika moja wapo ya kazi za sanaa zinaweza kuonekana kwa wingi na ambazo zinathibitisha ushawishi wa usufi ni usanifu majengo. Usanifu majengo unatokana na mchanganyiko wa hesabu, jiometri na uwezo wa kiroho wa wanadamu, vitu ambavyo huchanganywa kwa utulivu katika chungu kimoja. Kwa upande mwingine tunaweza kusema usanifu majengo unawakilisha uwezo wa mtu wa kiakili na kiroho ambao umehamishiwa kwenye vitu halisi kama vile mawe na mbao.





Usufi ulikuwa na ushawishi mkubwa katika usanifu wa kiislamu. Kwa mfano tunaweza kuliona hili wazi katika msikiti wa Suleiman na majengo yanayozunguka. Kwa kutazama usanifu huu wa majengo kwa jicho la kisufi tutagundua kuwa msingi wa uislamu umejikita ndani yake. Kuvutia kwake katika macho kunaendana na imani iliyowakilishwa kwa vipengere vilivyopo katika kila sehemu ya msikiti. Kilichobuniwa kwa ustadi zaidi ni kuba yake ya katikati na vinavyoizunguka, kuba ambayo kuanzia kwenye msingi mpaka juu tunaweza kuona alama iliyogawanyika gawanyika ambayo inawakilisha moja (Wahid); kuba hii ndiyo alama kuu ya jengo. Mpangilio wa kuba ya katikati pamoja na nyingine ni waajabu mno, kwani unawakilisha kanuni ya kisufi ‘umoja ndani ya mgawanyiko, mgawanyiko ndani ya umoja’. Hivyo msikiti wa Suleiman umebeba safu za alama za kiroho kwa namna yenye kuvutia, na ni mfano wenye kuonyesha kuhama kutoka kwenye wingi kwenda kwenye ‘moja’ tukufu, na kinyume chake. Na namna unavyoakisi visomo vya Qur’an tukufu na dua mbalimbali zinazotekelezwa ndani ya msikiti, pia kuba hiyo hiyo inamuashiria Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kazi yake ya kusambaza ujumbe mtakatifu kwa wafuasi wake.

Msikiti huu wa kipekee kinadharia ni makutano ya vipawa na uwezo wa mwanadamu. Utulivu uliofinyangwa na kuwa utukufu katika mtindo mzuri umepelekea kuwepo kwa makumbusho makubwa ya usanifu wa majengo wenye kuvutia. Pamoja na minara yake yenye kuvutia ikielekea angani, msikiri umekuwa kama mja mtiifu ambaye amejisalimisha kwa kunyanyua mikono yake huku akimuomba Mola wake.

Pia mandhari ya ndani ya msikiti wa Suleiman inaakisi ushawishi mkubwa juu ya roho ya mwanadamu. Wageni wengi wa dini mbalimbali wanaonyesha kuvutiwa kwao na mandhari ya msikiti huu na namna nyoyo zao zinapopata utulivu pindi wanapokuwa ndani yake. Ilisimuliwa kuwa msikiti huu ulijengwa kutokana na maagizo yaliyopatikana katika ndoto ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

Tofauti na misikiti kama wa Suleiman ambayo ilijengwa ili kudumu mpaka siku ya mwisho, pia kuna aina mbalimbali za taasisi za kisufi kama vile shule za madaruwesh, Nyumba za mapumziko na majiko ya umma, taasisi ambazo zilijengwa kwa ajili ya kukuza mandhari ya kiroho katika miji ya waislamu kwa namna tofauti tofauti. Majengo mengi ya aina hii makubwa kwa madogo yanaonyesha hali ya kupita, wepesi, udhalili na staha. Yalijengwa kutokana na matumizi yake, inamaanisha kuwa yalikuwa





yakitosha kuendeshea mafunzo ya kisufi; hivyo yamekuwa mbali na kuonyesha hali ya utukufu kutokana na kujengwa kwake kwa nia ya kutumika kwa muda mfupi. Cha zaidi ni kwamba majengo haya yote yanadhihirisha imani ya kiislamu iliyo ndani ya usanifu wa majengo.

### c. Kaligrafia

Kaligrafia ya kiislamu au *husn-i hat* ni sanaa ya kuandika herusi za Qur'an tukufu kwa mkono kulingana na utaratibu wenye kuleta mvuto mkubwa mbele ya macho. Kwa maneno mengine kaligrafia ya kiislamu inawakilisha usanii wa hali ya juu ambao ulipatikana kutokana na juhudi halali za kutaka kuiandika Qur'an tukufu katika namna nzuri yenye kuvutia. Katika historia nzima ya uislamu majumba ya sufi na mashule yao yamekuwa mbele katika kukuza kaligrafia. Maduara ya sufi wakati wote yamekuwa yakiunga mkono sanaa hii na wamefadhili wanakaligrafia wazuri ambao waliweza kupata nafasi nzuri katika taasisi za kisufi kwa ajili ya kukuza ujuzi wao na kuongezewa zaidi elimu ya sanaa. Wakati huo waliweza kupata mafunzo ya kiroho; kwani wakati wote moyo uliotakasika umechukuliwa kuwa ndio unaofaa kwa mwanakaligrafia ili kumuwezesha kutokana na kipaji chake kuzitafakari herufi kwa namna ambayo inaweza kugusa nyoyo za watazamaji. Zaidi ni kwamba ukomavu wa kiroho wa mwanakaligrafia ambao utampelekea kuwa mkufunzi katika sanaa ulimtaaka apitie katika hali ngumu ya uanagenzi ili kuboresha kiwango chake cha subira na kujisalimisha. Kutokana na hayo alihitaji mwanakaligrafia aliyekomaa kiroho ili amuige. Hivyo kwa kuzingatia upekee huo tutaona kuwa sanaa ya kaligrafia inahusiana na usufi kwa ukaribu mno.

Uhusiano kati ya kaligrafia na usufi unaweza kubainika tunapoangalia muandiko wa mtu katili na mwenye hasira; utaonekana umepinda na kuka-tika, hili linatokana na dalili za mahangaiko ya kiroho yaliyo ndani yake. Lengo la usufi ni kuifunza na kuisafisha nafsi na hivyo kiuokoa kutokana na madhara yake, haya hufanywa kwa kumuingizia amani na umakini. Wanakaligrafia nao wanahitaji amani na umakini wa namna hiyo, kwani sanaa ya kaligrafia haishii tu kwenye kuandika kwa mkono. Bali kimsingi ni fani inayolenga kuzitakasa roho na kuzijaza nyoyo kwa hisia za kiroho.

Uimarishaji wa kiroho umeweza kuandaa njia kwa wasanii wengi wenye vipaji katika kufikia katika daraja la ukomavu na ukufunzi. Ni kwa kupitia mafunzo ya kiroho ya maduara ya kisufi ndio ikapelekea watu





wakubwa wengi katika kaligrafia ya kiislamu kama vile Sheikh Hamdullah, Karahisari, Yesarizade and Mustafa Rakim wakafikia ukomavu kama huo. Mfano ufuatao umebeba umuhimu mkubwa katika kuakisi ushawishi mkubwa wa usufi katika sanaa za kiislamu.

Mwanakaligrafia mkubwa aliyeitwa Karahisari alikuwa amepewa jukumu la kuandika kaligrafia kwenye kuba ya msikiti wa Suleiman. Alifanya juhudi kubwa ili kuhakikisha anamaliza kazi yake katika ubora unaohitajika kadiri ya uwezo wake, ili kaligrafia hizo ziweze kubakia mpaka mwisho wa msikiti huo mtukufu. Aliifanya kazi ile kwa umakini mkubwa mno kiasi kwamba mwishoni akawa amepoteza uoni wa macho yake yote. Pindi ujenzi wa msikiti ulipokamilika na kuwa tayari kufungulia kwa ajili ya kutumiwa na watu, Sultani wa Uthmainiyya Suleiman alisema, “Heshima ya kufungua msikiti huu mtukufu kwa ajili ya matumizi haina budi kwenda kwa msanifu majengo mkuu Sinan kwa kukamilisha jukumu la kujenga msikiti huu wenye kuvutia”. Licha ya kuwa mkufunzi wa usanifu majengo lakini pia alikuwa mkufunzi wa staha. Mara moja Sinan akakumbuka kujitolea kwake muhanga Karahisari na hivyo kwa upole akamjibu Sultani kwa kusema, “Mheshimiwa, mwanakaligrafia Karahisari aliyatoa muhanga macho yake mawili alipokuwa anapamba msikiti kwa kaligrafia zake zenye kuvutia. Kwa maoni yangu naona ingelikuwa vizuri umpe yeye heshima hiyo”. Sultani Suleiman akakubali na kumpa Karahisari heshima hii ya kukumbukwa daima huku machozi yakiwatoka watazamaji.

Zaidi ya viwango vyake vya sanaa, ukuzaji na uendelezaji wa kaligrafia ya kiislamu unachukua nafasi kubwa katika kipengele cha kiroho cha uzuri. Kwa mtazamo huu unakiliji wa Qur’an tukufu na maelezo ya wema wa watu binafsi na sifa za Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – (*Hilya-i Sharifah*) umebeba ubora wa hali ya juu katika kaligrafia ya kiislamu. Kulingana na desturi wale wanakaligrafia ambao walithibitisha ustadi mkubwa katika kaligrafia ndio pekee wanaopewa nafasi ya kunakili Qur’an tukufu na *Hilya*. Mwenendo huu wenye kuvutia ndio uliopelekea kazi za kaligrafia zivutie nyoyo na roho kwa kuzishawishi kwa upole zitiكية amri takatifu ya “Soma!”.

Kutokana na kuwa kwake matokeo ya desturi hiyo ya kinadharia na kivitendo tokea mwanzo sanaa ya kaligrafia ilikuwa ikifundishwa bure kwa wanafunzi maalum. Kila mwanakaligrafia anachukulia huduma yake ya kufundisha kaligrafia kama sadaka ya wajibu na kamwe hawatarajii malipo ya kifedha katika ufundishaji wake.







Kwa ufupi ni kwamba muumini ambaye anakubaliana na *hadith* ifuatayo hata kidogo hawezi kuacha kuupenda uzuri. Hadith yenyewe inasema, “Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni mzuri na anapenda uzuri” (Muslim, iman, 147).

Mtu hujitahidi kuonyesha na kudhihirisha uzuri wake wa ndani. Lakinii msanii wa kiislamu huwa na shauku ya kutaka vipawa vyake vibainike kulingana na misingi maalum, bila shaka kwa namna ambayo inakubalika katika uislamu na hujiepusha na mitego ya kujivuna na kujionyesha. Hivyo aina zote za sanaa zinazoendeshwa kwa kuzingatia mipaka ya uislamu huungwa mkono na kulindwa na sufi. Aina nyingi za sana ambazo zinakubalika katika usufi kutokana na ustadi na imani ya mtu hufikia daraja la juu la uzuri kutokana na msukumo wa kisufi ulioko ndani yake.





**B**ila ya msaada wa utambuzi na hisia za kiroho mtu  
hawezi kuingia kwenye ulimwengu wa uhalisia  
kwa kupitia fikra za kibinadamu peke yake.



## 5. USUFI NA FALSABA

Sayansi asilia huchunguza vitu halisi na uwepo wake kimoja baada ya kingine na kujaribu kuziwakilisha sifa zake kwa kuzingatia kanuni za ujumla na kuziita 'kanuni za asili'. Falsafa ni nyanja ya kiakili ambayo unahusika na ama kuziunganisha hizi kanuni za kisayansi au kuanzisha zaidi nadharia za ujumla; pia ni tawi la kujifunza ambalo linashughulikia kulinganisha nyanja mbalimbali za kielimu na kudhihirisha undani wa muunganiko wake.

Kwa mtazamo huu falsafa inatambulika kama sayansi ya sayansi. Njia yake pekee ya kutaka kufikia kwenye ukweli wa hali ya juu ni uwezo wa mwanadamu wa kimantiki. Ingawa sio matawi yote ya falsafa yanayotegemea kukua kutokana na fikra za kibinadamu kama ilivyo katika tawi la falsafa la mantiki, lakini kwa ujumla wake yote yanategemea akili kama njia ya pekee ya kutafuta na kupata ukweli. Falsafa mantiki inakwenda mbali zaidi kiasi cha kujipachika uwezo wa kufikiri wa kiungu.

Uislamu unatambua akili ya kibinadamu na kuwa na akili timamu kama sharti la msingi la kuweza kuruhusiwa kutekeleza mambo ya wajibu. Lakini bado unatambua udhaifu wake katika kupata ukweli wa mambo, ndio maana unamtaka mtu ategemea masimulizi na mwenendo wa kidini (*naql*), huku ukitofautiana na falsafa iliyoegemea upande mmoja katika kuendea kwenye vyanzo vya elimu ya mwanadamu. Kutokana na uelewa wa kiislamu na kiu ya kutaka kufikia kwenye ubora wa hali ya juu, usufi unafuata uhalisia wa kimetafizikia wa namna fulani ingawa katika upande wake wa kimantiki unafuata mwenendo wa kidini na hauthubutu kwenda nje ya mipaka ya udhihirisho wa kiroho au utambuzi (*kashf*). Ukweli kwamba mawazo ya kisufi ya msingi yameegemea kwenye kanuni za kidini unalazimu utambuzi wa juhudi makini za kisufi kutokana na kujikita kwake kwenye mwenendo wa kiislamu wa masimulizi.





Ingawa akili ya kibinadamu imepewa uhuru maalum wa kuchukua na kutafakari juu ya hekima ya mwenendo wa masimulizi, lakini nafasi yake ya kujitegemea katika kutoa mwongozo wa kiislamu inaonekana kutotolewa. Kutokana na sababu hii ili kuufanya uwezo wa mwanadamu wa kimantiki uwe wenye manufaa uislamu umeagiza usahihishwe kwa ufunuo, hivyo kudhihirisha uhalali wake. Lakini bado jamii kwa ujumla au watu wasio na ujuzi katika suala hili hawatakiwi kukubali kila wazo linalowajia kwa kupitia kwenye utambuzi wake wa kiroho. Kuweka kiwango katika jambo hili ndio kanuni ya sufi ambayo inasema, "...Utambuzi wa kiroho unapatikana kwa mtu ambaye anauhisi na si kwa wengine".

Kwa njia yoyote ile hakuwezi kusemwa kuwa ukweli wa hakika unatosha kupatikana kutokana na uwezo wa akili ya mwanadamu; kwani hata baada ya akili kukamilisha utafiti fulani lakini bado roho huwa haitosheki na huendelea kutafuta ukweli zaidi. Hii ni sifa ya mwanadamu ya asili na ambayo amezaliwa nayo. Kwa sababu hii, karibia mifumo yote yenye kutumia akili ikiwa ni ya kidini ama la, inautambua ukweli huu ambao unauweka pembeni uelewa wa kimantiki. Ndio maana inafahamika kuwa sehemu kubwa ya mashauriano ya kimetafizikia imejawa na falsafa. Lakini kwa kuwa hawana njia nyingine zaidi ya akili ya kibinadamu katika jitihada zao za kusonga mbele katika utafiti wao, wanafalsafa wamejikuta wapo katika hatari ya kukinzana. Zaidi ni kwamba nyanja ya falsafa ni yenye kurejea, kwani kila wanafalsafa huanza kazi yake kwa kukataa au kukanusha nadharia za wanafalsafa waliopita ili kujitafutia nafasi yake binafsi, jambo ambalo hoja za kulinda nadharia mpya zinakuwa zimeegemea ubinafsi. Hata hivyo kinachotumika ili kukamilisha kazi hii ni kile kile; akili ambayo kamwe haiishi kuwa na kasoro.

Kwa hakika akili ya mwanadamu ni kama upanga wenye ncha mbili; mtu anaweza kuitumia kwa wema au ubaya. Akili ile ile ya mwanadamu ambayo inamuwezesha kufikia katika daraja la 'mfano bora' (at-Tin, 4) pia inaweza kumuangamiza na kumpeleka katika daraja la chini la 'waliopotea' (al-Araf, 179). Haya yanamaanisha kuwa akili ya mwanadamu haina budi kufuata kile kinachotokana na ufunuo. Pindi akili itakapokuwa chini ya usimamizi wa ufunuo itamuongoza mwanadamu kuelekea kwenye uongofu; na pale itakapoweka pembeni uongozi wa ufunuo itampeleka mtu kuangamia. Hivyo ili kupata radhi za Mola ni jambo la msingi kwa akili ya mwanadamu kuongozwa.

Historia imekuwa shahidi wa udhalimu mwingi uliofanywa kwa kuz-





ingatia mantiki, udhalimu huu umepelekea kutekelezwa mauaji makubwa bila ya kuhisi majuto hata kidogo, kwani watekelezaji wa mauaji haya walijichukulia kuwa wapo sahihi kulingana na uwezo wao wa kimantiki. Kwa mfano Hulagu Khan aliwazamisha katika maji ya Tigris watu wasiokuwa na hatia laki nne, na alilifanya hili bila ya kuhisi majuto hata kidogo. Kabla ya uislamu watu wa Makka walikuwa wakiwachukua watoto wao wa kike na kuwazika huku wakiwa hai licha ya makelele ya chini kwa chini kutoka kwa mama zao ambayo yaliumiza nyoyo zao. Kukata kichwa cha mtumwa hakukuwa tofauti na kukata kuni; na waliliona hili kama haki yao ya asili. Na wao pia walikuwa na akili na walikuwa wakifikiria kama sisi, jambo ambalo hata hivyo lilikuwa kama meno ya gurudumu linaloelekea katika upande mwingine hivyo kutarajia uharibifu.

Haya yote yanadhihirisha hitajio la wanadamu juu ya kuongozwa na kuelekezwa kutokana na matamano hasi na chanya waliyonayo. Hata hivyo maelekezo yatakayotolewa hayana budi kuendana na muongozo wa asili; na hili litawezekana kwa kupitia elimu itokanayo na ufunuo, yani muongozo na maelekezo ya Mitume. Kinyume chake maelekezo yatakayopingana na muongozo wa asili yatapelekea kwenye uovu.

Kwa kuwa wanafalsafa wanajaribu kukielezea kila kitu kwa kutumia akili basi hawawezi kujiongoza wao wenyewe kuelekea kwenye njia ya haki achilia mbali jamii yao. Hata hivyo kama uwezo wa kibinadamu wa kimantiki ungelikuwa unatosha kumuongoza mwanadamu katika njia iliyonyooka basi taasisi ya utume na kujitokeza kwa Mitume kusingelikuwa na ulazima. Kutokana na mtazamo huu akili inaendelea kuhitaji uongozi wa ufunuo.

Kutokana na kutambua udhaifu wa akili ya kibinadamu baadhi ya wanafalsafa walijaribu kutafuta njia nyingine za kutafuta ukweli. Mmoja wapo alikuwa mwanafalsafa wa kifaransa aliyetitwa Henry Bergson (aliyefariki 1941), ambaye badala yake alichukulia hisia za kibinadamu kama njia za kiepistemolojia za kufikia kwenye ukweli. Suala hili linaendana na kile sufi walichokiita 'matokeo ya ndani' (*sunu-hat- i qalbiyya*), wakimaanisha kuutumia moyo kama njia ya kupata elimu ya kweli. Bergson anadai kuwa itakuwa si sahihi kukataa ukweli wa matokeo ya ndani baada ya kupokea namna fulani ya mafunzo ya kiroho kwa kipindi fulani. Anadai kwamba kimantiki si sahihi kupinga uwepo wa ufahamu kutoka moyoni wakati ufahamu huu ambao ndio unaohusika katika usufi, upo katika hali tofauti ambayo inaondoa uchanganuzi wote wa kinadharia. Ukweli huu unaas-





hiria kuwa ni sehemu ndogo tu ya falsafa ndio inayokaribiana na fikra za kidini na kiroho. Kwa upande mwingine wanafalsafa wengi hawakubali njia yoyote ya kiepistemolojia katika kupata ukweli zaidi ya uwezo wa mwanadamu wa kimantiki, huku wakitumia masaa mengi katika siku kupotoshana wenyewe kwa wenyewe. Kinyume na hali ya mparaganyiko katika falsafa, Mitume na watu wema ambao ndio warithi wao sahihi wao wamejengeka katika utaratibu na utambuzi unaotokana na ufunuo. Hivyo Mitume na watu wema wakati wote hukubaliana wenyewe kwa wenyewe.

Ghazzali ambaye ni muislamu aliyekuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri anasema, “Pindi nilipomaliza uchunguzi na uchanganuzi wangu juu ya nyanja ya falsafa nilifikia muafaka kuwa nyanja hii isingeliweza kutoa majibu ya kuridhisha juu ya mahitaji yangu. Niligundua kuwa akili ya kibinadamu peke yake haiwezi kuelewa kila kitu na kwamba si wakati wote ingelishindwa kujaribu kufunua pazia lililofunika upande wenye kuonekana katika vitu”. Katika kufafanua maneno ya Ghazzali Necip Fazil Kisakiirek anaongezea, “Kwa kuwa huyu mwenye uwezo mkubwa wa kufikiri ambaye aliitwa ‘ushahidi wa uislamu’ alifanikiwa kuweka pembeni aina zote za muelekeo wa kimantiki na kisayansi na kuanza kuegemea kwenye elimu ya kweli, alidokeza kuwa, ‘...suluhisho la kweli ni kutafuta hifadhi katika imani ya Mtume wa Mitume; yote yaliyobakia ni aina fulani ya udanganyifu na kiini macho. Na akili si chochote bali ni mpaka tu!’ Hivyo kichwa hiki kizuri kikasimamia katika maswali yake yote na kikapata hifadhi chini ya imani ya Mtume wa Mitume, na pia kikagundua mambo yasiyo na mwisho” (Vetile r Ordusundan, uk. 213).

Katika kuthibitisha hili ni kwamba mtu anaweza kufikia katika kiwango fulani cha uhalisia wa mambo kutokana na uwezo wenye mipaka wa akili yake; lakini ni vipi uwezo huo utaweza kudhihirisha uhalisia wote? Je hakuna uhalisia mwingine nje ya huo? Ingawa falsafa hujaribu kutafuta majibu ya maswali ya kimetafizikia lakini haitoi majibu yenye kuridhisha juu ya maswali hayo. Lakini kwa kuwa usufi unatofautiana sana na falsafa katika kujiegemeza katika chanzo cha ufunuo mtakatifu, hapo mtu ataweza kupata majibu ya maswali haya yenye kusumbua.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye aliyemuumba mwanadamu na Yeye ndiye anayejua zaidi asili yake, mahitaji yake na mipaka yake. Hili linapelekea ufunuo mtakatifu kuwa wa lazima kwa ajili ya akili ya kibinadamu kutokana na shauku yake kubwa ya kutaka kufahamu ukweli wa mambo. Nje ya mpaka unaoweza kufikiwa na akili ya mwanadamu kuna ulimwen-





gu mwingine ambao hudhihirisha uhalisia wake katika moyo katika hali ya ufunuo au utambuzi wa kiroho. Kwa hiyo kufikia kwenye ulimwengu wa uhalisia usio na mipaka hakuwezekani bila ya msaada wa kiroho.





**K**ufahamu si kutazama bali kufumbua hekima na siri.



### G. ELIMU YENYE MANUFAA

Pindi ufahamu wa kawaida unapopatikana na kupenya kwenye vina vya utambuzi makini basi hufikia kwenye kiwango cha ufahamu wa hali ya juu au hekima (*irfan*). Mtu mwenye ufahamu mkubwa (*arij*) ni yule mwenye utambuzi juu ya siri na hekima za mambo matakatifu ambayo yamejikita katika moyo wake kama ufahamu. Kwa wepesi tunaweza kusema *arij* ni yule mwenye *irfan*. Mtu ambaye ni mjuzi katika nyanja za kawaida za elimu hufahamika kama mwanachuoni ingawa hajihusishi na mambo ya kiroho, lakini bado hawi *arij*. Elimu waliyonayo watu kama hao imetwama mahali kama elimu iliyoandikwa kwenye vitabu. Hali hii inaweza kulinganishwa na mbegu iliyopo ghalani; haiwezi kuota hali ya kuwa ipo mbali na udongo. Kwa kuwa imewekwa mbali na moyo elimu hiyo haiwezi kumfikisha mtu kwenye utambuzi wa kweli. Hivyo elimu ya namna hiyo imeitwa ‘elimu ya vitabu’ au ‘elimu ya kalallahu’.

Hata hivyo bila shaka elimu za aina zote zina manufaa kama zitatumika vizuri. Lakini tukizingatia furaha ya kweli na uongofu wa mwanadamu katika dunia hii na kesho akhera, kuzingatia vipengele vya nje vya sayansi hakutoi suluhisho la kudumu. Katika kuziba pengo hili uislamu umedokeza vipengele vya sayansi vya kiroho na kuagiza vitumike katika njia nzuri na yenye kuleta manufaa kwa wanadamu wote, na visije kutumika kwa malengo mabaya. Hivyo katika suala hili uislamu umeleta neno ‘elimu yenye manufaa’ (*al-ilmu’n-nafi*), neno ambalo linafufua mambo ya nje ya sayansi ya mwanadamu kutoka kwenye mtazamo ulio nje ya uwezo wa mwanadamu.

Marehemu Mahir Iz anahamasisha juu ya udhaifu wa elimu ya sayansi ambayo imekosa kipengele cha kiroho. Suluhisho pekee la kuondoa udhaifu huu ni kupata mafunzo ya kiroho. Iz anasema, “Ni vigumu kuweka kwa pamoja vipengele vidogo vya elimu ya kawaida katika namna nzuri. Kwa hiyo, nimefikia kwenye muafaka kuwa ingawa sihitajiki kujitoa kwe-





nye mambo ya kisayansi lakini elimu ya kweli na ukweli unapatikana chini ya usimamizi wa mwalimu aliyebobea katika masuala ya kiroho. Hii ndio sababu iliyonifanya baada ya kupata ishara ya kiroho nikaamua kuwa mfuasi wa mwalimu wetu Sami Efendi” (Yillarin Izi, uk. 396).



Ukomavu wa ndani unaopatikana mwishoni mwa barabara ya kiroho hupandisha utambuzi wa binadamu mpaka kwenye upeo wa juu zaidi ya ule wa sayansi za dhahiri, na upeo huu huitwa kwa jina la *marifah*; mtu huweza kufikia upeo huu kwa kutumia njia maalum za matendo ya kiroho. Hata kama mwanachuoni atakuwa mkubwa kiasi gani, pindi atakapofikia katika utambuzi wa juu kiasi hicho ataweza kutambua udhaifu wake, hivyo atakuwa ameponywa kutokana na ugonjwa wa kujivuna. Huwa amejawa na hisia za shauku na udhaifu mbele ya upeo ambao humpelekea kutambua uhalisia usio na mipaka. Akitafakari kwa umakini zaidi atagundua kuwa kufahamu jambo sio tu kuangalia vipengele vya nje vya kitu husika. Bali ni kufumbua siri zilizopo ndani ya uumbaji wake mkubwa na mwishoni kutambua hekima ya uumbaji wake.

Rumi anatoa maelezo mazuri juu ya umuhimu wa kuwa na ufahamu mtakatifu kwa ajili ya kupata furaha ya nje kwa mwanadamu kwa kupitia ishara za mafumbo, na anaonyesha matokeo mabaya yanayowangojea wale wasioingia kwenye njia yake ya utambuzi. Mwanasarufi anapanda katika boti. Anaanza kuongea na mwenye boti katika hali ya kuridhika kabisa, na anaendelea hivi katika safari yake yote. Muda baada ya muda anamuuliza mwenye boti maswali juu ya maelezo ya kina ya sarufi. Kila mara mwenye boti akikiri kuwa hafahamu majibu ya maswali anayoulizwa basi mwanasarufi hujisikia zaidi, na kila mara anamsikitikia kwa kumwambia, ‘masikitiko yaliyoje! Umepoteza nusu ya uhai wako katika ujinga!’ Ingawa anaumia moyo lakini kutokana na kukomaa kwake na wema wake hajibu lolote katika maneno mabaya yanayotolewa na mwanasarufi yule na anashia kukaa kimya. Huku mazungumzo yao yakiendelea mara kunatokea gharika kubwa na kujaribu kulivuta boti kuelekea kwenye dimbwi lenye kuzunguka na lenye kutisha. Wakati abiria wengine wakiwa wameshikwa na hofu kubwa, mwenye boti anaamua kumgeukia mwanasarufi na kumuuliza, ‘Je unaweza kuogelea mheshimiwa?’ Sura ya mwanasarufi inadhoofika na anasema kwa sauti ya chini, ‘Hapana, siwezi.’ Kisha mwe-







nye boti anajibu, 'Naweza kuwa nimepoteza nusu ya uhai wangu kwa kutojifunza sarufi...lakini wewe rafiki yangu umepoteza uhai wako wote kwa kutojifunza namna ya kuogelea. Lau kama ungelijua kuwa cha muhimu katika bahari si elimu ya sarufi bali ni elimu ya kuogelea!'

Katika fumbo hili elimu ya sarufi inaashiria sayansi za kidunia na za dhahiri. Lakini elimu yenye manufaa ni ile inayokidhi mahitaji ya mwanadamu; na hitajio kubwa kuliko yote kwa mwanadamu kimwili na kiroho ni kupata furaha ya milele. Na hili linategemea katika kupata radhi za Mola, jambo ambalo hutegemea imani thabiti na matendo mema.

Kisa hiki kinatufahamisha kuwa utakuja wakati ambao roho itakuwa inakaribia kuachana na mwili huku tukiwa kwenye kitanda cha mauti, elimu pekee itakayotufaa hapa si ile isiyo ya kiroho au isiyo na manufaa ambayo itachafua nafsi zetu, bali ni elimu ambayo itahamisha ufahamu wetu wa kawaida na kuwa *irfan* na hivyo kukidhi mahitaji yetu ya nje na kutupatia furaha.

Kwa hiyo kabla ya kufikwa na mauti hatuna budi kuibadilisha kila aina ya elimu tuliyonayo ambayo imetulia katika vichwa vyetu na kufanya kuwa elimu yenye manufaa, elimu ambayo itaridhiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Katika kipindi ambacho mwili unakaribia kurudi katika hali yake ya asili ambayo ni udongo, vipande vya elimu vilivyoparaganyika ambavyo viliufanya mwili uishi kwa raha havitaendelea kumsaidia tena. Wakati huo tunahitaji moyo madhubuti na uliotakasika. Kabla ya kifo kuu-fikia moyo, moyo unahitajika kuondoa vikwazo vya nafsi na kuwa na moyo safi. Kushindwa kufanya hivi kutapelekea kufa maji katika bahari pana ya akhera. Lakini wale ambao hujiepusha na sifa hasi kiasi cha kuweza kuiua nafsi chafu kinadharia. Watakuwa wanakaribishwa kwa furaha katika maisha mapya, maisha ambayo yako mbali na madhara yoyote. Kanuni ya kisufi isemayo 'Kufa kabla ya kifo' ni yenye kuonyesha njia katika suala hili. Kuitekeleza kanuni hii kunahitaji kujichunguza mwenyewe wakati wote. 'Jihesabu kabla hujahesabiwa' ni kanuni nyingine ya kiroho katika usufi ambayo inahamasisha kuangalia na kutafakari juu ya matamanio ya nafsi yasiyo na mwisho na kujitahidi kuirekebisha nafsi kabla ya kufika katika ulimwengu unaotungoja.

Mwanachuoni mmoja anasimulia kuwa siku moja "...alimuona Abu Hamid Ghazzali akiwa miongoni mwa kundi lililoelimika huku amevalia mavazi yenye viraka na akiwa amebeba chungu cha maji kikubwa. Nika-





muuliza, ‘Je wadhifa wa uprofesa mkuu katika chuo cha Nizamiya kili-chopo Baghdad haukuwa bora kuliko hili?’. Aliniangalia machoni mwangu kwa kitambo kisha akasema, ‘Nipo hapa kwa kuwa pindi mwezi mkamilifu wa furaha ulipoandama katika anga ya utashi, jua la tafakuri lilionyesha njia ya makutano’ (Muhammad ibn Abdullah al-Hani, Adah, uk. 9).

Kwa sababu hii, aina muhimu ya elimu ambayo itamuongoza mwanadamu kuelekea kwenye furaha na uongofu hapa duniani na kesho akhera ni elimu ya moyoni ambayo itampelekea mtu kumtambua Mola wake. Hii ndio aina ya elimu ambayo itampa mtu hisia za wajibu wa kiakili na kiroho ambapo kwa kupitia hisia hizi ataweza kutekeleza amali njema kadiri awezavyo. Bila ya kuwa na hisia hizi za umakini sayansi itapelekea kumuangamiza mwanadamu ingawa mwanzoni ilikuja kama msaada kwake. Kwa hiyo elimu yenye manufaa inahusiana na upeo mpana na akili. Bila ya elimu yenye manufaa vipengele vingi muhimu katika sayansi za wanadamu havitatambulika. Kinyume chake vitakuwa ni nyenzo za kumpeleka mtu kwenye mwisho mbaya. Njia pekee ya kujizuia na janga hili ni kwa kupitia ukomavu wa ndani ya moyo na sifa tukufu zinazotokana na tunachokiita ‘elimu yenye manufaa.’

Kuna uthibitisho mwingi wa watu kuitumia na kuitafsiri vibaya elimu fulani, licha ya kuelimika lakini wanakosa ukomavu wa elimu yenye manufaa. Kwa mfano mtu mwenye shahada ya sheria anaweza kuhukumu kwa ukatili wakati ukweli ni kwamba alifundishwa asimamie haki na uadilifu kwa wanadamu. Vili vile mtu mwenye shahada ya udaktari anaweza kugeuka na kuwa mtu mwenye kuua watu kikatili wakati anatarajiwa kuwatibu watu. Vile vile licha ya kuwa na elimu mtawala anaweza kuwaongoza watu wake bila ya huruma wala upendo. Ingawa wana aina fulani ya elimu ya sayansi, hawa watu wanaoitwa watu walioelimika hufanya uhalifu ambao hata kwa watu wasio na elimu unaonekana umepitiliza mipaka. Hivyo Yunus Emre anasema:

*Lengo halisi la mtu kujifunza,  
Ni kufahamu ukweli.  
Kama umejifunza, lakini bado hufahamu,  
Hiyo ni jitihada ya bure.*

Matokeo yake kila mtu cha kwanza na cha muhimu zaidi anahitaji uelewa na undani wa elimu yenye manufaa, huku akiwa anaendelea kujifunza aina mbalimbali za sayansi ili aweze kufanikiwa katika mambo ya





dunia na kesho akhera, kimwili na kiroho. Kiuhalisia ingawa inaweza kuwa na manufaa ya muda mfupi na ya nje, elimu ambayo itampelekea mtu kujivuna, kujiona na kujiangamiza mwenyewe itakuwa ni mzigo mkubwa kwake. Kwa sababu hii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa wakati wote akitafuta kuwa na elimu yenye manufaa na kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu amjaalie kuwa elimu ya namna hiyo. Katika suala hili Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiomba dua ifuatayo, “Ewe Mola! Ninakuomba unijaalie elimu yenye manufaa kutoka kwako na ninajikinga kwako dhidi ya elimu isiyo na manufaa!” (Muslim, Dhikr , 73). Pia kutokana na kuwa elimu muhimu katika usufi, elimu yenye manufaa inamaanisha juhudi katika kumfanya mja ashikamane na uvumilivu, uchamungu na kuiingiza imani moyoni. Pindi elimu ya muumini itakapofikia kiwango hiki cha ukamilifu wa kiepistemolojia basi itakuwa imefikia daraja la *marifah* au utambuzi wa hali ya juu.

Katika kuelezea tofauti hii ya elimu ya kiroho Rumi anasema, “wana-chuoni wenye elimu ya sayansi za dhahiri wanatambua ugumu wa jiometri, falaki, udaktari na falsafa kutegemeana na fani zao. Lakini zote hizi ni elimu zilizopo kwenye ulimwengu huu wenye kupita, ulimwengu ambao upo kwa kipindi kifupi tu. Elimu ya namna hiyo haiwezi kumpandisha mtu (*miraj*) mpaka kwenye sehemu iliyopo juu ya mbingu ya saba. Wajinga ambao ni watumwa wa nafsi zao hawawezi kupata elimu juu ya njia ya kuwafikisha kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na vituo vya kiroho vilivyopo kati yake. Watu wenye utambuzi na hekima pekee ndio watakaoweza kupata elimu ya namna hii; na ni kwa kupitia kwenye nyoyo zao na si akili zao”.

Wale wasio na ukomavu wa ndani wa elimu yenye manufaa hawawezi kufikia kwenye ‘uhalisia wa kweli’, hata kama watakuwa hodari kiasi gani katika fani zao. Ukweli ni kwamba elimu humuongoa mwenye nayo, na baada ya hapo ndipo ambapo mwenye nayo ataweza kuihamisha kutoka kwenye akili yake mpaka kwenye moyo wake ili kuikomaza na kuiweka katika maadili na matendo mema. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur’an, “Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Haki. Wala usiifanyie haraka hii Qur’ani, kabla haujamalizika ufunuo wake. Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie ilimu.” (Taha, 114). Ongezeko hili la ufahamu linaashiria kukua kwa daraja la mja la ukamilifu wa kidini, daraja lake la uchamungu na hofu yake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Pia Qur’an anasema, “Na katika watu, na wanyama, na mifugo,





pia rangi zao zinakhitalifiana. Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe.” (al-Fatir, 28). Katika suala hili Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

إِنَّمَا يَخْشَى اللَّهَ مِنْ عِبَادِهِ الْعُلَمَاءُ

“Miongoni mwenu mimi ndiye niliye katika daraja la juu la mchamungu na ndiye ninayemfahamu Yeye zaidi yenu” (Bukhari, Adab, 72).

Hivyo mtu ambaye elimu yake haijazama katika moyo na ambayo haijampelekea kumuogopa na kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu atakuwa si mwanachuoni wa kweli katika maana halisi ya neno hili, hata kama wale wanaomzunguka watamchukulia kuwa mwanachuoni.

Imam mkubwa Ghazzali anawazungumzia wale ambao wametekwa na sayansi za dunia za dhahiri na kuteketeza uhai wao katika mambo yasiyo na umuhimu, pale anaposema, “Nitakuonea huruma sana mwanangu kama utashindwa kuifanya elimu yako ya thiolojia, mantiki, balagha, ushairi na sarufi kuwa hekima na utambuzi mkubwa (*irfan*). Kama ni hivyo basi hautakuwa umepata manufaa yoyote, bali utakuwa umepoteza uhai uliopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kumuabudu”.

Basi kuna faida gani kuwa na elimu ambayo haitakusaidia kukuwezesha kuingia peponi ili kukutana na Mola? Elimu ya namna hiyo itakuwa sawa na kuvunja miadi mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Je elimu itakayompelekea mtu kwenye uovu, majivuno na uasi kama ilivyokuwa kwa Balaam ambaye alikuwa mtoto wa Beor na Qarun, kweli inaweza kuitwa elimu? Kwa hakika hapana! Kwa sababu hii watu wakubwa katika uislamu wanaelezea uelewa wa uislamu juu ya elimu kama ifuatavyo:

“Elimu inamaanisha uwezo wa kuelewa kitu, ambapo bila uwezo huu elimu haiwezi kuwepo. Mahala pa mwisho pa uelewa ni elimu juu ya Mwenyezi Mungu (marifatullah) ambayo ni kiini cha elimu zote. Kadiri sayansi inavyokuwa karibu na kiini hiki ndivyo inavyotukuzwa”.

Vile vile mhashimiwa Rumi anasema, “Mtu mwenye elimu na maarifa anastahiki kusifiwa...lakini kuna funzo la kuchukua katika suala la Shetani ambaye elimu yake haikumwezesha kumkubali Adam, pale alipohukumu kwa kuzingatia umbile la nje la Adam. Elimu na utambuzi wa aina nyingi





huwa kama mharamia ambaye anamzuia mtafutaji wa haki kupita njia kuu. Ndio maana watu wengi wa peponi ni wale wenye moyo safi na makini ambao waliweza kujilinda dhidi ya uovu wa wanafalsafa. Kwa hiyo jio- koe kutoka katika majivuno na kujisifu na jitenge na vitu vyote ambavyo havina manufaa ili uweze kupokea rehema takatifu kutoka juu”.

Hakuna mwanadamu ambaye anaweza kupata uhalisia wa mambo kutumia akili yake tu, kwani akili yenyewe haiwezi kujinasua kutoka kwe- nye mafumbo mengi inayokutana nayo pindi inapouangalia ulimwengu. Akili inasaidia sana katika kutambua vitu vya dunia vinavyoweza kumaki- nishwa na viungo vya fahamu; lakini bila ya msaada wa ufunuo mtakatifu haitakuwa njia bora ya kuwezesha kupata uhalisia wa juu wa mambo. Pamoja na akili ili kupata uhalisia wa mambo kunahitajika imani na upendo. Uwezo mzuri wa kimantiki uliofunzwa na ufunuo unaweza kum- fikisha mja katika hatua fulani katika utafutaji wake wa haki. Ili kutambua siri na hekima kubwa kubwa mbali na hatua hii mja atahitajika kupaa kwa kutumia mabawa ya moyo pekee.

Akili ni kama lango dogo ambalo linamruhusu mtu kuingia kwenye ulimwengu wa uhalisia na siri mbalimbali. Bila akili mtu hawezi kufikia daraja la *marifah*; mjinga hawezi kuwa na hekima. Lakini akili peke yake haitoshi kuwezesha kupata hekima hiyo, kwani inahitajika kupiga hatua zaidi kwa msaada wa upendo. Njia ya kuwezesha kwenda mbali zaidi ya mafunzo ya kawaida ya kimantiki imetajwa katika maneno ya Rumi ambayo yanahamasisha ‘kutoa muhanga akili yako mbele ya Mustafa (Mtume aliyebarikiwa)’. Ili kuwepo katika njia ya haki kunahitaji namna nyingine zaidi ya uwezo wa mantiki ya kibinadamu.

Watu wote wema wanathibitisha kuwa upendo ndio uliowawezesha kukatiza bahari hii ya uwepo wetu. Ndio maana tunakutana na sauti za upendo kwenye maneno yao tena na tena. Mbele ya macho yao dunia hii yenye kupita si chochote na haina umuhimu; hivyo umakini wao wote umelekezwa kwenye lengo la kweli. Watu watukufu ni waja wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambao wametenga muda wao kwa ajili ya kutekeleza jukumu la kiutume la kuzifunza na kuzitakasa nyoyo zao na kudhihirisha mifano hai katika maelekezo ya dini.

Muumini ambaye macho yake ya ndani yako wazi huona udhihirisho wa Mola popote anapoangalia. Hili lisionekane kama muujiza; bali ni elimu ambayo imebadilishwa na kuwa utambuzi wa hali ya juu (*marifah*).





Hili ni zao la upendo wa kweli ulio ndani ya moyo. Kwa msaada wa utambuzi wa kiroho ambao unatokana na upendo mtakatifu, watu wema na walimwengu wote wameweza kupata hekima na uhalisia juu ya viumbe vyote. Utambuzi wa kiroho wa namna hiyo ni zawadi kubwa takatifu. Maisha yangelikuwaje na maana kama mtu asingeliweza kuelewa lugha ya chini kwa chini ya pepo, mito na milima? Kunawezaje kuwa na raha yoyote katika maisha kwa mtu ambaye hawezi kupata mazingatio kutoka kwenye asili? Vyote hivyo ni ushuhuda wa wazi juu ya upekee wa uumbaji mtakatifu. Kushindwa kuhisi chochote mbele ya ustadi huu wa kipekee kunadhihirisha udhaifu wa ndani wa kiroho.

Sadi Shirazi anadokeza juu ya hekima na anawahamasisha watu kuzingatia juu ya elimu ya kweli pale aliposema:

*Mbele ya macho ya mtu aliye macho hata majani  
ya chanikiwiti ni baraza (kiushairi);  
Je si kwamba kila chembe chembe inadhihirisha ustadi  
wa Mwenyezi Mungu Mtukufu?*

Ulimwengu ni maonyesho yenye kuvutia ambayo yanatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kiumbe mwenye kuvutia katika ulimwengu huu ni mwanadamu kutokana na kubeba kwake moyo uliopambwa kwa vito vya kiroho ambavyo vinampa nafasi ya kukomaza roho yake katika maisha haya. Licha ya Hallaj kupigwa mawe na watu wake lakini bado alikuwa anazidi kukomaza roho yake kwa kutubu kwa niaba ya wale waliokuwa wanamrushia mawe.

Kila chembe chembe katika ulimwengu huu inaendelea kutuletea habari safi na salamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Tokea kwenye tabasamu la mtoto mdogo mpaka kwenye kupigapiga mabawa kwa kipepeo, tokea kwenye sauti za vinega mpaka kwenye radhi zenye kuvutia na harufu nzuri katika majira ya kuchipua, kila kitu ni udhihirisho wa furaha takatifu isiyo na kifani. Dalili za manufaa ya haya yote huonekana pale mtu atakapoanza kusoma kitabu cha ulimwengu kwa kupitia jicho la ndani na kutambua kuwa ulimwengu mzima ni kitabu cha hekima kitakachowezesha kupata mazingatio juu ya uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, "Na hatu-kuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake kwa mchezo." (ad-Dukhan, 38). "Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?" (Muminun, 115).





Ili kuendana na kanuni hizi kila nyanja ya elimu haina budi kumuongoza mwanadamu katika kutambua malengo ya kuumbwa kwake; na pia katika kuuangalia ulimwengu na kutambua utukufu wake kunapaswa kumpeleka kwa Muumba wa vyote. Mtu ambaye hajafikia upeo wa namna hii hawezi kuwa kamili, hata kama atakuwa na wadhifa au utaalumu kiasi gani katika nyanja fulani. Manufaa ya sayansi ya aina yoyote yapo katika kutoa ukomavu wa ndani na uzuri wa maadili; haya pekee ndiyo yatakatay-omnufaisha mwanadamu hapa dunia na kesho akhera.

Nukta zote hizi zinaonyesha kuwa mja ataweza kuwa na elimu yenye manufaa pale tu atakapokuwa na sifa za kiroho ndani ya moyo wake. Suala hili ni la pande mbili. Wakati mtu anaitakasa nafsi yake dhidi ya sifa mbaya kama vile kujiona, kujivuna, husda, kujisifu na kupenda umaarufu, wakati huo huo hana budi kuzibadili kwa kuingiza moyoni utukufu, tabia za Mtume kama vile uchamungu, usafi wa moyo, huruma, subira, kushukuru, staha, kutosheka, kujiheshimu, maadili mema na kumuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Imam Rabbani anatoa maelezo mafupi juu ya tabia inayoweza kuku-zwa na elimu yenye manufaa. Anasema, “Ndugu zangu, jukumu letu la kwanza na kipaumbele ni kusahihisha imani zetu kulingana na Qur’an na *Sunnah*. Wazushi na watu waliopotea wanaamini kuwa hukumu zao zinakubaliana na Qur’an na *Sunnah* wakati kiuhalisia zinaweza kuwa mbali zaidi”.

Pindi muumini atakapokuwa amejijengea tabia hii baada ya hapo atatakiwa kujifunza mwongozo wa dini, shughuli za halali na haramu na maagizo yaliyoelezewa katika Qur’an na *Sunnah*. Pia anatakiwa kuiweka katika matendo elimu yake ya kinadharia. Ili kuweza kuyafanya haya yote kiukamilifu hana budi kuingia kwenye harakati zenye kuendelea za kuutakasa moyo na nafsi yake. Elimu juu ya mwongozo wa dini hautakuwa na faida mpaka imani iwe sahihi. Kutekeleza matendo mema hakutakuwa na faida kama mtu hatakuwa na elimu juu ya mwongozo wa dini. Kuutakasa moyo na nafsi bila ya kutekeleza matendo mema hakutakuwa na faida yoyote. Na imani, matendo na elimu vyote havitakuwa na faida kama hautakasa moyo na roho. Mwenendo huu ndio unaopeleka elimu yenye manufaa itoe njia kwa ajili ya *marifah*.

***Ewe Mola wetu! Tunakuomba utujaalie kuwa na elimu yenye manufaa na utulinde dhidi ya elimu zote zisizo na manufaa! Tujaalie tuwe***





*miongoni mwa wale walioiweka elimu yao katika vitendo! Tujaalie tuwe miongoni mwa wale waja wako waliobarikiwa ambao wanaibadilisha elimu yao na kuwa utambuzi wa hali ya juu (marifah) na wanafikia kukufahamu Wewe; hivyo wakamilishie safari yao ya kiroho (miraj)!*

*Amin!*







---

# SURA YA PILI

---



## Mafunzo ya Usufi

(Sayr-Suluk)

### A - NAFSI NA UTAKASO WAKE (TAZKIYA)

- 1- Uhalisia wa nafsi
- 2- Utakaso wa nafsi
- 3- Hali za nafsi
  - a- Nafsi yenye kuamrisha maovu (an-nafsu'l-ammara)
  - b- Nafsi yenye kujilaumu (an-nafsu'l-lawwama)
  - c- Nafsi iliyopokea ufunuo (an-nafsu'l-mulhama)
  - d- Nafsi tulivu (an-nafsu'l-mutmainna)
  - e- Nafsi iliyotosheka (an-nafsu'r-radhiya)
  - f- Nafsi yenye kutosheleza (an-nafsu'l-mardhiyya)
  - g- Nafsi iliyokamilika (an-nafiu'l-kamila)

### B - MOYO (QALB) NA UTAKASO WAKE (TASFIYA)


- 1- **Tabia ya moyo**
- 2- Aina za nyoyo
- 3- Utakaso wa moyo
  - a- Chakula cha halali
  - b- Toba na swala
  - c- Kuisoma Qur'an na kutii maamrisho yake
  - d- Kuabudu kwa umakinifu wa hali ya juu
  - e- Kuhuisha nyakati za usiku kwa ibada
  - f- Ukumbusho mtakatifu na tafakuri (muraqaba)
  - g- Kumpenda Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake
  - h- Kutafakari juu ya mauti
  - i- Kukaa pamoja na watakatifu na watu wema
  - j- Kuwa maadili mema
- 4- Kuutazama ulimwengu kwa moyo safi

### C - KANUNI ZA MSINGI KATIKA MAFUNZO YA USUFI

### D - MURSHID-I KAMIL (MWALIMU MKOMAVU) NA NJIA ZA KUONGOKA KIROHO

- 1- Murshid-i Kamil
- 2- Njia za kuongoka kiroho
  - a- Mahabbah (Upendo) na Rabitah
  - b- Kuwa pamoja (Sohbah)
  - c- Huduma (Khidmah)
  - d- Egemeo zuri (tawajjuh)
  - e- Maombi (dua)

### E - UPEKEE WA SUFI

- 1- Upekee wa uongofu na huruma
  - 2- Upekee wa upole na upendo
- 



*“Hakika amefanikiwa aliye itakasa” (as-Shams: 9)*



## Mafunzo ya Usufi (Sayr Suluk)

*L*engo la mwenendo wa kisufi ni kuingiza ladha ya maadili ndani ya moyo wa muumini; ladha ya huruma, upendo, ukarimu, msamaha na shukurani.



Wanadamu wameumbwa katika viwango mbalimbali huku wakiwa na vipaji na uwezo tofauti. Kwa hiyo walimu wa kisufi hutumia mbinu mbalimbali kulingana na vipaji na silka za watu wahusika. Hata hivyo hatuna budi kusema kwamba haiwezekani kumbadilisha mwanadamu moja kwa moja; lakini anaweza kukomazwa kwa kiwango fulani kama atafunzwa na kuongozwa kwa maelekezo matakatifu. Sheria ya kiislamu (*Shariah*) huweka kanuni za ujumla sawa kwa waislamu wote. Kwa kuongezea na kwa kutegemea kanuni hizi za ujumla mwenendo wa kisufi unatumia mbinu maalum za mafunzo ya kiroho kulingana na sifa za watu binafsi. Hapa hatuna budi kufafanua nukta muhimu na ambayo mara nyingi hueleweka vibaya: Usufi hautumii kanuni ambazo zinakinzana na *Shariah*. Uhusiano kati ya *Shariah* na usufi unaweza kulinganishwa katika dira. Mhimili wa dira uliosimama ni *Shariah*, wakati ule mwingine wenye kuzunguka ni Usufi. Ingawa umbali katika mihimili hii miwili huongezeka kulingana na silka na uwezo binafsi wa mhusika lakini ule wenye kuzunguka wakati wote unalazimika kuutii ule uliosimama na kamwe hauendi kinyume na mwongozo wake.

Kwa upande mwingine masharti haya hufanya kazi kwa wale tu wanaojitahidi kuzingatia maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa sababu hii sufi wa kweli ni wale ambao wanarekebisha vipengele vya nje yao huku wakati huo huo wakizingatia katika kukomaza sifa zao za ndani. Sufi wa namna hiyo wakati wote hujitahidi kujipamba na sifa bora zaidi, nje na ndani, katika hali ya usawa. Si tu kwamba wanatambua umuhimu wa kusahihisha na kuboresha sifa za nje za kibinadamu,





bali pia wanasisitiza juu ya umuhimu wa kuboresha sifa za kibinadamu za ndani, hasa moyo; kwani matendo ya mwanadamu hutekelezwa kutokana na msukumo wa moyo.

Moja ya kanuni muhimu aliyoifuata Mtume aliyebariwa – rehema na amani ziwe juu yake - katika elimu ya kiroho ilikuwa ni kamwe kutomshutumu mshiriki wa majadiliano hata kama atakuwa amekosea katika vipengele vyote. Zaidi ni kwamba Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akimtahadharisha mtu bila kumwambia moja kwa moja bali kwa kuliashiria kosa kwake mwenyewe. Kuna masimulizi mengi yenye kufafanua tabia nzuri na za mfano kutoka kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alizozionyesha katika masuala hayo. Kwa mfano mara nyingi Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akionyesha kutokubaliana na jambo fulani kwa kusema yafuatayo katika hali ya taratibu na upole, “Nina tatizo gani kiasi kwamba nakuona umefanya hiki na kile?” Katika kuiiga tabia hii sufi wanahamasishana kujihesabu kila siku na kuishi na watu wengine kwa huruma ya hali ya juu. Kwa kuwa wamegubikwa na usafi wa ndani na elimu ya kiroho huwa wanachanganyika na watu, hata waasi, kwa upendo na uvumilivu. Hivyo sufi hujitahidi kuepukana na aina zote za madhambi. Kabla ya kusahihisha sifa za mbaya za kibinadamu Sufi hujaribu kulainisha nyoyo za washiriki wao katika mijadala kwa kutumia nguvu ya kiroho na baraka zitokazo kwenye mikusanyiko yao, na huziandaa nyoyo zao kwa ajili ya mchakato wa usahihi na kuwaboresha. Hivyo sufi huwasaidia wengine waweze kudhibiti hasira na ghadhabu zao na wakati huo huo kuwashawishi watubie.

Mfano usio na kifani wa utakaso wa kiroho unaweza kuonekana kwa Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – kwa namna alivyoishi na ndugu zake. Wakati wa utawala wake ndani ya Misri ndugu zake ambao mwanzoni walijaribu kumuua kwa kumtupa ndani ya kisima kilichotelekezwa jangwani walikuja kumuomba msaada. Katika kuhakikisha kuwa hawajihisi vibaya Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – alificha utambulisho wake halisi na kuwapatia kila walichohitaji; akawahudumia kwa utu, heshima na huruma. Kumbuka kwamba wakati ule Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa na uwezo wa kila namna wa kulipiza kisasi kwa ndugu zake na kumaliza mambo. Lakini badala yake kutokana na kuwa mfano wa kuigwa kiroho alionyesha msamaha wa hali ya juu na kuweka kila kitu pembeni kwa ajili ya Mola. Qur’an imeyaeleza maneno ya





Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – aliyowaambia ndugu zake pale utambulisho wake halisi ulipodhihirika: “Akasema: Leo hapana lawama juu yenu. Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mwingi wa kurehemu kuliko wote wanao rehemu.” (Yusuf; 92). Baada ya kuona kitendo hiki kitukufu ndugu wa Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – walijuta mno kutokana na kile walichokifanya miaka mingi iliyopita na kutubu kutokana na madhambi yao. Walitambua tabia njema za Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – na kuthibitisha imani yake; na hivyo kukawa na matokeo mazuri kutokana na hatua hii.

Mfano mwingine wa udhihirisho wa njia za kiroho za elimu ambazo zilifuatwa na Sufi katika historia ni kama ifuatavyo. Kundi la vijana wasiokuwa makini walikuwa wamekaa pembezoni mwa mto Tigris huku wakinywa na kufurahia siku yao. Sheikh mmoja mkubwa aliyetitwa Maruf Karhi alikuwa akipita pale walipokuwa na walipomuona anakuja walidhanja kuwa Sheikh yule angeliona jambo lao lile ambalo halikuwa na cha kujitetea na hivyo angeliwalaani. Kutokana na kuliona hilo walikosa utulivu. Mtu mmoja akasimama kwa jazba na kuita kwa kejeli, “Sheikh, kwa nini huanzi kutulaani mara moja tukaharikishwa kwenye haya maji ya Tigris na kupotea moja kwa moja?” Na bila ya kuonyesha dalili yoyote ya kusita Sheikh alinyanyua mikono yake kwa upole na kuomba, “Ewe Mola! Wajaalie vijana hawa wapate furaha kesho akhera kama ambavyo ume-wajaalia wafurahie siku yao katika dunia hii!” Kutokana na mshangao juu ya dua ya Sheikh vijana wale waliopigwa na butwaa waliuliza “Unasema nini Sheikh” Maneno yako hayaleti maana kabisa!” Maruf Karhi ambaye dua yake ndogo ilikuwa tayari imegusa nyoyo za wale vijana kutokana na usafi wake wa moyo alijibu, “Wana....Kama Mwenyezi Mungu atataka mje kuwa na furaha kesho akhera basi Atawaongoza kwenye kutubia”. Baada ya kusikia jibu lile wasilokuwa wamelitarajia vijana wale wakawa wameingia kwenye tafakuri nzito. Huku wakiwa wamegubikwa na majuto makubwa waliachana na chupa zao na ala zao za muziki na kutubia madhambi yao yote yaliyopita na wakawa watafutaji wa furaha na uongofu katika hii dunia na kesho akhera.

Kama ilivyokwishatajwa hapo juu kanuni nyingine ya msingi ya usufi katika elimu ya kiroho ni kutumia mbinu mbalimbali za kimafunzo kulingana na silka ya mtafutaji. Sababu ya kuwa na dhana nyingi za kisufi ni kuweza kuelezewa na kipengele hiki cha saikolojia ya kibinadamu; kwani





kutegemeana na aina za silka za watu binafsi kanuni za sufi zinatoa mbinu mbalimbali za elimu na maelekezo. Kwa mfano mtafutaji wa elimu mwenye shauku kubwa angelikuwa amepata mahala pazuri ndani ya aina ya mafunzo ya Qadiria, mafunzo ambayo yangelimuwezesha kuendelea katika njia ya kiroho kwa ufanisi mkubwa. Kwa upande mwingine mtafutaji wa elimu mwenye silka ya ushairi, sanaa na mahaba wangelijihisi nyumbani zaidi katika kanuni ya Mawlawi. Vile vile mtafutaji mwenye asili ya umakini na utulivu watakuta dhana ya Naqshbandi ndio inayowafaa zaidi. Kwa hiyo katika mafunzo yake ya kiroho na maendeleo yake mtafutaji wa elimu hutafuta na kupata mahala ambapo panamfaa zaidi kulingana na silka yake.

Silka ya mwanadamu haiwezi kubadilishwa moja kwa moja. Kutokana na kulifahamu hili walimu wa kisufi wamejiona wana wajibu wa kuwasaidia wafuasi wao watambue upande hasi na chanya katika tabia zao binafsi na hapo kuwaongoza katika uelekeo wa akhera. Walimu wa kisufi wanajitahidi kutoa njia maalum kwa kila mfuasi katika kukabiliana na matatizo yake ya kiroho.

Waarabu wa kabla ya uislamu walikuwa hawajastaarabika kabisa na walikuwa na nyoyo ngumu kiasi kwamba walifikia kuwazika watoto wao wa kike wakiwa hai. Walikuwa ni wafuasi wa jamii ambayo haki za binadamu zilikuwa mikononi mwa wenye nguvu, na watu wa kawaida walilazimika kupitia kwenye aina zote za mateso. Kwa kupitia mafunzo ya kiroho ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake – jamii hii ilipata uongofu ambao uliwapelekea kuwa wanadamu waliostaarabika kuliko wote hapa duniani. Hatuna budi kushukuru juu ya nguvu ya kiroho iliyokuwa nyoyoni mwao na ambayo haikuweza kuharibiwa kirahisi, nguvu iliyotokana na mapenzi yao makubwa kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, walitekeleza ibada zao kwa ikhlas ya hali ya juu. Katika kuacha alama kama maswahaba watukufu (*Ashab- i Kiram*) walicha urithi wenye kuendelea kwa vizazi vilivyofuata juu ya viwango vya kuigwa katika dini na maadili.

Chini ya usimamizi na mafunzo ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – maswahaba watukufu walifikia katika madaja ya juu ya imani. Abdullah ibn Masud anaelezea maendeleo yao ya imani yasiyo na kifani pale anaposema, “Tulifikia kwenye daraja la kuweza kusikia funda la chakula likishuka kooni huku likimtukuza Mola”.





Kwa hiyo usufi unaawakilisha njia za mafunzo alizozitumia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - katika kuwafundisha maswahaba zake ili kuwaongoza kuelekea kwenye utakaso wa kiroho na kidini. Usufi unawakilisha shule ya kiroho ambayo ndani yake moyo na nafsi hupitia mafunzo ya kusafisha na kutakasa chini ya uongozi wa waelimishaji wa kweli ambao kwa upande mwingine ndio warithi wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Na mafunzo ya usufi (*sayr suluk*) ni neno linalotumika kuelezea shule hii ya kiroho na njia ya maendeleo ya kuwa mwanadamu kamili.





Mwenye kuijua nafsi yake atamjua Mola wake.”



## A. NAFSI (NAFS) NA UTAKASO WAKE (TAZKIYA)

### 1. UHALISIA WA NAFSI

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuumba Adam – rehema na amani ziwe juu yake – peponi, Adam ambae ndie baba wa wanadamu wote, na kwa kupitia kwake alimfanya mwanadamu awe kiumbe mwenye kuheshimika kuliko viumbe vyote. Hata hivyo baada ya upendeleo huu Mwenyezi Mungu Mtukufu alitaka mwanadamu astahiki kuishi katika maisha matukufu na ya furaha ndani ya pepo. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu alimuumba Adam, Adam – rehema na amani ziwe juu yake – alitenda kosa linalojulikana na wengi ndani ya pepo na kupelekea kutolewa peponi na kuletwa hapa duniani; ingawa pepo ilibakia kuwa nyumbani kwake na hii dunia kuwa uhamishoni na sehemu ya majaribu. Hivyo kurudi kwa mwanadamu peponi kumekuwa ni jambo la malipo na kufaulu jambo ambalo linampelekea kutokuwa na budi ya kupitia mitihani mbalimbali.

Kwa sababu hizo Mwenyezi Mungu Mtukufu amemjaalia mwanadamu kuwa na sifa za kipekee miongoni mwa viumbe vyote. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliamua kumuumba mwanadamu kulingana na sifa zao za matendo yao yenye kutukuzwa na kulaumiwa, kuanzia “wa chini katika walio chini (*asfal al-safilin*)” mpaka kwa “wa juu katika walio juu (*ala al-'illiyin*)”. Kwa maneno mengine ili kuwa lulu ya viumbe vyote mwanadamu ana uwezo wa kuzaliwa nao katika kuendea mema na maovu; na hivyo nafasi yake ya chini au ya juu inategemeana na namna atakavyoutumia uwezo wake. Mafanikio ya mtu katika jukumu hili yanalingana na mafanikio yake binafsi katika kukuza sifa zake za wema na wakati huo huo kudidimiza upande wake wa maovu. Ubora wa mwanadamu hudhihirika katika uwanja huu wa vita ambao sifa za wema na uovu zinagombana kwa ajili ya kumuendesha mwanadamu.







Kulingana na sufi, viegemeo hasi na chanya ambavyo vipo kwa mwanadamu vina mandhari au vitovu viwili, katika “roho ya kiunyama” na “roho ya kiungu”.

Roho ya kiunyama ni kitu muhimu ambacho kinamuwezesha mwanadamu kubakia hai katika dunia na kuwezesha uwepo wake kibailojia uweze kuendeshwa. Pia inaitwa “uhai” au “nafsi”. Wakati roho ya kiunyama inaendeleza kazi zake ndani ya mwili wa binadamu hata wakati mtu amelala lakini shughuli nyingi za kibailojia huendelea ndani ya mwili. Lakini roho ya kiungu huondoka mwilini wakati mtu amelala na kurejea wakati wa kuamka. Roho ya kiunyama hufanya mwili usogee, uongee na kuwezesha kutekeleza kazi nyingine za mwili. Roho ya kiunyama huuacha mwili wakati wa mauti. Mahala pake ni kati ya ubongo na moyo, kuanzia hapo hutawanyika katika mwili mzima na hutekeleza majukumu yake kwa kupitia damu inayozunguka. Roho hii inahusiana na “dunia yenye muda mfupi na iliyumbwa (*alamu'l-khalq*)”<sup>1</sup> na imebeba mwanzo wa matendo ya kibinadamu. Na kama roho hii haitafunzwa basi itamletea mwanadamu ushawishi hasi.

Roho ya kiungu ni roho ya mwanadamu ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amepulizia nuru Yake ndani yake. Hii ndio sifa inayomtofautisha mwanadna viumbe wengine. Roho ya kiungu ipo katika “ulimwengu usio na hiari (*alamu'l-amr*)”<sup>2</sup> na huufanya mwili wa mwanadamu utekeleze matendo mema. Ni jambo la kushukuru kutokana na roho hii ambayo humfanya mtu aina maisha ya upole na ya mazingatio katika utumishi na utii mbele ya Mwenyezi Mungu. Roho ya kiungu haiondoki baada ya mwili kufa licha ya kwamba baada ya kifo athari ya roho ya kiungu juu ya mwili hufikia mwisho.

Mtu huyapa maisha yake muelekeo kulingana na mapambano yanayofanyika ndani yake kati ya roho ya kiungu na ya kiunyama. Pindi roho ya kiungu inaposhinda vita basi mtu anakuwa ameegemea kwenye matendo mema na maadili mema. Lakini pindi roho ya kiunyama inapochukua

1. Ulimwengu huu umepakana na nyakati na nafasi na imebeba viumbe. *Alamu'l-khalq* pia linaitwa “ulimwengu wenye kupita au unaoonekana”. Vitu tunavyovitambua kutokana na viungo vyetu vitano vya fahamu vinatokea kwenye ulimwengu huu.
2. Ulimwengu huu upo mbali na fikra za nyakati na maada na umekuwepo kutokana na amri takatifu ya “Kuwa!”. Pia inatambulika kwa majina kama vile “Ulimwengu wa kiroho au ulimwengu usioonekana”.





uskani basi mtu huegemea kwenye kila aina ya dhambi na utovu wa hes-hima. Kuwajibika kwa mtu juu ya matendo yake kunategemeana na vipa-umbele vyake na maamuzi yake kati ya matendo mema na mabaya. Kwa kuwa mwanadamu amepewa uwezo wa kufanya mambo yake bila ya kush-urutishwa na uwezo wa kuindesha roho yake ya kiunyama kwa kiwango fulani, basi atawajibika kwa kile alichokifanya na atatakiwa kupata malipo ama adhabu.

Nafsi ya mwanadamu huwa na moja ya kikwazo kikubwa kuliko vyote kinachosimama mbele ya mwanadamu ndani ya dunia hii yenye miti-hani na majaribu. Kwa sababu hii tutaifikiria nafsi ya mwanadamu katika mtazamo hasi. Kiuhalisia ni kwamba hata kama nafsi ina sifa chanya ndani ya kiini chake, lakini ili kukifanya kiini hiki kijitokeze na kutawala itambidi mwanadamu kuing'arisha nafsi yake dhidi ya kila aina ya uchafu kwa kupi-tia kwenye utakaso wa kiroho. Mtu hana budi kuendelea kujitahidi kuta-futa kufikia mahala pazuri huku akiwa hapa duniani ili aweze kuja kuishi kwa raha kesho akhera, kwani kila mtu hujenga maisha yake ya milele akiwa hapa duniani na huvuna kile alichokipanda. Kulingana na ubora wa matendo yake mtu ataweza kupata maisha ya raha au karaha kesho akhera. Kwa upande mwingine tunaweza kusema kuwa mtu mwenyewe ndiye anayejiandikia mwisho wake katika maisha haya.

Moja ya sharti muhimu kwa ajili ya furaha ya milele na uongofu wa mwanadamu ni kuweza kukomaza nafsi yake mpaka kwenye kiasi kizuri cha kuiva ili kuifanya iwe na desturi ya kutekeleza matendo mema. Nafsi iliyokosa uivaji huu ni sawa na farasi mwenye fujo na asiyedhibitiwa, farasi ambaye humpeleka muendeshaji wake kwenye uharibifu na si kule anapo-tarajia kufika. Kwa upande mwingine farasi mwenye tandiko lake ambaye amefunzwa vizuri na kufungwa kamba humpeleka mpandaji wake sehemu anakoenda kwa amani, hata kama barabara itakuwa ya hatari kiasi gani. Vivyo hivyo nafsi isiyodhibitiwa haiwezi kumfikisha mwenye nayo kwenye kilele cha malengo ya maisha.

Ukweli ni kwamba nafsi hufanya kazi kama usafiri wenye pande mbili. Wakati ina fursa ya kupandisha thamani ya mtu na kumfikisha kwenye kilele cha ukomavu na kumfanya kuwa lulu ya viumbe vyote, vile vile inaweza kushusha thamani yake mpaka kufikia chini miongoni mwa walio chini. Hivyo nafsi ina fursa ya kwenda pande zote mbili, kama kifu chenye





ncha mbili. Ikifunza vizuri itaelekea kwenye wema; kinyume chake itaelekea kwenye uovu bila moja kwa moja.

Kila roho ya mwanadamu ambayo imewekwa mbali na uongofu na udhibiti wa kiroho hufanya kazi kama pazia jeusi la ujinga ambalo limefunika juu ya uhalisia. Lakini kama ambavyo imetajwa hapo juu, licha ya kikwazo cha nafsi kama mtu atajitakasa kwa kuiokoa nafsi yake kutoka kwenye mikono ya sifa mbaya ataweza kufikia daraja la juu hata kupita malaika. Kwani stahili ya kila mwisho inaendana na kiwango cha ugumu kilichopitiwa na kiwango cha vikwazo vilivyoepukika kwa ajili ya kuufikia mwisho huu.

Sifa mbaya katika roho huingilia mawasiliano kati Mwenyezi Mungu Mtukufu na mja. Ni kwa kupitia mafunzo ya kiroho yanayohitaji ndipo mtu ataweza kusimama imara dhidi ya vikwazo hivi vyenye kuendelea; na hili linamaanisha kuwa na mapambano sawa yasiyokoma dhidi ya matamanio na ushawishi wa nafsi. Juhudi kama hiyo inahitaji kazi ya suluhu yenye kuendelea. Katika suala hili Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

الْمُجَاهِدُ مَنْ جَاهَدَ نَفْسَهُ

“Mpambanaji [wa kweli] (*mujahid*) ni yule ambaye anapambana na nafsi yake” (Tirmidhi, *Fadailu'l-Jihad*, 2; Ahmad ibn Hanbal, *Musnad*, VI, 20).

Ingawa mapambano dhidi ya nafsi hayaiui, lakini hupelekea kuidhibiti. Ukweli ni kwamba usufi nao haujaribu kuiangamiza nafsi bali kuizuia dhidi ya matamanio na ushawishi mbaya. Sufi wanatekeleza shughuli hii kulingana na maelekezo matakatifu. Katika suala hili Ghazzali analingani-sha nafasi ya mtu na ile ya mpanda mnyama na anasema, “Nafsi ni mnyama aliyevikwa kipando cha kiroho. Kama mtu ataachia kamba ya nafsi na kufuata uelekeo wake basi maangamizi juu yake si yenye kuepukika. Kama atajaribu kuiangamiza nafsi (kama ilivyo kwenye baadhi ya falsafa za kidini za wahindu), basi atawajibika kubakia nyuma kwenye njia ya uhalisia bila ya mnyama yeyote mwenye kikalio. Ni vyema ushikilie kwa nguvu kamba za mnyama na kujizoesha kufanya hivyo”.

Kufuata utaratibu huu katika kuishughulikia nafsi ni jambo muhimu na pia ni kipengele muhimu katika mbinu za kiutume katika elimu ya wan-





adamu. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – haku-kubaliana na tabia ya kujizua kula, kunywa na kuishi maisha ya kifamilia kwa ajili ya kuelekeza nguvu yote kwenye ibada. Mara kwa mara alisisitiza kwamba mazoea hayo ya kiutawa ya kujitenga moja kwa moja hayakuwa sehemu ya uislamu. Hivyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alionyesha uwezekano na mbinu za kuendelea kiimani huku unaishi maisha ya kijamii.

Kwa upande mwingine wakati wa kuiendea elimu hii, jambo ambalo ni gumu hupelekea mhusika kukabiliana na hali na vituo mbalimbali vya nafsi. Moja ya magumu makubwa yanayoikabili nafsi wakati inasonga mbele katika njia ya kiroho ni hatari ya kujikweza na baadae kujiingiza katika majivuno. Hatari yake ni kwamba hapa ndipo majivuno na kujiona vinapokuja kumtawala mtu. Katika juhudi ya kupambana na nafsi hata makosa madogo si ya kuvumiliwa, kwani yataruhusu nafsi kurudi kwenye asili yake.

Kwa kuwa nafsi wakati wote iko makini na inasubiria mashambulizi, mtu hana budi kutohisi yuko salama dhidi ya udanganyifu na madhara yake. Kwa sababu hii muumini hana budi kuwa macho wakati wote juu ya hatari na hila zitokanazo na nafsi yake mwenyewe. Hana budi kukabiliana nazo kwa umakini na kuzidhibiti kwa utambuzi utokanao na ufunuo mtakatifu.

Tutawezaje kuitakasa nafsi, ambayo ndiyo kipando cha mtu kilichowekewa tandiko, wakati ina ushawishi wa ndani juu ya maovu? Pia ni hatua gani za kiroho zinazosubiri kufikiwa katika jitihada hizi za utakaso? Sasa ni wakati wa kutafakari juu ya maswali haya mawili.





**S**wali ni kwamba je utaweza kuwa kama waridi au la. Kinachomaanishwa hapa ni kwamba ingawa unaona kila aina ya miba ndani ya bustani ya dunia hii, lakini hutakiwi kuwa kama mwiba hata kama utajeruhiwa kiasi gani na hiyo miba. Badala yake huna budi kujaribu kuwa kama waridi ambalo licha ya kuhisi baridi kali katika majira ya baridi lakini bado huendelea kuchanua kama kawaida...



## 2. UTAKASO WA NAFSI

Neno *tazkiyah* linamaanisha kusafisha na kutakasa. Pia linamaanisha kukua, kuboreka na baraka. Kutokana na maana hii *tazkiyah* imebeba mchakato mzima wa elimu ya kiroho.

Kuitakasa nafsi kunamaanisha kwanza kuisafisha dhidi ya ukafiri, ujinga, fikra potofu, hukumu za uongo na utovu wa maadili. Kwa maneno mengine utakaso wa nafsi ni kitendo cha kusafisha kilicholenga kuepukana na aina zote za uchafu wa kinadharia na kivitendo. Mchakato huu huishia pale nafsi itakapojazwa tabia nzuri za kidini na kimaadili kama vile imani thabiti, elimu, utambuzi, hekima na mambo ya kiroho.

Utakaso wa kisufi huzingatia katika kupunguza matamano ya nafsi, kuvunja mamlaka yake juu ya mwili na badala yake kujenga utawala wa kiroho. Jambo hili litawezekana kwa kupitia uvumilivu ambao utaimarisha nguvu ya kupambana na nafsi; na jambo hili linahusisha kujichunga katika kula, kulala na kuongea. Hivyo usufi unatoa njia za kuweza kuidhibiti nafsi kwa kupitia dhana tatu zenye ushirikiano: chakula kidogo (*qillatu't-taam*), usingizi kidogo (*qillatul-manam*) na maongezi mafupi (*qillatu'l-kalam*). Katika kujenga mamlaka ya kiroho juu ya nafsi hakuna budi kuzingatia kanuni hizi katika hatua za mwanzo. Pia ni lazima izingatiwe kwamba mhusika hatakiwi kuvuka mipaka wakati wa utekelezaji wa kanuni hizi. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ametupatia mamlaka ya kusimamia miili yetu, hatuna budi kuweka kichwani hitajio la kwenda nayo kwa staha.

Kwa maneno mengine wakati wa mchakato wa kuitakasa nafsi mja hana budi kujiepusha na kuzidisha katika uelekeo wowote ule. Hapaswi kufanya mazoezi ya kiroho kupita kiasi kwa kisingizio cha kutaka kuidhibiti nafsi; kwani uislamu unaamrisha staha katika hali zote na matendo yote na unawatahadharisha watu dhidi ya aina zote za mwenendo wa





kufanya mambo kupita kiasi. Pia haitakiwi kuitenga nafsi moja kwa moja na jambo hili haliruhusiwi katika dini. Badala yake muumini anatarajiwa kuitakasa nafsi yake katika namna ya kuifunga na kuifunza kulingana na maelekezo matakatifu.

Kitendo cha kuifunza na kuitakasa nafsi chenyewe ni kigezo cha kutambua mwisho wa mtu; kama utakuwa wa kuangamia au wa furaha. Ili kukamilisha mchakato huu wa utakaso mja hana budi kujisalimisha mwenyewe chini ya matakwa ya Mwenyezi Mungu na kupambana na matamania ya nafsi yake. Kila muumini hana budi kutambua kasoro, udhaifu na ujinga aliokuwa nao. Wakati huo huo hana budi kutambua utukufu na nguvu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuyadhibititi matendo yake kulingana na maagizo yake. Kama muumini atafanikiwa juu ya hili basi nafsi yake yenye kuamrisha maovu itakuwa imetakaswa dhidi ya uovu na kupelekea kuwa nafsi yenye kutukuzwa.

Jeshi la waislamu la watu thelathini elfu lilisafiri karibia kilomita elfu moja na kurudi. Mwishoni walipokuwa wanarejea Madina walikuwa wamebakia ngozi na mifupa kutokana mapambano yaliyoacha athari kwenye miili yao iliyochakaa. Ni katika mazingira haya ndipo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa akiwahutubia maswahaba zake ili wahamishie umakini wao kwenye mapambano makubwa yanayowangojea mbele yao. Kwa akili ya kawaida maswahaba walipigwa na butwaa hivyo wakamuuliza Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, “Ni ipi ambayo itaweza kuwa jihad kubwa zaidi ya hii?”. Kisha Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – akajibu, “Ndio, sasa hivi tunarejea kutoka kwenye jihad ndogo na tunaelekea kwenye jihad kubwa... jihad dhidi ya nafsi”.<sup>3</sup>

Kwa upande mwingine kisa kingine maarufu ni kile cha watu watatu ambao walishindwa kushiriki kwenye vita vya Tabuk. Ingawa walishiriki katika vita vyote vilivyotangulia lakini walishindwa kutii amri ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake - katika hili bila ya sababu yoyote. Pindi jeshi la waislamu liliporejea kutoka vitani wale maswahaba watatu walikuwa wametengwa kiroho na jamii; Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – pamoja na maswahaba wengine walikata mawasiliano yote na watu wale. Matokeo yake maswahaba wale watatu





wakahisi majuto ya hali ya juu kutokana na udhaifu na kushindwa kwao kuungana na wenzao kwenye mapambano ya vita.<sup>4</sup>

Sasa hivi hatuna budi kusimama na kutafakari kwamba ikiwa jihad ile ngumu ya kiwiwili ilionekana kuwa ‘jihad ndogo’, na kushindwa kuhudhuria kwenye jihad ile kuliwagharimu mno maswahaba waliotajwa, itakuwaje gharama ya kushindwa kuhudhuria kwenye ‘jihad kubwa’?. Kama ambavyo imekwishatajwa hapo kabla, Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alielezea jitihada ya mtu katika kuitakasa nafsi yake kama ‘jihad kubwa’. Kujiweka mbali na jihad ya aina hii kutapelekea mwisho mbaya kwa mtu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa kuzingatia ukubwa wa jukumu hili kila muumini mwerevu hana budi kukusanya amali zake pamoja na kuzihesabu kabla ya kuhesabiwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Katika suala hili Mwenyezi Mungu ametoa tahadhari kali ndani ya Qur’an: “Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa?” (al-Muminun, 115). Vile vile aya nyingine ndani ya Qur’an inasema: “Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure?” (al-Qiyamah, 36). Pia Mtume mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – anasema, “Mtu mwerevu ni yule anayeidhibiti nafsi yake na kuiwajibisha na kutekeleza matendo mema kwa ajili ya kesho akhera. Mtu mjinga ni

4. Majina ya maswahaba hawa watatu yalikuwa ni na walikuwa ni washairi. Maswahaba wote watatu walishiriki katika vita vyote isipokuwa Kaab – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye alikosa kushiriki vita vya Badr. Mara dunia ikawa nyembamba kwao na kukandamiza nyoyo zao, na wakawa wamepuuziwa na waislamu kutokana na kuamua kwao kubaki nyuma wakati wa vita vya Tabuk. Kibaya zaidi ni kwamba Mtume - rehema na amani ziwe juu yake – alijitenga nao kiasi kwamba akawa hajibu hata salamu zao. Dunia nzima ikawa ngeni kwao kwani hata wake zao wakawa kama wageni. Hawakuweza kufanya chochote zaidi ya kulia usiku na mchana. Walikuwa kama mishumaa iliyoyeyuka kutokana na kulia kwao. Walikuwa wamekosea lakini kukosea huko hakukuwaweka mbali na unyenyekevu na msimamo wa dini; wala hawakupoteza imani yao juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, wala hawakuwekwa mbali na majuto na toba. Zilipopita siku hamsini ndipo walipozawadiwa kutokana na unyenyekevu wao na toba ya kweli katika aya ifuatayo ya Qur’an: “Na pia wale watatu walio achwa nyuma hata dunia wakaiona dhiki juu ya ukunjufu wake, na nafsi zao zikabanika, na wakayakinika kuwa hapana pa kumkimbia Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwake Yeye. Kisha akawaelekea kwa rehema yake ili nao waendeleo kutubu. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu. Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli” (at-Tawbah, 118-119). Kwa malezo zaidi kuhusiana na suala hili rejea Othman Nuuri Topbas, Mlolongo wa Mitume, IV, 289-294.





yule anayetaraji wema kutoka kwa Mwenyezi Mungu bila ya jitihada yoyote na wakati anafuata matamaniao ya nafsi yake” (*Tirmidhi*, Qiyamah, 25; *Ibn Majah*, Zuhd, 31).

Hivyo kila muumini hana budi kutambua sifa za nafsi yake na jukumu lake la kuitakasa. Hana budi kuwa makini mno na kutumia mbinu stahiki ili asije akarubuniwa na nafsi katikati. Mwenyezi Mungu Mtukufu anatutahadharisha juu ya hila za nafsi kwa kusema:

أَرَأَيْتَ مَنْ اتَّخَذَ إِلَهَهُ هَوِيَهُ أَفَأَنْتَ تَكُونُ عَلَيْهِ وَكَيْلًا

“Je! Umemwona aliye yafanya matamaniao yake kuwa ndio mungu wake? Basi je, wewe utakuwa ni wakili wake?” (al-Furqan, 43). Pia Mtume Muhammad – rehemu na amani ziwe juu yake – anadokeza juu ya umuhimu wa jambo hili kwa kusema: “Kuhusiana na umma wangu, nahofia juu ya uwezekano kwamba watafuata matamaniao ya nafsi zao” (*Suyuti, jamiu’s-Saghir*, 1, 12). Hivyo kuitakasa nafsi ni jambo muhimu mno na ni jukumu kubwa kwa kila muumini. Mwenyezi Mungu Mtukufu anayasema haya ndani ya Qur’an katika aya ifuatayo:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّيْهَا وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّيْهَا

“Hakika amefanikiwa aliye itakasa, Na hakika amekhasiri aliye iviza.” (As-Shams, 9-10). Kwa maneno mengine ni kwamba yeyote atakayeisahishia nafsi yake atafika mwishoni mwa safari yake kwa amani na utulivu, wakati yule atayeiacha nafsi yake iingie kwenye uvukaji wa mipaka na majivuno atakuwa na mwisho mbaya. Haya yanamaanisha kwamba nafsi ina kazi mbili katika ncha tofauti. Kama mtu ataifuata hivi hivi ataishia kwenye hasara. Lakini kama mtu ataifunza na kuidhibiti basi ataweza kufikia kwenye daraja la juu la kiroho hata zaidi ya malaika. Nafsi ni njia ya kipekee ambayo inaweza kumuongoza mtu katika pande zote mbili.

Ingawa matendo yote mema yanatendeka kwa nje lakini wakati wote yana nafasi muhimu ndani ya mtu. Kwa mfano sadaka kwa nje inaonekana ni kumsaidia mhitaji; lakini kwa ndani huipelekea nafsi kuwa njema na nzuri. Kwa minajili hii matendo mema yanakuwa yamefika mahala pake ndani ya nafsi na humuathiri mtu kiroho. Vile vile kuisoma Qur’an ambayo







imebeba maneno mazuri na yenye ukweli kuliko maneno mengine yoyote yale, pamoja na kuzingatia maagizo yake na kuyafanyia kazi maelekezo yake ni njia moja wapo ya kuisahihisha nafsi. Mja ambaye huyaendesha maisha yake kulingana na Qur'an huwa salama dhidi ya ushawishi wa nafsi yake na hivyo humpelekea kutimiza lengo kuu katika maisha ambalo si lingine zaidi ya kupata radhi za Mola. Kisha moyo wake huwa tayari kupokea siri takatifu. Pindi mja atakapofikia hatua hii ya ukamilifu wa kiroho, visivyooneka hujidhihirisha kwake na ulimwengu hujidhihirisha kwake kama kitabu kilichowazi ambacho kimebeba hekima na maajabu. Kwa hiyo kila muumini hana budi kuzingatia maamrishi ya Qur'an na makatazo yake ili asije akahatarisha furaha na uongofu wake hapa duniani na kesho akhera.

Qur'an tukufu inatoa aya nyingi kuhusiana na kuitakasa roho. Neno 'utakaso' (*tazkiyah*) katika aya hizi liko katika namna kuu tatu:

- a. Utakaso kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.
- b. Utakaso kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake.
- c. Utakaso wa mtu mwenyewe juu ya nafsi yake.

#### **a. Utakaso kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu**

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur'an:

فَلَا تُزَكُّوا أَنْفُسَكُمْ هُوَ أَعْلَمُ بِمَنِ اتَّقَى

“Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vichafu, isipo kuwa makosa khafifu. Hakika Mola wako Mlezi ni Mkunjufu wa magh-fira, naye anakujueni sana tangu alipo kuumbeni kutoka kwenye ardhi, na mlipo kuwa mimba matumboni mwa mama zenu. Basi msijisifu usafi. Yeye anamjua sana mwenye kujikinga na maovu.” (An-Najm, 32). Mfasiri mmoja aliyelitwa Elmalili Hamdi Effendi alitoa maana ifuatayo kwa ajili ya aya hii: “Msijisifu na kuona kwamba hamna madhambi na kasoro na kwamba mmetakasika. Kwani mnaweza kuwa na kasoro nyingi bila ya nyinyi kutambua”. Katika aya hii hii ya Qur'an mfasiri mwingine aitwae Alusi anasherehesha kuwa “Imepokewa kuwa aya hii ilishushwa kuhusiana





na kikundi cha watu ambao walifikia kusema ‘swala, funga na hija ndivyo vitakavyotuokoa!’. Ni vizuri kwa mja kuficha ibada zake na amali zake njema ili zisije zikachafuliwa na kujiona na kuangukia patupu. Lakini bila nia mbaya kama hiyo hakuna tatizo kwa mja kuzungumzia amali zake njema ili kuwashawishi watu wengine nao wafanye kama yeye”.

Katika aya nyingine ya Qur’an Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, “Jee huwaoni wale wanao dai kuwa ati wametakasika? Bali Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye. Na hawatadhulumiwa hata kadiri ya kijiuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.” (an-Nisa, 49). Huku ni kujinadi mwenyewe kuwa umetakasika kutokana na kujisifu. Ukweli ni kwamba utakaso unategemeana na uchamungu wa mtu ambao unatokana na matendo mema. Na pia uchamungu ni jambo la ndani ya moyo ambalo uhakika wake anaujua Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee. Kwa sababu utakaso utakaokubalika ni ule tu uliotangazwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu na si ule wakujitangazia mwenyewe. Kutokana na hili ndio maana Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiomba, “Ewe Mola...jaalia roho yangu ikuhofie wewe na uitakase; kwani Wewe ndiye mtakasaji wake bora zaidi; yenyewe ni rafiki mlinzi na muongozaji” (Muslim, Dhikr , 73). Vile vile aya nyingine ya Qur’an inadokeza juu ya umuhimu wa utakaso wa Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwenyewe kama ifuatavyo, “Enyi mlio amini! Msizifuate nyayo za Shet’ani. Na atakaye fuata nyayo za Shet’ani basi yeye huamrisha machafu na maovu. Na lau kuwa si fadhila ya Mwenyezi Mungu na rehema yake juu yenu, asingeli takasika miongoni mwenu kabisa hata mmoja. Lakini Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua” (an-Nur, 21).

Yote haya yanathibitisha kuwa kiuhalisia utakaso unatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenyezi Mungu ambaye kutokana na fadhila na huruma yake isiyo na kikomo humuwezesha mja wake afanye matendo mema na humuongoza kuelekea kwenye njia za utakaso. Kwa hiyo mja hana budi kujiweka mbali na kujiona na kujisifu na badala yake ashikilie kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye mtakasafi wa kweli. Mja hana budi kutambua kuwa juhudi zake zote kuelekea kwenye utakaso hazitakuwa na manufaa kesho akhera ikiwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hatamtakasa. Utambuzi huu hutoa njia muhimu ya kufikia kwenye uongofu. Ingawa utakaso unaweza kuwa umenasibishwa na mja kutokana na uwezo na





juhudi binafsi, na Mitume na walimu wa kiroho kutokana na kutoa kwao muongozo na mafundisho, lakini mwishoni tutagundua kuwa utakaso unatakiwa unasibishwe na Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake, ambaye hutengeneza njia za utakaso kwa ajili ya mja wake na kumuwezesha kuzifahamu njia hizi.

**b. Utakaso kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake**

Katika kuelezea majukumu ya Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake, Qur'an inataja mambo yafuatayo:

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِنْكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ آيَاتِنَا وَ يُزَكِّيكُمْ  
وَ يُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ وَ الْحِكْمَةَ وَ يُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ

“Kama tulivyo mtuma Mtume kwenu anaye tokana na nyinyi, anakusomeeni Aya zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu na hikima na kukufundisheni mliyo kuwa hamyajui” (Al-Baqarah, 151).

“Hakika Mwenyezi Mungu amewafanyia wema mkubwa Waumini vile alivyo waletea Mtume aliyemiongoni mwao wenyewe, anaye wasomea Aya zake, na anawatakasa, na anawafunza Kitabu na hikima, ijapo kuwa kabla ya hapo walikuwa katika upotovu ulio wazi” (Al-i imran, 164).

Aya hizi za Qur'an zinabainisha majukumu makuu matatu aliyopewa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake:

**a. Kuwapelekea wanadamu aya za Mwenyezi Mungu Mtukufu**

Mitume kuwasilisha ufunuo mtakatifu ndio mwanzo wa utume wao. Pia hii ndio hatua ya kwanza na ya msingi katika kuwawezesha wanadamu kufika kule wanapoelekea kwa usalama.

**b. Kitendo cha utakaso**

Maana halisi ya imani juu ya upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu (tawhid) inaweza kupatikana kwa kusafisha nafsi ya mwanadamu dhidi ya uchafu kama vile ukafiri, ushirikina na madhambi. Kwa kuongezea ni kwamba ujumbe huu mtakatifu utakuwa umefika mahala pale utaka-





pokuwa umefikia kwenye nyoyo zenye amani na utulivu. Mfano mzuri katika hili unaweza kupatikana katika maisha ya maswahaba wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Licha ya kufanya maovu makubwa katika kipindi kabla ya uislamu lakini pindi walipopata uongozi sahihi kutoka kwenye mafundisho na mafunzo ya kiroho kutoka kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – waliamua kuzitakasa nafsi zao ili waje kuwa watu watukufu hapa duniani. Waliacha urithi wenye kuendelea kwa vizazi vilivyofuatia kutokana na kujikomaza na kujisahihisha kwao kiimani; Urithi huu utaendelea kubakia mpaka siku ya mwisho.

#### c. Kufundisha kitabu na hekima

Hapa kinakuja kitabu ambacho kinaelezea kanuni na masharti ambayo wanadamu wanapaswa kuyafuata. Kitabu hiki ni Qur'an tukufu. Sifa za mtu za kiroho ndizo zitakazodhihirisha uelewa wake wa masomo ya Qur'an. Ukweli ni kwamba Qur'an haina budi kusomwa na kuzingatiwa ndani ya moyo. Na macho ndiyo yenye kuusaidia moyo.

Kwa kuwa Qur'an, wanadamu na ulimwengu vyote vimekuwepo kwa kupitia udhihirisho na ufunuo wa Majina matukufu, basi vyote hivi vinawakilisha hazina kubwa ya siri. Siri na hekima hizi hujifungua zenyewe kwa mtu kulingana na kiwango chake cha utakaso na ukomavu wa kiroho. Mafundisho ya hekima yanakuja mwisho wa hatua zote hizi; kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu huwaruhusu wale tu waliozitatasa nafsi zao ndio wapate hekima na siri za Qur'an. Qur'an yenyewe inawakilisha siri za Majina matukufu katika mfumo wa "waadhi" ili akili ya mwanadamu iweze kuzielewa.

Aya za Qur'an zinataja utakaso pamoja na mafundisho ya kitabu na hekima. Hili linaashiria kuwa wale wasio na nafsi safi hawawezi kupata elimu ya kweli ya vitu mbalimbali na hasa ile ya Qur'an. Elimu yao haitawanufaisha hata kama itakuwa imejumuisha sehemu ndogo ya hiyo Qur'an. Kwa kuwa elimu na hekima vina thamani kubwa mno haviwezi kukaa mahali popote tu. Moyo ambao umeandaliwa kuwa mafikio ya elimu na hekima hauna budi kuwekwa mbali na aina zote za masizi hatari na yasiyo na manufaa yoyote. Kwa sababu hii kwanza kabisa Mitume huwasilisha aya takatifu na kisha wanajiingiza katika kuzitatasa nyoyo za wale ambao wameshawawasilishia aya. Baada ya mchakato huu ndipo Mitume wanapowafundisha kitabu na hekima watu ambao tayari wameshatakasika





kiroho. Siri zilizomo kwenye ulimwengu huu hujidhihirisha kidogo kidogo kwa wale walio na nyoyo zilizotakaswa kwa namna iliyotajwa. Wale walio na nyoyo za namna hiyo wanaweza kufikia kuwa chemchem za hekima.

Upande wa nje wa majukumu na maelekezo ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake – utaendelea kubakia mpaka siku ya mwisho kutokana na jitihada za makusudi za wanachuoni wa kiislamu ambao wanaisoma Qur’an na kuwafundisha wengine maamrishi yake na makatazo yake. Pia upande wa ndani wa majukumu yake utaendelea kubakia mpaka siku ya mwisho kutokana na jitihada kubwa za walimu wa kiroho ambao wamechukua jukumu la kuzitakasa nyoyo na roho.

### c. Mtu kuitakasa nafsi yake mwenyewe

Qur’an tukufu imesema yafuatayo kuhusiana na utakaso wa mtu mwenyewe juu ya nafsi yake, “Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake, Hakika amefanikiwa aliye itakasa, Na hakika amekhasiri aliye iviza.” (As-Shams, 7-10). Kulingana na masharti ya maneno haya ya Qur’an, watakaofanikiwa na kuongoka ni wale tu ambao watakuwa wametakaswa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kuwekwa mbali na madhambi na kujazwa baraka Zake na hofu juu Yake. Aya nyingine inaelezea mafikio ya watu hao kesho akhera kama ifuatavyo, “Basi ingia miongoni mwa waja wangu, Na ingia katika Pepo yangu.” (al-Fajr, 29-30). Bado aya nyingine nayo inasema,

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ تَزَكَّىٰ وَ ذَكَرَ اسْمَ رَبِّهِ فَصَلَّىٰ

“Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa. Na akakumbuka jina la Mola wake Mlezi, na akasali.” (al-Ala, 14-15).

Agizo la kutakasa lililotajwa katika aya hii ya mwisho lina mazingatio makubwa. Mja anatarajiwa: 1) Kwanza kusafisha moyo wake, mwili wake na mali zake dhidi ya uchafu wa kila aina; jambo ambalo 2) litapelekea kufunuka kwa mapazia ya ujinga yaliyopo kati ya mja na Mwenyezi Mungu Mtukufu; 3) baada ya hapo huku mwili ukiwa umekuzwa kwa chakula cha halali na moyo ukiwa unamtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu, hapo mja atakuwa ameingia kwenye ulimwengu wa utumishi uliokomaa na furaha ya kiroho.





Mfasiri aitwae Bursawi anaifasiri aya hii ya Qur'an kama ifuatavyo, “Aya hii inaashiria kwamba mja anatarajiwa kusafisha roho yake dhidi ya aina zote za vitu vilivyotajwa na uislamu kuwa ni haramu, kuutakasa moyo wake dhidi ya mapenzi ya dunia, kuuelekeza umakini wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kadiri awezavyo na kujitahidi kutokumbuka kingine chochote zaidi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu”. Katika kuisitiza jambo hili hili Abu Bakr Kattani alisema yafuatayo pindi alipokuwa juu ya kitanda cha mauti: “Kamwe nisingeliweza kuongelea juu ya amali zangu kutokana na hofu ya kuingia kwenye unafiki, lakini kwa kuwa kifo changu kimekaribia nahisi sina budi kusema mambo machache kwa ajili yenu. Nimekuwa mlinzi katika mlango wa moyo wangu na nimejitahidi ubakie umefungwa dhidi ya kitu kingine chochote kile isipokuwa Mola...na mwishoni moyo wangu ukafikia katika hali ambayo nikawa mgeni kwa kitu chochote kile isipokuwa Mola”.

Kutokana na tafsiri ya Ibn Abbas, neno *tazakka* (as-Shams, 14-15) linamaanisha “tamko la mtu la maneno hakuna Mungu apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu (*la ilaha illa Mwenyezi Mungu*)” (Qurtubi, jami, xx, 22). Mantiki iliyopo kwenye tafsiri hii ni kwamba kuusafisha moyo dhidi ya ukafiri na ushirikina kunaandika hatua ya kwanza katika mchakato wa utakaso. Sehemu ya kwanza ya tamko la upweke wa Mwenyezi Mungu (kalimatu't-tawhid) inaanza kwa kukanusha (*la*); yani ‘hakuna Mungu’ (*la ilaha*). Hili linaashiria kuwa muumini anatarajiwa kuusafisha moyo wake dhidi ya kila kitu kilicho kinyume na sifa za kimaadili zinazoendana na uungu mdogo. Kisha kunafuatia kuthibitisha ‘isipokuwa Mwenyezi Mungu’ (illa Mwenyezi Mungu), hapa ni pale moyo unapokuwa tayari kupokea na kujazwa nuru ya *tawhid*. Mshairi mmoja analielezea jambo hili vizuri sana pale anaposema:

*Toa kila kitu moyoni isipokuwa Mola*

*Kwani Yeye hatembelei mahali pasipo na mwenyeji mzuri*

Ibrahim Dasuqi - Mwenyezi Mungu atakase siri yake - anasema yafuatayo kuhusiana na utakaso huu, “Mwanangu...kamwe usije ukatawaliwa na majivuno, hata kama utatumia nyakati za mchana kwa kufunga na nyakati za usiku kwa kuswali; na hata kama una roho safi ambayo inafurahia ukaribu na Mola. Usikubali kamwe kutawaliwa na kujisifu na kuiacha nafsi ikuongoze; kwani madaruweshi wengi waliofanya hivyo waliishia kwenye maangamizi”.





Mtakatifu mwingine aitwae Hatam Asamm - Mwenyezi Mungu atakase siri yake – anasema, “Usije ukadanganywa na makasri ya kifahari, mabustani yaliyostawi na malisho ya kijani; kwani hakuna busutani lililo zuri zaidi ya pepo. Na kumbuka kilichomtokea Adam – amani iwe juu yake – katikati ya pepo. Kutokana na matamania ya kuishi humo milele alinyoosha mkono wake mpaka kwenye ‘tunda lililokatazwa’, baada ya hapo aliadhibiwa kwa kuletwa hapa duniani. Usidanganyike na wingi wa amali zako na sifa zako. Kwani licha ya sifa zake nyingi za kipekee, Balaam ambaye alikuwa mtoto wa kaburu aliishia kwenye maangamizi, licha ya kwamba wakati fulani Mwenyezi Mungu alimfundisha Jina Lake tukufu, (ismu’l-azam)<sup>5</sup>. Kuna funzo kubwa katika kitendo kile peke yake.

Amka na usidanganyike na wingi wa elimu na amali zako. Kwani hujapata kusikia kilichomtokea Shetani ambaye mwanzoni alijaaliwa elimu kubwa na ambaye alikuwa ametekeleza matendo mengi ya ibada? Kwa hiyo jihadharini na hila za Shetani na nafsi, vitu ambavyo Mola wetu Mtukufu ametuonya kwa kusema: ‘Kwa kuwa umenihukumia upotofu, basi nitawavizia katika Njia yako Iliyo Nyooka.’ (al-Araf. 16) na pia, ‘Mola wangu Mlezi! Ilivyo kuwa umenitia makosani, basi nahakikisha nitawazaini hapa duniani na nitawapoteza wote’ (al-Hijr, 39).

Usijidanganye kwa kuhisi uko salama kwa kukaana pamoja na wafanyaji ibada na wajitengao na anasa za kimwili; kwani ushirika wa nje pekee hauna faida. Kwani hujapata kusikia kisa cha Thaalaba<sup>6</sup> ambaye alikuwa akihudhuria madarasa ya Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake? Lakini alikuwa akikaa pale bila hisia zozote, jambo ambalo lilimpelekea kuangamia.

Licha ya kwamba alikuwa mtoto wa Mtume, mtoto wa Nuhu – rehema na amani ziwe juu yake – alijitia uziwi katika ujumbe wa baba yake kwa kiburi na kufikiria kuwa alikuwa amejitosheleza. Na pindi maangamizi yalipomfikia uhusiano wa damu na baba yake haukumsaidia.

5. Rejea al-Araf, 175-176

6. Mwanzoni Thaalaba alikuwa akitumia muda wake wote katika msikiti wa Mtume-rehema na amani ziwe juu yake – akisikiliza mafundisho ya dini. Lakini kadiri muda ulivyokuwa unasogea alianza kujikusanyia mali na kugubikwa na mapenzi ya kuipenda dunia. Kidogo kidogo akaanza kukosa swala za kila siku na hatimae akajitenga kabisa na jamii ya kiislamu. Alienda mbali zaidi kiasi kwamba akakataa hata kutoa sadaka katika jamii. Lakini mwishoni alifikwa na maangamizi makubwa. Tabari, *Tafsir*, XIV, 370-372; Ibn Kathir, *Tafsir*, II, 388.





*Na mke wa Lut – rehemu na amani ziwe juu yake...alikuwa na urafiki na makafiri na waovu bila ya kutofahamu hata kidogo nini kilikuwa kinaendelea ndani ya nyumba yake mwenyewe. Kutokana na kuhadaishwa na giza la ukafiri hakuweza kuona nuru ya uongofu.*

*Hivyo Mtegemeo Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake na si mwingine yeyote; kwani kinyume na Yeye hakuna elimu, amali, mali, mtoto au rafiki ambaye ataweza kukuhakikishia furaha ya milele”.*

Aya za Qur’an zilizokwishatajwa (al-Ala, 14-15) zinasema kuwa wale waliojitakasa na kuyashinda matamania mabaya ya nafsi zao ndio watakaofanikiwa. Hili linamaanisha kwamba wale ambao hawajakamilisha utakaso wao hawataweza kufikia furaha ya kweli na uongofu. Katika kuthibitisha haya kuna aya nyingine za Qur’an ambazo moja wapo inasema:

إِنَّمَا تُنذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ  
وَمَنْ تَزَكَّى فَإِنَّمَا يَتَزَكَّى لِنَفْسِهِ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ

“Na mbebaji habebi mzigo wa mwingine. Na aliye topewa na mzigo wake akiomba uchukuliwe hautachukuliwa hata kidogo, na angamwomba jamaa yake. Hakika wewe unawaonya wale wanao mcha Mola wao Mlezi kwa ghaibu, na wanashika Sala. Na anaye jitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.” (al-Fatir, 18). Kutokana na aya hii tunaweza kuhitimisha kuwa maelekezo na maonyo ya Mitume yatawasaidia wale tu ambao nyoyo zao zimejawa na usafi wa moyo na hofu juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu; na wale ambao wanaswali swala tano pamoja na ibada nyingine.

Wakosefu watalipwa kutokana na makosa yao na kukabiliwa na adhabu. Hakuna yeyote atakayeweza kuwasaidia ili wapunguziwe adhabu. Vile vile amali njema zitawafaa wale waliozitenda. Hivyo wale wanaozitakasa nafsi zao wanafanya hivyo kwa ajili ya nafsi zao.

Katika suala hili aya ifuatayo iliyopo ndani ya Qur’an inaelezea vizuri zaidi, “Na katika watu, na wanyama, na mifugo, pia rangi zao zinakhitafifiana. Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu,







Mwenye kusamehe” (al-Fatir, 28). Aya hii inaashiria kuwa kadiri mja atakavyokuwa na elimu zaidi ndivyo atakavyozidi kumtambua Mola wake ndani ya vina vya moyo wake. Nyoyo za wale waliopumbazwa na kutojali juu ya Mola wao zitakuwa zimekufa. Kuwaonya na kuwashauri kunakuwa hakuna manufaa yoyote. Qur’an (Yasin, 70) inaligusia jambo hili na inasema kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na ujumbe wa Qur’an vina msaada kwa wale tu walio hai. Ili mtu kuwa hai kiroho hana budi kujipamba na hofu juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kulidhihirisha hili kwa nje kwa kutekeleza swala za kila siku kwa umakini mkubwa.

Malipo ya kutakaswa dhidi ya madhambi ni ya daraja la juu peponi kama ambavyo Qur’an inathibitisha katika aya ifuatayo:

“Na atakaye mjia naye ni Muumini aliye tenda mema, basi hao ndio wenye vyeo vya juu. Bustani za milele zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa.” (Taha, 75-76).

Pindi mja anapouelekeza moyo wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu malipo yake huwa makubwa zaidi; hustahiki pepo ili kushuhudia uzuri na ukamilifu wa Mwenyezi Mungu (*jamalullah*), vitu ambavyo vipo nje ya mipaka ya maelezo ya lugha za hapa duniani. Yeyote atakayemgeukia Mola peke yake na kumfanya Mola wake kuwa ndiye kimbilio atawekwa mbali na aina zote za madhambi. Kwani ili kumfahamu Mwenyezi Mungu (*marifatullah*) huna budi kwanza kuitakasa nafsi jambo ambalo litapelekea kwenye kujitambua. Maneno maarufu ya kisufi, “Yeyote anayeifahamu nafsi yake basi anamfahamu Mola wake” yanaashiria uhusiano huu muhimu kati ya nafsi ya mwanadamu na kumfahamu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Leo hii na miaka hii ambayo wanadamu wanaishi chini ya nira ya uya-kinifu na ubinafsi, vitu ambavyo vinachafua roho zao, kuna vikwazo vingi ambavyo vinamzuia mtu dhidi ya jukumu muhimu la kuelekeza umakini wake kwenye uhalisia wa roho ya kibinadamu na mambo mengine ya kiroho. Hivyo leo hii kuna hitajio kubwa kwa walimu wa kiroho kusahihi-sha uelekeo wetu mbaya.

Historia ya waislamu imejawa na mifano mingi ya watu wa kuigwa. Miongoni mwa watu hao ni Sultani wa dola ya Uthmainiyya aliyetitwa Selim I. Wakati anarejea kutoka kwenye mapambano kutoka Misri alisikia kuwa watu wa Istanbul walikuwa wamejikusanya katika mitaa kwa ajili





ya sherehe kubwa ya kumpokea Sultani wao mshindi. Lakini kutokana na kujihisi vibaya juu ya wazo lile Selim aliamua kuchelewesha kuingia kwake Istanbul kutokana na kuona kwamba nafsi yake ingeliweza kupumbazwa na makaribisho makubwa yaliyokuwa yakimngojea. Alimwambia msiri wake aliyetwa Hasan Can kwamba wangelilingia kwenye mji “baada ya jua kuzama na kila mtu amerejea nyumbani kwake ili kuzuia mapokezi na salamu ambazo zitachochea nafsi zetu ziweze kututawala”. Kutokana na amri ile jeshi la waislamu liliingia Istanbul kimya baada ya jua kuzama bila ya dalili yoyote ya kujionyesha. Selim alikuwa akitambua hatari ya nafsi ya mwanadamu na hivyo alichukua tahadhari muafaka. Hivyo alikuwa ‘Sultani’ katika suala hili pia.

Muumini anatarajiwa kuihesabu nafsi yake na kuidadisi mara kwa mara. Hana budi kuangalia kwa umakini hali yake ya kiroho na maendeleo yake. Katika istilahi za kisufi mwenendo huu unaitwa ‘uchunguzi wa ndani’ (*at-tafahhusu’l-batini*). Uchunguzi huu wa nafsi ambao matendo yote yanatathminiwa tena hauna budi kufanyika angalau mara moja kwa siku. Pindi mtu atakapozoea kufanya hivi atakuwa na mkazo mdogo juu ya makosa yake ya kila siku. Sasa tuangalie Ghazzali anasema nini katika suala hili:

“Katika alfajiri ya kila siku muumini hana budi kukaa pamoja na ‘nafsi’ yake mara tu baada ya swala ya alfajiri na kufikia makubaliano kadhaa juu ya mambo kadhaa. Jambo hili ni sawa na makubaliano kati ya mfanya biashara na mbia wake kuhusiana na hisa zao kabla ya kuwasilisha mtaji wake kwa mbia. Wakati huu mfanya biashara hapuuzii kutoa tahadhari kadhaa kwa mbia. Vile vile mtu hana budi kuipa nafsi yake tahadhari na maelekezo yafuatayo. ‘Mtaji wangu wote ni uhai wangu. Pindi nitakapoteza uhai wangu pia mtaji wangu utakuwa umefikia mwisho, na faida na hasara havitakuwa na maana yoyote kwangu tena. Lakini sasa hivi siku mpya inanza. Mwenyezi Mungu Mtukufu amenipatia siku hii kama fursa kubwa kwangu. Kama angeli jaalia nife ningelitoa chochote ili nirudi kwenye maisha haya hata kwa siku moja tu ili nitekeleze amali njema pekee.’ Sasa chukulia kwamba ulikuwa umekufa na sasa hivi umefufuliwa na kurudi katika maisha tena. Hii ndio ile siku, usichafue kwa madhambi na maasi. Usipoteza hata sekunde yake moja, kwani kila pumzi moja ni zawadi yenye thamani kubwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu.





Tambua kwamba siku ina masaa ishirini na nne. Siku ya kiamu mtu ataletewa mbele yake masanduku ishirini na nne yaliyofungwa kwa ajili ya kila siku. Pindi atakapofungua sanduku moja wapo na kuona malipo ya amali zake njema katika saa lile atagundua kuwa sanduku limejaa nuru jambo ambalo litampelekea kuhisi furaha ya hali ya juu. Kisha atakapofikiria juu ya malipo mengine atakayoyapata atazama ndani ya furaha kubwa ambayo kama watu wa motoni wangelipata sehemu ndogo ya furaha hiyo wasingeliendelea kuhisi maumivu yoyote. Pindi atakapofungua sanduku la pili atahisi harufu mbaya sana ya saa alilolitumia katika maasi. Atahisi majuto ya hali ya juu kiasi kwamba kama watu wa peponi wangelipewa sehemu ndogo ya majuto yake wangelisahau moja kwa moja raha za peponi. Pindi atakapofungua sanduku la tatu atalikuta halina kitu; hiyo ni saa aliyoitumia kwa kulala au kufanya shughuli za halali. Bado atajuta kwa kutolitumia vizuri saa lile, jambo ambalo lingelimsaidia katika siku hii. Majuto yake yanalingana na yale ya mfanya biashara pindi anaposhindwa kuwekeza katika kitega uchumi kikubwa. Hivyo lijaze sanduku lako kabla hujachelewa; usiliache likawa tupu. Uvivu utapelekea kuzidisha ukubwa hasara yako.

Viungo vya mwili vinafanya kazi kwa msaada wa roho. Hatuna budi kuvisimamia kwa uangalifu na kuzielekeza nafsi zetu katika kutumia viungo vya mwili kwa usahihi. Hatuna budi kuyachunga macho yetu kutokana na kuangalia vitu vya haramu na visivyo na maana ili visije vikazishughulisha nyoyo zetu katika upuuzi. Hatuna budi kuchunga ndimi zetu dhidi ya usengenyaji, kulamba kisogo, kashfa, uongo, kujinyanyua, kuwaponda wengine na kujipendekeza; badala yake hatuna budi kuzishughulisha na kumkumbuka Mola na kuhakikisha zinatamka vitu vizuri tu. Hatuna budi kuyachunga matumbo yetu dhidi ya vyakula vya haramu na vyenye mashaka, na hata kupunguza matumizi ya vile vya halali. Katika suala hili Mtume aliyebarikiwa – anatuelekeza kwa kusema, “Kujizuia na mambo yasiyo ya msingi ni dalili ya kuwa muislamu mzuri” (Tirmidhi , Zuhd, 11; ibn Majah, Fitana, 12). Haya yanamaanisha kwamba kusema na kukaa kimya kwa muumini hakuna budi kuwa katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kutafakari juu Yake.

Pia muumini hana budi kuwa makini na kutekeleza ibada zake kulingana na utaratibu wake. Pindi anapotaka kuihesabu nafsi yake hana budi kuhakikisha kwamba amali zake zote zimetetelezwa kwa ajili ya Mwenyezi





Mungu pekee, na si kwa ajili ya yeyote yule ikiwemo nafsi yake mwenyewe.

Kutokana na kuitakasa nafsi hupelekea moyo kupata sifa ya ‘utulivu’ (*salim*). Muumini mwenye moyo uliotulia huwa na sifa tatu:

1. Hamdhuru yeyote. Hili linatokana na hofu juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Moyo huwa unachungwa dhidi ya uovu wa nafsi jambo ambalo linapelekea kuleta nje tabia nzuri za kuigwa.
2. Kamwe haumizwi wala kudhuriwa na yeyote. Hili linatokana na hisia yake kubwa ya upendo. Kamwe hatilii maaneni sifa au lawama za watu wa kawaida. Mshairi anatoa mukhtasari wa sifa hizi mbili kwa kusema, “Lengo la mwanadamu na jini kwenye bustani ya dunia...si kudhuru, kutamani vya wengine na kudhuriwa”.
3. Wakati wote hutoa kipaumbele katika kutafuta radhi za Mola kwa gharama yoyote ile. Pindi anapotakiwa kuchagua kati ya dunia na akhera, huwa hasiti kuchagua akhera.

Kwa ufupi ni kwamba Mwenyezi Mungu amejaalia dunia hii kuwa mahali pa mitihani na amempa mwanadamu jukumu la kurejea kwake baada ya kukishinda kikwazo ambacho ni nafsi; kubadilisha uasi wake na kuwa wema, jambo ambalo malipo yake hayawezi kulinganishwa na chochote hapa duniani.

***Mola wetu atujaalie tuzishinde nafsi zetu!***

***Amin!***





**M**tu mwenye roho iliyotakasika huwakilisha kazi bora ya Muumbaji Mkuu - Mwenyezi Mungu Mtukufu – kwani anakuwa ni mahala pa kud-  
hihirisha siri takatifu.



### 3. HALI ZA NAFSI

Kulingana na mchanganuo maarufu kutoka kwa sufi katika mchakato wa mafunzo ya kiroho na ukamilifu wake, nafsi ya mwanadamu inaweza kuwa katika aina saba za hali na vituo. Sasa ngoja tuingie kwenye maelezo ya kina juu ya hali hizi.

#### a. Nafsi yenye kuamrisha maovu (*an-nafsu'l-ammara*)

Hii ni hali ya chini kuliko zote na hali isiyo na utii miongoni mwa hali zote za nafsi ya mwanadamu. Hali humuondoa mja kwa Mola wake na kumshawishi ajiingize katika mambo ya uovu. Neno “*ammara*” lina-  
maanisha kushurutisha. Nafsi iliyokwama kwenye hali hii huwa inafuata matamaniao ya nafsi yake bila kutosheka. Hii ni nafsi iliyo katika kiini cha tamaa na urafiki na Shetani; huwa ina tamaa kubwa ya kufuata matamaniao ya nafsi yake na kutenda madhambi.

Dalili ya mtu katika hali ya nafsi yenye kuamrisha maovu ni kwamba huwa wakati wote anafuata matamaniao ya nafsi yake bila ya kuonyesha ukinzani hata kidogo. Vile vile huwa anafuata miito ya shetani kutoka ndani yake bila kizuizi chochote. Nafsi yenye kuamrisha maovu inaweza kuwa ya hatari zaidi kuliko hata Shetani. Katika kuthibitisha ukweli huu Ibn Ataullah al-Iskandari anasema, “Jambo la kuwa makini nalo zaidi ni nafsi yako. Si kwamba inafanya kazi dhidi yako, lakini pia huwa na wewe mpaka mauti yakufike. Angalau Shetani humuachia mtu katika kipindi cha Ramadhani, mwezi ambao mashetani hufungwa minyororo. Na kuto-  
kana na ukweli kwamba huwa tunaona mauaji na wizi katika mwezi wa





Ramadhani, huwa tunaelewa kwamba si Shetani ambaye humpelekea mtu kutekeleza uhalifu huu bali ni nafsi yenye kuamrisha maovu”.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur’an:

إِنَّ النَّفْسَ لَأَمَّارَةٌ بِالسُّوءِ

“Kwa hakika nafsi ni yenye kuamrisha maovu.” (Yusuf, 53). Hii ni nafsi katika hali yake ya kuamrisha maovu.

Katika istilahi za kisufi nafsi yenye kuamrisha maovu inawakilishwa kwa picha ya nyoka mwenye sumu. Kwa kupitia ishara hii sufi wanawatahadharisha watu juu ya sumu ya hii nafsi. Mshairi Nevizade Atai anaitumia picha hii katika ushairi wake pale anaposema, “Kila tabia ya uovu inafanana na nyoka; na nyoka mfalme ni nafsi yenye kuamrisha maovu”. Kwa sababu hiyo kila muumini mwenye akili hana budi kujiingiza kwenye mapambano yenye kuendelea dhidi ya nafsi yenye kuamrisha maovu. Watu wengi ambao wamewahi kupata baraka za uhodari wa hali ya juu wameishia kufadhaika kwa kukumbatiwa na ujinga kwa manufaa hafifu.

Katika suala hili kisa cha Qur’an kuhusiana na mazungumzo kati ya mke wa Potiphar na Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – kinatoa ishara muhimu zenye kuelekea kwenye uelewa wa asili ya nafsi yenye kuamrisha maovu. Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – amekuwa na kuwa kijana mzuri sana na Zulaykha anavutiwa naye kimapenzi, Qur’an inasomeka kama ifuatavyo, “Na yule bibi wa nyumba aliyo kuwamo Yusuf alimtamani kinyume cha nafsi yake, na akafunga milango.” (Yusuf, 22-24).

Hatuna budi kushukuru msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu uliopheleka Yusuf kuokolewa kutokana na kuangukia kwenye hadaa za Zulaykha ambaye hawakilishi kingine isipokuwa nafsi yenye kuamrisha maovu. Kutokana na kuwa waja dhaifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, hatuna budi kugeuza nyuso zetu kwake kwa maombi na hofu na kumuomba msaada wake atulinde dhidi ya vishawishi vya nafsi zetu wenyewe juu ya maovu.

Hapa Mwenyezi Mungu Mtukufu anatupatia maneno ya heki-





ma. Anatuagiza tusikaribie hata kidogo matendo maovu ili uharibifu wake usije ukatutawala. Kwa maana hii ndio maana kumeharamishwa kwa mwanamme kumuangalia mwanamke ambaye kisheria unaweza kumuoa, kwani uangaliaji huo unaweza kufungua mlango wa zinaa. Kwa hakika kisa cha Zulaykha na Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – kimebeba maana nyingi kwa ajili yetu ili tutafakari juu ya mitihani mbalimbali ya dunia.

Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa kijana kama malaika kutokana na uzuri usiowahi kuonekana hapo kabla. Pindi wanawake wa kawaida walipomuona walikata vidole vyao na kushindwa kuhisi hata maumivu au damu iliyokuwa ikitiririka viganjani mwao. Kama Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – angelikuwa mtu mzima kiasi cha kutokuwa na matamano yoyote juu ya jinsia tofauti basi mitihani aliokuwa amepangiwa kuupitia usingelikuwa mgumu kiasi kile.

Zulaykha alikuwa amepambiwa na nafsi yake mambo makuu mata-tu: utajiri, umaarufu na tamaa. Alikuwa kijana na mzuri na hivyo kuwa na ushawishi ambao ungeweza kuwateka wengi. Ili kufanya mambo yawe magumu zaidi aliukomea mlango kwa nguvu kabla ya kutekeleza nia yake. Katikati ya nyakati zile ambazo kulikuwa na usiri wa hali ya juu wenye kurahisisha njia ya kuangukia kwenye dhambi Zulaykha alimuita Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kumwambia ‘njoo usitarehe na mimi’. Alikuwa amekabiliwa na mtazamo ambao ungeliveza kuyeyusha ukinzani wa uwezo imara kuliko wa wengine, Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuelezea ugumu wa mazingira ya tukio hata kwa mtu kama Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake: “na Yusuf angeli mtamani lau kuwa hakuona ishara ya Mola wake Mlezi...”

Kuanzia pale na kuendelea Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – akaomba, ‘Mola awe mlinzi wangu’, na kwa kufanya vile alionyesha kwamba njia pekee na ya uhakika ya kutoka kwenye mazingira magumu inatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Haya yanathibitisha ukweli kwamba kujizoeshwa kuwa na hofu juu ya Mwenyezi Mungu ni muhimu katika kuvuta karibu msaada wa Mwenyezi Mungu. Kwa maneno mengine ni kwamba ni kwa kupitia kwenye kuimarisha hisia za hofu juu ya Mwenyezi Mungu ndipo mtu ataweza kuzuia matamano mazito yatokanayo na nafsi yenye kuamrisha maovu. Ukweli ni





kwamba kukataa ushawishi wa mwanamke kijana, mzuri na tajiri huku mkiwa faragha ni miongoni mwa vitu vigumu kwa kijana mwenye afya.

Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake - anasema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu atawapa kivuli watu wa aina saba siku ya kiama; katika siku ambayo hakutakuwa na kivuli zaidi ya kivuli cha Mwenyezi Mungu. Katika orodha hii ametajwa “mtu ambaye atakataa mwaliko wa mwanamke mzuri na mtukufu kwa ajili ya kitendo cha zinaa na akasema, ‘Mimi ninamuogopa Mwenyezi Mungu.’” (Bukhari , Adhan, 36).

Upande dhaifu wa saikolojia ya mwanadamu hudhihirika pindi mtu anapofikwa na usumbufu wa aina fulani ambao utampelekea kupoteza udhibiti wa nafsi yake. Lakini hili halikutokea kwa Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake, kwani ulinzi wa Mwenyezi Mungu ulimzuia asiingie kwenye mtego huu; hata hivyo alikuwa mja mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na pia alikuwa na nafsi yenye ukamilifu (an-nafsu’l-kamila). Ulinzi mtakatifu ulimpa nguvu Yusuf dhidi ya ulaghai ambao kinyume chake angeliweza kuingia kwenye njia ya nafsi yenye kuamrisha maovu.

Pia kuna funzo lingine ambalo tunaweza kulipata kutoka kwenye tukio hili. Zulaykha alimtishia Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – kwamba angelimfunga gerezani kama angelikataa kukidhi matamanio yake ya kingono. Kutokana na nafsi iliyotakasika ambayo ilikuwa ikimzidishia hofu juu ya Mwenyezi Mungu ilimpelekea Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – aseme yafuatayo baada ya kuitwa na Zulaykha, “Ee Mola Mlezi wangu! Nastahabu kifungo kuliko haya anayo niitia. Na usipo niondoshea vitimbi vya wanawake mimi nitamili kwao, na nitakuwa katika wajinga.” (Yusuf, 33). Kwa kuongezea ni kwamba Yusuf aliomba kinga ya Mwenyezi Mungu dhidi ya vitimbi vya mwanamke kwa kusema, “Ee Mola Mlezi wangu! Nastahabu kifungo kuliko haya anayo niitia. Na usipo niondoshea vitimbi vya wanawake mimi nitamili kwao, na nitakuwa katika wajinga.” (Yusuf, 33). Kuchagua kwake gereza juu ya kukubaliana na matakwa ya Zulaykha kunadhirisha uzito wa hofu ya Yusuf – rehema na amani ziwe juu yake – juu ya Mwenyezi Mungu.

Kutokana na kisa hiki tunaweza kuhitimisha kwa kusema kwamba njia pekee aliyonayo mwanadamu ya ukinzani wa ndani dhidi ya aina







zote za matamaniao ya dunia ni moyo. Moyo pekee ndio unaoweza kuamua kukataa vishawishi vya dunia na kutafuta ulinzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Qur'an tukufu inasema kwamba silaha madhubuti ya kumlinda muumini dhidi ya janga linalotokana na nafsi yenye kuamrisha maovu ni kujipamba na hofu juu Mwenyezi Mungu. Katika suala hili tukio lingine ndani ya Qur'an linaloangaza kwenye uhalisia wa nafsi linapatikana katika kisa cha nabii Musa – rehema na amani ziwe juu yake.

Musa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokea jukumu la utume katika mlima Sinai, mahali ambapo aliambiwa, “Na tupa chini fimbo yako. Basi alipo iona ikitikisika kama nyoka, akarudi nyuma wala hakutazama. (Akaambiwa): Ewe Musa! Njoo mbele wala usiogope. Hakika wewe ni miongoni mwa walio salimika.” (al-Qasas, 31). Mwenyezi Mungu Mtukufu alimuonyesha Musa – rehema na amani ziwe juu yake – ishara za nguvu zake zisizo na kikomo kwa kupitia kwenye fimbo. Baada ya pale Musa – rehema na amani ziwe juu yake – alitambua nguvu za Mwenyezi Mungu kwa kupitia kile alichokiona.

Mwenyezi Mungu Mtukufu alimchagua Musa – rehema na amani ziwe juu yake – kuwa Mtume na kumfanya awe karibu Naye ili aongee naye. Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa Musa – rehema na amani ziwe juu yake – majukumu kadhaa na kumwambia, “Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa?” (Taha, 17). Musa – rehema na amani ziwe juu yake – akajibu, “Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine.” (Taha, 18). Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akamwambia, “Itupe, ewe Musa!” (Taha, 19). Musa – rehema na amani ziwe juu yake – akatii kile alichambiwa na Mwenyezi Mungu na “Akaitupa. Mara ikawa nyoka anaye kwenda mbio.” (Taha, 20). Pindi alipoona tukio hili la kimiujiza Musa – rehema na amani ziwe juu yake – aliogopa na kuanza kukimbia, lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu akamwambia, “Ikamate, wala usiogope! Tutairudisha hali yake ya kwanza.” (Taha, 21).

Nafsi na vitu vinavyolingana nayo vilijidhihirisha mbele ya macho ya Musa – rehema na amani ziwe juu yake – katika hali ya nyoka mwenye kutisha. Pale Musa – rehema na amani ziwe juu yake – akaona asili





ya nafsi jambo ambalo lilimpelekea kutandwa na hofu. Katika lugha ya kiistiari Musa – rehema na amani ziwe juu yake – alipata uhakika ufua-tao: “Musa, nyoka huyu anawakilisha kushikamana na mambo ya dunia yenye kupita wakati Mwenyezi Mungu ndiye wa kushikamana naye. Pindi kushikamana na dunia kunapomkamata mtu kisawa sawa na mtu huyo akaona uhalisia wake, atakimbia kwa hofu. Kwa sasa ambapo umepewa ufahamu wa *tawhid*, yani upweke wa Mola wako, inaweze-kanaje uitegemee fimbo hiyo kwa kuegemea na kutimiza mahitaji yako mengine? Huu ni udhihirisho wa kushikamana na *tawhid* kisawa sawa. Hatua ya kwanza ya *tawhid* ni kuweka kila kitu pembeni na kukumbatia imani thabiti juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwake ndipo unapostahiki kujisalimisha. Ni bora uachane na matamano mengine yote na uamue kumtii Mwenyezi Mungu kikamilifu”.

Pia sufi wanasema, “Wale ambao wamesikia mwito wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuona nuru ya uzuri wake hawana budi kuachana na vitegemezi vingine kinyume na Yeye. Wakiwa ndani ya rehema za Mwenyezi Mungu wataweza kujinusu na hila za nafsi”.

Nafsi yenye kuamrisha maovu ndiyo inayomfanya mtu ahisi tofauti kuelekea kwenye furaha ya kweli na raha za milele, kwa kuweka mbele ya macho yake raha za uongo na zenye kupita. Nafsi yenye kuamrisha maovu humpelekea mtu kudhoofisha lengo lake la asili na kumfanya aanguke chini kutoka madaraja ya juu ya pepo mpaka kwenye mashimo ya chini ya Moto.

Mtu aliyetawaliwa na nafsi yenye kuamrisha maovu ni mkaidi na mwenye kujiona, hata pale anapokutana na njia zitakazoweza kumpeleka kwenye furaha na uongofu wake. Njiani hufurahia kuwadharau watu wanaomzunguka, kudanganya, kusengenya na kujishughulisha na vitu rahisi na vya kipuuzi. Hawezi kujilinda dhidi ya uchafu. Idadi ya watu waliotawaliwa na nafsi hii ya hatari ni kubwa mno. Wanafanya mambo yao kwa ujinga na kupuuzia huku wakipendelea ladha za dunia hii zenye kupita na kuacha raha za milele za peponi na furaha isiyo na kifani ya kushuhudia uzuri wa Mola kesho akhera.

Pindi mtu anapotawaliwa na nafsi yenye kuamrisha maovu roho ya kimantiki inakuwa imetawaliwa na roho ya kinyama; na sifa za kibinadamu hupotea na kutoa nafasi kwa ajili ya sifa za kinyama. Qur’an tukufu





inasema yafuatayo kuhusiana na haya, “Na tumeiambia Jahannamu majini wengi na watu. Wana nyoyo, lakini hawafahamu kwazo. Na wana macho, lakini hawaoni kwayo. Na wana masikio, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama nyama howa, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walio ghafilika.” (al-Araf, 179).

Pia watu waliotawaliwa na nafsi yenye kuamrisha maovu hujidanganya kuhusiana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Huendelea kufanya maovu huku wakitumaini kuwa Mwenyezi Mungu atawaonea huruma na kuwasamehe licha ya yale wanayoyafanya. Kwa namna wanavyojiona wako salama dhidi ya ghadhabu za Mwenyezi Mungu Mtukufu husema yafuatayo kwa kejeli, “Hatutakuwa pamoja na makafiri, labda tuhalalishe vilivyoharamishwa. Hivyo hakuna haja ya kukimbilia kutubu; hata hivyo siku moja tutafanya hivyo”. Katika kuzungumzia hisia hizi potofu za kunusurika Qur’an inasema, “Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi, na iogopeni siku ambayo mzazi hatamfaa mwana, wala mwana hatamfaa mzazi kwa lolote. Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala asikudanganyeni na Mwenyezi Mungu mdanganyifu.” (Luqman, 33).

Muumini hana budi kutambua ukweli kwamba Mola wake mwenye nguvu anajua kila kitu na pia kufikiria juu ya maswali atakayoulizwa ndani ya kaburi na siku ya kiama, na mahangaiko na magumu ya ndani ya Moto. Hana budi kutubia mara moja na kuchukua hatua ya kujisahihisha. Lakini toba hii haina budi kuwa ya umakini na ifanywe kwa moyo safi. Uwepo wake wote, ulimi na moyo wake vinapaswa kushiriki katika tukio hili. Kinyume chake kutubia kwa ulimi pekee hakutaleta manufaa yanayotarajiwa; hii ni toba mnafiki ambayo yenyewe inahitaji kutubiwa zaidi. Majuto ya mtu ambaye atatubia kwa nje wakati anaendelea kufanya maovu yatakuwa makubwa mno. Huku ni kutoheshimu mamlaka kubwa aliyonayo Yule ambaye toba zote zinaelekezwa kwake. Toba ya kweli ni kuhisi majuto makubwa kuhusiana na makosa yako na kuomba msamaha wa Mwenyezi Mungu kwa moyo wako wote.

Kwa upande mwingine ili mja ajiweke mbali na uthibiti wa nafsi yenye kuamrisha maovu, hana budi kuzitazama kwa umakini kanuni za Shariah na kuelewa asili ya tamko la upweke wa Mwenyezi Mungu (*kalimatu’tl-tawhid i.e. la ilaha illa Mwenyezi Mungu*). Pindi mja ataka-





posema ‘*la ilaha*’, hana budi kufuta moyoni mwake kila kitu kinyume na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hasa matamano ya kimwili hayana budi kufutwa ndani ya moyo kwani humuweka mja mbali na Mola wake. Pindi vitu hivi vitakapofutwa ndani ya moyo mja atakuwa tayari kutambua uhalisia wa ‘*illa Mwenyezi Mungu*’. Kwa njia hii mja atatambua udhaifu na utupu wake na hivyo atafanya jitihada za makusudi ili kuboresha hali yake ya kidini kutoka kwenye kufuata mkumbo mpaka kwenye utambuzi wa kweli. Baada ya hapo imani yake huongezeka zaidi na zaidi ndani ya moyo wake na kumpelekea kutekeleza amali njema zaidi na kufikia daraja za juu za kiroho.

#### **b. Nafsi yenye kujilaumu (*an-nafsu’l-lawwama*)**

Wale ambao wanazihesabu nafsi zao zenye kuamrisha maovu kwa majuto na kujitahidi kuzinusuru dhidi ya sifa zake hasi na za uovu, watakuwa wamepiga hatua kiroho na kufikia kwenye nafsi yenye kujilaumu. Watu kama hao hawajidanganyi kwa kujiweka mbali na rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu zisizo na kikomo, jambo ambalo nafsi yenye kuamrisha maovu ndilo inalofanya ili kumuweka mja mbali na uwezekano wa kubadilika. Watu hawa hujilaumu kutokana na makosa yao na kuomba msamaha wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutubu. Tunaweza kutaja wa aina mbili zifuatazo za watu walio katika kundi hili. Aina ya kwanza ni ya watu ambao wana elimu na ambao hawishi kulingana na elimu yao na hivyo hushindwa kuifanyia kazi elimu yao ya kinadharia. Lakini huwa wanatambua kasoro zao na huhisi majuto ya hali ya juu. Aina ya pili ni ya wale wanaotoa machozi wakati kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha katika mikusanyiko ya watu; lakini pindi wanapoondoka kwenye mikusanyiko hii hurejea kufanya makosa yale yale kama mwanzoni.

Neno la kiarabu “*lawm*” linamaanisha “kulaumu” au “kusuta”. Hivyo maneno *an-nafsu’l-lawwama* yanamaanisha nafsi ambayo hujilaumu na kujisuta kutokana na makosa na kasoro zake. Nafsi ya aina hii inafahamu kwamba haifuati maelekezo ya Mwenyezi Mungu kwa umakini ndio maana inajilaumu kwa majuto makubwa. Mtu ambaye nafsi yenye kujilaumu huwa anatubia na kujilinda dhidi ya baadhi ya maasi yanayopatikana katika nafsi yenye kuamrisha maovu. Haya yanamaanisha kwamba kupuuzia kwake na tamaa yake ya kufanya maovu





huwa ni ndogo ukilinganisha na nafsi yenye kuamrisha maovu. Lakini kwa kuwa daraja lake la ukomavu wa kiroho linakuwa halijakamilika basi ataendelea kukabiliwa na madhambi.

Katika hali ya nafsi yenye kujilaumu huwa roho ya kimantiki inakuwa haijatekwa moja kwa moja na roho ya kinyama. Kila wakati mtu anapotenda maasi hugubikwa na majuto. Pindi anapojilaumu humuomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu. Lakini anakuwa hawezi kujiweka katika mahala salama na imara kutokana na toba yake, kwani anakuwa bado hajaidhibiti nafsi yake. Ingawa utambuzi wake unapinga maovu lakini hawezi kujilinda moja kwa moja dhidi ya kuyafanya kwa kuwa yupo wazi kupokea ushawishi mabaya kama ule wa makundi.

Kwa ujumla mtu mwenye nafsi yenye kujilaumu huwa anafurahia amali zake njema na kuchukua amali zake mbaya. Hujitahidi kujilinda dhidi ya matamanio ya kimwili na kuweka ukinzani. Anakuwa ameegemea zaidi kwenye toba. Moyo wake huwa umeangaziwa na mwale mdogo wa nuru ya kiroho na akili yake huwa imeamka kwa kiasi fulani dhidi ya kupuuzia mambo. Huwa na msukumo mkubwa katika kutekeleza maamrisha ya Mwenyezi Mungu na kufanya amali njema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Lakini kwa kuwa bado hana nafasi ya kupokea amani na utulivu unaotokana na ufunuo mtakatifu, pia anakuwa amebeba tamaa ya kutaka amali zake zionekane kwa watu. Hili linamaanisha kwamba nafsi yenye kuamrisha maovu kwa kiasi fulani inafanya kazi; ingawa pia baada ya hapo mja hujilaumu kutokana na udhaifu wake.

Qur'an tukufu inaelezea hatua hii ya roho ya mwanadamu kwa kuiapia kama ifuatavyo:

وَلَا أُقْسِمُ بِالنَّفْسِ اللَّوَّامَةِ

“Na ninaapa kwa nafsi inayo jilaumu!” (al-Qiyamah, 2). Nukta hii ndogo inahitaji msisitizo. Kujilaumu si maongezi matupu au matendo matupu; kwani matokeo yake hayawi ya kweli. Kuna mstari mwembamba kati ya “nafsi yenye kuamrisha maovu” na “nafsi yenye kujilaumu”. Kama mtu atahisi kujisifu kutokana na kufanya matendo yanayoashiria ana nafsi





yenye kujilaumu, hili linamaanisha kuwa bado yupo chini ya udhibiti wa nafsi yenye kuamrisha maovu. Qur'an tukufu inalielezea hili katika aya ifuatayo:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ وَ نَعَلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِ نَفْسُهُ

“Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.” (Kaf, 16). Kwa hiyo mja hana budi kuwa macho dhidi ya miito ya siri na ulaghai unaotokana na nafsi yenye kuamrisha maovu na kuchukua hatua za kujilinda dhidi ya hisia potofu za kuwa salama.

Hapa panahitajika kuzungumziwa suala jingile muhimu kuhusiana na nafsi yenye kujilaumu. Baadhi ya watu hujilaumu ili kuwavuta watu wengine wamsifu kutokana na unyenyekevu wake. Bila shaka huu ni unafiki wa wazi. Ni kwa kupitia mafunzo ya kiroho pekee ndipo mtu ataweza kusimama imara katika toba yake na kujiweka mbali na maasi. Mtu mwenye nafsi yenye kujilaumu ataweza kujilinda dhidi ya maovu pale tu atakapokuwa chini ya uangalizi wa kiroho na mazingira ya kiroho. Ingawa akiwa chini ya mazingira ya kawaida anaweza kujizuia kurejea makosa yake yaliyopita lakini baadhi ya tabia mbaya kama vile chuki, husda na kujiona vitabakia ndani ya moyo wake; na haya yatampelekea kuwa katika hatari kubwa ya kuangukia kwenye madhambi.

Akiwa chini ya uangalizi huu wa kiroho mja ataweza kusonga mbele kutoka kwenye nafsi yenye kujilaumu mpaka kwenye nafsi iliyopokea ufunuo (*an-nafsu'l-mulhama*), haya ni kwa kupitia *rabitah* ambayo ni mbinu muhimu katika mafunzo ya kiroho. Hapa mtu wakati wote hukumbuka ahadi yake kwa Mola wake ya kujiweka mbali na vitu vya haramu na kutekeleza maamrisha ya dini. Ahadi hii humfanya ahisi uwepo wa Mola wake wakati wote, jambo ambalo huwa kama njia ya kumfanya kuwa makini katika matendo yake. Huku akiwa anaihesabu nafsi yake mara kwa mara itampelekea kubakia katika hali yake ya mabadiliko na kuachana na tabia zake mbaya na kumfanya awe mtu wa toba. Pia hana budi kuzibadilisha tabia zake mbaya na kuziweka zilizo nzuri; kwa mfano hana budi kubadilisha tabia yake ya kujiona na husda kwa kuwa na unyenyekevu na urafiki usio na husda. Hana budi kujiepusha na kuchunguza makosa





ya rafiki zake na badala yake ajishughulisha na kasoro zake binafsi. Hana budi kukumbuka kuwa muumini ni kioo kwa muumini mwenzake; hivyo kama atamuangalia kwa jicho baya bila shaka hataona chochote bali ubaya. Lakini pindi atakamuangalia kwa jicho jema basi hataona chochote ila mazuri yake.

Pia kumkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wote na kujiweka mbali na maovu ni jambo muhimu katika suala hili, haya yatapelekea kuuangazia moyo kwa nuru ya mapenzi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

### **c. Nafsi iliyopokea ufunuo (*an-nafsu'l-mulhama*)**

Kwa kuvuka kutoka kwenye nafsi yenye kuamrisha maovu na nafsi yenye kujilaumu mtu hufikia kwenye nafsi iliyopokea ufunuo, haya huwezekana kwa kupitia toba, kumuomba Mwenyezi Mungu msamaha, kujiweka mbali na madhambi na kutekeleza mambo yaliyolazimishwa kwetu. Katika ngazi ya nafsi iliyopokea ufunuo mja hupata uwezo wa kutofautisha kwa usahihi kati ya mema na maovu, jambo ambalo bila shaka lhumpelekea kushukuru kutokana na rehema za Mola. Pia mja huwa na ukinzani mkubwa dhidi ya matamanio ya kimwili ya nafsi yake. Huondoa kila kitu ambacho humuweka mbali na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Huwa hajali sana ni vipi anaonekana mbele ya macho ya watu; anachojali zaidi ni namna gani anaonekana mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Uhalisia wa imani hukita moyoni mwake na kubakia humo. Chimbuko la nafsi ya aina hii linapatikana ndani ya Qur'an: "Na kwa nafsi na kwa aliye itengeneza! Kisha akaifahamisha uovu wake na wema wake" (as-Shams, 7-8).

Nafsi iliyopokea ufunuo hupokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mtu aliyejaaliwa nafasi hii ya kiroho huanza kufahamu na kuzoea rehema za Mwenyezi Mungu na utambuzi uliomulikwa ndani ya moyo wake. Jambo hili huwezekana kwa kupitia moyo safi na kutekeleza maamrisha ya Mwenyezi Mungu wakati wote. Nafsi iliyopokea ufunuo hugeukia kwenye upendo na ulimwengu wa kiroho, jambo ambalo humpatia ubora unaohitajika ili kuweza kupokea ufunuo mtakatifu. Lakini bado hana budi kuhakikisha kuwa ufunuo huu unatoka kwa Mwenyezi Mungu na si kutoka kwa Shetani. Na ili kulitofautisha hili anahitajika uthibitisho kutoka kwa kiongozi wa kiroho kwa





sababu ingawa katika hali hii nafsi haina nguvu lakini bado inakuwa imebakiwa na kiasi kidogo cha nguvu hatari yenye kuweza kuiangu-sha nafsi iliyopokea ufunuo kutokana na hila na ushawishi wake. Kwa sababu hii nafsi iliyopokea ufunuo sio kituo cha mwisho cha kiroho na sifa za ndani zilizopatikana mpaka hapa bado hazina budi kuboreshwa.

Katika hali ya nafsi iliyopokea ufunuo ingawa ni kana kwamba haina tabia za uovu lakini bado ipo katika hatari ya kushambuliwa. Nafsi iliyopokea ufunuo bado haiwezi kuingia kwenye ulimwengu wa uhalisia kwani mtu anakuwa bado hajaufungua akili yake kutoka kwenye tabia za zinazohusiana na dunia hii. Kwa sababu hii anakuwa hayuko huru moja kwa moja dhidi ya mashaka, ghamu, mbano wa ndani, uongo na tamaa. Huwa amani na furaha ya kujisalimisha mwenyewe kwa Mwenyezi Mungu inakuwa bado haipo kwa ajili yake. Bado huwa moyo wake unashughulishwa na uhai na kusumbuliwa na tamaa ya makuu. Licha ya kuwa leo ana mkate wa kula mkononi lakini bado ana wasiwasi juu ya nini atakula kesho. Kukubali kwake kwa nje juu ya sifa tukufu ya “Mwenye kuruzuku” (*Razzaq*) huwa kunakuwa kunakinzana na wasiwasi wake wa ndani. Ukinzani huo huashiria kwamba ubora na ukomavu wa kuridhika kwake na mgao wa Mwenyezi Mungu, kujisalimisha kwake na kuamini kwake katika udhibiti wa Mwenyezi Mungu vinakuwa havijafikia kwenye ukamilifu. Hivyo huwa anakuwa katika hitajio la marekebisho zaidi ya ndani ili kusahihisha kiroho migongano hii.

Nafsi iliyopokea ufunuo hupatikana kwa kupitia hatua fulani ya mafunzo ya nafsi, hasa hasa kwa kuachana na vitu vinavyoivutia nafsi na kutekeleza vitu ambavyo haviivutii nafsi. Hata kama roho ya unyama itadhibitiwa kiasi gani katika nafasi hii lakini bado roho ya kimantiki itakuwa haijajipamba kwa sifa bora za kimaadili kikamilifu. Sifa hizi hazipatikani kwa kuacha vitu ambavyo vinaivutia nafsi na kufanya mambo ambayo yanaichukiza nafsi peke yake. Kwa maneno mengine ni kwamba sifa hizi hazitegemei uvumilivu na maadili mema pekee. Licha ya hayo yote inahitaji zoezi la kumkumbuka Mwenyezi Mungu (*dhikrullah*). Lakini hapa kuna jambo lingine la msingi ambalo hatuna budi kulitambua. Hali ya kuwa moyo umetekwa na mambo ya kidunia na tamaa ya makuu, haitaweza kufikia kwenye raha ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kufurahia utulivu wa kiroho wa hali ya juu. Hivyo







ili kuuweka moyo mbali na uchafu wote huu na kutambua uhalisia wa utajo mtakatifu ndani ya moyo wake katika njia sahihi, mtu huwa ana-hitaji kuwa na kiongozi wa kiroho aliyefuzu katika hayo.

Pindi mja atakapoanza kuhisi raha ya hali ya juu wakati wa kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu, atakuwa yuko katika njia ya kweli ya kumfikisha kwenye raha halisi. Hapo ufunuo mtakatifu hupata njia ya kupita na kufikia kwenye moyo wake na kumfanya azifahamu siri za viumbe vyote, na kumuacha katika hali ya kustaajabu na kutosheka. Hapa ndipo atakapoanza kuifahamu maana halisi ya aya ya Qur'an isemayo:

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحِكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ

“Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoaka.” (an-Nahl, 125). Baada ya kupata mazingatio kutokana na aya hii ya Qur'an kila neno atakalolitamka litakuwa katika namna ya hekima; kwani sasa amekuwa mja wa kipekee ambaye anapokea ufunuo mtakatifu. Katika hali hii ya kiroho roho ya unyama huanza kuelekea yenyewe kwenye roho ya kimantiki, mahali ambapo mtu huokolewa kutokana na kuchafuliwa na matamania ya nafsi. Tabia tukufu za mwanadamu za uvumilivu, subira na ustahamilivu hujidhirisha; na staha, kutosheka na ukarimu huanza kujitokeza na kutawala tabia zake.

Vyovyote itakavyokuwa, nafsi inayopokea ufunuo hubeba kitu ambacho ni cha hatari mno. Mtu atakapojidanganya kwa kuona kuwa katika hatua hii amefikia ukamilifu na amekamilisha mchakato wake wa kujitakasa, ataweza kurejea kwenye kupuuzia mambo na kujiona. Kwa sababu hii mja hana budi kutambua kuwa wakati wote yupo chini ya uangalizi mtukufu na hivyo adhibiti akili yake kulingana na uhalisia huu. Wakati huo huo hana budi kutafakari katika kifo jambo ambalo ni maarufu kwa usufi likilenga kuleta uelewa wa kweli juu ya muda mfupi uliopo katika kila kitu hapa duniani. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema, “Jikumbusheni mauti mara kwa mara; kwani kuweka mauti kichani kutamtakasa mtu dhidi ya madhambi na kumfanya ajihisi hayuko tofauti katika dunia hii. Kama utakumbuka





mauti wakati ukiwa tajiri, kitaondosha mambo mabaya katika utajiri wako. Kama utakumbuka mauti wakati ukiwa masikini, kitakufanya ufurahie hali uliyonayo kwa wakati huo” (Suyuti, Jamiu’s - Saghir, 1, 47).

Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anatoa ushauri kama huu pale aliposema, “Zihesabuni nafsi zenu kabla hamjahesabiwa. Zipimeni amali zenu kabla hazijapimwa katika mizani ya siku ya kياما. Jiandaeni kwa ajili ya siku ya kياما kabla hamjapelekwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye kwake hakuna amali yenu yoyote itakayofichwa” (Ibn Kathir, Tafsir, 1, 27).

#### **d. Nafsi tulivu** (*an-nafsu’l-mutmainna*)

Nafsi tulivu ni aina ya nafsi ambayo imeokolewa kutoka kwenye mateso ya ndani. Usalama huu wa kiroho umetokana na kutekeleza maamrisha matakatifu na kuacha makatazo kwa umakini mkubwa. Hivyo nafsi hii inakuwa imefikia imani ya kweli na yenye kudumu, imani ambayo hupelekea kuwa na furaha halisi, amani na utulivu. Kwa kupitia utajo wa Mola wa mara kwa mara moyo unakuwa umetakaswa dhidi ya mashaka na kasoro; hapo unakuwa katika hisia za kumshukuru na kumtukuza Mola.

Mja mwenye nafsi tulivu anakuwa amebadilisha kwa usahihi maadili yake mabaya na kuwa na sifa za maadili mema, haya yatakuwa ni zao la kufuata mwenendo wa kuigwa wa Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake. Moyo wake unakuwa umejaa subira, kutosheka na imani juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nafsi tulivu huwa ni ya watu wachamungu, watu ambao wana ufahamu juu ya

Mwenyezi Mungu Mtukufu. Nyoyo zao huwa zinamkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wote. Pia wanakuwa wamepata utambuzi mkubwa juu ya maana za ndani za maelekezo ya dini.

Katika kuielezea nafsi tulivu Sheikh Ahmad Sirhindi (aliyefariki mwaka 1624) anasema, “Mpaka hatua ya nafsi tulivu matendo ya ibada yanakuwa yanatekelezwa kwa njia ya kuiga (*taqlid*). Lakini baada ya hapo kuiga kunabadilishwa na kuwa uhakika (*tahqiq*)”.

Kabla ya kufikia hatua hii ya uyakini mja hana budi kujipamba





na 'hali ya *haqiqah*', au 'uhakika.' Nafsi tulivu ni hatua ya juu kabisa katika ukomavu wa kiroho; pia ni zawadi yenye kuvutia lakini wakati huo huo ni jukumu kubwa. Katika kulinganisha haya ni kwamba wale ambao uwezo wao wa kimantiki haujakomaa hawawezi kuwajibika kwa kutotekeleza majukumu ya kidini, kwani uwajibikaji unategemeana na kuwa na uwezo wa kiakili. Katika maana sawa na hii ni kwamba mfuasi mgeni katika usufi huchukuliwa kama mtoto mdogo asiye na hatia kulingana na majukumu makubwa ya usufi. Wakati bado hajafikia kwenye hatua fulani ya mafunzo yake ya kiroho makosa yake huweza kuvumiliwa; kwani katika usufi ukomavu wa kiroho hupatikana kadiri siku zinavyosogea. Lakini baada ya kupata kiasi fulani cha mafunzo atachukuliwa kuwa anawajibika kwa vitu ambavyo si majukumu ya ya kutekelezwa na muumini wa kawaida, kama ilivyo *Shariah* kuhusiana na mtoto. Kabla ya kuingia kwenye mlango wa nafsi tulivu mfuasi hatakuwa ni mwenye kuwajibika kwa vitu ambavyo vinachuliwa kuwa makosa katika mtazamo wa *haqiqah*. Jukumu hili huanza pale tu mfuasi atakapofikia kwenye nafsi tulivu, kwani hapa ndipo anapofikia kwenye ukomavu wa *haqiqah*.

Kwa kufuata mfumo huu huu kuna vitu ambavyo vinachukuliwa kuwa vinaruhusiwa na *Shariah*, lakini vikawa vinaonekana ni makosa madogo kwa upande wa *tariqah*. Pia kuna vitu ambavyo vinachuliwa kuwa ni makosa madogo kwa upande wa *tariqah*, lakini vikachuliwa kuwa ni makosa makubwa kwa upande wa *haqiqah* na *marifah*. Kwa mfano kulingana na *Shariah* kuendelea kula baada ya kushiba kunachukuliwa kuwa ni vibaya. Lakini kulingana na *tariqah*, hata kula kiasi cha kufikia kushiba kunachukuliwa kuwa vibaya. Kwa upande wa *haqiqah*, ikiwa hutambui uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hata kula kiasi cha kukuwezesha kuishi ni vibaya ikiwa hutambui uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kwa kumalizia ni kwamba kulingana na *marifah* kipande chochote cha chakula ambapo kitaliwa bila ya kushuhudia siri takatifu ndani yake basi kitakuwa hakifai, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu hudhihirisha dalili za kuwepo kwake katika kila kitu.

Kwa rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu nafsi tulivu imefikia





kwenye uhakika (*haqiqah*), amani (*sakinah*) na yakini (*yaqin*)<sup>7</sup>. Imelindwa dhidi ya tabu na matatizo ya dunia, na cha zaidi ni kwamba imepokea funuo kadhaa za kiroho.

Katika hali ya nafsi tulivu huwa mapazia ya kiburi na ujinga ndani ya moyo yanakuwa yamefunuliwa. Katika hatua ya *ayn al-yaqin* moyo hushuhudia uhalisia ulio nje ya mipaka. Kwa kuongezea ni kwamba moyo huwa salama dhidi ya mashaka na kasoro. Unakuwa umepata utulivu na amani kwa kupitia kwenye kujisalimisha kikamilifu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Mja aliye katika hali huwa anakaribisha majukumu ya kidini ya nje na ndani kwa moyo wake wote na hutekeleza matakwa yake kama inavyostahiki. Upokeaji wake na imani yake katika majukumu haya ni kubwa kiasi kwamba hata kama wanadamu wote watajaribu kupinga maamuzi yake, wangelishindwa kuingiza ndani ya moyo wake mashaka hata kidogo; kwani mja anakuwa ameshuhudia kwa macho siri za ndani kwa kupitia dirisha la uhalisia.

Kutokana na imani ya namna hiyo isiyoyumbishwa, hupelekea waumini kutohofia chochote. Hukabili matatizo na shida za aina yoyote. Mfano dhahiri juu ya hili unaweza kuonekana kwa Musa – amani iwe juu yake – pindi alipokutana na wachawi. Pindi wachawi walipogundua asili ya ushindi wa ajabu wa Musa – amani iwe juu yake – walilitambua hili kama miujiza aliyopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Baada ya pale waliingiwa na imani ya hali ya juu kwa kumuamini Mwenyezi Mungu na walikuwa na msimamo juu ya hilo licha hatari kubwa waliyotishiwa na Firauni. Alijaribu kuwatishia kuwa angelikata mikono yao na miguu yao kwa kupishana na kisha kuwasulubu, kama hawataki hayo basi waupe mgongo ujumbe wa Musa – amani iwe juu yake – wazi wazi. Majibu ya wachawi kwa Firauni yalikuwa kama ifua-

7 *Yaqin* ni neno la kiarabu lenye kumaanisha hakika. Hakuna nafasi ya shaka katika *yaqin*. Katika *yaqin* moyo unakuwa umetosheka kabisa kuhusiana na jambo Fulani. Pia *yaqin* inamaanisha kuvuka mipaka ya uhusiano wa sababu kwa athari na hivyo kuona uhalisia wa vitu wazi wazi kutokana na imani. Qushayri anasema kwamba *yaqin* ipo katika aina tatu:

*Ilm al-yaqin*: Uhakika unaotokana na masimulizi na mapokezi.

*Ayn al-yaqin*: Uhakika unaotokana na kushuhudia kwa macho.

*Haqq al-yaqin*: Uhakika unaotokana na hali ya kiroho ya mtu.





tavyo, “Wakasema: Sisi ni wenye kurejea kwa Mola wetu Mlezi. Nawe hukuudhika nasi ila kwa kuwa tumeziamini Ishara za Mola Mlezi wetu zilipo tujia. Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na utufishe hali ni Waislamu.” (al-Araf, 125-126).

Wachawi wale walikuwa zaidi ya kuweza na kuwa tayari kutoa uhai wao kwa ajili ya imani zao; kwani mapazia yaliyokuwa mbele ya muonekano wa vitu vyote vya kidunia yalikuwa yamenyanyuliwa na hivyo wakawa wanaviona vitu kwa uhalisia wake kwa kupitia nuru ya kiroho waliyokuwa wamepewa. Roho zao zilikuwa kama zile alizozitaja Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ifuatavyo:

يَا أَيُّهَا النَّفْسُ الْمُطْمَئِنَّةُ

“Ewe nafsi iliyo tua!” (al-Fajr, 27).

Kwa kuzingatia aya hii ya Qur’an tunaweza kuona kwamba hali za nafsi kabla ya nafsi tulivu hazipokei mahubiri matakatifu. Ni nafsi tulivu na zilizo juu yake pekee ndizo zilizopendelewa kuwa na sifa hii. Ili mja aweze kupata utukufu wa kupokea sifa hii hana budi kufanya jitihada kubwa ili kuitawala nafsi yake. Waja watukufu ambao wanafurahia hali hii ya nafsi tulivu huanza kusogea taratibu kuelekea kwenye hali za juu tatu katika mfulululizo huu; na zenyewe ni nafsi iliyoridhia (*an-nafsu’r-radhiya*), nafsi iliyoridhiwa (*an-nafsul-mardhiyya*) na nafsi kamilifu (*an-nafsu’l-kamila*). Kadiri mja anavyopata mafanikio zaidi katika mchakato huu ndivyo anavyokuwa karibu na Mola wake.

#### **e. Nafsi iliyoridhia (*an-nafsu’r-radhiya*)**

Hii ni nafsi ambayo imeendelea kuweka umakini wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu; na kutokana na kuendelea kujichukulia kuwa iko mbele ya uwepo mtakatifu wa Mwenyezi Mungu itakuwa imefikia daraja la juu zaidi la uchamungu. Hapa nafsi iliyoridhia inakuwa imetosheka na kuridhika na Mola wake. Si kwamba inakuwa imeweka pembeni uwezo wake bali inakuwa pia imeuporomosha kabisa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Katika maneno ya Qur’an inakuwa imerejea kwa Mola wake,





ارْجِعِي إِلَىٰ رَبِّكَ رَاضِيَةً مَّرْضِيَةً

“Rejea kwa Mola wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha” (al-Fajr, 28).

Hali ya kiroho ya ‘kuridhika’ inaashiria namna ambavyo mja anakabiliana na aina zote za magumu yatokayo kwa Mwenyezi Mungu kwa subira na ukarimu. Na hivi ndivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anavyotarajia kutoka kwake; yani kuridhika na chochote kitakachomkuta kutoka kwa Mwenyezi Mungu: “Hapana shaka tutakujaribuni kwa chembe ya khofu, na njaa, na upungufu wa mali na watu na matunda. Na wabashirie wanao subiri” (al-Baqarah, 155).

Subira, kwa maana yake halisi inahusiana na kukaribisha kila kitu ambacho kinatoka kwa Mwenyezi Mungu kwa kuridhika nacho, ikiwa ni kizuri au kibaya. Kwa hakika kila kitu kinatoka kwake pekee; vyote vinabeba dalili nyingi za siri Zake. Wale tu wenye uwezo wa kuzama kwenye uhalisia wa baraka na magumu ataweza kubeba sifa ya “subira” ambayo imetajwa kwenye aya hii. Wakati wote huwa wameridhika na kadari ya Mwenyezi Mungu na kamwe hawaonyeshi dalili hata kidogo ya utovu wa nidhamu au malalamiko. Kwao kila kitu, kiwe ni kizuri au kibaya wanakichukulia kuwa kimeshakadiriwa na Mwenyezi Mungu. Hii ni hatua ya kiroho ya wale walio na nafsi iliyoridhia.

Mitihani na magumu ambayo yanapitiwa na nafsi iliyoridhia ni magumu zaidi kuvumilia kuliko yale ya hali zilizotangulia; kwani kadiri nafsi inavyopanda daraja ndivyo njia yake inavyokuwa na vikwazo vingi zaidi. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anaelezea uzani huu kwa kusema, “Miongoni mwa wanadamu Mitume ndio wanaokabiliwa na changamoto kubwa ya mitihani...na baada yao wanafuatia wale walio karibu nao. Watu hupata mitihani kulingana na viwango vyao vya uchamungu” (Tirmidhi, Zuhd, 57).

Pale tu mtu atakapovishinda vikwazo vya nafsi ndipo atakapoweza kufikia daraja la ukomavu wa kiroho na kumuwezesha kukabiliana na mitihani kwa uvumilivu na kuridhika na Mola wake ambaye ndiye anayemletea mitihani hiyo. Malipo makubwa yatakayopatikana kutokana na ukomavu huu wa kiroho yatakuja baada ya mtu kuonyesha subira





na uvumilivu wa hali ya juu. Mbele ya macho ya muumini mwenye nafsi iliyoridhia kila kitu katika dunia hii kinastahili kutendewa usawa, bila kujali kama kinasababisha furaha au huzuni. Kwa kuwa moyo wake umejitenga na dunia, raha za dunia zenye kupita na maumivu yake yanakuwa katika hali moja. Kutokana na utambuzi wake mkubwa juu ya ukweli kwamba kila kitu kinatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi huridhika na kila kitu, kiwe ni kizuri au kibaya. Kama linavyosemeka shairi lifuatalo:

*Chochote kinachotoka Kwako ni sawa,  
Kiwe ni tumba la waridi au mwiba!  
Joho la heshima au sanda,  
Rehema Yako ni sawa na pia ghadhabu yako!*

Hata hivyo hatuna budi kufahamu kwamba utekelezaji wa kile kilichotajwa kwenye shairi hili kuhusiana na sifa za nafsi iliyoridhia ni mgumu mno. Ni pale tu mja atakapokuwa katika hali ya nafsi iliyoridhia ndipo atakaporuhusiwa kusema maneno ya ujasiri kiasi hicho. Katika nyakati zote zingine hana budi kufunga mdomo wake ili asiweze kusema vitu visivyofaa kwa wakati huo huku akiwa katika safari ya kiroho. Kinyume chake maneno hayo machanga yangelikuwa sawa na kutoa madai ambayo huwezi kuyathibitisha; na kama Mwenyezi Mungu Mtukufu angeliamua kupima ukweli wa maneno hayo kungelimpelekea mtu kuingia katika makosa.

Pindi mja anapokuwa katika hali ya kiroho ya nafsi iliyoridhia huanza kupata utambuzi juu ya siri takatifu. Huweza kutambua maana ya upweke mtakatifu na uhalisia wa kiroho huwa umefunguliwa mbele ya macho yake. Hupewa heshima ya kupokea siri za kipekee juu ya Majina na Sifa takatifu. Tabia yake huwa chemchem ya wema, uzuri na ukweli yenye kutiririka. Huwa mchungaji mzuri wa maamrishi matakatifu na makatazo. Hutekeleza matendo yote ya ibada kwa uzuri kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na hivyo kupelekea kutojihisi kuchoshwa hata kidogo kutokana na utekelezaji wake. Kwa mtazamo wa nje tunaweza kusema matendo ya ibada yanachosha. Lakini kwa mtazamo wa ndani huwa yanakuwa yamejaa malengo ya





kiroho ambayo hufuta muonekano wake wa kuchosha, hayo ni malengo ambayo humpitisha mja kwenye vituo vya kiroho na kumuwezesha kupata baraka za kufunguliwa mapazia ya kiroho. Lakini haya bado si malengo makuu. Lengo kuu ni Mwenyezi Mungu mwenyewe. Kwa mfano kama mja angelisahau ukweli huu na kutoa kipaumbele katika kupokea siri za kiroho, ingelimaanisha kuwa hazuui chochote isipokuwa mafanikio yake mwenyewe. Huku ni kukosa mpangilio ambako huishia kwenye kumchosha mja. Hivyo kuanzia mwanzo wa safari ya kiroho mpaka mwisho, mja hana budi kujiweka mbali na nia na malengo ya aina yoyote kinyume na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu yupo karibu yetu zaidi ya mishipa yetu ya fahamu. Jambo muhimu zaidi kwetu ni kutambua ukaribu huu na kujiandaa ili kuudhihirisha. Mwenyezi Mungu Mtukufu huwaridhia waja wake hali ya kuwa watakuwa wanajitahidi kubakia na msimamo katika njia Yake iliyonyooka na kutosheka na kile Anachowaruzuku.

#### **f. Nafsi iliyoridhiwa (*an-nafsul-mardhiyya*)**

Nafsi iliyoridhia ipo katika hitajio la ukamilifu zaidi wa kiroho. Ili nafsi iliyoridhia ipate manufaa yote ya siri zote takatifu zilizoangaziwa katika moyo wake haina budi wakati huo huo kutafuta kuwa 'mwenye kuridhiwa' na Mwenyezi Mungu pia. Kwa maneno mengine ni kwamba kumridhia Mola peke yake hakutoshi, kwani kunatarajiwa pia kuridhiwa na Mwenyezi Mungu. Maridhiano hayatakiwi kuwa ya upande mmoja, yanatakiwa kuwa ya pande zote. Ingawa sifa ya 'kuridhiwa' inaashiria kutoka kwa Mwenyezi Mungu lakini mja ndiye anayetarajiwa kufanya jitihada za kuwezesha kuwepo kwa maridhiano haya. Tofauti hii ndogo inafanya sifa hii apewe mja mwenyewe na hivyo nafsi yake. Kwa hiyo kunaweza kusemwa kuwa wakati nafsi iliyoridhia inaashiria hali ya kiroho ya wale walioridhika na Mola wao, lakini nafsi iliyoridhiwa inaashiria Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye Ndiye anayewaridhia watu hao.

Katika hali ya nafsi iliyoridhia sifa mbaya za kimaadili huwa zinakuwa zimetoweka na nafasi yake kuchukuliwa na sifa nzuri. Wale ambao wamefikia hali hii ya kiroho huwaangalia viumbe wote kwa mtazamo wa huba, huruma, upendo, ukarimu na msamaha. Kwa kuwa







viumbe vyote vinatokana na ustadi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hivyo pindi wanapoviangalia huona wema pekee. Mja ambaye yuko katika hali ya nafsi iliyoridhiwa hujihesabu mwenyewe katika njia sahihi zaidi na hutafakari juu yake. Katika kila pumzi anayovuta huwa yuko katika mazingatio juu ya uhalisia wa ndani wa uumbaji na hali ya nafsi yake mwenyewe, na hasa huwa na utambuzi mkubwa juu ya uovu wa nafsi.

Pia katika hali hii ya kiroho mja hujisalimisha moja kwa moja kwa Mola wake katika hali zote. Chochote kinachomuenda kutoka kwa Mola wake hukikaribisha kutokana na kufahamu kuwa hicho si kingine bali ni udhihirisho mtakatifu. Na mwishoni mwa uhai wake wa muda mfupi atajumuishwa miongoni mwa wale waliopewa bishara njema ya pepo na Mwenyezi Mungu Mtukufu kabla ya kukaribishwa kuingia ndani yake: “Rejea kwa Mola wako Mlezi umeridhika, na umemridhisha” (al-Fajr, 28). Kwa hakika,

رَضِيَ اللهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

“...Mwenyezi Mungu yu radhi nao, na wao waradhi naye...” (al-Bayyinah, 8). Mja ambaye amepata ukamilifu huo wa kiroho huona kila kitu kwa kupitia jicho la *haqq al-yaqin*; yani kwa kupitia elimu iliyoege-meza kwenye uzoefu binafsi wa kiroho. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu anaweza hata kupata siri kadhaa za ulimwengu usioonekana. Kutokana na nguvu yake kubwa ya kiroho Mwenyezi Mungu Mtukufu humsogeza karibu Yake kiasi cha kukaribia kuwa jicho lake analoonea, sikio lake analosikilizia, Ulimi anaotamkia. Baada ya hapo maneno na tabia ya mtu huyo huanza kuongeza ushawishi mkubwa kwa watu wanaomzunguka.

Udhihirisho wa kiroho ambao alikuwa ameushuhudia akiwa na ‘nafsi iliyoridhia’ kwa sasa unakuwa umechanganuliwa na kuingizwa ndani moyo na hivyo kuwa sehemu ya fikra zake. Kwa sasa subira yenye kuendelea na imani juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu inakuwa imetawala tabia zake.

Kwa kugeukia mifano ya kuigwa ya kimaadili ya mitume tunaweza kutoa mifano kadhaa kuhusiana na hali hii ya kiroho. Kwa mfano pale





Yaqub – amani iwe juu yake – alipokabiliwa na aina nyingi za tabu, lakini alisema “Lakini subira ni njema” (Yusuf, 18). Vivyo hivyo ilitokea kwa Ayyub – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye alipitia kipindi kizito cha kuumwa na kutaabika. Ingawa watu waliomzunguka walimsihi mno amuombe Mola wake amuondolee tabu ile, lakini Ayyub – amani iwe juu yake – hakufuata ushauri wao na akajibu, “Mola alinijaalia miaka themanini ya afya. Njia pekee itakayonifanya nijisikie vizuri ni kumuomba aniponye baada ya kuhangaika angalau kwa miaka themanini ya kuumwa”. Ibrahim – amani iwe juu yake – naye anatoa mfano mzuri juu ya hili. Pindi alipokaribia kurushwa kwenye moto mkubwa malaika walimuendea kwa ajili ya kumsaidia, lakini nabii Ibrahim – amani iwe juu yake – alikataa msaada wao kwa kusema, “Yule aliyeuwasha huu moto anajua hali yangu...kwa hiyo sihitaji chochote kutoka kwenu”.

Kulingana na mchanganuo wa sufi hatua za nafsi ya mwanadamu katika njia ya kiroho ya utakaso zimegawanyika katika aina hizi sita. Lakini baadhi ya wakuu wa kisufi huzungumzia kuhusiana na hatua ya nyongeza inayoitwa nafsi kamilifu (*an-nafsu'l-kamila*) au nafsi safi (*an-nafsu's-safiya*).

#### **g. Nafsi kamilifu (*an-nafsu'l-kamila*)/ nafsi safi (*an-nafsu's-safiya*)**

Nafsi kamilifu ni aina ya nafsi ambayo inakuwa imetakasika kwa kupitia kwenye mchakato wa kiroho. Hii ni nafsi safi, iliyokomaa na tukufu. Katika hali hii ya kiroho nafsi hupokea aina zote za siri za mbinguni. Hali hii ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake. Jitihada binafsi haziwezi kutoa uhakika wa kuipata nafsi kamilifu; hii ni sifa ya kiroho itokayo kwa Mwenyezi Mungu peke yake, ambayo ni siri ya qadari tukufu.

Kituo cha nafsi kamilifu kinaitwa “kituo cha uongofu”, kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu huwapatia wale waliofikia kwenye hatua hii jukumu la kuwaongoza watu wengine. Maneno yao na vitendo vyao huaminika katika kuharakisha usahihishaji wa kasoro na makosa ya wengine.





Pindi mtu mwenye nafsi timilifu anapokutana na mfanyaji maovu huelewa hali yake mara moja na kwa kupitia mwenendo wake wa kuigwa humfahamisha tiba itakayomuokoa dhidi ya maradhi yake ya moyo na ya kiroho. Baada ya kuhisi majuto kutokana na mwenendo wake, mkosaji huyu atafungua macho na kuachana na tabia yake ya kupuuzia mambo hali ya kuwa moyo wake haujapigwa muhuri au kufungwa kiasi cha kushindwa kupokea uhalisia wa kiroho.





**M**oyo ni sehemu ya mapambano kati ya wema na uovu, uchamungu na kufuru na ushetani na umalaika. Nyoyo hujigeuza na kupinda kwa kuegemea ama kwenye ushetani au umalaika na huku ukitetemeka kutokana na kudhihirikiwa na haki.



## B. MOYO NA UTAKASO WAKE

### 1. TABIA YA MOYO

Lengo la uislamu ni kumkuza mwanadamu ili kufikia uzuri na ukomavu, na kutambua kuwa yeye ni mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ili kulitambua lengo hili kiuhakika kunategemeana na kutambua ni ipi maana ya halisi ya kuwa mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kufikia anga za juu za ukomavu wa kiroho kutawezekana pale tu utakapohisi raha na hofu za hali ya juu ndani ya moyo.

Moyo ni kitovu chetu cha kiwiliwili na kiroho. Unachukua nafasi kubwa katika kukilea kiwiliwili. Sekunde nne tu za ucheleweshaji wa msukumo wa kiasi kinachohitajika cha damu safi kuelekea kwenye seli hupelekea kwenye mwisho wa uhai wake; na hivyo ndivyo ilivyo kwa mabilioni ya seli nyingine zilizojenga miili yetu.

Licha ya kutoa mchango mkubwa katika ukuaji wa kiwiliwili, pia moyo ni johari ya kiroho ambayo ndio kitovu cha nguvu na uwezo wa utambuzi wa kiroho. Kwa maana hii moyo ndio mfalme wa kiwiliwili, kimwili na kiroho kiasi kwamba hata ubongo ambao ndio kitovu cha akili.

Ndani ya Qur'an Mwenyezi Mungu Mtukufu ametutumia tahadhari sisi waja wake tusiruhusu nyoyo zetu zikatunyang'anya furaha yetu ya nje kwa kutudanganya na starehe za dunia zenye kupita: "Enyi watu! Hakika ahadi ya Mwenyezi Mungu ni ya kweli. Basi yasikudanganyeni maisha ya dunia, wala mdanganyifu asikudanganyeni juu ya Mwenyezi Mungu." (Fatir, 5).

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - anaelezea hitajio la mtu kukaza kamba za matamanio ya nafsi yake ili asije akatoka nje ya lengo kuu:





*“Msihangaike kuilisha miili yenu kupita kiasi na kuinawirisha, kwani itaishia kuwa chakula cha ardhi. Hangaikeni kuzilisha nyoyo zebu! Kwani hizo ndizo zinazotakiwa kupaa mpaka kwenye anga za juu kabisa na kupata heshima.*

*Ilisheni miili yenu kwa vyakula vyenye shahamu na sukari. Kwani wale wanaoilisha miili yao kupita kiasi huangukia kwenye mashimo ya mata-manio yao na hatimaye kuishia kwenye maangamizi.*

*Zilisheni nyoyo zenu kwa vyakula vya kiroho. Zipeni fikra komavu, uelewa mzuri na vyakula vingine vya kiroho ili ziweze kwenda zinakokusudiwa kwenda huku zikiwa na afya na nguvu tele.*

Vile vile Luqman (a.s) anamshauri mwanae apambane dhidi ya kupuu-zia mambo: “Mwanangu dunia ni bahari isiyo na kina ambayo imewaha-rikisha wengi katika mfoko wake wa nguvu, wakiwemo wanachuoni wasio na hekima na mfano wao. Jaalia kiunzi cha meli yako kiwe imani thabiti juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Jaalia zana zako ziwe uchamungu na ibada. Jaalia matanga ya meli yako ambayo yatakusaidia katika kupangua mawimbi yawe uaminifu kwa Mwenyezi Mungu. Ninatumaini kwa kutu-mia njia hizi utafanikiwa kuongoka” (Bayhaki, Kitab’uz - Zuhd, uk. 73).

Licha ya moyo kuwa kitovu cha mwili na roho lakini una umuhimu sawa kwa vyote viwili. Kwa kuwa roho haihusiani na muonekano wa nje kama ulivyo mwili wa mwanadamu, umuhimu wa kiroho unaopati-kana katika moyo ni mkubwa kuliko umuhimu wake wa kimwili katika vipengele vyake vyote. Kutokana na sifa yake hii bila ya kusahau siri na hekima kubwa ilizobeba, moyo ndio sababu ya pekee ya kumfanya mwanadamu aendane na maana na sifa ya ‘uanadamu’. Hii ndiyo hekima iliyopo katika suala kwamba imani hupatikana kwa kupitia uthibitisho wa moyo kabla ya kutamkwa kwa ulimi. Cha kuzingatia ni kwamba uthibitisho wa moyo unachukuliwa kuwa unatosha hata bila ya kukubalika katika fikra.

Kama ilivyo namna mwanadamu anavyochukuliwa kuwa kiini cha ulimwengu na kubeba desturi na uwezo wa kuendea mema na mabaya, utukufu na udhalili kutokana na silka yake ya asili, pia moyo ambao ndio kiini cha mwanadamu unakabiliwa na desturi na uwezo huu unaoto-fautiana. Kama ambavyo anaweza kuvutiwa na kuwa na sifa za malaika, pia mwanadamu yupo katika hatari kushawishiwa na shetani. Tunaweza kusema kuwa moyo ni sehemu ya mapambano kati ya wema na uovu,





uchamungu na kufuru, huvutiwa katika ushetani na umalaika. Nyoyo zitaendelea kuvutwa na nguvu za kishetani na kimalaika mpaka pumzi yake mwisho.

Kutokana na ukweli kwamba moyo unaweza kushawishiwa na sifa za kimalaika na kishetani: Ushawishi wa kimalaika huingiza ndani ya moyo hisia za kiroho kama vile imani, tabia njema, matendo mema, upendo na sifa za ibada. Na kwa upande wa ushawishi wa kishetani huingiza moyoni mambo mabaya kama vile kufuru (kufr), mashaka, uovu, uroho na tamaa. Shetani ataweza kufukuzwa ndani ya moyo kwa kupitia kumuabudu na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu (*dhikrullah*). Kutokana na kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu nyoyo zetu hupata amani, na kutokana na kuipata amani hiyo kwa kupitia *dhikr* basi imani hupanda zaidi na kupelekea moyo kuwa katika daraja la juu la kutosheka. Na hufikia kipindi ambacho moyo hufunguka ndani kwa ndani kama pazia na kudhihirisha maajabu ya mambo yanayoweza kufikirika (*nasut*) na mambo yasiyoweza kufikirika (*lahut*). Ulimwengu pamoja na maajabu yake hugeuka na kuwa kitabu kinachongojea kusomwa.

Kutokana na moyo kuwa sehemu ya mapambano kati ya desturi za kimalaika na kishetani lakini bado huwa na muundo hai na wenye msukumo ulio tayari kuingia kwenye hatua za ushindi na kujipamba na sifa zake. Moyu uko tofauti na viungo vingine katika kujisalimisha na kutii ridhaa. Silka yake ya asili kuelekea kwenye mema na maovu haiamshwi sana na ushawishi wa ndani zaidi na ilivyo kwa ushawishi wa nje. Kwa maneno mengine ni kwamba hisia haziamki kutokana na mawazo yanayokuja moyoni bila kutarajia (mawazo ambayo yanaitwa *sunuhat*) lakini hutokana na vigezo vya nje. Kwa maana hii moyo ni kama maji ambayo huchukua umbile na rangi ya chombo kilichowekea hayo maji. Watu wa kiroho huwa wanachagua desturi chanya ndani ya nyoyo zao, jambo ambalo huwapelekea kufikishwa kwenye mahala pa amani.

Qur'an tukufu inasema:

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.” (At- Tawba, 119).

“Na unapo waona wanao ziingilia Aya zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shet’ani akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhaalimu.” (Al- Anam, 68).





“Naye amekwisha kuteremshieni katika Kitabu hiki ya kwamba mnapo sikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakanushwa na zinafanyiwa kejeli, basi msikae pamoja nao, mpaka waingie katika mazungumzo mengine. Hivyo mtakuwa nanyi mfano wao hao. Hakika Mwenyezi Mungu atawakusanya wanaafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannamu” (An- Nisa, 140).

Dhamira huanza kufanya kazi tokea mwanzo ili kutambua na kucha-gua kati vishawishi vizuri na vibaya ambavyo vitakuwa na athari ndani ya moyo. Kutokana na kwenda kulingana na vishawishi vilivyo mbele yake, hapa moyo unakuwa kama propela la hali ya hewa lililowekwa juu ya dari. Kiuhalisia ni kwamba moyo huweza kubadili kitu na kuwa kinyume chake na kubadilika umbile na rangi yake, jambo ambalo linaimarisha sifa hii ya moyo iliyokwishatajwa, yani kiungo muhimu kwa mwanadamu. Had-ith ifuatayo inalithibitisha hili: “Moyo ni kama nyoya lililo juu ya ubapa mtupu, huku likiyumba kuelekea huku na kule kutokana na upepo una-ovuma”

Tukio lifuatalo linadhihirisha tabia ya moyo ya ‘kubadilika’:

*Siku moja Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ali-kutana na Handhwala – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na kumuuliza juu ya hali yake. Handhwala alijibu kwa huzuni, “Handhwala amekuwa mnaafiki!”.*

*“Subhanallah”, Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alijibu na kusema “Hilo linamaanisha nini?”*

*Handhwala – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alifafanua, “Pindi tunapokuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – huwa anatukumbusha kuhusu pepo na Moto na huwa tunaguswa sana kiasi kwamba tunaona pepo na Moto mbele ya macho yetu. Lakini pindi tunaporejea katika familia zetu na kutekwa na kutafuta riziki huwa tunapuuzia sehemu kubwa ya kile tulichokisikia”*

*“Kwa hakika wakati mwingine huwa nahisi Vivyo hivyo”, Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikiri. Baada ya hapo walienda kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kum-uelezea wasiwasi wao. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:*

*“Naapa kwa jina Mwenyezi Mungu ambaye uhai wangu uko kwenye*





*mikono yake mitakatifu, kama mngeliweza kubakia katika hali mliyokuwa nayo wakati mpo pamoja na Mtume na kuwa katika hali ya dhikr wakati wote, malaika wangeliwashika mikono yao wakati wamelala na wakati wanatembea". Kisha akarudia mara tatu:*

*"Handhwala, wakati mwingine huwa hivi, na wakati mwingine huwa vile!" (Muslim, Tawbah, 12).*

Kusonga mbele kwa maisha kunaenda sambamba na mja ambaye amejawa na shauku na msukumo wa ukweli na maajabu ya kesho akhera .

Hivyo ndivyo ambavyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anavyoangazia nuru katika *talwin* ya moyo, yani sifa yake ya kubadilika kutoka hali moja mpaka nyingine. Miongoni mwa malengo makuu ya *tasawwuf* ni kuibadilisha hii *talwin* na kuwa *tamkin* au uimara, kadiri iwezekanavyo kwa kupitia kwenye msukumo unaoletwa na *sohbah* (majadiliano ya kiislamu) na *dhikr*; yani kuuelekezea moyo kwenye uelekeo mtakatifu na kuuimarisha hapo hapo. Miongoni mwa maswahaba, Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anatoa mfano bora zaidi katika hali hii ya kiakili. Usadikishaji wake wa moyo usiotetereka kuhusiana na kuthibitisha ukweli wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kuhusiana na *Miraj* bila ya kusita hata kidogo, hakuwezi kuelezewa kwa namna nyingine kinyume na uimara wa moyo wake aliokuwa nao wakati ule.

Washirikina waliibuka katika dhoruba ya kupinga Miraj. Walitaka kupandikiza mbegu za mashaka katika nyoyo za waislamu na hivyo kuwapunguzia imani yao. Kama ambavyo walienda kwa maswahaba mbalimbali kwa ajili ya kuwaelezea mawazo yao juu ya Miraj pia walienda kwa Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na kumwambia: “Je umesikia habari mpya? Rafiki yako anasema kuwa amepanda mbinguni”, walisema kwa kejeli. “Unasemaje kuhusiana na hili?”.

Abu Bakr– radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye alikuwa mtu mwenye imani ya hali ya juu alitoa maneno ya uaminifu yenye kuvutia mno, maneno ambayo washirikina hawakudhania kwamba wangeluweza kuyasikia kutoka kwake. Maneno hayo yalizidia kuvuruga hali yao kutokuwa na matumaini: “Chochote anachokisema ni cha kweli kwani kamwe hajapa kusema uongo. Chochote anachokisema ninamuamini papo kwa hapo!” (ibn Hisham, as-Sirah, II, 31).







Kwa kawaida malaika wana silka ya kutenda mema peke yake; hivyo ndivyo walivyoubwa. Mashetani huwafanya kazi ya kuasi na kuwapoteza watu. Wanadamu wapo katikati ya viumbe hivi viwili. Ili kujiepusha na maasi wanadamu hawana budi kujizuia na kujiingiza katika mazingira ya uovu. Hili halimaanishi kwamba wanahitajika kufanya jambo lolote hata lililo nje ya uwezo wao ili waweze kufikia kwenye nafasi ya kimalaika. Kinachohitajika katika silka ya asili ni staha.

Jambo kubwa la kuzingatia na kutilia maanani kwa mwanadamu ni kifo ambacho hakiwezi kuzuilika na akhera. Hili litawezekana pale atakapofahamu uhalisia wa moyo, kuulinda dhidi ya maasi na kuingiza katika mambo ya kiroho. Usawa na amani katika dunia na uongofu kesho akhera vinategemeana na kuwa na moyo safi (*al-qalbu 's-salim*), moyo ambao upo katika njia ya utakaso ya uislamu, na ambao umeshikilia tabia zake nzuri zinazotokana na silka ya asili (*fitrah*). Kama ambavyo kumeashiriwa na mpendwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake -: “Kila mtoto huzaliwa katika *fitrah* (ya uislamu). Kisha wazazi wake humfanya kuwa mkristo, myahudi au mshirikina...” (Muslim, Qadar, 22), tokea mwanzo silka na umbile ya asili la moyo limeegemea kwenye uislamu. Pindi moyo utakapowekwa kwenye vishawishi vibaya ndipo utakapoharibu umbile lake la asili na kutoa uwezekano wa kuipoteza.

Kinyume chake moyo uliojazwa imani kwa kupitia kwenye kujiingiza kwenye anga ya kiroho, utazalisha maadili mema, matendo mema na kuongeza imani. Ni kwa kupitia njia hii pekee ndipo mtu ataweza kutambua siri ‘*ahsan-i taqwim*’<sup>8</sup> zilizopo kwenye silka yake, na hapo ndipo utambuzi wake juu ya viumbe na matukio yote yanayomzunguka yatakapopata kuzingatiwa kwa umakini wa hali ya juu. Hili linamaanisha kuwa mapazia yanakuwa yamefunuliwa kutoka kwenye ‘jicho la moyo’ na kuliwezesha kuona nje ya mipaka, kama ilivyogusiwa katika Qur’an<sup>9</sup>. Bila shaka maono haya yapo nje ya uhalisia wa maono ya kawaida ya kiwiliwili.

Wale ambao macho yao ya nyoyo yako wazi huwa na shauku ya kupata mafunzo ya kiroho na kuongeza utambuzi wao na jitihada katika kusonga mbele kwenye kuelekea kwenye ukweli. Lakini wale wasio na shauku

8. *Ahsan-i Taqwim*: Kuumbwa katika umbile lililo bora zaidi; maelezo ya Qur’an juu ya uumbaji wa mwanadamu.  
9 Rejea al-Hajj, 46



njema, wale wasio na shauku ya kufikia kwenye imani ya kweli hupuuzia ushauri wa Mitume na watakatifu. Kutokana na kiburi chao huingia kwenye uovu zaidi kutokana na kuzama kwao zaidi na zaidi kwenye madimbwi ya ujinga. Huwaonea huruma vipofu ambao hawawezi kuona njia bila ya msaada wa wengine, lakini wao wenyewe hawatambui hata kidogo upofu wao wa kiroho.

Kutokana na desturi ya kuelekea ama kwenye mema au maovu mwanadamu huwa na uwezo na nguvu ya kuchagua katika dunia hii yenye mitihani, dunia ambayo ndani yake hana budi kuchunga maamrishi na makatazo kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mistari ya uelekeo (*istiqamah*) ikiwa ni mema au mibaya iliyopo ndani ya moyo ndio inayoweza kumua ni namna gani uwezo na nguvu itaweza kusaidia katika kuchagua, ni jambo la wazi kwamba moyo ambao umeelemewa na vishawishi vya nje na desturi za nafsi hujisogeza muda baada ya muda kutoka kwenye lengo la kuumbwa na hivyo kuharibu akhera ya mtu.

Moyo zilizo sambamba na nafsi hujawa na ukafiri, uovu, tamaa na wasiwasi (*waswasah*). Nyoyo za aina hiyo huwa zimeenda kinyume na malengo ya uumbaji wake. Kutokana na kuhadaiwa na utukufu zimekuwa na msukumo mkubwa juu ya matamania ya nafsi. Huwa zinakanganyikiwa zaidi kuliko wanyama<sup>10</sup> mbele ya maneno ya Qur'an, huharibu uhai wake katika kiini macho cha ujinga. Nyoyo za namna hii zina maradhi, hivyo zinahitaji matibabu.





**T**ibia zetu huakisi hali za nyoyo zetu. Huwa tunafanya mambo yetu kilingana na kupwa na kutiririka kwake.



## 2. AINA ZA NYOYO

Kwa ujumla nyoyo zinaweza kugawanywa katika aina kuu tatu:

- a- Nyoyo ambazo zinafuata lengo na heshima ya kuumbwa kwake.
- b- Nyoyo zilizopigwa muhuri na kufa.
- c- Nyoyo zenye maradhi na zisizozingatia mambo.

### **a- Nyoyo ambazo zinafuata lengo na heshima ya kuumbwa kwake.**

Hizi ni nyoyo ambazo zimeamka kutoka kwenye ujinga kwa kupitia *dhikr*. Hapa imani ndio inakuwa inaitawala nafsi na moyo unakuwa umezingirwa na nuru ya imani. Watu waliojaaliwa kuwa na moyo wa aina hii wamekuwa makini katika kutekeleza kile walichoitiwa katika aya ifuatayo:

“Enyi mlio amini! Mdhukuruni Mwenyezi Mungu kwa wingi wa kumdhukuru.” (al-Ahzab, 41).

“Na lidhukuru jina la Mola wako Mlezi, na ujitolee kwake kwa ukamilifu.” (al-Muzzammil, 8).

“Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka.” (an-Nur, 37).

Katika nyoyo za watu wa namna hiyo, udhahirisho wa majina matakati-fu ya uzuri (*jamal*) hushinda ule wa yale ya ghadhabu (*jalal*). Watu walio na nyoyo za aina hii hupata ukomavu kwa kupitia kwenye kujipamba na maadili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na Qur’an tukufu. Hizi ni nyoyo ambazo zimeondoa desturi ya nafsi kwa kupitia kwenye rehema ya mapenzi yake juu ya Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake, hizi ni nyoyo ambazo kinyume na hawa hakuna





kingine chochote kilicho na umuhimu. Nyoyo za aina hii zimetajwa ndani ya Qur'an kama nyoyo zilizosalimika (*qalb salim*), nyoyo zenye kujuta (*qalb mutmain*) na nyoyo zilizotosheka (*qalb mutmain*). Nyoyo hizi zinaweza kufafanuliwa kama ifuatavyo kulingana na kukubalika kwake mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu:

Moyo uliosalimika (*qalb salim*) ni moyo uliolindwa au kuwekwa mbali na mashambulio ya nafsi. Huu ni moyo aliopewa mtu na Mola wake, pamoja na silka ya asili iliyo safi, kwa sharti kwamba avilinde vyote viwili. Moyo unaweza kufikia hatua hii ya usafi kwa kupitia kwenye mbinu za kisufi zijulikanazo kama utakaso wa roho na moyo. Hivyo mja hutuliwa mzigo mzito wa madhambi na kuingiziwa nuru ya imani. Kama ambavyo kikundi cha miale ambacho kinamulika kwenye lenzi kinavyojikusanya katika eneo moja na kuanzisha moto kwenye upande wa pili, ndivyo ambavyo imani iliyojikusanya kwenye moyo inayotokana na nuru takatifu inavyoweza kuunguza dhambi na matamano yote ya nafsi na kuwa majivu. Hii ndio dalili ya kuwa na moyo uliosalimika, moyo ambao ndio utakaokubalika mbele ya Mwenyezi Mungu. Qur'an inasema yafuatayo kuhusiana na hili: "Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi." (as-Shuara, 88-89).

Mshairi wa Baghdad aitwae Ruhi analizungumzia hili katika mistari ifuatayo:

*Mfanya biashara usifikirie kwamba utaombwa dhahabu au fedha kwa ajili ya dhamana,*

*Ni moyo uliosalimika pekee, siku ambayo hakuna kitu kingine chochote kitakachokusaidia...*

Moyo wenye kujuta (*qalb mutmain*) ni moyo ambao unamuelekea Mola wakati wote. Kutokana na kuwekwa huru kutoka kwenye kifungo cha vivutio vyenye kupita, hufurahia kuingia kwenye ardhi ya milele kwa upendo na shauku kubwa. Moyo huu hutetemeka kutokana na furaha ya kuhisi mtiririko wa nguvu takatifu. Aya ndani ya Qur'an inasema: "Haya ndiyo mnayo ahidiwa kwa kila mwenye kurejea kwa Mwenyezi Mungu na akajilinda. Mwenye kumwogopa Mwingi wa Rehema hali kuwa hamwoni, na akaja kwa moyo ulio elekea-" (Qaf, 32 - 33).





kuelekea kwenye kuyatakasa maadili yake chini ya kivuli cha amani cha imani. Matendo ya ibada hayaendelei kuwa ya kuiga (*taqlidi*); yanakuwa yametambulika katika kiini chake (*tahqiqi*) na kufanyiwa kazi kwa namna hii. Moyo unakuwa umetiwa nuru kwa kupitia *dhikr* na nafsi inakuwa imejisalimisha kwenye imani. Kito cha imani kinakuwa kimezama kwenye moyo ambao ndio kituo cha imani na kinakuwa hakiwezi kuondolewa. Kutokana na imani iliyozama kwenye moyo (iman-i tahqiqi) na kutosheka, hupelekea moyo kupata amani na uimara. Kwa sasa hali iliyotajwa ndani ya Qur'an katika aya ifuatayo inakuwa imetambulika kiukamilifu:

أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ

“Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!” (ar-Rad, 28) Maana ya ndani ya aya hii ni kwamba nyoyo zilizo mbali na uta jo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu zitaendelea kuumizwa na maumivu ya kutotosheka kwao na kuwa mbali na uwezekano wa kupata utulivu wa akili.

Alama za wale walio na moja ya aina hizi tatu za nyoyo zilizotajwa ni kwamba ni zenye huruma, upendo kwa viumbe wengine, kutosheka na kile walichojaaliwa na hutoa huduma katika njia ya haki na wema. Kutokana na shauku yao ya upendo mtakatifu wanaweza kuyakimbia maovu na kukimbilia kwenye uongofu wa wengine kiasi cha kutoa machozi kwa ajili ya wengine.

Rasilimali inayohitajika ili kuhakikisha kwamba moyo unafikia katika hali hii ni kwa kupitia swala sahihi na toba na kuzingatia kula *halal* peke yake, yani chakula cha halali. Kwa upande mwingine kutawezekana kuilinda rasilimali hii kwa kutekeleza matendo mema pekee. Kutokana na kuwa kwetu wanadamu inakuwa vigumu kujiepusha na madhambi moja kwa moja. Kwa kuwa madhambi yanapunguza umakini wa moyo na kuufanya usione wala kusikia haki, hivyo hatuna budi kushikamana na swala na toba ili nyoyo zetu ziwe kitovu cha mambo mema. Masomo ya tasawwuf hayaanzi kwa toba bila ya sababu ya msingi. Kama ambavyo imesemwa katika kanuni maarufu za *Majalla*: “Kuyaondoa madhara ni jambo la kipaumbele zaidi ya kupata faida”. Tunaweza kusema kujiepusha na maovu ni jambo la kulipa kipaumbele ukilinganisha na kupata wema.





Kuhusiana na kula *halal* sufi wamesema: “Mwenyezi Mungu huupa utambuzi moyo wa yule anayekula cha *halal* tu, na humimina ndani ya moyo wake chemchem ya hekima”. Kwa upande mwingine matendo mema huhakikisha moyo unatunza kiwango ulichokifikia. Utukufu maalum utokao kwa Mola ni wale tu walio na nyoyo za aina hii, na juu ya hawa kuna nyoyo zilizo hai, nyoyo ambazo zimepambwa na nuru ya Mola ambayo inapatikana kwa Mitume na watakatifu wakubwa. Kutokana na nyoyo zao kuhuishwa na mapenzi matakatifu, hawafanyi masihara pindi wanapoitazama hii dunia na kesho akhera, hawafanyi hivi hata kwa kona ya macho yao. Mwenyezi Mungu Mtukufu amewafanya Mitume na warithi wao, wanachuoni na watakatifu kuwa wakaribishaji wa wanadamu katika *darussalam*<sup>11</sup> kwa njia ya kuwahuisha na kuwasaidia wanyanyue mapazia ya yaliyofunika nyoyo zao, na pia kuwahasisha kuwa na maadili mema na matendo mema ya kiibada na kuwaongoza, hivyo kuwaunganisha na Mola wao (*wasl ila – Mwenyezi Mungu*).

Kiwango kinachotamaniwa na salik, yani mhitaji, mwishoni mwa mafunzo haya ya moyo ni moyo wake kufikia kwenye ihsan, yani kutambua kuwa upo na Mola wakati wote na kwa kufanya hivyo kutampeleka kupata ‘moyo hai’.

### **b- Nyoyo zilizopigwa muhuri na kufa**

Hizi ni nyoyo zilizo kinyume kabisa na nyoyo zilizohuishwa kwa kupitia utajo wa Mola. Milango ya imani huwa imefungwa kwa nguvu kwa ajili ya kuzizuia nyoyo hizi; nyoyo hizi zimepigwa muhuri na kufa. Hazina tofauti na baadhi ya makaburi ambayo yameelezwa kuwa mashimo kutokana na moto wa Jahannam. Nyozo za namna hiyo ni kinyume kabisa na zile za Mitume, watakatifu na watu wema. Wenye nyoyo hizi ambao hawahitaji kingine kinyume na kuiridhisha nafsi hawaoni malengo mengine yoyote yale katika maisha yao tofauti na kula, kunywa na kupitiza miaka yao huku wakifukuzia tamaa za makuu zenye kupita. Kwa upande wa malengo yao ni kwamba hawana tofauti na wanyama; na baadhi yao wamewazidi wanyama. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“Hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walio amini na wakatenda





mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Na walio kufuru huji-furahisha na hula kama walavyo wanyama, na Moto ndio makaazi yao.” (Muhammad, 12).

Na katika aya nyingine:

“Au wewe unadhani kwamba wengi wao wanasikia au wanaelewa? Hao hawakuwa ila ni kama nyama hoa tu, bali wao wamepotea zaidi njia.” (al- Furqan, 44).

Kutokana na nyoyo za watu hao kuwepo kwa malengo na matamania ya nafsi zao, hivyo wanangojewa na adhabu kali kesho akhera, kwa upande mwingine anakuwa katika balaa lenye kuendelea milele. Kwa kawaida watu wa namna hiyo huwa katika giza la maajabu ya ulimwengu. Si kwamba wao peke yao ndio waliopotea bali huwapoteza wengine ambao wana ush-awishi juu yao. Licha ya kwamba wanaishi chini ya uangalizi na baraka za Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini wamejiingiza kwenye hatari ya kukana uwepo wake na kwenda kinyume na maamrishi na makatazo yake. Kuhusiana na watu wa namna hii, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“Kwani mwanaadamu haoni ya kwamba Sisi tumemuumba yeye kuto- kana na tone la manii? Kisha sasa yeye ndio amekuwa ndiye mgomvi wa dhaahiri!” (Yasin, 77).

“Viziwi, mabubu, vipofu; kwa hivyo hawatarejea” (al-Baqara, 18).

“Kwa hakika wewe huwezi kuwafanya maiti wasikie, wala kuwafanya viziwi wasikie wito, wanapo kwisha geuka kwenda zao. Wala huwezi kuwa- ongoa vipofu waache upotovu wao. Huwezi kuwafanya wasikie isipo kuwa wenye kuziamini Ishara zetu; na hao ndio wat’iifu” (an-Naml, 80-81).

Katika kuonesha kwamba nyoyo hizi zimepigwa muhuri na kufungwa Qur’an tukufu inatufahamisha yafuatayo:

خَتَمَ اللَّهُ عَلَى قُلُوبِهِمْ وَ عَلَى سَمْعِهِمْ وَ عَلَى أَبْصَارِهِمْ غَشَاوَةً

وَ لَهُمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ

“Mwenyezi Mungu amepiga muhuri juu ya nyoyo zao na juu ya masikio yao, na juu ya macho yao pana kifuniko. Basi watapata adhabu kubwa” (al-Baqara, 7).





Haya ni maajabu na hekima kubwa kiasi cha kuweza kufanya wanadamu wote watetemeke. Kwa kuwa mwanadamu ana sehemu ya majina matakatifu *Hadi*, yani kiongozi na *Mudhill*, yani mfedheheshaji, ni jambo la kustaajibisha kwa moyo wa mtu kupigwa muhuri kwa uwezo mtakatifu kwa uhakika na kufungiwa milango ya uongofu wakati bado yupo hai. Kwani milango hii haikuwa imefungwa hata kwa Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye alitoka nyumbani kwake huku akiwa na nia mbaya ya kumuua Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, au Wahshi ambaye alimuua Hamza – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, au hata Hind ambaye alipasua maiti yake kwa ukatili na kuzamisha meno yake kwenye ini lake.

Wanajituliza kwa kujidanganya na kutaza ulimwengu usio na kifo wala akhera na kujaribu kupata utulivu ndani yake. Kama ambavyo popo wanafurahia giza pia watu aina hii wanachukulia uharibifu kuwa furaha, haya ni kutokana na mtazamo hasi uliopo kwenye tabia zao. Miili yao ni mizigo kwao, tunakumbushwa haya katika mistri ifuatayo kutoka kwa mshairi Mehmed Akif:

*Imani ni hiyo lulu...na Mola, uzito ulioje juu yake,  
Moyo wenye kutu na kukosa imani, unakuwa mzigo kwenye kifua.*

Kwa hakika wale waliozama kwenye dimbwi la nafsi wataamka na kuingia kwenye ulimwengu wa uhalisia kutokana na mitetemeko mikubwa ya nyakati za mwisho za uhai na mipulizo ya moto kutoka kwa malaika wa mauti. Lakini hakutamnufaisha na chochote, kwani kipindi alichopewa mwana wa Adam ili aamke huisha pale anapomuona malaika wa mauti mbele yake. Wakati huo nafasi inakuwa imepotea moja kwa moja. Katika kipindi hicho majuto huwa hayana nafasi tena, kama ambavyo Firauni alichelewa kumkubali Mwenyezi Mungu na sijda yake wakati akiwa katika mahangaiko ya mauti. Hukumu inayowangojea watu hao ni kuingia katika miale mikali ya Moto wa Jahannam, Moto ambao kiu yake ya kuangamiza huongezeka kadiri watu wanavyozidi kuingizwa.

### **c. Nyoyo zenye maradhi na zisizingatia mambo**

Nyoyo hizo zinasimama kati ya nyoyo zilizo hai na nyoyo zilizokufa. Hali zao zinafanana na maisha ya maumivu ya wale wenye kusumbuliwa na maradhi. Hawana utulivu katika maisha yao wala amani ndani ya nyoyo







zao. Udhaifu wao wa ndani unaashiria ubaya wa nje yao na ukosefu wa utulivu nje yao unachukua nafasi kubwa katika kuashiria hali ya uimara ndani ya nyoyo zao. Kasoro iliyopo katika vichwa vyao inaashiria tabia zao na matendo yao. Nyoyo hizo zenye maradhi ambazo zinayumbayumba katikati ya mzunguko wa mashaka, kukosa maamuzi na ukinzani, huwa wakati wote zipo katika hatari ya kuangukia kwenye uovu kutokana na ujinga wake, tamaa ya makuu na matamania ya nafsi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo kuhusiana na haya: “Nyoyoni mwao mna maradhi, na Mwenyezi Mungu amewazidishia maradhi. Basi watakuwa na adhabu chungu kwa sababu ya kusema kwao uwongo.” (al-Baqara, 10).

**Mashaka** ni jambo lenye kumfanya mtu ashindwe kutua kwenye tawi la ukweli, mashaka ni ugonjwa unaomuweka mtu mbali na maisha ya kiroho na hatimae kuufanya moyo ufe. Hivyo ukosefu wa upatanisho wa kiimani ambao ungelipelekea moyo kuridhika huutesa kwa maradhi yenye kuendelea na hivyo kukosa utulivu.

**Ujinga** ni upofu na njia yenye kiza ambayo haimruhusu mtu hata kuhisi maumivu yatokanayo na kuwa mbali na ukweli. Maradhi haya husambaa mpaka kwenye uwepo wao wote na kuwaongoza watembee katika njia ambayo huishia kwenye kushindwa na kuangamia.

**Tamaa ya makuu na matamania** ni ugonjwa wa kutoridhika ambao huchukua udhibiti mzima wa moyo, haya ni kutokana na kupoteza hali yake ya usafi na uwajibikaji. Haya ni mahangaiko mabaya ambayo yataisha pale mtu atakapoingizwa katika udongo wa kaburi chini ya kivuli kizito cha mvinje.

**Uovu** ni saratani ya kiroho ya moyo. Kama itatibiwa mapema kwa Uwezo wa Mwenyezi Mungu itapona.

**Ugumu** ni maradhi mengine ya moyo yenye kutisha: yanahusiana na utofauti juu ya hisia za kibinadamu na miguso laini ya kiroho. Nyoyo hizi hazijui kutii; hujitia upofu mbele ya sauti za uongofu na hazina hata chembe ya huruma na upendo. Hata mawe ni malaini, angafu na yenye upendo ukilinganisha na nyoyo hizi, kama ambavyo imetajwa ndani ya Qur’an tukufu: “Kisha nyoyo zenu zikawa ngumu baada ya hayo, hata zikawa kama mawe au ngumu zaidi; kwani kuna mawe yanayo timbuka mito, na kuna mengine yanayo pasuka yakatoka maji ndani yake, na kuna mengine huan-guka kwa sababu ya khofu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na mnayo yafanya.” (al-Baqara, 74).





Kama ambavyo tunaona kutoka kwenye aya hii, ugumu wa moyo ni zao la kawaida la kumsahau Mola na kujiweka mbali sana na ukweli mtakatifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo katika aya nyingine: “Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaa-hiri.” (az-Zumar, 22).

Matendo ambayo hutekelezwa na nyoyo zenye maradhi na zisizozingatia mambo huwa yanapoteza thamani yake mbele ya Mola. Bila ya kuwa na nuru ya haki nyoyo huwa na upofu na kutowajibika. Huwa haziwezi tena kutambua mambo mbalimbali na dalili mbalimbali za ulimwengu ambazo zinadhihirisha siri takatifu. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuani” (al-Hajj, 46). Hivyo uoni wenye mazingatio huamsha moyo. Dirisha la macho huwa halina faida mpaka liangalie kwa kupitia nuru ya moyo, kwani haiwezekani kupata uoni mzuri nyuma ya dirisha lenye ukungu.

Hata maradhi madogo madogo ya moyo ambayo hupuuziwa huweza kuupelekea moyo kupata majeraha yasiyoona na hata kupelekea kufa kabisa. Kwa hiyo ni muhimu kuzilinda nyoyo kwa imani thabiti na kuzisalimisha mbele ya Mola. Hakuna mwingine kinyume na Mola ambaye ataweza kumuelekeza na kumuongoza mtu ambaye amejisalimisha kisawa sawa kwa Muumba. *Hadith* ifuatayo inaelezea kwa uzuri zaidi umuhimu wa kuulinda moyo:

أَلَا وَإِنَّ فِي الْجَسَدِ مُضْعَةً إِذَا صَلَحَتْ صَلَحَ الْجَسَدُ كُلُّهُ

وَإِذَا فَسَدَتْ فَسَدَ الْجَسَدُ كُلُّهُ أَلَا وَهِيَ الْقَلْبُ

“Fahamuni kwamba kuna kipande cha nyama ndani ya mwili; kama kitasalimika basi mwili mzima utasalimika, na kama kitaangamia basi mwili mzima nao utaangamia. Na kipande hicho ni moyo!” (Bukhari, Iman, 39).





Dunia ni bonde la Mola la mitihani na majaribu. Hapo zinavuma pepo mbalimbali za majaribu na kuuburuza moyo kutoka sehemu moja mpaka nyingine.

Ni muhimu kuulinda moyo ili kuuzuia usikumbwe kama jani kavu kabla ya kufikiwa na pepo za matukio mbalimbali, pepo ambazo kwa kawaida zinavuma kutokana na dunia kuwa sehemu ya majaribu. Kinachohitajika ni kuusalimisha moyo kwenye pepo mwanana zinazovuma kutoka kwenye njia ya msaada mtakatifu kutoka kwa Mola; na hili litawezekana kwa kutafuta ulinzi kutoka kwake, kumtii na kujisalimisha kwenye maamrishi na makatazo yake.





**M**oyo ni kama maji meupe. Lakini pindi utakapotiwa matope kwa matendo maovu na madhambi hubadilika na kuwa mweusi. Hivyo kunakuwa hakuna budi kuyachuja hayo matope ili uweze kuonyesha lulu za kiroho na nuru za ukweli zilizomo ndani yake.



### 3. UTAKASO WA MOYO

Masharti makuu ya kuweza kuufanya moyo ubakie katika hali ya kuwa mbali na kasoro, kujuta na kutosheka, kutibu nyoyo zenye maradhi na kuji-  
zuia na hatari ya nyoyo zilizopigwa muhuri ni:

- a. Chakula cha halali.
- b. Toba na dua.
- c. Kuisoma Qur'an na kutii maamrisha yake.
- d. Kufanya ibada kwa unyenyekevu wa hali ya juu (*khushuu*).
- e. Kuzihuisha nyakati za usiku kwa ibada.
- f. Mapenzi ya hali ya juu kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na kuendelea kuonyesha mapenzi hayo kwa kupitia *salawat*.
- h. Kutafakari juu ya mauti.
- i. Kukaa karibu na watakatifu na watu wema.
- k. Kuutazama ulimwengu kwa kupitia moyo safi.

Kwa kuanza tu ni kwamba huwa ni jambo la muhimu kuwa na uelewa sahihi wa asili na umuhimu wa masharti haya ambayo utekelezaji wake halisi ni muhimu.

#### a. Chakula cha halali

*“Ndugu...msidhani kwamba mtapata alama ya hekima hali ya kuwa mnakula chakula cha haramu”.*

*Ibrahim Dasuki - Mwenyezi Mungu atakase siri yake.*

Kama ambavyo yanategemea chakula cha kiroho ambacho kinanawir-





isha roho, vile vile matendo ya ibada yanategemea uimara na ukunjufu unaopatikana kutoka kwenye chakula cha kimwili. Wakati vyakula vya halali vinaingiza mwilini imani na msukumo, vyakula vya haramu na vyenye kutia mashaka ambavyo ni kinyume chake vinautia kiza, uzito na kupuuzia mambo. Kuna uhusiano mkubwa kati ya vyakula vya halali na matendo mema. Ulaji wa vyakula vya halali una mchango mkubwa katika kukubaliwa kwa swala kama ambavyo amelielezea hili Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake: “Watu...Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu ametakasika na ni msafi. Kwa hiyo hakubali chochote kile isipokuwa kiwe kimetakasika na kisafi. Amewaelekeza waumini yale aliyowaelekeza Mitume:

“Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa mnayo yatenda.” (al-Muminun, 51).

“Enyi mlio amini! Kuleni vizuri tulivyo kuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa kweli mnamuabudu Yeye tu.” (al-Baqara, 172).

Baada ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kuzitaja aya hizi, alimzungumzia mtu mmoja ambaye nywele zake zilikuwa zimevurugika na huku amejawa na vumbi mwili mzima kutokana na safari ndefu, na kisha mtu huyu akanyanyua mikono yake juu na kuomba, ‘Mola wangu...Mola wangu’, na kisha akaongezea: “Ni vipi dua zake zitajibiwa wakati anachokula, kunywa na kuvaa vyote ni vya haramu” (Muslim, Zakat, 65).

Kwa ajili ya mafanikio ya kiroho juu ya nyoyo zao Sufi wamekuwa makini mno kuhusiana na vitu viwili kama ambavyo vimetajwa katika usemi: “Kueni makini na kila kinachoingia midomoni mwenu pindi mnapokula na kila kinachotoka pindi mnapoongea!”

Hadith ifuatayo inatukumbusha vizuri kwa mukhtasari juu ya kiasi cha tahadhari ambacho hatuna budi kuwa nacho kuhusiana na *halal* na *haram*.

“Bila shaka *halal* na *haram* vimewekwa wazi. Lakini kati ya hivi viwili kuna baadhi ya vitu vyenye kutia mashaka, vitu hivyo havifahamiki na wengi miongoni mwetu. Yeyote atakayejipusha na vile vyenye kutia mashaka atakuwa ameilinda dini yake na heshima yake. Na yeyote atakayeacha kujizuia na vile vyenye kutia mashaka ataingia kwenye haramu





kidogo kidogo. Kama ambavyo mchungaji anayechunga wanyama wake karibu na shamba la mwingine...wakati wote anakuwa katika hatari ya wanyama wake kuingia kwenye shamba hilo bila ruhusa. Fahamuni kwamba kila mfalme ana shamba ambalo limepigwa marufuku kuingia yeyote. Shamba la Mwenyezi Mungu lilikataziwa ni haramu” (Bukhari, Iman, 39).

Nyoyo ambazo zinajisalimisha zenyewe na kutii maamrisho ya Mola huwa misingi ya hekima na utambuzi wa kiroho. Kinyume chake ni kwamba nyoyo zisizolindwa dhidi ya haramu na zile zenye mashaka hukimbilia kwenye hifadhi ya uovu na utovu wa maadili wakati wote. Mifano ifuatayo inatoa mafunzo makubwa kuhusiana na namna ambavyo suala hili halina budi kushughulikiwa kwa umakini mkubwa:

*Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa na mtumwa. Yule mtumwa alikuwa akimletea Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kiasi fulani cha kile alichokuwa akikichuma kwa ajili yake ili akitumie kwa matumizi yake binafsi. Siku moja yule mtumwa kwa mara nyingine tena alimletea Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kisha Abu Bakr akaanza kukila. Mara yule mtumwa akamuuliza, “Je unakifahamu hicho unachokila?”.*

*“Hapana, sifahamu. Kwa nini usiniambie?” alijibu.*

*“Ingawa sifahamu chochote kuhusiana na utabiri”, yule mtumwa alianza kuelezea, “siku moja katika masiku yangu ya ujahiliya nilimtabiria na kumdanganya huyu mtu. Leo nilikutana naye na hivyo akanilipa hicho unachokila sasa hivi!”*

*Mara tu baada ya Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kusikia hivi alichokonoa koo lake kwa kidole chake na licha ya adha aliyoipata lakini alitapika kile alichokila. (Bukhari, Manaqibu'l-Ansar, 26).*

Kutokana na mapokezi mengine, baada ya pale yule mtumwa alisema, “Kwa nini upate tabu yote hii kwa tonge moja tu?” Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alijibu, “Hata kama ningelifahamu kuwa ningelikufa kwa kufanya hivi bado ningelitoa tonge hilo”. (Ahmad ibn Abdullah at-Tabari, ar-Riyadu'n-Nadra, II, 140-141).

Pia kuna majadiliano mengine mazuri ambayo yalikuwa kati ya Khidr (a.s) na Abdulkhaliq Gujdawani – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, majadiliano hayo yalifanyika pindi Khidr (a.s) alipomtembelea





Abdulkhaliq Gujdawani. Khidr (a.s) hakugusa vyakula alivyotengewa na Abdulkhaliq Gujdawani (k.s) na akaamua kutoka mezani.

*“Vyakula hivi ni halali. Kwa nini huli?” Gujdawani (k.s) alimuuliza kwa mshangao.*

*“Ni kweli, vyakula hivi ni halali”, Khidr (a.s) alijibu. “Lakini aliyekian-daa amefanya hivyo kwa hasira na ujinga”.*

Kutokana na mifano hii katika kuhukumu ikiwa kinacholiwa ni halali au haramu pia hali ya kiakili ambayo chakula kinapikwa kwayo ina nafasi kubwa katika roho ya mtu, tabia na kiwango cha matendo yake ya ibada. Jambo hili linatoa ufafanuzi zaidi juu ya umakini unaotakiwa kuchukuliwa kuhusiana na chakula.

Umakini wao juu ya chakula uliwapelekea watu wema kufunika vyakula vyao wanavyovinunua kutoka sokoni au sehemu nyingine wakati wanavipeleka majumbani mwao. Haya yote ni kwa ajili ya kuzuia macho ya watu ya matamania ‘yasije yakakitazama chakula’ na tamaa ya masikini na mtazamo wa kimatamania wa wasiokuwa nacho usije ukasababisha madhara kwenye nishati na nguvu inayotarajiwa kupatikana kutokana na chakula kile.

Pamoja na kujiweka mbali na haramu na vitu vyenye kutia mashaka lakini pia muumini hana budi kuweka usawa na kujizuia na ubadhirifu wakati wa kula chakula cha halali. Aya ifuatayo inatuamrisha: “Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo. Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashet’ani. Na Shet’ani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi.” (al-Isra, 26-27).

Kwa kutumia sauti ya kisitiari Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - anasema yafuatayo katika Mathnawi zake kuhusiana na athari za chakula cha halali juu ya roho na mwili:

*“Utambuzi wetu wa kiroho ulikuja katika sura mbalimbali usiku, haya ni kutokana na matonge kadhaa ya chakula cha mashaka kupata njia na kupita mpaka tumboni na kuzuia njia ya utambuzi wa kiroho.*

*Vyakula vya mashaka vinavyopendwa na nafsi ni kama miba iliyopo chini ya nyayo zenu ambayo inawazuia katika njia ya haki. Ndio maana wale ambao hawakuchukua tahadhari juu ya kile walichokuwa wakikila mapema sana waliingia kwenye uasi.*





*Enye watu! Mna waridi zuri ambalo kama mtalilinda mabustani ya waridi ya hekima na marifa yasiyo na idadi yatachipua kutokana na harufu inayotoa”.*

Yafuatayo ni maneno kama hayo kutoka kwa Abdulqadir Jilani – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kuhusiana na umuhimu wa chakula cha halali katika kuutakasa moyo:

*“Sikiliza mwanangu! Chakula cha haramu huuu moyo. Kuna matonge ambayo huuangazia moyo wako na kuna matonge ambayo huufunika moyo na kuufanya uwe gizani. Pia kuna matonge ambayo yatakufanya uikumbatie dunia na kuna mengine yatakufanya uikumbatie akhera. Kuna matonge ambayo yatakufanya uwe mtii juu ya vyote viwili, dunia na akhera; na kuna matonge ambayo yatakuelekeza kwa Muumba wa vyote viwili, dunia na akhera. Kula kilicho cha haramu kutakushughulisha na dunia na kupelekea madhambi yako yawe ni kitu chenye kukubalika kwako. Kula kilicho mubah (kisichoharamishwa) kutakupelekea kushughulikia akhera na kupenda kufanya ibada. Kwa upande mwingine kula chakula cha halali kutakukurubisha zaidi kwa Mola. Kwa kupitia marifatullah (ufahamu juu ya Mwenyezi Mungu) pekee ndiko kutakapopelekea kufahamu hulka na ushawishi wa vyakula. Na marifatullah huandikwa katika moyo pekee na si katika kurasa za vitabu. Marifatullah huingizwa ndani ya moyo na Muumba na si kiumbe. Na hili hutokea baada ya kuthibitisha upweke wa Mwenyezi Mungu na kuyafanyia kazi maamrisho yake”.*

Ibrahim Dasuki – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - anasema hayo hayo, “Ndugu...msidhani kwamba mtapata alama ya hekima hali ya kuwa mnakula chakula cha haramu”.

Pia ni muhimu kuzingatia maneno yafuatayo kutoka kwa Sayyid Qasim Tabrizi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliyoyasema kuhusiana na kula kilicho halali, maneno ambayo yalisimuliwa na Ubaydullah Ahrar – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake:

*“Siku moja Sayyid Qasim aliniambia, Je unafahamu kwa nini siku hizi hekima na ukweli hujidhihirisha vyenyewe mara chache? Ni kwa sababu kuna watu wachache tu ambao wamezitakasa nyoyo zao. Ukamilifu unategemeana na kuutakasa moyo. Na hilo linawezekana kwa kula chakula cha halali pekee. Siku hizi chakula cha halali ni hadimu mno ndio maana ni kana kwamba hakuna hata mtu mmoja ambaye amefikia kwenye utakaso wa moyo. Ni kipi kingine! Ni vipi unategemea siri takatifu kuwafunukia?”.*







## b. Toba na dua

**“Sema: Mola wangu Mlezi asinge kujalini lau kuwa si kuomba kwenu...” (al-Furqan, 77).**

Kwa ujumla watakatifu, wachamungu na watu wema, na juu ya hao wote Mitume wamekuwa wakati wote wakitafuta ulinzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumuomba katika nyakati za shida na raha. Kwa kuwa hata Mitume wana vikosa vidogo vidogo (*dhalla*)<sup>12</sup> hivyo ni jambo la kushangaza kwa mtu yeyote kutokuwa na haja ya kufanya toba na maombi. Kwani toba na dua zinamaanisha kujuta na hali ya juu ya maombi, hii ni namna nzuri ya kujikurubisha kwa Mola. Kwa hakika moja ya hekima kubwa iliyopo juu ya swala tano za kila siku kuitwa kwa jina la *salat*, likimaanisha ‘dua’ katika kiarabu, ni kutokana na kuwa namna bora kabisa ya dua na maombi.

Huwa dua inatanguliwa na toba; yani kuomba msamaha kwa Mola. Kama toba ya mtu itaenda pamoja na kujuta na kujirudi kuwa kamwe hutorudia tena kosa ulilolitenda, basi itafutilia mbali uchafu na kutu iliyokuwa imeuziba moyo na kuufanya kuwa kioo safi chenye kuakisi ukweli. Njia hii pekee ndio inayoweza kuufanya moyo uwe tayari kupokea uongofu wa kiroho.

Maelezo juu ya namna ambavyo moyo ambao umefunikwa kwa kiza cha madhambi unavyoweza kupata nuru kwa kupitia toba yanatolewa na *hadith* ifuatayo ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake: “Pindi mja anapotenda dhambi tone jeusi hugandishwa moyoni mwake. Kama ataachana na dhambi ile na kutubia basi moyo wake hung’arishwa. Lakini kama hatafanya hivyo na akaamua kuendelea kutenda dhambi, basi matone meusi yataongezeka na mwishowe kuufunika moyo mzima. Hili ndilo Mwenyezi Mungu Mtukufu analolimaanisha pindi anaposema:

كَلَّا بَلْ رَانَ عَلَى قُلُوبِهِمْ مَا كَانُوا يَكْسِبُونَ

“Hasha! Bali yametia kutu juu ya nyoyo zao hao walio kuwa wakiyachuma.” (al-Mutaffifin, 14) (Tirmidhi, Tafsir, 83).

<sup>12</sup> Dhalla ni kosa lisilo la makusudi.





Pindi tutakapoitazama dunia kwa jicho la moyo, tutagundua kuwa viumbe vyote vipo katika hali ya kukubali udhalili wao kabla ya kushukuru kwa kile Mola anachowapatia kwa namna ya kipekee wanayoifahamu wenyewe. Kwa upande wa mwana wa Adam ambaye hawezi kufanya jambo lolote bila ya kukosea toba kwake ni hatua ya kwanza ya *taqarrub*, yani kujikurubisha kwa Mola.

Kutokana na asili yake ya kuvuta rehema takatifu, dua ni muhimu sana katika kumlinda mtu dhidi ya maangamizi. Kama ambavyo kumekwishatajwa hapo kabla hii ndio sababu iliyopelekea kwamba katika kanuni zote za kisufi mafunzo ya kiroho yanaanza kwa toba. Kuhusiana na umuhimu wa dua Qur'an tukufu imesema:

قُلْ مَا يَعْبُؤُا بِكُمْ رَبِّي لَوْلَا دُعَاؤُكُمْ

“Sema: Mola wangu Mlezi asinge kujalini lau kuwa si kuomba kwenu. Lakini nyinyi mmemkadhibisha. Basi adhabu lazima iwe.” (al-Furqan, 77).

“Na waja wangu watakapo kuuliza khabari zangu, waambie kuwa Mimi nipo karibu. Naitikia maombi ya mwombaji anapo niomba. Basi na waniitikie Mimi, na waniamini Mimi, ili wapate kuongoka.” (al-Baqara, 186).

“Muombeni Mola wenu Mlezi kwa unyenyekevu na kwa siri. Hakika Yeye hawapendi warukao mipaka” (al-Araf, 55).

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema yafuatayo katika *hadith* ifuatayo: “Hakuna chochote chenye thamani zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu zaidi ya kumuomba Yeye. Dua ni kiini cha utumishi” (Tirmidhi, Daawat, 1).

“Yeyote anayetaka dua zake zikubaliwe wakati wa matatizo basi na aombe dua nyingi katika nyakati za wepesi na raha” (Tirmidhi, Daawat, 9).

“Muombe Mwenyezi Mungu kwa imani kwamba utajibiwa. Fahamu kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hakubali dua iliyoombwa kwa moyo usio na utambuzi” (Tirmidhi, Daawat, 65).

Hivyo kutarajia kukubaliwa kwa dua iliyoombwa kwa moyo usio na utambuzi na katika njia ya mteremko si chochote bali ni ulaghai wa Shet-





ani. Imam Rabbani – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Vita huweza kushindwa kwa msaada wa nguvu za majeshi mawili. Moja wapo ni jeshi la askari na jingine ni jeshi la dua”. Katika kuthibitisha hili ni pale maswahaba walipokuwa wakiwaomba wanafunzi wa *suffa* wawaombe kabla ya kwenda vitani. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Hakuna dua inayokubalika kwa haraka zaidi kuliko dua ya muislamu anayomuomba muislamu mwingine ambaye hayupo” (Tirmidhi, Birr, 50).

Watu hutafuta dua za wale wanaoamini kuwa dua zao zitakubalika kwa haraka. Lakini bado sharti kuu la kuhakikisha dua inakubaliwa si kumtegemea mtu mwingine bali ni usafi wa moyo anaokuwa nao wakati anaomba. Hili linamaanisha kwamba dua sahihi iliyooombwa na mtu mwenye dhambi juu ya muislamu mwingine ni bora kuliko dua ya kusita sita iliyooombwa na mwingine, hata kama ana nafasi kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Haya ni kwa sababu haimaanishi kuwa mtu mwenye dhambi ameachwa na Mola; na Mwenyezi Mungu anatukataza kabisa kutofikiria hivyo. Kama ingelikuwa hivyo, kuzungumzia kuhusu madhambi ya mtu kusingelichukuliwa kuwa ni kusengenya (*ghiybah*), jambo ambalo ni moja wapo ya madhambi makubwa. Hapa thamani ipo katika kuushinda moyo wa mtu, yeyote awaye, na kupokea dua zake sahihi kutoka moyoni.

“Ni dua ipi yenye kukubalika zaidi kuliko dua zote?” siku moja maswahaba walimuuliza Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. “Dua iliyooombwa katika masaa ya mwisho ya usiku na baada ya kila swala ya faradhi” alijibu. (Tirmidhi, Daawat, 78).

Ili dua ikubalike haitoshi tu kuisema kwa maneno. Moyo hauna budi kutetemeka kutokana na kutafakari juu ya maana za maneno yaliyochaguliwa kwa ajili ya dua; na kama dua inahusiana na kuomba msamaha wa madhambi basi haina budi kuongozana na kujirudi kuwa hutarudia kosa lile tena. Kwa kuongezea ni kwamba msimamo (*istiqamah*) na matendo mema ni mambo muhimu kwa ajili ya kupelekea dua kupata njia ya kufika mbele ya Mwenyezi Mungu. Haya yamedhihirishwa katika aya: “Mwenye kutaka utukufu basi utukufu wote uko kwa Mwenyezi Mungu. Kwake Yeye hupanda neno zuri, na a’ mali njema Yeye huitukuza. Na wanao panga vitimbi vya maovu watapata adhabu kali. Na vitimbi vya hao vitaondokea patupu.” (Fatir, 10).





Hivyo ni muhimu angalau kujaribu kuomba katika hali ambayo ni kati ya hofu (*khawf*) na matumaini (*rajaa*). Dua na toba huwaongoa watu binafsi na jamii na kuzuia majanga ya mbeleni. Ili dua zikubalike na moyo uponywe kutokana na maradhi yake ndani ya mchakato huu, Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anashauri yafuatayo: “Omba na utubu huku moyo ukiungua ndani ya moto wa majuto na huku macho yakiwa na unyevu nyevu; kwani maua huchanua sehemu ambazo kuna jua na unyevu nyevu!”

Toba kwanza ilianza na Mtume wa kwanza Adam (a.s) ambaye aliomba:

رَبَّنَا ظَلَمْنَا أَنْفُسَنَا وَإِن لَّمْ تَغْفِرْ لَنَا وَتَرْحَمْنَا

لَنَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ

“Mola wetu Mlezi! tumejidhulumu nafsi zetu, na kama hutusamehe na kuturehemu, hakika tutakuwa katika wenye kukhasirika.” (al-Araf, 23). Dua hii imeweka mfano wa toba kwa vizazi vyake vilivyofuatia mpaka saa ya mwisho.

Ili kuziamsha nyoyo zilizolala na kuzipatia tiba ya maradhi yake ya kiroho, Mwenyezi Mungu Mtukufu anawaita waja wake watubie kwa kusema: “Enyi mlio amini! Tubuni kwa Mwenyezi Mungu toba iliyo ya kweli! Asaa Mola wenu Mlezi akakufutieni maovu yenu na akakuingizeni katika Pepo zipitazo mito kati yake...” (at-Tahrim, 8).

Dua na toba ni vichocheo muhimu katika kumfanya mtu amuelekee Mola wake na kuupandisha moyo wake mpaka kwenye daraja la juu kabisa. Kwa kuwa moyo upo wazi kushambuliwa na vishawishi mbalimbali ambavyo vinaweza kusababisha ‘moyo kubadilika’, mtu hana njia nyingine zaidi ya kushikamana na dua ili kuhakikisha moyo wake unabaki imara katika njia ya uongofu. Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anatufundisha kurudia dua ifuatayo:

رَبَّنَا لَا تُرِغْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً

إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَّابُ





“Mola wetu Mlezi! Usizipotoe nyoyo zetu baada ya kwisha tuongoa, na utupe rehema itokayo kwako. Hakika Wewe ndiye Mpaji...” (Al-i Imran, 8).

Katika kuyarudia maelekezo haya matakatifu katika uhai wake wote, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa mara kwa mara akiomba:

يَا مُقَلَّبَ الْقُلُوبِ ثَبِّتْ قَلْبِي عَلَى دِينِكَ

“Ewe mwenye kuzibadilisha nyoyo! Uimarishe moyo wangu katika dini yako” (Tirmidhi, Qadar, 7).

Dua ni moja wapo ya njia muhimu za kuutakasa moyo dhidi ya uchafu wake wa kiroho. Aya ifuatayo inalidhihirisha hili kwa uzuri zaidi: “Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu.” (al-Hashr, 10).

Hivyo ni muhimu kwanza kabisa kuusafisha moyo dhidi ya machafu yote ambayo yanakuwa kama kikwazo katika njia yake ya kufikia kwenye lengo kuu, na kufanya sakafu ya moyo ifae kwa ajili ya kufikia lengo kuu. Dua zifuatazo kutoka kwa Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – ni mifano tosha kwa ajili ya kuusafisha moyo dhidi ya kutojali na hisia hasi:

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ninajilinda kwako dhidi ya elimu isiyo na manufaa, moyo usio tetemeka, roho isiyoridhika na dua isiyojibiwa!” (Muslim, Dhikr, 73).

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ambavyo unasafisha nguo nyeupe dhidi ya uchafu, naomba uisafishe moyo wangu dhidi ya madhambi na uufanye uwe safi!” (Bukhari, Daawat, 39).

Kupata moyo usio na kasoro kutawezekana kwa kupitia baraka za Mola. Ibrahim (a.s) ambaye aliweza kuhudhurisha mbele ya Mola moyo usio na kasoro aliomba dua ifuatayo ili asije akasumbuliwa siku ya kiama: “Wala usinihizi Siku watapo fufuliwa. Siku ambayo kwamba mali hayato faa kitu wala wana. Isipo kuwa mwenye kumjia Mwenyezi Mungu na moyo safi.” (as-Shuara, 87-89).





Katika kufuata nyayo za babu yake huyo wa mbali, Mtume aliyebarikwa – rehemu na amani ziwe juu yake – naye aliomba dua hiyo hiyo: “Ewe Mwenyezi Mungu! Ninaomba kutoka kwako ulimi ambao unasema ukweli na moyo usio na kasoro!” (Tirmidhi, Daawat, 23).

Jambo la muhimu katika dua ni kurudia rudia na kuendelea nayo. Imekuwa ni kama kanuni kurudia dua angalau mara tatu ili kuonyesha uendelevu. Kama dua itaombwa kwa moyo safi kamwe haitakataliwa. Hata hivyo ingawa baadhi ya dua wakati mwingine haziendani na utaratibu wa Mwenyezi Mungu. Lakini bado mtu hana budi kuendelea na dua bila ya kuchoka (*futur*), kwani ikiwa haitajibiwa hapa dunia kwa hakika itafidiwa kesho akhera.

### c. Kuisoma Qur’an na kutii maamrishi yake

*Kuuajaza moyo kwa hekima itokanayo na Qur’an kunategemea kiwango cha imani katika moyo wa mtu pindi anapoisoma.*

Mola kumfanya mtu kuwa katika uelekeo wa Qur’an bila shaka ni moja ya baraka kubwa ambayo Mola amemjaalia Mwanadamu. Vipimo kamili vya amani ya kweli na usawa wa kiroho na kimwili vinapatikana ndani ya maudhui za Qur’an zenye kuvutia. Furaha na uongofu wa mtu huwezekana kwa kiasi cha sehemu aliyonayo katika vipimo hivi kamili. Mtu ambaye hupoteza uzani wake wa ndani kutokana na kuipa mgongo imani juu ya Qur’an badala ya kutafuta ulinzi ndani yake, atakuwa amepoteza heshima yake ya kibinadamu. Kuielekea baraka hii kubwa kuliko baraka zote bila ya shukurani kutakuwa ni kuiingiza nafsi yako katika maangamizi kutokana na matamania na tamaa yako ya makuu.

Qur’an ni kisima cha hekima takatifu ambacho hutoa tiba na tulizo kwa ajili ya nyoyo zenye kuvuja damu na roho zilizochoka. Yenyewe ni zawadi takatifu ambayo imebeba funguo kwa ajili ya kukaribisha tukio lenye kuogopesha mauti ambayo ndio njia, wakati huu ni kama usiku wa harusi (*shab-i arus*), kwa ajili ya kumuwezesha muumini kukutana na Mola wake. Kuhusiana na hili Mwenyezi Mungu Mtukufu anawapa wanadamu wote maneno yake matakatifu katika aya ifuatayo:





يَا أَيُّهَا النَّاسُ قَدْ جَاءَتْكُمْ مَوْعِظَةٌ مِنْ رَبِّكُمْ  
وَ شِفَاءٌ لِمَا فِي الصُّدُورِ وَ هُدًى وَ رَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ

“Enyi watu! Yamekujieni mawaidha kutoka kwa Mola wenu Mlezi, na poza kuponyesha yaliyomo vifuani, na uwongofu, na rehema kwa Wau-mini.” (Yunus, 57).

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema yafuatayo katika *hadith*:

“Kila mwenye karamu hupenda watu wahudhurie kwenye karamu yake na huwa anafurahishwa na jambo hilo. Qur’an nayo ni karamu ya Mwenyezi Mungu. Hivyo msijiweke mbali nayo” (Darimi, Fadhailul-Quran, 1).

“Isomeni Qur’an...kwani Mwenyezi Mungu hatauadhibu moyo ambao utakuwa na Qur’an ndani yake” (Darimi, Fadailul-Quran, 1).

“Watu wa kweli mbele ya Qur’an ni watu wa Mwenyezi Mungu...na hao ni waja wake wa kweli” (Hakim, Mustadrak, I,743).<sup>13</sup>

Nyoyo zilizo mbali na utajo wa Mwenyezi Mungu na kuisoma Qur’an huwa ngumu na zilizodhoofika, kama ambavyo tunaweza kuelewa kutoka kwenye maneno ya Abu Musa al-Ashari – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kwa wale waliokuja kumtembelea: “Endeleeni kuisoma Qur’an! Kamwe usipite muda mrefu bila ya kuisoma...kinyume chake nyoyo zenu zitakuwa ngumu kama za wale waliotangulia!” (Muslim, Zakat, 119).

Tukio lifuatalo linadhihirisha namna ambavyo Qur’an ina athari hata kwa wanyama na malaika:

*“Usiku mmoja nilikuwa nikisoma Surat Baqara. Farasi wangu alikuwa*

13. Watu wa Mwenyezi Mungu’ ambao si tu wameihifadhi Qur’an bali wanatii ma-amrishi yake na kushikamana na maadili yake, wanapata baraka nyingi kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Pia imepokewa kwamba maiti za baadhi ya *huffadh* hubakia bila hata dalili yoyote ya kuoza baada ya vifo vyao. Mpendwa Mahmud Sami Ramazanoglu - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – binafsi amethibitisha kuiona maiti ya *hafidh* ndani ya Adana ambayo haijaoza hali ya kuwa imepitiwa na miaka thelathini. Si tu maiti hiyo ilikuwa haijaoza bali hata sanda yake ilikuwa haijarahibika.





*karibu yangu huku amefungwa. Lakini katika hatua fulani farasi alianza kunyanyua miguu yake ya nyuma. Niliacha kusoma na farasi akatulia. Kisha nikaendelea kusoma lakini yule farasi akaanza kunyanyua miguu yake ya nyuma kwa mara nyingine kadiri nilivyokuwa nikisoma. Kwa kuho-fia kuwa angelimkanyaga mtoto wangu nililazimika kumsogeza mwangu Yahya karibu yangu. Kisha nikatazama angani na kuona alama kama taa, alama ambazo baada ya muda mfupi zilipanda juu zaidi angani na kupotea machoni mwangu. Asubuhi yake nilimuelezea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – juu ya kile nilichokishuhudia.*

‘Soma Usayd, soma’, aliniambia hivyo kabla ya kuniuliza, ‘je unafahamu ni vitu gani vile ulivyoviona?’

‘Hapana’ nilijibu.

‘Wale walikuwa malaika ambao walikuja kusikiliza kisoma chako cha Qur’an. Lau kama ungelindelela kusoma, wangelindelela kukusikiliza mpaka asubuhi. Pia wasingelijificha kwa watu wengine, wangelibaona wazi wazi kama wewe uliyowaona’” (Bukhari, Fadail’ul-Quran, 15).

Qur’an iliteremshwa kwa wanadamu; kwa mtu mwenye moyo safi Qur’an kwake huwa hazina kubwa ya mazingatio. Kujiweka mbali na Qur’an kunamaanisha kukengeuka na maangamizi makubwa. Kuhusiana na wale wasiotambua kuwa Qur’an ni bahari ya hekima na maajabu, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

أَفَلَا يَتَذَكَّرُونَ الْقُرْآنَ أَمْ عَلَى قُلُوبٍ أَقْفَالُهَا

“Je! Hawaizingatii hii Qur’ani? Au kwenye nyoyo (zao) zipo kufuli?” (Muhammad, 24).

Qur’an ni udhahirisho wa majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yaliyoakisiwa katika uelewa wetu kwa namna ya maneno. Mwenyezi Mungu Mtukufu anataeleza utukufu wa hali ya juu wa Qur’an katika maana yake katika aya ifuatayo:

“Na lau kuwa miti yote iliyomo duniani ikawa ni kalamu, na bahari (ikawa wino), na ikaongezewa juu yake bahari nyengine saba, maneno ya Mwenyezi Mungu yasingeli kwisha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.” (Luqman, 27).







Kuujaza moyo kwa hekima itokanayo na Qur'an kunategemea kiwango cha imani katika moyo wa mtu pindi anapoisoma. Hivyo ili kuupate ukweli wa Qur'an ni jambo la lazima kuupandisha moyo ili ufikie kiwango kinachostahiki, kwani Qur'an ina kawaida ya kumuongoza au kumpoteza mtu, kutegemeana na nia na kiwango cha imani cha msomaji. Haitoshi, kama Qur'an itasomwa katika namna nzuri, aya zake zitatema raha ya kiroho ndani ya nyoyo za waumini. Kuhusiana na hili Qur'an inasema:

“Mwenyezi Mungu ameteremsha hadithi nzuri kabisa, Kitabu chenye kufanana na kukaririwa; husisimua kwacho ngozi za wenye kumkhofu Mola wao Mlezi. Kisha ngozi zao na nyoyo zao hulainika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Huo ndio uwongofu wa Mwenyezi Mungu, na kwa huo humwongoa amtakaye. Na ambaye ameachwa na Mwenyezi Mungu kupotea, basi hapana wa kumwongoa.” (az-Zumar, 23).

“Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi.” (al-Anfal, 2).

Sharti la kwanza la kuweza kunufaika na Qur'an ni kuiendea kwa heshima; aina ya heshima yenye kuonyesha umuhimu ulioambatana na maneno ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutokana na kubeba ukweli wote na utambuzi wa mambo yote kwa ajili ya kumhudumia mwanadamu mpaka saa ya mwisho, kunaifanya Qur'an kuwa muongozo usio na kifani. Sifa hii ya Qur'an imegusiwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwenyewe: “Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyo nyooka kabisa, na inawabashiria Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba watapata malipo makubwa.” (al-Isra, 9).

Kwa kuwa Qur'an ni kitabu kitakatifu ambacho wajibu wake kama muongozo umefanywa uendeleo mpaka saa ya mwisho, hivyo waislamu wote walio chini ya nuru ya muongozo wake hawana budi kuishi kulingana na mwenendo wa kimaisha wa Qur'an mpaka hapo kifo kitakapowagongea hodi kwa ajili ya kuwapeleka kwenye maisha ya milele. Kupata furaha ya kiroho na uongofu hapa duniani na kupata radhi za Mola na baraka zake kesho akhera kutawezekana kwa kupitia njia hii pekee.

Mtu atanufaika vizuri na Qur'an pale atakapoisoma kwa moyo wake. Jambo hili linaelezwa vizuri zaidi katika jibu lifuatalo la Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – pindi alipoulizwa kuhusi-





ana na sauti na namna inayopendekezwa pindi Qur'an inaposomwa: "Ni kisomo cha yule ambaye atakuingizia hisia kuwa anamuogopa Mwenyezi Mungu" (Darimi, Fadailu'l-Quran, 34). Bila shaka ilikuwa ni kisomo kizuri cha Qur'an nyumbani kwa dada yake Fatma – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ndicho kilichochochea hisia za shauku ndani ya Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na kumuongoza kwenye ukweli.

Aya zifuatazo zinatoa mwangaza wa namna nzuri ya kusoma Qur'an:

"Na hiki Kitabu, tumekuteremshia wewe, kimebarikiwa, ili wazizingatie Aya zake, na wawaidhike wenye akili." (Sad, 29).

"Au izidishe - na soma Qur'ani kwa utaratibu na utungo." (al-Muzammil, 4).

Imepokewa kuwa Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alimaliza kusoma surat Baqara ndani ya miaka kumi na mbili kamili na kisha akachinja ngamia kama shukurani ya kufanya hivyo. (Qurtubi, al-jami, 1,40). Vile vile Abdullah ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alitumia miaka nane kukamilisha kisomo cha sura hiyi hiyo. (Muwattaa, Quran, 11).

Pindi maswahaba walipokuwa wakimaliza kujifunza aya kumi kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kamwe walikuwa hawaendelei kujifunza aya nyingine kumi kabla hawajazielewa kiundani na kufanyia kazi hekima na maamrisho yaliyomo ndani ya aya zilizotangulia. Kwa kufanya hivyo waliweza kuipata elimu halisi ya Qur'an na taratibu waliweza kujipamba kikamilifu kwa hekima zake. (Ahmed, V, 410).

Kinachoonekana katika mifano hii ni kwamba wakati mtu anaisoma Qur'an asitamke tu maneno yake bali atafute undani wa hekima zake ambazo zitamuwezesha kutii maamrisho yake kwa uaminifu na kujipamba na maadili yake.

Hatuna budi kutambua kwamba watu wa dola ya Uthmainiyya ambao baada ya zama za neema walikuwa katika mwenendo bora kabisa wa uislamu wanastahiki heshima hii kutokana na baraka zilizotokana na kuheshimu kwao Qur'an. Ni jambo linalofahamika na wengi katika historia kuwa Osman Ghazi ambaye alikuwa mwanzilishi wa dola, alitumia usiku wake katika nyumba ya Sheikh Edebali huku akiwa macho mpaka asubuhi, alifanya hivi kwa kuhofia kuwa isingelikuwa heshima kwa yeye kulala chini ndani ya chumba ambacho Qur'an imening'inia ukutani. Pia upigwaji





marufuku juu ya kuigusa Qur'an ukiwa huna udhu unaashiria ulazima na umuhimu wa heshima wakati wa kuindea Qur'an. Pia inafahamika katika adabu za kiislamu (adab) juu ya kutoishikilia Qur'an chini ya kiuno. Achana na kuisoma Qur'an, kunashauriwa hata kuzitazama tu herufi zake kuna malipo, kwani kunakufanya uwe na mapenzi na Qur'an. Hivyo kila mtu hana budi kujiepusha na kuivunjia heshima Qur'an na anatakiwa awe na desturi ya kuisoma mara kwa mara hata kidogo. Pia hatuna budi kutambua kuwa amri ya Qur'an ya kwanza kabisa ni 'kusoma' (al-Alaq, 1). Umuhimu wa amri ya kusoma pia unabainika kutokana na ukweli kuwa kusoma angalau sehemu ya Qur'an ni jambo la msingi katika swala bora.

Hotuba ya kwanza iliyotolewa na Sulayman ibn Abdulmalik baada ya kuchaguliwa kuwa khalifa wa kwanza wa dola ya Umayyad ilikuwa kama ifuatavyo: "Waja wa Mwenyezi Mungu...Kifanyeni kitabu cha Mwenyezi Mungu kama muongozo. Zikubalini hukumu zake na myafanyie kazi maamrisha yake, kwani bila shaka Qur'an hutawanya mitego na mbinu za Shetani kama ambavyo mwangaza wa asubuhi unatawanya giza la usiku!" (Bayhaki Kitabu'z-Zuhd, uk. 61).

Kwa kuzingatia mambo yote inakuwa wazi kuwa kujenga mshikamano mzuri na Qur'an ni sehemu muhimu ya maisha. Hivyo hatuna budi kumuomba Mola wetu atumiminie ndani ya nyoyo zetu furaha ya maneno matakatifu. Ili kuwa na uhakika juu ya hili moja ya dua za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ilikuwa:

"Mola wangu...Kwa niaba ya kila jina miongoni mwa majina yako mazuri ambayo utakuwa umemfundisha mmoja wa waja wako kwa kumfunulia katika kitabu chako au kuyaficha kwako, ninakuomba uifanye Qur'an iwe chemchem ya moyo wangu, nuru ya kifua changu na tiba ya huzuni na machungu yangu!" (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, 1, 391).

#### **d. Kufanya ibada kwa umakinifu wa hali ya juu (*khushuu*)**

***"Muabuduni Mwenyezi Mungu kana kwamba mnamuona. Kwani hata kama nyinyi hamumuoni, kwa hakika Yeye anawaona!" (Bukhari, Iman, 37).***

Matendo ya ibada ni ushahidi wa utii juu ya makubaliano ya mwanzo kabisa yaliyofanyika kati ya mja na Mola wake. Kuabudu kunaashiria





nyakati ambazo mja yupo karibu zaidi na Mola wake kadiri nafasi ya utumishi unavyoruhusu. Huu ni ulimwengu wa kipekee. Kuondoa akilini mwake matatizo yote ya dunia humpelekea mja kutulia na kuimarisha roho yake kwa fikra bora za kufahamu kuwa hili ni moja ya jambo analolifanya kwa ajili ya Muumba wake. Takbir inayotolewa katika mwanzo wa kila swala inawakilisha jambo hilo; na kwa kunyanyua mikono yake kunampelekea mja kuweka nyuma yake kila kitu na kumgeukia Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake.

Kuabudu kunatoa tiba bora na utulivu kutokana na hofu ya kifo na zaidi ya hilo. Hili ni bustani la kiroho ambalo kwa kupitia hili kunapatikana njia ya kuelekea kwenye furaha ya milele; hii ni chemchem yenye kuvutia ambayo inatoa amani na utulivu wa roho, vyote hivi ni vitu ambavyo kamwe havitakiwi kupuuziwa.

Kufanya ibada kwa Khushuu au umakinifu wa hali ya juu ni sharti la kwanza kabisa litakalopelekea kupata matokeo yanayotarajiwa. Khushuu inahusiana na kuweza kusimama mbele ya Mwenyezi Mungu kwa moyo safi na uliotulia, huku ukiwa umegubikwa na hisia za mapenzi na hofu. Ili kumfikiria Mwenyezi Mungu peke yake pindi unaposimama mbele yake, huna budi kuweza kukata mawasiliano ya kitu kingine chochote na kuwa naye peke yake, huku ukitambua kuwa uliumbwa kwa lengo pekee la kumuabusu Yeye.

Ibada bora na nzuri kuliko zote ni swala. Swala ni moja ya zawadi kubwa kuliko zote ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu amempatia mwanaadamu. Hadith inasema: “Pepo imeandikwa (ni *wajib*) kwa ajili ya muumini ambaye huchukua udhu kamilifu na kuswali raka mbili kwa moyo na roho yake yote, huku akiwa na amani na umakinifu wa hali ya juu”. (Muslim, Taharah, 17). Swala ni moja ya kitu cha msingi katika kuboresha imani ya mtu. Swala ya namna hii huhitaji fikra ya kila kiungo, hata nafsi ya mtu, kila kiungo hakina budi kupoteza thamani yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kujizalilisha kwake.

Sulayman Darani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Kama ningelitakiwa kuchagua kati ya raka mbili za swala na pepo ya Firdaws ningelichagua raka mbili. Kuingia peponi ni jambo ambalo nafsi yangu ingelipenda sana, lakini kama nitaswali nitakuwa pamoja na Mola wangu”.





Wakati mtu yupo ndani swala hatakiwi kushughulishwa na kitu kingine chochote. Swala itaweka fikra zote nyingine pembeni. Wakati wa swala ambayo inaswaliwa sawa sawa, nyoyo hufunua mapazia yake na kuruhusu zimulikwe na nuru ya ukweli. Hiki kipindi kati ya mja na Mola wake ambacho hakiwezi kuelezewa. Raha hii hupatikana katika swala pekee na kamwe haiwezi kupatikana katika ibada nyingine yoyote. Kwa mfano mtu aliyefunga anaweza wakati huo huo kununua na kuuza sokoni na kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Vile vile ni hivyo hivyo kwa upande wa hijja. Lakini mtu ambaye yupo ndani ya swala hawezi kuuza wala kununua. Anachofanya ni kuswali peke yake. Lazima atakuwa yupo mbele ya Mwenyezi Mungu kiroho na kimwili.

Swala iliyoswaliwa kwa usahihi humuongozea imani muumini na kumuokoa asiangukie ndani ya mashimo ya matamano ya nafsi yake, na hivyo kumingizia utambuzi kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anamuan-galia katika kila hatua anayoipiga. Maneno yafuatayo kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – yanaligusia jambo hili:

“Muabuduni Mwenyezi Mungu kana kwamba mnamuona. Kwani hata kama nyinyi hamumuoni, kwa hakika Yeye anawaona!” (Bukhari, iman, 37).

“Kumbukeni mauti wakati mpo ndani ya swala, kwani kama mtu atakuwa anaswali na huku mauti yapo akilini mwake swala yake itakuwa nzuri na kamili. Swalini swala zenu kama mtu ambaye anafikiria kuwa hiyo ndiyo swala yake ya mwisho. Jiepusheni na kila kitu ambacho kitawasa-babishia majuto hapo baadae” (Darimi, Musnad, 1, 431)

Swala sahihi ni hii iliyoelezewa katika aya ifuatayo: “SOMA uliyo funuliwa katika Kitabu, na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu. Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa. Na Mwenyezi Mungu anayajua mnayo yatenda.” (al-Ankabut, 45).

Swala itamkinga mtu dhidi ya maovu ikiwa amani na umakinifu uliopatikana ndani ya swala utaendelezwa hata nje ya swala. Mtu ambaye haendelezi hali hii atakuwa haitekelezi swala yake vilivyo. Kuna onyo kali juu ya watu wa namna hii: “Basi, ole wao wanao sali, Ambao wanapuza Sala zao; Ambao wanajionyesha, Nao huku wanazuia msaada.” (al-Maun, 4-7). Kwa hiyo mtu ambaye anatekeleza ibada yake ya swala bila ya kukipa haki kila kitendo chake (tadilu'l-arkan), na ambaye hatambui kuwa yupo





mbele ya Mola wake na ambaye akili yake inashughulishwa na mambo yake mengine, asitarajie kuwa swala yake italeta matunda yanayotarajiwa. Swala ya namna hii ni sawa na kulipa deni chini ya kitisho kwa sababu hakuna budi. Ifuatavyo ndivyo namna ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anaielezea swala ya kweli na kamilifu: “Hakika wamefanikiwa Waumini, ambao ni wanyenyekevu katika Sala zao...” (al-Muminun, 1-2)

Swala aitwae Abdullah ibn Shihhir – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaielezea hali aliyokuwa nayo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - wakati alipokuwa anaswali: “Nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akiwa ndani ya swala. Sauti kama ile ya chungu chenye kuchemka ilikuwa ikitoka kifuni mwake kutokana na kulia” (Abu Dawud, Salat, 156-157; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, IV, 25). Pindi Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipokuwa anaswali alikuwa akififia rangi yake na kutupilia pembeni kila kitu, hata nyama yake mwenyewe. Kipindi fulani alipotaka kuchomolewa mshale ambao alichomwa vitani aliamua kuswali kwa kutambua kuwa hii ndiyo namna pekee ambayo ingelimfanya asisikie maumivu wakati wa kuondolewa mshale ule. Ni wangapi wana uwezo wa kuswali swala ambayo itakuwa imejitenga kabisa na dunia?

Baada ya kuyasema hayo wale ambao hawawezi kuswali kwa ukamilifu wa kiasi hicho wasiache kabisa kuswali. Kwani kila mtu ambaye ataendelea kuswali kawaida kwa namna ambaye atakuwa angalau amejivua deni la wajibu atakuwa amekaribia ukamilifu wa namna fulani.

Swala tano zilizoswaliwa katika nyakati maalum humuingiza mtu katika ratiba maalum za kila siku, kwa namna hiyo mtu atakuwa katika utaratibu mzuri wa maisha yake na kuhisi kuwajibika. Hakutakuwa na utulivu wa moyo, amani na usawa kwa mtu ambaye maisha yake yatakosa utulivu na utaratibu maalum. Cha zaidi ni kwamba swala hutoa ulinzi imara juu ya imani, humuongezea mtu mazingatio, humpa mtu utulivu katika nyakati za hofu na bidii katika nyakati za furaha. Swala ni aina ya ibada yenye msukumo na mafanikio ambayo huiamsha roho, huupa moyo furaha na nuru na huongeza mapenzi ya Mwenyezi Mungu.

Aina nyingine ya ibada ambayo hunyoosha maadili ya mtu kwa kuleta subira, uwezo na ukinzani dhidi ya matamano ya nafsi, sifa ambazo ni muhimu katika maisha ya mtu, ni kufunga (swawm)





Kutokana na malengo yake makuu kufunga ni kupambana na kikwazo ambacho ni nafsi kutokana na utambuzi wa kuwepo ndani ya ibada na kisha kuifunga na kupunguza ushawishi wake kwa kiasi kikubwa. Pamoja na kuwa na maadili mema kama vile subira, uvumilivu, kuridhika na matukio mbalimbali yanayokufika na kuvumilia magumu mbalimbali, lakini wakati huo huo kufunga nako kwa kupitia kujinyima na njaa humkumbusha mtu juu ya namna anavyoikumbuka mara chache thamani ya baraka takatifu ya chakula. Katika kuwapa ladha ya njaa wote matajiri na masikini hupelekea wawe katika hali moja. Husaidia kuwapa matajiri hisia za huruma kwa kuwakumbusha juu ya magumu wanayokutana nayo masikini na walio na fursa chache. Inawapelekea wote kuwa na hisia za shukurani.

Funga huhuisha hisia za uchamungu (taqwa) na kuongeza usafi wa moyo. Aya ifuatayo inasema: “Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu.” (al-Baqara, 183)

Katika kuifunza nafsi hakuna njia bora zaidi ya kufunga. Nafsi ni moja vitu vya kwanza vyenye kumfanya mtu avuke mipaka. Kuhusiana na kula kidogo ili kuweza kupata furaha ya milele kesho akhera Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Chakula halisi cha mtu ni upendo na hekima. Ndio maana si sawa kuulisha mwili kwa chakula kingi kupita kiasi”.

Mwanadamu yupo katika tabu kwa sababu amesahau chakula chake cha kiroho na ana wasiwasi juu ya chakula cha mwili wake. Huwa hatosheki. Amepauka kwa ajili ya tamaa, miguu yake inatetemeka na moyo wake unagonga kutokana na wasiwasi. Chakula cha hapa duniani kina thamani gani ukilinganisha na chakula cha milele? Kuhusiana na mashahidi Mwenyezi Mungu amesema, ‘Wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.’<sup>14</sup> Katika chakula hicho cha kiroho hakuna mdomo wala mwili kwa ajili yake.

Ili kupata ukweli wa funga na kunufaika nayo kikamilifu hakuna budi mtu kujizuia na kupuuzia mambo yenye kuiharibu. Hadith ifuatayo inasema: “Funga haihusiani na kuacha kula na kunywa pekee. Funga bora na yenye malipo ni ile iliyofungwa kwa kupitia kuachana na maongezi na

14. Al-i Imran, 169.





matendo ya kupuuzi na maneno machafu. Kama mtu atakufanyia ubaya wowote mwambie, ‘Mimi nimefunga’” (Hakim, Mustadrak, I, 595).

Pia jambo lingine la faradhi kinyume na funga ambalo litakuwezesha kujiepusha na matamano ya nafsi ni utoaji wa zaka. Malengo makuu ya kutoa zaka ni kuondoa uvukaji mipaka unaotokana na kumiliki kiasi kikubwa cha mali, pia kuondoa hisia za kinyongo na wivu kutoka kwa masikini na hivyo kusababisha maisha ya jamii yenye upendo. Katika utaratibu wa jamii ya kiislamu kutoa zaka na sadaka (*infaq*) ni njia muhimu mno katika kuleta upendo kati ya masikini na matajiri na kufuta hisia mbaya kati yao. Matajiri wataitwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kuulizwa ni kwa namna gani walipata fedha zao na wapi walizitumia na wataulizwa ikiwa walitoa zaka na sadaka. Kutokana na kuhitajika kutoa sehemu ya mali yake na kuwapa masikini kunapelekea tajiri kuwa katika mtihani mkubwa wa kifedha. Hivyo kufaulu mtihani huu na kutekeleza majukumu mengine ya kiutumishi hupelekea kupata baraka za Mola na kuingia peponi.

Umuhimu wa kutoa zaka uliotajwa mara kadhaa ndani ya Qur’an unadhihirishwa na ukweli kwamba kutoa zaka kumetajwa mara 27 sambamba na swala ambayo ndiyo nguzo kuu ya dini. Zaka ni deni walilionalo matajiri juu ya masikini. Qur’an inasema: “Na katika mali yao ipo haki ya mwenye kuomba na asiye omba” (ad-Dhariyat, 19). Hivyo kutoa zaka ni desturi ya kutenga kiasi fulani cha mali ambacho kinafikia kiwango maalum (*nisab*) kama kodi ili kufanya kiasi kilichobakia kuwa halali. Hivyo sehemu inayotengwa hupelekwa kwa masikini walio ndani ya jamii. Kwa namna hii si tu kwamba mali za matajiri zitatakaswa dhidi ya uchafu bali kutapatikana usawa wa kijamii, haki na utulivu. Tukiangalia aya ifuatayo tutatosheka na kuweza kukubaliana na ukweli huu: “Hakika amekwisha fanikiwa aliye jitakasa (*tazakkaa*)...” (al-Ala, 14). Kiuhalisia neno *zakat* linamaanisha tazkiya, kwa maneno mengine kutakasa.

Kutoa zaka ni deni la chini ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuwajibishia tajiri. Kinyume chake hakuna kikomo katika kutoa sadaka, na kama ilivyo kwa upande wa funga, malipo yanayowangojea wale waliotoa sadaka kwa hiari yao yamefichwa ili kuwashawishi matajiri watoe zaidi. Kinyume na nyumati zilizotangulia Mwenyezi Mungu huwahesabia watu wa *ummah* wa Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake –







kosa moja kwa kila dhambi wanayoitenda na thawabu kumi kwa kila jema wanalolitenda. Kwa kuongezea ni kwamba kuna matendo mengine ambayo yana malipo mara mia saba, hata zaidi ya hapo. Lakini malipo ya funga na sadaka yamefichwa. Kuhusiana na hili Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe na uwatakase kwazo, na uwaombe rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua” (at-Tawbah, 103).

Ni wazi kutoka kwenye aya kuwa kutoa zaka na sadaka hutakasa mali na moyo. Pia Mwenyezi Mungu Mtukufu anawatahadharisha wale wanaojizua kutoa wakati wana uwezo wa kufanya hivyo katika aya ifuatayo:

“Enyi mlio amini! Hakika wengi katika makuhani na wamonaki wanakula mali za watu kwa baat’ili na wanazuilia Njia ya Mwenyezi Mungu. Na wanao kusanya dhahabu na fedha, wala hawazitumii katika Njia ya Mwenyezi Mungu, wabashirie khabari ya adhabu iliyo chungu. Siku zitapo tiwa moto katika Moto wa Jahannamu, na kwazo vikachomwa vipaji vya nyuso zao na mbavu zao na migongo yao, wakaambiwa: Haya ndiyo mlio jilimbikia nafsi zenu, basi onjeni mliyo kuwa mkilimbika” (at-Tawba, 34-35).

Kutokana na kuingiza moyoni mapenzi ya mali, hupelekea kuzuia utoaji wa sadaka na kwa kufanya hivyo masikini wanakuwa wamenyimwa haki zao. Na jambo hili hupelekea kuwa na mwisho mbaya kama ambavyo imeelezwa katika aya iliyopita.

Ni aina mbili tu za baraka, yani watoto na mali, ndizo zilizotajwa kuwa *fitnah*, au sababu ya kuangamia. Mapenzi ya kupita kiasi juu ya vitu yanaweza kuzama ndani ya moyo na kuutawala, jambo ambalo ni hatari kama alivyotukumbusha Mwenyezi Mungu Mtukufu: “Hakika mali yenu na watoto wenu ni jaribio. Na kwa Mwenyezi Mungu upo ujira mkubwa.” (at-Taghabun, 15).

Kwa kuzuia ukuaji wa mapenzi kupita kiasi juu ya vitu hivi na kuviweka nje ya moyo hapo mtu ataweza kuzuia mapenzi juu ya watoto na mali kuwa *fitnah*. Kutekeleza sharti takatifu la kutoa zaka na sadaka kutaweza kufanyika baada ya kuzuia mapenzi juu ya mali yasije yakaingia ndani ya moyo, kwa kutambua kuwa mali ni kitu ambacho amejaliwa mtu mpaka muda maalum. Kwa hiyo mtu hana budi kutafakari kwa kina juu ya tahadhari tukufu ambayo sehemu yake imetolewa hapo juu na kujitahidi kutoa





zaka ambayo itamuwezesha kupita kiasi cha chini cha utoaji zaka. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَيَسْأَلُونَكَ مَاذَا يُنْفِقُونَ قُلِ الْعَفْوَ

“Na wanakuuliza watoe nini? Sema: Kilicho chepesi...” (al-Baqara, 219).

Matajiri ambao ni wakarimu na wenye kushukuru na masikini ambao ni wenye subira na utu hupata heshima na radhi za Mwenyezi Mungu. Kinyume chake matajiri wenye majivuno na ubahili na masikini wasio na subira na matokeo yake wakaasi ni wenye kulaumiwa sana.

Kutoa zaka ni kuonyesha shukurani kwa wale wenye kumiliki mali. Na ahadi takatifu kuwa shukurani haiongezi kingine kinyume na baraka. Katika hili Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

لَئِنْ شَكَرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ

“Mkishukuru nitakuzidishieni...” (Ibrahim, 7).

Utoaji wa sadaka ulikuwa ni jambo ambalo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akilipenda sana na kulihamasisha kwa wengine. Anasema: “Ewe mwana wa Adam...toa sadaka ili na wewe uhurumiwe...” (Bukhari, Nafaqat, 1).

Kipenzi chetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akipenda ukarimu uwe ni sehemu ya tabia ya muislamu. “Watu wa namna mbili pekee ndio wakuonewa wivu”, anasema. “Wa kwanza ni yule aliyejaaliwa mali na Mwenyezi Mungu na akajaaliwa kuitumia katika njia Yake, na mwingine ni yule aliyejaaliwa elimu ambayo anaifanyia kazi na kuwafundisha wengine (Yule anayetoa sadaka kwa kupitia elimu yake)” (Bukhari, ilm, 15).

Kwa ufupi ni kwamba kwa kawaida mwanadamu ameegemea kwenye dunia. Nafsi huona utajiri wa hapa duniani ni wenye kuvutia. Wale walio-danganywa na nafsi kamwe hawawezi kutosheka. Kadiri wanavyopata mali zaidi ndivyo wanavyokuwa na tamaa zaidi juu ya mali. Huruma na upendo huondoka pindi unapotekwa na njaa ya mali. Hivyo kutoa sadaka kunakuwa ni jambo gumu mno kwako. Mtu wa namna hiyo anakuwa hana kizuizi





dhidi ya ulaghai wa nafsi yake ambayo inamshawishi, “Tafuta mali zaidi ili uwe tajiri. Utatoa sadaka baadae!”. Kadiri mtu wa namna hii atakavyokuwa anafurahia utulivu wa kiwiliwili chake lakini kiroho atakuwa ni mgonjwa. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Wale wenye kuahirisha wameangamia”. Hivyo *zakat* ni tiba bora ya tamaa ya dunia ambayo ndiyo maradhi ya hatari ya moyo.

Imeelezewa ndani ya Qur’an kuwa wakati wa kukata roho mtu hupata fahamu upya kana kwamba ameamka kutoka kwenye ndoto na anaomba kwa majuto makubwa:

رَبِّ لَوْلَا أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ أَجَلٍ قَرِيبٍ فَأَصَّدَّقَ وَ أَكُنُ مِنَ الصَّالِحِينَ

“Na toeni katika tulicho kupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu mauti, tena hapo akasema: Mola wangu Mlezi! Huniakhirishi muda kidogo nipate kutoa sadaka, na niwe katika watu wema?” (al-Munafiqun, 10).

Pia adabu hufikia mahala pake pindi unapotoa zaka na sadaka. Hasa mtoaji hana budi kuonyesha hisia za shukurani kwa mpokeaji kwa kumpa fursa ya kulipa deni la lazima kwake. Wakati huo huo sadaka iliyotolewa huwa kinga kwa mtoaji dhidi ya maradhi na bahati mbaya. Katika kusisitiza utoaji kwa ajili ya masikini kwa moyo safi aya ifuatayo inasema:

“Je! Hawajui ya kwamba Mwenyezi Mungu anapokea toba ya waja wake, na anazikubali sadaka, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kupokea toba na Mwenye kurehemu?” (at-Tawba, 104).

“Enyi mlio amini! Msiharibu sadaka zenu kwa masimbulizi na maudhi, kama anaye toa mali yake kwa kuwaonyesha watu, wala hamuamini Mwenyezi Mungu wala Siku ya Mwisho. Basi mfano wake ni kama mfano wa jabali ambalo juu yake pana udongo, kisha likapigwa na mvua kubwa, ikaliacha tupu. Basi hawatakuwa na uweza wowote kwa walivyo chuma. Na Mwenyezi Mungu hawaongoi watu makafiri” (al-Baqara, 264).

Viumbe vyote vinaishi na kubakia hai chini ya usimamizi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa kupitia ubadilishaji wenye kuendelea (*isti-halah*) wa kiasi kikubwa cha udongo hapa duniani, Mwenyezi Mungu Mtukufu huabadilisha na kuwa ghala la kulishia kiasi kikubwa mno cha viumbe. Je wanadamu si wa kipekee miongoni mwa viumbe wengine





kutokana na kujaaliwa akili na utambuzi? Je hawaoni na kutambua kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndiye anayewalisha viumbe wote bila ya ubaguzi, bila ya kubagua kuwa wao ni waumini ama makafiri, ni wenye nguvu ama madhaifu? Na tafakari juu ya je mali zao wanazitumia kwa ajili ya nani wengine?

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameumba ulimwengu mzima kutokana na upendo, kutokana na upendo huu ndipo akawajaalia baraka za rehema zisizo na kifani. Muhanga ndio zao halisi la upendo. Mpenzi huchukulia kujitolea muhanga kwa ajili ya kipenzi chake kama jukumu lenye kupendeza kwake, na hata anaweza kutoa uhai wake kama itabidi. Kwa kufanya hivyo hataona hata kidogo kuwa kitendo chake hicho ni muhanga mgumu kwake. Kunaweza kusemekana kuwa kwa upande wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ukarimu kwa viumbe vyake ndio udhihirisho mzuri juu ya Mpenzi kwa kipenzi chake.

Pamoja na ibada hii ya kifedha pia kuna ibada ya hijja ambayo ni ya kiroho na kimwili. Hili ni tukio tukufu lenye kuamsha kumbukumbu za huzuni tokea Mtume wa kwanza Adam (a.s) mpaka Mtume wa mwisho – rehema na amani ziwe juu yake, si kwamba tukio hili linaleta ukamilifu moyoni bali kutokana na kitendo cha ufufuo mkubwa waumini hupata funguo za siri ambayo ni: “Kufa kabla hujafa!”

Hijja ina hekima kubwa kwa ajili ya hapa duniani na kesho akhera. Hijja ya kweli ni tukio tukufu la ibada, tukio ambalo waislamu waliosamehewa kwa kupitia rehema za Mola hukutana kwa pamoja huku wakiwa na shauku kubwa juu ya imani ya hali ya juu na mapenzi. Hijja inahusiana na kuvua mavazi ya uwepo na kutafuta njia ya kutoka kwenye dhoruba ya nafsi kwa kuzama ndani ya vina vya roho. Hijja ni ibada ambayo kwa kiasi kikubwa inaleta udhihirisho wa kiroho, ambapo mtu hurudisha utulivu na sura ya roho yake ambayo ndiyo mkazi wa kweli, na hapo ndipo anaporudisha utambulisho wake wa msingi na alichokuwa anakitafuta, kwa kuwa moyo wake utakuwa umesafishwa kwa mvua kubwa ya uongofu wa kiroho.

*Kaaba* ambayo ndicho *qibla*, yani uelekeo wa ibada kwa ajili waumini, ni kiini cha swala, swala ambayo maagizo yake yametolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kusema: “Nawe sujudu na ujongee!” (al-Alaq, 19). Huu ndio uelekeo wa waislamu wote, ndipo sehemu ambayo moyo wa ulimwengu wa kiislamu unapogonga. Ndani ya wanadamu moyo ndiyo





sehemu ambayo uoni mtakatifu unajidhihirisha wenyewe, wakati katika ulimwengu sehemu hiyo ni *Kaaba*. Kwa maana hiyo Kaaba ni kwa ajili ya ulimwengu kama ambavyo moyo ni kwa ajili ya mwanadamu. Kwa hiyo hijja ni kitendo cha ibada ambacho kinahitaji moyo wenye umakini mkubwa na usahihi pamoja na kuthamini mvuto wa *Kaaba*. Kutokana na kujawa na ubainifu wa upendo na huruma ratiba nzima ya hijja huupeleka moyo kwenye umakini wa hali ya juu, jambo ambalo linatoa mfano mzuri wa kujiweka mbali na kudhuru viumbe vya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Huku wakiwa wamevalia *ihram* nyeupe, hijja ni kitendo chenye kuja-ribu kupata mgao wa werevu wa malaika kana kwamba wanawaiga. Mtu akiwa kwenye *ihram* hatakiwi kuwinda au kuchuma majani na magugu, au hata kuondoa kipande cha nywele kwa kukusudia. Kunakuwa hakuna *rafath*, hakuna *fisq*, hakuna *jidat*...<sup>15</sup> bali upendo, huruma na upole juu ya viumbe wengine kwa ajili ya Muumba.

Kusisahaulike kwamba mauti ni jambo lisilokwepeka na kiumbe yeyote yule. Muda wake halisi tayari umeshapangwa, zimeshaandika hata dakika halisi na pumzi za kuvuta mpaka kifo kikukute. Ni jambo la uhakika kwamba kuahirisha kifo au kukisogeza mbele hakuwezekani hata kidogo; wala hakujapata kusikika habari yoyote ya mtu aliyewahi kukwepa kifo. Hivyo wale wenye uwezo wa kutekeleza hijja hawana budi kutafakari kwa kina jambo hili na kujizuia na tabia ya uzembe na ubwege. Kinyume chake watakutana na tahadhari kali ifuatayo kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake:

“Hakuna kitu kitakachomzuia mtu kufa akiwa yahudi au mkiristo pale atakapoacha kutekeleza ibada ya hijja na huku ana uwezo wa kifedha wa kutosheleza gharama za chakula na usafiri” (Tirmidhi, Hajj, 3).

Tahadhari hii ya Mtume inasisitiza kwamba wale wenye kupuuzia kutekeleza hijja, si kwa kuwa hawana uwezo wa kifedha bali kutokana na uzembe, basi wapo katika hasara kubwa na wameandaliwa adhabu kali, labda waamue kujirekebisha. Kwa hakika ni upuuzi usioelezeka kwa waislamu kutotambua umuhimu wa hijja, ibada ambayo ndio fursa kubwa ya kuweza kutakasa nyoyo zao na kufuta madhambi yao.

15. Rejea al-Baqara, 197. *Rafath*: Kufanya jimai, kuzungumzia jimai au aina yoyote ya maneno mabaya. *Fisq*: Aina yoyote ya uovu. *Jidat*: Kujihusisha katika maongezi ya upuuzi.



Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema: “Yeyote atakayeitembelea Al-Kaaba kwa nia ya hijja na kuikamilisha bila ya kushiriki kwenye fisq au rafath basi atarejea nyumbani kwake huku akiwa msafi kama siku aliyozaliwa” (Muslim, Hajj, 438).

#### e- Kuhuisha nyakati za usiku

*Ijaze kwa hiyo divai, imimine tena,  
Jaalia usiku usimame, usimamishe usiku,  
ninakusihhi sana!  
Ufunge minyororo usingizi wangu na uudhibiti  
vilivyo; jaalia muda huo usipite,  
Kamwe walalaji hawausifu usiku,  
usiku ambao kamwe hawaudhibiti.*

Kujipima na kudharau uzito wa kiroho na kimwili katika siku huwezekana baada ya kujigubika mwenyewe ndani ya ukimya tulivu wa usiku. Nyakati za mchana haziwezi kutoa utulivu wa kiroho na kimwili ambao unapatikana katika nyakati za usiku. Wale ambao hawauthamini usiku kamwe hawawezi kufahamu thamani ya mchana. Pindi usiku unapoingia hupatikana hitajio la kuuhuisha.

Kwa watu wenye hekima kamwe hakuna wakati unaowavutia zaidi ya utulivu wa usiku. Hivyo kutumia sehemu ya usiku ukiwa macho ni jambo muhimu lenye na kukupelekea kupata matunda yake. Aya zifuatazo zinasema yafuatayo kuhusiana na hili:

تَتَجَافَى جُنُوبُهُمْ عَنِ الْمَضَاجِعِ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ خَوْفًا وَ طَمَعًا  
وَ مِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ

“Mbavu zao zinaachana na vitanda kwa kumwomba Mola wao Mlezi kwa khofu na kutumaini, na hutoa kutokana na tulivyo waruzuku” (as-Sajda, 16).

“Na likumbuke jina la Mola wako Mlezi asubuhi na jioni; Na usiku msujudie Yeye, na umtakase usiku, wakati mrefu” (al-Insan, 25-26).





Mwenyezi Mungu Mtukufu amezipa thamani kubwa nyakati za usiku na ameweka siri kubwa ndani yake. Siri iliyopo katika viapo vyake juu ya nyakati za usiku kama pale aliposema, “Na kwa usiku unapo pungua, Na kwa asubuhi inapo pambazuka...” (at-Takwir, 17-18) ni kama vile madirisha matakatifu yaliyofunguliwa kwa ajili ya nyoyo zetu na uelewa wetu ili tuweze kutambua thamani yake.

Waumini waliokomaa huziangalia nyakati za usiku kama hazina kubwa kutokana na utulivu wake na uongofu wa kiroho uliojificha ndani yake. Wale wenye kuweza kutambua thamani ya hazina hii huona nyakati za usiku kuwa nyakati muafaka za kumuelekea Mola kwa dua na ibada nyingine kwa moyo wao wote, hizi ni nyakati ambazo watu wengi huwa wamepumzika.

Katika *Divan-i Kabir* Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anatoa ushairi juu ya upendo na raha anayokuwa nayo wakati wa usiku:

*Lijaze bilauri la mtumishi kwa mapenzi matakatifu  
Usitaje chochote kuhusiana na mkate mbele ya msheherekeaji wa divai  
Toa kawthar na kuzikinaisha nyoyo zote zenye kiu  
Ni sehemu gani nyingine zaidi ya maji ambayo samaki angependa kuogelea?  
Ijaze kwa hiyo divai, imimine tena,  
aalialia usiku usimame, usimamisha usiku, ninakusihani sana!  
Ufungue minyororo usingizi wangu na uudhibiti vilivyo; jaalia muda huo usipite  
Kamwe walalaji hawausifu usiku, usiku ambao kamwe hawaudhibiti...<sup>16</sup>*

Kuhusiana na waja wake waliobahatika na ambao wanastahiki kupata baraka tele kesho akhera kutokana na kumuogopa Yeye kwa kuamka katika nyakati za usiku na alfajiri, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

كَانُوا قَلِيلًا مِّنَ اللَّيْلِ مَا يَهْجَعُونَ وَبِالْأَسْحَارِ هُمْ يَسْتَعْفِرُونَ

“Walikuwa wakilala kidogo tu usiku. Na kabla ya alfajiri wakiomba maghfira” (ad-Dhariyat, 17-18).

“Na wale wanao kesho kwa ajili ya Mola wao Mlezi kwa kusujudu na kusimama” (al-Furqan, 64).

16. Imetolewa kwenye tafsiri ya kituruki ya *Divan-i Kabir* ya Profesa Emin Isik kutoka chuo kikuu cha Marmara, kitengo cha Utakatifu.



Na katika aya nyingine Mwenyezi Mungu Mtukufu anatufahamisha yafuatayo:

“...Ambaye anakuona unapo simama, na mageuko yako kati ya wanao sujudu” (as-Shuara, 218-219).

Qadi Baydawi anasema yafuatayo Kuhusiana na aya hii: “ Pindi swala tano zilipokuwa faradhi na swala za usiku kuwa *sunnah* Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – alitoka chumbani kwake usiku na kwenda kuwachunguza maswahaba. Alikuta nyumba zao zikitoa sauti za Qur’an, *dhikr* na *tasbih* kana kwamba ni mizinga ya nyuki” (Anwaru’t-Tanzil, IV, 111).

Ukilinganisha na nyakati nyingine Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweka thamani kubwa katika *dhikr* zinazofanywa alfajir kama ambavyo ilivyo vigumu kwa watu kufanya *dhikr* na ibada nyingine katika nyakati za alfajir ukilinganisha na nyakati nyingine. Hiyo ndiyo sababu inayopelekea kuhuisha nyakati za usiku kuwa dalili ya upendo na unyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kadiri mapenzi matakatifu yanapoongezeka ndani ya moyo, ndivyo mtu anavyokuwa na hamu kubwa ya kuamka usiku kwa ajili ya swala na *tasbih*. Kwa hiyo kuamka usiku kwa ajili ya swala na *tasbih* ni kama kukutana na kipenzi chako. Kuwa macho wakati watu wengine wamelala fofofu kunaashiria kuwa miongoni mwa waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu waliobahatika kuingizwa katika chumba cha rehema zake, mapenzi yake na elimu yake.

Kwa muumini ambaye anautumia usiku kwa malengo mazuri na kwa usahihi na kunufaika na faida za kiroho za *dhikr* za alfajir inamaanisha kuwa nyakati zake za usiku zitakuwa ni zenye kuangaza zaidi kiroho kuliko mchana. Lakini zile nyakati za usiku zilizotumika bila malengo kinyume na kulala peke yake huwa ni hasara isiyoweza kufidiwa kama vile matone ya mvua yanapodondoka juu ya miamba, baharini na jangwani, kisha yakapotea papo kwa hapo. Kama tutaruhusu masaa yetu na nyoyo zetu zigubikwe na imani ya *tawhid* ambayo inaanza alfajir, basi wakati wa kuiga dunia na kutoa pumzi ya mwisho -*insha-Mwenyezi Mungu*- utakuwa kama *shab-i arus*<sup>17</sup>.



17. *Shab-i arus*: Kiuhalisia ni usiku wa harusi lakini hapa linamaanisha kukutana na Mola.





Abdullah ibn Amr ibn As – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anakumbusha na Mtume aliyebanikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alivyomtahadharisha:

“Usiwe kama fulani na fulani ambao walikuwa wakiamka usiku kwa ajili ya ibada lakini kwa sasa hawafanyi hivyo” (Bukhari, Tahajjud, 19; Muslim, Siyam, 185).

Pia kipenzi wetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – amenukuliwa kuwa aliwaamba maswahaba zake: “Jitahidini kufanya ibada za usiku, kwani hiyo ilikuwa desturi ya watu wema waliotangulia. Bila shaka kuamka usiku kwa ajili ya ibada ni sababu ya kuwa karibu zaidi na Mwenyezi Mungu. Kunamlinda mtu dhidi ya madhambi, humuepusha mtu na makosa na kumuweka mtu mbali na maumivu ya mwili” (Tirmidhi, Daawat, 101). Pia faida za kiafya za kutolala usiku mzima na badala yake kuamka mara kwa mara katika nyakati za usiku ni jambo lililothibitishwa kitiba. Mara nyingi pindi mtu anapolala kwa muda mrefu bila ya kukatiza usingizi huwa anaamka kichwa kikiwa kinamuuma. Hili linasababishwa na ubongo kukosa hewa ya oksijeni ya kutosha wakati wa kulala kutokana na upumuaji wa taratibu. Hivyo kuugawa usingizi husaidia kurudisha kasi ya upumuaji katika hali yake ya kawaida; na wanaofanya hivyo huamka asubuhi wakiwa wachangamfu licha ya kulala kidogo.

Pia ni jambo la kuzingatia kwamba mara nyingi **mauti** humfika mtu **katika masaa ya mwanzo** ya asubuhi. Jambo hili huwatokea sana sana wazee. Hivyo baadhi ya madaktari wameiita alfajir kuwa ni ‘saa ya kifo’ kwa sababu huo ni wakati ambao usingizi ni mzito kabisa na mapigo ya moyo yako chini kabisa, baada ya mtu kuamka na kuchukua udhu kwa maji ya baridi shughuli zote za kimwili hurejea katika hali yake ya kawaida. Ingawa maamrishi ya uislamu yamegemea katika kumfahamisha mwanadamu juu ya jukumu lake la utumishi wake kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, lakini kila moja wapo huja na manufaa ya kimwili. Vile vile swala, fungu na ibada nyingine ziko Vivyo hivyo, zote zina hekima na manufaa makubwa mno. Lakini kwa kawaida manufaa hayo si sababu za kuwepo ibada hizo bali ni faida za ziada.





#### f- *Dhikrullah na Muraqaba*

**‘...Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua’ (ar-Rad, 28)**

Inasemekana kwamba neno *insan* ambalo ni neno la kiarabu lenye kumaanisha ‘mtu’ limetokana na neno *nisyan* lenye kumaanisha usahaulifu. *Nisyan* ni kinyume cha *dhikr* au ukumbusho; na sifa hiyo inaashiria udhaifu mkubwa kuliko yote kwa mwanadamu. Kimazungumzo jambo hili limewakilishwa na maneno “Kumbukumbu ya mwanadamu huathiriwa na usahaulifu” (Hafiza-yi beser nisyan ile maluldur). Njia bora ya kupunguza usahaulifu kwa kiasi kikubwa ni ‘kukumbuka’ kwa kupitia *dhikr*.

Ili kuishi kulingana na sababu ya kuumbwa roho haina budi kutunza ahadi iliyotoa kwa Mola kule Bazm-i Alast<sup>18</sup>, na kamwe mtu asitoe fikra za Muumba wake ndani ya moyo wake na akili yake. Matokeo yake ili kurekebisha ubovu uliotokana na usahaulifu ambao ni kasoro iliyopo ndani ya silka ya mwanadamu, kunahitajika *dhikr* ambayo huhuisha utambuzi juu ya ‘Mwenyezi Mungu’ na ‘utumishi’ wa mja; kwani kila kitendo cha kumkumbuka Mwenyezi Mungu kinaimarisha fikra na utambuzi juu ya Yule anayekumbukwa. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu haangalii sura ya mtu bali anaangalia moyo wake. Kwa hiyo muumini hana budi kuchukua jukumu la kuulinda moyo wake dhidi ya kupuuzia mambo na kujipamba na utajo mtakatifu, kwani moyo ndio kitovu cha Jicho takatifu.

Kutokana na umuhimu wake ndani ya majukumu ya kiutumishi neno *dhikr* limetajwa katika zaidi ya sehemu 250 ndani ya Qur’an. Hivyo utumishi sahihi mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kupelekea kufikia *marifatullah* kunategemeana na nafasi ya *dhikr* ndani ya moyo na uzito wa hisia zake ndani ya moyo. Hii ndiyo sababu inayofanya *marifatullah*, yani kumtambua Mola kwa kupitia moyo, kuchukuliwa kuwa elimu tukufu kuliko zote. Hata hivyo hii ndiyo ‘ile’ elimu ambayo wanadamu wote wanahitaji. Ili kuwafanya waja wake wasishindwe kupata faida zinazopatikana katika *dhikr*, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema:

18. *Bazm-i Alast*, au makutano ya roho katika wakati usiokumbukwa, ni pale roho zote zilipokiri Uungu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kujibu swali la Mwenyezi Mungu, “Je, Mimi si Mola Mlezi wenu? Wakasema: Kwani! Tumeshuhudia” Angalia al-Araf, 172.





أَلَمْ يَأْنِ لِلَّذِينَ آمَنُوا أَنْ تَخْشَعَ قُلُوبُهُمْ لِذِكْرِ اللَّهِ  
وَمَا نَزَلَ مِنَ الْحَقِّ

“Je! Wakati haujafika bado kwa walio amini zikanyenyekela nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu na haki iliyo teremka? Wala wasiwe kama walio pewa Kitabu kabla yao, muda wao ukawa mrefu, kwa hivyo nyoyo zao zikawa ngumu, na wengi wao wakawa wapotovu” (al-Hadid, 16).

“...Na kwa yakini kumdhukuru Mwenyezi Mungu ndilo jambo kubwa kabisa” (al-Ankabut, 45).

“Basi nikumbukeni nitakukumbukeni, na nishukuruni wala msinikufuru” (al-Baqara, 152).

“Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara zangu, wala msichoke kunikumbuka” (Taha, 42).

Kumkumbuka na kumtaja Mwenyezi Mungu Mtukufu si kutaja jina lake kwa mdomo tu, bali inatakiwa utajo mtakatifu uingie ndani ya moyo ambao ndio kitovu cha imani. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Tofauti kati ya yule anayemkumbuka Mwenyezi Mungu na yule asiyemkumbuka ni kama tofauti kati ya mtu aliye hai na maiti” (Bukhari, Daawat, 66).

“Dalili ya kumpenda Mwenyezi Mungu ni kupenda *dhikr*” (Suyuti, al-jamiu’s-Saghir, II, 52).

Wale waliojiweka mbali na utajo wa Mwenyezi Mungu wanaingia kwenye tishio la Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani kwa kufanya hivyo wanakuwa wamejitoa kwenye mapenzi ya Mola. Qur’an inasema: “Je! Yule ambaye Mwenyezi Mungu amemfungulia kifua chake kwa Uislamu, na akawa yuko kwenye nuru itokayo kwa Mola wake Mlezi (ni sawa na mwenye moyo mgumu?) Basi ole wao wenye nyoyo ngumu zisio mkumbuka Mwenyezi Mungu! Hao wamo katika upotofu wa dhaahiri” (az-Zumar, 22).

Ulazima wa kuwa katika hali ya ukumbusho mtakatifu ambao unatoa ulinzi dhidi ya matokeo ya tishio hili umebainishwa kama ifuatavyo:





“Na mkumbuke Mola Mlezi wako nafsini kwako kwa unyenyekevu na khofu, na bila ya kupiga kelele kwa kauli, asubuhi na jioni. Wala usiwe miongoni wa walio ghafilika” (al-Araf, 205).

Kwa mara nyingine tena Mwenyezi Mungu Mtukufu anatuonya dhidi ya hatari ya kujiweka mbali na *dhikr*.

“Anaye yafanyia upofu maneno ya Rahmani tunamwekea Shet’ani kuwa ndiye rafiki yake. Na hakika wao wanawazuilia Njia na wenyewe wanadhani kuwa wameongoka. Hata atakapo tujia atasema: Laiti ungeli kuwako baina yangu na wewe kama umbali baina ya mashariki na magharibi. Rafiki mwovu mno wewe!” (az-Zukhruf, 36-38).

“Na atakaye jiepusha na mawaidha yangu, basi kwa yakini atapata mai-sha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama tutamfufua hali ya kuwa kipofu. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu, nami nilikuwa nikiona? (Mwenyezi Mungu) atasema: Ndivyo vivyo hivyo. Zilikufikia ishara zetu, nawe ukazisahau; na kadhaalika leo unasahauliwa” (Taha, 124-126).

“Zinamtakasa zote mbingu saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye maghfira” (al-Isra, 44).



Kuhusiana na thamani ya kukusanyika kwa ajili ya *dhikr* Mtume Mtukufu – rehemu na amani ziwe juu yake - anasema yafuatayo ndani ya *hadith al-qudsi*:

“Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: Mimi humlipa mja wangu kulingana na kile anachonifikiria. Pindi anaponikumbuka na Mimi huwa pamoja naye. Kama atanikumbuka kimya kimya, na Mimi pia nitamkubwa Vivyo hivyo. Kama atanitaja mbele za watu na Mimi pia nitamtaja mbele ya kundi bora kuliko lake” (Bukhari, Tawhid, 15).

Siku moja Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – alipokuwa anawahutubia maswahaba zake aliuliza:

“Je niwafahamishe amali iliyo safi zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu, iliyo juu katika daraja, iliyo bora kuliko sadaka iliyotolewa kwa dhahabu na fedha, iliyo bora kuliko kupambana na maadui na nyinyi mkawachinja au





wao wakawachinja?” “Tafadhali tufahamishe ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu”, walijibu, baada ya hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alisema:

“Amali hiyo ni utajo wa Mwenyezi Mungu” (Tirmidhi, Daawat, 6).

*Dhikrullah* au utajo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu unaweza kufanywa ukiwa peke yako au mkiwa katika kundi.

Muawiya – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alianza kuelezea. “Hakuna mtu aliyekuwa karibu mno na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – kama nilivyokuwa mimi licha ya kwamba nimesimulia machache mno kutoka kwake. Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipolikaribia kundi la maswahaba zake waliokuwa wamekaa na kutengeneza duara aliwauliza:

‘Kwa nini mmekaa hapa?’

‘Tumekaa hapa kwa ajili ya kumshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu kutokana na kutubariki kwa neema kubwa ya uislamu’, wale maswahaba walijibu.

‘Kwa jina la Mwenyezi Mungu semeni ukweli. Ni kweli mmekaa hapa kwa sababu pekee ya kumtaja Mwenyezi Mungu?’ Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – aliuliza tena.

‘Ndio, kwa jina la Mwenyezi Mungu hiyo ndiyo sababu pekee’, walijibu, baada ya hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:

‘Si kwamba nililirudia swali langu kwa kuwa siwaamini. Bali Jibril alinijia na kunitaarifu kwamba Mwenyezi Mungu anawasifu mbele ya malaika Zake. Ndio maana niliongea kwa namna hiyo” (Muslim, Dhikr, 40).

Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiwaelekeza maswahaba zake kwa aina mbalimbali za *dhikr* kulingana na uwezo wao. Mfano mzuri juu ya hili ni ushauri wake kwa binamu yake Ummu Hani – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye alikuwa mtoto wa kike Abu Twalib.

“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nimeshakuwa mzee na dhaifu”, Ummu Hani alisema. “Je unaweza kunishauri kitendo cha ibada ambacho ninawe-





za kukifanya pindi ninapokuwa nimekaa?” Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akasema:

“Sema Subhanallah mara mia moja, Alhamdulillah mara mia moja na La Ilaha ill-Mwenyezi Mungu mara mia moja” (Ibn Maja, Adab, 56; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, VI, 344).

Miongoni mwa aina zote za *dhikr*, kusema *La ilaha ill-Mwenyezi Mungu (kalima-i tawhid)* katika kikundi kunashika nafasi ya peke yake, kama ambavyo inaashiria *hadith* ifuatayo iliyosimuliwa na Shaddad ibn Aws – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

“Siku moja tulipokuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – alituuliza, ‘Je kuna mgeni miongoni mwetu?’ Aliposema mgeni alimaanisha mtu wa kitabu (Mkristo au myahudi).

‘Hapana, hakuna mtu wa aina hiyo ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu’, tulijibu.

Kisha akaagiza milango yote ifungwe. Baada ya hapo akatuambia, ‘Nyanyueni mikono yenu na msembe *La ilaha ill-Mwenyezi Mungu*’.

Tulinyanyua mikono yetu juu na kusema *La ilaha ill-Mwenyezi Mungu* kwa kitambo kirefu. Baada ya hapo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – alishusha mikono yake na kuomba:

‘Ewe Mola wangu... Shukrani zote unastahiki wewe! Umenituma mimi kwa hii ‘sentensi’ na kuniamrisha juu yake (kuitaja na kujipamba nayo). Na kwa kufanya hivyo umeniahidi pepo...na kamwe huvunji ahadi yako!

Baada ya hapo akatugeukia na kusema, ‘Bishara njema kwenu nyote! Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewasamehe!’” (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, IV, 124).

Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – anasema anasema yafuatayo katika *hadith*: “*La ilaha ill-Mwenyezi Mungu* ni maneno yenye thamani na nafasi kubwa mno mbele ya Mwenyezi Mungu. Yeyote atakayeyataja kwa moyo safi na unyenyekevu Mwenyezi Mungu atamuingiza peponi. Na yeyote atakayeyataja kwa ulimi tu bila ya kuyaamini atakuwa ameyalinda maisha yake na mali zake. Lakini kesho atakapokutana na Mwenyezi Mungu atashughulikiwa.” (Haythami, Majmau’-Zawaid, I, 26).





Haitoshi *hadith* ifuatayo inasisitiza juu ya hitajio la kuwa katika hali ya *dhikr* na *muraqaba* wakati wote: “Msimsahau Mwenyezi Mungu na kujiingiza katika maongezi ya upuuzi. Kwani pamoja na maongezi mengi kumfanya mtu amsahau Mwenyezi Mungu pia huufanya moyo kuwa mgumu. Na mtu aliye mbali zaidi na Mwenyezi Mungu ni yule mwenye moyo mgumu zaidi”. (Tirmidhi, Zuhd, 62).

Mpenzi huhisi hitajio la kumkumbuka yule anayempenda sawa na kiwango cha mapenzi aliyonayo juu yake. Hivyo kila unapomkumbuka ndivyo unavyoongeza mapenzi juu yake. Wale ambao walikuwa na ladha ya utamu wa *iman* huzidisha shauku yao juu ya Mola na kumkumbuka kwao kadiri imani zao zinavyoongezeka. Kwa upande wa uwezo wao kutosheka kuna tofauti kati tamaa ya nafsi na tamaa ya roho. Wakati uchu wa nafsi unatulia baada ya kula, kunywa na kadhalika, na kutohitaji zaidi, lakini tamaa ya roho huongezeka zaidi kadiri unavyouhudumia. Hivi ni kama kunywa maji ya chumvi ili kumaliza kiu. Kila kidogo unachokunywa kinaongeza tamaa ya kunywa maji zaidi. Watu na aina hiyo huwa katika hali ya *dhikr* wakati wote, huku akitafakari juu ya hekima iliyopo katika uumbaji wa dunia na anga, na kisha baada hapo wakaomba:

“Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa kitako na wakilala, na hufikiri kuumbwa mbingu na ardhi, wakisema: Mola wetu Mlezi! Hukuviumba hivi bure. Subhanaka, Umetakasika! Basi tukinge na adhabu ya Moto” (Al- i imran, 191).

Barabara ya kuelekea kwenye maisha ya imani na kuridhika, ya kufikia furaha za akhera na kikubwa zaidi kukutana na Mwenyezi Mungu Mtu-kufu huku ukiwa na moyo safi, inapita kwenye hali *dhikr* yenye kuendelea. Hali yoyote mtu atakayofia ndiyo atakayofufuliwa nayo, kama ambavyo imewekwa wazi na *hadith* ifuatayo:

“Kesho akhera wanadamu watafufuliwa kutokana na hali waliyokufa nayo” (Muslim, Jannah, 83).

“Mtu hufa kutokana na namna alivyoishi na hufufuliwa kutokana na namna alivyokufa” (Munawi, Fayzu’l-Qadir, V, 663).

Hakuna kitu bora kitakachoweza kutosheleza hamu ya mwanadamu juu ya utambuzi wa kiroho zaidi ya kutambua vilivyo uwepo wa *Wajibu’l-Wujud*, *Hakim*, mwingi wa hekima na Nazim, yani Mpangaji, wa ulimwengu na kumpenda Yeye. Aya ifuatayo inatukumbusha juu ya suala hili:





الَّا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ

“Wale walio amini na zikatua nyoyo zao kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu. Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua!” (ar-Rad, 28).

**g- Upendo juu ya Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – na Salawat-u Sharifa**

**“Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu” (al-Ahzab, 56).**

Kutokana na uwezo na nguvu zetu sisi kama wanadamu hatuwezi kumuelewa kikamilifu Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - ambaye ni shujaa miongoni mwa viumbe. Picha tunayoiyapata kutoka duniani inadhihirisha udhaifu wetu katika kumuelewa na kumuelezea. Kama isivyowezezana kumimina bahari yote ndani ya kikombe ndivyo isivyowezezana kuelewa nuru ya Mtume Muhammad kikamilifu. Aya ifuatayo inalidhihirisha hili:

إِنَّ اللَّهَ وَمَلَائِكَتَهُ يُصَلُّونَ عَلَى النَّبِيِّ

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا صَلُّوا عَلَيْهِ وَسَلِّمُوا تَسْلِيمًا

“Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu” (al-Ahzab, 56).

Ili kutekeleza agizo takatifu kutoka kwenye hiyo aya hatuna budi kuta-ja *salawat-u sharifa* kwa kumtakia salamu na amani *huyo* Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, Mtume ambaye kwa kupitia yeye ulimwengu unajisifu. Hii ni sehemu ya sharti ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu anauamrisha umma mzima ushikamane nalo na kulitekeleza kwa heshima kubwa juu ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Ni sharti la *iman* kuzisogelea rehema na mwenendo timilifu wa *huyo* Mtume mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake, Mtume ambaye ametumiwa







salamu na baraka na Mwenyezi Mungu Mtukufu na malaika wengi wasio na mfano. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“Sema: Ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu” (Al- i Imran, 31).

Pindi muumini atakapoanza kutetemeka kutokana na imani yake juu ya Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – na kuhisi hisia nzuri zikijikita moyoni mwake na kusafisha roho yake dhidi mionekano na vivuli vya nafsi, hapo atakuwa amefanikiwa kufikia kwenye mapenzi yake na mwenendo wake wa kuigwa. Mpaka siku hii mashujaa wa moyo miongoni mwa umma, mashujaa ambao wameweza kupata sehemu ya mwenendo wake mtukufu kiasi cha kuwa nao katika uhai wao wote, watakuwa wameonyesha vizuri mapenzi yao kwa Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake.

Waislamu wanaendelea kuwatukuza wale waliofanikiwa kufikia chanzo cha mapenzi, yani Mola na Mjumbe wake, mpaka saa ya mwisho, wanawakumbuka watu hawa kwa upendo na dua nzuri hata baada kufa kwao. Miongoni mwa wafuasi hao wa Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – ambao wametunukiwa nafasi hii, historia ya wawili miongoni mwao haiwezi kusahaulika.

*Wakati wake Mtume Mtukufu – rehemu na amani ziwe juu yake – alikuwa akituma walimu kwenda kwenye makabila ya jirani kwa ajili kuzungumza nao na kuwafundisha dini ya kweli. Baadhi ya walimu waliangukia kwenye njama mbaya, moja wapo ilitokea kwenye janga lililojulikana kama Raji.*

*Makabila ya Ada na Qari waliomba walimu kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – kwa ajili ya kufundishwa uislamu. Mtume Mtukufu – rehemu na amani ziwe juu yake – akawajibu kwa kuwatumia kikosi cha maswahaba. Lakini pindi kikosi kile kilipowasili Raji kilivamiwa. Nane waliuwawa na wawili waliobaki walipelekwa kwa washirikina wa Makka.*

*Maswahaba wawili walioangukia kuwa mateka walikuwa ni Zayd na Hubayb – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao. Baadae washirikina*





wale makatili waliwauwa maswahaba wale wawili. Muda mfupi kabla Zayd – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – hajauwawa Abu Sufyan alimuuliza:

“Je ungelitamani Mtume awe katika nafasi yako hii kama ungelifahamu kuwa kwa kufanya hivyo ungeliachiwa?”

Zayd – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alimuangalia Abu Sufyan kwa huzuni na kumjibu, “Kamwe...si kwamba nisingelitamani yeye kuchukua nafasi yangu hii bali nisingeliweza kuvumilia hata mwiba kumchoma mguuni mwake huko Madina.

Kutokana na kuvutiwa na majibu yale Abu Sufyan alishindwa kujizuia na akakiri, “Naapa kamwe sijapata kuona mtu anayependwa na rafiki zake zaidi ya anavyependwa Muhammad!”

Baadae wakaenda kwa Hubayb – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na kumthibitishia kuwa angeliachiwa kama angelikana imani yake.

“Hata kama ingelikuwa ni kunipa dunia nzima”, alijibu. Kisha washirikina wale wakamuuliza lile swali walilomuuliza Zayd – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Wakapata jibu lile lile.

Hubayb – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa na ombi moja tu la mwisho kabla hajauwawa: ombi lenyewe lilikuwa ni kutuma salamu kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake.

Lakini ni nani angelimtumia ujumbe wake? Hakukuwa na muislamu hata mmoja karibu yake. Huku akikaribia kukata tamaa alinyanyua uso wake na kuangalia angani na kisha akaomba:

“Mola wangu! Hakuna mtu yeyote karibu yangu atakayeweza kuzipeleka salamu zangu kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema amani ziwe juu yake. Naomba uzifikishe salamu zangu za amani kwake!”

Wakati ule Mtume aliyebarikiwa – rehema amani ziwe juu yake – akiwa amekaa pamoja na maswahaba zake kule Madina akasema kwa sauti, “Amani iwe juu yake pia!”

“Ni salamu za nani ulizozitikia hivi punde ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?” maswahaba waliuliza.

“Ni salamu za ndugu yenu Hubayb”, alisema Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.





*Baada ya hapo wale washirikina wakawatesa wote wawili kwa ukatili mpaka wakafa. Maneno ya mwisho ya Hubayb – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ni muhimu sana:*

*“Haijalishi kufa kwa namna hii au ile, cha muhimu ni kufa hali ya kuwa ni muislamu!”<sup>19</sup>*

Hayo ndiyo mapenzi na ujasiri wa maswahaba! Walikuwa hawana uwoga mbele ya tukio lenye kutisha kiasi cha kuweza kuwaingiza katika hofu kubwa. Walichokuwa wakijali zaidi ni kuvuta umakini wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Na mwisho wake salamu zao zilizotokana na nyoyo zao safi zilifikishwa mahala husika huku zikisindikizwa na Mola Mwenyewe. Ufuatao ni mfano mwingine wenye kuweka wazi mapenzi na shauku ya maswahaba juu ya Mjumbe Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake.

*Siku moja Abdullah ibn Zayd al-Ansari alikuja kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kutoa masikitiko yake:*

*“Ninakupenda ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuliko kitu chochote kile nilichonacho, watoto wangu, familia yangu na hata mimi mwenyewe. Kama nisingelikuwa nimepata bahati ya kukuona ningelitamani kufa!” Kisha akaanza kutokwa na machozi.*

*“Kwa nini unalia?”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliuliza.*

*Zayd – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alijibu, “Ninalia kwa sababu ninafikiria kuwa na wewe siku moja utaiaga dunia na kuungana na Mitume wengine katika madaraja ya juu, wakati mimi hata kama ningelitakiwa kuingia peponi ningelikuwa katika madaraja ya chini na hivyo kutoweza kukuona tena!”*

*Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye alikuwa bahari ya huruma aliamua kubakia kimya kwa muda. Baada ya muda mfupi ufunuo ufuatao ukashuka:*

*“Na wenye kumt’ii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wa pamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao!” (an-Nisa, 69).*

<sup>19</sup> Rejea Bukhari, Maghazi, 10; Waqidi, Maghazi, uk. 280-281.





*Baada ya miaka kadhaa wakati Abdullah ibn Zayd al-Ansari – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipokuwa anashughulikia bustani yake alijiwa na mwanae ambaye alikuwa akikimbia kiasi kwamba akawa anapumua kwa shida, mwanae huyo alimpa taarifa za kusikitisha za kifo cha Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake. Kutokana na mshutuko alioupata Zayd – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akaomba dua ifuatayo:*

*“Ewe Mola wangu...niondolee uoni wangu sasa hivi ili kuanzia sasa hivi nisiweze kumuona mtu yeyote yule kinyume na kipenzi changu cha pekee, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake”*

*Dua yake ilijibiwa mara moja. Kuanzia pale akawa amepoteza uoni wake.<sup>20</sup>*

Upendo na huba ni kama waya wa umeme uliounganisha nyoyo mbili. Kamwe wapenzi hawaondoi fikra za wapendwa wao ndani ya nyoyo zao na hawaweki kumbukumbu zao mbali na ndimi zao. Kabla mauti haya-jawafika huishi kwa amani ndani ya nyoyo zao inayotokana na kiwango cha kujitolea muhanga walichokionyesha mbele ya vipenzi vyao, pamoja na kuridhika kuwa wametumia mali zao na uhai wao katika njia ambayo inaridhiwa na kipenzi chao. Aya inasema: “Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na mt’iini Mtume, ili mpate kurehemewa” (an-Nur, 56).

Ni jambo la muhimu kushikamana na kipenzi chetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – katika kila kipengele cha maisha yetu, kwani Mtume ndiye mfano wa kuigwa kwetu. Pia hatuna budi kushikamana na kanuni isemayo, “Mpenzi hupenda kila kitu ambacho anakipenda kipenzi chake”. Kumpenda na kushikamana na mafundisho yake ndio uti wa mgongo wa mapenzi matakatifu.

Kinachofuata mara baada ya maneno لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ (hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu) katika maneno ya Tawhid, yani katika kukiri imani, ni مُحَمَّدٌ رَسُولُ اللَّهِ (Muhammad ni Mjumbe wake). Kila neon la tawhid, kila *salawat* ni sababu ya kuelekea kwenye kupata upendo na ukaribu na Mwenyezi Mungu. Uwekezaji huu ndio sababu ya kupata furaha kubwa hapa duniani na kesho akhera, furaha ambayo inafungua mlango wa kuelekea kwenye himaya zote za kiroho.





Ulimwengu unabainisha wazi mapenzi matakatifu. Kiini cha ubainifu huu ni nuru ya Muhammad ambaye mapenzi yake ndiyo njia pekee ya kuelekea kwa Mola.

Utukufu wa ibada, uzuri wa tabia, adabu inayoongoza maadili, ulaini wa moyo, uzuri wa muonekano, raha ya lugha, rehema zinazopenya ndani ya hisia, uzuri wa mtazamo, na kwa kifupi ni kwamba uzuri wote umetokana na cheche za upendo wa nuru ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – iliyoangaziwa kwenye nyoyo.

Mawlana Rumi anasema: “Njoo ewe moyo, njoo kwenye sherehe ambayo ni makutano na Muhammad...kwani nuru unayoiona hapa duniani si nyingine bali ni mng’ao utakao kwenye uso wa kiumbe huyo mtukufu”

Kurudia rudia *salawat-u sharifa* wakati wote na sehemu yoyote hasa alfajir ni jambo lenye umuhimu mkubwa, kwani linapelekea msukumo mtakatifu kubakia katika moyo wako, kuleta mshikamano na Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – na hivyo kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Watu wema waliohuishwa na uhalisia wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – wametaja faida za kumswalia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na hivyo kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, kama ifuatavyo:

1. Mtu atakuwa ametikia amri ya Mola na wakati huo huo atakuwa amesalimia kwa *salawat* ya malaika. Aya inasema: “Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu” (al-Ahzab, 56)

Hatuna budi kusema kwamba kuna tofauti katika maana kati ya *salawat* ya Mwenyezi Mungu juu ya Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – na *salawat* ya malaika, na vile vile yetu. *Salawat* ya Mwenyezi Mungu ni kwa Yeye kumpa rehema Mjumbe wake na kumpandisha daraja. *Salawat* ya malaika ni ya kumuomba msamaha. *Salawat* yetu, yani *salawat* yetu ummah wake ni kwa ajili ya kumuomba Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake.

2. Ni sababu ya kusamehewa madhambi.





Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ameapa: “Yeyote atakayenishwalia mara moja, Mwenyezi Mungu atamrehemu mara kumi, atamfutia madhambi kumi na atampandisha daraja kumi” (Nasai, Sahw, 55)

3. Ni sababu ya kuwa karibu na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – siku ya kiama.

“Watakaokuwa karibu na mimi siku ya kiama ni wale wanaonishwalia mara nyingi zaidi”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema. (Tirmidhi, Witr, 21)

4. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – yeye bin-afsi anamjibu yule aliyemtumia *salawat*. Amesema:

“Mwenyezi Mungu hunirudishia roho yangu kwa ajili ya kujibu salamu za wale walionishwalia” (Abu Dawud, Manasiq, 96)

5. Jina la kila aliyemshwalia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – hupelekwa kwake.

“Mwenyezi Mungu ana malaika ambao wanazunguka katika ardhi na kuniletea salamu pale pale zinapotolewa” (Nasai, Sahw, 55)

6. Kwa kuwa mtu ambaye anamshwalia Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – anakuwa ameweka mbele mapenzi yake juu ya Mtume juu ya mtu mwingine yeyote, hili linampelekea kupiga hatua kubwa katika kuji-pamba na mwenendo wake na kuachana na maovu.

7. Si tu mapenzi ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – juu ya mtu huyu yanaongezeka, bali mapenzi ya mtu huyu juu ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – yanahifadhiwa na kuendelea kuongezeka.

8. Licha ya baraka zisizo na kifani ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametujaalia kwa kupitia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kutokuwepo uwezekano kuzilipa, lakini kwa kupitia *salawat-u sharifa* angalau tutakuwa tumeonyesha kujali na kupiga hatua katika kushukuru.

9. Hiyo ni sababu ya kuwasili kwetu rehema ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kipenzi wetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:





“Yeyote atakayeniswalia mara moja Mwenyezi Mungu atamhurumia mara kumi zaidi ya kiwango hicho” (Muslim, Salat, 70).

10. Hiyo ni sababu ya kukusanya tena kile kilichosahaulika.

11. Hiyo ni sababu ya kukubaliwa dua zetu.

Siku moja Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alimuona mtu mmoja ambaye baada ya kumaliza swala alianza kuomba dua bila ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumswalia Mjumbe wake.

“Yule mtu alikuwa na haraka sana”, alisema kabla ya kumuita mtu aliyekuwa karibu yake na kumwambia, “Pindi yeyote miongoni mwenu atakapotaka kuomba dua na aanze kwa kumshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu na kisha aendelee kwa kuniswalia mimi. Kisha anaweza kuomba kwa namna yoyote atakayo.” (Tirmidhi, Daawat, 64)

Na katika *hadith* nyingine: “Dua haifiki mahala pake mpaka muombaji atume *salawat* kwa Mtume” (Munziri, at-Tarhib wa’t-Tarhib, III, 165)

12. Kunamlinda mtu dhidi ya kulaumiwa siku ya kiamaa.

“Na isongwe kwenye vumbi pua ya yule asiye nitumia *salawat* licha ya mimi kutajwa mbele yake” (Tirmidhi, Daawat, 100)

13. Mwenyezi Mungu atamtosheleza katika mambo yake yote mtu mwenye kawaida ya kumswalia Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, na ataitawanya huzuni yake hapa duniani na kesho akhera.

Ubay ibn Qab – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia yafuatayo:

*‘Ninakutumia salawat’u-sharifah nyingi ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Nifanye hivyo kwa kiasi gani?’ siku moja niliuliza.*

*‘Kwa kadiri utakavyo’ alijibu.*

*‘Je itakuwa sawa nikitumia robo ya dua yangu kwa ajili hiyo?’ niliuliza tena.*

*‘Tumia muda mwingi kadiri uwezavyo’, alishauri. ‘Lakini ingelikuwa bora kama ungelitumia muda mwingi zaidi’*

*‘Basi nitatenga nusu yake’, nilisema.*





*'Kama utakavyo...lakini ingelikuwa bora kama ungelitenga muda mwingi zaidi ya huo', alisema.*

*'Vipi kama nitatenga robo tatu ya huo muda?'*

*'Kama utakavyo...lakini ingelikuwa bora kama ungelitenga muda mwingi zaidi ya huo'.*

*'Basi itakuwaje kama nitatumia muda wote wa dua kwa ajili ya kutuma salawat'us-sharifah?' kisha niliuliza.*

*'Kama utafanya hivyo basi Mwenyezi Mungu atakuondoshea matatizo yako yote na kukusamehe madhambi yako yote', alisema Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. (Tirmidhi, Qiyamat, 23/2457)*

*Salawat-u Sharifa humuwezesha mtu kukutana na utukufu wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kupata fursa ya kuan-gaziwa na nuru yake. Kwa upande mwingine malipo ya kila salawat hulin-gana na usafi wa moyo wa mtu na mapenzi yake kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.*

*Ewe Mtume, Ewe Mjumbe...salawat na salam tele zikufikie !*

*Dahilak ya Rasulallah...!<sup>21</sup>*

#### **h. Kutafakari juu ya mauti**

***Kwenye dunia hakuna nafasi wala nyakati ya kuweza kukusaidia kukikwepa kifo, wala hakuna fursa ya kuweza kutoka kaburini, wala hakuna sehemu salama ya kukuwezesha kukimbia adha ya siku ya kiama...***

Katika maisha mwanadamu hujikuta akitetemeka kati ya pande mbili zinazotazamana, nazo ni furaha ya maisha na hofu ya kifo. Bila ya kutambua maana halisi ya uhai na mauti itakuwa ngumu kuelewa siri na hekima ya uumbaji na mwenendo halisi wa mwanadamu. Mauti ambayo hayakwepeki na ambayo yatamkabili kila mwenye kuishi hapa duniani ni fumbo lisilokwepeka ambalo viumbe vyote wenye uwezo wa uelewa hawana budi kulitatua.



21. "Ninahitaji uombezi na huruma yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu!"





Mwenyezi Mungu anasema yafuatayo katika aya ya pili ya surat al-mulk:

الَّذِي خَلَقَ الْمَوْتَ وَالْحَيَاةَ لِيَبْلُوَكُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا

“Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha”

Vile vile katika aya ya thelathini na tano katika surat al – Anbiya Mwenyezi Mungu anasema: “Kila nafsi itaonja mauti; na tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na kwetu Sisi mtarejeshwa”

Kama dunia ni shule takatifu kwa ajili ya kujaribu imani za watu, basi mauti ni kanuni ya msingi ya kupitiwa na kila mtu. Kwa sababu hii Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Kufa ili ufufuliwe!”

Uhuishwaji wa moyo utawezekana pale tu mtu atakapoachana na matamano ya nafsi. Mtume aliyebanikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema: “Mara kwa mara kumbukeni mauti ambayo yanaharibu raha zote tokea kwenye mizizi yake” (Tirmidhi, Qiyamah, 26). Kutafakari juu ya mauti kunamaanisha kutafakari juu ya mauti kabla hakijakukuta na hivyo kujiandaa kukutana na Mola wako kwa kuachana na matamano yote ya nafsi. Huku ni kutafakari na kutambua kunakohitajika katika imani. Tamaa za kidunia zenye kupita, matumaini yenye kupita na starehe, vitu ambavyo mwanadamu hawezi kutosheka navyo ni kama majani yanayodondoka chini ndani ya sekunde wakati wa majira ya kupukutika kwa majani.

Makaburi ni marejeo ya wazazi waliotumia muda wao duniani, pia ni marejeo ya watoto, marafiki, ndugu na vipenzi. Kaburi ni kituo cha mwisho cha mikondo ya barabara zote za maisha, ikiwa maisha hayo yalikuwa katika nyasi au ndani ya kasri. Hakuna kipimo cha nyakati wala nafasi cha kukuwezesha kukikwepa kifo. Qur’an inalifanua hili kama ifuatavyo: “Sema: Hayo mauti mnayo yakimbia, bila ya shaka yatakukutteni. Kisha mtarudishwa kwa Mwenye kuyajua yaliyo fichikana na yanayo onekana. Hapo atakwambieni mliyo kuwa mkiyatenda” (al- Jumaa, 8).





Kwa maana hii desturi ya kuweka makaburi ndani ya miji pembezoni mwa barabara au ndani ya viwanja vya misikiti ni ili kuhuisha utafakariji juu ya mauti na hivyo kuweza kuyaongoza vizuri mambo ya kidunia. Huku likiwa limegubikwa na kimya cha mauti jiwe la kaburi lenyewe ni mhitutubu mzuri kutokana na kuwepo kwake pale. Uzito wa mauti ni mkubwa mno kiasi cha kushindwa kuvumiliwa na maneno yetu dhaifu, pia ni tukio lenye kutisha, tukio ambalo nguvu na tawala zote hunyenyekeka mbele yake.

Dunia ni ndoto ya mchana yenye kulaghai, Akhera ni uhalisia usiohitaji kifo. Mara nyingi mwanadamu ni mtumwa wa ulaghai unaoakisiwa kutoka kwenye kioo cha maisha ndani ya maelfu ya taswira zenye kuvutia. Basi maisha ni nini?, maisha ambayo yanatandaza mtandao wake wa uongo na kutotii si chochote bali ni mahala pa ulaghai.

Je mwanadamu hajifunzi kutokana na ukweli kwamba kinu cha muda bila huruma kinaponda ujana na uchangamfu wa viumbe wote wenye kufa? Ukubwa ulioje wa ulaghai ambao unaongoza bila uhalisia maisha ambayo yako mbali na uhalisia wa akhera huku yakivutiwa na mapambo ya dunia yenye kupotosha, na huku yamepambwa na utoto wa kucheza na midoli! Kucheza utotoni, tamaa ujanani, kutokuwa makini wakati wa utu uzima na tamaa, kujuta kwa masikitiko makubwa baada ya umri kukutupa mkono, yote haya ni mambo yatokanayo na maisha ya kutojali mambo.

Kifo ni siku ya kiama ya mtu binafsi. Hatuna budi kuamka kabla siku yetu ya kiama haijafika ili tusije tukajuta. Kuhusiana na kila mtu kukutana na malaika wa mauti sehemu yoyote na wakati usiojulikana ni jambo lisilokwepeka. Hakuna sehemu ya kuweza kukikimbia kifo. Bila kupoteza muda mfupi tulionao kila mtu hana budi “kukimbilia kwa Mwenyezi Mungu...” (ad-Dhariyat, 50) na kutambua kuwa kilichobaki pekee cha kukimbilia ni rehema za Mwenyezi Mungu.

Msukumo mkubwa wa kutafakari juu ya mauti upo katika kimya cha kudumu cha midomo ya maiti. Kinachoweza kuonyeshwa na dunia kutokana na tahadhari kubwa ya kifo ni machozi na vilio.

Ni jambo la kushangaza kumuona mwanadamu anajidanganya kwenye dunia ambayo hubakia kwa muda mfupi kama mgeni. Licha ya kushuhudia vifo kila siku lakini anajiona yeye yuko mbali na kifo. Anajidanganya kwa kuona kuwa yeye ni mmiliki wa vile alivyonavyo, vitu ambavyo ataweza kuvipoteza wakati wowote. Lakini mwanadamu amepangiwa kufa mapema





tu roho yake inapovishwa nyama na kutangulia kwenye mlango wa maisha hapa duniani. Ingawa mlango huu humuingiza kwenye barabara ya mafunzo kwa ajili ya kuongoka lakini mara nyingi mwanadamu huyu halitambui hili. Kisha siku ambayo roho yake inatolewa kwenye mwili wake inafika na kisha anaagwa kuelekea kwenye kaburi, kaburi ambalo ndio mlango wa kuelekea akhera, safari ambayo haina kurudi nyuma.

Kila muda unapopita ndipo tunavyosogezwa karibu zaidi na ukweli huu, kama ambavyo tunafahamishwa katika aya ifuatayo: “Na tunaye mze- esha tunamrudisha nyuma katika umbo. Basi je! hawazingatii?” (Yasin, 68).

Aya hii inamuusia mwanadamu katika namna nzuri yenye kufikirika. Sifa maarufu ya dunia ni kwamba dunia haina uungwana. Huchukua kwa haraka kile inachokitoa. Siku moja humuinua mtu ili siku inayofuata imtupe shimoni. Ni kama kivuli ambacho mara kwa mara kinapotaka kuguswa kinakimbia. Lakini kadiri unavyokikimbia ndivyo kinavyoku- fuata. Huku mtu akiwa na matumaini kwamba siku moja atakipata kile anachokitafuta mara anakatishwa na mwito wa mauti. Kuipenda dunia kunakuwa kama mchawi mwenye gubu, mchawi ambaye anampiga mtu makofi ya uso, mtu ambaye usumbufu juu yake na malalamiko hayaishi. Huwasaliti upesi wale walioikumbatia.

Hakuna budi kutambua kuwa kwenye dunia hakuna nafasi wala nyakati ya kuweza kukusaidia kukikwepa kifo, wala hakuna fursa ya kuwe- za kutoka kaburini, wala hakuna sehemu salama ya kukuwezesha kukimbia adha ya siku ya kiama. “Ni muislamu yupi mwenye akili kuliko wote?” siku moja swahaba mmoja alimuuliza Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. “Ni yule anayeyakumbuka mauti mara kwa mara na kujian- daa vilivyo kwa ajili ya akhera. Hao ndio wenye akili kisawa sawa”, alijibu. (Ibn Majah, Zuhd, 31).

Kipenzi wetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – amesema tena, “Kumbukeni mauti na namna ambavyo nyama na mifupa vinaoza baada ya kifo. Yeyote anayeitamani akhera basi na ajitenge na mng’ao wa maisha katika ardhi” (Tirmidhi, Qiyamah, 24). “Mauti yanatosha kuwa mawaidha”, anasema Fudayl ibn Iyad.

*Swahaba mmoja alikuwa amefariki. Wengine walimsifu na kukum- bushia amali zake nyingi alizokuwa akizitenda wakati wa uhai wake. Wakati ule Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ali-*





kuwa akiwasikiliza huku amekaa kimya. Walipomaliza kuongea aliwauliza:

“Je mtu mnayemzungumzia alikuwa akikumbuka mauti?”

“Hapana” walijibu.

“Kama ni hivyo, je alijitahidi kuachana na mambo yasiyokuwa ya lazima na tamaa zilizokithiri zilizotokana na nafsi yake?”

Kwa mara nyingine tena maswahaba walitoa jibu hasi. Kisha Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:

“Basi inaonekana rafiki yenu hakuwa kama ambavyo nyinyi mnamdhania” (Haythami, *Majmau’z-Zawaid*, X, 308-9)

Abdullah ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ana-simulia namna ambavyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alivyomshika mkono na kumshauri: “Ishi hapa duniani kama mgeni au mpita njia! Jihesabu u miongoni mwa maiti ambao ni wakazi wa makaburini”

Mwanachuoni mkubwa katika kipindi cha Tabiun, Mujahid ibn Jabr r.alayh anasema, “Pindi Ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aipomaiza kusimulia hii *hadith* ainishauri kama ifuatavyo:

‘Ewe Mujahid, usifikirie usiku pindi inapofika asubuhi! Na usifikirie asubuhi pindi usiku unapofika! Itumie vizuri afya yako kaba ya kuumwa na utumie uhai vizuri uhai kaba ya mauti! Kwani wewe mja hufahamu utakuwa katika hai gani (hai au maiti) siku inayofuata!” (Tirmidhi, *Zuhd*, 25).

Anas ibn Malik – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea: “Kia siku ardhi inamtahadharisha mwanadamu juu ya mambo kumi:

Mwana wa Adam!

1. Unatembea juu yangu lakini marejeo yako ni kwangu.
2. Unatenda madhambi mbalimbali juu yangu lakini utakuja kuadhibiwa ndani yangu.
3. Unacheka na kufurahia juu yangu lakini utakuja kulia ndani yangu.
4. Unapata raha juu yangu lakini utakuja kuhuzunika ndani yangu.
5. Unahifadhi mali zako ndani yangu lakini utakuja kujuta ndani yangu.





6. Unakula haramu juu yangu lakini na wewe utaliwa na funza ndani yangu.
7. Unafanya kiburi juu yangu lakini utakuja kuwa chini na kudhalilika ndani yangu.
8. Unatembea juu yangu kwa furaha lakini utakuja kuzama kwenye dimbwi la huzuni ndani yangu.
9. Unatembea chini ya mwangaza wa juu juu yangu lakini utakuja kuachwa kwenye kiza ndani yangu.
10. Unatembea pamoja na makundi ya watu juu yangu lakini utakuja kuingia ndani yangu peke yako. (ibn Hajar al-Asqalani, Munabbihat, 37).

Katika kumzungumzia Quss ibn Saida ambaye alikuwa mtu mwenye hekima na lugha ya kushawishi, siku moja Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alisema: “Siku moja tulipokuwa katika soko la Uqaz nilimsikia Quss ibn Saida akiwahutubia watu huku akiwa juu ya ngamia, alisema yafuatayo:

*‘Enyi watu! Njooi, msikilize, mijifunze na kupata somo! Yeyote anayeshi atakufa, yeyote anayekufa hutoweka na chochote kilichopangwa kutokea hutokea. Mvua hunyesha, majani huota na watoto huzaliwa kuchukua nafasi ya wazazi wao. Kisha wote huondoka. Kutokea kwa mambo hakuishi; yote yanafuatana. Anga zimejaa habari, ardhi imejawa na masomo ambayo hayana budi kuzingatiwa. Ardhi ni godoro lililotandikwa na anga ni dari tukufu. Nyota na bahari zitafikia mwisho. Yeyote anayekuja habaki na yeyote anayeondoka harudi. Nani ajuaye? Je ni kwa sababu wameridhika na huko walipo ndio maana wanabakia huko au je ni kwa sababu wamezuiwa na kupewa usingizi?*

*Enyi watu wa lyad! Wako wapi baba zenu na mababu zenu? Wako wapi watu wa Ad na Thamud ambao walijenga majengo makubwa kwa mawe? Wako wapi Namrut na Firauni ambaye licha ya kuwa na utajiri mkubwa wa mali lakini alifikia kuwauliza watu wake, je mimi siye mola wenu mkuu?*

*Ardhi iliishia kuwatwanga wote ndani ya kinu chake. Hata mifupa yao imeoza na kutawanyika. Makazi yao yamekuwa magofu na kukaliwa na mbwa. Kamwe msije mkawa wenye kupuuzia mambo kama wao! Msifuate njia yao! Kila kitu kitatoweka isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee.*





*Kuna njia nyingi za kukuwezesheni kuingia kwenye mto wa mauti, lakini hakuna njia ya kutokea*<sup>22</sup>

Mauti ambayo ndiyo pazia la mwisho la igizo la maisha ni kama kioo ambacho kitabainisha mwisho wa kila mtu. Mtu atakayeishi chini ya udhibiti wa nafsi yake na kuifanya dunia kuwa lengo lake kuu, kwake kaburi litakuwa kama njia ya mzingo yenye giza. Hata kuyakumbuka mauti kwake kutakuwa ni maumivu makali yasiyolinganishwa na kitu chochote kile. Hata hivyo kama mtu ataweza kukiruka kikwazo cha nafsi na akaweza kufikia tabia za malaika kwa kutafakari juu ya mauti, uwezo uliojificha ndani yake, kwake mauti yatakuwa ni njia ya lazima ya kumuwezesha kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kifo ambacho kwa kawaida husababisha kutetemeka kwa baridi kwenye mili ya wanadamu wa kawaida, kwa mtu wa aina hii hugeuka na kuwa furaha ya kukutana na kipenzi chake. Sufi Mkubwa Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aita-kase siri yake – katika maneno yake anasema kuwa kifo cha namna hii ni *shab-i arus*, yani usiku wa harusi. Hii ni njia ambayo inapendezesha hata kitu chenye kumtisha mwanadamu, yani mauti. Ili kuyapendezesha mauti ni muhimu kufikia kwenye ukamilifu wa kiimani kwa kupitia toba, uchamungu, kumuamini Mola, kutosheka, kumkumbuka Mwenyezi Mungu na subira.

Katika ushawishi juu ya kuutakasa moyo kutafakari juu ya mauti ni jambo bora kabisa. Katika suala hili Rabi ibn Husayn anasema: “Ninahofia moyo wangu usije ukachafuliwa pindi nitakapoacha kukumbuka mauti. Ningelikuwa nimekaa makaburini mpaka pumzi yangu ya mwisho kama ningelikuwa na uhakika kwamba kufanya hivyo nisingelienda kinyume na mafundisho ya waliotutangulia”

Moyo hutetemeka kutokana na misukosuko ya roho na nafsi mpaka kufa. Mauti ni mwanzo muhimu katika safari ya akhera. Kabla ya kuianza safari hii kuuandaa moyo kwa ajili ya mauti kwa kupitia *marifatullah*, kuu-patia afya ya kiimani na utulivu ambao utaulinda dhidi ya hofu na wasi-wasi juu ya mauti, vyote hivi ni vitu ambavyo havipaswi kupuuziwa. Kama siri ya ‘kufa kabla ya kifo’ itadhihirika basi mwanadamu ataondokana na kutawaliwa na nasfi yake na badala yake atajawa mapenzi juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa namna inayostahili.





### **i. Kukaa pamoja na watakatifu na watu wema**

***“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli” (at-Tawba, 119)***

Ili kuulinda moyo dhidi ya *masiwa* au kitu kingine kinyume na Mola na kuufanya uweze kupokea mambo mema pekee ni jambo linalohitaji kuwa pamoja na watakatifu na watu wema, watu ambao unaweza kupata manufaa ya kiroho kutoka kwao. Kinyume na viungo vingine vya mwili ambavyo hutii moja kwa moja matashi ya kimwili, lakini kwa upande wa moyo sifa hii haipo, bali una kawaida ya kufuata ushawishi wa mazingira yanayomzunguka mtu husika.

Moyo huchukua umbile, rangi na wizani wa mazingira yanayozunguka. Lakini huu ni mwanzo wa ushawishi fulani kukita mizizi na kutulia ndani ya moyo. Ushawishi ambao hufuata baadae na kuuweka moyo chini ya udhibiti wake unaweza kuja kuwa hasi au chanya, hili linategemeana na namna ambavyo ushawishi wa awali ulivyokita mizizi yake ndani ya moyo. Hivyo moyo utakuwa kwenye hatari kubwa kama hautapambwa kwa vishawishi vizuri na kupata upatanisho unaostahiki. Kutokana na kuwepo katika hatari ya ushawishi kutoka nje moyo unaweza kuyumbishwa na vishawishi hivyo kiasi kwamba ukafikia kuwa na mapenzi juu yake au ukajiweka mbali navyo kiasi kwamba ukawa na chuki juu yake. Hivyo matumizi mazuri ya mapenzi na chuki ni muhimu katika kumkuza au kumdidimiza mwanadamu kiimani. Kwa hakika kuyaweka mapenzi na chuki katika sehemu zake husika kuna mchango mkubwa katika kumhui-sha mtu kiimani. Kinyume chake kuwaonyesha mapenzi wale wasiostahiki au kuwachukia wale wasiostahiki humpelekea mtu kuharibikiwa kulingana na kiwango cha mapenzi au chuki alichonacho juu yao.

Kwa kuyazingatia haya utaona kuwa hitajio na umuhimu wa kuwa karibu na waja wa Mwenyezi Mungu wema kama ambavyo inahitajika kwa ajili ya kummakinisha mtu kiimani ni jambo la msingi mno. Lakini hapa napo manufaa ambayo yataweza kupatikana yatalingana na kiwango cha mapenzi ulichonacho juu ya watu hao wema. Mahusiano matupu ambayo si ya kiroho huwa hayana mwisho mwema, bali yatapatikana manufaa machache tu. Katika kulifafanua zaidi hili hebu tuangalie tukio lifuatako linalomuhusu Bayazid Bistami – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake:





Siku moja mmoja wa wanafunzi wake walimuuliza, “Je unaweza kunitendea wema kwa kunipatia kipande cha koti lako la hariri ili niweze kuwa nalo kwa ajili kupata manufaa ya kiroho (*tabarruk*)?”

“Mwanangu”, alijibu Bayazid, “Si tu kumiliki kipande cha koti langu, bali hata kama ingelikuwa ni kuchuna ngozi ya Bayazid na kuingia ndani ya mwili wake kusingelikuwa na manufaa yoyote kama wewe hauna msimamo sahihi!”

Ulimwengu mzima unaonyesha mwelekeo kuelekea kwenye kuungana. Hili linatokana na ukweli kwamba asili ya wanadamu ni moja. Mwelekeo huu kuelekea kwenye kuungana na kuwa wamoja na kutafuta ufanano ndani yake ni sahihi kwa upande wa kimwili na kiroho. Kwa mfano kama chupa iliyojaa kimiminika chenye harufu kali itamiminwa katika moja ya kona ya chuma basi harufu yake itasambaa tokea upande mmoja mpaka mwingine kwa kupitia chembechembe za hewa mpaka kufikia chumba kizima kuwa na harufu moja. Hii ni kanuni ya fizikia ambayo inakubali kwa hali nyingine kama vile joto na baridi. Lakini ili hii kanuni ya ufanano iweze kujidhihirisha katika maisha ya mwanadamu kunahitajika njia ya kuwezesha huu muungano. Na njia hiyo ni upendo. Kimazungumzo jambo hili limekuwa maarufu kwa kupitia msemu usemao, “Kuna njia itokayo kwenye moyo mmoja na kuelekea kwenye mwingine”.

Sifa za nguvu na nishati zimekuwa sababu za msukumo kwa walio dhaifu. Shauku ya kuiga ni jambo lililomo katika silka ya mwanadamu. Mtoto huendesha matendo yake na tabia zake zote kwa kuiga. Mwenendo huu huendelea kwa namna tofauti tofauti hata baada ya utoto. Hivyo kiwango cha umakinifu walichonacho watakatifu na watu wema pindi wanapotekeleza ibada zao, mwenendo wao mtukufu katika maadili, viwango vyao vya imani, huwa vinaleta hisia za kuiga na kujipamba nazo kwa wale wanaowazunguka. Ni kwa kupitia si kingine bali ari hii ya kumuiga Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ndio maana maswahaba karibia wote wakawa na historia zenye kuvutia na kuwapelekea kuwa vilele vya wema.

Tunafahamu kutokana na uzoefu kwamba pindi mwalimu atakapoonysa upendo kwa wanafunzi basi hata somo analolifundisha litakuwa rahisi na lenye kufurahiwa na wanafunzi. Upendo una namna fulani ya maajabu katika kubadili ugumu kuwa wepesi. Sehemu yenye upendo







hupelekea jukumu lolote lile litekelezwe kwa wepesi hata kama litakuwa zito kiasi gani. Kwa upande mwingine jukumu lililotekelezwa kwa chuki huwa zito kuliko lilivyo. upendo hufanya rakaa ishirini za swala ya *tarawih* kuwa kama upepo mwanana wakati ukosefu wa upendo hupelekea rakaa nne za swala ya alfajir kuwa mzigo. Katika ibada hizi ubwege na uvivu ni matokeo ya ukosefu wa upendo. Pindi yote haya yatakapozingatiwa na mtu akaruhusu kutawaliwa na upendo utakaotokana na kuwa karibu na watakatifu na watu wema basi upendo huwa utakuwa kama fimbo ya maa-jabu yenye kugeuza kilima katika njia ya kiroho na kuwa njia iliyonyooka.

Jambo lingine ni kwamba ili kuubakiza moyo kwenye amani mtu hana budi kujiweka mbali na ujinga na ukaidi (*fasiq*). Licha ya yote hayo upepo wenye kuvuma kwa kupitia kwenye mzoga au shimo la maji machafu hubeba harufu yake mbaya na kuisambaza hivyo kusumbua upumuaji na kuwasumbua watu.

Sheikh Ubaydullah Ahrar – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliwapa rafiki zake ushauri ufuatao: “Kuwa karibu na watu wasio makini hudhoofisha moyo na kuvuruga utaratibu wa roho na moyo”.

Siku moja Bayazid Bistami – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alihisi uvurugwaji huu na ukosefu wa utulivu. Kila alichokuwa anakifanya alikuwa hapati suluhisho. Akaamua kuwageukia wale aliokuwa nao na kuwaambia, “Angalieni miongoni mwetu kama mtamuona mgeni”. Ingawa waliangalia lakini hawakumuona mgeni yeyote. Lakini Bayazid hakuridhika. “Angalieni vizuri...hasa walipo watumishi”, alisisitiza. Waka-fanya kama walivyoagizwa. Na baada ya kuangalia kwa makini walimpata mtumishi ambaye alitoka kwa mtu asiyekuwa makini, kisha wakamtoa nje upesi. Baada ya hapo ndipo Bayazid akapata utulivu wa akili.

Vile vile siku moja Ubaydullah Ahrar

- Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alimuambia yafuatayo rafiki yake aliyekuwa amemtembelea, “Unanukia ugeni”, kisha baada ya kunyamaza kidogo akaongezea, “Inawezekana umevaa mavazi ya mtu mgeni”. “Hilo ni kweli kabisa”, yule mtu alijibu huku akistaajabishwa na jambo lile, alitoka nje upesi na kurejea baada ya kubadili yale mavazi.

Uwezo wa kuhamisha tabia mbaya kwa wengine pia unaweza kuwepo katika kuhamisha tabia njema. Mfano mzuri juu ya hili ni suala la Yaqub





(a.s) na Yusuf (a.s). Baada ya kuona taswira yake na tabia zake kwa Yusuf (a.s), Yaqub (a.s) alitokea kumpenda sana kuliko watoto wake wengine. Ufanano wake na Yusuf (a.s) ulikuwa wa kiwango kikubwa sana kiasi kwamba pindi shati la Yusuf (a.s) lilipokuwa linaletwa kwake kutoka Misri aliweza kuhisi harufu yake licha ya kwamba lilikuwa mbali mno tokea Canaan. Hakuna mtu mwingine aliyeweza kuhisi siri ya harufu ile hata Judah mwenyewe ambaye aliyekuwa amelibeba shati lile. Shati lile lilipopanguswa kwenye macho ya Yaqub (a.s) ndipo akaanza kuona tena. Na huu ndio udhihirisho wa muungano wa kiroho uliojipenyeza kwenye hata vitu vinavyoonekana kutokuwa na uhai. Tukitafakari namna ambavyo hali ya kiroho inaweza kuingia hata kwa maada tutagundua hitajio lililopo katika kuulinda moyo ambao bila shaka ni muhimu kuliko maada.

Wakubwa wa kisufi wanasema:

“Hata vitu visivyo na uhai hupata mwangaza juu ya matendo na maadili ya watu. Hivyo kuna tofauti kubwa katika thamani kati ya matendo ya ibada yaliyotekelezwa katika sehemu ambayo madhambi ya kila namna yametapakaa na sehemu ambayo imekuwa mahala pa matendo mema. Hii ndiyo sababu inayopelekea swala iliyoswaliwa jirani na Al- Kaaba kuwa bora zaidi ya swala iliyoswaliwa sehemu nyingine”.

Kinyume kabisa na sehemu kama hizi zenye msukumo mkubwa wa kiroho kuna sehemu nyingine ambazo zinaleta ugumu na huzuni. Maswahaba walipokuwa wanarejea kutoka katika vita vigumu vya Tabuk walifika kwenye bonde la Hijr, sehemu ambayo walikuwa wakiishi watu wa kabila la Thamud. Kisha Mtume aliyebarikiwa (s.a.w) akawaonya:

*“Hapa ni mahala ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwaangamiza watu wa Thamud”, alisema. “Kwa hiyo msichote maji yoyote sehemu hii msije mkafikiwa na mgao wa ghadhabu za Mwenyezi Mungu”.*

*“Tumeshajaza chupa zetu za maji ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, isitoshе tayari tumeshaandaa mikate kwa kutumia maji haya”, maswahaba walisema.*

*“Mwageni hayo maji na hiyo mikate muwalishe ngamia”, Mtume aliwaamrisha. (Bukhari, Anbiya, 17)*

Hadith hizi ni mifano hai juu ya namna ambavyo hali ya kiroho ya eneo husika inavyosambaa na kuvigusa hata vitu visivyo na uhai.





Ili mtu akuze na kustawisha tabia za kiroho za moyo hana budi kujitahidi kupata muongozo wa kiroho na nguvu kutokana na mwenendo wa watakatifu na watu wema. Namna nzuri ya kuwezesha kupata tafakuri hii ya kiroho ni kwa kupitia *sohbah*, yani maongezi ya kiroho au hotuba. Hili linathibitishwa na ushauri wa Luqman (a.s) kwa mwanae:

“Kuwa karibu na watu wenye elimu na jitahidi usijitenge na *sohbah*; kwani Mwenyezi Mungu huhuisha moyo wenye mwangaza wa hekima kama anavyohuisha ardhi iliyokauka kwa mvua” (Ahmed ibn Hanbal, Kitabu’z-Zuhd, na: 551).

*Hadith* ifuatayo inaonyesha vizuri zaidi umuhimu wa *sohbah* na manufaa yake kwa muumini: “Pindi kundi la watu litakapokusanyika katika nyumba miongoni mwa nyumba za Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kusoma Kitabu cha Mwenyezi Mungu na kujadiliana kuhusu kitabu hicho wao kwa wao basi kwa hakika *sakina* (utulivu wa kiroho) itawafikia; watagubikwa na rehema takatifu na kuzungukwa na malaika. Na Mwenyezi Mungu atawataja mbele ya malaika zake” (Abu Dawud, Witr, 14; Ibn Maja, Muqaddima, 17).

Abu Idris al-Hawlani anasimulia:

“Nilikuwa nimeingia kwenye msikiti wa Umayya ndani ya Damascus. Ndani yake alikuwepo kijana mwema mwenye meno kama lulu. Watu walikuwa wamemzunguka huku wanajadiliana kuhusu mambo fulani. Pindi walipotofautiana walikuwa wakimuuliza yule kijana na kukubali hukumu yake. Muda si mrefu nikagundua kuwa yule kijana hakuwa mwingine bali alikuwa Muadh ibn Jabal – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.

Mapema siku iliyofuata nilienda tena pale msikitini. Nilipofika pale alikuwa tayari ameshafika kabla yangu na anaswali. Nilimsubiri amalize. Kisha nikamsogelea na baada ya kumsalimia nikamwambia:

‘Ninakuhakikishia kwamba ninakunda kwa ajili ya Mwenyezi Mungu’

‘Je ni kweli kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?’ aliuliza Muadh – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. ‘Ndio’, nilijibu. Alilirudia swali lile mara tatu na mara zote nilitoa jibu lile lile.

Kisha akakamata shati langu na kunivuta karibu yake na kuniambia, ‘Nakupa bishara njema, kisha...kwani nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – anasimulia maneno yafuatayo kutoka kwa Mola wake:





‘Mapenzi yangu yapo juu ya wale wanaopendana wao kwa wao, wanaokuwa pamoja na kutembeleana kwa ajili Yangu, na ambao wamejitolea kutafuta radhi zangu’” (Imam Malik, Muwattaa, Shaar, 5).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.” (at-Tawba, 119).

Kama tulivyotangulia kusema, hali ya akili ya kiroho (*hal*) husambazwa kulingana na hisia za upendo na udugu zilizopo. Ili kuimarisha imani ni muhimu kujenga udugu kwa watakatifu na watu wema, kuwapenda na kuwa karibu yao kadiri iwezekanavyo na kuruhusu mwenendo huu ukue zaidi ili mwishoni ulete matokeo yanayotarajiwa.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anafanua zaidi juu ya umuhimu wa kuwa karibu na watu wema katika maneno yafuatayo:

“Mfano wa rafiki mwema na rafiki mbaya ni kama mfano wa mtu anayeuzua miski na mfua vyuma. Kwa upande wa muuza miski, ama upate harufu kutoka kwake au ununue manukato hayo kwake. Kwa upande wa mfua vyuma, ama uunguziwe nguo zako au utapakaliwe na harufu ya moshi” (Bukhari, Buyuu, 38)

Licha ya umuhimu wa kuwa pamoja na watu wema katika maisha yetu, lakini pia Mjumbe Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – amegusia juu ya umuhimu wa kuzikwa karibu yao: “Zikeni maiti zenu karibu na watu wema” (Darimi, Musnad, 1, 102).

Pia kupata mahitaji yako kwa kupitia watu wema kumetajwa. Ibnu'l-Firasi anasimulia kwamba siku moja baba yake alimuomba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ikiwa anaruhusiwa kuwaomba wengine wamkidhie mahitaji yake.

“Hapana, usifanye hivyo!” alijibu, kisha akaongezea, “Likini pindi utakapojikuta katika hali ambao hauna budi basi angalau waombe watu wema” (Abu Dawud, Zakat, 28; Nasai, Zakat, 84).





Vile vile Mtume wetu kipenzi amesema: “Kuna watu ambao ni ufun-guo wa *dhikrullah*. Pindi watu wanapowaona upesi humkumbuka Mwe-nyezi Mungu” (Haythami, x, 78).

Siku moja Qadi Shurayh alimuandikia barua Omar – radhi za Mwe-nyezi Mungu ziwe juu yake – akimuuliza yeye kama jaji atatakiwa ahu-kumu vipi kati ya watu. Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akajibu kama ifuatavyo:

“Hukumu kati yao kwa kile kilichofunuliwa ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Kama hutaweza kupata hukumu ndani yake basi igeu-kie *sunnah* ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake. Kama hutaweza kupata hukumu ndani yake basi tumia hukumu za watu wema. Na kama hutaweza kupata hukumu kwao basi ni juu yako ikiwa utasonga mbele na kuhukumu au utarudi nyuma. Mimi nipo kwenye mawazo kwamba kurudi nyuma kutakuwa bora kwako” (Nasai, Qudat, 11/3).

Siku moja daruwesh alimtaka Bayazid Bistami – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amshauri juu ya amali ambayo itamsogeza karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

“Wapende waja wa Mwenyezi Mungu walio wema! Wapende kiasi kwamba nao wakurudishie mapenzi yako. Jaribu kutafuta njia ya kuingilia nyoyoni mwao, kwani Mwenyezi Mungu huangalia moyo wa mtu mwenye hekima mara mia tatu na sitini kwa siku. Mfanye akukute humo wakati wa kuangalia kwake!”

Hakuna sababu nyingine inayopelekea mafunzo ya kisufi kuhitaji muendelezo wa kujizoeshwa na *rabitah*<sup>23</sup>, kuhakikisha kuwa *murid* au mwanafunzi anakuwa na mapenzi juu ya mtu mwema aliye juu yake.

Hakuna budi kukumbukwa kuwa kwa kupitia mshikamano huu mtu aliyekamatwa na madhambi na maovu ataweza kuzuia hasara nyingi za kiroho ambazo zinaweza kutokea. Na zaidi ni kwamba kwa kupitia mshika-mano huu wa kiroho ataweza hata kupata manufaa zaidi hapo baadae.

Kulingana na kiwango cha mapenzi, *rabitah* hujenga mkondo wa nguvu ya kiroho ambayo imejaa utambuzi na hisia za kiroho. Baada ya

23 Kwa maelezo zaidi rejea ukurasa wa 249-257.





hapo uhamishaji wa kiroho huanza kati ya watu wa wawili walio katika pande mbili zinazotazamana na ambazo zinaendana na muungano. Katika uhamishaji huu wakati mtu ambaye ndiye mpokeaji anasonga mbele kiroho, lakini mtu mwema au mtakatifu ambaye ndiye mtoaji huweza kuathirika kwa kiwango fulani. Huu ni mchakato ambao watu wema ambao ndio sababu ya msukumo wa kiroho wanapoweza kuwasafisha wale wanaokuja kwake, ambao wamechafuka kwa uchafu wa kiroho, jambo ambalo linaweza kulinganishwa na kufua. Watu hao wema ambao wamepewa kibali cha kuongoza (*irshad*), kusafisha na kuondokana na uchafu na kutu ya wale wanaowalazimu kuwafundisha, hasa kutoka ndani ya nyoyo zao. Katika jamii watu wa namna hii hutambulika kama watakasaji, kama mimea inavyobadilisha chembechembe ambazo zimeoza na kusagika na kuwa maua yenye rangi nzuri na matunda matamu.

Baada ya kuyasema hayo, katika maisha ya kila mtu mwema na mtakatifu mwenye kibali cha kuongoza kuna kipindi cha upweke, kinaweza kuwa kifupi au kirefu. Hili halitokani na tamaa ya kuwa karibu na Mwenyezi Mungu peke yake bali pia kutokana na hitajio la kujiweka mbali na vitu vibaya katika maisha kwa kiasi fulani cha muda.

Upendo ulioambatana na urafiki wa karibu mno humpelekea mpenzi kuteketezwa mbele ya kipenzi chake, kama alivyoliezea hili Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake: “Mto unaoingia baharini hauwi mto tena; unakuwa ni sehemu ya bahari inayoiingia. Kipande cha mkate tuna-chokila huyeyuka ndani ya miili yetu na kuwa sehemu ya miili yetu. Vivyo hivyo uwepo wa mpenzi huyeyuka ndani ya kipenzi chake kulingana na uzito wa mapenzi yake”.

Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anaendelea kufafanua hali ya roho inayopitia hali ya muungano na kuteketea: “Upendo ulikuja na kama damu ulijaza mishipa yangu na ngozi yangu. Ulinipeleka mbali na mimi na kuniingiza kwa kipenzi changu. Kipenzi changu kimefunika kila chembechembe ya mwili wangu. Kilichobaki kwangu ni jina pekee. Vingine vyote ni yeye.

Haya ni yale yanayofahamika katika *tasawwuf* kama *fanafillah* na *bakabillah*<sup>24</sup>. Lakini hakuna muendelezo wa njia hii ambao utamuongoza





mtu kuelekea kwenye mapenzi ya Mola wake, ni jambo la msingi kwa moyo kuwa na tabia ambayo itakuwa na manufaa na ambayo itakuwa ni muafaka katika jukumu hili. Na hili hupatikana kwa kujizoeshia mapenzi ya kibinadamu.

Mapenzi kati ya wanadamu yameruhusiwa na yameitwa mapenzi ya sitiari (*ashk-i majazi*);

Kama mapenzi anayohisi mtu juu ya watu wa familia yake. Haya yote ni kwa kuwa yanafanya kazi kama maandalizi ya kuelekea kwenye mapenzi ya kweli lakini ikiwa hayatapita mipaka halali. Lakini bado katika kuyafafanua mapenzi na kufahamu kiwango chake mtu hana budi kuzingatia maelekezo fulani, maelekezo ambayo mwangaza wake umetolewa na Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kama ifuatavyo:

“Kuwa na huruma...mapenzi ni kitu kizuri. Kinachoyaharibu ni tabia zako mbaya. Tamaa unaiita mapenzi. Hapana...lau kama ungelifahamu ukubwa wa umbali uliopo kati ya mapenzi na tamaa!

Mapenzi matakatifu na furaha humfanya mja awe macho wakati wote. Tamaa ya kidunia na ya kifisadi humpelekea mtu kuwa mjinga na kumuacha kwenye bumbuwazi. Mapenzi ni kuungua na kutapatapa kwa mwanadamu ambaye ameumbwa kwa maji na udongo. Usafirishwaji wa damu kwenye mishipa si muhimu...cha muhimu ni mapafu kuungua kwa mapenzi”

Kilele cha mapenzi ya kibinadamu hufikiwa pale mpenzi anapokuwa kitu kimoja na kipenzi chake kwa kiasi cha mapenzi waliyonayo. Katika *tasawwuf* kilele cha mapenzi aliyonayo mwanafunzi juu ya mwalimu wake kiasi kwamba akazama kabisa ndani ya mwalimu wake kinaitwa *fana fi’s* – *sheikh*.

Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa aki-hisi raha isiyo na kifani pindi alipokuwa akikutana na kuongea na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Licha ya kuridhika pindi

---

*Fanafillah* ni kuangamia kwa Mwenyezi Mungu; yani kuondoa moyoni vitu vyote vinavyohusiana na dunia na kutakasika dhidi ya tabia za nafsi.

*Bakabillah* ni pale mja ambaye amejivua tabia zote za nafsi na kushikamana na maadili ya Mola ambayo hutokana na kushikamana na maadili na mwenendo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na Qur’an tukufu.





walipokuwa wanapokutana na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – lakini pia mapenzi na shauku yao juu yao vilikuwa viki-ongezeka.

Wakati fulani Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – alisema, “Sijapata kunufaika na mali za mtu yeyote zaidi ya nilivyonufaika na mali za Abu Bakr”. Baada ya Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kusikia maneno haya alishindwa kujizuia na hisia kuwa alichukuliwa kuwa mtu ‘mwingine’. Kwa kuwa yeye ndiye mtu aliyekuwa akizungumziwa na hapa tunaona kuwa uzungumziwaji huu unamaanisha mwingine, alihisi kuwa ametolewa kwenye ukaribu na Mtume - rehema na amani ziwe juu yake. Aliibuka na hisia kali ndani ya moyo wake, hisia za utenganisho. Kwa kuhofia kuwa angelichukuliwa kuwa mtu ‘mwingine’, alilalamika: “Je mimi na mali zangu si kwa ajili yako peke yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?” (ibn Majah, Muqaddima, 11).

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amelezea hali hii ya akili kwa maneno mazuri sana kama ifuatavyo:

“Mapenzi ni nini, Maisha ya mtu binafsi ni nini...Nini lulu na marijani zipi ambazo hazijatumika kama muhanga kwa ajili ya kipenzi?”

Vile vile wakati mwingine Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa hoi kitandani kutokana tu na huzuni aliyoipata baada ya kusikia kuwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ni mgonjwa. Kutokana na kufanana huku ndio maana Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akatoa maneno yafuatayo yenye kudhihirisha muungano wa kiroho unaotokea kati ya moyo mmoja na mwingine:

“Abu Bakr anatokana na mimi, na mimi ninatokana na yeye. Yeye ni ndugu yangu hapa na kesho akhera” (Daylami, Musnad, 1,437),

Vile vile katika kuonyesha mkondo uliopo kati ya moyo mmoja na mwingine Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake- alitoa maneno yafuatayo pindi alipokuwa juu ya kitanda cha mauti:

“Fungeni milango yote isipokuwa wa Abu Bakr” (Bukhari, Ashabu’n-Nabi, 3).

Sheikh Sadi Shirazi anaelezea uhamishaji wa *hal*, yani dhamira ya







kiroho, kama ifuatavyo: “Ni kutokana na kuwa pamoja na watu wema ndio maana ikapelekea mbwa wa watu wa pangoni akapata heshima kubwa ya kutajwa ndani ya Qur’an. Kwa upande mwingine mke wa Lut (a.s) alijisababishia aibu mwenyewe kutokana na kubakia kwenye upande wa makaidi.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake- anatuonya juu ya madhara ambayo yanaweza kutokea ndani ya moyo kutokana na kufanya urafiki na mjinga: “Itafika kipindi ambacho sehemu ya watu miongoni mwa umma wangu ambao watadai kuwa wameelimika katika dini, watasoma Qur’an na kusema, ‘Tutaenda kwa magavana na kunufaika kutokana na wanavyovimiliki na kuwatoa kwenye dini zao’. Lakini hili halitakuwa hivyo. Kama ambavyo mtu anakusanya miba watu hawa wataishia kukusanya vitu ambavyo vitawadhuru” (Ibn Majah, Muqaddima, 23).

Sheikh Sadi katika Gulistan yake anatumia mafumbo kuelezea uhamishaji wa dhamira ya kiroho unapatikana kwa kujenga urafiki na watakatifu na watu wema na kupelekea kwenye ‘ufanano’:

“Mtu mmoja anaenda kuoga. Mmoja wa marafiki zake anampatia kipande cha udongo wenye harufu nzuri kwa ajili ya kujisafishia. Ule udongo unatoa harufu nzuri kiasi kwamba unaupendezesha moyo wake. Kisha yule mtu anaauliza ule udongo:

*‘Mimi sitokani na maski wala kaharabu’, udongo ulijibu. ‘Mimi ni udongo wa kawaida kama mnavyofahamu. Nilikuwa niko chini ya ua la waridi huku nikinyunyiziwa kila siku na umande uliokuwa ukidondoka kutoka kwenye kikonyo cha waridi. Harufu unayoihisi haitokani na kingine zaidi ya waridi hilo’*

Kama ilivyodokezwa katika maana ya ndani ya fumbo, wale wanaowafungulia nyoyo zao watu wema kwa imani, kujisalimisha na unyenyekevu, taratibu huanza kutafakari juu ya uzuri wanaopigania kuupata.

Kama ulivyo upande wa mwezi ambao unaakisi miale ya mwanga wa jua na hivyo kuwa sehemu ya jua licha ya kuwa hauna mwanga wake wenyewe, watu wa namna hiyo huwa kama mishumaa ambayo inaangaza viza vinene vya wanadamu, vina vinavyotokana na vumbi la dhulma.





## j. Kujipamba na maadili mema

***“Hakuna kitu kitakachokuwa kizito katika mizani ya muislamu kesho akhera zaidi ya maadili mema. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawachukia wale wenye kutenda na kuongea machafu” (Tirmidhi, Birr, 62).***

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajaalia wanadamu kuwa na usanifu, huruma na imani. Thamani ya wanadamu inategemeana na namna ambavyo wataruhusu sifa hizi zistawi kwenye udongo wa moyo wake. Kuwa mwanadamu kimwili na cha muhimu zaidi kiroho kunapelekea kuwepo ulazima wa kujipamba na maadili mema na kujitenga na tabia mbaya.

Nyoyo zilizojawa na imani huwakilisha maadili mema, mwenendo mwema na hali bora ya kiroho. Ni kwa namna hii ndipo mja anaweza kuishi huku akitambua kuwa ameumbwa katika umbile bora kabisa.

Kinyume chake nyoyo zilizotawaliwa na nafsi, zenye kufi, shirk, tabia mbaya humsahau Mola wake na kuwa kipofu na kwenda kinyume kabisa na lengo la kuumbwa kwake. Kibaya zaidi unaweza kuwa muovu zaidi kuliko viumbe vipumbavu.

Muumba wa ulimwengu anamuongelesha mwanadamu kwa kumtahadharisha huku akimuusia ajitambue na kuacha kujishusha:

يَا أَيُّهَا الْإِنْسَانُ مَا غَرَّبَكَ بِرَبِّكَ الْكَرِيمِ الَّذِي خَلَقَكَ

فَسَوِّيكَ فَعَدَلَكَ فِي أَيِّ صُورَةٍ مَا شَاءَ رَكَّبَكَ

“Ewe mwanaadamu! Nini kilicho kughuri ukamwacha Mola wako Mlezi Mtukufu? Aliye kuumba, akakuweka sawa, akakunyoosha, Katika sura yoyote aliyo ipenda akakujenga.” (al-infitar, 6-8)

Pia ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَاللَّهُ يَدْعُوا إِلَى دَارِ السَّلَامِ





“Na Mwenyezi Mungu anaita kwendea Nyumba ya Amani, na anamwongoa amtakaye kwenye Njia Iliyo Nyooka” (Yunus, 25).

“Mola wangu amenifundisha na uzuri ulioje kwa namna alivyoni-fundisha” (Suyuti, al-Jamiu’s-Saghir, 1,12).

“Hakuna kitu kitakachokuwa kizito katika mizani ya muislamu kesho akhera zaidi ya maadili mema. Mwenyezi Mungu Mtukufu anawachukia wale wenye kutenda na kuongea machafu” (*Tirmidhi, Birr, 62*).

“Nimetumwa kwa ajili ya kutimiza tabia njema” (imam Malik, Muwat-taa, Husnu’l-Khulq, 8).

Mtume Muhammad Mustafa – rehema na amani ziwe juu yake – si tu Mtume pekee ambaye kila hatua ya maisha yake imewekwa kwenye kumbukumbu bali ni mtu pekee katika historia ambaye amefanyiwa hivyo. Kila neno lake, tendo lake na hisia alizozitoa vyote viliandikwa na kusambazwa kwa wanadamu wote kama ishara ya heshima. *Uswatu’l – hasanah* yake, yani mfano mtukufu wa kuigwa, imetoa mwongozo kwa wanadamu wote kama ambavyo imeelezwa ndani ya Qur’an: “Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana” (al-Ahzab, 21).

Kwa kuwa ni jambo jema kutafuta kuwa sehemu ya maadili na tabia njema ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, jambo hili linaweza kufanyika kulingana na kiwango cha upendo juu yake na ni kwa kiwango gani anashikamana naye. Kutokana na kutafakari juu ya mafunzo yanayopatikana ndani yake kutampelekea muislamu kuwa na shauku ya kuwa na tabia kama vile huruma, upendo, wema, msamaha na kugawana na waislamu wenzake kile alichonacho. Maswahaba, watakatifu na watu wema ni mfano mizuri wa kuigwa katika hili.

Kwa kujisogeza karibu zaidi kwenye ukweli wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kuwa kama miale ndani ya moto wa imani yake, wakati wote waumini hawa watukufu wamechukulia kughariki ndani ya imani ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kama baraka kubwa kuliko zote miongoni mwa baraka ambazo anaweza kuzipata mtu ndani ya dunia hii. Katika historia nzima waislamu





ambao waliweza kuwa na sehemu ya mfano wa kuigwa wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – wamesababisha imani zao kukua kwa kiasi kikubwa mno na hivyo kukomaza furaha takatifu iliyopo ndani ya silka yao, watu hawa wamekuwa kama tochi kwa wanadamu. Katika kumpenda Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kunapatikana tiba ya nyoyo zenye maradhi na zisizojitambua.

Ifuatayo ni baadhi ya mifano halisi juu ya mwenendo na tabia yake njema:

*Uso wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ulikuwa maridadi na wenye kuvutia kuliko nyuso za watu wengine wote. Baada tu ya hijra myahudi mmoja aliyeitwa Abdullah ibn Salama aliulizia namna ambavyo ataweza kumkamata Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – lakini pindi alipomuona alisema:*

*“Sura kama hiyo kamwe haiwezi kudanganya”. Haya yalikuwa maneno yake ya mwisho kama myahudi kabla ya muda mfupi kuingia kwenye uislamu. (Tirmidhi, Qiyama, 42/2485; Ahmed ibn Hanbal Mus-nad, V, 451).*

Kutokana na uzuri na utukufu wake hakuhitaji ushahidi zaidi wala miujiza ili kuthibitisha ukweli kwamba yeye ni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa akikwazwa au kuvutiwa na jambo upesi liliweza kudhihirika usoni mwake. Alikuwa ni mwenye ari kubwa, haya na utambuzi wa hali ya juu. Alikuwa na adabu kuliko mwanamwali aliyejigubika ushungi. Kutokana na uzito wa imani yake hakuna ambaye anaweza kumuelezea kwa ufasaha.

Kamwe hakuwahi kutoa neno lisilo na faida, kila neno lake lilibeba hekima na ushauri. Katika maneno yake hakukuwahi kusikika usengenyi wala maneno ya upuuzi. Alikuwa akiongea na watu kulingana na uwezo wao. Alikuwa mwema na mwenye staha. Ingawa hakuwa anadhihirisha furaha yake kwa kicheko kilichopita mipaka lakini wakati wote uso wake ulikuwa ni wenye kutabasamu. Ilikuwa pindi unapomuona tu basi unajawa na shauku juu yake ingawa maongezi naye machache yalitoshwa kukuizingizia hisia za mapenzi makubwa juu yake.

Alikuwa akikaa na watu wema kwa heshima kulingana na kiwango cha uchamungu wao. Aliishi na ndugu zake kwa heshima na taadhima.





Alikuwa na kawaida ya kupeleka kwenye jamii yote ukarimu aliokuwa nao juu ya familia yake na marafiki zake, na huku akisema: “Hamtofikia daraja la juu la wema mpaka mtamani kwa ndugu zenu yale mnayoyatamani kwa ajili ya nafsi zenu” (Bukhari, iman, 7; Muslim, iman, 71-72). Alikuwa akiwatendea wema wa hali ya juu watumishi wake, pia alikuwa akiwavisha na kuwalisha na kila alichokuwa akikivaa na kukila. Kutokana na ukarimu na huruma ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – aliweza kuweka uwiano mzuri kati ya matumaini na wema kulingana na hali iliyokuwa mbele yake.

Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa ni mtu mwenye kutekeleza ahadi zake, siku zote alikuwa mkweli katika ahadi zake. Kutokana na kuwa bora kuliko wote kimaadili na kiakili upekee wake wa kimwili na kiroho haukuweza kuelezewa kwa ufasaha zaidi.

Wakati wote alikuwa akionekana ni mwenye huzuni. Huku akiwa kati-hali hali ya kutafakari, alikuwa akiongea pale tu kulipokuwa na umuhimu wa kufanya hivyo. Kimya chake kilikuwa kirefu zaidi. Zaidi ya hayo ni kwamba alikuwa akikamilisha kila sentensi aliyokuwa akiitoa, pia alikuwa akikusanya maana nyingi katika maneno machache. Alikuwa akitoa maneno yake kipande baada ya kipande. Maelekezo yake ya upole yalipelekea kuwavutia mno watu.

Kamwe alikuwa hanyanyuki kwenye kiti chake pindi alipokuwa na hasira. Na kamwe alikuwa hashikwi na hasira ila pale tu kulipokuwa na uvunjaji wa haki. Pale palikuwa na uvunjifu wa haki alikuwa hatulii mpaka ahakikishe muhusika anapata haki yake. Na baada ya hapo alikuwa akirejea katika hali yake ya kawaida ya utulivu. Hakuwa na tabia ya kuwa na hasira kwa sababu zake binafsi, kamwe hakuwa akijenga kisasi na kuwa mwenye furugu kwa ajili ya nafsi yake.

Alikuwa haingii kwenye nyumba ya mtu mpaka apewe ruhusa. Alipokuwa akirejea nyumbani kwake alikuwa akiugawa muda wake katika sehemu tatu: ya kwanza kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, ya pili kwa ajili ya familia yake na ya tatu kwa ajili yake mwenyewe, ingawa kiuhalisia muda huu alikuwa akiutumia kwa ajili ya watu wote, watu wa kawaida na watukufu, na alikuwa hamnyimi hata mtu mmoja muda huu adhimu, hivyo kugusa moyo wa kila mtu.





Kila hali na tabia ya Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – vilikuwa vikidhihirisha *dhikrullah*.

Misikitini alikuwa akikaa sehemu tofauti tofauti ili kuzuia watu wengine wasije wakawa na tabia ya kukaa sehemu moja tu, na kuzuia sehemu fulani fulani zisije zikafanywa kuwa takatifu. Alikuwa hapendi tabia ya kujisifu mbele za watu. Kila alipokuwa akiingia kwenye mkusanyiko wa watu alikuwa akikaa sehemu yoyote ile iliyokuwa wazi, na pia alikuwa akiwasisitiza wengine kufanya hivyo.

Pindi mtu yeyote alipokuwa akihitaji kitu kutoka kwake kwa ajili ya kutatua tatizo fulani, bila kujali tatizo lilikuwa na uzito kiasi gani alikuwa hatulii mpaka aone limetatuliwa. Pale alipoona hawezi kutatua tatizo lile alikuwa akimliwaza mtu husika na kumpa maneno ya kumtia moyo. Alikuwa msiri wa watu wote. Haikujalisha watu fulani walikuwa katika nafasi gani katika jamii, ama matajiri au masikini, wajuzi au wajinga, wote walikuwa wakitendewa wema sawa sawa kwa kuwa wote walikuwa ni wanadamu. Katika mikusanyiko yake yote kulitawaliwa na wema, hekima, subira na uaminifu, kwanza kabisa kati yao na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kisha kati yao wenyewe.

Kamwe hakuwa akimlaumu mtu mbele ya watu kutokana na makosa yake. Pindi kulipokuwa na hitajio la kumuonya mtu, Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akionya juu ya jambo lile kwa upole bila ya kuumiza moyo wa mtu husika. Alikuwa anaweza akasema: “Usifurahie juu ya ubaya unaomfika ndugu yako...kwani Mwenyezi Mungu anaweza kumuondolea ubaya ule kwa rehema zake na kukujaribu na wewe kwa janga hilo hilo” (Tirmidhi, Qiyamah, 54).

Kamwe hakuwa akishughulishwa na kudadisi kasoro za wengine, badala yake alikuwa mkali katika kuwakataza wengine wasijishughulishe na upuuzi huo. Hata hivyo kudadisi na kuwadhanja watu ubaya ni jambo lilikatazwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – hakuwa akiongea isipokuwa kwa lengo la kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Mazungumzo yake yalikuwa yakileta raha katika nyoyo. Maswahaba walikuwa wakimsikiliza kwa umakini mkubwa pindi alipokuwa akiongea na





hili linadhihirishwa na maneno ya Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, ‘kama ingelitokea ndege wakatua juu ya vichwa vyao basi wangeliveza kubakia hapo bila ya kusumbuliwa kwa masaa kadhaa. (Abu Dawud, *Sunnah*, 23-24/4753). Maadili na *haya* waliyokuwa nayo maswaha vilikuwa na uzito mkubwa kiasi kwamba hata kumuuliza maswali Mtume kulionekana ni utovu wa nidhamu. Hivyo walikuwa wakisubiri Bedui kutoka jangwani aje na kumuuliza maswali Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na hapo ndipo walipokuwa wakiibua mjadala ambao waliona utakuwa na manufaa kiroho. (Angalia, Ibn Saad, 1,422-425; Haythami, EX, 13).

Abu Hurayra – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea wingi wa huruma yake kama ifuatavyo:

“Wakati wa kipindi kigumu cha vita tulimsihi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – awalaani washirikina ili waangamie. Lakini alisema, ‘Sikuletwa kwa ajili ya kulaani bali kuwa rehema’” (Muslim, *Birr*, 87).

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo ndani ya Qur’an kuhusiana na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ

“Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote” (al-Anbiya, 107).

Ahmed ar-Rifai - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - ambaye ni mtu mkubwa katika imani anatoa ushauri ufuatao kwa watoto wake wa kiroho:

“Enyi watafutaji wa hekima, utumieni umri wenu wote katika njia ya haki. Shikamaneni na *Sunnah* ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake. Tumieni usiku na mchana kwa ajili ya ibada na mwenendo mwema. Kwa kupitia njia hii ndipo mtakapoweza kupata *mari-fah*. Kinyume chake hamtopata kitu katika hili. Kwa kushindwa kuwa kitu kimoja na *hal* yake basi mtaishia kuwa waja wabaya”.

Mwenendo mwema wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambao tumetoka kutoa mukhtasari wake licha ya fursa ndogo ya





maneno, ni kama matone yaliyopo kwenye uelewa wetu ambayo yanatoka kwenye bahari hiyo kubwa. Siri iliyopo katika *wasl ila'Mwenyezi Mungu* au kumfikia Mwenyezi Mungu Mtukufu imejikita katika kushikamana na Kitabu cha Mwenyezi Mungu na *Sunnah* za Mtume wake kwa moyo safi, na pamoja na kuwapenda wale ambao Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake wanawapenda na kuwachukia wale ambao wanawachukia.







**K**wa wenye busara ulimwengu ni gwaride lenye kuvutia ambalo linamdhihirishia mwanadamu utukufu na ustadi wa Mwenyezi Mungu, wakati kwa upande wa wajinga ulimwengu ni jukwaa la kutumia na tamaa.



#### 4.KUUTAZAMA ULIMWENGU KWA MOYO SAFI

Kutokana na kuwa msafi pamoja na rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu na ziada ya mafunzo ya kiroho ya tasawwuf, moyo hufikia mahali mwenye nao huwa kama malaika licha ya kuendelea kuwa na sifa za kibinadamu. Baadhi ya watu wenye sifa hizi hawajifahamu wenyewe wala hawafahamiki kwa watu kuwa wana sifa hizo, kama ambavyo nyota miongoni mwa mamilioni ya nyota nyingine imejifisha kwenye uoni wa mwanadamu licha ya kuzagaa kwenye ulimwengu mzima. Watu wa namna hiyo ni vigumu kuwatambua.

Baada ya kuyasema hayo ni kwamba kutokana na majukumu ya kijamii waliyopewa watu hao baadhi yao huweza kutambulika kwa kiwango fulani. Hivyo wanakuwa kama nuru zenye kuongoza, watu ambao hawapuuzii maisha yao ya kawaida licha ya kuegemea kwenye akhera, nuru yao huendelea kuongoza hata pindi wanapokuwa hawapo hapa duni-ani kimwili, haya yanatokana na kupewa siri ya milele. Wanatambua uwezo wa Mola uliojificha katika msururu wa matukio ya asili. Hivyo wanaishi katika mazingira ya amani na utulivu kutokana na kupewa hekima na kulindwa dhidi ya kasoro zinazowasumbua wanadamu kama vile pupa ya mambo na wasiwasi.

Kwao kila kitu kina maana. Kutokana na kutembea juu ya njia ya kiroho iliyopambwa na kanuni isemayo, 'wavumilie viumbe kwa ajili ya Muumba', huanza kuutazama ulimwengu kwa jicho la hekima na kujifunza kwa upendo na shauku.

Hutazama jua lenye kuchomoza na rangi zenye kuvutia zinazochorwa na miale ya jua wakati wa kuzama kwa mtazamo wa hofu. Pia humuangalia hata nyoka kwa mtazamo huu; hivyo nafasi ya hofu inayopatikana mara tu baada ya kumtazama nyoka anayetambaa inachukuliwa na pumbazo





la mabaka yake yenye kuvutia na mvuto wa kasi yake na urahisi wake wa kutembea licha ya kutokuwa na miguu.

Kwa kuwa wanawatazama viumbe wengine kwa busara na upendo wanakuwa salama hata dhidi ya mashambulio ya wanyama mwitu; kwani kwa hakika upendo ni kama nguvu inayowafanya wengine washindwe kuleta upinzani.

Hawapo kama wanadamu wengine wanaotazama maajabu ya dunia kama jambo la kawaida. Mtu wa kawaida ambaye huvutiwa na michoro ya kibinadamu, michoro ambayo mara nyingi inatokana na kuiga vitu vya asili, hawezi kuhisi hivi pindi anapoutazama ulimwengu na kumuangalia Muumba wake. Vitu ambavyo vilitakiwa kumletea hofu kwake ni vitu vya kawaida.

Kwa upande mwingine watu wema ambao nyoyo zao zimetakaswa hawana kawaida ya kusifu michoro iliyotengenezwa na wasanii wenye shauku ya kupata umaarufu, bali wanapeleka sifa zao kwa sanaa ya kweli na Mtengenezaji wake. Wanafurahia kuona sanaa takatifu iliyopo katika vitu mbalimbali vya asili. Wanatazama maua yenye rangi mbalimbali na majani ya mimea, mvuto katika tofauti za rangi, harufu na maumbile katika kila mti, ladha ya kipekee katika kila tunda, ingawa vyote vinachipukia kutoka katika udongo wa aina moja, na pia wanatazama na kuvutiwa na muundo wa ajabu wa mabawa ya kipepeo na kisha wanatambua wazi upekee wa maumbile ya mwanadamu. Wanasikiliza kwa makini maneno ya kustaajabisha yanayotokana na lugha isiyosikika (*lisan'ul-hal*) ya maajabu matukufu mengi kama vile uoni na uelewa, vitu vinavyoonekana na wengi kama vitu vya kawaida.

Kwa watu kama hao ulimwengu mzima ni kama kitabu ambacho kinangojea kusomwa. Baada ya kupata elimu iliyoandikwa wanageukia elimu ya moyoni; kama ambavyo Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - ambaye kama mwanachuoni alimaliza kusoma vitabu vyake na kugeukia kwenye madrasa ya Saljuk, mahala ambapo alivutiwa na kumpenda mno daruwesh aliyeitwa Shams. Baada ya kuzaliwa tena kwenye anga ya upendo ni Mawlana yule yule ambaye alishusha thamani ya vitabu vilivyoandikwa na watu mara tu alipoanza kusoma ruwaza ya kustaajabisha ya ulimwengu kwa macho yake ya moyo. Ni baada ya hatua hii ndipo ikaja kazi bora ya *Mathnawi*, kazi ambayo ni kilio chenye kuweka wazi maajabu ya Qur'an, ulimwengu na mwanadamu.





Kuingiza moyoni hali hii kutawezekana kama muumini atagundua nguvu muhimu na upendo uliopo ndani ya moyo wake.

Kutokana na kuwa vitovu vya uoni mtakatifu nyoyo za aina hiyo huweza kufuzu. Labda kwa kuwa kuna nguvu ya kibinadamu inayohusika katika kukupelekea kufikia hapo ndio maana Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akaelezea thamani ya moyo huu uliotakasika kwa kusema:

*Al – Kaaba ilinyanyuliwa na Khalil Ibrahim ambaye ni mtoto wa Azer,*

*Lakini moyo ndiyo sehemu linapotazama jicho la Mwenyezi Mungu Mtukufu...*

Mara kwa mara ndani ya kazi za historia za watakatifu (*manaqib*) utona kuna mfananisho kati ya moyo na *Al- kaaba*. Hili linatokana na mfano wao wa wazi: Moyo kwa mwanadamu unachukua nafasi ile ile ambayo inachukuliwa na *Al- kaaba* ndani ya ulimwengu. Vyote vinachukua nafasi moja muhimu kutokana na kuwa uelekeo wa jicho takatifu. Ndipo sehemu ambapo jicho takatifu linazingatia zaidi. Mtindo wa historia hizi ambazo hujaribu kuupa moyo utukufu zaidi ya *Al- kaaba* unatokana na namna fulani ya kuonyesha mapenzi juu yake. Lakini cha muhimu zaidi ni kwamba haya yote yana lengo la kuwashawishi watu waupandishe moyo ili ufikie kwenye daraja unalostahili, mahala ambapo utakuwa unatazamwa kwa umakini zaidi kama ilivyo *Al- Kaaba*.

Katika suala la moyo kuwa kitovu cha mtazamo mtakatifu maneno ya Ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliyoyasema wakati anaiangalia *Al- Kaaba* yanaweza kutoa mwangaza katika hili:

“Utukufu ulioje uliokuwa nao ewe *Al- Kaaba!* Utukufu ulioje wa jina lako! Lakini utukufu alionao muumini wa kweli mbele ya Mwenyezi Mungu ni mkubwa zaidi!” (Tirmidhi, Birr, 85).

Moyo ni ua la imani. Ukweli kwamba moyo wa muumini aliyekomaa ni bora kuliko hata *Al- Kaaba* umewekwa wazi na Ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Katika kuthibitisha jambo hili Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amesema:

*“Kama unafikiria yajayo basi izunguke Al- Kaaba ambayo ni moyo! Moyo ndio uliobeba maana ya kweli ya Al- Kaaba ambayo unadhania imetengenezwa kwa udongo peke yake.*





*Mola amewalazimisha kuizunguka Al- Kaaba ili muweze kuwa na moyo uliotakaswa dhidi ya masiwa, yani Al- Kaaba ya moyo iliyotakasika.*

*Fahamu kwamba kama utauvunja moyo ambao ndio kitovu cha uelekeo wa jicho takatifu basi hata malipo ya kutembelea Al- Kaaba kwa miguu hayataweza kufidia dhambi uliyovuna”.*

Sharti la kukuwezesha kuwa na moyo wa namna hiyo limetolewa na Abdulqadir Jilani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake: “Moyo pekee wa yule mwenye kutafuta *marifatullah* na moyo ambao umetakaswa dhidi ya *masiwa* ndio unaoweza kuwa *Al- Kaaba*”

Ismail Hakki Bursawi anatoa maneno kama haya: “Yeyote atakayetafuta njia ya kuingia kwenye moyo ni bora kuliko yule atakayetafuta njia ya kuingilia kwenye *Al- Kaaba*. Ndio maana ni jambo la kawaida kuwaomba watu wema na watakatifu, ‘tuweke ndani ya moyo wako’ na kuomba utambuzi wa kiroho (*istimdad-i fayz*) na umakini (*talab-i himma*).”<sup>25</sup>

Imam Rabbani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anaelezea ukweli kwamba mwanadamu ni ulimwengu mdogo kwa namna ifuatayo: “Mwanadamu ni mukhtasari wa ulimwengu uliobanwa kwa pamoja. Chochote kinachopatikana kwenye ulimwengu, yeye ana sehemu yake ndogo.”

Kama ambavyo kumekwishatajwa katika maeneo mbalimbali mpaka sasa, tutaona kwamba mwanadamu ana pande mbili, yani yuko wazi kuchukuliwa na wema na uovu. Lengo la maamrishi ya dini na nyongeza ya mafunzo yaliyoshauriwa na tasawwuf ni kwa ajili ya kumfanya mwanadamu ajiepushe na uovu kadiri iwezekanavyo. Ili kufanikisha jambo hili ni jukumu la kila kiungo ndani ya mwili kushikilia kamba ya maamrishi matakatifu. Baada ya kuyasema hayo ni kwamba maamrishi na mafunzo ambayo hayana budi kuingizwa moyoni yana umuhimu mkubwa kutokana na kuwa kitovu cha hisia, moyo hutoa muongozo wa kutafakari na hivyo kuweza kuendesha nguvu za nafsi. Kinachomaanishwa hapa ni kwamba kitu cha kwanza katika kusababisha mambo yote yanayofanywa na mwanadamu ni moyo. Mara nyingi hisia huingia ndani ya moyo na kuota mizizi na hivyo kuufanya moyo uwe nguvu yenye kujitegemea inayoenda kinyume na nafsi. Hivyo si peke yake muhimu kuingiza moyo kwenye utekelezaji wa maamrishi matakatifu bali pia vigumu. Ushahidi wa kuto-



25. *Istimdad-i fayz* ni kuwa na utambuzi wa kiroho. *Talab-i himma* ni kutafuta kusikilizwa na mwalimu wa kisufi.



sha ni yale tuliyokwisha kuyasema hapo kabla katika kuzungumzia ugumu wa kutibu nyoyo zenye maradhi. Hata hivyo kwa kuwa thamani ya kila matokeo inalingana na ugumu unaopatikana katika kuyapata basi kuusimamia moyo kuna thamani kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Na hivyo katika ugumu huu kunapatikana sababu iliyopelekea Mola kuwabariki wale waliofuzu katika kazi hii ngumu, na kuwajaalia sifa za kimalaika na wakati mwingine hata zaidi yake.

Sufi wote wamechukulia kitendo cha kuvunja moyo kama dhambi kubwa mno kutokana na nafasi yake kubwa katika kumhakikishia mwanadamu furaha na uongofu. Suala hili limetahadharishwa na Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitikase siri yake – kama ifuatavyo:

“Moyo wenye kuhuzunika sana ambao mnaupa thamani ya chini kuliko kipande cha bua ni bora kuliko kiti cha Enzi...vile vile Ubao na Kalamu! Msiudharau moyo hata kama unastahili dharau! Hata ukiwa unastahili dharau lakini bado ni mbora kuliko vitu vyote vingine. Moyo uliovunjika ndipo mahala ambapo anapatazama Mola. Utukufu ulioje kwa yule anayeutengeneza! Kuunga moyo uliovunjika na kuwa vipande mia mbili ni bora mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko amali njema nyingi! Nyamaza! Hata kama kila unywele ungelikuwa na ndimi mia mbili lakini moyo ungelibakia kuwa wenye kustaajabisha!”

Moyo umefanywa kuwa sehemu ya kudhihirisha utukufu wa Mola na kuwa ua lenye kufunika utukufu huo, haya yote ni kutokana na sehemu yake tukufu ndani ya mwili wa mwanadamu. Kwa hakika kama ambavyo tumekwishataja mahala pengine ni kwamba kuikubali imani kunahitaji ‘kukiri kwa moyo’. Katika suala la ufunuo mtakatifu Qur’an haizingatii peke yake akili ambayo ndiyo kitovu cha tafakuri bali moyo ambao ndio kitovu cha hisia za kiroho:

نَزَلَ بِهِ الرُّوحُ الْأَمِينُ عَلَى قَلْبِكَ لِتَكُونَ مِنَ الْمُنذِرِينَ

بِلِسَانٍ عَرَبِيٍّ مُبِينٍ

“Ameuteremsha Roho muaminifu, Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji, Kwa ulimi wa Kiarabu ulio wazi.” (as-Shuara, 193-195).

Kama ilivyo kwa upande wa shughuli nyingine, kusonga mbele katika





mafunzo ya kiroho kunawezekana kwa kupitia kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee, kutokana na kumuongezea ari kwa msaada wake, rehema na huruma zake. Ingawa juhudi zote za mwanadamu na amali zake njema zinatoa msingi wa kiroho ambao utasaidia kusonga mbele lakini zote hizo si chochote bali ni sababu za kupata rehema za Mwenyezi Mungu na msaada wake. Kwa hiyo yeyote aliyeingia kwenye njia hii kimsingi hana budi kutegemea huruma na rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwani 'msaada' huo ndio utakaomvusha mwanadamu kutoka sehemu aliyopo mpaka sehemu nyingine bora zaidi, kwa namna yoyote ile mafanikio ni lazima yapatikane. Hata hivyo mtu hana budi kufanya jitihada anayoitara-jia Mola kutokana na rehema aliyomjaalia.

Kuna msembo wa kale usemao: 'Mtu asiache kabisa kile ambacho hawezi kukipata chote' (مَالًا يَدْرُكُ كَلِمَةً لَا يَدْرُكُ كَلِمَةً). Pia hili ni jambo linalosisitizwa kulizingatia katika mafunzo ya kiroho; mtu hapaswi kupuuzia angalau kile kidogo kilichopo ndani ya uwezo wake.

Pia katika *tasawwuf* kuna kisa kifuatacho kinachojulikana na wengi. Kijana mmoja aliyekuwa akitamani kuwa mwanafunzi anamuuliza Sheikh, 'Himma baba' na Sheikh naye anajibu, 'Ghayra (onyesha jitihada) mw-nangu!' Mtu anayetarajia kufikiriwa na mwalimu wake kiroho hana budi kuwa tayari kufanya jitihada. Anachokitarajia Mola kutoka kwa mja katika mafunzo ya kiroho ni kwa yeye kutambua udhalili na udhaifu alionao mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kufanya jitihada za makusudi ili kuifahamu siri iliyoelezewa na kanuni isemayo, 'Yeyote anayejitambua yeye mwenyewe basi atamtambua Mola wake'. Barabara ya kuelekea kwe-nye kuishinda nafsi inahitaji jitihada kutoka kwa mja wakati mafanikio yanatoka kwa Mola. Na bila shaka Mola atamuwajibisha mja kulingana na neema alizomjaalia katika maisha. Cha muhimu ni kwa mja kushikamana na haki kulingana na neema alizojaaliwa.

Mola...Washa cheche za haki katika nyoyo zetu ili tuweze kushika fun-guo za siri na hekima za hapa duniani na kesho akhera; na usizidumishe nyoyo na macho yetu ili tuweze kutukuka kwa *Jamal* yako hapo kesho akhera!

Amin...





**U**komavu wa kiroho utawezekana pale tutakapoachana na tabia chafu na kujipamba na tabia njema kwa kuzingatia umuhimu na utukufu wa moyo.



### C. KANUNI ZA MSINGI ZA MAFUNZO YA KISUFI

Katika tasawwuf kuna kanuni kadhaa zilizotajwa na sufi mkubwa aitwae Abdulkhaliq Gujdawani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Ni muhimu kushikamana na kanuni hizi pamoja na kufuata njia ya Naqsh-bandi, vyote hivi vinalenga katika kumuokoa mtu kutoka kwenye tabia chafu na kumfanya kuwa mwanadamu aliyekomaa kiimani. Kanuni hizi zinaweza kuorodheshwa kama ifuatavyo:

1. *Hush dar Dam*: Kujitambua kiroho katika kila pumzi uivutayo.
2. *Nazar bar Qadam*: Kuwa makini.
3. *Safar dar Watan*: Kuiendea haki katika kila hatua upigayo.
4. *Halwat dar Anjuman*: Kusimamia haki hata pale unapokuwa na watu.
5. *Yad-Kard*: Wakati wote moyo kuwa katika hali ya *dhikr* juu ya Mwenyezi Mungu.
6. *Baz-Gasht*: Malengo na tamaa yako iwe ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu pekee.
7. *Nigah-Dasht*: Kujilinda dhidi ya hisia za kishetani na za kiovu.
8. *Yad-Dasht*: Kujiona upo mbele ya Mwenyezi Mungu wakati wote.
9. *Wuquf-i Zamani*: Kuzingatia nafsi yako na kuutumia muda wa sasa kwa manufaa.
10. *Wuquf-i Adadi*: Kuzingatia kiwango cha *dhikr*.
11. *Wuquf-i Qalbi*: Moyo kugubikwa na *dhikr* na kuongezeka imani wakati unafanya *dhikr*.





Kuna faida katika kuelezea kwa ufupi maana ya kanuni hizi:

1. *Hush dar Dam*: Hii inagusia hali ya kuwa macho kiroho katika kila pumzi ivutwayo. Kanuni hii imefafanuliwa na Mawlana Sadaddin Kashgari - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kama ifuatavyo: “Chukulia kuan-gukia kwenye upuuzi hata katikati ya pumzi mbili kuwa kunakutoa mbele ya Mola wako”.

Kuwa macho katika kila pumzi uivutayo kutawezekana pale *dhakir*, yani mtu anayefanya *dhikr*, atakapokuwa akimtambua Mwenyezi Mungu Mtukufu pindi anapokuwa akifanya *dhikr* na wakati mwingine wowote. Kuilinda pumzi dhidi ya upuuzi kunapelekea moyo kuwa na amani. Ili kufanya fikra juu ya Mola ziwe kichwani mwako katika kila pumzi unay-ovuta na kutoa kunategemeana na kuihuisha pumzi yako kwa kupitia rehema itokanayo na kumtii Mola wako. Kutokana na moyo kufikia hali ya utambuzi na amani kutokana na kuwa karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi mwenendo na tabia nyingine zote zitaanza kuboreka kidogo kidogo.

2. *Nazar bar Qadam*: Hii inamaanisha kutembea huku macho yako yakiwa yameelekea kwenye ncha za vidole vya miguu. Mja hana budi kujipamba na namna hii ya utembeaji ili macho yake na moyo wake visije vikawa vinazunguka ovyo na hivyo kushindwa kuona lengo lao halisi. Kupendelea masiwa bila ya ulazima wowote kutapelekea kuondoka kwa amani ya moyo na kushusha pazia kati ya mja na Mola.

Mwenendo huu si mwingine bali ni namna alivyokuwa akitembea Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Pindi alipokuwa akitembea kamwe hakuwa akiangalia pembeni impaka imlazimu kufanya hivyo. Huku macho yake yakiwa yameelekea kwenye vidole vyake vya miguu alikuwa akitembea upesi kwa adabu kana kwamba alikuwa aki-shuka kwenye mteremko. Ndio maana kanuni hii imejumuisha miongoni mwa tabia za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

Pale ambapo macho yameelekea ndipo na moyo nao unapoelekea, huu ndio ukweli. Filamu zilizotengenezwa kwa msaada wa macho kwa mfano kwa kutumia kamera ya video mara nyingi huuteka moyo. Huchukua nafa-si isiyo ya lazima katika hifadhi za moyo. Kwa hiyo kuulinda moyo dhidi ya upotofu na mkanganyiko kunategemeana na ubora wa picha zinazoakisiwa ndani yake.







Pindi moyo wa mja unapozama ndani ya *masiwa* (vitu vya kidunia) basi miito ya upotovu huanza kuingia kichwani. Kama atakuwa karibu na wajinga basi tabia zao mbaya na mawazo yao mabaya huanza kuingia moyoni mwake na kumfanya kuwa katika hali ya hatari.

Ili kuwa na mwenendo na tabia zinazoendana na mtu mwema mja anapotembea asiyaelekeze macho yake kwenye ncha za vidole vyake vya miguu pekee bali pia hana budi kuwa makini juu ya vitu vingine anavyo- viangalia. Kuyaelekeza macho vidoleni wakati wa kutembea ni udhihirisho wa staha, kujitambua, kuyalinda macho dhidi ya *haram* na cha muhimu zaidi ni kutii *Sunnah* ya kipenzi chetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

3. *Safar dar Watan*: Licha ya safari iliyo na lengo la kumtafuta *murshid-i kamil* (mwalimu mkomavu), pia inamaanisha safari iliyochukuliwa na mja ili kuachana na tabia mbaya na kujiondoshea mzigo wa madhambi na badala yake kujipamba na tabia njema na hisia tukufu, hii ni safari ya kuelekea kwenye utambulisho wake halisi, yani nyumbani kwake. Mja asichukulia kuwa hali aliyofikia kuwa inatosha bali hana budi kuendelea kujiimarisha. Kwa ufupi hana budi kuwa katika safari wakati wote, safari ya kutoka kwenye hali moja ya kiroho na kuelekea kwenye hali nyingine ya juu zaidi.

Abu Othman al-Maghribi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amesema:

“Mja hana budi kuachana na tamaa na matamano ya nafsi yake na badala yake kumtii na kumuabudu Mola. Maneno *safar dar Watan* haya- maanishi safari kutoka mji mmoja kwenda mwingine bali ni safari ya kiroho ya kuelekea kwenye kukutana na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Pindi mja anapompata *murshid-i kamil* huachana na safari ya nje na kuianza safari ya ndani”.

Hivyo wakati wa *sayr-u suluk* (mafunzo ya kiroho) mja hutawaliwa na shauku ya kuwa karibu na Mola katika kila hatua, sawa na Ibrahim (a.s) pale aliposema “Nakwenda kwa Mola wangu Mlezi” (as-Saffat, 99).

4. *Halwat dar Anjuman*: Kujiona upo pamoja na Muumba hata pindi unapokuwa pamoja na viumbe wengine. Mja hana budi kuwa na hisia ya ndani ya kuwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu hata pale anapokuwa





pamoja na watu wengine au anapokuwa katika shughuli zake za kila siku. Jambo hili litamfanya aweze kuendelea kumpenda Mola wake bila ya kuwaonyesha wengine na hivyo kumfanya atafute mahitaji yaliyo ya lazima kwa maisha yake. Msemo ufuatao unatoa picha halisi ya hali hii ya akili, “Mikono inajitahidi kutafuta kipato lakini moyo uko kwa Kipenzi chake”.

Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu Mtukufu anawasifu wale wanaoweza kubakia na hali tukufu kama ifuatavyo:

رَجَالٌ لَا تُلْهِهِمْ تِجَارَةٌ وَلَا بَيْعٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ  
وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخَافُونَ يَوْمًا تَتَقَلَّبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَبْصَارُ

“Watu ambao biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kumdhukuru Mwenyezi Mungu, na kushika Sala, na kutoa Zaka. Wanaikhofu Siku ambayo nyoyo na macho yatageuka.” (an-Nur, 37).

*Sohbah* (somo la kiroho) na ujamii ni vitu vya msingi katika njia ya Naqshbandi. Hivyo kuufanya moyo ubakie katika hali ya ukaribu na upweke na Mola hata pale unapokuwa na watu kumepewa kipaumbele ukilinganisha na pale unapokuwa peke yako.

5. *Yad-Kard*: Hii ni kwa ajili ya kuufanya moyo kuwa na desturi ya kupenda *dhikr* na kuzama ndani yake; yani moyo ufikie mahala ambapo utakuwa katika hali ya kumkumbuka Mola wakati wote. Kwa kutumia njia ya *nafy-u isbat* (kukana na kuthibitisha kwa kurudia rudia *dhikr* ya *La ilaha ill-Mwenyezi Mungu*), mabaki yote machafu ya *masiwa* (vitu vya kidunia) ambayo yanafanya kazi kama masanamu ndani ya moyo husafishwa, matokeo yake suala la kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee ndiye marejeo linakuwa limegandia kwenye moyo.

Pindi joto la *dhikr* linalotoka kwenye moyo linaposambaa kwenye mwili mzima hisia tukufu zilizojificha ndani ya mwanadamu huja juu na kuchukua nafasi ya kusaidia kubadili tabia ya mtu. Ni jambo lisiloweze-kana kwa mtu ambaye fikra zake zote ziko kwa Mola wake akakosa neema za takatifu kama vile huruma, subira, ukarimu na kusamehe. Yote haya ni masharti ya kumfanya mtu kuwa mwanadamu aliyekomaa kiimani. Kwa hiyo kuufufua moyo kwa kupitia *dhikr* ni moja ya kanuni muhimu mno za *tasawwuf*.





6. *Baz-Gasht*: Hii inahusiana na kuyafanya malengo na tamaa yako kuwa ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu.

Baada ya kumaliza *dhikr* ya *nafy-u isbat* mja husema « إلهي أنتَ مَقْصُودِي وَرِضَاكَ مَطْلُوبِي » (Mola...Makusidio yangu ni Wewe na radhi zako ndiyo tamaa yangu) na kujitahidi kuzama zaidi kwenye tafakuri ya *dhikr*. Hii inalenga kumfanya mja atambue maana ya ndani ya *dhikr* ya *nafy-u isbat* na kumpelekea kukita *tawhid* (Upweke wa Mwenyezi Mungu) ndani ya moyo wake.

Moyo hutosheka baada ya kuweka pembeni matamania na tamaa zote ambazo huwa kama pazia lenye kumtenganisha mja na Mola wake. Vile vile wasiwasi ambao unaweza kutokea mara kwa mara na kuulaghai moyo kwa kuuonyesha kuwa utapata *karama* (miujiza) au utapanda daraja za kiroho kutokana na *dhikr* unazozifanya huweza kuepukwa na kuingizwa moyoni malengo halisi ambayo ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu.

Pindi maana halisi ya *dhikr* inapokuwa imezima ndani ya utambuzi wa mtu na kujidhihirisha katika tabia zake, basi mtu anakuwa huru dhidi ya hisia nyingine mbaya na macho yake huanza kupata mazingatio kwa kila yanachokiona.

7. *Nigah-Dasht*: Hii inahusiana na kuilinda akili dhidi ya hisia za uovu na matamania ya nafsi, kuyachunga macho yasitazame vitu vibaya, kuzilinda hisia zisihisi vitu viovu na kuuchunga moyo wakati wote ili kuulinda dhidi ya shambulio la *masiwa*.

Moja ya malengo ya *tasawwuf* ni kuulinda moyo dhidi ya fikra mbaya na hisia za uovu. Kujiepusha na vyote hivi si jambo rahisi. Lakini atakayefanikiwa kufanya hivyo atakuwa amevuna manufaa halisi ya *tasawwuf*.

8. *Yad-Dasht*: Hii inahusiana na wakati wote kutambua kuwa upo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na hivyo kufanya mambo yako kwa kulizingatia hili. Pia kanuni hii inaitwa *muraqabah*.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo katika aya: “Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake” (Qaf, 16).

Hivyo ni jambo la msingi kutojitenga na hisia za ihsan, Kuingiza





imani moyoni na kutambua kuwa Mola anamuona mtu katika kila hatua apigayo na anajua kila anachokifikiria. Hisia hizi zinakuwa kama ngao yenye kukulinda dhidi ya madhambi; kwani mtu atawezaje kufanya dhambi wakati moyo wake uko na Mola wakati wote na anatambua kuwa kamwe hawezi kuondolewa mbele yake?

9. *Wuquf-i Zamani*: Hii inahusiana na kuchunguza muda wako ulio-kupita na kuangalia kama uliutumia katika hali ya kiroho (*hudur*) au upuuzi (*ghafla*), na hivyo kuutumia vizuri muda wako. Mja hana budi kutambua thamani kubwa ya huu wakati alionao na hivyo kuuhifadhi kwa kutekeleza amali njema, hasa kwa kujiweka mbali na mambo ya kipuuzi. Mara kwa mara ajichunguze mwenyewe ili kuona ikiwa ameutumia muda wake vizuri au ameupoteza bila manufaa yoyote.

Kwa mtazamo mwingine wa kimaana kanuni ya *wuquf-i zamani* inahusiana na mja kuwa katika hali ya tahadhari juu ya fikra zinazomjia akilini mwake mara kwa mara na kuona ikiwa ziko katika hali ya kushukuru au zinamshawishi kutubu. Baada ya hayo mja hana budi kutafakari juu ya matendo yake usiku na mchana, moja baada ya jingine, na kisha kumshukuru Mola kwa kumjaalia kutekeleza matendo mema, na baada ya hapo kujitahidi kupiga hatua zaidi mbele na kutubia makosa yake na kuomba ulinzi wa Mola huku ukijutia juu ya makosa yaliyopita. Hana budi kufahamu kuwa kila hatua katika maisha yake ni yenye thamani, hasa zile nyakati zilizoteuliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni zenye thamani zaidi. Na kutokana na utambuzi wa kiroho hana budi kutumia nguvu zake zote kwa ajili ya kutosheleza matakwa ya muda husika na hivyo kuuhuisha.

Kwa ufupi mja hana budi kuzingatia kila wakati unaopita na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kila wakati aliotumia kwa manufaa ya kiroho na kutubia kwa ule alioutumia katika upuuzi. Vile vile mja hana budi kushikamana na toba pindi anapokuwa anapitia kwenye mbinyo wa kiroho (*qabd*) na kuendelea kushukuru pindi anapokuwa anapokea uhuishaji wa kiroho (*bast*). Hivyo yule mwenye kujiweka mbali na upuuzi katika mambo yake yote hujikuta ni mtu asiyeyumbishwa na mitihani na matatizo yaliyokwishapita na wasiwasi juu ya mambo yajayo, na hivyo kushughulishwa na jitihada za kuhuisha wakati ulio mbele yake, jambo ambalo limetajwa katika kanuni ya kisufi isemayo, “Sufi ni mtoto wa wakati uliopo”.





10. *Wuquf- I Adadi*: Hii inahusiana na kufahamu kiwango halisi cha *dhikr*. *Murshid* humpa mwanafunzi wake kiwango Fulani cha *dhikr* kulingana na hali yake ya kiroho.<sup>26</sup> Ili kufanya itoe matokeo yanayokusudiwa kila *dhikr* huja na kiwango maalumu, tunaweza kusema dozi maalum. Ili mwanafunzi asije akapoteza umakini wakati wa *dhikr* na kuweza kuingia kwenye mitego ya shetani hana budi kuzingatia kiwango halisi cha *dhikr* kilichopendekezwa na *murshid*. Hata hivyo ubora wa *dhikr* una umuhimu mkubwa mno. Kama *dhikr* haitakuwa na kiwango na kiasi maalum basi wakati wote kutakuwa na hatari ya kukosa utulivu kiakili na kiroho. Kama ilivyo kwa shughuli nyingine ukosaji huu wa utulivu husababishwa na kasoro zinazopatikana kutokana na kuzidisha na kutozingatia kiasi kilichowekwa. Kwa hiyo *dhikr* haina budi kutekeleza kwa namna iliyo bora zaidi kwa kuzingatia kiasi na ubora. Baada ya kuyasema hayo ni kwamba isieleweke kuwa kufanya *dhikr* kwa kiwango maalum si sawa na kuhesabu namba za kawaida. Lakini kinyume chake ni kwamba hauna budi kuizamisha *dhikr* ndani ya moyo kwa kuzingatia idadi maalum. Hivyo ni wazi kwamba kufanya *dhikr* kwa kuzingatia kiwango maalum si tu kunapelekea kupata ubora unaokusudiwa bali cha zaidi ni kwamba jambo hili ni chachu ya kukuwezesha kumaliza *dhikr* yenyewe.

Jambo la kustaajabisha ni kwamba pindi akili inapokuwa imezungukwa na fikra nyingi na moyo unapokuwa umeshughulishwa na mambo mengi hupelekea kukaribia kutowezekana kufanya *dhikr* kwa kuzingatia kiwango chake maalum. Hivyo ni jambo la msingi kuilinda akili dhidi ya mkanganyiko na kuweka umakini wote katika maana ya *dhikr* na wakati huo huo kuzingatia kiwango chake maalum.

11. *Wuquf-i Qalbi*: Hii inahusiana na moyo kuwa katika hali ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wote. Hii inadhihirisha uingizaji wa *ihsan* ndani ya moyo, yani wakati wote kuwa macho juu ya matendo yako. Mwanafunzi hana budi kuuchunguza moyo wake kila wakati na kuangalia kama upo katika hali gani, kwani lengo la *dhikr* ni kuufanya moyo utambue kile kinachotamkwa na ulimi. Jambo la msingi wakati wa kufanya *dhikr* ni kuwa katika hali ya *muraqabah*, yani hali ya kuzingatia maneno unayoyatamka. Sufi wakubwa wanachukulia *wuquf - I qalb*, yani

26. Kuhusiana na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kupendekeza viwango mbalimbali vya *dhikr* kwa watu sambamba na mazingira na hali zao rejea uk. 196-197.





kufanya jambo kwa moyo wako wote, kama sharti la lazima katika *dhikr*. Ili kuweza kufikia kwenye malengo y a kweli ya *dhikr* ni jambo lazima kuelekeza kila kiungo chako hasa moyo kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

وَ اذْكُرْ اسْمَ رَبِّكَ وَ تَبَتَّلْ اِلَيْهِ تَبْتِيلاً

“Na lidhukuru jina la Mola wako Mlezi, na ujitolee kwake kwa ukamilifu”(al-Muzzammil, 8).





**W**atu wema ambao wamezitakasa nafsi zao ndio wenye kustahili uhai na utaratibu katika nyoyo zao.



## D. MURSHID-IKAMIL NA NJIA ZA KUONGOKA KIROHO

### 1. MURSHID-IKAMIL

Pindi muumini anaposonga mbele katika njia ya kiroho hukutana na ubainifu wa mambo mengi. Moyo kama bahari. Wakati mwingine maji yake hutulia; lakini wakati mwingine maji yake hupanda na kufikia kwenye vimo vyenye kutisha kutokana na kukumbwa na dhoruba za ghafla. Katika mawimbi haya anahitajika nahodha mahiri ili kuweza kuipitisha salama meli yake. Pindi nahodha atakaposhindwa kuingoza meli yake wakati akijaribu kuipitisha meli katika mawimbi haya makubwa atakuja kugundua ugumu uliopo pindi unapokuwa baharini; kwani meli yake itaweza kuzamishwa mpaka kwenye vina vya bahari na kupotea kabisa. Huwa ubainifu huu haujitokezi kwa wale walio wageni katika safari hii. Lakini pindi mtu anapoendelea kupiga makasia kwenye bahari ya wazi ataanza kudhihirikiwa na baadhi ya dalili za kiroho, mabadiliko ya kiroho yenye kutofautiana kati ya mtu mmoja na mwingine, huwa na hali kama *inqibad* na *inbisat*,<sup>27</sup> hali ambazo vyanzo vyake havifahamiki ikiwa vinatokana na Mwenyezi Mungu (*Rahmani*) au Shetani. Hivyo ili kuzichanganua na kuchukua tahadhari inayostahiki kunahitajika usimamizi wa *murshid-i kamil*, yani mwalimu aliyekomaa kiimani.

Ili kufikia kwenye uelekeo huu kila muislamu hana budi kujichunga mwenyewe. Hatuna budi kuiga mwenendo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kadiri ya uwezo wetu, kwani Mtume ndiye kiigizo cha umma huu kisicho na mfano. Uaminifu wake na kum-

27. *Inqibad* na *inbisat* ni hali mbili tofauti ambazo humsibu mwanafunzi. *Inqibad* ni mbano wa kiroho utokanao na hofu au wasiwasi, wakati *inbisat* ni nafuu ya kiroho itokanayo na matumaini.



tegemea kwake Mola, subira yake pindi alipokabiliwa na matatizo, kujiweka kwake mbali na hazina za dunia zilizokuwa zikimiminika mbele yake na staha yake isiyo na kifani, vyote hivi havina budi kufanyiwa kazi kadiri iwezekanavyo. Ili kuweza kuvuka vikwazo vilivyo katika njia maendeleo ya kiroho mja hana budi kutafuta msaada wa *murshid-i kamil* wenye busara kwa unyenyekevu na heshima, kwani hawa ndio warithi wa Mtume aliyebarikiwa – rehemana na amani ziwe juu yake, na baada ya hapo mja hana budi kujitahidi kufuata mapendekezo yao kwa moyo safi. Kama ambavyo mwezi unavyothibitisha uwepo wa jua kutokana na kupokea mwanga wake hata pale jua linapokuwa halionekani na macho yetu ndivyo ambavyo watu wema ambao wameangaziwa na nuru ya Muhammad – rehemana na amani ziwe juu yake – wanavyokuwa mashahidi na warithi wa Mtume aliyebarikiwa – rehemana na amani ziwe juu yake.

Lengo la *tasawwuf* ni kuendeleza uwezo wa kiroho ulio ndani ya silka ya mwanadamu. Kila moyo ni kama ardhi iliyo na petroli chini yake. Kamwe petroli haiwezi kujitokeza juu ya ardhi mpaka litobolewe tundu. Petroli iliyotulia ndani ya ardhi ni kama uwezo wa kiroho aliopewa kila mwanadamu. Kama ulivyo uwezo wa kiakili, uwezo huu nao unapatikana kwa wanadamu katika viwango mbalimbali.

*Murshid-i kamil* ndiye mwenye kuweza kutoboa na kuutoa uwezo huu mpaka juu ya ardhi na kuifanya hazina hii ipigwa na mwanga wa jua. Lakini ili petroli iweze kutoka nje ya ardhi keeke itakayotumika kutobolea haina budi kufika mpaka kwenye tabaka ambalo ndipo petroli ilipo. Keekee lazima liwe imara na lenye kuweza kujirudisha katika umbile lake la mwanzo, kinyume chake litaweza kugonga mwamba na kukatika vipande vipande. Hii inamaanisha kwamba *murshid* ambaye ana jukumu la kumungoza mtu hana budi kuwa mahiri katika jukumu hilo.

*Murshid-i kamil* wa kweli huweza kutambulika kwa sifa kuu tatu:

*Sifa ya kwanza:*

*Murshid-i kamil* wa kweli huzitii kikamilifu Qur'an na *Sunnah*. Huwa maisha yake na vitendo vyake havitawaliwi na chochote zaidi ya kuhuisha maadili ya Qur'an na *Sunnah*. Utii wa *murshid-i kamil* juu ya Qur'an na *Sunnah* ni mkubwa mno ukilinganisha na waumini wengine. Kushikamana kwake na nguzo hizi mbili kunalingana na mtu ambaye anamfuata mwongoza njia kwa umakini mkubwa mno katika eneo lenye theluji nzito,







mtu huyu yuko makini katika kuhakikisha kuwa anakanyaga pale pale ali-popakanyaga mwongoza njia licha ya kukwama kwama katika theluji ile. Hivyo *murshid-i kamil* anaweza kuitwa *warathatu'l-anbiya*, yani mrithi wa Mitume. Hivyo hatuna budi kusema kwamba utii wa kiwango hicho hautoi nafasi kwa maisha ambayo yametawaliwa na nafsi.

*Sifa ya pili:*

*Murshid-i kamil* wa kweli humkumbusha juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika maneno yake na vitendo vyake. Kwani viigizo hivi vyema hupokea ubainifu wa majina matakatifu na huwa na uwezo wa kuchukua uzuri (*jamali*) wa majina haya matakatifu na kuubadilisha na kuwa tabia zao njema, hivyo mara kwa mara kuwakumbusha watu juu ya Mola wao. Kwa hakika pindi maswahaba walipomuomba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – awafahamishe ni nani *wali* au waja watakatifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, alitoa jibu lifuatalo:

الَّذِينَ إِذَا رُئُوا ذُكِرَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ

“Hao ni wale ambao mtazamo wao humkumbusha mtu juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu” (Haythami, *Majmau'z-Zawaid*, X, 78; Ibn Majah, *Zuhd*, 4).

Pindi umuonapo *murshid-i kamil* huna budi kupata fikra juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na akhera, pia upate utulivu ndani ya moyo na kuingizwa kwenye ulimwengu wa kiimani. Hili halitokani na sababu nyingine bali ni kutokana na kushikamana na maadili kutoka kwa Mola na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

Miongoni mwa majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu yenye kutukuzwa zaidi ni *Rahman* (Mwingi wa rehema) na *Rahim* (Mwenye kurehemu). Pia waja wema wa Mola huwa na huruma ya hali ya juu. Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *Sattaru'l-uyub*; Yani ni mwenye kusitiri madhambi ya watu. Pia *murshid* huwa hachunguzi makosa ya watu wengine na huwa anayaficha pale anapobainikiwa nayo. Mola ni *Karim*, mwingi wa ukarimu. Pia mtu mwema naye huwa ni mkarimu; huridhika pale anapotoa na kuwapa wengine. Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *Ghafur*; Mwingi wa kusamehe. Pia *murshid* naye ni huwasamehe wengine. Mola ni *Halim*, yani mwingi wa kustahamili; pia watu wema nao ni wastahamilifu.





Kutokana na kuwa maswahaba (*wali*) wa Mola, watu hao hutofautiana na watu wengine kwa namna nyingi. Huwa nyoyo zao ziko karibu na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Matendo yao ya ibada hufanywa kwa umakini mkubwa. Huwa makini mno katika tabia zao. Kwa kuwa wanafuata vyema nyayo za Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake, hivyo maombi yao hukubaliwa zaidi ya maombi ya watu wengine. Kwa kuwa miili yao inajishughulisha na *dhikr* wakati wote hivyo huacha athari katika sehemu wanazokuwepo.

Muumini wa kweli hujikuta ni mwenye wasiwasi pindi anapochanganya mzigo wake wa masuala ya kiroho pamoja na mtu mwingine mwenye tabia ya uovu. Kinyume chake kuwa karibu na watu wema pekee huweza kumletea mtu amani. Kikubwa zaidi katika faida ya kuwa karibu na Mtume aliyebarikiwa -rehema na amani ziwe juu yake – ni kupata furaha isiyo na kifani. Raha ya kiroho ya kuwa katika mazingira yaliyobarikiwa na utukufu wa nuru ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – ni jambo lisiloweza kuelezewa kwa urahisi. Lakini pia kwa kuwa *murshid-i kamil* anafuata vilivyo nyayo za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kushikamana na *Sunnah* zake na hivyo kumpelekea kukaribia mwenendo wa kiutume, basi atakuwa amebeba utukufu wa kiroho na pia atakuwa ni sababu ya msukumo kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kama ilivyo kawaida kwa mtu aliyepigwa shoti kutetemeka, pia *murshid* wa kweli hana budi kwanza kutetemeshwa na nguzo za imani kisha ndio apate nguvu ya kuweza kusonga mbele kwenye safari ya kiroho.

*Sifa ya tatu:*

Alama ya mwisho ya *murshid-i kamil* ni uteuzi wa kiroho. Haitoshi kwa baraza la watu kukaa na kumchagua *murshid*. Bali anatakiwa kuteuliwa na *murshid-i kamil* mwenye mamlaka ya kufanya hivyo, mtu huyu ni yule mwenye mfuatano sahihi mpaka kumfikia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kama mnyororo huu utafikia mahali na kushindwa kuendelea mpaka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – basi mtu huyo atakuwa amepungukiwa vigezo. Pindi atakapokosekana mtu mwenye vigezo vinavyohitajika basi *murshid-i kamil* wengi hujizuia kumchagua mtu mwingine yeyote ambaye ataendeleza njia yao. Wakati mwingine humuacha mrithi mmoja na wakati mwingine wengi, kama ilivyokuwa kwa Khalid Baghdadi - Mwenyezi Mungu aita-





kase siri yake. Hekima iliyopo katika jambo hili anaijua Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake.

Kwa ufupi ni kwamba kuukomaza moyo ili uweze kupokea uhalisia wa kiroho kutawezekana kwa kupitia mafunzo kadhaa ya kiroho. Kwa upande mwingine ili kuweza kuvishinda vikwazo vilivyotapakaa kwenye njia hii kunahitajika usimamizi wa watu wema na waja watakatifu mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kila mwanafunzi wa kweli hana budi kumtafuta *murshid* kwa ajili ya kusimamia maendeleo yake ya kiroho lakini wakati huo huo hana budi kumtazama kwa umakini kuona ikiwa kweli *murshid* huyo ana sifa zinazohitajika.

Maneno machache na muhimu ya kuzingatia:

Kwa kuwa *murshid-i kamil* ambaye sifa zake zinakidhi sifa zilizokwishatajwa ni mja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu wa kipekee, na ni mtu mwenye maadili ya kipekee, basi mwanafunzi wake hana budi kumuonyesha heshima ya hali ya juu na kuathiriwa na tabia zake. Lakini pindi mja akiwa anamuonyesha *murshid* huyu heshima inayostahili na kutafuta kufaidika na tabia zake, lakini hana budi kuwa makini asije akaingia kwenye janga la kuvuka mipaka. Hatuna budi kufahamu kuwa achalia mbali watu wema na watakatifu, bali hata Mitume walikuwa juu ya waja wote wa Mwenyezi Mungu. Huwa wanakuwa na kiasi fulani cha bahari ya elimu ambayo wamejaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kuna wakati macho yao yanakuwa yamedhirikiwa na hekima za hapa duniani na kesho akhera; na vile vile kuwa wakati ambao hawawezi kuona hata kile kitu kilicho mbele yao.

Sheikh Sadi katika *Gulistan* yake anasimulia:

“Siku moja mtu mmoja alimuuliza Yaqub (a.s), ‘Wewe ambaye ni Mtume mwenye busara na mwenye moyo ulioongoka! Ilikuwaje uliweza kuhisi harufu ya shati la Yusuf (a.s) ambalo lilikuwa likiletwa kwako kutoka sehemu ya mbali karibia na Misri, lakini bado ukashindwa kumuona Yusuf (a.s) pale alipokuwa akitumbukizwa ndani ya kisima kilichokuwa karibu na wewe?’

‘Sehemu ya ujuzi tuliojaaliwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu’ Yaqub (a.s) alijibu, ‘ni kama mipigo ya radi. Hivyo kuna wakati ukweli unajidhirisha bayana na wakati mwingine unakuwa umefichwa’”.





Siku moja Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipotakiwa kumjibu mtu aliyemuuliza maswali kadhaa na akawa hayajui majibu yake lakini akawa ana uhakika kuwa ufunuo mtakatifu ungelishuka muda si mrefu, alisema:

“Nione kesho ili nikupe majibu ya maswali yako”. Hakufuatishia maneno yake kwa *insha-Mwenyezi Mungu* au Mwenyezi Mungu akipenda.

Ufunuo aliokuwa akiutarijia haukushushwa siku iliyofuata; ukweli ni kwamba zilipita siku kumi na tano kabla ya ufunuo huo kumfikia. Hata nuru yetu – rehema na amani ziwe juu yake - ambaye kwa ajili yake ulimwengu mzima uliumbwa aliachwa bila ya msaada. Pindi ufunuo ulipowasili baada ya kuchelewa sana ulikuja na tahadhari ifuatayo:

“Wala usisema kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho. Isipo kuwa Mwenyezi Mungu akipenda. Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unapo sahou, na sema: Asaa Mola wangu Mlezi ataniongoa kwenye uwongozi ulio karibu zaidi kuliko huu” (al-Kahf, 23-24) (Angalia Ibn Kathir, III, 83; Alusi, XV, 247).

Kwa kuzingatia kuwa hili ndilo sharti ambalo hata Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliagizwa kulitekeleza, hivyo kila mtu hana budi kuelewa vilivyo kiwango cha matumizi yake kwa wanadamu wote. Hivyo hatuwezi kusema kwamba pindi kipenzi cha Mwenyezi Mungu Mtukufu atakapomba dua au kumuomba mtu mwenye maradhi basi ni hakika maombi yake yatajibiwa kama anavyotarajia. Ili maombi yaweze kufikia kile kilichokusudiwa si tu kunahitajika usafi wa nyoyo katika pande zote mbili, yani yule anayeomba na yule anayeombewa, bali pia ni lazima maombi yale yakutane na qudra ya Mwenyezi Mungu. Inafahamika kuwa maombi yote yanakubaliwa lakini ni jambo la msingi kukumbuka kuwa kukubaliwa kwa maombi kunaweza kuahirishwa mpaka kesho akhera badala ya kubainishiwa katika maisha ya hapa duniani na kwamba kukubalika na kutokubalika kwake kunategemeana na moja kwa moja na qudra ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Jambo jingine la kuzingatia ni kwamba wote Mitume na watakatifu huwa wana sifa na silka tofauti na kwamba sifa inayoweza kubainika kwa Mtume mmoja inaweza isipatikane kwa Mtume mwingine kwa kiwango kile kile. Hivyo itakuwa ni makosa kutarajia kuwa kila mmoja kati yao ana sifa na silka za aina moja.





Kama ambavyo imetajwa ndani ya Qur'an kuwa Musa (a.s) alipewa elimu ambayo Khidhir (a.s) hakuwa nayo; na kinyume chake ni kwamba Khidhir (a.s) alijaaliwa elimu ambayo Musa (a.s) hakuwa nayo. Vile vile mtu hawezi kutarajia Jilani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kuwa sawa na Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Walichopewa wote wawili na kinachotarajiwa kutoka kwa wote wawili ni tofauti. Lakini hata hivyo kwa hakika ni kwamba walichonacho wote wawili ni utumishi mbele ya Mwenyezi Mungu na *marifah*. Na kwa hakika njia zenye kutuwezesha kufika kwa Mola wetu ni nyingi kama kiasi cha pumzi walizonazo viumbe.

Pia ni muhimu kufahamu kuwa hakuna mja yeyote achilia mbali Mitume ambaye ana uhakika mia kwa mia kuwa atajibiwa maombi yake. Hata kama mja alikuwa anakaribia kufikia kwenye kilele cha utumishi, lakini bado anakuwa katika tishio la kuteleza. Mfano katika suala hili ni Balam ibn Baura. Mwanzoni alikuwa ni mtu mwena, lakini baadae akatekwa na nafsi yake na kujisababishia maangamizi. Qur'an inamzungumzia mtu huyu kama ifuatavyo:

“Na wasomee khabari za yule ambaye tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na Shet'ani akamuandama, akawa miongoni walio potea. Na tungelitaka tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari.” (al-Araf, 175-176).

Vile vile ilimtokea Qarun au tajiri mkubwa, mtu ambaye kisa chake kimesimuliwa katika surat al - Qasas. Mtu ambaye alikuwa mwema na mwenye msimamo katika dini aligeuka na kuwa mtu mwenye uasi mkubwa mno. Mwenyezi Mungu alimzamisha ndani ya ardhi yeye pamoja na mali zake alizokuwa akijitamba nazo. Hivyo pamoja na cheo cha kiimani au utukufu aliojaaliwa mtu hana budi kutambua kuwa nafsi imetulia ndani yake na inangojea kumshambulia wakati wowote na kumtoa kwenye kiti chake cha enzi. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – hakuomba ulinzi wa Mola bila sababu ya msingi pale alipoomba:

“Ewe Mwenyezi Mungu...Ninatarajia rehema zako! Usiniache peke yangu na matamano ya nafsi yangu hata kama ni kwa sekunde! Nirekebishie kila hali yangu! Bila shaka hakuna Mola ila Wewe...” (Abu Dawud, Adab, 100-101).





Waja wema wa Mwenyezi Mungu wakati wote huchukua tahadhari juu ya maana ya *hadith* hiyo na kamwe hawajidanganyi kwa kuwa na fikra kuwa ‘tayari wameshafanikiwa.’ Wale walioingia kwenye fikra hizi zenye kudanganya wakati wote wamejikuta wanaachwa watupu hata kama walifanikiwa kukamilisha *sayr - u suluk* yao. Kinyume chake wale walio- amini kuwa bado wana safari ndefu ili wafikie mafanikio na hivyo wakawa wanajikumbusha juu ya makosa yao na udhaifu wao, waliweza kusonga mbele katika njia ya kiroho. Hatuna budi kufahamu kuwa licha ya ubainifu wa wazi wa ubora aliokuwa nao Mtume Muhammad Mustafa – rehemana na amani ziwe juu yake – ambaye ndiye kinara wa Mitume lakini kamwe hakuacha kutekeleza swala kiasi kwamba miguu yake ilikuwa ikivimba, alipoulizwa na Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - kutokana na kustaajibishwa kwake na jambo lile, alisema:

“Je nisiwe ni mja mwenye kushukuru ewe Aisha?” (Muslim, Munafiqun, 79).

Pia kutokana na masimulizi kutoka kwa wake zake watukufu, baada ya ufunuo: “Zitakase sifa za Mola wako Mlezi, na umwombe msamaha; hakika Yeye ndiye anaye pokea toba” (an-Nasr, 3) Mtume aliyebanikiwa – rehemana na amani ziwe juu yake – alianza kujishughulisha na kumshukuru na kumtukuza Mola katika kila sekunde iliyopita.

Kwa hiyo licha ya cheo anachokuwa nacho mtu katika njia ya imani, kamwe hatolewi katika kutekeleza majukumu ya utumishi na kwa vyovyote iwavyo hatakiwi kupunguza amali zake wala kujiona kuwa yeye hahusiki tena katika majukumu yanayotokana na yeye kuwa mja wa Mwenyezi Mungu. Kanuni zote tukufu na majukumu wamepewa wanadamu katika aina zote za maisha na hayatatolewa kwao mpaka pale watakapovuta pumzi zao za mwisho. Hivyo *murshid-i kamil* wa kweli hujitahidi katika maisha yake yote kuishi kwa kushikamana na amri ya muongozo isemayo:

“Basi mtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanao msujudia. Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini” (al-Hijr, 98 – 99).

Viongozi wa kiroho wa namna hii huwa hawaombi kitu hata kidogo kama fidia ya huduma zao. Pia hawatarajii hata fidia ya utumishi wao kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu; kwani wanaofanya hivyo thamani ya matendo yao na vyeo vyao vya kiroho hushuka baada ya muda. Licha ya Ali na Fatma – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – kufunga kwa siku





tatu mfulululizo lakini walitoa chakula chao na kumpa masikini aliyewag-  
ongea mlango wao kutokana na njaa katika usiku wa kwanza, pia walimpa  
yatima katika usiku wa pili na kumpa mfungwa katika usiku wa tatu, na  
wao wakafutura kwa maji peke yake. Na baada ya kuwapatia watu hao  
chakula alikuwa akiwaambia maneno yafuatayo pindi walipowashukuru:

“Hatakukupeni chakula chetu kwa kutarajia shukurani kutoka kwenu.  
Jambo pekee lililotusukuma kufanya hivyo ni kutafuta radhi za Mola  
wetu...”<sup>28</sup>

Kwa kifupi ni kwamba *murshid*-i kamil wa kweli ni vinara vya maisha  
ya kiroho, vinara ambao wanaendeleza majukumu ya Mitume ya kufunza  
na kufundisha kutokana na kuonyesha mfano wa kuigwa katika jamii.  
Kutokana na kuwa kwao karibu na Mola na sifa zake tukufu waja hawa  
wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati huo huo wanakuwa wame-  
fikia kwenye daraja la *ihsan*. Huwa wanakuwa wamepewa elimu kama  
vile elimu ya *ladunn*, hekima na *marifa*. Lakini mpaka hapo hakuna mtu  
anayewafikia maswahaba. Pia maswahaba hawako katika daraja moja na  
Mitume na Mitume nao hawako katika daraja moja na Mtume aliyebariki-  
wa – rehema na amani ziwe juu yake. Na kwa upande Mtume aliyebarikiwa  
– rehema na amani ziwe juu yake, yeye ni mja wa kwanza na mtukufu zaidi  
katika ya waja wa Mwenyezi Mungu na baada ya hapo ni Mjumbe Wake.

Hivyo kila mtu hana budi kujizuia na kuwapa wanadamu thamani  
kubwa kupita kiasi na hivyo tunachotakiwa ni kuishi na watu kulingana na  
hali zao. Uways al-Qarani au hata Abu Hanifa ambaye alikuwa mkusanyaji  
wa hukumu za kiislamu hawawezi kuwa katika daraja moja na maswa-  
haba. Heshima na unyenyekevu uliovuka mipaka ambao mara kwa mara  
unaelekezwa kwa watu wema kutoka watu walio wajinga ni nje ya kosa  
la kawaida; bali ni kupotea kuliko wazi kabisa. Kupotea huku ni tabia ya  
uvukaji wa mipaka usio wa kawaida, jambo ambalo linaweza kumpelekea  
mtu kuwa mbali na Mola wake na pia kuwa mbali na ukweli. Kutokana na  
kuhofia watu wasije wakaangukia kwenye kosa hili ndio maana Mtume  
aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwakataza watu wasi-  
imbe mashairi yenye kuwatukuza watu wengine kwa ujinga. Na pale mtu  
aliyesifiwa alipohofia kuwa sifa zile zingeliweza kuipa nguvu nafsi, Mtume  
aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alimshauri:

28 Rejea al-Insan, 8-11; Wahidi, uk. 470. Zamakhshari, VI, 191-192.





“Apige uso wake (uso wa aliyesifiwa) kwa vumbi!” (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, VI, 5).

Sifa zenye kuichochea nafsi si chochote bali ni saina ya maangamizi kwenye moyo.







**U**wepo wetu hapa ulimwenguni umeshikiliwa na upendo na rabitah; kwani rabitah si kingine bali ubainifu wa upendo ambao ndio wenye kubeba kiini cha uwepo wetu hapa ulimwenguni. Rabitah ni udumishaji wa uchangamfu na cheche za upendo.



## 2. NJIA ZA MWONGOZO WA KIROHO

### a. *Mahabbah* (Upendo) na *Rabitah*

Pindi utakapoangalia ari na malengo ya usufi utagundua kuwa kichocheo cha kwanza katika *sayr-u suluk* ni upendo, wakati lengo lake kubwa ni maadili ya kiroho (*adab*). Hapa upendo ni sababu wakati maadili ya kiroho ni matokeo. Hakuna mtu anayeweza kuelezea kwa ukamilifu umuhimu wa vipengele hivi viwili; pindi upendo juu ya mtu unapozidi basi sehemu fulani ya upendo huo huvienea vitu vinavyomzunguka, vitu hivi huonekana vimefanana au vimekaribia kufanana kwa namna fulani na mtu anayependwa .

Kwa mfano mwanafunzi ambaye ana mapenzi makubwa juu ya *murshid* wake hawezi kujizuia na hisia za kuonyesha mapenzi hayo kwa yeyote atakayekuwa na tabia sawa na zile za *murshid* wake, ijapokuwa hayatakuwa sawa kabisa na yale ya *murshid* wake. Pindi anapokutana na *murshid* wake huwa kama mtu aliyempokea ndugu yake aliyetoka kuhiji. Mapenzi yake huongezeka pale anapomiliki kitu ambacho alikuwa akikitumia *murshid* wake. Tunaweza kuyalinganisha mapenzi haya na furaha aliyokuwa nayo Uways al-Qarani pindi alipopokea joho kutoka kwa Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake.

Pamoja na uongezeakaji wa upendo lakini wakati huo huo ukaribu (*nisbah*) juu ya kipenzi ambao unaongezeka taratibu huwa ni jambo pana zaidi, kiasi kwamba unaanzia kwa kipenzi, ukaribu unaongezeka zaidi, unafikia katika kiini na baada ya hapo unasambaa na kuwajumuisha watu wengine. Katika *tasawwuf* kusambaa na kuvuka duara hili la mapenzi na kumuweka kipenzi katikati ya duara hilo kwa namna ambayo itawaenea





wote walio karibu na mbali kunaitwa mapenzi kamili (*ashk-i mutlaq*).<sup>29</sup> Tujikumbushe maneno ya Yunus Emre,

*Vithamini viumbe kwa ajili ya Muumba.*

Hii ni hali ya kuvipenda na kuvihurumia viumbe vyote bila ya kujali sifa zao, tabia zao na matendo yao, kuvipenda huku ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Muumba. Hii ndiyo hatua ya mwisho ambayo mpenzi anaweza kuifikia. Na baada ya hapo kila kituo cha mapenzi njiani ni mapenzi ya sitiari (*ashk-i majazi*).

Mapenzi ya sitiari huanza pale mwanafunzi anapoamua kumpenda *murshid* wake. Mapenzi haya pia ni ya sitiari. Kwa kuwa kiasili moyo upo kwa ajili ya mapenzi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu pekee hivyo hauwezi kuwa na kipenzi kingine tofauti na Mwenyezi Mungu. Vitu vingine ambavyo anashikamana navyo ni kama ngazi yenye kumsaidia mja kufikia mapenzi matakatifu. Kwa ujumla hii ni njia ya kuweza kumfikia *Mawla* au Mola kwa kupitia *Layla*. Katika suala hili hatua yenye kuvutia zaidi ni kukutana na *murshid-i kamil* wa kweli na kupitia kwenye raha ya mapenzi ya kiroho pamoja naye. Na ubainifu wa hili wenye mafanikio zaidi ni *rabitah*. *Rabitah* ni ukuzaji wa mapenzi ambao hauwezi kulinganishwa na vitu vingine vya kawaida.

Kiuhalisia *rabitah* inamaanisha kitu unachoshikamana nacho na ulicho na shauku nacho. Kwa maana hiyo hakuna kiumbe hata mmoja hapa ulimwenguni ambaye yuko nje ya *rabitah*. Kila kitu kipo katika muunganiko na vitu vingine. Katika hatua nyingine *rabitah* ni ubainifu wa mapenzi ambayo yanazalisha kiini cha uwepo wetu hapa ulimwenguni. Pia *rabitah* ni ni udumishaji wa uchangamfu na cheche za upendo.

Kuna aina tatu za *rabitah*:

### 1. *Rabitah* ya asili

Huu ni upendo wa asili anaokuwa nao mtu kwa wale walio karibu naye. Haya ni matokeo ya silka ya mtu, kama mapenzi anayohisi mama kwa mwanae na kadhalika.

29. Qur'an tukufu inasisitiza juu ya hitajio la kumpenda Mwenyezi Mungu Mtukufu zaidi ya kitu chochote kile: *وَالَّذِينَ آمَنُوا أَشَدُّ حُبًّا لِلَّهِ*: "...Lakini walioamini wanampenda Mwenyezi Mungu zaidi sana" (al-Baqara, 165). kiwango hiki cha juu cha mapenzi katika lugha ya kila siku kinaitwa 'mapenzi matakatifu'.





## 2. *Rabitah* mbaya

Hii inahusiana na tabia ya kushikamana na mambo ya haramu na mabaya; kama ambavyo mpiga ramli moyo wake una tamaa ya kupiga ramli kiasi kwamba inafikia mahali anasahau kuhusu mahitaji ya nyumbani kwake.

## 3. *Rabitah* tukufu

Kutokana na hisia nzuri zinapelekea *rabitah* hii kumshawishi mtu kuelekea kwenye vitu ambavyo vitamfikisha kwa Mola. Hii inahusiana na kuwa karibu kimwili au kiroho na wale ambao nyoyo zao zimepamba (*tajliyah*) na ambao wamefikia kwenye cheo cha *mushahadah*, haya yote ni ili anufaike nao kiroho.

Hapa tutaelezea zaidi juu ya aina hii ya tatu ya *rabitah*. Hii inaashiria namna ambayo baada ya mwanafunzi kupata uwezo fulani anavyoweza kutunza mapenzi ya *murshid* wake ndani ya moyo wake kwa lengo la kunufaika naye kiroho.

Njia ya kisufi ya *rabitah* inapatikana katika majina mbalimbali na mafunzo mbalimbali katika kila *tariqah*. Kwa kawaida huwa jukumu la mwanafunzi kumuingiza akilini mwake *murshid* wake aliye mbele yake, na kutokana na hisia tukufu ajaribu kuwa kama yeye, hili litawezekana kwa kupitia kwenye kukumbuka hali ya akili yake na tabia yake kiimani. Pindi atakapotunza na kuhuisha mapenzi na heshima ya *murshid* wake kwa namna hii kutampelekea kuwa na uchangamfu wa kiroho.

Wakati wote mwanadamu anakabiliwa na vishawishi. Kama ilivyo kwa magonjwa yaliyo mengi pia hali za ndani za akili zinaweza kuambukizwa kwa mwingine. Uhamishaji wa tabia kutoka kwa mtu mmoja mpaka kwa mwingine katika maisha haya ni jambo lisiloweza kuzuilika. Hasa tabia za kiroho zilizo imara zinazoweza kuonekana kwa watu muhimu katika jamii huweza kusambaa kwa wengine kwa viwango tofauti tofauti. Usambaaji huu haujalishi ikiwa msambazaji ana tabia nzuri au mbaya. Hua unafanyika tu ikiwa kuna muunganiko wa pande mbili kimapenzi na ukaribu.

Kwa mfano misimamo ya watu wenye huruma na kujitolea huweza kusambaa na kuwafikia wale wanaowazunguka. *Rabitah* ambayo ni ubainifu wa upendo hujaribu kuongeza na kuharakisha uhamishaji huu wa tabia njema na kuifanya kuwa imara zaidi kwa mpokeaji. Hivyo kila muislamu





mwenye uelewa mzuri hana budi kuonyesha upendo kwa watu wema na kujenga nao ukaribu na hivyo kukuza uwezekano wa kuipata misimamo yao mizuri.

Inastajaabisha kuona pindi matope yatakaporukia kwenye nguo ya mtu inamfanya ajisikie vibaya sana kuliko pale tabia mbaya zinapouvamia moyo na kuuweka mbali na nuru ya *wahy* na hivyo kuuchafua kwa madhambi bila yeye kutambua. Kwa kuwa anakuwa amepigwa gazi na mivumo ya nafsi na ya Shetani anakuwa hatambui hatari inayoikabili imani yake. Mbele ya kitu tunachokiita ‘uhamishaji wa tabia’ ni kweli kuwa mwanadamu ameachwa huru kuchagua kati ya viigizo vizuri ama vibaya. Hata hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ametufahamisha chagua sahihi ndani ya Qur’an kama ifuatavyo:

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na kuweni pamoja na wakweli.” (at-Tawba, 119).

Kitu cha kuzingatia katika aya hii ni kwamba Mwenyezi Mungu hawaagizi waja wake ‘wawe wema’ bali ‘wawe pamoja na wema’ ili waweze kuulinda uchamungu wao. Kwa hakika hatua ya kwanza ya kuelekea kuwa mwema ni kuwa karibu na watu wema, kuwa nao karibu kwa upendo. Wema ni matokeo ya lazima katika muunganiko huu.

Ukitaka kuitawala nafsi kuwa karibu na watakatifu na watu wema, ukaribu huu utakuwa kama mwangaza wenye athari kubwa mno. Kuwa karibu na watu wema, kushuhudia mwenendo wao na matendo yao katika kila hatua na hata kushuhudia nyuso zao zenye kung’aa kunazingatiwa katika hili. Hii ndiyo sababu inayopelekea kuwa karibu na watu wakubwa katika imani kuchukuliwa kama baraka kubwa. Misimamo huwa inahama. Huwa ni jambo la kawaida kwa harufu ya waridi kupenya kwenye nguo zilizoanikwa karibu na bustani la mawaridi. Vile vile baraza la watu wema ni kama soko la kuchukulia imani.

Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Maneno ‘kuwa pamoja na’ katika amri ya Qur’an ya ‘kumuogopa Mwenyezi Mungu na kuwa pamoja na watu wema’ inamaanisha kudumisha kuwa pamoja nao. Kama ambavyo imetajwa wazi wazi ‘kuwa pamoja na’ kuna vipengele viwili, kimoja ni kivitendo na kingine ni kisheria. Kivitendo au kimwili inamaanisha kuwepo kimwili katika mkusanyiko wa





watu wema, wakati kisheria inamaanisha kuonyesha misimamo yao pindi wakiwa hawapo”.

Hivyo kama ilivyo muhimu kuwa na hisia njema pindi utakapokuwa mbele ya watu wema, lakini pia huna budi kuendeleza ukaribu huu ndani ya moyo pindi wanapokuwa hawapo. Si wakati wote inawezekana kuwa pamoja nao kimwili. Hivyo mtu anahitaji *rabitah* ili kuwa pamoja nao ndani ya moyo.

Lakini kama ambavyo tumekwishaona hapo awali huwa mafunzo ya *tasawwuf* yanatoa njia za kuwa pamoja na watu wema kimwili kwa namna iliyo bora zaidi. Kuna watu wengi ambao wapo karibu mno na *murshid* lakini bado hawawezi kuvuna hata sehemu ya imani yake kutokana na ujinga wao. Kinyume chake kuna watu ambao wapo mbali mno na *murshid* wao lakini wamebarikiwa kwa kuwa na misimamo, zawadi za kiroho na heshima kutokana na hisia za upendo, ukaribu na shauku juu ya *murshid* wao. Msemo wa wakubwa katika imani kuwa ‘yule aliye ndani ya Yemen yuko karibu wakati yule aliye karibu yupo Yemen’ unalidhihirisha hili. Kwa hiyo cha msingi ni kutopoteza hisia zao ndani ya moyo popote pale utakapokuwepo.

Kwa upende mwingine ingawa watu makini katika imani hujaribu kusahihisha misimamo ya watu wanaowazunguka lakini hili peke yake halitoshi. Uhamishaji wa msimamo katika *tasawwuf* ni suala la kiroho ambalo manufaa yake makubwa yanategemeana kiwango cha upendo alichonacho mtu juu ya *murshid* wake. Hivyo si kila mwanafunzi hupata msimamo sawa na mwingine kwa sababu tu yeye ni mwanafunzi. Kinyume chake ni kwamba utofauti katika viwango vya imani kati ya wanafunzi hutegemeana na viwango vya uwezo na upendo wa kila mmoja. Katika mfano tunaweza kusema kwamba mtu mwenye nia ya kuchota maji kwa ndoo atapata kiasi kile kile kinachoruhusiwa na ndoo ikiwa ataizamisha ndani ya ziwa au ndani ya bahari isiyo na mipaka. Hivyo mwanafunzi hana budi kutambua uwezo wake.

Yunus Emre analielezea jambo hili vizuri kama ifuatavyo:

*Kama utakiweka kikombe bombani kwa ajili ya kukijaza, hata kama utakiacha hapo kwa miaka elfu moja hakitaweza kujaa chenyewe.*

Njia nyingine iliyotumika katika vyote viwili *rabitah* na *muraqabah* ni





kusoma *silsila-i sharifah*<sup>30</sup>. Jambo hili hufanyika kwa lengo la kupokea seh-emu ya rehema ambazo zinatarajiwa kushuka kwenye moyo kutokana na kuyataja majina ya watu wema wanaotengeneza mlolongo huu na kuguswa na misimamo yao mizuri. Mwanachuoni mkubwa aitwae Sufyan ibn Uyay-nah amesema: “Rehema hushuka kwenye mkusanyiko ambao watu wema wanatajwa” (Ajluni, Kashful-Khafa, n, 70).

Utungaji wa vitabu mbalimbali vinavyoelezea historia za watu wema hauna sababu nyingine kinyume na kuwashawishi wale wanaowapenda wawataje kwa namna iliyoelezewa. Hivyo lengo la *rabitah* ni kuzishawishi na kuzivutia nyoyo kiimani kwa kuzifanya zikumbuke mlolongo mtukufu wa watu wema ambao mlolongo wao unaishia kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – mwenyewe. Baada ya kuufahamu mlolongo wa watu husika, huku ukiwa unatetemeka kutokana na waya wa umeme wenye moto ulio kwenye mkono wa mtu wa kwanza katika mlolongo huo, ni jambo la kawaida kwa mtu kuanza kutetemeka bila ya kuweza kujizuia kutokana na volteji za umeme unaomfikia. Kuikuza *rabi-tah* kiasi cha kumuwezesha mwanafunzi kushikamana na mwenendo wa kimaadili wa *murshid* kutokana na kuendeleza upendo na heshima juu ya *murshid* pindi anapokuwepo na hata pale anapokuwa hayupo kunaitwa *fana fi’s-sheikh*, yani kujiangamiza kwa sheikh.

Ukivuka kituo cha *fana fi’s-sheikh* utakutana na kituo cha *fana fi’r - rasul*, yani kujiangamiza kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Kabla ya kurehemewa kwa kupewa uislamu, maswahaba wengi watu-kufu ambao ndio nyota katika anga ya kiislamu walikuwa wakiishi maisha yaliyokuwa kinyume na silika ya asili. Lakini baada ya kupokea nuru ya uongofu na baada ya kufikiwa na hisia za kiroho za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ndani ya mienendo yao, wamekuwa watu wema zaidi kuliko wanadamu wote. Uongofu wa kiroho utokao kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - na kumfikia *murshid* unakuwa umepelekwa kwenye nyoyo za wanafunzi wake kwa kupitia *rabitah* na *sohbah*. Kwa njia hii mwenendo wa kuigwa wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – unakuwa umeingia kwenye tabia ya mwanafunzi kadiri unapoishia uwezo wake.



30. *Silsila-i Sharifah* ni neno linalomaanisha msururu wa *murshid* ambao unafika kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.



Katika hatua hii mja hujiweka kana kwamba yupo mbele ya Mtume aliyebarikiwa - rehema na amani ziwe juu yake - katika kila jambo analo-lifanya na hujitahidi kujipamba kwa mwenendo wake bora. Ili kuimarisha mshikamano wa kiroho uliopo kati ya mja na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – ni muhimu kuupamba kwa salat- u salam na kuzitekeleza *Sunnah* zake kwa mapenzi na hivyo kujenga upendo na ukaribu ndani ya moyo.

Pia hatuna budi kusema kwamba ndani ya Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – utaweza kukuta ubainifu wa wazi wa *fana fir-rasul*. Kutokana na kuridhika na msimamo wake wa kiroho ilifikia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kusema:

“Abu Bakr ni mimi, na mimi ni Abu Bakr. Abu Bakr ni ndugu yangu hapa duniani na kesho akhera” (Daylami, Musnad, 1, 437).

Kilichoelezewa katika *hadith* zilizopita bado hakijafikia kwenye raha yenyewe, kituo kinachopita raha hii ya moyo ni kituo cha *fana fillah*, yani kujiangamiza kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ili kuweza kugundua maa-jabu yaliyopo kwenye aya zifuatazo huna budi kufikia kwenye kituo cha *fana fillah*.

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ

“Naye yu pamoja nanyi popote mlipo” (al-Hadid, 4).

“...Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake.” (Qaf, 16)

Moyo wa *murshid* ambao tayari umeshajiangamiza kwa Mola huwa unakuwa ukiongoka kiroho kutokana na ubainifu wa Majina Matukufu. Hivyo moyo wa *murshid* huwa kama lenzi ambayo imekusanya miale ya mwanga katika sehemu moja. Baraka za ubainifu huu huunguza uovu wote na kubakisha majivu. Mwanafunzi hutafuta kunufaika na baraka hizi kwa kupitia *rabitah*. Hisia za nafsi na ubinafsi huondoka kwenye moyo na nafasi yake kuchukuliwa na msimamo wa kiroho wa mwenendo bora. Vitu vyote ambavyo vilikuwa vimeuvamia moyo vinaondolewa na kufungiwa kule vilipotoka.

Uhamishaji huu wa msimamo wa kiroho kutoka kwa *murshid* na kuelekea kwa *murid* unaashiria mafanikio katika kuelekea kwenye muungano.





“Mtu huwa pamoja na yule anayempenda”, *hadith* inatueleza.

Katika suala hili ni jambo la msingi kuwazungumzia watu wa pangoni, watu ambao kisa chao kimetajwa ndani ya Qur’an tukufu<sup>31</sup>. Kiwango cha utii kilichoonyesha na *Qitmir*, ambaye alikuwa mbwa wa wale watu wa pangoni, kutokana na kulilinda kwake kundi la watu wema na watakatifu kilikuwa ni cha hali ya juu. Matokeo yake naye pia ataingia peponi pamoja na watu wema na watakatifu.<sup>32</sup> Kwa kuzingatia kuwa hata mbwa anaweza kufikia hatua hiyo kutokana kuwa kwake pamoja na watu wema na watakatifu, basi mafanikio ya kiroho ambaye anaweza kuyapata muumini wa kweli pindi atakapokuwa karibu na watakatifu na watu wema ni jambo lisilopingika.

Tungelipenda kugusia kipengele kingine cha *rabitah*, kipengele chenye umuhimu mkubwa katika *tasawwuf*.

### ***Rabitah-i Mawt* (Kutafakari juu ya mauti)**

Katika *tasawwuf* kujenga mahusiano au *rabitah* na fikra ya mauti kunajulikana kama tafakuri juu ya mauti (*tafakkur-i mawt*). Kuyafikiria mauti kunaweza kuleta mabadiliko makubwa katika msimamo wa mtu na tabia yake. Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – anasema:

اَكْتَبُوا ذِكْرَ هَاذِمِ اللَّذَاتِ يَعْنِي الْمَوْتِ

“Mara kwa mara kikumbukeni kitu chenye kung’oa raha zote; kitu hicho ni mauti” (Tirmidhi, Zuhd, 4).

Kutafakari juu ya mauti bila shaka hupunguza matamano ya nafsi na mapenzi ya kuipenda dunia, mapenzi ambayo humpelekea mtu kupata shida hapo baadae. Kuvipenda kupita kiasi vitu vya dunia vyenye kupita, tamaa ya makuu, na kuvipata vitu vinavyoonekana ni vizuri na nafsi, ni mwanzo wa maradhi ya kiroho. Katika kuelekea kwenye kuulinda moyo ili usiathiriwe na ugonjwa huu, kulikumbuka kaburi na adhabu za kaburi



31. Rejea al-Kahf, aya ya 9 mpaka ya 26.

32. Kwa maelezo zaidi rejea Ismail Hakki Bursawi, *Ruhu'l-Bayan*, Toleo la 226.





ambazo tunaweza kukutana nazo muda si mrefu kutatupelekea kufanya toba na kufanya ibada zetu kwa umakini mkubwa na wakati huo huo kutulinda dhidi ya tamaa za dunia na matamano yasiyo na faida. *Dhikr* na *rabitah* tunazoendelea kuzitekeleza zitakuwa sababu ya uongofu wetu na furaha kesho akhera.

Imesimuliwa kuwa Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alimuachia mwanae Hasan - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – maneno yafuatayo ya ushauri:

“Mwanangu! Jitahidi kujikumbusha juu ya umauti na uuzoeshe moyo wako uendeleo kuukumbuka huo umauti. Usisahau kwamba vyovyote vile kitu kitakavyokuwa lakini mwishowe kitashushwa na kupoteza thamani na kubakia dhalili kabisa! Ukumbushe moyo wako juu ya hatari kubwa ya dunia!”

Kwa hakika kwa kuwa wakati hauendelei kupita bila ya kukatishwa, kama mstari ulionyooka, mtu anapaswa kutambua kuwa bila shaka nyakati za shida zinaweza kuja kupita kama zilivyo nyakati za raha.

Imam Ghazzali naye anatoa maneno ya ushauri kama hayo:

*“Mwanangu...ishi utakavyoishi lakini siku moja utakufa! Mpende yeyote utakayempenda lakini siku moja utatengana naye! Fanya chochote utakacho lakini siku moja utahesabiwa juu ya kitu hicho!”*

*Mwanangu...Lengo lako pekee linatakiwa liwe kuikomaza roho yako, kuichunga nafsi yako na kuuandaa mwili wako kwa ajili ya kifo; kwani kaburi ndilo litakalokuwa kituo chako cha mwisho. Watu waliopo maka-burini wanasubiria siku ambayo utaenda kuungana nao. Kamwe usifikirie kwenda kule bila ya kuandaa chakula chako kwa ajili ya hiyo safari!”*

Sehemu ya ushauri alioutoa Omar ibn Abdulaziz kwa waislamu katika hotuba yake ya mwisho ni kama ifuatavyo:

*“Enyi watu!”*

*Akhera yenye kupumua moto ni yenye kutisha. Hata Mitume na Malai-ka wenye kutambua Maajabu ya Jalali (Ghadhabu za Mwenyezi Mungu) hutetemeka mbele ya msukosuko wa siku ya kiama. Na ni nani atathubutu kuvumilia ghadhabu za Mwenyezi Mungu Mtukufu?*





*Bado usikate tamaa juu ya rehema za Mola zisizo na mipaka.*

*Lakini fahamu fika kwamba uongofu mbele ya hesabu kesho akhera ni wa wale wenye kumuogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu, wenye kujichunga na maasi na wenye kupendelea maisha ya milele kuliko maisha ya hapa duniani yenye kupita. Yule mwenye kwenda kinyume na havi anakuwa amejidanganya mwenyewe na anakuwa ameyatumia maisha yake kwa namna isiyu na faida na mwishoni ataambulia patupu.*

*Leo mmekuja kuchukua nafasi ya watu waliopita. Kwa hakika watakuja wengine kuchukua nafasi yenu!*

*Kama uonavyo, wale wanaokuja wanaondoka na wale wanaoondoka hawarudi tena. Ondokaji huu usio na hiari na utaratibu mzima wa maisha yetu upo chini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake.*

*Karibia kila siku mnawaaga wale wenye kuondoka miongoni mwenu na kuelekea akhera, mnabeba miili yao mabegani mwenu...Bado hampati funzo? Mnawaacha ndani ya tumbo la ardhi wakiwa peke yao bila vitanda wala mito. Wingi ulioje wa mafunzo yanayopatikana kutoka kwa maiti ambao tayari wameshaonja ladha ya mauti! Wameenda mahali ambapo hawapafahamu, wametenganishwa na vipenzi vyao, wameamshwa kutoka kwenye hii ndoto ya maisha yenye kupita...Sasa wanauona ukweli lakini hawana cha kufanya...Ndege ameondoka kwenye kiota chake pamoja na kila namna ya kulipa fidia...Hakuna kingine kinachobaki kwenye mikono yake isipokuwa amali zake njema. Katika siku hiyo dhambi zao zitajaa machoni mwao wakati wakisubiria hukumu kwa huzuni. Watakuwa na wasiwasi huku wakitetemeka kutokana na hofu juu ya siku hiyo ya kufufuliwa.”*

Mauti ni njia inayompelekea mtu kuamkia kwenye ulimwengu mwingine na kuuona ukweli kwa macho yake. Lakini kuamka wakati wa kifo hakuna faida kama utakuwa hujajiamsha mwenyewe kabla ya kifo kwa kurarua mapazia ya ujinga.

Tafakuri juu ya mauti ni kama ngao yenye kumlinda murid dhidi ya tamaa, kuiweka imani yake katika dunia na mambo mengine yote yanayosababishwa na nafsi. Kwa kuwa lengo kuu la tasawwuf ni kuitawala nafsi basi tafakuri juu ya mauti ndio njia pekee yenye kutumiwa na kada zote za kisufi.





## b. Mkusanyiko wa kiroho (Sohbah)

***Mikusanyiko ya sohbah na dhikr ni mabustani ya pepo kwenye ardhi, mabustani yaliyojaa rehema na utulivu kutoka Mwenyezi Mungu.***

Miongoni mwa njia muhimu zenye kutumiwa na *murshid-i kamil* wengi katika kuushawishi vyema moyo na roho ya *murid* ni mkusanyiko wa kiroho na hotuba au *sohbah*. Maneno ya mtu aliyeitakasa nafsi yake na moyo wake huwa yamejawa na hisia za msimamo wake imara. Maneno ambayo yatatolewa kwa kupitia hisia hizi hupata njia ya kupita mpaka ndani ya moyo wa msikilizaji na kuacha athari yenye manufaa.

*Ikhlas* au usafi wa moyo ndio kitu cha msingi chenye kufanya mazungumzo yawe ni yenye faida. Hotuba ya *murshid-i kamil* ambayo inalenga kumpelekea mlengwa hisia za kiroho huwa inakuwa imegemea kwenye *Sunnah* za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Ubora wa *ikhlas* unaoweza kuleta hisia hizi ni ule uliotokana na mtu kukiweka katika vitendo kile anachokifahamu na kutamani kwa moyo wake wote kwamba msikilizaji ayafanyie kazi yale yote anayomshauri.

Jambo jingine lenye kupelekea hotuba kuwa ni yenye kushawishi ni ufupi wa hotuba (*wajiz*). Ili uweze kufupisha hotuba inategemea uko mahiri kiasi gani katika lugha husika na uchaguzi wa maneno yaliyo bora zaidi. Upeo wa juu kabisa katika suala hili unapatikana katika Qur'an tukufu.

Katika kipindi ambacho Mtume alikuwa Makka binti wa Imru'l-Qays ambaye alikuwa mshairi mkubwa wa kiarabu bado alikuwa hai. Walimso-mea mshairi huyu surat al- Zilzal. Mwanamke yule aliyekuwa mzoefu wa lugha ya kushawishi na ufasaha alipigwa na butwaa.

“Maneno hayo hayawezi kuwa maneno ya mwanadamu. Hakuna mwanadamu mwenye uwezo wa kutoa maneno ya kiwango cha juu kiasi hicho. Si sawa kwa mashairi ya baba yangu kuendelea kwenye kuta za Al-Kaaba wakati kuna maneno kama haya hapa duniani. Tafadhali...nenda na ushushe yale mashairi!”

Vile vile *hadith* inatufahamisha:

إِنَّ مِنَ الْبَيَانِ سِحْرًا





“Kwa hakika kuna maajabu katika baadhi ya maneno” (Bukhari, Nikah, 47)  
Inamaanisha maneno yana namna fulani ya maajabu kwenye moyo.

Hivyo kutoa uongofu wa kiroho kwa kupitia hotuba kuna umuhimu mkubwa mno. Ili kutambua kiasi cha baraka alizoleta Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kupitia hotuba zake inatosha kutafakari juu ya sababu iliyopelekea kile kipindi ambacho hizo hotuba zilitolewa kiliitwa *Asr-u Saadah*, yani enzi ya furaha kamili, na si katika kipindi kingine chochote katika historia nzima ya mwanadamu. *Sunnah* za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – za *muakkad*, yani matendo ambayo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiyarudia mara kwa mara pamoja na *sohbah* vinachukua nafasi kubwa katika matawi yote ya kisufi, hasa katika Naqshbandi, vinatumika kama njia za kupitishia uongofu wa kiroho kutoka kwenye moyo mmoja kuelekea kwenye moyo mwingine.

Tukizungumzia ufupi wa hotuba mtu anaweza kujikumbusha maneno ya ushairi ya Yunus Emre, maneno ambayo yanabainisha nguvu ya maneno, ikiwa ni hasi au changa:

*Kwa neno vitu humalinzwa,  
Kwa neno mwingine hukatwa kichwa,  
Sahani yenye sumu hugeuzwa,  
na kuwa asali na siagi kwa neno.*

Nyoyo za maswahaba zilizokuwa zimeegemea kwenye dunia hapo mwanzoni zikawa zimefikwa na mafuriko ya furaha ya rehema kwa kupitia maneno ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Ni jambo la kushuru kwa kuwa mbegu zao za kipekee za wema na imani ambazo zilibakia katika usalama chini ya udongo ziliweza kusitawi. Usambazaji wa imani na upendo kutoka kwenye roho moja na kuelekea kwenye nyingine kuliwezesha kujitokeza kwa watu wenye tabia njema mno. Mtu aliyekuwa mjinga, aliyekuwa na moyo mgumu kiasi cha kuweza kumzika binti yake huku akiwa hai, mtu ambaye hakutambua haki zozote zile, aliweza kuyeyuka na kutoweka. Badala yake katika taswira ile ile akaibuka mtu aliyejawa machozi, mkarimu na mwenye imani thabiti.

Hatuna budi kufahamu kuwa neno *sahabah*, neno la kiarabu lenye kumaanisha swahaba, lina mzizi mmoja na neno *sohbah*. Hisia za hali ya juu za upendo na heshima walizokuwa nazo maswahaba juu ya Mtume ali-





yebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ziliwapelekea kuwa mifano bora ya kuigwa katika manufaa yanayotarijiwa kupatikana kutokana na maneno na mafunzo ya kiroho. Na bado hali yao ya kiroho na maadili waliyokuwa nayo mbele ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ilikuwa ni ya hali ya juu kiasi kwamba walikuwa wakiielezea kwa kusema:

“Ilikuwa ni kana kwamba kulikuwa na ndege aliyetua vichwani mwetu na sisi tukaogopa kutikisika hata kidogo ili asije akaruka na kukimbia zake”.<sup>33</sup>

Hivyo walibeba tabia na maadili ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – kila walipoenda. Walionyesha wema wa hali ya juu mno kiasi kwamba kumbukumbu yake haitofutika mpaka siku ya mwisho. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo kuwahusu wao:

“Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa” (at-Tawbah, 100).

Kila sohbah iliyofanywa kwa hisia za ibada ni sawa na sohbah nyingi za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake; kwani yeye ndio kitovu cha manufaa yote ya kiroho yanayopatikana kutokana na sohbah hizo. Kila sohbah ambayo imezama ndani ya raha ya kiroho ni mwangaza utokao kwenye kitovu hicho. Kwa hiyo hata kama mtu atapata sehemu ya nuru ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kupitia njia ya mja mwema wa Mola, kwa kuwa chanzo cha nuru hiyo ni kimoja na kitaendelea kuwa kimoja, basi mtu huyo atakuwa kana kwamba amepata nuru hiyo moja kwa moja kutoka kwenye chanzo chake; kama ambavyo mshumaa mmoja unavyounguza mishumaa mingine. Moto unaoiwasha mishumaa hiyo ni mmoja na ni ule ule. Hata ule mshumaa wa mwisho kuwashwa utakuwa na moto ule ule wa mwanzo ambao ndio chanzo chake.

Mikusanyiko ya *sohbah* na *dhikr* ni mabustani ya pepo kwenye ardhi, mabustani yaliyojaa rehema na utulivu kutoka Mwenyezi Mungu. Kuna *hadith* isemayo:

<sup>33</sup> Rejea Abu Dawud, *Sunnah*, 23-24.





“Pindi kundi la watu linapokutana kwa ajili ya kumkumbuka Mwenyezi Mungu, basi rehema za Mwenyezi Mungu zitawafunika, watahushiswa utulivu na Mwenyezi Mungu atawataja mbele ya malaika zake.” (Muslim, Dhikr, 38).

Watu wenye nyoyo safi na ambao ni wenye hekima na wema huwapatia mapenzi yao na furaha *sohbah* wao. Huwapatia nuru ya siri zilizopo nyoyoni mwao. Na matokeo ya utambuzi wa kiroho (*inikas*) na kupakaza (*insibagh*) hupelekea nyoyo kujawa na nuru ya ukweli kwa viwango tofauti tofauti kulingana na uwezo wao. Haya ni sawa na upepo mwanana wa asubuhi ambao unavuma na kupitia kwenye bustani lililopendezeshwa kwa mawaridi, karafuu na maua mengine yenye kuvutia, upepo huu hupeleka harufu yake nzuri kwa kila utakachokipitia.

Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

و ذَكَرْ فَإِنَّ الذِّكْرَ تَنْفَعُ الْمُؤْمِنِينَ

“Na kumbusha, kwani ukumbusho huwafaa Waumini” (ad-Dhariyat, 55).

Baada ya kuifafanua aya hiyo kwa namna iliyo nzuri kabisa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema: “Dini imebeba *nasihah*.” (Bukhari, iman, 42). *Nasihah* ina maana mbili. Maana ya kwanza ni kuwaalika watu kwenye kile kilicho kizuri, na ya pili ni usafi wa moyo.

*Abdullah ibn Rawahah - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - pindi alipokuwa akimuona swahaba mwenzake alikuwa akimwambia, “Njoo ndugu yangu. Hebu tukae kwa muda mfupi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na kuzijaza tena imani zetu juu yake”*

*Swahaba mmoja ambaye hakuelewa alichokuwa akikimaanisha alimfahamisha Mtume aliyebarikiwa - rehema na amani ziwe juu yake - juu ya maneno ya Ibn Rawaha - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake.*

*“Mwenyezi Mungu amrehemu Abdullah”, alimuomba. “Yeye anapenda mikusanyiko ya dhikr ambayo malaika wanaitukuza”<sup>34</sup>*

Pia katika kufahamu umuhimu wa *sohbah* tuangalie *hadith* ifuatayo:

34 Rejea Ahmed ibn Hanbal, Musnad, III, 265.





*Siku moja mwanamke mmoja alimuendea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na kulalamika, “Wakati wote wanaume ndio wenye kuvuna faida za maneno yako. Kwa nini labda usitenge siku moja kwa ajili yetu na sisi tukakusanyika kwa ajili ya kujifunza kutoka kwako kile ulichofundishwa na Mwenyezi Mungu?”*

*“Basi jikusanyeni sehemu fulani katika siku fulani”, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alisema. Kisha siku ile ilipofika maswahaba wa kike wakajikusanya katika ile sehemu na kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – akawafundisha. (Bukhari, ilm, 36).*

Maswahaba wale wa kike ambao kutokana na baraka za maneno ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – walikuwa mama wa kuigwa na umma mzima, walikuwa wakiwasema watoto wao pale walipopuuza kwenda kumuona Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwa muda mrefu. Mmoja miongoni mwa watoto hao alikuwa ni Hudayfah - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alisemwa na mama yake kutokana na kuacha kwenda kumtembelea Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa masiku kadhaa. Anasimulia tukio hili kama ifuatavyo:

“Mama yangu aliniuliza ni muda gani umepita tokea nimuone Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake. ‘Ni masiku kadhaa yamepita mpaka sasa’, nilisema. Alinifokea kwa ghadhabu. ‘Sawa basi usikasirike. Nitaenda sasa hivi kumuona na nitaswali naye swala ya *maghrib* na kumuomba atuombe msamaha sisi sote’, nilimwambia.” (Tirmidhi, Manaqib, 30; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, V, 391-2).

Sufi mkubwa aitwae Muhammad Ziyauddin - Mwenyezi Mungu aita-kase siri yake – kuna wakati alikuwa akiwakusanya watoto na kuwapa soh-bah. Mwishoni mwa sohbah moja wapo mke wake alimuuliza, ‘Wataelewa nini kuhusu sohbah? Wao bado ni wadogo.’

“Watafaidika kidogo au zaidi”, alisema. “Lakini lengo langu si kwamba waelewe. Mikusanyiko ya sohbah inavuta rehema takatifu. Mimi ninachota-futa ni hiyo rehema; watoto si chochote bali sababu tu...”

Shah Naqshbandi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Njia yetu ya mafunzo ya kiroho ipo juu ya sohbah. Wema unapatikana kwa kuwa pamoja na watu wema kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Kutokana na kuendelea kuwepo mbele ya hotuba zao kutapelekea kupata imani ya kweli”





Mwanachuoni Jafar ibn Sulayman r.alayh anatuambia faida alizoweza kuzipata kutokana na kuwa karibu na watu wema: “Kila nilipohisi ugumu katika moyo wangu nilienda kwa Muhammad ibn Wasi kwa ajili ya kuhudhuria mikusanyiko yake na kumuangalia usoni. Kisha moyo wangu ulikuwa ukilainika na uvivu niliokuwa nao ulikuwa ukiondoka na nafasi yake kuchukuliwa na shauku kubwa ya kufanya ibada. Shauku hiyo ilikuwa ikibakia kwa wiki moja.”

Maneno ya Omar ibn Abdulaziz r.alayh yanafanana na haya: “Kuwa pamoja na mwanachuoni Ubaydullah ibn Abdullah kutoka Madina kwangu ni bora kuliko dunia nzima na vilivyomo. Kuwa karibu na watu kama yeye kunaongoa akili, kunaleta amani ndani ya moyo na kusaidia kujenga maadili mema”

Mwanafunzi wa mtukufu Abu'l-Hasan Shazali - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliacha kuwa karibu naye. Baadae alimuona mwanafunzi yule na kumuuliza ni kwa nini aliacha sohbah yake.

*“Nilichovuna na kujifunza kutoka kwako mpaka sasa kinanitoshwa”, alijibu. “Sikuhitaji tena”. Huku akiwa amekasirishwa na maneno yale Shazali - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akasema:*

*“Sikiliza mpendwa; kama ingelikuwa mtu anatakiwa kutosheka na uongofu wa kiroho anaoupata kutoka kwa mwingine basi kwa hakika Abu Bakr - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – angelitosheka na kile alichokipata kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Lakini kinyume chake ni kwamba alikuwa naye bega kwa bega mpaka pumzi yake ya mwisho...”*

Bila shaka si Abu Bakr - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – peke yake ndiye aliyekimbilia sohbah ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa ajili ya uongofu wa kiroho, bali maswahaba wote walifanya hivyo. Vyovyote iwavyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiwashauri wafanye hivyo katika kila nafasi wanayoipata; kwani sohbah ilikuwa moja ya njia zake za kwanza za mafunzo.

Kama ulivyo umuhimu wa kuwa na tamaa ya kupata faida za sohbah vile vile ni muhimu kuangalia mahali na muda muafaka. Katika suala hili Abdullah ibn Masud amesema: “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema







na amani ziwe juu yake – alipotaka kutupatia ushauri aliangalia muda mzuri wa kufanya hivyo ili asije akatuchosha”.

Swahaba mwingine aitwae Abu Waqid al-Laysi anasimulia:

“Siku moja tulikuwa pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemama na amani ziwe juu yake – ndani ya msikiti, wakaja watu watatu mlan-goni. Mmoja aliondoka bila ya kuingia. Na wale wengine wawili waliingia na kukaa karibu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemama na amani ziwe juu yake. Mmoja miongoni mwao alikaa sehemu iliyokuwa wazi ndani ya duara. Kwa kuwa hakukuwa na nafasi nyingine iliyokuwa wazi yule mwingine alihofia kuwasumbua wengine hivyo akakaa nyuma ya duara.

Muda mfupi baadae Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemama na amani ziwe juu yake – akasema, “Je niwafahamisha kuhusiana na hali za watu hawa watatu? Wa kwanza aliyekaa ndani ya duara alitafuta ulinzi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu; na hivyo Mwenyezi Mungu alimlinda. Na wa pili alijisikia vibaya mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kushikamana na haya (maadili ya kiimani). Na Mwenyezi Mungu naye akatahayari mbele ya mja wake na hivyo akamuokoa na adhabu yake. Na yule mwingine ambaye hakingia na akaamua kuondoka, Mwenyezi Mungu naye amempa mgongo.” (Bukhari, Ilm, 8).

Wachamungu wanafahamu hekima iliyopo kwenye *hadith* hii ndio maana wameruhusu nyoyo zao zijengwe na mikusanyiko ya *sohbah* na kamwe hawakai mbali na sehemu hizo. Kwa hakika Imam Ahmad ibn Hambal – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye ni mwanafiqh mkubwa alikuwa akimtembelea Bishr ibn Khafi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – na kujadiliana naye. Alishikamana naye kikweli kweli.

Pindi wanafunzi wake walipomuuliza, “Je ni sawa kwa wewe kuendelea kumtembelea mtu w kawaida kama yeye wakati wewe ni *mujtahid* wa sayansi za Qur’an na *Sunnah*?”

“Ni kweli. Mimi nina ufahamu mkubwa zaidi kuliko yeye katika hilo ulilolizungumzia”, mwanachuoni yule mkubwa alijibu. “Lakini yeye anamfahamu Mwenyezi Mungu zaidi ya ninavyomfahamu mimi”.





### c. Huduma

***Kutoa huduma bora ni kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu kwa kuviendea viumbe kwa moyo safi, huruma na moyo wa ukarimu.***

***Watu wa huduma hawana budi kuwa makini katika mambo yao yote kana kwamba wananyata karibu na eneo lililopandwa mabomu; kwani makusudio yao ni nyoyo ambazo ndizo zenye kutazamwa na Mola.***

*Khidmah* au huduma ina umuhimu mkubwa katika mafunzo ya kisufi. Huduma ndio njia bora kwa ajili ya kuingiza hisia za staha, ukarimu (*mah-wiyah*) na huruma ndani ya nyoyo za viumbe. Hivyo *murshid* wote wameichukulia kuwa ni njia muhimu mno ya kuwafundishia wanafunzi.

Kama tungelitakiwa kutafuta nguzo ya maadili ya kiislamu bila shaka tungeliipata katika kumgeukia Mola kwa mapenzi na moyo safi, jambo ambalo kithibitisho chake ni huduma. Kutokana na ukweli wa kanuni ‘hudumia ili upate rehema (*himmah*)’, kuhudumia kunakuwa ni hatua kubwa katika ngazi yenye kuzipeleka nyoyo kwenye vilele vya utukufu.

Hatua hiyo ndiyo waliyoitumia Mitume yote na watakatifu walio-barikiwa kwa makutano matakatifu na malipo tele kwa ajili ya kufanyia tathmini. Waliyafanyia kazi maneno ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake: “Mtu muhimu katika kabila ni yule anayelihudumia” (Daylami, Musnad, H, 324).

Hivyo barabara ya kuelekea kwenye kilele na kuipata pepo inategemeana na huduma zilizotolewa kwa moyo safi. Kuna wakati ambapo huduma ndogo unayoitoa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu inaweza kuwa bora kuliko ibada nyingi za *Sunnah*. Hebu tujikumbushe tukio lifuatalo:

*Wakati wa mapambano katika joto kali Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaambia maswahaba zake wapumzike katika sehemu iliyokuwa nzuri kwao. Baadhi yao walikuwa wamefunga na wengine hawakuwa wamefunga. Wale waliokuwa wamefunga walilala haraka kutokana na kuchoka. Wale ambao hawakuwa wamefunga waliwabebea maji wale waliofunga na kuwatengenezea mahema kwa ajili ya kuwapa kivuli. Ulipofika muda wa kufuturu Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alisema: “Wale wasiofunga leo wamepata malipo makubwa kuliko wale waliofunga” (Muslim, Siyam, 100-101).*





Mtume aliyebarkiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye ametoa mahimizo mengi yahasuyo kupenda kuhudumia kwa ajili ya umma wake, alibeba mawe mgongoni mwake wakati wa ujenzi wa msikiti wa Quba na ule wa Madina licha ya maswahaba zake kumshauri asifanye vile. Staha ya hali ya juu na moyo wa kuhudumia aliokuwa nao Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – vinatoa mfano wa kipekee kwa waislamu wote. Kwa hakika maisha yake yote alijitolea kumhudumia Mwenyezi Mungu, wanadamu na viumbe vyote.

Kwa kawaida huduma huwa sifa bora ya mwenye hekima ambaye humuiga ‘huyo kiumbe mtakatifu’. Kila mtu ambaye anampenda Mola na ni mfuasi wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – huwa ni mtu wa kuhudumia. Watu wenye kuhudumia ni kama jua na mwezi, vitu ambavyo hung’aa zaidi pale vinapoangazia zaidi mahala fulani. Si msawajiko wa kipupwe wala kiangazi ambao unaweza kupunguza mng’ao wake. Ni kama mto wenye kwenda masafa marefu na kuwahudumia wanyama, miti, mawaridi, karafuu na vinega, mto ambao mwisho wake ni bahari ya upendo na makutano ya milele.

Wale wenye kuukubali ukweli huu hujiona ni watumishi hata kama watafanywa kuwa watawala wa watu. Pindi Sultan Selim alipoitwa ‘Mtawala wa ardhi mbili tukufu’ (*Hakimul-Haramayn’is-Sharifayn*) baada ya kuziweka Makka na Madina chini ya usimamizi wake alilikataa hilo katika hotuba yake ya kwanza kwa kusema, ‘Hapana; bali niiteni Mtumishi wa ardhi mbili takatifu’. Huu ni ubainifu wa utambuzi mkubwa juu ya huduma na ufahamu wa lengo la kweli la utumishi mbele ya Mola.

Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anadhania kuwa kiwango chake cha imani kinatokana na baraka za huduma yake pale aliposema, “Hatukupiga hatua katika njia hii kutokana na kusoma vitabu vya tasawwuf pekee bali kutokana na kuyafanyia kazi yale tuliyoyasoma kwa kadiri tulivyoweza na kuihudumia jamii. Kila mtu huongoka kwa kupitia njia fulani. Sisi tuliongoka kwa kupitia njia ya huduma.”

Na hili linaonyesha kuwa kufahamu peke yake hakutoshi bila ya kuyafanyia kazi yale unayoyafahamu kwa kupitia kwenye kuhudumu. Lakini bado kukubalika kwa huduma inayotolewa kunategemeana na ubora uliyonayo. Huduma yenye kukubaliwa au huduma bora ni ile ya kuwaenda watu kwa moyo safi, huruma na moyo wa ukarimu. Kwa maneno mengine





tunaweza kusema kuhudumia hakutakiwa kuambatane na dhamira binafsi na kinyume chake kunatakiwa kuwe kwa malengo ya kupata malipo kesho akhera. Kama kutafanywa kwa nia hii basi hata ‘nusu ya tende’ inaweza kuwa njia muhimu ya kupata uongofu, kama ambavyo imetajwa ndani ya *hadith* ifuatayo.

Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake anasimulia:

*“Siku moja nilikuwa sokoni mara mtu mmoja akanisogelea na kuniambia, ‘Nina njaa, je unaweza kunilisha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu?’*

*Wakati ule nilikuwa sina kitu zaidi ya imamah kuukuu iliyochakaa. Nikaenda kwenye mgahawa na kumuuliza mhusika kama angeliweza kumlisha mtu yule kwa malipo ya ile imamah. ‘Imechakaa lakini ni safi’, nilimwambia. ‘Unaweza kuitumia kwa ajili ya kukaushia vyombo vyako’.*

*Si tu yule mpishi alimlisha yule mtu bali pia alinitaka nikae nayo ile imamah. Licha ya kunisihi sana lakini sikuichukua. Nilisubiri mpaka yule mtu alipokula kwa kiasi alichotaka ingawa na mimi nilikuwa nikihitaji chakula”*

Kwa rehemu za Mwenyezi Mungu Mtukufu Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliishia kuwa na utajiri mkubwa; utajiri wake ulikuwa mkubwa kiasi kwamba alikuwa na maelfu ya wafanyakazi waliokuwa wakiyahudumia mashamba yake. Lakini bado hakurudi nyuma na kuacha huduma hata kwa hatua moja . Anasimulia tena msimamo wake pindi alipokuwa tajiri:

*“Nilijitwisha jukumu la kuwahudumia mwenyewe wagonjwa wanne ndani ya Madrasa ya Qutbuddin ndani ya Samarkand. Nilikuwa nikiwao-gesha na kuwavisha kwa mikono yangu. Kwa kuwa nilikuwa nikihudumia bila ya kupumzika muda si mrefu nikawa mtu wa kitandani. Lakini hata baada ya hapo niliendelea kubeba maji kwa chungu na kuwasafisha wale wagonjwa na kuwafulia nguo zao.”*

Maisha ya watu hawa wema yanatoa mifano ya kuigwa juu ya faida za kutumia na kuhudumia katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hata kama muislamu atakuwa tajiri kiasi gani lakini bado anaweza kuutendea wema utajiri wake kwa ajili kuimarisha imani yake na kujiongezea kiwango cha uchamungu wake. Pindi mtu atakapochunga viwango vya uchamungu na subira (zuhd) ndipo atakapoweza kusonga mbele kiimani na kuwa na staha





ya hali juu licha ya utajiri alionao, hili litampeka muislamu huyu mpaka kwenye daraja lililoonekana kwa Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake.

Kiwango kingine cha huduma ambacho ni vigumu kukifikia kinapatikana kwenye tukio lifuatalo la mwema Maruf Karhi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake.

*Siku moja mtu mmoja aliyekuwa mgonjwa, mzee na dhaifu alikuja kumtembelea Maruf Karhi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Mtu yule dhaifu alikuwa amekauka kana kwamba amekufa; alikuwa ni kana kwamba anajichomeka mwiba kwenye mwili wake dhaifu kwa kila pumzi aliyokuwa akivuta. Maruf Karhi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alimtandikia godoro chini ili apumzike.*

*Huku akiweweseka na kutaabika mtu yule alishindwa kupata usingiza mpaka asubuhi, pia hakuna mtu mwingine aliyeweza kulala kutokana na kuweweseka kwake. Kibaya zaidi alikuwa hatulii na hivyo alikuwa akiwasumbua wale waliomzunguka. Kutokana na kushindwa kukaa naye pale watu wengine walianza kuondoka kwenye ile nyumba mmoja baada ya mwingine. Maruf Karhi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – na mkewe ndio pekee waliokuwa wamebakia na mzee yule.*

*Ili kuhakikisha anamhudumia mzee yule vizuri alikuwa halali usiku. Lakini usiku mmoja bila ya kujitambua alipitiwa kidogo na usingizi kutokana na kukosa kwake usingizi kwa muda mrefu. Pindi alipomuona amelala badala ya kushukuru kwa kumpata mtu yule mwenye huruma na upendo ambaye anasimamia mahitaji yake, alianza kulalamika chini kwa chini:*

*“Ni daruwesh wa aina gani huyu? Watu kama hawa wanataka sifa tu. Ukweli ni kwamba wanataka kujionyesha. Tamaa ndio mwisho wa huduma yao. Watu hawa ni wasafi kwa nje lakini wachafu kwa ndani. Wana-washauri watu kwa uchamungu lakini wao wenyewe wanaupuuzia huo uchamungu. Ndio maana yule mtu pale amelala kwa raha bila ya kujali hali yangu. Inawezekanaje mtu aliyelala kwa kuridhika huku tumbo lake limejaa akaelewa tabu za mtu aliyelazwa kitandani ambaye hawezi hata kutikisa jicho lake kutokana na maumivu?”*

*Maruf Karhi alikuwa amesikia kila neno. Lakini kwa upole na ukarimu alijifanya hakisikia neno lolote. Lakini mkewe hakuweza kuvumilia,*





akamnong'oneza mmewe, “Umeshasikia alichokisema mzee huyu asiye na upendo. Hatuwezi kuendelea kuwa naye ndani ya nyumba yetu. Siwezi kuruhusu awe mzigo kwako na kukusababishia usumbufu zaidi ya huu ambao tayari ameshakusababishia. Mwambie ajisimamie mwenyewe. Wema hufanyiwa wale wenye kushukuru. Si vizuri kumfanyia wema mtu asiye na shukurani. Wema huo huwafanya kuwa wabaya zaidi. Hutakiwi kuwabembeleza na kuwawekea mito chini ya vichwa vyao. Kutengana nao ndio sahihi kwao.”

Huku Maruf Karhi akisikiliza hisia za mkewe kwa utulivu, alitabasamu na kujibu:

“Kwa nini maneno aliyasema yakuumize mpenzi? Kama amelalamika muache. Kama amefanya ukatili utakuwa dhidi yake. Maneno yake mabaya yanapendeza masikioni mwangu. Utaona kwamba yupo katika maumivu makali yenye kuendelea. Huoni kwamba mzee huyu dhaiifu hawezi hata kutikisa jicho? Fahamu kwamba werevu wa kweli, rehema ya kweli na huruma na kweli vinapatikana katika kujitahidi kuwavumilia watu kama hawa.”

Sheikh Sadi ambaye ndiye anayesimulia kisa hiki anaongezea ushauri ufuatao:

“Ubora katika huduma ni kuvumilia mzigo wa mdhaiifu pindi unapokuwa na nguvu na afya, haya ni kwa ajili ya kuonyesha shukurani. Moyo uliojaa huruma ni wenye kusamehe. Kama utaridhika na muonekano wako na mwili wako, basi jina lako litakufa. Lakini ukiwa ni mtu mwenye ukarimu na mwenye kujitolea katika kuhudumia, basi uhai wako utaendelea kuwepo kwenye nyoyo za wale uliowafanyia huduma hata baada ya kufa kwako. Je huoni kwamba kuna makaburi mengi ndani ya Karh lakini hakuna kaburi linalotembelewa na kuheshimiwa zaidi ya lile la Maruf Karhi?”

Watu wema tayari wameshalizungumzia jambo hili kwa uzuri zaidi: “*Tasawwuf* inahusiana na kupendwa bila ya wewe kuwa mzigo”.

Milango ya rehema hufunguliwa kwa huduma iliyotolewa kwa mapenzi na ukarimu. Thamani ya huduma inategemeana na ukubwa wa muhanga uliojitolea na kama huduma hiyo imetolewa kama ibada au la. Pia huduma bora ni ile iliyotolewa kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu, na kwa namna ambayo haitapelekea yule aliyepewa huduma aazirike. Kama





ambavy imesemwa na Abdullah ibn Munazil - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake: “Maadili katika huduma ni muhimu zaidi ya huduma yenyewe”.

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – naye ana mtazamo huo huo: “Fanya kazi kwa ajili ya kumpenda Mwenyezi Mungu. Hudumia kwa ajili ya kumpenda Mwenyezi Mungu. Unajali nini ikiwa watu watakukubali ama la? Je Mwenyezi Mungu hatoshi kuwa mteja wa heri katika soko ambalo ni hii dunia? Ni kipi ambacho watu watakupa kili-cho bora kuliko kile ambacho Mwenyezi Mungu atakupa? Hivyo usigeuzia macho yako kuelekea kwenye shukurani kutoka kwa watu bali geuzia uso wako kuelekea kwenye kukubalika kutokako kwa Mwenyezi Mungu!”

Kwa hakika huu ndio uzuri na utukufu ambao *tasawwuf* inalenga kuuingiza ndani ya nyoyo za watu. Maneno ya ushauri yaliyotolewa na kwa mwanafunzi wake aliyelitwa kwa lengo la kuukinga moyo wake dhidi ya vishawishi vya nafsi ni ya msingi mno:

Miongoni mwa watu waliokuwa na moyo wa huduma ni Wahb ibn Kabshah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Kaburi la swahaba huyu maarufu lipo China.<sup>35</sup> Mtume aliyebanikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alimpata jukumu la kwenda China kwa ajili ya kuipeleka nuru ya uongofu. Kwa mazingira ya wakati ule China ilikuwa na umbali wa masafa ya mwaka mmoja kutoka Uarabuni. Baada kukaa kule kwa miaka mingi swahaba huyu aliamua kufunga safari ya kuelekea Madina ili kutuliza shauku yake kubwa ya kumuona Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Aliwasili Madina baada ya safari ndefu ya mwaka mmoja lakini alikuta Mtume aliyebanikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – tayari ameshafariki. Hivyo hakuweza kumuona. Lakini kutokana na kutambua utukufu wa jukumu alilokuwa amepewa na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – aliamua kurudi tena China na kuhudumu mpaka mauti yalipomkuta.

Hizi ni faida za *Khidmah* ambazo imani thabiti ndiyo inayoweza kuzi-

35. Pia kuna bango (*maqam*) lililonasibishwa na Saad ibn Waqqas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - katika mji wa Guangzhou, china. Ni jambo linalofahamika kihistoria kwamba makaburi ya maswahaba na watu wema yanachukua nafasi kubwa katika kuamsha hisia za dini za wakazi wa eneo husika. Kuna mifano mingi kama hii katika Asia ya kati kama vile Samarkand, Bukhara na Tashkent.





fafanua. Kupenda kwao na moyo wao wa kuhudumia ni kama nyota zenye kuangazia anga zetu za uongofu wa milele.

Hakuna shaka kwamba maswahaba waliweza kufikia kwenye daraja hili kutokana na kushikamana kwao na kanuni tisa za huduma chini ya nuru ya mafunzo bora ya Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake. Kanuni hizo kama ifuatavyo:

1. Kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu na kwa moyo wako wote kushikamana na maamrisha yake na kujiweka mbali na makatazo yake.

2. Kumtumikia Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake; kumpenda kwa moyo wako wote na kuishi kulingana na *Sunnah* zake.

3. Kuwatumikia watu wazima katika uislamu kwa utii na upendo.

4. Kuwatumikia wazazi; kujitahidi kupata baraka bila ya kuwatamkia hata ‘ah’.

5. Kuwahudumia watoto kwa kuhakikisha kuwa wanalelewa kwa ajili ya kuwa waislamu wema.

6. Kuwahudumia ndugu; kuwatembelea na kuwakidhia haja zao.

7. Kuwahudumia waislamu, kushirikiana nao katika furaha na mau-mivu.

8. Kuwahudumia wanadamu wote, kujitahidi kutoa maneno na kufanya vitendo vyenye manufaa kwao.

9. Kuvihudumia viumbe vyote; kuviweka viumbe vyote chini ya mbawa zao za huruma.

Kuna somo kubwa katika maneno yafuatayo ya Ali Ramitani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – yanayohusiana na utekelezaji wa huduma zote zilizotajwa hapo juu: “Kuna watu wengi wanaochanganya huduma zao na matusi. Lakini kuna wachache ambao wanatambua ukubwa wa baraka ya kuhudumia. Kama utachukulia fursa ya kuhudumia kuwa ni baraka na kumshukuru yule unayemhudumia basi kila mmoja atakuridhia na hivyo wachache tu ndio watakaolalamika”.

Ikiwa tunatambua au la lakini wote tunatafuta amani na utulivu wa kiroho. Na vitu hivyo ni hazina kubwa ambayo huweza kupatikana kwa







kupitia kwenye huduma zinazotolewa kwa upendo ule ule anaokuwa nao mtu pindi atelekezapo ibada nyingine. Hivyo muumini mwenye mapenzi na moyo wa kuhudumia wakati wote hufahamu namna ya kupata fursa na njia za kumuwezesha kufanya hivyo. Shauku anayoinyesha katika vitu anavyojitolea muhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kubwa zaidi ya tamaa za wale wenye kutafuta faida za dunia.

Pindi tamaa ya kuhudumia ambayo inanawirishwa na mazingira ya upendo, itakapokuwa imekamatana na moyo itampelekea mtu kuwa msafiri wa kuelekea peponi. Moyo utajivua ugumu wa Hajjaj na kujifunika kwa joho laini la Yunus. Ujuzi, sanaa na maadili yaliyopatikana katika hali hii hupelekea kupata maisha ya milele ya peponi. Hivyo huduma halisi na ya kweli ni kazi bora ya moyo uliokomaa. Na kama inavyofahamika moyo ndipo mahala ambapo Mwenyezi Mungu anapatazama.

Ni hasara iliyoje kufanya upuuzi katika maisha, kufanya mambo yaliyo nje ya ubora wa moyo! Na ni furaha iliyoje kwa wale wenye kuweza kuzijaza nyoyo zao kwa mapenzi ya kuhudumia!

#### **d. Utegemezi wenye kupendekezwa (*Tawajjuh*)**

*Tawajjuh* inahusiana na *murshid* kuelekeza nguvu zake zote za kiroho kwa murid na hivyo kupeleka msimamo wake kwake; ni kitendo cha kujitolea kwake kiroho. Kwa meneno mengine ni kwamba *tawajjuh* inahusiana na *murshid-i kamil* kumpelekea *murid* wake hali zake nzuri za kiimani kwa ujumla wake. *Tawajjuh* ina namna mbalimbali, zote za msingi na za juu zaidi. Miongoni mwake tutaziongelea mbili: jicho (*nadhwar*) na dhati.

#### **Jicho**

Jicho ndilo lenye kuwezesha kuona. Athari inayopatikana katika kuona inaitwa ‘kijicho’, jina hilo limetokana na kazi ya jicho ambayo ni ‘kuangalia’. Katika matumizi ya lugha ya kila siku neno ‘kuona’ (*nadhwar*) linatumika mara nyingi kwa kumaanisha athari mbaya inayotokana na kuangalia, yani ‘jicho ovu’. Neno ‘jicho ovu’ (*nadhwar* au *isabatul-ayn*) linatumika mara nyingi kuashiria madhara ya kimwili na kiroho yanayopatikana kutokana na jicho la mwingine. ‘uangaliaji wa namna hii umetajwa katika *hadith* kadhaa:

“Kijicho (*nadhwar*) kipo” (Bukhari, Tibb, 36).





“Kijicho humpeleka mtu kaburini na ngamia kwenye maangamizi (humuua)” (Suyuti, al-Jamiu’s-Saghir, II, 60).

Watu wote wanakubaliana juu ya kuwepo kwa athari za jicho. Lakini jicho halina athari mbaya peke yake kama inavyofahamika kwa watu wengi; pia kuna athari nzuri katika jicho. Sababu inayopelekea kuwepo kwa athari hizi ni kutokana na jicho kutoa miale kuelekea kwa yule linalomuangalia, miale ambayo asili yake haifahamiki. Na athari zake zinategemeana na ubaya au uzuri uliobebwa kwenye miale hiyo. Ufahamu unaopatikana katika fizikia ya leo kuhusiana na miale ipo kwa namna ambayo haina jinsi bali kukubaliana na miale hii.

Mwangaza wa leza ambao ndio umegunduliwa katika karne hii pia ni aina moja wapo ya miale. Sasa hivi inafahamika na wengi kwamba miale ya leza inatumika katika kazi nyingi zilizo ngumu, kuanzia kwenye kukata chuma cha pua kizito mpaka kwenye kufanyia upasuaji hospitalini. Hapo kabla ilikuwa ikifahamika kuwa kuna mabadiliko mengi katika vitu mbalimbali, hasa rangi zake, pindi vinapopigwa na miale ya mwanga.<sup>36</sup>

Athari zinazosababishwa na miale inayotolewa na macho kwenye vitu vigumu haiko katika kiwango kimoja wakati wote, ikiwa ni kwa upande wa muangaliaji au muangaliwa. Kama ambavyo baadhi ya macho yanavyoweza kutoa miale, mizuri au mibaya, ndivyo ambavyo kunavyokuwa na baadhi ya watu ambao wapo kwenye athari ya kuathiriwa zaidi. Watu wengi huwachukulia watu wenye kutambulika kuwa wanatoa miale mikali mibaya kama ‘watazamaji waovu’ na hujitahidi kujiepusha na macho yao.

*Nadhwar* inapatikana hata kwa wanyama. Macho ya nyoka kifutu yana

36. Katika baadhi ya maktaba wameweka kava za kijani kwa ajili ya kuzuia macho yasichoke. Kuangalia baharini au angani kuna athari fulani katika macho; sawa na kuangalia katika kitu cha kijani. Sababu inayowapelekea watu kuvaa mavazi meupe wakati wa majira ya joto ni kutokana na uwezo wake wa kuakisi miale ya jua. Rangi nyeusi ni kinyume kabisa na hivyo. Kinyume na kuakisi mwanga rangi nyeusi hufyonza miale ya jua na kufanya mwili upate joto zaidi. Wakati kuvaa mavazi meupe hospitalini ni ishara ya usafi wakati huo huo madaktari wa upasuaji huvaa mavazi ya kijani ndani ya vyumba vya upasuaji. Hili linatokana na sababu ile ile; rangi ya kijani inaleta athari ya kubembeleza mbele ya macho. Mchanganyiko wa rangi ya njano na bluu kwa upande mwingine ni una tabia ya kufyonza miale inayoufikia. Ndio maana watoto huvalishwa hirizi za bluu au sarafu za dhahabu ili waepushie mbali athari za jicho la shari.





nguvu mno kiasi kwamba yanaweza kusababisha mimba kutoka na hata kifo katika baadhi ya viumbe hai.<sup>37</sup>

'Kijicho' kinachofahamika na watu wengi ingawa hakijathibitishwa kisayansi, kinachukua nafasi kubwa katika kuwafundisha wanafunzi katika *tasawwuf*. *Murshid*-i kamil ambaye ndiye mrithi wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ni mtu ambaye nguvu yake ya kuona imeenda mbali zaidi kwa namna yanavyoshawishi, hii inatokana na mafunzo ya kiroho na usafi wa moyo.

Tukitazama nyuma ya Mitume katika vyeo vya kiroho kuna maswahaba. Neno la kiarabu sahabah lenye maana ya 'swahaba', neno ambalo lina mzizi sawa na neno sohbah, linaashiria wale waliojaaliwa kuwa mbele ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, watu walioamini kila alichokuja nacho. Ingawa wanahitaji heshima kubwa kutoka kwetu kutokana na kuwa kwao mbele ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – lakini sababu kubwa iliyowafanya kuwa vile ilikuwa ni kutokana na kukutana na 'jicho' lake. Licha ya kuwepo vipengele mbalimbali vihusavyo uhalali wa mtu kukubaliwa kama 'swahaba' lakini chenye kukubalika zaidi na wengi ni kwa mtu kuonana na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, mtu huyo akamuangalia Mtume na Mtume naye akamuangalia mtu huyo.

Hata mtakatifu katika safu ya juu kwa namna yoyote ile hawezi kulinganishwa na swahaba, hata awe swahaba wa daraja la chini kabisa. Haya ni kwa sababu kila swahaba anabeba ubora wa peke yake ambao unatokana na kuangaliwa na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, ubora usioweza kulinganishwa na chochote kile, na ubora ambao hauna mbadala. Kwa kuwa waislamu waliowafuatia maswahaba hawakujaaliwa kuangaliwa na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, hivyo hawakuweza kufikia kwenye nafasi ya 'uswahaba'. Lakini bado wale waliojaaliwa kuwaona wale waliomuona Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – wanaitwa *Tabiun* na waliowafuatia wanaitwa *Taba-i Tabiin*.

Baada ya kuyasema hayo, watakatifu kutokana na kuwa kwao warithi wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – wana mam-laka na nguvu isiyoweza kulinganishwa na mtu mwingine yeyote. Hivyo ili

37. Rejea Bukhari, Badu 1-Khalq, 14.





kunufaika na *murshid-i kamil* kwa ukamilifu haitoshi tu kuwa miongoni mwa wale wanaohisi upendo kwake. Mtu hana budi kwenda mbali zaidi kwa kutafuta heshima tukufu ya kuangaliwa na jicho lake lenye kuongoa.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema: “Kuweni makini na mtazamo wa muumini; kwani hutazama kwa nuru ya Mwenyezi Mungu” (Tirmidhi, Tafsir, 15). Nguvu ya mtazamo ya kila muislamu inalingana na kiwango chake cha imani. Hivyo kutokana na kuwa kwao wakomavu wa imani nguvu za mtazamo za watakatifu zinazidi zile za waislamu wengine.

Neno ‘kuweni makini’ lililotajwa kwenye *hadith* limetumika kumaanisha tahadhari pindi mtu anapoenda mbele ya waislamu waliokomaa kiimani huku wakiwa na agenda walizozificha pamoja na akili chafu, kwani kwa msaada wa nguvu kubwa ya mtazamo wanaweza wakahisi kile unachotaribu kukificha. Kwa kuwa mapazia yamenyananyiwa kwa wale ambao uwezo wao mtazamo umefikia kiwango hiki, mara moja wanaweza kutambua vitu katika uhalisia wake. Hivyo maadili ya dini yanaagiza kuchunga ulimi wako mbele ya mwanachuoni na kuchunga moyo wake mbele ya mtu mwenye hekima.

Kwa kuwa ‘jicho’ ni moja ya njia muhimu anazozitumia *murshid* kwa ajili ya kumfundishia murid, hivyo kubahatika kuwa katika upande wenye kupokea kumechukuliwa kuwa ni fursa adhim.

### **Kumbukumbu binafsi**

Nilikutana na Ahmed Can, mtu mwenye moyo mzuri, katika miaka ambayo nilikuwa mwanafunzi katika ukumbi wa Imam-Hatip. Alikuwa ni mpakistani aliyekuwa na mapenzi makubwa na mheshimiwa Mahmud Sami Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Pia alikuwa akimpenda baba yangu Musa Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, kamwe hakutaka kukaa naye mbali. Mara kwa mara alikuwa akija Uturuki kwa ajili ya kumtembelea Mahmud Sami Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake na kukaa kwenye nyumba ya wageni katika bustani yetu.

Alikuwa ametekwa mno na mapenzi makubwa juu yake kiasi kwamba katika siku ambazo hakukuwa na *sohbah* alikuwa akiumia ndani ya moyo wake kutokana na kukosa kumuona Mahmud Sami Effendi - Mwenyezi





Mungu aitakase siri yake, hivyo alikuwa akitembea huku na kule karibu na nyumba yake kwa matumaini kuwa angeliweza kumuona hata kidogo tu. Usiku mmoja alisimulia ni vipi haya mapenzi yalijitokeza:

“Kilikuwa ni kipindi cha Hijja. Nilikuwa nimekaa ndani ya msikiti wa mmoja wa Madina katika eneo lililojulikana kwa jina la *Ashab-i Suffah* ndani ya *Rawdah*. Wakati fulani nilimuona mtu aliyekuwa na jamala na sura safi, mtu ambaye muonekano wake ulikuwa ni wenye kumfanya mtu amkumbuke Mwenyezi Mungu Mtukufu, mtu huyu alikuwa akitembea kuelekea pale nilipokuwa nimekaa huku akiwa na kundi la marafiki zake nyuma yake. Pindi alipokuwa anapita karibu yangu alinitazama kidogo.

Mtazamo ule uliokuwa mtukufu na wenye kung’aa mara moja ulinipeleka kwenye mazingira mengine, yani ulimwengu wa aina nyingine. Mara kila kitu kikabadilika. Raha ya kiroho niliyoipata kutokana na mtazamo ule ilikaribia kunifanya nipoteze fahamu. Baada ya muda mfupi niliporudiwa na fahamu zangu nilinyanyuka kwa lengo la kumtafuta yule mtu. Lakini msongamano mtukufu wa *Rawdah* ulipeleka kutowezekana.

Kwa matumani kwamba angelirudi karibu na sehemu ile nilianza kumsubiria karibu na pale nilipokuwa nimekaa mwanzoni. Na ninamshukuru Mwenyezi Mungu matumaini yangu yalitimia. Nilianza kumfuata kwa furaha. Wale waliokuwa wamemzunguka lazima watakuwa walidhania kuwa mimi ni omba omba, kwani baadhi yao walinisogelea na kutaka kunipa sadaka. Ukweli ni kwamba sikuwa tajiri; lakini baraka zilizotokana na mtazamo wa yule mtu zilifanya kila kitu kipoteze thamani mbele ya macho yangu. Nilijihisi kana kwamba nimeanza kuogelea kwenye bahari ya kuridhika. Muda si mrefu waliikaribia nyumba na kuanza kuingia ndani. Pindi nilipowafuata nyuma walitaka kunizuia kwa kuwa hawakufahamu mimi ni nani. Lakini Mahmud Sami Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, mtu aliyekuwa na hekima, aligeuka nyuma na kunikaribisha ndani. Siku ile nilibainikiwa na mambo mengi ya kiroho, mitazamo mingi na kuthaminiwa (*tawajjuh*).

*Alhamdulillah* kuanzia siku ile maisha yangu yakabadilika na kuwa bora zaidi, na nikawa mtu tofauti kabisa, mtu mwenye kujitahidi kutafuta maisha ya akhera tu. Kutunza fedha kila mwaka kwa ajili ya kuja hapa kwa lengo la kufaidika na mtazamo wake kumekuwa ndiyo sababu kubwa ya furaha ndani ya moyo wangu.”





## Dhati

Matumizi ya 'dhati' ndiyo njia bora na ya mkato yenye kutumiwa na *murshid* kwa ajili ya kuudhibiti moyo na nafsi ya *murid*. Hili linaweza kudhihirishwa na sifa ya *murshid* ijulikanayo kama *quddisah sirruh* (Mwenyezi Mungu aitakase siri yake) pale anapoifanyia kazi *sirr* au siri. Asili ya jambo hili inafahamika na yule anayeitumia, haipatikani katika tasawwuf ya kuongelewa (*qal*) bali katika msimamo wa kiroho (*hal*). Hivyo ufafanuzi wake hauwezi kupatikana katika vitabu.

### e. Maombi (Dua)

Maombi ni njia nyingine inayotumiwa na *murshid-i kamil* katika kumuelekeza mwanafunzi ili awe mwema. Pia maombi yana asili katika *Sunnah* za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

Inafahamika vyema kwamba kabla ya Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kuingia kwenye uislamu alitaka kufanya uovu mkubwa mno, alitaka kumuua Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake. Lakini kutokana na dua aliyoiomba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa niaba yake ilimuepushia kufanya vile na badala yake kutukuzwa kwa kupewa uongofu wa uislamu. Kuna mifano mingi kama hiyo katika maisha ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

Pia tukio lingine maarufu ni kipindi ambacho Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipoambiwa awalaani watu wa kabila la Thaqif pindi walipoikomboa Taifa, watu ambao walisababisha madhara makubwa kwa waislamu. Badala yake Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaombea uongofu, dua nzuri ambayo muda si mrefu baraka zake zililiwezesha kabila lote kwenda kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kuelezea nia yao ya kuingia kwenye uislamu.<sup>38</sup>

Shaybah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwa juu yake – anasimulia yafuatayo:

“*Nilikuwa karibu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani*





ziwe juu yake - katika vita vya Hunayn, si kwa sababu ndio niliingia kwenye uislamu au nilimkubali Mtume bali ni kwa sababu sikuweza kuvumilia kuona kabila la Hawazin likiongoza jeshi dhidi ya Maquraish. Vita vilipokolea huku Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akiwa karibu yangu nilisema:

‘Ninaona farasi weusi na weupe!’

‘Shaybah’, alisema Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, ‘makafiri peke yao ndio wanaoweza kuwaona farasi hao ambao wamekuja kwa ajili ya kuwasaidia waislamu’. Kisha akanihenga henga kwa kuni-gusa mgongoni na kusema, ‘Ewe Mola...Mpe Shaybah uongofu’. Alifanya hivi mara tatu. Aliposema kwa mara ya tatu pindi aliposhusha mkono wake tu nikahisi hakuna mtu katika dunia nzima ninayempenda kuliko yeye” (Ibn Kathir, al-Bidayah, IV, 333).

Licha ya kukataa maombi mengi ya kuingia kwenye uislamu kutoka kwa mwanae, mama wa Abu Hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliishia kuwa muislamu kutokana na dua ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake,<sup>39</sup> Abu Hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ni msimuliaji mkubwa wa *hadith*. Pia dua iliyombwa na mrithi wa kiroho wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ina athari kubwa; na hii inatoa nafasi nyingi za kurekebisha imani za watu.

Kwa namna yoyote ile dua hutoa majibu. Kama dua itakuwa inaenda kinyume na ‘majaaliwa ya Mwenyezi Mungu’ na hivyo kuachwa inaning’inia basi fidia yake itatolewa kesho akhera kama ilivyothibitishwa katika *hadith* mbalimbali.<sup>40</sup>

Kwa upande mwingine si lazima dua itolewe na mtu mwema mwenye msimamo mkubwa katika dini ndio ijibiwe, bali itajibiwa dua yoyote iliyoombwa kwa moyo safi na tamaa ya kweli juu ulichokiomba. Hivyo hata dua aliyoiimba muislamu muovu kumuombea ndugu yake ina thamani kubwa. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu hawaachi waja wake hata kama watakuwa na madhambi kiasi gani. Kama isingelikuwa hivyo kusenganya (*ghiybah*), yani kutaja ubaya wa mwingine nyuma ya mgongo wake, kus-

39. Rejea Muslim, Fadailu’s-Sahabah, 158.

40. Rejea Ahmed ibn Hanbal, Musnad, III, 18.





ingelitajwa kuwa ni dhambi kubwa.

Kwa sababu hiyo si sawa kwa mtu ambaye kwa namna moja au nyingine ameshindwa kujiepusha na madhambi akaacha kuuomba umma na vipenzi vyake kwa kudhania kwamba dua zake hazina thamani yoyote kutokana na hali yake ya kutenda madhambi. Hata dua za watu walio na madhambi mengi zaidi juu ya wengine inaweza kupokelewa ili mradi iwe imeombwa kwa moyo safi kana kwamba mtu anakihitaji mwenyewe kile alichokiomba. Mola hukubali dua ya yeyote anayemtaka.

Katika suala hili kuna umuhimu zaidi wa kuzungumzia kuhusu sifa nyingine za dua.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amewashauri waislamu kuombeana wao kwa wao mara kwa mara, wote wakiwa pamoja au kuwamuomba wengine wakati hawapo. Pindi Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipoenda kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa ajili ya kumuomba ruhsa ya kwenda kwenye umra alimuambia:

“Usitusahau katika dua zako ewe ndugu!” (Tirmidhi, Daawat, 109; Abu

Dawud, Witr, 23).

“Nilifurahi sana nilipoambiwa vile, ilikuwa kana kwamba nimepewa ulimwengu mzima”, Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisema.

Bila shaka Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - ndiye kiumbe kitukufu kuliko vyote mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Licha ya nafasi yake hii lakini aliwaomba maswahaba zake wamuombee. Hii inashiria kuwa watu wenye madaraja ya juu ya kiimani wanaweza kunufaika kutokana na dua za wale wenye madaraja ya chini.

Wakati mwingine Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake- alimwambia Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – yafuatayo: “Wabora miongoni mwa *Tabiun* ni mtu aitwae Uways. Kama ingelikuwa atoa kiapo kwa jina la Mwenyezi Mungu basi Mwenyezi Mungu angelifanya kiapo chake kuwa sahihi. Yeyote atakayekutana naye amuombe







amuombee msamaha”<sup>41</sup> Wakati fulani baadae Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikutana na Uways al-Qarani, hivyo akamuomba amuombee.

Hivyo ni wazi kwamba kuwaomba watu wema na watakatifu wakuombee dua kwa ajili ya kukuondolea matatizo na magumu na kupata vile vilivyo vyema ni jambo alilolishauri Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa umma wake.

---

41 Rejea Muslim, *Fadailu's-Sahabah*, 223-225





*Shikamana na kusamehe, na amrisha mema,  
na jitenge na majaahili. (al-Araf, 199)*



## E. UPEKEE WA USUFI

### 1. NAMNA YA MUONGOZO NA REHEMA

Kutokana na *Murshid* kufahamu fika kwamba mtindo wa kuongozea ni muhimu kama ulivyo muongozo wenye, wamekuwa wakifuata njia ya kiutume katika suala hili pia, hivyo kuwaongoza wengi. Kutokana na kuw-aongoza wanafunzi wao kwa upendo na huruma imewasaidia kuwafikisha mbali kiimani na kupata matokeo mazuri. Maisha ya watu wema yamebeba mifano mingi katika suala hili. Mfano ufuatao kutoka kwa Sufi mkubwa aitwae Ibrahim Hakki Erzurumi ni wenye mazingatio makubwa:

*Siku moja Ibrahim Hakki alialikwa kwenye kijiji cha jirani ndani ya Erzurum kwa ajili ya kutoa mawaidha ndani ya mwezi wa Ramadhani. Wanakijiji walimtuma kijana asiyekuwa muislamu kwa ajili kwenda kumchukua Ibrahim Hakki kutoka kwenye mji wao na kumpeleka kwenye kijiji chao. Kwa kuwa kulikuwa na farasi mmoja, Ibrahim Hakki - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alipanda kwa zamu pamoja na yule kijana, kama ambavyo Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alivyowahi kufanya pindi alipokuwa anaelekea Jerusalem pamoja na mtumwa wake licha ya mtumwa yule kukataa kitendo kile.*

*“Kama wanakijiji watasikia kuhusu jambo hiki si tu watanifokea bali watazuia malipo yangu!”, yule kijana aliendelea kusiondwa.*

*“Hakuna hata mmoja kati yetu anayefahamu hali atakayokuwa nayo wakati wa pumzi yake ya mwisho. Wewe unahofia watakachokufanyia wanakijiji lakini mimi ninahofia nitakachokuja kujibu mbele ya Mwenyezi Mungu!” Ibrahim Hakki alijibu. Hivyo waliendelea kupokezana kumpanda farasi yule licha ya hayo.*





Hekima ambayo ingeliweza kupatikana na kama ilivyotokea katika safari ya Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – pamoja na mtumwa wake, ilikuwa ni zamu ya yule kijana pindi walipokuwa wanaingia katika kijiji. Kutokana na kuwahofia wanakijiji yule kijana akaanza kumsihi Ibrahim Hakki achukue zamu yake.

“Hii ni zamu yako”, Ibrahim Hakki alijibu huku wakiwa wanaingia kwenye kijiji yule kijana akiwa juu ya farasi na Ibrahim akitembea mbele yake.

Pindi wanakijiji walipoiona hali ile walimzunguka yule kijana na kuanza kumfokea.

“Ewe fedhuli na fakiri usiyefikiria mambo!” walimbwatukia. “Yani wewe umeridhika kuendesha farasi ili kujikweza dhidi ya mtu huyu mtukufu na mwenye kuheshimika, si ndio? Je hivi ndivyo unavyofanya kazi zako? Je hiki ndicho tulichokulipia?”

Lakini Ibrahim Hakki - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliwatu-liza kwa kuelezea hali ilivyokuwa. Kisha mwanakijiji mmoja akamwambia yule kijana kwa sauti:

“Kutokana na kufanyiwa wema huu ni vyema uingie kwenye uislamu!”

Baada ya kimya kifupi yule kijana akasema:

“Kama unaniitia kwenye dini yako kamwe siwezi kuingia...Lakini kama unaniitia kwenye dini ya mtu huyu mtukufu tayari nilishaingia kwenye dini hiyo tokea tulipokuwa njiani!”

Tukio hilo la Ibrahim Hakki - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – linaweka kiwango cha mtindo unaotakiwa katika kumuongoza mtu kwa kupitia kwenye huruma. Inahusiana na kumtendea wema mwingine kwa ajili ya dhati yake, yani kumtazama kiumbe kwa jicho la Muumba. Kwa hiyo watakatifu ni wenye kutambua kuwa wamepewa jukumu la kuwa makhalifa wa Mwenyezi Mungu Mtukufu hapa ardhini, na kwamba wanaingia katika maneno ya aya isemayo, “nikampulizia roho yangu”.<sup>42</sup> Hivyo hata kama mtu atakuwa amechafuka kwa madhambi kiasi gani, kutokana na kuona usafi wa dhati yake kamwe hawawezi kumpuuzia. Mara nyingi hawakati tamaa juu ya mtu; hasa hasa humsaidia kushikamana na

42 Rejea al-Hijr, 29.





matumaini mpaka mwisho. Kwao matumaini ni kichocheo kisichopingika, kwa upande wa kiakili na kihisia. Hata ndani ya Qur'an tunakuta Mwenyezi Mungu Mtukufu anatumfundisha majina ar-Rahman na ar-Rahim mara nyingi zaidi ya Majina yake mengine, kiasi kwamba ameshusha sura iliyopewa jina la ar-Rahman, sura yenye kuanza kwa jina hilo hilo lenye kumaanisha, 'Yeye ambaye Huruma yake inavienea viumbe vyote'.

Kusimamia kwenye mtindo wenye kuridhisha Mwenyezi Mungu, yani kuwatazama wanadamu kwa kupitia dirisha la moyo na kuongoza kwa upendo pia kunasaidia kuibua uzuri uliojificha ndani ya moyo wa mwingine na hivyo kutoa matokeo yenye kuvutia. Mtindo huu unawaingizia wote mtendaji na mtendewa jamala ya hali ya juu, ukomavu, upendo na tamaa ya kuwa na Mwenyezi Mungu. Hii ndio dawa iliyowapunguzia maumivu ya mauti Yunus na Rumi.

Vyote tasawwuf na matumizi ya mtindo wa kisufi katika kuwaita watu waingie kwenye uislamu vimethibitisha kuwa na umuhimu mkubwa mno. Ni ukweli wa kihistoria kwamba katika kipindi ambacho kanuni ya kijamii ya Anatolia iliposhika kasi kwa watu wa Mongolia Sufi wakubwa kama vile Mawlana Rumi na Yunus Emre walitoa mchango mkubwa katika kurudisha amani na utulivu kwa watu wengi ambao walikuwa wamechanganywa, hivyo waliwaletea utulivu na ponyo kwa ajili ya vidonda vyao vilivyokuwa vikivuja damu pamoja na nyoyo zilizokuwa zimekata tamaa. Pindi utakapowachukulia wajinga kana kwamba ni wagonjwa wenye kungojea tiba utawafanya waondokane na hisia za kudhuru na chuki katika maisha yao. Yunus analizungumzia hili kwa vizuri kabisa kama ifuatavyo:

*Nimekuja kuleta malalamiko,<sup>43</sup>  
Mapenzi ndicho ninacholenga,  
Nyoyo ndizo zinazowakutanisha marafiki,  
Nimekuja kwa ajili ya kuzirekebisha nyoyo.*

Kwa kuwa watu hawa watukufu walijitahisi kuzirekebisha nyoyo, wamekuwa wakiwaangalia wengine kwa kupitia dirisha la moyo na kueneza upendo na huruma kwa wale wanaowazunguka, waliweza kuwaongoza wengi kuelekea kwenye uongofu. Kama wangelienda kinyume na mwenendo huu wenye kuvutia wangelikuwa wamepoteza kile kidogo kilichokuwa





kimewaunganisha na jamii, na hivyo kuondoa uwezekano wowote wa kuwaongoza. Na hili lingeenda kinyume na kutii matakwa ya Mola yenye kutaka watu waokolewe kutoka kwenye madimbwi waliyotumbukia. Mwenyezi Mungu Mtukufu ametuma maelfu ya Mitume katika historia nzima na kuwaagiza wazitakase nyoyo katika namna iliyo bora kabisa. Watu wema (ahlullah) nao ambao walipewa jukumu hili hili wamekuwa wakiuendeleza mtindo huu wa Mitume katika mafunzo yao ya kiroho.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ndiye chanzo cha rehemu na upendo anاتفahamisha namna bora kabisa ya kutumiwa na waja wake katika kuwaita watu kwenye haki:

“Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka” (an-Nahl, 125).

“Na ni nani mbora wa kusema kuliko aitaye kwa Mwenyezi Mungu na akatenda mema, na akasema: Hakika mimi ni katika Waislamu? Mema na maovu hayalingani. Pinga uovu kwa lilio jema zaidi. Hapo yule ambaye baina yako naye pana uadui atakuwa kama rafiki jamaa wa kukuonea uchungu” (Fussilat, 33-34).

Utumiaji wa mtindo huu umeweza kugeuza roho zilizozingirwa na miba mingi na kuwa waridi, na moyo ulio na kiza kama vile gereza lililo chini ya ardhi na kuwa bustani linalomulikwa na mwanga wa jua.

Kwa kuzingatia kanuni hii Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aita-kase siri yake – anagusia umuhimu wa kuwaingiza wanadamu wenye madhambi kwenye njia ya haki na vile vile namna ya kuyanya hivyo:

“Hata kama atakuwa kama chuma cheusi chenye kutu, kutu yake itaondolewa pindi kitakaposuguliwa na kung’arishwa. Ukikifuta kioo utaona kinaanza kung’aa na kuvutia, hata kama kitakuwa ni cha chuma, kitaanza kuakisi sura na maumbile mazuri.

Usiyamwagia matope maji ya ziwa la moyo kama unataka kuona mwezi na nyota zikielea juu yake! Wanadamu ni kama mto; pindi maji yake yatakajozwa matope hayataweza kuakisi chochote!”





Kama ambavyo Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anavyosema, roho ya mwanadamu ni kama maji safi; kama itachafuliwa kwa madhambi itakuwa nyeusi na hivyo kushindwa kuakisi wema wowote. Hivyo kunakuwa hakuna budi kuyasafisha maji hayo ili kuileta juu johari ya kiroho na nuru ya ukweli. Kwa hiyo lengo la *tasawwuf* ni kuitawala nafsi na hisia za ubinafsi na kumpeleka mtu na jamii kwa ujumla kwenye amani na utulivu. Kwa hakika Mola amempamba mwanadamu kwa jamala na utukufu. Thamani ya kweli ya mwanadamu inategemeana na namna anavyozistawisha sifa hizi. Nyoyo zilizojaaliwa kuwa na imani ni nyoyo zilizotunukiwa maadili mema, matendo mema na ubainifu wa kiroho. Ni kwa njia hii pekee ndipo mwanadamu ataweza kuwafikiana na kuumbwa kwake katika *ahsan-i taqwim*, yani katika maumbile bora zaidi.

Hivyo haijalishi ni kwa kiwango gani mtu amekufuru na kutenda madhambi, bado hawezi kunyang'anywa haki yake ya kualikwa kwenye haki. Moja ya mifano ya namna hii katika maisha ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – unasimuliwa kama ifuatavyo:

*Mjumbe Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alim-tuma swahaba aende akamuite Wahshi katika uislamu; huyu ni mtu yule yule alimuingiza Mtume – rehema na amani ziwe juu yake - katika huzuni kubwa kwa kumuua mjomba wake kipenzi Hamza – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Wahshi alistaajabisha na hili hivyo akasema:*

*“Mnaweza kuniita mtu kama mimi ndani ya uislamu wakati Mwenyezi Mungu anasema, ‘Na wale wasio mwomba mungu mwengine pamoja na Mwenyezi Mungu, wala hawau nafsi aliyo iharimisha Mwenyezi Mungu isipo kuwa kwa haki, wala hawazini - na atakaye fanya hayo atapata madhara, Atazidishiwa adhabu Siku ya Kiyama, na atadumu humo kwa kufedheheka” (al-Furqan, 68-69). Mimi ni mtu niliyeyatenda matendo yote hayo mabaya. Inawezekanaje kukawa na njia ya kutokea kwa upande wangu?’*

*Kuhusiana na hilo ilishushwa aya ifuatayo:*

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِن رَّحْمَةِ اللَّهِ  
إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ





rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu” (az-Zumar, 53).

Matumanini aliyoyapata kutokana na ujumbe wa aya yalimfanya Wahshi aseme yafuatayo kwa hisia kali:

“Ukubwa ulioje wa rehema zake ewe Mola!” Baada ya kutubia kwa moyo safi kisha akaingia kwenye uislamu yeye pamoja na marafiki zake.

Wahshi ambaye alimuua Hamza – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - katika vita vya Uhud sasa amekuwa swahaba. Kutokana na kuingiwa na raha ya imani kutokana na kupokea uongofu na kutokana na matumaini ya kurekebisha kosa lake la kumuua Hamza – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Wahshi – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliamua kuhatarisha maisha yake mpaka akamuua Musaylamatu’l-Kadhhab ambaye alikuwa ni mtume wa uongo na hivyo kukata mzizi wa fitna.

“Je utafutaji msamaha wa namna hii unakubalika kwa Wahshi peke yake ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?” maswahaba waliuliza.

“Unakubalika kwa waislamu wote”, alijibu.<sup>44</sup>

Kama tulivyoona kwa masimulizi yaliyopita, nyoyo zilizogeukia kwenye toba ya kweli kwa wakati ule zilisia ushuhuda muhimu wa huruma na upendo wa kweli kutoka kwenye midomo ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – mwenyewe. Pia kutoka kwenye midomo hiyo hiyo wanadamu wote wamesikia maneno yenye kutia faraja juu ya tiba na faraja. Pia ni kutokana na nuru ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – ndio maana wanadamu wanaweza kuona bahari ya rehema na ukarimu isiyo na mipaka na fukwe ya matumaini. Na pia kutokana na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – waja wameitwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mwito wa ‘Enyi waja wangu!’

Hivyo katika zama hizi kuipa kipaumbele rehema na huruma ya Mola na kusambaza matumaini ni jambo lenye umuhimu mkubwa katika kuondoa janga la kiimani lililosambaa kutokana na ushawishi wa wayakinifu wa magharibi. Ni rahisi kuwapata watu kihisia kuliko kuwachochea katika malumbano ya kimantiki. Leo hii watu wengi wanaenda pabaya kutokana na kuegemea katika mantiki, jambo ambalo linapelekea kuwa vigumu mno

44 Rejea Haythami, Majmau’z-Zawaid, X, 214-215.





kuwashawishi kwa kutumia hoja. Pindi mtu anapokuwa kimantiki ameingia katika mfumo wa kujibu mambo katika njia aliyokwishajengewa hapo kabla inamzuia kukubaliana na uthibitisho wa kimantiki. Katika kuzihofisha nyoyo kuelekea kwenye ukweli ni bora zaidi kwanza kuwaendea kwa huruma na uvumilivu na kisha kuwasaidia wastawishe hali zao za kiroho za ndani.



Mtu hana budi kwanza kuuteka moyo wa mtu aliyezama katika dimbwi la makosa, uasi na madhambi kabla ya kumkosoa, kumpinga na hata kumuomba atekeleze maamrishi ya dini. Kwa msingi huu mtu hana budi kujenga upendo na mtu yule jambo ambalo ndilo msingi wa ukaribu wao. Pindi moyo wa mtu utakapoanza kupatana naye hapo mtu ataweza kuanza taratibu kusahihisha makosa yake. Mtu asije akadharau baraka zinazotokana na kumjenga mtu kimwili na kiroho. Kwa msingi huu mtu hana budi kukamata vyema maneno yafuatayo kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye ndiye dirisha la matumaini lililofunguliwa kwa ajili ya nyoyo zilizozongwa na moshi wa dhambi, hivyo kuzipa pumzi safi ya uhai:

“Uombezi wangu hasa ni kwa wale waliotenda madhambi makubwa miongoni mwa watu katika umma wangu” (Abu Dawud, *Sunnah*, 20).

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anafafanua juu ya huruma ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa waovu: “Dawa hutafuta wagonjwa na waliojeruhiwa kwa ajili ya kuwaponya. Tiba huenda kwenye ugonjwa. Maji huelekea kwenye mfereji. Kama unahitaji maji ya rehema na huruma basi kuwa kama hivyo pia!”

Lakini ili dawa ifanye kazi vizuri huna budi kukisafisha kidonda kwanza na kuwaondoa bakteria wote. Ili kuzisafisha nyoyo zenye maradhi kwa ajili ya kuondoa bakteria wa madhambi huna budi kuziosha kwa maji ya toba. Uombezi wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambao ndio dawa hufuatia baada ya hapo.

Katika *hadith* nyingine Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Mwenye kutubia madhambi yake ni kana kwamba hakutenda madhambi kabisa” (Ibn Majah, *Zuhd*, 30). Haya ni maneno







yenye kutoa bishara njema kwa upande mmoja na kuashiria uzito wa huruma tukufu kwa upande mwingine.

Namna bora ya kuwaongoza ambayo ni kuwaongoza watu kwa huruma inayopatikana kwa Mitume wote pia imefuatwa kwa umakini na watu wema. Vile vile imekubalika kuwa matunda ya kwanza ya imani ni huruma na utumishi, jambo hili limeelezewa ndani ya viwango viwili vifuatavyo:

*Ta'zim li-amrillah*; au kutekeleza maamrisho ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa umakini na heshima.

*Shafqat li-khalqillah*; au kuvihurumia viumbe kwa ajili ya Muumba.

Fudayl ibn Iyad - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anatoa mfanoo bora juu ya muislamu mwenye kuishi kwa namna hii:

Siku moja walipomuona analia walimuuliza sababu.

“Ninalia kwa sababu ninajisikia vibaya juu ya muislamu mwingine ambaye amefanya makosa”, alijibu. “Ninahofia atapata tabu kesho akhera”.

Katika kutumulikia juu ya jambo linalowapelekea waislamu waliokomaa kiimani na wenye sifa kama hiyo kuhisi huruma na upole kama huo, Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema: “Pindi bahari za huruma zinapojaa hata mawe yatakunywa maji ya uhai. Maiti za watu waliokufa miaka mia moja iliyopita zitanyanyuka kutoka makaburi mwao na nyuso zenye uchafu na uovu zitachukua uzuri wa kimalaika na kuonewa wivu na hata mahurulaini wa peponi”.

*Imepokewa kwamba siku moja Ibrahim Adham - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliuosha mdomo mchafu wa mlevi, aliwajibu wale wali-oshindwa kumuelewa kwa nini alifanya vile kwa kusema:*

*“Ingelikuwa si heshima kwangu kuacha mdomo na ulimi uliombwa kwa ajili ya kutaja jina la Mwenyezi Mungu kuwa mchafu!”*

*Pindi yule mtu aliporudiwa na fahamu walimwambia, “Ibrahim Adham wa Khorasan ameosha mdomo wako!”*

*Kutokana na kuhisi aibu mtu yule mara moja aliamka kiroho, akajisemea moyoni mwake, “Kama ni hivyo, ninatubia madhambi yangu!”*

*Ibrahim Adham - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye alisaid-*





*ia kuongoka kwa mtu yule usiku wake alisikia sauti katika ndoto ikisema:*

*“Uliosha mdomo wake kwa ajili yetu; na Sisi tumeosha moyo wake kwa ajili yako!”*



Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu Mtukufu anamshauri Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – pamoja na waislamu wengine kama ifuatavyo: “Shikamana na kusamehe, na amrisha mema, na jitenge na majaahili” (al-Araf, 199).

Katika kuyafanyia kazi maagizo haya bila shaka mfano bora wa kuigwa unapatikana kwa Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Tunaweza kusema maadili, huruma na kusamehe alikuwa nako kuliko kwa kiwango ambacho kingeliwafanya hata malaika wamuonee wivu. Mfano ufuatao ni mmoja miongoni mwa mingine mingi:

*Katika siku ilipokombolewa Makka Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alitangaza msamaha wa jumla kwa wale wakosaji wa kisiasa. Pamoja na Makka kushuhudia dhulma, ukandamizaji na uadui mkubwa kwa miaka mingi, sasa ilikuwa ikipata upepo mwanana wa huruma na upole uliotokana na msamaha mkubwa uliowaeneo wote. Lakini mkazi mmoja wa Makka aliyekuwa anaitwa Fadala huku akiwa na nia ya kuichafua siku ile nzuri kwa kuleta kivuli kibaya alimuendea Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa lengo la kumuua. Huku akiwa na utambuzi juu ya nia yake mbaya wakati anamuendea Mtume, Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – bila ya kuonyesha dalili yoyote ya wasiwasi au hasira alimnyooshea Fadala mbawa zake za huruma, alisema yafuatayo huku akiweka mikono yake iliyobari kiwa kwenye kifua cha Fadala:*

*“Ewe Fadala, tubia juu ya nia uliyonayo kichwani mwako!” Kuanzia pale nia mbaya iliyokuwa kichwani mwa Fadala ikatoweka. Hivyo moyo wake ukanyenyekea na kujawa na nuru ya imani. Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akawa ndiye kipenzi chake kikubwa miongoni mwa viumbe wengine wote”.<sup>45</sup>*





Bila shaka huu ni ukomavu mkubwa katika tabia, jambo ambalo linadhihirisha kanuni isemayo ‘Mfanye yule aliyekuja kuua ahuishwe kwa kupitia wewe’; na historia ya uislamu imejaa mifano kama hiyo. Wengi miongoni mwa watu akiwemo Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ni matunda ya mtindo huu mzuri wenye kustaajabisha. Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

*“Kutokana na utukufu wa rehema za Mwenyezi Mungu na mawimbi makubwa ya bahari ya wema kila ardhi kavu hupata mvua na kila udongo mkavu huunganishwa kwa maji”.*

*“Ewe unayewaita watu kwenye uongofu...! Fahamu ya kwamba dawa ya jicho ovu ni jicho jema! Jicho jema na mtazamo mwema hulikamata jicho ovu na kuliangamiza. Jicho jema na mtazamo mwema hufanya hivyo kutokana na ukweli kwamba huruma ya Mwenyezi Mungu iko juu ya ghadhabu Yake. Jicho hili ni sawa na rehema na jicho ovu ni sawa ghadhabu. Kwa kuwa mtazamo mwema unatokana na rehema takatifu ndio maana uko juu ya jicho ovu. Huu ni ubainifu ulioelezwa katika hadith qudsi isemayo ‘Huruma yangu inazidi Ghadhabu Zangu’ (Bukhari, Tawhid, 55). Fahamuni kwamba katika mazingira yoyote yale huruma ya Mwenyezi Mungu inazidi ghadhabu Zak. Hii ndio sababu iliyopelekea kila Mtume aweze kuwashinda maadui zake.*

*Hivyo matatizo hayaondolewi kwa kulalamika au kukandamiza. Tiba yake ni kuonyesha wema na kusamehe. Amka kutokana na tahadhari ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – isemayo ‘sadaka huondoa matatizo’.<sup>46</sup> Tambua njia ya kuondokana na maradhi na matatizo!*

*Lakini msisahau kwamba kuwasamehe madhalimu ni kuwadhulumu wale waliodhulumiwa! Kuwaonea huruma wezi na mafedhuli ni kuwapiga madhaifu na kuwanyang’anya rehema!”*

Hivyo mtu hana budi kujenga uwiano sahihi. Ni kweli kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *Ghafuru’r-Rahim*, yani mwingi wa kusamehe na mwingi wa rehema; Lakini pia Yeye ni *Azizun Dhu’ntiqam*, Mwenye kuwalipizia kisasi wale waliodhulumiwa.

Hivyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

<sup>46</sup> Rejea Tirmidhi, Zakat, 28; Suyuti, al-Jamiu’s-Saghir, I, 108.





*“Pindi utakapoona ndugu zako wawili wanapigana wakimbilie ukamuokoe mwenye kudhulumu na mwenye kudhulumwiwa”.*

*“Tunaona ni namna gani tunaweza kumsaidia aliyedhulumwiwa ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu; ni vipi tutamsaidia mwenye kudhulumu?” maswahaba waliuliza, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akawajibu kwa kusema:*

*“Kwa kumzuia asidhulumu...” (Bukhari, Ikrah, 7; Muslim, Birr, 62).*

Kwa ufupi tunachotaka kusema ni kwamba vyote imani na hekima waliyonayo wanadamu wa leo wakiwemo waislamu ni kama ndege aliyejeruhiwa. Hivyo hatuna budi kuwaendea kwa umakini mkubwa na kuyafunika majeraha yao. Na hili litaweza kufanyika kwa kutekeleza mtindo na maelekezo tuliyokwishayajadili.





**U**vumilivu kwa mtu aliyetenda dhambi usihamishiwe kwenye dhambi; na uadui juu ya dhambi usihamishiwe kwa mtenda dhambi. Muislamu wa namna hii hana budi kujikosoa mwenyewe na kuwavumilia wengine, kama njia bora ya kuwaita watu kwenye haki.



## 2.NAMNA YA UPOLE NA UPENDO

Pindi utakapowatazama wanadamu kwa jicho la kisufi utazingatia zaidi dhati yao na si upande wa utendaji wao wa madhambi. Hii ni hekima kubwa inayodhihirisha namna mtindo huu wa *tasawwuf* unavyopelekea kumhurumia na kumpenda mtenda madhambi lakini si madhambi yake. Sufi wa kweli humchukulia mtenda madhambi kama ndege aliyevunjika bawa, hivyo anahitaji uangalifu na huruma. Huwa anahisi jukumu la kumrudishia mtenda madhambi afya yake na kuishughulikia roho yake iliyo katika matatizo na kumfanya apae tena. Juu ya yote hayo uvumilivu na huruma juu ya viumbe kwa ajili ya Muumba ndiyo njia muhimu ya kumwezesha muislamu kufikia kwenye wema na ukomavu unaokusudiwa.

Imesimuliwa kuwa wakati Abu'd-Darda – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alipokuwa jaji ndani ya Damascus alilisikia kundi la watu likimlaumu hadharani mtu mwingine ambaye alikuwa mtenda madhambi.

“Kama mngelimuona mtu amedondokea ndani ya shimo je mngelifanyaje?”, aliwauliza.

“Tungelimshushia kamba na kujaribu kumvuta ili atoke”, walijibu.

“Kama ni hivyo basi msimseme vibaya, badala yake mshukuruni Mwenyezi Mungu kwa hali zenu kuwa nzuri na jaribuni kumuokoa ndugu yenu ambaye ameingia kwenye shimo la madhambi”.

“Je hauna uadui na huyu muovu”, waliuliza huku wakistaajabu.

Swahaba huyu aliyekuwa ameiva kutokana na mafunzo ya kipekee ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alitoa jibu zuri lifuatalo:

“Mimi ni adui wa madhambi na si wa utu wake. Atakuwa ndugu yangu katika imani mara tu atakapochana na madhambi yake”.<sup>47</sup>

47. Rejea Abdurrazzaq, Musannaf, XI, 180; Abu Nuayra, Hilyah, 1/225.





Hizi ni sifa bora anazokusudia kutupatia Abu'd-Darda – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Sifa hizo ni mwangaza kutoka kwenye mwenendo mtukufu wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – pamoja na maamrisho na radhi za Mwenyezi Mungu. Kutokana na kuangukia kwenye udongo wa wema wenye rutuba sifa hizi zimetambuliwa katika historia nzima ya uislamu kama kipimo cha ukomavu wa kiimani na njia ya kupatia nuru na furaha ya uongofu.

Mtindo huu unajaribu kumtakasa muovu kwenye maji ya uvumilivu, kusamehe, huruma na upendo bila ya kumgharikisha katika madhambi yake. Mtume

aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaendea hata washirikina wakubwa kama vile Abu Jahl kwa mtindo huu, bila ya kuingilia anasa zake wala kuyavutia madhambi yake kwenye nuru, bali kuwaa-likia waingie kwenye utakaso ndani ya maji ya imani, ambayo ndiyo bahari ya uongofu na furaha. Lililopo mbele yetu ni funzo kubwa la kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hufuta moja kwa moja madhambi yote ya wale wenye kutubia kwa moyo safi na kuwafanya kana kwamba hawakutenda madhambi yoyote hapo kabla, hufikia hata kubadilisha makosa yao yaliyopita na kuwa thawabu kulingana na kiwango chao cha usafi wa moyo. *Ayah* inasema:

“Isipo kuwa atakaye tubu, na akaamini, na akatenda vitendo vyema. Basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu” (al-Furqan, 70).

Wale wasio na huruma ya namna hii ni maadui wa nafsi zao na wanadamu wote. Watu wa aina hii wasio na huruma na uvumilivu hata kidogo ni wenye kuhuzunisha kutokana na kuzuia kwao furaha ya nafsi zao kwa mikono yao wenyewe. Kinyume chake watu kama Yunus na Mawlana ambao wamefaulu katika kuwa na huruma ni kama mawaridi mazuri ya peponi yaliyopambwa si kwa wanadamu peke yao bali na wanyama pia, wanyama kuanzia wale wakali kama mbwa mwitu mpaka wale wapole kama ngege. Wanapendezesha mazingira yao hata kwa kutumia ukali wao, hivyo kutibu roho zilizojeruhiwa. Ufunguo ni kujipamba na tabia ya waridi. Hatuna budi kupenda kila kiumbe hapa duniani licha ya kuhuzunishwa na tabia zake zisizokupendezea. Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - anasema yafuatayo juu ya suala hili:





“Ilikuwa ni kwa sababu haukuogopa usiku na kulikimbia giza ndio maana mwezi ukawashwa na kuanza kusambaza mwanga. Na waridi lilipata harufu nzuri kutokana na kukaa vizuri na miba.

Sikiliza ukweli huu kutoka kwenye waridi; tazama waridi linasema, ‘Kwa nini nihuzunike kutokana na kuwa pamoja na miba? Sikupata tabasamu hili kwa sababu nyingine tofauti na kuwa karibu na miba. Miba ndiyo sababu iliyonifanya niweze kutoa harufu nzuri hapa duniani..”

Esrefoglu Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anatoa sauti ya kiushairi juu ya namna ya kuwa na mtazamo huu.

*Kwa ajili ya rafiki,*

*Mtu anapaswa kumeza sumu kana kwamba ni tamu.*



Swahaba mmoja alimlaani mtu kutokana na kuchoshwa na kumuadhibu mtu huyo kwa kosa la ulevi. Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipolisikia hili alisema: “Usimlaani mtu huyo. Ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba kuna kitu kimoja ninachokifahamu kutoka kwake, kitu chenyewe ni kwamba anampenda Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake” (Bukhari, Hudud, 5).

Mwanafunzi wa marehemu Mahmud Sami Ramazanoglu - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye alikuwa katika msongo wa mawazo alikosea kufanya maamuzi hivyo akaenda kwenye mlango wa mwalimu wake huku akiwa amelewa. Mtu aliyefungua mlango alimsema.

“Jiangalie!” alisema. “Je unafahamu umekuja kwenye mlango wa nani?”. “Ndio, ninafahamu” mwanafunzi yule dhaifu na mwenye kuhuzunisha alijibu. “Lakini kwani mlango mwingine ambao utaweza kunikumbatia kwa upendo?”

*Sami Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – baada ya kuyasikia mazungumzo yao yote alikuja mlango upesi na kumuingiza ndani yule mwanafunzi wake aliyekuwa ameumia kihisia na kumuingiza kwenye kasri la moyo wake. Alihuisha moyo wake uliokuwa na majonzi kwa upendo, huruma na upole. Kutokana na kupata fursa ile mwanafunzi yule baada akaachana na tabia yake mbaya na kuungana na watu wema.*





Maana ya kutazama viumbe kwa kupitia jicho la Muumba, kanuni muhimu iliyotumika kwenye maisha watu wengi wema inaelezewa vizuri zaidi katika *hadith* ifuatayo:

*“Naapa kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye uhai wangu uko Mikononi mwake kwamba hamuwezi kuingia peponi mpaka mhurumiane”.*

*“Sote tuna huruma ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu” maswahaba walisema.*

*Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alifafanua, “Nikisema huruma simaanishi huruma mliyonayo katika yenu kwa namna mnavyoelewa nyinyi. Bali ni huruma yenye kuvienea viumbe vyote...huruma yenye kuvienea viumbe vyote” (Hakim, Mustadrak, IV, 185).*

Haijalishi mwanadamu yupo mbali na lengo lake kuu kwa kiasi gani, lakini bado ataheshimiwa kwa kuwa yeye ni ‘mwanadamu’. Kuzama kwake kwenye dimbwi la madhambi bila kufahamu utukufu uliobebwa na dhati yake labda kunaweza kulinganishwa na jiwe jeusi lililoning’inia kwenye ukuta wa Al-Kaaba pindi linapodondoka chini na kuchafuka. Kama kiten-do hicho kimetokea je inaingia kwenye akili ya muislamu kuliacha pale na kuendelea na mambo yake kana kwamba hakuna kitu kilichotokea. Hata kama lingelikuwa limechafuka waislamu wasingecha kuliheshimu. Bali wangelikota pale chini pamoja na uchafu wake na kulisafisha huku wakitokwa na machozi na kisha kushindana juu ya atakayelirudisha kwenye sehemu yake ya juu lilikokuwa kabla ya kudondoka. Kutokana na kukumbuka kuwa asili yake ni peponi watasahau uchafu wake wa nje na kutaza thamani yake. Hata kama mtu ataangukia kwenye dhambi kwa kiasi gani lakini thamani yake ya ndani haitobadilika.

Hakuna daktari mweledi ambaye atamkasirikia mgonjwa kutokana na kupatwa na maradhi. Hata kama maradhi yake yangelikuwa yamesababishwa na uzembe wa mgonjwa lakini bado angelimuelezea sababu za ugonjwa ule ikiwa za kimwili au za kiakili. Hivyo badala ya kumkasirikia mgonjwa kutokana na kuchangia kwake kwa namna yoyote ile katika kuathiriwa na ugonjwa husika, daktari atatuliza maumivu yake na kuharakisha kumtibu kwa wema na huruma bila ya kupoteza muda. Atajihisi anawajibika katika kupona kwa mgonjwa. Sufi naye pia anaishi katika jamii huku akiwa na mtazamo kama wa daktari ambaye yuko wodini, mtazamo ambao unakuwa kama boya la kuwaokolea watu majini.







Kumpelekea mtu boya hilo na kumvuta ili kumuondoa kwenye mawimbi makubwa ya dhambi kunatoa nafasi muhimu katika kuelekea kwenye furaha ya milele. Ushauri wa Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – aliompatia Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - katika vita vya Khaibar una umuhimu mkubwa mno:

“ewe Ali...mtu kuongoka kwa kupitia kwako ni bora kuliko kumiliki bonde la ngamia wekundu” (Bukhari, jihad, 143).

Ukweli huu unatolewa tena katika aya ifuatayo:

وَمَنْ أَحْيَاهَا فَكَانَتْ أَحْيَا النَّاسِ جَمِيعًا

“...Na mwenye kumuokoa mtu na mauti ni kama amewaokoa watu wote.” (al-Maidah, 32).

Hili ni suala la imani. Bila shaka ukafiri ni kosa kubwa mno ambalo linaweza kufanya na mtu. Kwa kuwa njia ya upole ni yenye mafanikio makubwa katika kumuokoa mtu kutoka kwenye ukafiri ndio maana pindi Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomtuma Musa (a.s) aende kwa Firauni ili kumshauri kuhusiana na imani, Alimuagiza Mtume Musa (a.s) azungumze naye kwa maneno laini (*qawl-i layyin*). Mwenyezi Mungu Mtukufu akiwa akijua fika juu ya uzito wa ukafiri wa Firauni. Hivyo hata kama mtu atakuwa mkorofi kama Firauni hatuna budi kuwa makini hisia zetu zisije zikatutawala kiasi kwamba tukatumia maneno ya kuogopesha na kutishia. Badala yake hatuna budi kujitahidi kuongozwa na mafundisho matakatifu ambayo yanasisitiza juu ya matumizi ya maneno laini. Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – analielezea jambo hili kwa vizuri kama ifuatavyo:

“Yazingatie kikamilifu maneno ya Mola kwa Musa, ‘Zungumza na Firauni kwa ulaini na umuonyeshe upole’

Kwa kumimina maji kwenye mafuta yanayochemka utaharibu vyote jiko na chungu”.

Katika aya ifuatayo ambayo Mwenyezi Mungu anamuongelesha Mjumbe wake – rehemu na amani ziwe juu yake – na umma mzima, anasema yafuatayo:





فَبِمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظًا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ

“Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia. Basi wasamehe, na waombe maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea” (Al-Imran, 159).

Njia hii haitumiki kwa makafiri na waovu peke yao bali haina budi kutumika kwa waislamu wenye udhaifu wa namna fulani na kasoro za kibinadamu, waislamu ambao kwa upande mwingine wanaishi maisha ya kiislamu. Njia ambayo itamdhalilisha na kumuumiza mtu kihisia wakati ingelitakiwa kumsahihisha inaweza kuleta athari mbaya jambo litakuwa ni kinyume na makusudio, kwani itaweza kumzamisha zaidi mtu kwenye madhambi. Watu watakaoendewa kwa namna hii wanaweza kuwa wasumbufu hata kwa wazazi wao na kupelekea kuwa vigumu kuwaelewa hata wengine wenye lengo zuri. Hata ukweli wenye kutolewa kwa ukali unaweza kuwa kama kisu chenye kukata ngozi na hivyo kupoteza faida yote. Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Hata baba yako ataonekana ni dubwana katili na lisilokuwa na huruma pindi anapokutahadharisha juu ya kosa. Hii ni athari iliyotokana na kukaripia kwake kwa ukali. Ingawa kukaripia kwa baba kulikuwa ni kwa manufaa yako lakini ukali wa makaripio yake yataifanya huruma na upole ndani ya moyo wake uonekane kama dubwana”.

Tabia hii ya kisaikolojia ya mwanadamu haina budi kuzingatiwa na hata mtu azame katika madhambi kwa kiasi gani lakini bado thamani yake haipaswi kusahuliwa kamwe. Hii ndio sababu iliyompelekea Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kusema:

“Kumdharau ndugu yako muislamu inatosha kuwa dhambi” (Muslim, Birr, 32).

Kutokana na kuvutiwa na *hadith* hiyo Bezmialem Valide Sultan alianzisha mfuko kwa ajili ya kufidia vitu ambavyo vinaweza kuvunjwa na watumishi wake licha ya kujisikia vibaya kutokana kuvivunja kwa bahati mbaya. Na huu ni mtazamo wa mfano ambao unajieleza wenyewe.





Muislamu mwenye utambuzi wa namna hiyo hana budi kujikoso mwenyewe na kuwavumilia wengine; kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: “Enyi mlio amini! Jiepusheni na dhana nyingi, kwani baadhi ya dhana ni dhambi. Wala msipelelezane, wala msisengenyane nyinyi kwa nyinyi. Je! Yupo katika nyinyi anaye penda kuila nyama ya nduguye aliye kufa? Mnalichukia hilo! Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, Mwenye kurehemu” (al-Hujurat, 12).

Wanadamu bora ambao wameweza kufuata mwenendo huu wameweza kuwa mashujaa wa wema na maadili, na kamwe hawakuikumbatia dunia na kuiacha akhera. Mfano mmoja wapo unatoka kwa Sheikh Edebali ambaye alikuwa Sultani wa imani na kiongozi wa kiroho wa Othman Gazi, aliyekuwa mmoja wa makamanda maarufu walioitengeneza historia. Ushauri wenye maana kubwa alioutoa Sheikh na kumpa Othman Gazi ni wenye thamani kubwa kwa viongozi wote kuanzia ngazi za juu mpaka za chini, na juu ya wote ni watu wa familia namna wanavyoishi wao kwa wao:

*“Mwanangu...Wewe ni mtemi! Kuanzia leo hasira iko juu yetu, upole uko juu yenu. Chuki iko juu yetu, mapatano yapo juu yenu. Kushitakiwa kuko juu yetu, ustahamilifu uko juu yenu. Udhalili na kasoro viko juu yetu, uvumilivu uko juu yenu. Utesu, migongano na kutokupatana vyote viko juu yetu, haki iko juu yenu. Mitazamo na maneno mabaya na hukumu zisizo za uadilifu vyote viko juu yetu, lakini msamaha uko juu yenu.*

*Kuanzia sasa ewe mwanangu, kugawanyika kuko juu yetu, kuungana kuko juu yenu. Uvivu uko juu yetu, tahadhari, ujasiri na umadhubuti vyote viko juu yenu...”*

Ushauri huu wa kipee ni ubainifu mkubwa wa utajiri wa moyo na utukufu wa wema ambao unaweza kumfanya mtu asamehe kiurahisi ubaya aliotendewa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na bila kujali mazingira yaliyopo kuwaendea waja wa Mwenyezi Mungu kwa huruma, upendo na huba.

Hata pale ilipotokea kwamba kuna mtu aliyetenda uovu, ili kuepusha kumdhalilisha Mtume aliyebarikiwa – kamwe hakuwa akimnyooshea mtu kidole mbele ya watu, badala yake alikuwa akimficha kwa kulitahadharisha kundi zima juu ya kosa lililotendeka, ilifikia akawa anaenda mbali zaidi kwa kujionyeshea kosa mwenyewe kwa kusema:





“Nina nini mimi kiasi kwamba ninawaona kama hivi?” (Bukhari, Manaqib, 25; Muslim, Salat, 119).

Hii ni njia bora ya kumlinda mkosaji dhidi ya aibu na udhalili, jambo ambalo ni la kawaida kwa wale wote wenye kuelewa na kuishi maisha kisufi kwa namna iliyo bora zaidi. Njia ya kuelekea kwa Mola haipitii kwenye nyoyo zilizoangamia bali nyoyo zilizotengemaa, kama anavyoelezea Yunus Emre:

*Moyo ni kiti cha enzi cha Mungu,  
Kwenye moyo Mungu anang'aa,  
Hapa duniani na akhera atahuzunika,  
Yule mwenye kuungamiza moyo...*

Kwa uthibitisho ni kwamba watu wengi waliokuwa wamekatajiwa na kulaumiwa na kutengwa kutokana na kasoro zao kwa sasa wamerudishwa kwenye ardhi za huruma kwa msaada wa njia hii tukufu.



*Imesimuliwa kwamba siku moja mwanafunzi wa Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikamatwa katika tukio baya. Kutokana na kusikia aibu mwanafunzi yule aliondoka pale chuoni na hakurejea tena. Wakati fulani wakati akiwa anapita sokoni huku akiwa na wanafunzi wake wengine alimuona mwanafunzi yule aliyekuwa amekimbia. Pindi mwanafunzi yule alipotambua uwepo wa mwalimu wake ndani ya soko aliondoka kutokana na kusikia aibu kuonana naye. Lakini jambo hili halikujificha kwa Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, hivyo akawageukia wanafunzi wake na kuwaambia:*

*‘Nyie nendeni; ndege ametoroka kutoka kwenye kiota cha moyo wangu!’ Kisha akaanza kumfuata yule mwanafunzi. Baada ya muda yule mwanafunzi alipoangalia nyuma yake aligundua kuwa anafuatwa na mwalimu wake. Kutokana na kutaka kumpoteza mwalimu wake aliamua kuelekea kwenye barabara iliyokuwa na mwisho, alipofika mwisho alikutana na ukuta na kujigonga kichwa chake ukutani kwa bahati mbaya na kuanguka chini. Pindi alipotazama juu alimuona mwalimu wake amesimama. Kutokana na kujisikia aibu aliangalia chini.*





*Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alimuuliza kwa maneno laini kabisa. “Hiki ni kipindi kigumu ambacho mwalimu hana budi kuonyesha thamani yake kwa kumsaidia mwanafunzi wake” Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alimsaidia kwa upole mwanafunzi wake anyanyuke na kisha akamchukua na kumrudisha chuoni. Kisha mwanafunzi yule aliyekuwa na majuto makubwa alitubia na kurejea kwenye hali yake kama ya zamani.*

Hii ni ishara ya matunda yanayotokana na ukomavu wa kumuendea mtu mwingine bila ya kujali uzito wa madhambi yake, kama ambavyo baba angelimuendea mwanae.

Na hatua zaidi ya hii ya kuwasamehe wengine madhambi yao ni kujibu ubaya kwa wema, na hata kumuomba yule aliyekudhuru atengenezewe imani yake; na hii haina budi kuwa ndiyo sifa yenye kumtambulisha muislamu aliyekomaa kiimani. Mfano tosha juu ya hili ni pale Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipowaomba uongofu wale waliompiga mawe kule Taif. Na ombi lake kwamba watu wa Makka wasamehewe kuadhibiwa kutokana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu na badala yake wapate uongofu wa uislamu lilikuwa ni sababu kubwa ya uongofu wa madhalimu wengi.

*Hadith* inasema: “Si vyema kurudisha wema kwa wema, uovu kwa uovu. Ubora upo katika kurudisha uovu si kwa uovu bali kwa wema” (Tirmidhi, Birr, 63).

Kama mtu aliyerudishiwa wema alikuwa ni adui basi atakuwa rafiki. Kama alikuwa kati kati basi atasogea karibu zaidi; na kama alikuwa karibu na wewe basi mapenzi juu yako yataongezeka zaidi. Hii ndiyo sababu kuu inayopelekea watu wa ulimwengu wa leo ambao wamekamatwa na uyakiniifu wanatafuta kutuliza nyoyo zao kwa wanavutika na namna yenye kustaajabisha katika kuitazama dunia. Kwa namna hii kunakuwa na faida kubwa kutumia mtindo wa *tasawwuf* katika kuutambulisha na kuusambaza uislamu. Watu wengi wa magharibi ambao wameingia kwenye uislamu wamegeukia kwenye kazi za sufi wakubwa kama vile Ibn Arabi na Mawlana Rumi kwa ajili ya kuzijaza nyoyo zao zilizo tupu. Vitabu vinavyoongoza katika orodha ya vitabu vya kiislamu ambavyo vinahitajika mno katika upande wa dunia wa magharibi ni vitabu vya *tasawwuf*. Hivyo katika nyakati zetu hizi tupu katika hitajio kubwa la kuimarisha nyoyo zetu,





maneno yafuatayo kutoka kwa Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – yanawaenea wanadamu wote:

*Njoo! Njoo! Na bado njoo, popote ulipo...  
Ikiwa unaabudia moto, mshirikina au hata kama huamini chochote,  
Nyumba yetu si ile ya kukatisha tamaa, hivyo njoo, hata kama  
Ulitubia mara mia moja kwa ajili tu ya kuvunja ahadi...*

Mualiko huu mzuri wa Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – umetokana na lengo lake la kumtambulisha mwanadamu kwenye maumbile yake, na kwa upande wa upendo na uvumilivu kumuokoa dhidi ya kasoro zake na kumfanya apende uislamu. Kinyume chake hili si tamko la bure la kumkubali mtu ambaye hataki kuachana na maisha yake yaliyojawa na uovu. Lengo ni kujenga upya imani zao. Hata hivyo ikiwa kifaa cha mtu kimevunjika huwa anakipeleka kikakarabatiwe. Watu wema kama vile Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ni kama maduka ya kukarabati vifaa hivyo. Kwa kuwa kazi kubwa hapo ni kukarabati kile kilichovunjika; ni wazi kwamba huo mualiko hapo juu hauna budi kuwafikia watu wenye kasoro..



Katika kipindi ambacho maisha ya kidini yamebakia ngozi na mifupa na wakati ambao watu wanafanya makosa mengi pindi wanapohukumiwa kwa misingi ya dini, inakuwa hakuna budi kugeukia utaratibu mwingine ulio na mtindo wa kisufi wa ukarimu, huruma na upole. Utaratibu huu ndio njia bora na wenye matunda katika kuongeza nguvu ya kuwakarabati wale waliozama katika madhambi na uasi.

Lakini hatuna budi kusema kwamba kumvumilia muovo kunategemeana na mtu binafsi. Vinginevyo kuwavumilia waovu na maovu ambayo yanasababisha uvunjifu wa haki za wengine na kuleta uharibifu katika jamii na hivyo kuondoa utulivu katika jamii ni jambo lililokubalika. Kwa kuongezea ni kwamba bila shaka si vibaya kwa mtu anayeishi maisha yanayozingatia mipaka ya uislamu kumtazama muovu kwa hisia za ‘hasira’. Kwani ni muhimu kukaa mbali na muovu ili moyo wake usije ukaingia kwenye hatari itokanayo na kufanya naye urafiki. Kwa watu wanaoishi bila ya kujitambua, dhambi kwao zinakuwa ni jambo lenye kuwavutia na





watu wengi miongoni mwao huangukia kwenye madhambi taratibu bila ya kuhisi kwamba wamefanya ubaya wowote. Kwa hiyo kuvumilia ovu la muovu ni hatari kwa watu wengi, kwani kunaweza kuwapelekea kuyachukulia maamrisha matakatifu kwa wepesi na hata kupelekea nyoyo zao kugemea kwenye maovu. Hivyo kumvumilia muovu kusihamishiwe kwenye ovu lenyewe; na uadui na maovu usihamishiwe kwa muovu.

Maneno yetu ya mwisho katika suala hili yatakuwa ni *hadith* ifuatayo:

“Rahisisha, usifanye jambo kuwa gumu. Fariji, usisababisha karaha” (Bukhari, Ilm, 11).

Bila shaka yote haya ni ili usije ukadhuru kiini cha uislamu na usije ukatoka nje ya njia ya haki...

Ewe Mola! Tujaalie tuwe miongoni mwa watu wenye mapenzi ya kweli ambao nyoyo zao zimejawa hekima na utujaalie tuzifahamu siri za hapa duniani na kesho akhera! Jaalia nyoyo zetu ziwe vyanzo vya huruma, upole na uvumilivu kwa viumbe kwa ajili ya Muumba!

Ewe Mola! Kutokana na fumbo ‘Huruma yangu imezidi ghadhabu zangu’, tuongoze katika njia ya kusamehe na utufanywe tuwe miongoni mwa waja wako wema ambao ndio viongozi wa haki!

Amin









---

# SURA YA TATU

---




*Marifatullah*  
*na*  
*Malipo Matakatifu*

**A- MARIFATULLAH AU KUMFAHAMU ALLAH**

- 1- Dhati takatifu
- 2- Sifa takatifu na ubainifu wake
- 3- Kumfahamu Mwenyezi Mungu na ubainifu wake kwa wenye hekima

**B- MALIPO MATAKATIFU**

- 1- Ufahamu wa Ladunn
  - 2- Firasah au Utambuzi wa kiroho
  - 3- Mamlaka ya kiroho na Karamah
  - 4- Ndoto za ukweli
- 



*"he who knows his self knows his Lord."*



# Marifatullah na Malipo matakatifu

*U*bainifu ni wa Mola ambaye haonekani  
kutokana na uzito wa dalili zake.



## A. MARIFATULLAH AU KUMFAHAMU ALLAH

### 1. DHATI TAKATIFU

Ugumu wa kufahamu asili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu umewekwa wazi na maneno yafuatayo ya Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake: “Tafakarini juu ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Msitafakari juu ya dhati yake, kwani kamwe hamtoweza kupata cha kumfananisha naye” (Daylami, Musnad, II, 56; Haythami, Majmau’z-Zawaid, -1,81).

Hata hivyo elimu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ambayo italeta uelewa kwenye ardhi ya imani na busara na kuiwezesha kuungana na nuru ya uongofu haitokani na dhati yake bali inatokana na sifa zake. Hii inatokana na ukweli kwamba Mola amevuka mipaka ya nafasi na muda. Kwa upande mwingine uelewa wa mwanadamu umejikita katika milango ya fahamu. Hivyo ili mwanadamu aweze kukielewa kitu basi kitu hicho hakina budi kufanana na kitu kingine cha hapa duniani na kitu hicho lazima kiweze kutambuliwa na akili. Kinyume chake Mwenyezi Mungu Mtukufu ana sifa ya ‘kutofanana na kitu chochote kilichoumbwa (*mukhalafatun Wl-hawadith*)’. Hii inamaanisha kwamba Mwenyezi Mungu hawezi kufanana na chochote kile kilichoumbwa na Yeye huko tofauti kabisa, ni Mbora na Mkamilifu ukimlinganisha na viumbe vyake. Kukubaliana na utukufu wake katika ulimwengu mzima kunatosha kuleta uelewa wa kimantiki katika suala hili. Litakuwa ni jambo la kushangaza kumlinganisha Muumba Mtukufu ambaye ndiye mwenye uwezo wa kuumba ulimwengu huu wenye kupendeza, kwa kitu alichokiumba. Ukamilifu, Utukufu na Nguvu





zake ziko juu ya vitu vyote vilivyoubwa, jambo lenye kukubaliana na akili na mantiki. Kwa hiyo haiwezekani wala si sawa kwa akili ya kibinadamu kutoa maoni kuhusiana na asili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa sababu hafanani na chochote kile.

Tunachohitajika sisi juu ya Mola ni kutambua na kukubali uwepo wake kwa kupitia sifa zake. Mfananisho na ufafanuzi alioutoa Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur'an kuhusiana na Yeye mwenyewe vinatosheleza lengo hili. Aya inatubainishia:

“Mwenyezi Mungu ni Nuru ya Mbingu na Ardhi. Mfano wa Nuru yake ni kama shubaka lenye kuwekwa ndani yake taa. Taa ile imo katika tungi. Tungi lile ni kama nyota inayo meremeta, inayo washwa kwa mafuta yanayo toka katika mti ulio barikiwa, mzaituni. Si wa mashariki wala magharibi. Yanakaribia mafuta yake kung'aa wenyewe ingawa moto haujayagusa - Nuru juu ya Nuru. Mwenyezi Mungu humwongoa kwenye Nuru yake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu huwapigia watu mifano. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua kila kitu” (an-Nur, 35).

Tunaweza kugundua kwamba mfanano uliotolewa katika Qur'an kwanza kabisa unalinganisha uelewa wa mwanadamu na vitu anavyoweza kuvilinganisha; na baada ya kuchukua uelewa huo kisha unaendelea kwenda juu zaidi na kupita mipaka ya utambuzi wa kibinadamu, hii inafahamika kama 'nuru juu ya nuru'. Mtu anaweza kupata maana tofauti lakini ukweli ni kwamba nuru yake haiwezi kuzidiwa na aina fulani au aina nyingi za nuru; kinyume chake nuru ya Mola haiwezi kuelezewa kwa urahisi kwani ni nuru ambayo inafuta jitihada zote za kuweza kuilewa; hata hivyo ili kuona kitu chochote kile mwanga unahitajika, si kila mtu anaweza kuona uhalisia wa Mola, kutambua dalili zake na uwezo wake. Juu ya yote hayo ni kwamba kipofu amenyimwa kuona vitu vinavyoonekana kwa msaada wa mwanga kinyume na wale waliojaaliwa kuona. Hivyo namna jicho lenye kuona lilivyo sharti kubwa la kuona ndivyo ilivyo pia kwa mwanga ambao ndio wenye kusaidia kuona. Mtu aliyejaaliwa jicho lenye kuona ndiye pekee mwenye kuweza kulitambua na kulithamini hili.

Kwa upande mwingine, pale Mwenyezi Mungu Mtukufu anaposema katika aya kwamba Yeye ni 'Nuru' na kujitangaza kama 'Nuru ya mbingu na ardhi', anamaanisha kwamba Yeye pekee ndiye aliyeumba viumbe vyote, na kisha akajaalia kuonekana kwa viumbe vingi hapa ulimwenguni,





na ndiye aliyevileta vitu mbalimbali, vinavyoonekana na vilivyojificha na kuleta furaha kwenye nyoyo. Kama isingelikuwa Nuru kuu ya Mola kusingelijulikana wala kupatikana kitu chochote; na furaha isingeliweza kupata njia ya kuingia kwenye nyoyo.

Vitu vyote vyenye kutoa mwanga asili yake ni Nuru hiyo kubwa. Ukilinganisha viwango mbalimbali vya nuru ya vitu vilivyopo mbinguni, ndivyo ilivyo kwa nuru zinazodhihirika hapa ardhini. Kwa mfano kama miale ya mwanga wa jua itagonga kwenye mwezi na mwezi nao ukaipeleka miale hiyo kwenye kioo kilichopo ndani ya nyumba hapa ardhini, na kisha kioo hicho kikaakisi miale hiyo kwenye bakuli lililojaa maji na mwishowe kurudi kwenye dari, daraja la kwanza la miale yenye uzito mkubwa ni ile kutoka kwenye jua kisha inafuatia ile iliyotoka kwenye mwezi na kuendelea. Ukiiangalia miale yote hii utagundua kuwa ile iliyopo karibu na chanzo ina uzito mkubwa zaidi ya ile inayofuatia. Pia nuru za mbinguni zina madaraja kama hayo; yani nuru inayotoka kwenye chanzo ina nguvu zaidi ya ile itokayo kwenye kitu kinachoakisi mwanga wake. Na hatimae utofauti huu katika uzito unafikia kikomo kwenye nuru yenye kuzipita zote, hii ni nuru ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Hivyo kuonekana kwa vitu vyote na kuvifahamu kwake kunatokana na Mola ambaye ndiye muangazaji wa mbingu na ardhi, na ambaye anavifanya vitu vyote vionekane na kufahamika. Bila ya nuru yake haitoweze kana kuonekana na kufahamika kwa chochote kile. Kwa mfano pindi utakapoangalia msitu ulio mbali na wewe wakati wa majira ya kuchipua, unaweza kusema, “Sikuona chochote zaidi ya ukijani!” licha kuona rangi mbalimbali zilizokolea. Unakuwa umetekwa na kijani chenye kuvutia kinachotokana na kipindi cha majira ya kuchipua, kiasi kwamba huwezi kuiona nuru iliyosababisha kijani hicho. Ni jambo la kushukuru kwamba kutokana na mwanga ndipo tunapoweza kuona rangi mbalimbali. Kwa namna hii mwanga huendelea kujificha bila kuonekana na macho yetu kutokana na ukali wake katika kuangaza.

Katika suala hili Sufi wanasema:

“Ukweli ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hajajificha. Lakini kwa kuzingatia uwezo wetu wa kutambua mambo Amejificha kwa sababu ya ugumu wa sisi kuweza kumuona”.

Aziz Mahmud Hudayi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:





*Ubainifu wake unafunika bayana,  
Je mtu ataweza kumuona kwa sababu ya mwanga?*

Kwa mfano, mtu hawezi kuona vitu vilivyo ndani ya chumba kili-chowashwa balbu yenye volti elfu tano. Kwa hiyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye anang'aa kuliko hata mwanga wa mamilioni ya volti bila shaka hawezi kuonekana na mwanadamu wa kawaida. Qur'an inalilisitiza suala hili pale inapowaongelea waumini kwa kusema:

“Ambao huyaamini ya ghaibu...” (al-Baqara, 3).

Lakini kwa mtu aliye makini kutoonekana huku kwake kunakuwa kunaonekana zaidi kuliko hata vile vitu vinavyooneka kwa uwazi kabisa. Kiasi kwamba: Tunaishi na hewa lakini hatuwezi kuiona licha ya kwamba kiuhalisia imetuzunguka. Tunaweza tu kuihisi pale tunapoivuta na kuitoa. Licha ya kushindwa kupinga kwamba kuna hewa licha ya kushindwa kuiona tumeenda mbali zaidi kiasi cha kusema: “Hatuwezi kuishi bila ya hewa!”

Vile vile viumbe wa baharini ni kama sisi. Kuna uwezekano hawahi-hisi mno bahari licha ya kuishi ndani yake. Lakini tofauti na bahari ni kipi kingine kinachowazunguka?

Haya yanamaanisha kwamba popote pale kilipo kiumbe tunaweza kukiona, ikiwa ni kuliani mwetu ama kushotoni mwetu, nyuma yetu ama mbele yetu. Lakini pale kinapotuenea huwa kinaweka kivuli kwenye mipaka yote ya uelekeo na ubainifu wa uwepo wake huvuka utambuzi wetu na hivyo kupelekea kutoonekana. Kama ingelikuwa ni kinyume chake, kwa mfano hewa ikawa haijajificha kwenye macho yetu maisha yangelikuwa hayawezekani; ingelikuwa ni kama ukungu mzito ulioziba macho ya kila mtu. Hiyo ndiyo sababu iliyompelekea Mola kutoweza kuonekana na macho yetu hapa duniani. Kama ingelikuwa aonekane, kutokana na uzuri wake (jamal) ambao ungelikuwa umewavutia wanadamu wote, wangelishindwa kuona kitu chochote isipokuwa Yeye. Na kusingelikuwa na kitu kinachoitwa maisha ya dunia ambayo lengo lake ni kuwajaribu wanadamu.

Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye amevuka mipaka ya utambuzi wetu amefichikana kwetu na pia anaonekana, au amejichikana katika dhati lakini anaonekana katika ubainifu wake.





Anaonekana na viumbe kwa kupitia nuru ya dhati yake.

Amefichikana kwao; kwani macho hayana uwezo wa kumuangalia.

Yeye anaonekana. Vyote vingine hubainika kwa kupitia sifa zake.

Yeye amefichikana, kwani hakuna mwingine kama Yeye. Akili ya mwanadamu imeumbwa kwa namna ambayo huviona vitu kinyume chake. Hivyo ni jambo la kawaida kwa Mola ambaye habadiliki na ambaye hana anayefanana naye akawa amejificha.

Kwa hakika hakuna kiumbe chochote hapa ulimwenguni chenye uwezo wa kutosha wa kuweza kumuangalia Mola. Ndio maana kutokana na sababu hii imani inahusiana na kukubali dhati yake na si kuona uhalisia wake; kwa kuwepo au kutokuwepo ni jambo moja, na kupitisha maamuzi juu ya asili yake ni jambo jingine.

Mola amemjaalia mwanadamu uwezo wa kufikiria, kutambua na kufahamu utukufu wake. Pia ameifanya dunia iweze kudhihirisha ubainifu wake ili akili iweze kupata mazingatia kutokana na athari zake. Tukio lifuatalo linalifafanua jambo hili vizuri zaidi:

*Sufi mkubwa aitwae Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – siku moja aliliona kundi kubwa la watu likielekea mahali kwa furaha na shauku.*

*“Mnaenda wapi?” aliwauliza.*

*“Mwanachuoni amewasili kutoka sehemu fulani. Huwa yeye anaelezea uwepo wa Mwenyezi Mungu kwa kutumia ushahidi mwingi. Tunaenda kuchukua ushahidi na maelezo yake. Ungana na sisi kama unataka!” walijibu.*

*Kisha Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akawaangalia kwa tabasamu jepesi na kusema:*

*“Katika ulimwengu huu kuna ushahidi mwingi mno wenye kumuelezea Mola kwa macho yenye kuona, masikio yenye kusikia na nyoyo zenye kuhisi. Zaidi ya hayo ni kwamba kuna uthibitisho mwingi alioutoa Mwenyezi Mungu Yeye mwenyewe. Kwa hiyo enyi watu...Yeyote ambaye bado ana wasiwasi na aende! Kwani kwa upande wetu hakuna hata chembe ya shaka ndani ya nyoyo zetu”*





Mwenyezi Mungu amembainishia mwanadamu siza zake nyingi mno, kwani mwanadamu ndiye kiini cha ulimwengu, katika ulimwengu yeye ni Qur'an iliyonyamaza, na ndani ya Qur'an yeye ni ulimwengu wenye kuongea. Katika kurahisisha zaidi mambo Ametuma Mitume wengi kwa ajili ya kuwaongoza na kuwasaidia wanadamu katika kutambua ubainifu wa sifa zake na kupata manufaa ndani yake. Na kwa kupitia Mitume Mwenyezi Mungu amemfunilia mwanadamu uhalisia wa ulimwengu unaoonekana na usioonekana katika namna iliyo bora mno; kwa namna ya 'hotuba', kama ilivyoelezewa ndani ya Qur'an tukufu.

Hivyo kuhusiana na dhati ya Mwenyezi Mungu hatuna budi kuzingatia yafuatayo kadiri inapoishia mipaka ya maneno yetu:

Mola Mkamilifu hawezi kuzuiwa na mpaka wowote ule; Hawezi kusifiwa na chochote kile nje ya kile alichojisifia Yeye mwenyewe. Kumuita 'Mkamilifu' ni kama vile kumuwekea kikomo, lakini kulingana upeo wetu wa uelewa na kwa ajili ya kufafanua hatuna budi kulitumia neno. Lakini ukweli ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu yuko tofauti na kitu chochote kile na jambo lolote linaloweza kuja akilini, hata kama ni neno lenye ufasaha kiasi gani.

Kutokana na dhati yake Mola mwenye utukufu usio na mipaka amekuwa akibainisha sifa Zake; kama ambavyo mshumaa unawaka na kutoa mwangaza. Viumbe vyote viko kwenye elimu ya Mola Mkamilifu, elimu ambayo ulimwengu ndio ubainifu wake. Viumbe katika ulimwengu huu ambao unaitwa ulimwengu wa ushuhuda (*shahadah*) vipo katika ushirikiano; hakuna kiumbe chochote kinachoweza kuishi chenyewe. Vina-chukuliwa kuwa vipo hapa duniani kama vipokezi vya sifa, kazi, qadari, nguvu na ustadi wa Mola Mkamilifu. Ingawa dhati ya Mola inabainisha nguvu Zake, hekima Yake, ulinzi Wake na Silka yake katika kila kiumbe lakini ulimwengu huu si ubainifu kamili wa dhati Yake. Kwa maneno mengine ni kwamba ulimwengu huu ni ubainifu wa sifa za Mola na si dhati Yake.

Hivyo dhati yake ina utukufu ulio juu ya kila kitu. Kama jua lingelikuwa halipo na miale yake pia isingelikuwepo. Hivyo ingawa miale haipo yenyewe bila ya jua lakini yenyewe si jua. Hata hivyo hatuna budi kuzingatia kwamba kukitambua kila kitu kuwa ni Yeye kunaweza kuwa sawa na kukubali kuwa ulimwengu na kila kilichopo ni mungu, jambo







ambalo linapelekea kwenye uyaikinifu ambao utapunguza ‘Mmoja’ na kuwa ‘Vyote’. Imani kwamba Mungu yupo katika kila kitu, imani iliyohusishwa na Plato inatokana na kutokuelewa kwake mambo. Ingawa baadhi ya watu wamejaribu kuingiza *Wahdat-i Wujud* ndani ya mfumo huu na kuutambua lakini Sufi wa kweli wamesimamia katika kulikataa hili na kuliita kwamba ni upotofu. Kwani ingawa kila kitu kimekuwepo kwa sababu Yake lakini mafundisho sahihi ya *Wahdat-i Wujud*<sup>1</sup> yanahusiana na kuitukuza dhati yake na kuitoa katika kitu kingine chochote. Ni kweli kwamba ulimwengu ni wenye kupokea sifa za Mola lakini Dhati yake si ulimwengu; kwani Muumba kamwe hawezi kujibainisha katika umbile la kiumbe chake. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *mukhalafatun lil’hawadith*, yani hafanani na kiumbe chochote kiumbile wala kitabia, hivyo kukubali kinyume na haya ni upotofu wa wazi kabisa (*kufur*). Hivyo Mola ana utukufu ambao hauwezi kufananishwa na sifa za kibinadamu ambazo watu wengi wanaweza kumhusisha nazo. Inafahamika vyema kuwa kutokana na wayahudi na wakiristo kuweka pembeni ukweli huu walifikia kutengeneza ‘Mwana wa Mungu’, wayahudi wakimuita hivyo Uzayr (Ezra) – Amani iwe juu yake – na wakiristo wakimuita hivyo Issa (Yesu) – amani iwe juu yake. Majibu matakatiifu juu ya upotofu huu ambao akili ya mwanadamu imejaribu kuutengeneza ndani ya dunia hii yametolewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ifuatavyo:

“Na wala hawakumheshimu Mwenyezi Mungu kama anavyo stahiki kadiri yake. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa mkononi mwake, na mbingu zitakunjwa katika mkono wake wa kuume. Subhanahu wa Taa’la Ametakasika na Ametukuka na hayo wanayo mshirikisha nayo” (az-Zumar, 67).

1. *Wahdat-i Wujud* ni utaratibu wa kisufi uliowekwa na Muhyiddin Ibn Arabi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Pia kuna utaratibu mwingine unaoitwa *Wahdat-i Shuhud* unaotoka kwa Imam Rabbani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, ambaye alisifika kwa jina la Mujaddid Alf-i Thani, yani mrudishaji wa milenia ya pili. Ukweli ni kwamba taratibu zote mbili ni ufafanuzi wa jambo moja katika mitazamo miwili tofauti; zote zinalenga kupata tofauti kati ya sifa tukufu na uungu na uelewa wetu katika ufahamu wa kidunia. Baada ya kusema hayo ni kwamba kuna tofauti moja muhimu kati ya vitu hivyo viwili. *Wahdat-i Wujud* ni kuhisi upweke mtakatifu (*tawhid*), *Wahdat-i Shuhud* ni kushuhudia ubainifu wa upweke huo. Kwa kuwa fikra zote mbili kimsingi zinahusiana na *hal* au msukumo wa kiroho, hatupaswi kuzichanganya na fikra za kifalsafa au kuchafuliwa nazo.





Kwa sababu hiyo ndio maana neno *Tawhid* ambayo ndio msingi wa itikadi ya kiislamu kwanza kabisa linatumika kufuta moyoni imani zote potofu juu ya miungu ya uongo kwa maneno ‘Hakuna mungu apasae kuabudiwa kwa haki...’ (*la ilaha*) na jambo la pili ni kuingiza moyoni imani ya kweli juu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa maneno ‘isipokuwa Mwenyezi Mungu’ (*il-Mwenyezi Mungu*). Qur’an tukufu ipo wazi kabisa juu ya hili:

“Mwenyezi Mungu - hapana mungu ila Yeye Aliye hai, Msimamia mambo yote milele. Hashikwi na usingizi wala kulala. Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani. Ni nani huyo awezaye kuombea mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao; wala wao hawajui chochote katika vilio katika ujuzi wake, ila kwa atakalo mwenyewe. Enzi yake imetanda mbinguni na duniani; na wala haemewi na kuvilinda hivyo. Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu” (al-Baqara, 255).

“...Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona” (as-Shura, 11).

“Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mku-sudiwa. Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anaye fanana naye hata mmoja” (al-ikhlas, 1-4).

Kwa ufupi ni kwamba tunachohitajika kuhusiana na dhati ya Mola ni kumfahamu na kujisalimisha kwake kulingana na utambuzi wetu hapa duniani. Hata kama mtu atakuwa na uwezo wa akili mkubwa kiasi gani ndani ya dunia hii yenye kupita hatoweza kamwe kuijua vilivyo dhati ya Mola...hatoweza kabisa.

Kama ilivyodokezwa ndani ya Qur’an pale Musa – amani iwe juu yake – alipoongea na Mwenyezi Mungu Mtukufu na kupata utambuzi mkubwa wa kiroho. Licha ya ubainifu mtakatifu aliokuwa amejaaliwa lakini alishindwa kuzuia hisia zake. Huku akiwa amejisahau kuwa ama yupo ardhini bado au amevuka mipaka ya nafasi na nyakati. Mara akawa na shauku kubwa ya ndani ya moyo wake ya kuona dhati ya Mola, aka-muomba Mwenyezi Mungu ampatie fursa hiyo. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu akamjibu:





iwe juu yake – atazame mlima. Mwenyezi Mungu akasema kama mlima utaweza kuhimili ubainifu huu basi na yeye ataweza kumuona. Kisha muale kutoka nyuma ya mapazia yasiyo na idadi, kama ilivyopokewa, ukaakisiwa kwenye mlima. Pale pale mlima ukaporomoka na Musa – amani iwe juu yake – akazimia kutokana na hofu. Alipopata fahamu akamtukuza na kumuomba msamaha Mola kutokana na kuvuka kwake mipaka.<sup>2</sup>

Uhalisia huu wa Qur'an unathibitisha udhaifu alio nao mwanadamu juu ya kuweza kuihimili dhati takatifu.

Baada ya kuyasema hayo kuna maneno mengi ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ambayo yanaashiria kwamba katika siku ya kiama waumini watamuona Mola wao kwa uwazi kama wanavyoweza kuuona mwezi ndani ya usiku usio na mawingu. Hakuna mgongana kati ya hili na ambayo tumekwishayasema, kwani mazingira ya hii dunia ni tofauti kabisa na yale ya kesho akhera. Hivyo waislamu watapewa uwezo wa kipekee wa kuona dhati ya Mola. Ndio maana Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – hakuachwa na hali ya kidunia na badala yake akapitia kwenye upasuaji wa kiroho uliofanywa na Jibril – amani iwe juu yake – kwa kupasua kifua chake ili aingiziwe uwezo ambao ungelimuwezesha kuhimili majukumu makubwa ya utume yaliyokuwa mbele yake. Vinginevyo nguvu zake za kawaida za kibinadamu zisingetosha kwa ajili ya jukumu hilo kubwa au ubainifu mkubwa wa safari ya *Miraj* (Kupanda mbinguni).

Hivyo wale wenye kuweza kuhama kutoka kwenye *iman* mpaka kwenye *ihsan*, yani kutoka kwenye imani mpaka kwenye kuikita moja kwa moja ndani ya moyo, ndio wenye kuweza kufikia kwenye ukweli na hekima chini ya nuru ya Mola. Waja hao hupendwa ndani ya hii dunia. Na kwa hakika hawa ndio wanadamu waliokamilika (*insan-i kamil*). Wakati wote huwa na shauku ya kuitafuta akhera kwa ajili ya kukutana na Mola wao. Kwao kushushwa katika dunia hii yenye vikwazo mbalimbali na yenye kupita wanaona ni kana kwamba wapo uhamishoni. Ndani ya dunia hii wanautumia umri wao huku wakitambua kuwa wapo hapa duniani kwa ajili ya Mola na hivyo hujisalimisha moja kwa moja kwa Mola wao.

<sup>2</sup> Rejea al-Araf. 143





Tunamuomba Mola atujaalie imani thabiti katika haki! Atupambie bustani zetu za imani kwa chipukizi za matendo mema pamoja na radhi zake! Atujaalie tuwe majirani wa Mjumbe wake kipenzi kesho akhera na atujaalie heshima ya kuja kuona uzuri wa dhati yake!

Amin...





**Y**ule mwenye kutazama kwa kupitia nuru ya Mola ni sawa na kuiona akhera kwenye kijiti, na bahari nzima ndani ya tone moja. (Mawlana Rumi)



## 2. SIFA TAKATIFU NA UBAINIFU WAKE

Dhati ya Mola ni moja, wakati sifa zake ni nyingi mno. Sifa zake hazina idadi maalum, hazina mwisho. Idadi yake kamili anaijua Yeye pekee. Baadhi yake zilifunuliwa kwa Mitume pekee. Nyingine kama vile Majina tisini na tisa yamenuliwa kwa wanadamu wote. Kwa upande mwingine wanachuoni wamejaaliwa kufahamu sifa takatifu ambazo hazipo kwenye hayo ‘tisini na tisa’.

Sifa zote tukufu zinazofahamika na zisizofahamika zina lengo la msingi ambalo ni kufikisha ujumbe kwamba Muumba pekee wa ulimwengu huu hana sifa zenye kasoro na Yeye ni Mtukufu mno, na amepambwa na sifa zenye ukamilifu pekee. Hivyo haiwezekani kwa sifa yoyote ya Mwenyezi Mungu Mtukufu iliyowekwa chini ya vichwa vya habari ulazima (*Dhati*) na usawa (*Thubuti*) zikawa na kasoro au upungufu wowote.

Kiasi kwamba:

Ukamilifu wa uwepo wake ni kwa Yeye kuwa hai; uhai wenye kudu-mu na uliokamilika. Sifa ya Mola ya uhai (al- Haya) si ile yenye mauti kama kinyume chake; bali ni uhai unaomuhusu Yeye peke yake. Qur’an inalielezea hili kama ifuatavyo:

“Na mtegemee Aliye Hai, ambaye hafi. Na umtukuze kwa sifa zake. Na yatosha kwake kuwa yeye ni Mwenye khabari za dhambi za waja wake” (al-Furqan, 58).

Kwa hakika Ujuzi wake (*al-Ilm*) si zao la fikra wala dhana. Kitu chenye kuthibitisha ujuzi wa Mwenyezi Mungu usio na mipaka ni mpangilio na muundo ulioenea kwenye ulimwengu mzima, mpangilio ambao hauwezi kuingiliwa na nguvu wala fikra nyingine yoyote. Kwani hata ugunduzi mdogo mno wa mwanadamu hapa duniani unahitaji ushirikiano wa





akili mbalimbali na kutumia karne kadhaa kwa msaada wa maendeleo ya kanuni mbalimbali za kisayansi. Kwa mfano, ni baada tu ya kupita kipindi fulani katika historia kufuatia kuumbwa kwa mwanadamu na kufanya jitihada nyingi ndio ikawezekana leo hii kuwasiliana kwa kupitia simu za mkononi, jambo lilioenea sehemu mbalimbali duniani. Kwa ujumla hayo ni maendeleo ya kisayansi. Ugunduzi na uvumbuzi uliofanyika mpaka sasa na siri nyingi kufunuliwa si chochote bali ni ufunuo kutoka kwa Mola kwa kupitia ujuzi wake juu ya huu ulimwengu.

Tofauti isiyo ni mpaka katika ujuzi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na ufahamu wa viumbe imeelezewa vizuri kama ifuatavyo:

Wakati wa safari yenye kustaajabisha ya Khidhir na Musa – amani iwe juu yao, safari ambayo hekima yake imefichikana kwetu, shorewanda alikuja na kutua kwenye meli yao. Baada ya muda mfupi akadonoa matone kadhaa ya maji ya bahari. Kisha Khidhir – amani iwe juu yake – akamgeukia Musa – amani iwe juu yake – na kumwambia: “Ufahamu wako, wangu na wa viumbe vyote ukiulinganisha na Ujuzi wa Mwenyezi Mungu ni kama kiasi cha maji yaliyodonolewa baharini na huyo ndege” (Bukhari, Tafsir, 18/4).

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anafafanua juu ya hekima iliyopo juu ya sababu iliyompelekea mwanadamu kujaaliwa sifa za elimu, kusikia na kuona:

*“Ili msije mkaacha kuhofia na hivyo mkajiingiza kwenye maovu Mola amewafahamisha kwamba Yeye ni Mjuzi; yani anakijua kila kitu nje ndani.*

*Ili mfunge midomo yenu na kuachana na maongezi mabaya Mola amewafahamisha kwamba Yeye ni mwenye Kusikia; yani anasikia kila kitu vizuri kabisa.*

*Ili msije mkajiingiza katika maovu kwa kujificha au kwa wazi, Mola amewafahamisha kwamba Yeye ni mwenye Kuona; yani anasikia kila kitu kwa uwazi kabisa.”*

Maneno yote yaliyopo hapa duniani si chochote bali ni ubainifu wa sifa takatifu ya maneno (*kalam*). Hivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu si tu anabainisha uwezo usio na kifani wa Maneno yake; bali pia anafanya Jina lake tukufu lisikike katika lugha mbalimbali. Katika Maneno yake Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia kila kiumbe kuwa na lugha inayoendana





nacho, wakiwemo wale wanaodhaniwa kuwa hawana uhai. Qur'an inasema:

“Na mtegemee Aliye Hai, ambaye hafi. Na umtukuze kwa sifa zake. Na yatosha kwake kuwa yeye ni Mwenye khabari za dhambi za waja wake” (al-Isra, 44).

Kwa kuwa *tasbih* zote, yani kumtukuzwa Mola kwa maneno, zinatekelezwa kwa kutumia majina yaliyo bayana, hivyo njia ya wazi ya kumuwezesha mwanadamu kumtambua Mola wake ni kwa kupitia Sifa zake takatifu. Tukizingatia maana zake tutagundua kuwa sifa hizi ni ‘vivumishi’; lakini ukuzielekeza kwa Mola zinakuwa ‘nomino’. Kwa maneno mengine ni kwamba sifa hizi amesifiwa kwazo kiasi kwamba kwake zinakuwa ni Majina. Haya yanaweza kulinganisha na namna watu katika historia walivyoitwa kwa sifa zao au vyeo vyao: *as-Siddiq* kwa Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, *Imam-i Azam* – Abu Hanifa, *Meyyitzade* n.k.

Hivyo ubainifu wa Sifa takatifu pia unaitwa ubainifu wa Majina matakatiifu. Katika suala hili Mwenyezi Mungu Mwenyewe amezitumia Sifa zake kama Majina pale anapotaka atambulike na waja Wake:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

“Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa...” (al-Araf, 180).

Uhalisia ni kwamba mja hujenga mahusiano na Mola wake kwa kupitia jina. Hii inafikia kuonyesha kwamba Jina la Mola ni kipengele cha msingi cha kukanusha kasoro juu Yake. Hivyo mema au mabaya yanayofanywa na mja huelekezwa kwenye Jina lake na si kwenye uhalisia wa Utukufu wake. Hivyo Uhalisia wa Mola unabakia hauna doa.

Kama ingelikuwa si Jina sahihi kwa Mwenyezi Mungu basi mwanadamu angeliona ni vigumu kuishi kama vile atakavyo Mola. Hata hivyo mwanadamu amezoea kumtambua kiumbe kwa jina na kumuelezea kiumbe huyo kwa kupitia jina lake. Kwa mwanadamu jina ndilo usajili wa huyo mtu. Hii ndio sababu iliyopelekea Mwenyezi Mungu baada ya kumuumbwa Adam – amani iwe juu yake – akamfundisha majina ya vitu vyote, kiasi kwamba akawa na ujuzi uliomfanya awe bora kuliko malaika. Kwa maana nyingine, kulifahamu jina la kitu kunapelekea kukifahamu kitu





hicho. Kwa hakika kama isingelikuwa kuyafahamu majina matakatifu ya Mola tungelimfahamu vipi?

Hivyo wakati wote mwanadamu anahitaji majina yenye kutoa sifa za Mola wake. Pindi mtu atakapokuwa katika hali yoyote ile atahitaji jina linaloendana na hali yake kwa ajili ya kumuitia Mola wake. Kama isingelikuwa kwa majina haya uhusiano kati yetu na Mola ungelikuwa dhaifu au usingelikuwepo kabisa. Kunaweza kusemwa kwamba kwa kiasi fulani majina haya ndiyo yenye kumuwezesha mwanadamu kuongea na Mola wake na kumuwezesha kupata funguo za kufungulia milango ya utambuzi wa kibinadamu. Bila shaka kuyataja au kuyakariri majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake kunanawirisha imani ya mtu na kumletea utulivu ndani ya moyo, pia kunamuongezea mapenzi na mazingatio juu ya Mola wake, na pia kumuongezea shauku ya kupata baraka zake na kumuepushia matamano ya dunia yenye kupita na kumchochea kuwa na tamaa ya kukutana na Mola wake. Faida hizi zinathibitishwa na ukweli kwamba maombi na utajo (*dhikr*) tulivyoshauriwa na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – vimetawaliwa na majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Pindi muumini anapojikuta yupo katika hitajio kubwa na hivyo kuhitaji huruma ya Mola hutafuta maneno ambayo yatajumuisha hali yake na kushikamana nayo, kwa mfano hutumia majina matakatifu kama vile Mwingi wa Rehema (*ar-Rahman*) na Mwenye kurehemu (*ar-Rahim*). Na pale ambapo anajikuta yupo katika hali nzito ambayo inaweza kumpelekea kupoteza imani yake kutokana na uzito wa madhambi, hutafuta njia ya kuwa karibu na Mola wake na hivyo kushikamana na Majina Mwingi wa kusamehe (*al-Ghaffar*) na Mwenye kusitiri madhambi (*as-Sattar*). Pindi anapobainikiwa na utukufu katika ulimwengu huu au ndani ya moyo wake hutafuta maneno yasiyopatikana ndani ya vitabu, maneno ambayo yata-paza sauti kwa niaba ya hisia zake na hivyo husema 'Mwenyezi Mungu-u Akbar' kwa ajili ya kutuliza nafsi yake. Kwa ufupi ni kwamba katika hali zake zote za kihisia mja hufungua milango ya nafsi yake iliyofungwa kwa msaada wa majina mbalimbali ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na hivyo kutibu maradhi ya kiroho ambayo anaweza kuyahisi mara kwa mara. Hii ndio sababu iliyopelekea Mwenyezi Mungu akajielezea kwa namna hii ambayo wanadamu wataweza kumuelewa. Kuna sababu kubwa kwa Mwenyezi Mungu kujiita Mjuzi, Mwenye hekima, Mwenye Nguvu, Mwingi wa







kusamehe na kadhalika na watu wakamfahamu kwa majina hayo; kwani wanadamu nao wanaweza kuitwa majina haya ingawa ni kwa kiwango kidogo sana. Na hii inaweza kuwa zawadi takatifu aliyopewa mwanadamu kwa ajili ya uongofu wake.

Hata hivyo ubainifu wa sifa na matendo ya Mwenyezi Mungu si chochote bali ni 'kujishusha kwa ajili ya uelewa wa mwanadamu'. Ubainifu huu unaelezea kile kilichobainika. Lakini ubainifu huu hauendani sawa sawa na Dhati yake; bali umeshushwa hadhi ili sisi tuweze kuuelewa kulingana na uwezo wetu mdogo wa kuelewa. Chini ya kivuli cha ukweli huu yanakuja maneno yafuatayo ya Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake:

“Yule mwenye kutazama kwa kupitia nuru ya Mola ni sawa na kuiona akhera kwenye chembe ndogo mno, na bahari nzima ndani ya tone moja.”

Kutokana na kuuelewa ukweli huu, Ibrahim Gulseni - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anatoa ushairi ufuatao:

*Inakuaje wewe ni bahari katika matone haya?*

*Au jua lenye kung'aa katika alama hizi ndogo mno?*

Jibu la swali hili limejihificha katika maneno yafuatayo ya Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake:

“Hivi mtu ataelewaje kazi za Mola wakati Hekima zake hazina kifani? Nani ataweza kupenya kwenye kiini cha maada? Hata maneno haya niyasemayo ni maneno yaliyotolewa kwa ajili ya ufafanuzi tu.

*Kujiingiza kwenye masuala ya dini ni kutokana na tamaa na shauku. Lakini tamaa hii si kwa ajili ya kukipa mgongo qibla cha ukweli kwa sababu tu fikra zetu haziwezi kukukabiliana nacho. Kinyume chake ni kuzama kwenye vina vya hofu ambayo itapelekea kumpenda Mola.*

*Pindi tunapolala tunapoteza fahamu kutokana na mapenzi yake. Kabla ya kuamka tunapitia maajabu mengi yaliyopo kwenye utendi ulioandikwa na Yeye mwenyewe.*

*Pindi tunapolia tunakuwa kama mawingu yaliyosheheni ustawi na baraka zake. Pindi tunapotabasamu tunakuwa kama radi yake yenye kuvutia.*

*Pindi tunapokasirika na kusababisha vita, huo unakuwa ni ubainifu*



wa Ghadhabu zake. Pindi tunapoleta amani na kuombana msamaha, hiyo inakuwa ufunuo na muonekano wa mapenzi Yake.

*Sisi ni nani ndani ya ulimwengu huu wenye kukanganya? Sisi si chochote bali ni vivuli kama herufi alif ambayo haiungani na herufi nyingine yoyote wala haikubali alama yoyote. Kila kitendo na hali inayotupata ni ubainifu wa Majina Yake na Sifa zake takatifu.”*

Kilichompelekea Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kustaajabu na kupata hofu ni Majina na Sifa takatifu zenye kuvutia na zilizo na ubainifu usio na kikomo hapa ulimwenguni na ndani ya roho yake, Sifa hizo ni zenye kustaajabisha sana. Wingi wa majina matakatifu unapelekea urahisi wa kuelewa wingi wa matendo yake; yanaashiria utukufu usio na kikomo. Yanamuweka Mola mbali na udhaifu na utambuzi mdogo. Sifa zilizo kinyume na viumbe zinakuwa kama kizuizi dhidi ya fikra zenye kumuweka Mola mipaka. Baadhi wanatamani kuona kwamba Mola anazingatia muonekano wa nje wa watu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu anazingatia muonekano wa nje wa watu lakini wakati huo huo anaangalia ndani ya mtu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *Jamiu'l-Azdad*, yani Mwenye kuungani-sha pande mbili; Amezileta pamoja sifa zote zenye pande mbili. Kutokana na jambo hilo ndio maana viumbe vyote vinatofautiana vyenyewe kwa vyenyewe. Vile kitu chochote kinachoruhusu kutambuliwa na akili ya kibinadamu hilo linaweza kufanyika kwa kupitia pande zake mbili. Kadiri tofauti inavyokuwa kubwa ndivyo utambuzi unavyokuwa bora zaidi.

Pia tofauti tunazoziona katika ulimwengu wetu wa uelewa zinakosa uwezo wa kukubaliana na huwa na kawaida ya kupambana zenyewe kwa zenyewe kwa ajili ya kuwa kitu kimoja. Kawaida hii inatokana na ukweli kwamba asili ya viumbe vyote ni moja. Tunaweza kusema kwamba yote haya ni matokeo ya *adatullah*, yani kanuni za Mwenyezi Mungu Mtukufu, zinafanya kazi katika ulimwengu mzima. Kama ambavyo usiku unatafuta kutawala mchana na joto linavyojaribu kulishinda baridi, vyote hivi vinatambulika kuwa vinafuata kanuni takatifu. Na pia tofauti hizi mbele ya Mola hazichukuliwi kuwa zinaangamizana zenyewe kwa zenyewe. Badala yake zina kawaida na uwezo wa kwenda pamoja. Hivyo kwa msingi huo Mola hana sifa zinazopingana zenyewe kwa zenyewe. Kwa mfano Yeye yu hai. Lakini uhai wake haufanyi mauti yawe kinyume chake. Uhai na





mauti kwa pamoja vinahusiana na viumbe vilivyoumbwa na vyenye kufa. Yeye yupo ingawa uwepo wake haudunishwi kwa namna yoyote ile. Yeye ni Mjuzi lakini ujuzi wake haufanyi ujinga kuwa kinyume chake. Yeye ni mwenye kukidhi mahitaji ya viumbe vyake lakini Yeye ha-hitaji chochote kutoka kwetu. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa sifa zake zilizobakia.

Baada ya yote kusemwa na kufanywa sisi hatuna uwezo wa kutambua na kuchanganua kwa kina undani wake, kwani hatuna uwezo wa kutambua hasa undani wa Sifa tukufu za Mwenyezi Mungu, kinyume chake tuna uwezo wa kukifikiria kile tu tulichopangiwa katika ulimwengu huu.

Tunaweza kulielezea suala hili kwa mfano ufuatao: Kutokana na waya mmoja wa umeme tunaweza kupata matokeo mawili: kwa mfano tunaweza kuchomeka upande mmoja wa waya kwenye friza na kupata baridi na upande mwingine kwenye kikanza na kupata joto. Ikiwa tunalifanya hili ndani ya chumba kimoja mapambano ambayo yangelitokea kati ya joto na baridi yangelipelekea kila upande kujaribu kuushinda upande mwingine, na yote haya yasingeliathiri ule waya wa umeme ambao ndio chanzo chao cha nishati, ungelibakia vile vile. Vile vile kwa kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu amewajaaliwa viumbe wake uwezo na nguvu tofauti tofauti ambazo zinaweza kuleta athari ya kiwango fulani, lakini kila kiumbe kinapokea ubainifu wa Majina Yake kulingana na uwezo wake. Na hivyo hili linasababisha mapambano ya viumbe wenyewe kwa wenyewe, mapambano ambayo yatapelekea yule mwenye uwezo zaidi kumshinda yule mwenye uwezo mdogo.

Hili linamaanisha kwamba mapambano kati ya pande mbili yaliyotapakaa hapa ulimwenguni si hasa mapambano ya kutafuta kumshusha mwingine ili asiwe na thamani bali ni mapambano ya kumshinda mwingine. Kwa kuwa kila sifa ya upande mmoja inakutwa katika jina takatifu moja au zaidi ya moja na kwa kuwa Majina haya ni matakatiifu basi tofauti hii haiwezi kufutwa kamwe.

Matokeo ya asili ya mambo haya ni kwamba pindi Jina takatifu la Muongozaji (*al-Hadi*) linapowaenea waumini, wakati huo huo Jina Mkengeushaji (*al-Mudill*) linawatawala makafiri. Hivyo mapambano kati ya imani na ukafiri yamefanywa yaendeleo mpaka siku ya kiamama. Haiwezekani kwa ubora wa mapambano haya ukaenda zaidi ya 'kutafuta ushindi' na badala yake kubakia kuwa vita vya msugano wenye kupelekea kwenye





maangamizi, kwani ubainifu wa kila Jina takatifu ni wenye kuendelea na ni wa milele.

Matokeo mengine ni kwamba hata kama makafiri watakuwa na nguvu kiasi gani lakini kamwe hawataweza kuishinda imani. Ni Vivyo hivyo kwa waislamu nao. Tulichogusia hapa kuhusiana na mapambano kati ya imani na ukafiri ni ukweli ambao upo katika usawa kati ya pande zote mbili katika ulimwengu mzima.

Katika maelezo mengine ni kwamba ulimwengu ambao upo ndani ya utukufu wa Majina matakatiifu haupo peke yake katika kupokea ubainifu wake. Vyote Qur'an na mwanadamu wanapokea ubainifu huo kwa viwango sawa.



Wakati ulimwengu unajitosheleza wenyewe kwa kupitia ubainifu huu, Qur'an inakuwa imebeba nathari za ukweli ambazo zinaelezea mambo yote yaliyopo ulimwenguni kwa namna ya 'maneno'. Kwa upande wa mwanadamu, yeye si kama ulimwengu katika kupokea ubainifu wa Majina matakatiifu bali yeye anaenda mbali zaidi, yeye ni kiini cha konde ambalo ni ulimwengu. Hii ndiyo sababu inayompelekea mwanadamu kuitwa ulimwengu mdogo (*alam-i saghir*).

Ni muhimu kwa mwanadamu kuwa na upinzani ndani Majina matakatiifu ambayo yana ubainifu mkubwa juu yake. Vile vile muumini ambaye Jina takatifu la muongozaji (*al-Hadi*) linamsimamia, lakini wakati huo huo anakuwa amebeba sehemu ya Jina Mkengeushaji (*al-Mudill*). Hivyo imani aliyonayo mtu ni matokeo ya majina hayo ambayo ndio msingi wa kumfanya mtu awe juu ya viumbe wengine. Suala hili ni tofauti mno kwa upande wa kafiri.

Matokeo ya asili ya hili ni kwamba kila muumini ana sehemu fulani ya ukafiri na kafiri naye Vivyo hivyo. Hivyo ni muhimu kwa muumini kuji-pamba na msimamo kati ya hofu na matumaini na kuishi kwa namna hiyo. Kwa hiyo muumini hana budi kutambua kuwa muda wowote anaweza kukengeuka. Pamoja na hayo muumini asichukulie kwamba kuna uwezekano siku moja Jina takatifu la *al-Hadi* litaipandisha daraja hata roho ya kafiri aliye mkorofi kuliko wote. Hivyo hana budi kumuangalia kila kafiri chini ya cheche za matumaini haya.





Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amelisisitiza hili kama ifuatavyo:

“Mtu hutenda matendo ya mtu wa peponi kwa muda mrefu lakini mwishoni huishia na matendo ya mtu wa motoni. Pia mtu hutenda matendo ya mtu wa motoni kwa muda mrefu lakini mwishoni huishia na matendo ya mtu wa peponi.” (Muslim, Qadar, 11).

Ndio maana ni muhimu kwa kila muumini kuuweka moyo wake uwe kati ya matumaini na hofu na kuifanya amri ifuatayo ya Mola kuwa msingi wa maisha yake:

“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini” (al-Hijr, 99).

Kwa kuwa hakuna mtu anayejua mwisho wake, ama ataishia kuwa muumini au la, kujiona uko salama dhidi ya adhabu na Mola au kujihukumu kuwa moja kwa moja wewe ni mtu wa motoni ni jambo lenye kumpelekea mtu kwenye *kufir*. Hakuna mtu yeyote aliye salama ukiwatoa Mitume na watu kama *ashara-i mubassharah*, wale ambao Mitume waliwapa bishara njema ya kuingia peponi wakati walipokuwa bado hai.

Kama ambavyo tumekwishasema hapo kabla, wakati sifa mbili pinzani zikikaa pamoja kwa amani na utulivu ndani ya Dhati ya Mola wakati huo huo zimebainika zikitafuta ushindi juu ya nyingine. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wale walioongozwa kwenye ubainifu wa jina *al-Hadi* au wale walioshikilia msimamo wao juu ya ukafiri kwa kupitia ubainifu wa jina la *al-Mudill*. Hata licha ya jitihada za hali ya juu za Mitume lakini jamii zimekumbatia sehemu kubwa ya ukafiri; na kinyume chake waumini wameweza kubakia na mwenendo wao hata pale ambapo makafiri na madhalimu wanaposhikilia tawala mbalimbali.

Qur'an yenyewe inathibitisha juu ya wengi waliopambana katika njia ya *iman* hata wakati wa pumzi zao mwisho bila ya kurudi nyuma; kwa mfano watu Ukhdud pindi walipotumbukizwa kwenye mashimo ya moto, wafuasi wa mwanzo wa Isa (Yesu) – amani iwe juu yake – pindi walipong'atwa mpaka kufa kati ya meno ya simba, *Habib'un-Najjar* pindi alipopigwa mawe na wenzake na wachawi wa Firauni ambao walining'inizwa juu ya vigogo vya mitende kwa sababu tu waliukubali wito wa Musa – amani iwe juu yake, watu ambao maneno yao ya mwisho kama mashahidi yalikuwa:





رَبَّنَا أفرِّغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ

“Nawe hukuudhika nasi ila kwa kuwa tumeziamini Ishara za Mola Mlezi wetu zilipo tujia. Ewe Mola Mlezi wetu! Tumiminie uvumilivu na utufishe hali ni Waislamu” (al-Araf, 126).

Kutokana na yote haya tunaweza kupata somo muhimu la msimamo na mwenendo bora. Hata kama mtu atakana imani kwa kiasi gani lakini hakuna mtu mwenye ruksa ya kuacha kumuita kwenye uislamu; kwani kinaweza kufika kipindi ambacho Sifa takatifu ya Muongozaji ikachomoza kutoka chini ya hali yake hiyo na kumpelekea kwenye mabadiliko makubwa ya mwenendo wake. Kwa maneno mengine ni kwamba hata yule kafiri mkaidi sana anaweza kuongoka. Suala hili limeelezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika aya ya Qur’an ifuatayo katika ushauri wake kwa Musa na Harun – amani iwe juu yao – kabla tu ya kuwatuma waende wakaongee na Firauni:

فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَّيِّنًا لَعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَى

“Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa” (Taha, 44).

Bila shaka aya hii ya Qur’an wakati huo huo inatuonesha njia bora ya kusambaza uislamu, njia yenye kanuni mbili:

1. Mtu ambaye anapelekewa wito wa kuingia kwenye haki hana budi kuongelehwa kwa ulaini, upole na kwa sauti yenye kubembeleza.

Kwa hakika badala ya kukubaliana na wito wa Musa – amani iwe juu yake - katika maeneo mbalimbali baada ya kushuhudia miujiza mbalimbali alizuiwa na waziri wake mkuu na watu wengine wakubwa. Hivyo kutokana na majivuno na kiburi chake hakuamini. Lakini pindi alipokuwa akimezwa na maji ya bahari njekundu huku akiwa katika hali ya kukata tamaa alijaribu kulitumia Jina tukufu la Muongozaji, hivyo alisema:

“...Naamini kuwa hapana mungu ila yule waliye muamini Wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa walio nyenyekeka.” (Yunus, 90).

Lakini kwa kuwa katika maisha yake yote alikuwa akitafuta ubainifu wa Jina tukufu la Mkengeushaji hivyo hakuweza kukubaliwa na imani yake





aliyoikiri katikati ya maumivu ya kifo. Na hivyo dhalimu yule mkubwa akaenda akhera huku akiwa kafiri.

Qur'an inaisisitiza njia hii katika aya nyingine kama ifuatavyo:

“Waite waelekee kwenye Njia ya Mola wako Mlezi kwa hikima na mawaidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora. Hakika Mola wako Mlezi ndiye anaye mjua zaidi aliye ipotea Njia yake, na Yeye ndiye anaye wajua zaidi walio ongoka” (an-Nahl, 125).

2. Bila ya kujali hali zao lakini wito wa kuingia kwenye uislamu hauna budi kujumuisha ili uweze kuwaenea wanadamu wote.

Licha ya ufedhuli alioufanya kwa kukataa wito wa kuamini lakini pia Firauni alikuwa muuaji katili ambaye aliwaua watoto waliokwisha tu kuzaliwa kwa ajili ya kumuua Musa – amani iwe juu yake. Lakini bado hili halikupelekea aache kuitwa kwenye wito wa kuingia kwenye haki. Mitume waliokuwa wamepewa jukumu la kumpelekea wito walifikia kuambiwa:

“Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa” (Taha, 44).

Kwa namna hiyo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – naye alimpelekea wito Abu Jahl katika nyakati mbalimbali. Licha ya kuukubali ukweli wa wito wa Mtume ndani ya moyo wake lakini hakuweza kuishinda nafsi yake. Hata hivyo mwenendo huu bora wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – uliwaongoza wengi miongoni mwa wale waliokuwa makafiri kuelekea kwenye uongofu, watu hao ni kama vile Omar ibn Khattab, Abu Sufyan, Hind and Wahshi.

Hivyo katika kupeleka mbele uislamu na katika mahusiano ya kijamii kwa ujumla mwenendo huu unafungua uwezekano wa kutumia mtindo wenye kupendezesha na kuzingatia masuala maalum. Na hivyo huu ni mtazamo muhimu na wenye msukumo mkubwa, na mwenendo huu ndio unaofanyiwa kazi na Sufi mpaka leo.



Kama matokeo ya asili na ya lazima kutokana na kumuamini Yeye kwa kukiri kwa moyo na kuthibitisha kwa ulimi Mwenyezi Mungu amependelea atukuzwe kwa kupitia ibada, jukumu ambalo miongoni mwa viumbe vyake amewapa wanadamu na majini peke yao. Amewajaalia akili na





utambuzi kulingana na majukumu aliyowapa. Licha ya ukweli kwamba majini ni wengi kuliko wanadamu na wametajwa katika sehemu mbalimbali ndani ya Qur'an, lakini kipaumbele cha heshima hupewa wanadamu. Baada ya kuyasema hayo ni kwamba majini pia wanawajibika kama walivyo wanadamu, nao wanawajibika kutekeleza majukumu yao kama watumishi na kuabudu, jambo ambalo ndilo lengo la ujumla la wote majini na wanadamu.

Mwenyezi Mungu anatufahamisha jambo hili ndani ya Qur'an kama ifuatavyo:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

“Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi” (ad-Dhariyat, 56).

Cha zaidi ni kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye huruma yake isiyo na kifani imepita Ghadhabu zake hakuwaacha majini na wanadamu peke yao, hakuwaacha tu na uwezo wa kufikiria na kutambua mambo na kutofautisha katika mazuri na mabaya, bali pia amewapa msaada mwingine zaidi. Kana kwamba ulimwengu peke yake hauna dalili za kutosha za kuthibitisha uwepo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwenyezi Mungu ametuletea kikosi cha Mitume na watakatifu kwa ajili ya kuziunganisha dalili hizo. Ili kuhakikisha kuwa hakuna mtu hata mmoja anayekosa msaada huu Mwenyezi Mungu amefungua msaada wake kwa mtu wa kwanza kwa kumvisha taji la utume Adam – amani iwe juu yake - ambaye ndiyo mwanadamu wa kwanza. Kutokana na ubora wa mwanadamu dhidi ya majini Mitume wote wametokana na kizazi cha mwanadamu, baadhi yao wamewajibika pia kuwaongoza majini.

Ingawa ujumbe wa kila Mtume ulikuwa ni mmoja kwa upande wa ukweli waliokuwa wanausambaza lakini hukumu zao za kijamii zilienda sambamba na maendeleo ya maisha ya mwanadamu, na mwisho wake zilifikia mwisho kwa Mtume wa mwisho – rehema na amani ziwe juu yake – na Qur'an tukufu aliyoshushiwa. Hivyo Qur'an tukufu itabakia mpaka siku ya mwisho, Qur'an ambayo ndio muujiza ulio katika maneno na ambao haupingiki kamwe. Vile vile kwa kuwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ametumwa kwa majini na wanadamu,







hivyo ameitwa *Rasulu'th-Thaqalayn*. Neno *thaqalayn* linaashiria kizazi cha wote wanadamu na majini.

Ulimwengu ambao umebeba utukufu wa Majina matakatifu ni wenye kudhihirisha nguvu ya Mola kwa namna yenye kuvutia sana. Kadiri sayansi inavyoendelea ndivyo ubainifu wenye kupendeza wa ustadi mtakatifu unavyofahamika kwa undani zaidi, hili linampelekea mtu kuufahamu vyema uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ukweli huu unathibitishwa na shughuli za kisayansi za aina zote, kuanzia kwenye utafiti wa kisasa wa anga ya mbali mpaka kwenye maendeleo ya sayansi za kinasaba na maajabu ya kompyuta. Ndio maana Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

“...Kwa hakika wanao mcha Mwenyezi Mungu miongoni mwa waja wake ni wanazuoni. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu, Mwenye kusamehe” (Fatir, 28).

Kila hatua inayopigwa katika maendeleo ya kisayansi ndivyo mwanadamu anavyopata ushahidi zaidi juu ya Nguvu na utukufu wa Mwenyezi Mungu. Kutokana na kupambwa na mwenendo huo ulimwengu umekuwa kama chanzo kikubwa cha ubainifu wa utukufu wa Mola kutokana na huduma ya akili ya mwanadamu ambayo ni ustadi wa hali ya juu ambao hauwezi kuelezewa kwa maneno. Wale wenye kupata ufahamu kwa kushikamana na maamrishi matakatifu hupita uhalisia ambao ni kuweka katika maneno na kuanza kusoma hekima na siri zilizoandikwa ndani ya kitabu cha ulimwengu.

Sayansi asilia zinalenga kutafsiri utaratibu mtakatifu ambao unaendelea ulimwengu chini ya kanuni za asili. Kwa kuufahamu ukweli huu ujulikanao kama ‘kanuni za asili’ katika uelewa wa kiulimwengu wale wenye ufahamu wa kina wanakuwa wamefikiria malengo matakatifu ambayo yanauongoza ulimwengu.

Mwanadamu ambaye ni ulimwengu mdogo pia naye amebeba dalili nyingi za kudhihirisha uwezo wa Mola. Ndio maana anaitwa *zubda-i kainat*, yani ulimwengu uliokandamizwa, na yeye ni kiini na mbegu. Kama ambavyo mbegu imebeba sifa zote za kile itakachokitoa, vile vile mwanadamu naye amewekewa siri zote na uhalisia ambao upo katika ulimwengu na ndani ya Qur’an katika umbile la nyuklia.

Mwenyezi Mungu ambaye uwepo wake haufanani na ule wa viumbe





vyake, na ambaye Dhati yake si bayana kwenye akili ya mwanadamu na ambaye ameacha wazi mlango wa kuweza kumfahamu kwa kupitia kazi zake na ustadi wake, amemuumba mwanadamu kwa ajili ya kuwa *khalifah* au muwakilishi wa Mwenyezi Mungu hapa ardhini. Ili kumfanya awe ni mwenye kuheshimika kuliko viumbe vyote amemuumba mwanadamu na kumfanya kuwa ndio kiini cha ulimwengu. Hivyo sayansi haina budi kumfanya mwanadamu awe juu ya vitu vyote na kumfahamisha sababu ya uwepo wake hapa duniani na kumfungulia mlango wa *marifatullah* au elimu takatifu.

Lengo kuu ambalo sayansi inapaswa kujitahidi kulifikia limefafanulia na Yunus Emre kama ifuatavyo:

*Kufahamu ni kujifunza elimu,  
Kujifunza ni kujifahamu mwenyewe,  
Kama hujifahamu wewe mwenyewe,  
Ni somo la aina gani hilo.  
Ninajifunza na ninafahamu, si ndio,  
Au kinyume chake ningeliwaabudu wengi,  
Kama humfahamu Mola,  
Yote mengine yatakuwa ni maongezi ya upuuzi.*

Thamani na cheo hiki ambacho Mola amemjaalia mwanadamu vimepata sauti kwa ujumla wake katika kazi nyingi za kisufi, kazi ambazo zinazama ndani ya nyoyo za watu. Labda kitu cha kwanza kuja kichwani miongoni mwa kazi zote zenye kuelezea thamani ya mwanadamu vizuri ni shairi maarufu la Sheikh Ghalib ambaye ni mshairi maarufu wa karne ya 18. Sheikh katika shairi lake anamuelezea ‘mwanadamu’ kama ifuatavyo:

*Ndani yako linapatikana ghala la siri za upendo,  
Pia kuna mwangaza na zawadi ya uumbaji,  
Na hali nyingine nyingi ziko ndani yako, zote zimejificha,  
Elimu, maarifa na uhalisia...ndani yako vimetulia,  
Angalia na utaona ndani yako kuna ardhi na anga,.  
Kiti cha enzi na malaika...na bila shaka mbingu na moto,  
Kisha itazame dhati yako, kwani wewe ni kiini cha ulimwengu,  
Wewe ni tufani la jicho kwa kuwa kwako kiini cha kokwa lake.*





Kwa hiyo kwa kifupi mwanadamu ni mukhtasari mfupi wa neema tukufu za Mola ambazo amezibainisha katika dunia hii yenye kupita. Kutokana na ubora huu mwanadamu anakuwa ni ulimwengu wa aina yake, pia anakuwa na ubora wa kipekee wa kumfanya awe Qur'an iliyo hai.

Bado utafiti wa kisayansi haujaweza kuyafanyia kazi vilivyo maendeleo yaliyotokana na kuviweka wazi vitu vya ulimwengu visivyoonekana kwa kupitia kwa mwanadamu. Hili linatokana na ukweli kwamba mwanadamu mkusanyiko wa mwili na roho na kwamba Mola amemfunulia mwanadamu taarifa ndogo kuhusiana na fumbo la roho. Kwa hiyo kwa upande wa ndani ya mwanadamu kuna siri kubwa kuliko ulimwengu wenyewe. Kukua kwa haraka kwa ufahamu wa mwanadamu katika milenia mbili zilizopita hazikwenda pamoja na uongezekaji wa elimu juu ya roho. Hili linathibitishwa na Qur'an kama ifuatavyo:

“Na wanakuuliza khabari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika ilimu ila kidogo tu” (al-Isra, 85).

Kwa upande wa ulimwengu, wenyewe unaendeshwa na kanuni timilifu ambazo zinaitwa *adatullah* or *sunnatullah*, yani kanuni za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wakati huo huo kuna kanuni za hekima zinazohusiana na ulimwengu wa kimwili na ule wa kimetafizikia ambazo zinampatia mwanadamu ufahamu juu ya ujuzi na uwezo wa Mola usio na mipaka. Malengo yake makuu ni kuthibitisha ukweli kwamba zote hizo zimewekwa na Mola pekee ambaye Uwezo wake ndio uliosababisha ulimwengu mzima kuwepo. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu anajibainisha kwetu sisi waja wake kwa kupitia hekima na siri za vile alivyoviumba, uislamu wenyewe unamualika mwanadamu katika kuzingatia ubainifu huu ndani ya ulimwengu kana kwamba anasoma mistari ya Qur'an. Qur'an inalithibitisha hili kama ifuatavyo:

“Je! Hawakuiona ardhi, mimea mingapi tumeiotesha humo, ya kila namna nzuri?” (as-Shuara, 7).

“Basi ziangalie athari za rehema ya Mwenyezi Mungu, jinsi anavyo ihuisha ardhi baada ya kufa kwake. Basi hakika huyo ndiye bila ya shaka Mwenye kuhuisha wafu. Na Yeye ni Muweza wa kila kitu” (ar-Rum, 50).

“Aliye umbamba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika





uumbaji wa Mwingi wa Rehema. Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote? Tena rudisha nadhari mara mbili, nadhari yako itakurejea mwenyewe hali ya kuwa imehizika nayo imechoka” (al-Mulk, 3-4) .

“Je! Hawamtazami ngamia jinsi alivyo umbwa? Na mbingu jinsi ilivyo inuliwa? Na milima jinsi ilivyo thibitishwa? Na ardhi jinsi ilivyo tandazwa?” (al-Ghashiyah, 17-20).

“Je! Hawaangalii mbingu zilizo juu yao! Vipi tulivyo zijenga, na tuka-zipamba. Wala hazina nyufa” (Qaf, 6).

Ni jambo la wazi kwamba ndani ya ulimwengu huu mkubwa kuna utaratibu maalum ambao unamfanya mwanadamu astajaabu. Utaratibu huu maalum umekuwepo tokea ulimwengu uumbwe kwa msawazo wa mahesabu ya hali ya juu. Kwa mfano kama dunia isingelikuwa imelala katika nyuzi 23.5 kusingelikuwa na kitu kiitwacho majira ya mwaka; kungelikuwa na kiangazi au kipupwe chenye kuendelea maisha yote. Pia kama umbali kati ya dunia na jua ungeliongezeka kidogo tu basi kila kitu juu ya dunia kingelikaribia kuganda kama barafu. Na kama ungelipungua basi kila mahali kungelikuwa kumekauka kutokana na joto. Hizi na sifa nyingi nyingine zisizotajwa hapa zinatoshia kuthibitisha ukweli kwamba vitu vyote ulimwenguni vimewekwa kwa namna ambayo itamrahisishia mwanadamu maisha yake hapa ulimwenguni.

Macho ambayo yanaweza kuona vyema yanatambua kuwa mbele ya mamlaka na utaratibu wa Mola dunia ni moja miongoni mwa mabilioni ya vumbi yanayoelea angani. Milima, tambarare, bahari na hata wanadamu ni vialama vidogo mno katikati ya vumbi hili lenye kuelea. Hivyo kutokana na udhaifu huo mwanadamu si chochote kinyume na kujaaliwa kuwa mja wa Mwenyezi Mungu.

Kutokana na kuumbwa kulingana na utaratibu wa kimahesabu wa matabaka yaliyoshikamanishwa kwa pamoja na hivyo kupelekea mwanadamu kuwa katika ubora unaoendana na utukufu wa Mwenyezi Mungu, ndio maana mwanadamu ataweza kutambua vyema utukufu uliopo angani na ardhini kutokana na maendeleo ya sayansi. Qur’an inasema:

“Tutawaonyesha Ishara zetu katika upeo wa mbali na katika nafsi zao mwenyewe mpaka iwabainikie kwamba haya ni kweli. Je! Haikutoshi kwamba Mola wako Mlezi kuwa Yeye ni Shahidi wa kila kitu?” (al-Fussilat, 53).





Na bila shaka maendeleo ya utafiti wa anga unatoa uelewa wa kina juu ya upambanuzi uliotolewa na Qur'an. Si tu kila uvumbuzi wa kisayansi unaithibitisha Qur'an bali wakati mwingine unatoa mwangaza juu ya aya nyingi zisizoeleweka kwa urahisi.

Wanasayansi wengi wenye mtazamo sahihi walio katika fani za embriolojia, anatomia na bailojia wamelazimika kukubaliana na Qur'an kutokana na kushangazwa kwao namna aya za Qur'an zilivyotoa maelezo juu ya utaratibu katika kila hatua ya ukuaji wa mwanadamu ndani ya tumbo la mama:

“Na kwa yakini tumemuumba mtu kutokana na asli ya udongo. Kisha tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti. Kisha tukaiumba tone kuwa damu iliyo ganda, na tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha tukaiumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa tukaivika nyama. Kisha tukamfanya kiumbe mwengine. Basi ametukuka Mwenyezi Mungu Mbora wa waumbaji.” (al-Muminun, 12-14).<sup>3</sup>

3. Profesa Marshall Johnson ambaye alipata umaarufu mkubwa kutokana na utafiti wake katika fani ya anatomia alistaajabu sana baada ya kusoma aya kadhaa zinazoelezea ukuaji wa wanadamu ndani ya tumbo la mama. Hasa alikazia macho yake pale palipoelezea kuhusiana na *mudhgha* (kijusi, hasa ‘pande la nyama lililotafunwa’):

Mtafuno mmoja wa nyama (*mudhgha*)...uliotengenezwa kulingana na mpangilio wa meno; kana kwamba ni alama za meno zilizopo kwenye nyama iliyotafunwa.

Kilichogundulika katika *mudhgha* ni sifa zote za mwanadamu. Baadhi yake zinafanya kazi na nyingine bado hazijaanza kufanya kazi. Sayansi ya udaktari haiwezi kupata maneno ya kuweza kulielezea jambo hili. Kama wangukuja na kusema kwamba viungo vya *mudhgha* vinafanya kazi, isingelikuwa kweli kwani baadhi yake vimetulia na vingine vinafanya kazi. Kinyume na hayo Qur'an inafafanua kwa kusema “...kipande cha nyama chenye umbo na kisicho kuwa na umbo” (al-Hajj, 5), maneno yenye kubeba taarifa yote ihusuyo *mudhgha*; maneno yaliyotolewa karne nyingi zilizopita. Mtu ambaye alikuwa akiipinga Qur'an hapo mwanzo aliona anawajibika kuikubali yote na alishindwa kujizuia na hivyo akakiri kwa kusema:

“Ndio”; hii Qur'an ambayo inamulika kwenye njia za wanachuoni bila shaka imetoka kwa Mungu. Pindi muda wao utakapofika kila uhalisia wake utajidhihirisha wenyewe mmoja baada ya mwingine, na kutoka nje. Yale anayoyasema Mungu ndani ya Qur'an kwamba “Kila khabari ina kipindi chake. Nanyi mtakuja jua” (al-Anam, 67) yatakuja kudhihirika. (Angalia, Abdulmajid Zindani, Kur'an'da Ilmi Mucizeler, uk. 31-36).





Kwa kuwa Qur'an si kitabu kilichohifadhiwa kwa ajili ya sayansi kama vile unajimu, botania, bailojia na kadhalika, na kwa kuwa sifa yake ni kuwa *jawamiul'-kalim*<sup>4</sup>, hivyo iko mbali na jukumu la kutoa maelezo maalum juu ya sayansi na teknolojia. Lakini bado kila uvumbuzi na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia yanatoa ukweli na hekima juu ya yale yaliyo-tajwa na Qur'an kwa ufupi, haya ni kwa ajili ya kumulika juu ya uhalisia wa mambo katika kila siku ipitayo. Sehemu ambayo inabainisha wazi uhalisia wa mambo haya kwa kina zaidi ni ulimwengu wenyewe. Sababu ya hili licha ya Qur'an kutoa ufafanuzi wa wazi juu ya uhalisia wa mambo ulioshikamana na mwanadamu ni kwamba sehemu kubwa ya ukweli wake umefichikana kwa namna fulani.

Hali ya Qur'an ya kuelezea mambo kwa kifupi inatokana na ukweli kwamba Qur'an imebeba mambo mengi kupita kiasi. Kama mambo ambayo yanawekwa wazi na sayansi kidogo kidogo yangelielezewa kwa uwazi ndani ya Qur'an basi kungelitokea matatizo kadhaa:

a. Kulingana na elimu ya wakati ule ingelikuwa vigumu kwa watu kuyakubali mambo hayo na matokeo yake wangeliveza kuyakana bila kujua. Hivyo rehema na huruma ya Mola imepelekea kufichwa kwa baadhi ya mambo ili yaweze kufichuliwa kidogo kidogo kadiri muda unavyopita.

b. Kama Qur'an ingelikuwa imetoa ufafanuzi wa kina juu ya mambo mbalimbali basi ingelikuwa na maneno mengi kiasi kwamba ingelikuwa vigumu kwa mtu kuisoma kuanzia mwanzo mpaka mwisho, achilia mbali kuihifadhi kichwani. Qur'an inasema:

"... Na tumekuteremshia Kitabu hiki kinacho bainisha kila kitu, na ni uwongofu, na rehema, na bishara kwa Waislamu" (an-Nahl, 89)

"...Na halidondoki jani ila analijua. Wala punje katika giza la ardhi, wala kinyevu, wala kikavu ila kimo katika Kitabu kinacho bainisha " (al-Anam, 59). Mwenyezi Mungu anasema kwamba Qur'an inagusia mambo yote ya hapa ulimwenguni kwa ufupi kwa kusema:

"Hebu hawaizingatii hii Qur'ani? Na lau kuwa imetoka kwa asiye kuwa Mwenyezi Mungu bila ya shaka wangele kuta ndani yake khitilafu nyingi" (an-Nisa, 82). Anawaalika waja wake wote katika kuvuta hewa ya tafakuri inayotokana na Qur'an.



4. Neno *Jawamiul'-kalim* linaashiria uwezo wa kuelezea maana kubwa katika maneno machache.



Kwa kutumia maelezo yake yenyewe Qur'an ni *Furqan*; yani Qur'an ni kitabu chenye kuweka bayana tofauti kati ya uongofu na upotofu, mema na mabaya, nuru na giza. Hutoa matokeo kulingana na nia na uwezo wa wale wanaoisogelea. Pindi itakaposogelewa kwa moyo safi itatoa nafasi ya kuongeza na kuimarisha imani; na katika hili Qur'an inathibitisha kwa kusema:

“Hakika Waumini ni wale ambao anapo tajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanapo somewa Aya zake huwazidisha Imani, na wakamtegemea Mola wao Mlezi” (al-Anfal, 2).

Kinyume chake wale ambao wataisogelea Qur'an kwa nia mbaya wataishia kuchochea upotofu wao. Kukiangalia kitu kwa jicho la upendo hupelekea kuuleta mbele uzuri wake. Na kinyume chake kukiangalia kitu kwa chuki huleta mbele ubaya juu yake; sawa na ulivyokuwa mtazamo wa Abu Jahl juu ya uislamu. Kadiri watu hao wanavyozidi kuisoma Qur'an ndivyo wanavyozidi kuwa na hisia za ukafiri na kupotea zaidi, kwani wanakuwa wamejiweka katika mazingira ambayo yatawafanya wawe wazito katika kufikia kwenye vilele vya uzuri wa Qur'an. Wanaweza kulinganishwa na wale walioshindwa na mahasimu wao kwenye mchezo; hupandwa na hasira na moto wa hasira yao isiyo na kifani huzidi kuongezeka. Na matokeo yake watakuwa ni wenye kustahili adhabu. Katika hili Qur'an inasema:

“Na tunateremsha katika Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara” (al-Isra, 82) .

“Na lau tungeli ifanya Qur'ani kwa lugha ya kigeni wangeli sema: Kwanini Aya zake haziku pambanuliwa? Yawaje lugha ya kigeni na Mtume Mwaarabu? Sema: Hii Qur'ani ni uwongofu na poza kwa wenye kuamini. Na wasio amini umu uziwi katika masikio yao, nayo kwao imezibwa hawaioni. Hao wanaitwa nao wako pahala mbali” (Fussilat, 44).

Hivyo kama ambavyo Qur'an ilivyo nuru tukufu ya uongofu kwa watu wema, pia ni yenye kuwaongezea uharibifu wale makaidi ambao hufunga macho yao mbele ya nuru yake.

Kuhusiana na watu hao Qur'an inatufahamisha tena yafuatayo:

“Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo zao za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayo pofuka, lakini zinazo pofuka ni nyoyo ziliomo vifuanii” (al-Hajj, 46).





Kama ambavyo tumeona ni kwamba ulimwengu ni mfumo wa uumbaji uliotokana na ubainifu wa Majina matakafifu, wakati Qur'an ni taswira ya mambo yaliyo wazi na yaliyojificha ndani ya mfumo huu kwa njia ya maneno. Na kwa upande wa mwanadamu yeye ni kiini, dhati na mbegu kwa kuwa amebeba ubainifu tofauti katika viwango mbalimbali.



Baada ya kuumba ulimwengu kwa kupitia ubainifu wa Majina yake, kisha akawajaalia wanadamu ubainifu kamili wa majina haya. Ndio maana mwanadamu ni *ashraf-i makhluqat*, yani mwenye kutukuzwa miongoni mwa viumbe. Pia kulingana na uwezo wao wanadamu wamejaaliwa sifa nyingine tofauti, hivyo wamekuwa ni *jamiu'l-azdad*. Huwa wanalia na kucheka, wanapenda na kuchukia, na kadhalika. Kwa maneno mengine ni kwamba mwanadamu kuwa kwake na hisia tofauti ni kutokana na sifa huruma na ghadhabu. Hivyo mwanadamu anaweza kuonyesha hisia za huruma na ukarimu na wakati huo pia anaweza kuonyesha hisia za hasira na uadui. Huwa wakati wote anayumba kati ya mawimbi ya utulivu na ghadhabu.

Mwanadamu amepokea sifa nyingi takatifu. Lakini kiwango cha ubainifu wake ni tofauti sana kutoka kwa mwanadamu mmoja mpaka kwa mwingine. Tokea chini kabisa ya mzani mpaka juu kabisa kiwango cha ubainifu walichonacho wanadamu ndicho kinachopelekea kuwepo kwa matabaka katika jamii.

Kwa mfano, bila shaka kila mwanadamu amebeba ubainifu wa Majina matakafifu ya Mwingi wa rehema (*ar-Rahman*) na Mwenye kurehemu (*ar-Rahim*). Lakini viwango vya ubainifu wake vinatofautiana kutoka kwa mtu mmoja mpaka kwa mwingine. Baadhi yao ni wenye kujihurumia wao wenyewe na wakizidisha huruma ni kwa familia zao au marafiki zao wa karibu, wakati kuna wengine ambao huruma yao imesambaa kiasi cha kuwaenea wanadamu wote na hata kizazi cha wanyama. Katika ubainifu wa sifa ya 'Mwingi wa Rehema' tunaweza kutoa mfano ufuatao:

*Siku moja Bayazid Bistami - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alipokua safarini kuelekea mahali fulani aliamua kupumzika chini ya mti kwa ajili ya kula. Baada ya kumaliza kula alinyanyuka na kuendelea na safari*







yake. Lakini baada ya muda na baada ya kufika mbali na pale alipokuwa alimuona sisimizi akitambaa kwenye mkoba wake, kisha akasema yafuatayo kwa masikitiko kubwa:

*“Nimekihamisha hiki kiumbe cha Mwenyezi Mungu kutoka kwenye makazi yake” na wakati huo huo akawa anarejea kwenye ule mti kwa ajili ya kumrudisha huyo sisimizi kwenye makazi yake.*

Pia ufuatao ni mfano mwingine mzuri kabisa katika kuonyesha huruma:

*Siku moja wakati Sari-i Saqati - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alipokuwa anawaelezea wanafunzi wake juu ya maneno ya kiutume yasemayo: “Yule asiyejisumbua kutokana na matatizo ya waumini si miongoni mwao” (Hakim, Mustadrak, IV, 352; Haythami, Majmau’z-Zawaid, I, 87), mara mwanafunzi wake mwingine aliingia ndani upesi na kusema:*

*“Mwalimu...Nyumba zote za majirani zako zimeungua. Nyumba yako pekee ndiyo iliyopona!”*

*“Alhamdulillah (Ninamshukuru Mwenyezi Mungu)”, Sari-i Saqati alivuta pumzi na kusema huku akiwa na furaha.*

*Miaka thelathini baadae alikuwa akionekana akikiri kwa rafiki yake wa karibu:*

*“Wakati ule wa janga nilisema alhamdulillah kwa kuwa nilikuwa nikijifikiria mwenyewe na kujiweka mbali na matatizo ya wengine ambao walikubwa na janga lile. Na miaka thelathini iliyopita sikufanya chochote zaidi ya kuomba toba juu ya kosa lile!”*

Kwa hiyo haijalishi ni wapi na ni wakati gani mtu anahisi huruma na upendo na chanzo chake ni nani, cha muhimu ni kwamba pale hisia hizi zinaporuhusiwa kustawi na kukua mpaka kuwaenea viumbe wote, bila shaka zitamfanya mtu kuwa ‘muislamu wa kweli’ au kwa maneno mengine, mtu mwenye upendo wa kweli. Hata kama upendo huo utakuwa umestawi kutokana na chanzo fulani kama mmea uchomozapo kutokana na kunyunyiziwa matone machache ya maji, kadiri siku zinavyoenda upendo huo utakuwa ‘upendo wa kweli’ kama utasambaa kwa viumbe wote kwa ajili ya Muumba.

Isipopanuliwa mipaka ya muunganiko huo wa huruma na ukaribu





ambao ni ‘upendo mtakatifu’ basi huruma na ukaribu wowote ambao utahisiwa hautakuwa upendo kwa maana yake hasa. Kinyume chake utabakia katika hatua iitwayo upendo wa kisitiari, upendo ambao ndio ngazi ya chini ya upendo wa kweli.

Muunganiko wa ubainifu wa Majina matakatiifu umetoa tabia mbalimbali, tabia hizo ni nyingi kama ilivyo idadi ya wanadamu. Kama ilivyo pindi uchanganyapo rangi mbalimbali hupata moja ambayo huzitawala nyingine, Vivyo hivyo mchanganyiko wa ubainifu huu wa majina matakatiifu hupelekea kuwepo kwa sifa moja ambayo huwa juu ya nyingine. Ndio maana mwenendo wa kisufi umegawanyika katika matawi mbalimbali; kila tawi au utaratibu (*tariqah*) hujihusisha na tabia ya namna fulani, hivyo kurahisisha njia ya mafanikio ya kiroho kwa kumvuta mhusika katika njia ambayo inaendana na silika yake. Hili linadhihirisha ulazima wa kutumia njia tofauti tofauti kwa kila *murid* kulingana na silika yake.

Viumbe vilivyo chini ya mwanadamu navyo vimegawanywa kwa namna hii hii, kuna wanyama au mimea, au viumbe vilivyo hai na visivyo hai, silika yao pia inaweza kuchangia katika mgawanyiko huu kulingana na sifa mbalimbali. Lakini hatuna budi kutambua kuwa tofauti katika vile viumbe vilivyo katika daraja la juu na vile vilivyopo katika daraja la chini katika kundi moja inaweza kuwa kubwa mno kuliko tofauti kati ya makundi mawili. Kwa mfano tofauti ya daraja kati ya mwanadamu wa daraja la chini na yule wa daraja la juu ni kubwa kuliko tofauti kati ya mwanadamu na mnyama. Nyuma ya tofauti hii kunapatikana tofauti kubwa zaidi ya ubainifu kwa kila mmoja. Hili ni sawa kwa sifa zilizo mbaya na zile zilizo nzuri. Kwa kweli ya kustaajabisha ni tofauti kati ya mtu aliye katika upande mmoja wa udhalimu au ukafiri na mwenzake ambaye yuko upande mwingine wa mzani.

Kwa mfano kafiri ambaye kwaye Jina la Mkengeushaji (*al-Mudill*) limeshahidi huishi maisha yaliyo dhalili kabisa. Huwa hajali kamwe juu ya imani ya waumini. Lakini kama ilivyokuwa kwa Abu Lahabi na walio-kuwa mfano wake, pindi ukafiri wake ulipomzidi upuuziaji wake mambo uligeuka na kuwa chuki na hivyo kumpelekea kupambana na waumini na hata kufikia kutaka kupambana na Mitume kama ikibidi, yote haya ni ili akidhi chuki yake. Hayo hayo hutokea katika suala la udhalimu. Muwindaji ambaye hawindi kwa ajili ya mahitajio yake bali kwa ajili ya kujifurahisha





muda si mrefu hujikuta ni mwenye moyo mgumu na hata kufikia kuwa katili. Watawala makatili wa Rumi ambao walikuwa wakiwaangalia simba waliokuwa na uchu wakiwararua kwa hasira waumini wa mwanzo wa Yesu – amani iwe juu yake, suala hili limegusiwa katika Qur'an kama ifuatavyo:

« بَلِّ هُمْ أَضَلُّ »

“Bali wao wamepotea zaidi kuliko hata wanyama”



Kutapaka kwa ubainifu juu ya viumbe vyote, vilivyo hai na visivyo hai wakiwemo wanadamu kunaweka wazi ‘tofauti’ kama kanuni muhimu ya ulimwengu. Hivyo kuvilinganisha viumbe viwili kuachilia mbali ulimwengu mzima ni jambo lisiloleta maana, kwani ubainifu usio na kifani wa Majina matakatiifu unamaanisha kwamba hakuna ‘mapacha’ katika ulimwengu; mapacha kwa maana ya mfanano kamili na usio na tofauti hata kidogo. Kwa kuzingatia maada na roho hakuna wanadamu wawili ambao ni kitu kimoja na ambao wanafanana kwa kila kitu. Vivyo hivyo ni sawa kwa miti miwili ambayo ni ya jamii moja, wakati wote hutofautiana kiwango cha matawi, majani na matunda inayozalisha.

Baada ya kumuelewa Mwenyezi Mungu, mwanadamu na ulimwengu katika mtazamo huu, mwanadamu ataweza kuvumilia tofauti hizi na hata kufikia kuweza kukaa na wenzake kwa huruma na upendo. *Tasawwuf* inasisitiza kwamba ukomavu wa mtu ni pale atakapoweza kuviangalia vitu vingine kwa upendo na huruma wakati vitu hivyo vingelisababisha hasira kwa wengine ambao hawajachagua njia hii ya upendo. Hii ni faida inayopatikana baada ya kufahamu hekima juu ya muonekano wa nje wa vitu.

Sifa na ukomavu wa namna hii vinatupa faida nyingi sana. Ya kwanza na ya muhimu kabisa ni kutufanya tuweze kuwasikitikia watenda madhambi badala ya kuwakasirikia. Sifa hizi zinatufanya tuwe wapole kwa makafiri na kupelekea upotofu wao kutupa matumaini, kwani unatupa nguvu na shauku ya kuwaita katika haki. Unatupafanya tumtazame yeyote ambaye anahitaji kusikia wito, kama kipofu ambaye anahitaji wengine wamsaidie katika kutembea na kumuongoza njia. Unatufanya tusiache kuwa na hisia ambazo tungelikuwa nazo pindi tunapomuona ndege aliyevunjika ubawa,





na hivyo kuzihamishia kwa mtu ambaye moyo wake umevunjika kutokana na kulemewa na madhambi. Mwishowe hisia zetu za upendo na huruma huwa kama maporomoko makali yaliyo juu ya tamaa zote za udugu na ambayo yanawaelekea wanadamu wote kwa upole. Katika jamii iliyo na wanadamu wa namna hii, mauaji na kutoelewana hugeuka na kuwa mshikamano wa hali ya juu. Na kutokana na mshikamano huo watatokea watu wengi wema katika miaka ijayo. Mwenendo mwema wanaokuwa nao kutokana na kumuiga Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – utasambaa kwenye jamii nzima. Mfano ufuatao unahusiana na mwenendo wa kujipamba nao mbele ya watu wenye makosa:

*Khatam Asamm - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - ambaye ni mwanachuoni kutoka Balkh ni mfano wa kuigwa katika historia ya usufi kutokana na kujitakasa kwake kwa kupitia urithi wa kiroho wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na hivyo kupandisha mwenendo wake mpaka kufikia daraja la juu imani. Alikuwa akijulikana kwa jina la kupanga la Asamm au kiziwi licha ya kuwa mtu mwenye kusikia vizuri kabisa, alitwa hivyo kutokana na tukio lifuatalo:*

*Siku moja alitembelewa na mwanamke mmoja aliyekuwa na matatizo, mwanamke ambaye alikuja kwake kwa ajili ya ombi. Alipoanza tu kuelezea matatizo yake akatokwa na upepo bila ya kujitambua. Alihisi aibu isiyokuwa na kifani; kinadharia aliyeyuka kama mshumaa. Lakini ili kuzuia yule mwanamke asije akahisi aibu zaidi, Khatami - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alijifanya hakusikia chochote. Na kisha akapeleka mkono kwenye sikio na kusema:*

*“Sisikii vizuri dada. Ongeza sauti yako kidogo...sikusikii!”*

*Huku akidhania kuwa aibu yake haikusikika mwanamke yule alivuta pumzi na kuendelea kumuelezea matatizo yake kwa sauti ya juu.*

*Imepokewa kwamba Khatam alijifanya kiziwi kwa miaka yote kumi na tano iliyofuata baada ya tukio lile mpaka mwanamke yule alipofariki, Khatam - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alijifanya kiziwi ili kumfanya mwanamke yule asije akamgundua na hivyo kuhisi amedhalilishwa. Ndio maana akaja kuitwa Khatam-i Asamm au Khatam kiziwi.*

*Bila shaka ni wazi kwamba kiwango cha juu cha tabia alichokionesha Khatam - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kilikuwa ni matokeo ya*





kuyafanyia kazi yale aliyoyasoma katika vitabu. Tabia ya Khatam inaweza kuelezewa kutokana na mafanikio yake ya kuchukua sehemu ya sifa takati-fu ya Mwenye kusitiri madhambi (*Sattaru'l-Uyub*) na kuifanya kuwa ndio mwenendo wake. Mwenendo huo umepewa jina la 'kujipamba na maadili ya Mwenyezi Mungu', jina hili linatumika sana katika *tasawwuf*.

Kwa hiyo watu wema hujisalimisha kwa Mola wao kutokana na ubainifu wa Majina yake matakatiifu walioupata. Kutokana na kufahamu kwao kwamba kile anachokitaka Mola ndicho sahihi huwapelekea kuwafahami-sha pia wale wanaowazunguka na kuwafanya wabakie katika msimamo huu. Katika suala hili tukio lifuatalo linatosha kutupa hekima:

*"Tuchukulie kwamba Mwenyezi Mungu amewafanya muusimamie ulimwengu...je mngelifanya nini?"*, siku moja Sunbul Sinan - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliwauliza wanafunzi wake.

*Kila mmoja alitoa jibu lake.*

*"Ningeliwaangamiza makafiri wote", mmoja alijibu.*

*"Ningeliwaangamiza walevi wote", mwingine alijibu.*

*"Nisingelimuacha mvutaji sigara hata mmoja", mwingine alieleza. Muslihiddin Effendi ambaye alikuwa mwanachuoni na mwanafunzi wa Sheikh Sinan alikuwa kimya kwa kitambo. Ukimya wake ulivunjwa na Sheikh ambaye alimgeukia na kumuuliza:*

*"Na wewe...wewe ungelifanya nini?"*

*Muslihiddin Effendi alitoa jibu lifuatalo kwa ukamini:*

*"Mwalimu...Je kuna upungufu katika uwezo na uongozi wa Mwenyezi Mungu mpaka nifikiria kuhusiana na kuwekwa msimamizi mwingine? Ninaweza kujibu kwamba kwa upande wangu ningelikiacha kila kitu kama kilivyo!"*

*Kisha Sunbul Sinan - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alisema yafuatayo kutokana na kufurahishwa na jibu lake:*

*"Sasa hivi suala letu limefika mahala pake (merkez)! (yani sasa hivi swali limepata jibu lake)"*

*Kuanzia siku ile Muslihiddin Effendi akawa anafahamika kwa jina la Merkez Effendi. Na baada ya Sunbul Sinan - Mwenyezi Mungu aitakase siri*





yake – kufariki yeye akawa mrithi wake, akawa anatekeleza majukumu yake ya kiroho.

Katika mukhtasari mwingine wa suala hili Ibrahim Hakki Erzurumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasimulia kujisalimisha kwake kwa Mwenyezi Mungu kama ifuatavyo:

*Kazi zake zote ni tukufu  
Zote ziko sawa sawa  
Chochote afanyacho kinavutia  
Subiri, Ni kipi anachokifanya Mola, na angalia  
Chochote akifanyacho ni kizuri.*

Hivyo kufikia kwenye mwenendo huu mzuri kutawezekana tu baada kuuweka moyoni ubainifu wa sifa za Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kinyume chake hatutakuwa tofauti na kipande cha karatasi chenye kushika kile kina-choandikwa na kuchorwa juu yake. Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema yafuatayo kuhusiana na hili:

*“Kama ungelitakiwa kuchora picha ya mtu mwenye huzuni katika kipande cha karatasi, vyote picha na karatasi visingelitambua huzuni au furaha ya kile kilichochorwa.*

*Ukiangalia kwa juu utaona picha ile ni yenye kuhuzunisha; lakini si picha wala karatasi chenye kulitambua hilo. Picha ya mtu anayetabasamu haina habari juu ya tabasamu lake.”*

Hivyo bila kujali ni kwa kiasi gani tumegubikwa na ubainifu wa sifa takatifu tuliojaaliwa kutokana na kuwa wanadamu, lakini hatutokuwa tofauti na karatasi na picha isiyo na uhai iliyopo juu yake mpaka pale tutakapoutambua ubainifu huo. Hivyo hatuna budi kuyeyusha sifa zote tulizojaaliwa kama sehemu ya mtihani ndani ya chungu cha ubainifu wa sifa takatifu za Mola. Hatuna budi kutambua vyema kwamba yaliyomo katika kila sifa ni mambo yasiyoweza kuelezewa kwa ukamilifu wake. Yote hayana mwanzo (*azali*) wala mwisho (*abadi*). Yote yana ukamilifu kwake na yana ubora usio na kifani. Tunaweza kusema kwamba hakuna sifa yake hata moja ambayo ina mpaka. Kwa hiyo maneno yake, ujuzi wake, Nguvu zake, ubunifu wake na sifa nyingine zote hazina mfano wake wala haziwezi kufafanuliwa kwa ukamilifu. Kwa upande mwingine dunia yetu na vyote vilivyomo vina mipaka na ni vyenye kupita; vitu vyote hivi ni kivuli tu





chenye kudanganya. Angali bado hatujafanikiwa kujielewa sisi wenyewe kwa ukamilifu ni jambo lisiloingia akilini kwa mwanadamu kuweza kuzifahamu vilivyo sifa za Mwenyezi Mungu ambazo ni Zake peke yake. Kama ambavyo hatuwezi kuifahamu vilivyo Dhati ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ndivyo ambavyo hatutaweza kuifahamu vilivyo kila Sifa yake.

Wale waliofanikiwa kukubaliana na ukweli huu na kutambua kuwa uoni wao, usikivu wao, uelewa wao, kuongea kwao na uwezo wao wote mwingine si chochote bali ni katika sehemu ndogo mno ya ubainifu wa sifa za Mwenyezi Mungu wanakuwa ni wenye kuishi katika mazingira ya udhalili huku wakivuta pepo mwanana za hekima zenye kuvuma ndani yake. Kutokana na kutosheka kwao na imani yao hufikia kusema:

لَا مَوْجُودَ إِلَّا هُوَ

“Hakuna mwingine ila Wewe”

Kuzisahihisha akili na nafsi zao ni hekima ya kutambua:

“Mola...Wewe uko kama ulivyo, Vyovyote utakavyokuwa!”

Matokeo yake hurejea kwa Mola wao huku wakiwa na nyoyo safi na huku wakiwa wametajwa ndani ya vitabu vya waja wema.

*“Ni majina yapi ya Mwenyezi Mungu ambayo ni makubwa kuliko yote?” siku moja daruwesh mmoja alimuuliza Bayazid Bistami - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake.*

*“Ni yapi miongoni mwa majina yake ambayo ni madogo? Usiwe mjinga. Majina yote ya Mwenyezi Mungu ni makubwa. Kama unataka akukubalie matakwa yako jitahidi kusafisha moyo wako dhidi ya chochote kile tofauti na Yeye. Majina yake hayajibainishi katika nyoyo ambazo hazijitambui. Lakini katika nyoyo ambazo zimehuishwa na Nuru Yake, Mwenyezi Mungu huzitazama nyoyo hizo kila wakati kwa kuzibainishia majina Yake mengi.”*

Ni kweli kwamba jina la Mwenyezi Mungu limepachikwa ukubwa zaidi katika aya nyingi za Qur’an:

“Basi litakase jina la Mola wako Mlezi aliye Mkubwa” (al-Waqia, 96).

Mtume aliyebarikiwa aliitekeleza amri hii kwa kusema *Subhana Rabbiya’l-Azim* (Ametakasika Mola wangu mtukufu dhidi ya upungufu





wa aina yoyote) pindi anaporukuu ndani ya swala, na kusema *Subhana Rabbiya'l-A'la* (Ametakasika Mola wangu aliye juu dhidi ya upungufu wa aina yoyote) pindi anaposujudu.

**Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie tuwe na ufahamu na upendo mtakatifu juu ya majina Yako mazuri na hasa juu ya jina Lako halisi!**

**Amin...**







**K**wa kuwa mtu aliyekomaa kiimani na ambaye amefikia kwenye marifatullah wakati huu anakuwa amesimama chini ya ubainifu wa mapenzi ya Mola, pia anakuwa ameteketeza matamania yote ya nafsi yake kama ambavyo karatasi inaungua kutokana na miale iliyokusanywa na lenzi kutoka kwenye jua.



### 3. KUMFAHAMU MOLA NA UBAINIFU WAKE KWA WENYE HEKIMA

*Marifatullah* au kumfahamu Mola ni elimu isiyo na mipaka na isiyo na mwisho itokayo kwa Mola, elimu ambayo imebeba siri na hekima zote zilizoenea katika ulimwengu mzima. Jitihada yoyote itakayofanywa kwa ajili ya kuweza kuilezea elimu hiyo itakuwa ni jukumu lililo nje ya uwezo wa kibinadamu. Lakini bado kila mtu hupata sehemu ya elimu hii kulingana na uwezo wake na jitihada zake. Hivyo Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ameomba:

لَا أَحْصِي تَنَاءً عَلَيْكَ أَنْتَ كَمَا أُثْبِتُ عَلَى نَفْسِكَ

“(Mola wangu) Mimi sina uwezo wa kukutukuza na kukusifa kama inavyokustahili! Vyovyote vile ulivyojisifu na kujitukuza ndivyo ulivyo!” (Muslim, Salat, 222).

Katika kuashiria umuhimu wa *marifatullah* pia kuna maneno yafuatayo ya *hadith ali-qudsi*: “Nilikuwa hazina iliyojificha. Nilipenda nifahamike, hivyo nikaumba viumbe ili wanifahamu.”<sup>5</sup>

Baada ya maneno ya Qur’an tukufu na *hadith* na mwenendo wa Mtume aliyebari kiwa – rehema na amani ziwe juu yake – hakuna maneno na tabia nyingine bora zaidi kuliko zile za waja wema wa Mwenyezi Mungu ambao wamefikia kwenye *marifah*, yani hiyo elimu tunayoizungumzia. Hayo yote ni kwa sababu maneno yao na tabia zao za kipekee ni bora mno na ni zile zilizo katika asili ya *ladunni*; kwani ni vigumu kuwa nazo. Ndio maana wanaitwa ‘warithi wa Mitume’ (*warathatu’l-anbiya*).

<sup>5</sup> Rejea Ajluni, *Kashfu’l-Khafa*, II, 132.





Nyoyo za wale wanaoshuhudia tabia za watu hawa wema na kuyasikia maneno yao wanakuwa wamejawa na msukumo wa kiroho. Kutokana na shauku yao kuongezeka hujikuta wamejiweka mbali na miito ya shetani na tamaa za kidunia, kiasi kwamba siri zinakuwa zinajidhihirisha kwao taratibu.

Baadhi ya watu hawa wana tabia kama ya Adam – amani iwe juu yake, wengine kama Ibrahim – amani iwe juu yake. Kuna baadhi ambao wana mwenendo kama wa Musa – amani iwe juu yake, wakati wengine wanafanana na Yesu – amani iwe juu yake. Na kuna wengine ambao wameiga mwenendo wa Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake.

Sifa za kipekee za wale wenye mwenendo wa Muhammad ni kwamba wao ni watu wenye elimu, mapenzi na umoja (*tawhid*). Miongoni mwao kuna wengine ambao huwezi kuwasifa kwa sifa moja ya ujumla, kwani wanakuwa wamejipamba na sifa zote njema. Maelezo zaidi ya hayo yatakuwa ni ziada.

Mola amewabainishia waja hawa mambo mbalimbali kulingana na hali zao kiimani. Amewafanya baadhi yao kuwa Shah Naqshiband, ambao ni bahari za kipekee zisizo na mipaka ndani ya elimu takatifu, na wengine kuwa Majnun huku wakitangatanga kwenye jangwa la mapenzi. Kuna wengine ambao Mola amewafanya watangatanga kwenye mabonde ya wasiwasi na wengine wamenyamazishwa mbele ya Utukufu wake. Wengine wamefanywa kuwa Yunus Emre, ambaye ni ndege mwenye kutoa milio ya upendo, wakati wengine wamekuwa Mawlana Rumi, ambao ndimi zao zinatoa hekima na kusambaza lulu hadimu za imani kote. Kutokana na Mola kuwapa watakatifu wake elimu ya *marifah* na kumpa kila mmoja ubainifu tofauti, anakuwa amewabariki na kuwafanya kuwa nuru za kuwangoza wanadamu wote.

Kwa kuwa mtu aliyekomaa kiimani na ambaye amepata *marifatullah* anakuwa amesimama chini ya ubainifu wa Mola, huteketeza tabia zote chafu ndani ya moyo wake kama inavyoshika moto karatasi iliyowekwa chini ya lenzi. Kutokana na kuwa kwake kitovu cha mwangaza watu wengine huzidisha upendo na heshima juu yake. Kwa kuwa anakuwa amejitoa kwenye matamanio ya kidunia yenye kupita huwa haangukii kwenye dimbwi la kujivuna, kujiona na kujikweza. Ingawa katika jamii yuko pamoja na Mola. Anakuwa yupo kati ya hisia za *tazim li amrillah*, yani kufuata





maamrishi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa unyenyekevu, na *shafqah li khalqil-lah*, yani kuonyesha heshima na upendo kwa viumbe vya Mwenyezi Mungu. Lakini kama ambavyo yanahitaji mapenzi yake kwa Mola, huwa haonyeshi mapenzi na ukaribu kwa madhalimu na watu wasio na fadhila, watu ambao ni kinyume kabisa na yeye. Lakini kama ambavyo huruma yake inamtaka, huwa anawaonea huruma na kuwaombea uongofu juu yao.

Huwa anahitaji utajiri na mali za kidunia ili aweze kuzitumia kwa kutoa sadaka katika njia ya Mwenyezi Mungu. Mtu mkomavu huwa wakati wote anajitolea kutafuta elimu takatifu na kuwa karibu na Mola wake. Kuanzia sasa anakuwa ni mtu mwema mbele ya Mola na anakuwa ni mtu hajali maumivu na tabu za hapa duniani.

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ametumia kisa kifuatacho katika kusisitiza namna uwezo wa kiroho unavyotofautiana miongoni mwa watu, na namna ambavyo kila mtu anajipamba na ubainifu wa Mola uliopo hapa duniani kulingana na hali za nyoyo zao, na namna wengine wanavyoendelea kuwa pamoja na Mola licha ya kuonekana kuwa ndani ya kundi kubwa la watu:

*“Siku moja sufi alienda kwenye bustani lililopendezeshwa kwa ajili ya kuongeza imani na kujiingiza kwenye tafakari nzito. Alivutiwa sana na rangi nzuri za bustani. Kisha akafunga macho yake na kuanza muraqabah na tafakari. Mtu mjinga aliyekuwa akipita pale alifikiri Sufi alikuwa amelala. Huku akiwa ameshangazwa na kukasirishwa na kitendo kile alimkari-pia yule sufi:*

*‘Kwa nini umelala?’ aliuliza. Fungua macho yako na utazame miz-abibu, miti iliyochanua na majani yaliyokoza! Angalia matokeo ya rehema za Mwenyezi Mungu!*

*Yule Sufi akajibu: ‘Tambua kitu kimoja ewe mtu mjinga, moyo ndio kitu kikubwa zaidi katika rehema za Mwenyezi Mungu. Vilivyobaki ni kama kivuli chake. Mkondo wa maji unatiririka katikati ya miti. Kutokana na maji yake unaweza kuona taswira za miti iliyopo katika pande zote mbili. Kilichoakisiwa ndani ya mkondo huo ni ndoto ya bustani. Bustani ya kweli ipo ndani ya moyo, kwani moyo ndio taswira ya mtazamo mtakatifu. Akisi zake nyingi huweza kuonekana ndani ya maisha haya kidunia iliyotengezwa kwa maji na matope. Kama vitu vya dunia hii visingelikuwa taswira za furaha ya moyo, basi Mwenyezi Mungu asingelisema kuwa dunia hii ni seh-emu ya udanganyifu. Qur’an inasema:*





*“Kila nafsi itaonja mauti. Na bila ya shaka mtapewa ujira wenu kaamili Siku ya Kiyama. Na atakaye epushwa na Moto na akatiwa Peponi basi huyo amefuzu. Na maisha ya dunia si kitu ila ni starehe ya udanganyifu” (Al-Imran, 185).*

*Wale wajinga ambao wanaiona dunia kama pepo na kudai ‘hapa ni peponi!’ ndio wale waliodanganywa na starehe za hii dunia. Wale waja wema wa Mwenyezi Mungu walioachwa mbali na mabustani ya kweli nao wameegemea kwenye ndoto hii ya mchana na hivyo kudanganyika. Itafika siku ambayo usingizi huu wa ujinga utafikia mwisho. Macho yatafunguka na ukweli utaonekana. Lakini kuna faida gani kuyaona hayo katika pumzi ya mwisho? Furaha kubwa iko kwa yule aliyekufa kabla ya mauti kumfika na ambaye roho yake imepata harufu ya ukweli wa bustani hii...”*

Na bila shaka mtu hana budi kupuuzia raha za dunia ambazo zinaishawishi nafsi na badala yake ajiweke nazo mbali, kwa kufanya hivyo kutapelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu aitakase roho yake na kuuongoa moyo wake.

*Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ali-  
posema, “Moyo ambao utatembelwa na nuru utafunguka na kutanuka”,  
maswahaba walimuuliza, “Dalili yake ni ipi ewe Mjumbe wa Mwenyezi  
Mungu?” Jibu lilikuwa:*

*“Kujiweka mbali na hii dunia yenye kupita, kufanya jitihada kwa ajili  
ya maisha ya milele ya akhera na kujiandaa na kifo kabla ya kufikwa nacho”  
(Tabari, Tafsir, VIII, 37).*

Nyoyo za wasafiri hawa watiifu katika njia hii ya marifah ni kama lulumizi zenye kutoa lulu kubwa kuliko matone ya mvua za mwezi wa nne. Huwa hazipunguzi ukubwa wa lulu za nyoyo zenye kuzipenda ilimradi zinaelewa tone la mvua ambalo linastahili kuachwa ndani ya lulumizi hilo!

Katika sherehe ya *Mathnawi* inasemekana kwamba:

*“Mwenyezi Mungu ambaye ndiye mmiliki wa maneno aliyandong’oneza  
mawingu siri kisha machozi yakaanza kumiminika kutoka kwenye macho  
yake katika mfano wa mfuko wa maji ulio mtupu. Alinong’oneza siri kwenye  
sikio la waridi na kulipamba kwa rangi na harufu nzuri. Alilinong’oneza jiwe  
siri na kulibadilisha kuwa ageti miongoni mwa madini yote. Hivyo tunaweza  
kusema kwamba Mola alibainisha sifa yake ya al-Latif (Mpambanauaji,*





*Mwingi wa rehemu) na kuyafanya mawingu yamwage mvua, na kulifanya waridi liwe ni lenye kupendeza na jiwe kuvutia.*

*Pia Mola aliunong'onezea mwili wa mwanadamu siri na kuujalia marifah ule ulioweza kuitunza siri hiyo. Watu hawa wamekuwa karibu na Mola kutokana na kunusuriwa dhidi ya matamano ya kidunia”*

Bila shaka siri hizi ni siri za upendo, upendo kwa kupitia ubainifu wa aina mbalimbali unaweza kukufikisha kwenye *marifah*. Katika mazingira ya msukumo wake siri ya upendo huficha ukamilifu na uzuri wa kila kitu.

Wale watakatiifu wa daraja la juu hubainikiwa na mapenzi hayo ya msingi kwa kiwango kikubwa zaidi. Kwa maana ya kawaida mapenzi ya msingi ni pale mtu anapopendana na mwenzake bila ya kukusudia na kujenga naye muungano wa mapenzi. Lakini kwa maana halisi mapenzi ya msingi ni kumpenda Mola kwa namna hiyo hiyo na kuangamia kwake.

Watu wema ambao wamejaaliwa kupata ubainifu wa mapenzi ya msingi si wale watu wanaopenda pindi mambo yanapowaendea vizuri na kupunguza mapenzi pale mambo yanapowaendea vibaya. Kisa kifuatacho kinatoa mfano mzuri juu ya mapenzi ya msingi:

Mawlana Jami - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasimulia:

*“Kulikuwa na kijana mmoja ambaye alikuwa akifulululiza kuhudhuria kwenye mikusanyiko ya mwalimu wetu Sadaddin Kashgari. Alikuwa juu katika heshima, tafakuri na mapenzi. Lakini ilifika siku ambayo alimpenda mwanamke mmoja mzuri kama ilivyokuwa kwangu; na kwa wakati ule mfupi akamhamishia mwanamke yule hazina yake yote aliyokuwa ameikusanya mpaka wakati ule.*

*Siku moja alinunua zawadi ya dhahabu na almasi na kuiacha katika njia ambayo mwanamke yule alikuwa akipita mara kwa mara na wakati huo huo akajificha mahali ili kuhakikisha hakuna mtu mwingine anayei-kota. Alifikiria kwamba kipenzi chake kingeliokota zawadi ile bila ya kujua kuwa imetoka kwa nani na kwa nini iliachwa pale. Nilipolisikia jambo hili nilimwambia:*

*‘Ni kitu gani hicho cha ajabu unachokifanya! Unakiacha kwenye njia yake kile ulichotumia jitihada kubwa katika kukitafuta! Hata kama ataiona na kuikota lakini bado hatajua imetoka kwa nani na ni kwa nini imeachwa*





*pale. Angalau weka alama ili afahamu kuwa imetoka kwako!*

*Kijana yule akajibu kwa mshangao huku machozi yakimtoka: “Unaongelea nini? Unafikiri sifahamu ni kiasi gani hiki ninachokifanya ni chenye kustaajibisha? Sitegemei fadhila kutoka kwake, kwani sitaki kumsumbua kwa kumfanya awe karibu na mimi kwa sababu ya zawadi zile!”*

*Nilistaajibishwa na kufikiria kwamba ikiwa mapenzi aliyonayo mtu kwa kiumbe yanaweza kufikia katika uzito na uzuri wa kiasi hiki, si jambo la kubahatisha ili kufahamu ni uzuri kiasi gani utakaokuwa kwenye ubainifu utakaokuwepo katika wale walioingia kwenye ‘mapenzi ya msingi’.*

Katika kuelezea hatua za kiroho za moyo kwa kukumbuka uzoefu wake binafsi na hatua za kiroho alizopitia Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ametumia neno *ghafi* katika kipindi alichokuwa *dersiam* (Profesa) katika Madrasa ya Seljuk alipokuwa anasimamia vitabu vihusavyo mambo yawezayo kufahamika na watu wote, na alitumia neno *aliyepikwa* kuashiria kipindi alichopokea ubainifu wa elimu takatifu, wakati ambao siri za ulimwengu zilifunuliwa kwake, na alitumia neno *aliyeunguzwa* wakati alipokuwa katika hali ya kuungua kinadharia mpaka kuwa majivu ndani ya moto wa mapenzi ya msingi.

Kufikia kwenye *marifatullah* kutawezekana tu kwa kupitia imani thabiti juu ya Dhati ya Mola na uelewa juu ya ubainifu mtakatifu, kwa kadiri uwezo wa kibinadamu unavyoruhusu.

**Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie tuzitumie vizuri neema ulizotujaalia! Tujaalie tuwe na amali njema za kutosha kutuwezesha kupokea rehema zako nyingi kesho akhera! Zijaalie nyoyo zetu zifikie katika hatua ambazo zitaziwezesha kudhihirikiwa na ubainifu wa Mapenzi Yako! Tujaalie tuitambua siri ya kuumbwa kwetu katika ‘umbile lililo bora’ ili tuweze kuzihuisha nyoyo zetu kwa umande wa Huruma Yako!**

**Amin...**





**K**uzipata zawadi takatifu kunategemeana na kilichopo ndani ya moyo.



## B. MALIPO MATAKATIFU

Vyote vyenye kuishi isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu vimeumbwa kwa kupitia ubainifu wa Sifa Yake ya *al-Latif* (Mwingi wa rehema); kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba vimeumbwa kwa rehema zake. Hakuna kiumbe yeyote ambaye amekuja hapa duniani baada ya kulipia chochote. Uwepo wote wa viumbe pamoja na sifa zao na hekima zipatikanazo kutokana na kuumbwa kwao, hauna budi kuelezewa kuwa vyote hivyo ni zawadi takatifu<sup>6</sup>. Hili linamaanisha kuwa uwepo wa vyote vilivyopo hapa ulimwenguni si chochote bali rehema, ukarimu na fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Ingawa uwepo wa viumbe vyote na sifa walizonazo ni matokeo ya ‘zawadi takatifu’ lakini sisi tutayatumia maneno haya kumaanisha fadhila wanazopokea wale wanaosafiri katika barabara ya usufi ukilinganisha na umbali wanaoutumia. Watu wenye vipaji huanza kupokea fadhila na sifa za kipekee kadiri wanavyosonga mbele katika njia hii, hata kabla hawajafika kwenye ‘ulimwengu mwingine’. Hata kama atafikiria kuwa upokeaji wa zawadi hizi takatifu ni suala lenye kuwastahili - kwa kuwa mtu hutumia maamuzi yake kuingia kwenye njia hii-, lakini katika siku ya hesabu rehema itautawala ustahilifu, ndio maana imekuwa kawaida kutumia neno ‘zawadi’ katika kuashiria fadhila hizi tulizopewa na Mola. Tofauti kubwa iliyopo kati ya kuzawadiwa kitu na kustahili kitu hicho imepelekea kufanya ustahilifu usiwepo. Suala hili si la kupuuziwa, hasa ukizingatia kuwa fursa aliyopewa mtu ili kustahili kitu fulani pia nayo kimsingi ni ‘zawadi takatifu’.

Baadhi ya watu wenye uwezo ambao hupanda daraja la kiroho kwa kupitia mafunzo ya *tasawwuf* hupata maarifa mengi katika safari hii ya

6. Zawadi takatifu (*mawhibatu 'l-ilahiyah*): Fadhila na rehema takatifu.





kiroho. Kiasi kwamba hekima za mafumbo mengi hunufunuliwa kwao na vifundo vingi hufunguliwa. Kilichokuwa hakifahamiki hapo kabla sasa kinakuwa kinafahamika, mafumbo hufumbuliwa. Uongofu ambao humulika kwenye moyo safi humfanya mwenye nao kumfahamu Mola wake vilivyo na kufahamu uhalisia wa mambo mbalimbali. Ndoto zenye ukweli zitokanazo na Ubao uliohifadhiwa (*Lawh-i Mahfuz*) ambazo zinaakisi utambuzi wa mambo yajayo kwenye nyoyo huanza kuonekana. Wenye nyoyo hizo hupata mazingatio makubwa na utambuzi ambao hupelekea kuliona lengo takatifu katika kila kitu wanachokiangalia.

Hali hizi ambazo zinapatikana kwa kupitia rehema takatifu inayo-ambatana na jitihada ya kweli huja katika aina mbalimbali za ubainifu. Zinapoelezewa katika hali ya ujuzi huwa zinaitwa *ladunni*. Ingawa maudhui yake yanavuka uwezo wa kibinadamu wa utambuzi wa mambo lakini wale waliojaaliwa kupata sehemu ya elimu ya *ladunni* kwa kupitia rehema na huruma ya Mola wakati huo huo hupata utambuzi na uelewa wa hali ya juu kulingana na jitihada walizozifanya. Tutajaribu kuelezea kwa mapana zaidi sifa za elimu hii ya *ladunni* kadiri uwezo wa kibinadamu unavyoruhusu na kadiri dini inavyoruhusu.







**P**indi ninapompenda mja wangu ninakuwa ulimi wake anaongelea, moyo wake anaotambulia mambo, masikio yake anayosikilizia, macho yake anayotazamia, mikono yenye kushikia na miguu yenye kutembelea. Humpa chochote atakacho kutoka kwangu. Kama anatafuta ulinzi kutoka kwangu, Ninamlinda. (Hadith al-Qudsi, Bukhari, Riqaaq, 38)



## 1. ELIMU YA LADUNNI

Aina hii maalum ya elimu inatoka kwa Mwenyezi Mungu moja kwa moja, na ni zawadi. Kwa kurejea ni kwamba Qur'an inatumia maneno "elimu itokayo kwetu".<sup>7</sup> Neno *ladunni* lenye maana ya 'kutoka kwetu' linatoka hapo.

Siri alizozifunua Mola kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – zipo katika makundi matatu. Kundi la kwanza limebeba siri ambazo zinaweza kutambuliwa kwa msaada wa nuru ya utume; Hivyo zimebakia kuwa siri kati ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mjumbe wake. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – hakuwahi kuzitoa siri hizi kwa yeyote miongoni mwa maswahaba zake.

Siri hizi ambazo kufunuliwa kwake hakuruhusiwi wala hakuwezekani – kwani hata kama zingelifunuliwa kwetu tusingeliweza kuzielewa – uwepo wake unaweza kukusanywa kutoka katika maneno mbalimbali ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

"Kama mngelifahamu kile ninachokifahamu mimi, mngelicheka kidogo na kulia sana", Mjumbe mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaambia maswahaba zake. (Bukhari, Kusuf, 2; Muslim, Salat, 112) .

Na katika *hadith* nyingine anasema, "Kuna vitu ninaambiwa na Mola wangu, vitu ambavyo si malaika wa karibu (*muqarrab*) wala mtume ambaye anaweza kuvielewa." (Munawi, Fayzu'l-Qadir, IV, 8).

Kuna kundi la pili la siri hizo ambazo Mwenyezi Mungu amemfunulia Mtume wake, siri hizo zinaweza kueleweka na watu wachache tu waliochaguliwa na ambao wamejaaliwa uwezo mkubwa wa kiroho na kiakili,

<sup>7</sup> Rejea al-Kahf, 65.





watu hawa wanaitwa *khawas* na *khawasul-khawas*.<sup>8</sup> Siri za aina hii ni zile ambazo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwafunulia maswahaba wakubwa wachache mfano wa Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Usambaaji wake kutoka moyo mmoja mpaka mwingine ni desturi. Kama zingelikuwa zimeandikwa kwenye vitabu zingeliweza kuangukia kwenye mikono ya watu wasio na uwezo wa kuzielewa, hili lingelipelekea watu hao kuzitafsiri kimakosa na hatimae kuangukia kwenye makosa. Kuwepo kwake pale zilipo zinamuwajibisha kila mtu kuzitafuta na kuzielewa kadiri ya uwezo wake.

Kundi la tatu la siri alizofunuliwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – limebeba siri za dini au sheria (*shariah*). Kundi hili la siri linawahusu wanadamu wote na wanawajibika kuzifanyia kazi. Kwa kuwa siri hizi zinawahusu wanadamu wote, Mwenyezi Mungu amezingatia kwamba kuna madhaifu na hivyo amezifanya ziweze kutekelezwa kiurahisi na watu hao. Na kwa kuwa zinahitajika na kila mtu, zimetangazwa kwenye ulimwengu mzima ili umuhimu wake utambulike.

Mara kwa mara Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiwafahamisha maswahaba zake juu ya matukio yaliyopangwa kutokea mpaka siku ya kياما, lakini bado wengi wao hawakuwa wakiyaelewa vizuri. Kuna wengine ambao walikuwa wakiishia kuyasahau.<sup>9</sup>

Kinyume na haya ni jambo linalofahamika kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliwafunulia baadhi ya maswahaba zake wakubwa siri nyingi zilizokuwa ngumu kueleweka, na maswahaba hao wakazisambaza kwa wengine waliokuwa na uwezo kama wao. Siri hizi hazihitajiwi na watu wote ukizingatia kuwa ziko katika hali ambayo inazidi utambuzi wa watu wengi. Usambaaji wake miongoni mwa watu wenye uwezo mkubwa wa kiimani haupitii kwenye mihadhara ya wazi bali ni kutoka kwenye moyo wa mtu mmoja na kwenda kwa mwingine; yani kutoka kwa mtu mmoja mwenye imani ya juu mpaka kwa mwingine kama huyo. Na kihistoria hivi ndivyo desturi hii ilivyoweza kubakia mpaka leo.

Zaidi ya Abu Bakr and Ali, Ibn Masud, Abu Hurayrah, Muadh

8 *Khawas*: Waja wema waliochaguliwa. *Khawasul-Khawas*: Waliochaguliwa kwenye miongoni mwa waliochaguliwa; yani zao la mbegu.

9 Rejea Bukhari, Qadar, 4.





ibn Jabal and Harith ibn Malik – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao– kuna maswahaba wengine ambao walipokea baadhi ya siri za aina hii.



Mwenyezi Mungu ameandaa vitu ambavyo havijapata kuonekana kwa macho na ambavyo haviwezi kudhaniwa na mwanadamu wa kawaida, vyote hivi ni kwa ajili ya waja wake waliomtii kwa usahihi na kufanikiwa kuyafanya matamaniao yao yote yawe ni kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ametufunulia ndani ya Qur’an kwamba huwapa elimu na hekima maalum wale waja wake walio wema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَلْ لَكُمْ فُرْقَانًا  
وَ يُكَفِّرْ عَنْكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَ يَغْفِرْ لَكُمْ وَ اللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ

“Enyi mlio amini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atakupeni kipambanuo, na atakufutieni makosa, na atakusameheni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa” (al-Anfal, 29).

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na muaminini Mtume wake, atakupeni sehemu mbili katika rehema yake, na atakujaalieni muwe na nuru ya kwenda nayo. Na atakusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu” (al-Hadid, 28).

*Hadith* inasema:

“Yule mwenye kukifanyia kazi kile anachokifahamu Mwenyezi Mungu atamfundisha kile asichokifahamu” (Abu Nuaym, Hilyatu’l-Awliya, X, 15).

Na *hadith al-qudsi* nayo inasema:

“Yeyote atakayemfanyia uadui mmoja miongoni mwa waja wangu wema nitatangaza vita dhidi yake. Mja wangu hatakuwa karibu na Mimi kwa kupitia njia yoyote yenye kupendeza zaidi ya kutekeleza matendo ya faradhi niliyomuamrisha kuyatenda. Na ataendelea kuwa karibu na Mimi kwa kupitia matendo ya sunnah mpaka nitampenda. Na pindi nitakapompenda nitakuwa macho yake anayotazamia, masikio yake anayosikilizia,





*mikono yake anayoshikia na miguu yake anayotembelea. Kisha ninampa chochote atakacho kutoka kwangu. Na kama atatafuta ulinzi kutoka kwangu, Nitamlinda. (Bukhari, Riqaq, 38).*

Kama inavyofahamika, kutekeleza matendo ya *sunnah* kwa mapenzi baada ya kutekeleza matendo ya faradhi kwa ukamilifu huwa sababu ya mja kupata baraka hizo na zawadi za Mwenyezi Mungu. Hivyo kwa sababu hii hatuna budi kujiepusha na matamania ya nafsi na kujichunga dhidi ya mambo ya haramu na yenye kutia mashaka, na wakati huo huo kushikamana na *sunnah* katika maisha yetu. Raha za kimwili hazina budi kuwa katika njia inayoruhusiwa, hili litamuwezesha mja kufikia kwenye daraja la juu la kiimani. Cha msingi ni kwamba pindi utakapopata baraka za Mola utanyanyuliwa mapazia ya siri, ukweli na hekima. Utapata umakini katika maamuzi yako na utambuzi wako. Matamania ya kidunia na muonekano wa nje wa vitu havitaweza kumdanganya mtu aliyezama kwa Mwenyezi Mungu. Baada ya hapo ataanza kugundua sababu zilizojificha za mambo yote yanayotokea hapa ulimwenguni pamoja na kupata utambuzi wa hali ya juu.

Pamoja na kuwa na uwezo wa kutoa maamuzi sahihi na kuwa na utambuzi wa mambo mbalimbali yanayotokana na msukumo wa moyo, lakini pia kuna fikra muhimu zinazokuja kichwani, ujumbe muhimu unaohusu ulimwengu wa roho, mara nyingi ujumbe huu hausambazwi sana katika maneno bali kwa kupitia alama. Alama hizi zinaitwa *latifah* au *lataif* katika wingi. Hizi ni alama zenye kuongoza ambazo Mola huwapa waja wake wenye kujitahidi kufuata njia ya imani.

Pia Mwenyezi Mungu anaweza kuwasaidia waja wake wema wakati wa shida kwa kuwatahadharisha kwa kutumia sauti isiyosikika. Sauti hizi zimekuwa zikiitwa *Khatif*, kwa kumaanisha sauti ya siri itokayo mahali pasipofahamika na kutoka muongaji ambaye haonekani.<sup>10</sup> Hizo ni sauti ziibukazo ndani ya moyo wa muumini aliye katika njia ya kisufi ambayo inamsogeza mtu kwa Mola wake.

Tukio lifuatalo ni lenye kuthibitisha ukweli wa sauti hizi zilizojificha:

*Pindi maswahaba walipotaka kuiosha maiti ya Mtume aliyebarikwa – rehemu na amani ziwe juu yake – baada ya kufa kwake, walikuwa hawana*





*uhakika ikiwa walitakiwa kumvua shati lake kama walivyokuwa wakifanyiwa watu wengine au aoshwe huku shati lake likiwa mwilini mwake. Kisha sauti ilisikika kutoka wasipopajua ikiwaambia wasimvue shati lake, hivyo kutuliza akili za maswahaba.<sup>11</sup>*

Mwenyezi Mungu mtukufu amewafundisha wanadamu ‘Kitabu’ na ‘Hekima’ kwa kupitia Mitume yake. Mafunzo haya wakati mwingine yamekuwa yakitolewa kwa wazi na wakati mwingine kama *ladunni*, yani katika hali ya msukumo wenye kuungazia moyo. Lakini kama tulivyokwishasema hapo kabla, hali hizi ni zenye kusambazwa katika njia ambayo ni vigumu kwa mwanadamu wa kawaida kuzielewa kwa urahisi, hivyo zimebakiwa kuwa siri kwa watu wengi. Hata hivyo vyote Qur’an na *Sunnah* vinathibitisha ukweli na uhalisia wa elimu hiyo ya *ladunni*. Tukio lifuatalo lenye kuwakutanisha Musa na Khidhir – amani iwe juu yao, tukio ambalo limesimuliwa ndani ya Qur’an<sup>12</sup> na kwenye baadhi ya maneno ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – linatoa mwangaza mzuri juu ya namna inavyokuwa elimu hii ya *ladunni*:

*Pindi Firauni na jeshi lake walipokuwa wakimfuata Musa – amani iwe juu yake – pamoja na waumini aliangamizwa ndani ya mawimbi makali ya bahari nyekundu mbele ya macho ya waizraeli. Baada ya tukio hili Musa – amani iwe juu yake – aliwakusanya watu wake na kuwatolea hotuba kali na yenye kushawishi, na hivyo kuyeyusha nyoyo za wasikilizaji na kuwapelekea wabubujikwe na machozi. Iliwafanya wastaajabu juu ya kiwango kikubwa cha elimu na hekima ya Mtume wao. Kutokana na msukumo wa maongezi yale, mmoja wao akauliza:*

*“Mjumbe wa Mwenyezi Mungu...Je kuna mtu mwenye elimu kubwa kuliko yako kwenye uso wa dunia hii?”*

*Kutokana na kutekwa na swali lile, badala ya kujibu “Mwenyezi Mungu anajua”, Musa – amani iwe juu yake – akajibu, “Hapana...Sifahamu kama kuna yeyote aliye hivyo”. Hivyo akawa ameteleza.<sup>13</sup> Mwenyezi Mungu hakukubaliana na jibu lake, hivyo pale pale akamfunulia Mjumbe wake huyo*

11 Rejea Abu Dawud, Janaiz, 27-28; Ahmed ibn Hanbal, VI, 267; Ibn Majah, Janaiz, 10.

12 Rejea al-Kahf, 60-82.

13 Kuteleza au *dhallah* kama ambavyo kunaitwa kunaashiria maneno au matendo ambayo hufanywa na Mitume mara chache sana bila ya kukusudia, lakini matendo hayo au maneno hayo yakawa hayapendezi mbele ya Mwenyezi Mungu.





juu ya “...mja aliyekuwapo mahali ambapo bahari mbili zinakutana, mja ambaye ana elimu kuliko wewe. Nimempa elimu kutoka kwangu (ladunni).”

Huku akiwa na shauku kubwa ya kujifunza elimu hii, Musa – amani iwe juu yake – akasema, “Sitoacha kuendelea mpaka nifike zinapo kutana bahari mbili, au nitaendelea kwa muda mrefu.” (al-Kahf, 60).

Aliamua kuanza safari huku akiwa ameongozana na mpwa wake aitwaye Yusha ibn Nun. Baada ya kupitia misukosuko mingi katika safari yao mwishowe wakampata mtu waliyekuwa wanamtafuta. Qur’an inayaelezea makutano hayo kama ifuatavyo:

“Basi wakamkuta mja katika waja wangu tuliye mpa rehema kutoka kwetu, na tukamfunza mafunzo yaliyo toka kwetu.” (al-Kahf, 65).

Mtu ambaye Musa – amani iwe juu yake – alifahamishwa habari zake kwa kupitia ufunuo alikuwa amekaa juu ya jiwe huku akiwa amejigubika joho la kijani. Musa – amani iwe juu yake – alimsogelea na kumsalimia, kisha akamwambia, “Mimi ni Musa”.

“Kwa hiyo wewe ndiye Musa, Mtume wa wana wa Izraeli”, Khidhir – amani iwe juu yake – alijibu.<sup>14</sup>

“Je wewe ndiye mtu ambaye Mwenyezi Mungu ameniambia ana elimu kuliko watu wote?” Musa – amani iwe juu yake – aliuliza.

“Mwenyezi Mungu amekupa elimu ambayo mimi sina”, alijibu, “na mimi nimepewa elimu ambayo wewe Musa hunu”.

“Nikufuate ili unifunze katika ule uwongofu ulio funzwa wewe?” (al-Kahf, 66), kisha Musa – amani iwe juu yake – alisisitiza.

Hivyo ndivyo ambavyo Musa – amani iwe juu yake – alivyodhihirisha shauku yake ya kufundishwa na Khidhir – amani iwe juu yake. Kama ina-

14 *Khidr*, katika kiarabu, neno hili linamaanisha kijani au kitu kinachohusiana na rangi ya kijani. Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Sababu ya yeye kuitwa khidr ni kwamba kila alipokuwa akikaa kwenye majani ya njano yalikuwa yakibadilika na kuwa ya kijani.” (Bukhari, Anbiya, 27; Tirmidhi, *Tafsir*, 18; Daylami, *Musnad*, 1,345). Mujahid ambaye ni mwanachuoni mkubwa amesimuliwa kwamba, “kila aliposimama kwa ajili ya kutekeleza swala ya faradhi maeneo yaliyomzunguka yalikuwa yakigeuka na kuwa ya kijani. “ Hivyo imeeleweka kwamba jina khidr halikuwa jina lake halisi bali lilikuwa ni jina la kupanga alilokuwa amepewa hapo baadae.





vyoweza kuonekana katika aya hii ya Qur'an, sharti la kwanza na muhimu la kupata elimu hii ni kuwa tayari kufuata; kwani elimu hii husambaa kutoka moyo mmoja kwenda kwenye mwingine, jambo ambalo linahitaji mfuatano wa kimwili na kiroho. Na hivi ndivyo inavyoendelea:

*Musa – amani iwe juu yake – alitaka kupata uwezo wa kutambua hekima za ndani za matukio yaliyokuwa yakionekana kwa nje kuwa ni yenye kustaaajabisha na ambayo ni vigumu kuyaelewa. Hivyo Khidhir – amani iwe juu yake – akamwambia, “Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami. Na utawezaje kuvumilia yale usiyo yajua vilivyo undani wake?” (al-Kahf, 67-68).*

*Kwa kupitia maneno haya Khidhir – amani iwe juu yake – alikuwa kwanza kabisa amegundua kitu kuhusiana na hali ya kisaikolojia ya Musa – amani iwe juu yake; hasa alikuwa akimuelezea namna alivyokuwa, maneno ambayo yalikuwa yanahitajika kuthibitishwa mwishoni kuwa yalikuwa sahihi. Licha ya yote hayo, elimu hii ilikuwa inahitaji subira na Musa – amani iwe juu yake – alikuwa anatoka katika maisha yenye ghasia. Somo ambalo Musa – amani iwe juu yake – alikuwa alipate lilikuwa ni kushindwa kwake kuvumilia mbele ya sayansi ya uhalisia mtakatifu.*

*Kisha Musa – amani iwe juu yake – akasisitiza kuungana naye. “Akasema: Inshaallah, Mwenyezi Mungu akipenda, utaniona mvumilivu, wala sitoasi amri yako.” (al-Kahf, 69).*

*“Basi ukinifuata usiniulize kitu mpaka mimi nianze kukutajia.” (al-Kahf, 70), Khidhir – amani iwe juu yake – alimsihi.*

*Kisha wakatembea kwenye ufukwe kwa muda kidogo na kisha wakapanda meli iliyokuwa ikimilikiwa na ndugu wawili. Watu hawa wawili waliruhusiwa kusafiri bila ya kulipia chochote. Licha ya hilo lakini Khidhir – amani iwe juu yake – alianza kutoboa sehemu ya chini ya meli hiyo.*

*“Je unataka kutuhilikisha watu wote sisi tulio ndani ya meli?” Musa – amani iwe juu yake – alipinga kwa hasira. “Kwa nini umefanya hivyo?” Wamiliki wa meli hii ni watu wawili masikini na meli hii ndiyo chanzo chao cha pekee cha kuwaingizia kipato. Kwa kweli umefanya kitu cha kustaaajabisha!”*

*Khidhir – amani iwe juu yake – hakusema chochote zaidi ya kumkumbusha Musa – amani iwe juu yake – juu ya tahadhari yake ya hapo awali.*





*“Je sikukuambia kuwa hutaweza kuvumilia kuwa pamoja na mimi?”*

*“Usinichukulie kwa niliyo sahai, wala usinipe uzito kwa jambo langu.”*  
*Musa – amani iwe juu yake – alisema kwa namna ya kuomba radhi.*

*Muda si mrefu shorewanda alikuja na kutua kwenye upande mmoja wa meli yao. Baada ya muda mfupi akadonoa matone kadhaa ya maji ya bahari. Kisha Khidhir – amani iwe juu yake – akamgeukia Musa – amani iwe juu yake – na kumwambia: “Ufahamu wako, wangu na wa viumbe vyote ukiulinganisha na Ujuzi wa Mwenyezi Mungu ni kama kiasi cha maji yaliy-odonolewa baharini na huyo ndege*

*Baada ya muda kidogo wakashuka kutoka kwenye meli na kuanza kutembea kwa miguu. Muda si mrefu wakakutana na mtoto wa kiume. Khidhir – amani iwe juu yake – akamuua mtoto yule pale pale.*

*“Ala!” Musa – amani iwe juu yake – aliamaki. “Umemuuwa mtu asiye na kosa, na wala hakuuwa! Ama hakika umefanya jambo baya kabisa!”*

*“Je sikukuambia kuwa hutaweza kuvumilia kuwa pamoja na mimi?”*  
*Khidhir – amani iwe juu yake – alijibu. Huku akiona aibu kutokana na kushindwa kwake kuchunga ahadi yake, Musa – amani iwe juu yake – alisema:*

*“Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami, kwani ume-kwisha pata udhuru kwangu!”*

*Kisha wakaendelea na safari yao mpaka walipofikia kwenye kijiji. Kutokana na kuhisi kwao njaa waliamua kuwaomba wanakijiji chochote kwa ajili ya kula. Licha ya wanakijiji wale kuwanyima chakula lakini pia hawakuwatendea wema wowote. Walipokaribia kuondoka pale kijijini Khidhir – amani iwe juu yake – aligundua kuwa kulikuwa na ukuta ulio-taka kudondoka, ukuta huo ulitengenezwa kwa matofali ya matope. Hivyo akachukua jukumu la kuujenga tena upya. Musa – amani iwe juu yake – akashindwa kuvumilia, hivyo akasema:*

*“Unawahudumia watu ambao walikataa kutukaribisha na hawaku-tupatia hata mkate kidogo wa kutuliza njaa yetu...Angalau ungeliswaomba ujira wa kazi yako!”*

*“Muda umefika kwa sisi kufarikiana”, Khidhir – amani iwe juu yake – alijibu. “Sasa nitakueleza maana ya yale uliyo kuwa huwezi kuyastahamia:*







*Ama ile jahazi ilikuwa ya masikini za Mungu wafanyao kazi baharini. Nilitaka kuiharibu, kwani nyuma yao alikuwako mfalme aliyekuwa anayachukua kwa nguvu majahazi yote mazuri.*

*Na yule mtoto...alikuwa awe muasi baadae. Kwa upande mwingine wazazi wake walikuwa ni watu wema. Tukakhofu asiye watia mashakani kwa uasi na ukafiri. Basi tulitaka Mola wao Mlezi awabadilishie aliye bora zaidi kuliko huyo kwa kutakasika, na aliye karibu zaidi kwa huruma.*

*Na ule ukuta niliousimamisha...ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini. Na chini yake ilikuwako khazina yao; na baba yao alikuwa ni mtu mwema. Basi Mola wako Mlezi alitaka wafikie utu uzima na wajitolee khazina yao wenyewe, kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Wala mimi sikutenda hayo kwa amri yangu. Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria.”<sup>15</sup>*

Maelezo mengi na sherehe zimeandikwa kuhusiana na hekima za ndani zilizopo kwenye makutano hayo. Tunaweza kuelezea baadhi yake kama ifuatavyo:

Elimu ya *ladunni* inahusiana na kuyatazama mambo yaliyo nje ya uwezo wa mwanadamu kwa namna ambayo wengi hawaifahamu. Kwa mfano wakati kuuliza maswali kunachukuliwa kuwa ni ufunguo wa kujifunza katika sayansi zote, lakini elimu hii haistahimili maswali wala mjadala. Badala yake inashauri ukimya, subira na utii. Majibu yake hupatikana mwisho wa mambo yote. Ibrahim Hakki Erzurumi analielezea suala hili kwa namna iliyo nzuri kama ifuatavyo:

*Watoaji wa kweli huwathamini waovu  
Na kuwadhania kuwa wanaweza kubadilika  
Kuangalia mbele ni kwa wenye busara  
Subiri, nini atakifanya Mola, na angalia  
Anachokifanya, hukifanya kwa ubora wa hali ya juu.*

*Usiulize ‘kwa nini hiki ni kibaya?’  
Kitakuwa tu kizuri  
Wewe subiri tu mpaka mwisho, na angalia  
Subiri, nini atakifanya Mola, na angalia  
Anachokifanya, hukifanya kwa ubora wa hali ya juu.*

<sup>15</sup> Ukitaka hadithi zinazohusiana na tukio hili rejea Bukhari, Tafsir, 18/4; Muslim, Fadail, 170.





Wale ndugu wema wa baharini waliwaruhusu Musa na Khidhir – amani iwe juu yao – wasafirie kwenye meli yao bure. Kwa kuwapa msaada mdogo watu wawili wema mwishowe walipata baraka kubwa ya kulindiwa meli yao kwa gharama ndogo mno ya uharibifu wenye kuweza kurekebishwa kwa wepesi. Kwa maneno mengine kipato cha halali na utoaji wa huduma nzuri havikwenda patupu.

Kwa upande wa uelewa wa *ishari*, au katika tafsiri yake ya masuala ya kiroho, ni kwamba kupata madhara madogo kwa ile meli na hatimaye kulindwa dhidi ya kukamatwa kwa nguvu na mfalme kunaashiria ukweli kwamba kuiona nafsi kuwa haina kasoro kutampelekea mtu kwenye maangamizi ndani ya dimbwi la kiburi na kujiona; na kwamba mtu hana budi kuendelea kukiri kasoro zake na udhaifu wake ili ajilinde dhidi ya kuharibiwa imani yake.

Vile vile kuna hekima nyingi juu ya mauaji ya yule mtoto asiyekuwa na hatia yaliyofanywa na Khidhir – amani iwe juu yake.

Mtu hana budi kuhakikisha kuwa mapenzi yake ya kawaida juu ya mkewe, watoto, marafiki na ndugu yanabakia katika mahala pake husika na hayaruhusiwi kupita mapenzi ya mja juu ya Mola wake. Kinyume chake yatamrudisha nyuma na hata kufikia kumtoa katika lengo lake la kweli.

Moja wapo ya majina makubwa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ni *ar-Raqib*, lenye kuashiria kutoridhika kwake pindi aonapo hata kivuli cha mapenzi ya watu wengine kikiyafunika mapenzi juu Yake katika nyoyo za wale anaowapenda. Kwa maneno mengine ni kwamba mapenzi matakatifu hayaruhusu ushirika.

Kuna wakati Yaqub – amani iwe juu yake – alionyesha mapenzi makubwa kwa mwanae Yusuf – amani iwe juu yake, hasa baada ya kupata kwake nuru ya utume kwenye paji lake la uso. Lakini mapenzi yake yaliyopindukia juu ya mwanae hayakujali Uwezo mtakatifu. Hivyo Mwenyezi Mungu akaamua Yaqub – amani iwe juu yake – apitie kwenye majaribu. Matokeo yake yanafahamika vyema: miaka mingi ya kutengana na mwanae kipenzi. Mapenzi yale ya kupindukia yalisababisha utengano wenye kuumiza.<sup>16</sup>





Kwa kupitia urithi wa kijamii baadhi ya vitu vya kweli huwa vinakuwa vikifahamika na watu wote na matokeo yake vinakuwa sehemu ya mambo ya kiutamaduni katika jamii husika. Mojawapo ya vitu hivyo ni msemu usemao ‘mapenzi yaliyopindukia huleta utengano wa mara moja,’ msemu huu unaashiria maangamizi makubwa ambayo yanaweza kumfika mtu baada ya kukipenda kitu kupita kiasi, kiasi cha kuweza kumuabudu.

Ni jambo la kuzingatia kwamba wazazi wa mtoto aliyekuwa ameuawa katika mikono ya Khidhir – amani iwe juu yake – angelifikwa na huzu-ni kubwa pindi angelisikia kuwa mtoto wao amekufa; kama ambavyo mwanzoni walifurahi sana baada ya kumzaa. Lakini kama mtoto yule angeliendelea kuishi angeishia kuwaharibia maisha yao hapa duniani na kesho akhera. Kama maamuzi wangeliachiwa wazazi wake, kwa hakika wasingelitaka mtoto wao auawe. Lakini kama ambavyo Mwenyezi Mungu alivyo Mwingi wa rehema na anavyowapenda waja wake wema bila ya mipaka zaidi ya mzazi yeyote anavyowapenda watoto wake mwenyewe, ndio maana akahukumu kifo cha yule mtoto ili awalettee mtoto mwingine mwema zaidi, hii ilikuwa fadhila kubwa sana kutoka Mola wao. Kwa kuwa mtoto aliyeuawa aliondoka hapa duniani bila ya hatia yoyote na bila ya kuchafuliwa na madhambi, Mola alifidia maisha yake mafupi kwa kumpa furaha ya milele kesho akhera atakapokuwa pamoja na wazazi wake. Hivyo baraka katika vazi la ghadhabu ilimaanisha kwamba maangamizi madogo yalikutubalika ili kuepusha maangamizi makubwa.

Imekuja kufahamika kwamba wakati mwingi wanadamu hukosea pindi wanapokuwa wanatathmini matukio ya nje kwa kuwa hawana mam-laka katika hekima takatifu. Ndani ya Qur’an tumeambiwa:

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ وَعَسَىٰ أَنْ تُحِبُّوا شَيْئًا  
وَهُوَ شَرٌّ لَّكُمْ وَاللَّهُ يَعْلَمُ وَأَنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

“...Lakini huenda mkachukia kitu nacho ni kheri kwenu. Na huenda mkapenda kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua na nyinyi hamjui” (al-Baqara, 216).

Kumuua mtu asiye na hatia ni kosa kubwa ambalo sheria ya kiislamu inaagiza muuaji naye auawe. Hivyo kuufanyia kazi mfano wa simulizi hii





ya Qur'an kwa kutumia elimu ijulikanayo na watu wachache ni jambo lisilovumiliwa na sheria ya kiislamu, jambo hili haliruhusiwi kutekelezwa na waislamu ambao wanawajibika kwa matendo ya dhahiri peke yake. Hivyo hata watu wema walio na elimu ya moyoni hawatekelezi hukumu hii mpaka sababu za dhahiri zitimie; kwa maneno mengine ni kwamba watu hawa kamwe hawajitengi na ulimwengu wa kawaida. Mipaka iliyowekwa na sheria ya kiislamu haina budi kutiiwa na watu wote.

Musa – amani iwe juu yake – alikuwa ni Mtume aliyefunuliwa sheria ambayo aliagizwa kuifanyia kazi. Kwa upande mwingine, Khidhir – amani iwe juu yake – naye alikuwa akifanya mambo kulingana na elimu aliyokuwa amefundishwa; hivyo hakuwa anafanya mambo kwa matamania yake mwenyewe, bali kulingana na matakwa ya Mwenyezi Mungu. Kumpinga kwa Musa – amani iwe juu yake – kulikuwa kunasukumwa na uchungaji wake wa mipaka aliyokuwa amewekewa na Mola wake. Na Mola ndiye aliyewafunulia wanadamu makutano ya watu hawa wawili ndani ya Qur'an. Hii inamaanisha kuwa matukio yaliyosimuliwa juu ya kukutana kwao ni ubainifu tofauti wa uhalisia wa aina moja, hata hivyo yanaweza kuonekana kuwa yanaenda kinyume na sheria ya dini. Kwa hakika wakati Musa – amani iwe juu yake – alipopata siri za ndani za ubainifu huu wenye kustaa-jabisha aliweka pembeni upingaji wake wote na kutambua kuwa *shariah* ilikuwa ni kitovu cha *haqiqah*, undani wake. Kadiri sheria inavyowaenea watu wote na watu wengi kushindwa kufahamu maana ya elimu yenye kufahamiwa na watu wachache, ndivyo inavyokuwa lazima kwetu kushikamana na sheria iliyopo.

Licha ya kutotendewa wema na wanakijiji lakini Khidhir – amani iwe juu yake – aliamua kukarabati ukuta uliotaka kuanguka bila kutarajia ujira kutoka kwao, hili linaashiria umuhimu na ubora wa kuwalinda mayatima. Pia wakati huo huo jambo hilo linatufahamisha kuwa kipato cha halali hakiwezi kupotea kamwe. Mapato wanayoyaingiza watu wema kwa kupitia njia za halali wakati wote huwa chini ya ulinzi mtakatifu.

Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia yafuatayo kuhusiana na hazina iliyokuwa imechimbiwa chini ya ukuta: “Hazina hiyo ilikuwa ubao uliotengenezwa kwa dhahabu, ndani yake kuli-andikwa mistari ifuatayo saba:





1. Anashangaza yule ambaye bado anaweza kucheka licha ya kufahamu kuwa kuna kifo.
2. Anashangaza yule mwenye kuikimbilia dunia licha ya kufahamu kuwa hii dunia ni yenye kupita.
3. Anashangaza yule mwenye kuhuzunika wakati anafahamu kuwa kila kitu kimekadiriwa.
4. Anashangaza yule mwenye kujikusanyia utajiri wakati anafahamu kuwa atakuja kuulizwa.
5. Anashangaza yule mwenye kutenda madhambi wakati anafahamu kuwa kuna Moto.
6. Anashangaza yule mwenye kuwaongelea wengine licha ya kufahamu fika kuwa Mwenyezi Mungu yupo.
7. Anashangaza yule mwenye kutarajia kupumzika hapa ardhini licha ya kufahamu fika kuwa kuna pepo; na Vivyo hivyo kwa yule mwenye kumtii shetani licha ya kufahamu kuwa yeye ni adui.” (Ibn Hajar Asqalani, Munabbihat, uk. 29).

Kwa mara nyingine tena kwa upande wa *ishari* maneno ‘zinapokutana bahari mbili’, mahali zinapokutana bahari mbili, yanamuonyesha Musa – amani iwe juu yake – bahari ya elimu ya mambo makubwa ya dhihiri, na kwa upande wa Khidhir – amani iwe juu yake – anaonyeshwa bahari ya elimu ya siri zenye kustaajibisha.

Suala kwamba Musa – amani iwe juu yake – aliongozana na Khidhir – amani iwe juu yake – kwa lengo la kupata elimu ya *ladunni* ni la kuzingatwa kwani linafanana na uhusiano kati ya *murshid* na *murid* au mwalimu na mwanafunzi ndani ya usufi. Kwa hiyo tunaweza kuhitimisha kwamba hata kama mtu atakuwa na elimu kubwa kama ya Musa – amani iwe juu yake – lakini bado atatakiwa awe tayari kupiga magoti kwa unyenyekevu na heshima mbele ya mtakatifu kwa ajili ya kupata uongofu wake.

*Siku moja maswahaba walimuuliza Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, “Tufanyeje endapo tutakabiliwa na tatizo ambalo suluhisho lake halipatikani ndani ya Qur’an au Sunnah?”*

*“Wafuateni mahakimu na watu wema kwa ajili ya kupata hukumu*





*kutoka kwao”, aliwajibu. “Msiyashughulikie mambo kwa maoni yenu bin-afsi” (Haythami, Majmau’z-Zawaid, 1,178).*

Imam Shafii ambaye alikuwa mwanachuoni mkubwa wa sheria za kiislamu alikuwa akimtembelea Shayban-i Rai - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye alikuwa mtu mwenye imani ya hali ya juu, na kisha akipiga magoti mbele yake kama alivyo mwanafunzi mtiifu kwa ajili ya kujadiliana naye masuala fulani kwa matumaini ya kunufaika kiroho. Wakati mwingine wanafunzi wake walikuwa wakipinga na kusema:

*“Jiangalie mwenyewe na umuangalie Shayban...kwa nini unamuonyesha heshima kubwa kiasi hicho”*

*“Kwa kuwa anavifahamu vitu ambavyo sisi hatuwifahamu”, Imam alikuwa akisema.*

Kwa namna hiyo hiyo Ahmed ibn Hanbal na Yahya ibn Main walikuwa wakimtembelea Maruf Karhi kwa ajili ya masuala mbalimbali.

Walimu wa kiroho hawatafutwi kwa ajili ya kujifunza sayansi za mambo ya dhahiri, bali sayansi za moyo, kwani hizo ni muongozo wenye kumulika kwenye njia zenye kuwapelekea watu kwa Mola wao. Wafasiri wengi maarufu, wanachuoni wa *hadith* na wanasheria wa kiislamu kama vile Ibn Abidin na Alusi miongoni mwa wengi waliingia kwenye njia ya kisufi na kukubali kuongozwa na watakatifu katika masuala muhimu ambayo wao wenyewe hawakuweza kuyatatua.

Imam Abu Hanifah ambaye alikuwa miongoni mwa wanasheria wakubwa wakiislamu waliofahamika katika dunia hii, naye vile vile alitafuta njia kwa kujiweka karibu na Jafar Sadiq - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Tukio lifuatalo linadhahirisha heshima kubwa aliyokuwa nayo Imam huyu kwa watu wa kiroho:

*Kumepokewa kwamba siku moja Ibrahim Adham - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alibahatika kumuona Imam Abu Hanifa. Wanafunzi wa Imam wakaanza kumuangalia Ibrahim Adham - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kwa namna fulani ya kutomuonyesha heshima. Baada ya kulingundua hili Imam akamuita Ibrahim Adham kwa namna ya kumkaribisha: “Tafadhali mwalimu...sogea karibu. Umetufanyia wema kwa kuja kwako kwenye somo letu!”*





*Ibrahim Adham - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - akamsalimia kwa haya na kisha akaondoka. Pindi alipopotea kwenye macho yao wanafunzi wake wakamuuliza, "Umemtukuza mtu yule kwa jambo gani? Inawezekanaje mtu kama wewe ukamuita mtu yule mwalimu?"*

*"Kwa kuwa wakati wote anamfikiria Mwenyezi Mungu", Imam akajibu kwa unyenyekevu. "Na sisi tunamfikiria kwa kiwango cha maneno tu."*

Kama ilivyo kwa matawi mengine ya elimu, ni jambo la msingi kukubaliana na mwenendo uliwekwa wakati unapokea mafunzo katika elimu ya *ladunni*. Miongoni mwa mwenendo huo ni kujivika unyenyekevu ambao utamfanya mtu ajihisi dhalili na dhaifu wakati wote.

Ni jambo lenye kustaajabisha kiasi gani kwamba Mtume kama Musa - amani iwe juu yake - ambaye alipewa heshima ya kuwa *Kalimullah* (aliyeongelehwa na Mwenyezi Mungu moja kwa moja) hata siku moja asifikirie, "Ninahitajika kukaa na kutatua matatizo ya watu wangu, kwani Taurati imejitosheleza. Licha ya hayo mimi ni mwenye kupokea ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu na kama ningelitaka ningelimuomba Mwenyezi Mungu anifundishe moja kwa moja". Badala yake huku akionyesha unyenyekevu wa hali ya juu alitii maagizo matakatiifu na hivyo kuweka mfano bora kwa watu watakaokuja baada yake. Ushahidi wa wazi juu ya hili ni uamuzi wake wa kuwa tayari kutembea kwa miaka mingi kama ingelibidi mpaka ampate (Khidhir). Unyenyekevu wa Musa - amani iwe juu yake - unatoa mfano bora kwa watafutaji wote wa elimu.

Kama Mwenyezi Mungu Mtukufu angelitaka, Angelimfanya Musa - amani iwe juu yake - ampate Khidhir - amani iwe juu yake - mara moja bila ya kuhangaika. Badala yake Mwenyezi Mungu akataka Mtume wake apitie kwenye safari ngumu, hili linamaanisha kwamba njia hii inahitaji mapenzi makubwa na uta, na bila shaka rehema za Mwenyezi Mungu.

Pia uzoefu wa wote wawili unaashiria hitajio la kutafuta mafunzo ya kiroho kutoka kwa mwalimu mwenye kuendana na hali halisi ya elimu hiyo. Si jambo jema kupuuzia sharti hili na kupata elimu hii bila ya kuwa na *murshid*, yani kiongozi. Kufanikiwa katika njia hii kunahitaji msaada mkubwa kama kunavyohitaji utambuzi wa hali ya juu.

Kwa upande mwingine mtu anaweza kujiuliza inakuwaje Mtume mkubwa kama Musa - amani iwe juu yake - akaomba kupata mafunzo





kutoka kwa Khidhir – amani iwe juu yake. Lakini ni jambo la kuzingatia kwamba tamaa ya Musa – amani iwe juu yake – ya kutaka kufundishwa na Khidhir – amani iwe juu yake – hakumaanishi kuwa yeye hana elimu na hekima yoyote na kwamba yeye hakujaaliwa sehemu ya utambuzi wa kiroho (*kashf*) na ufunuo. Suala hili ni sawa na mtu anayetafuta ujuzi kutoka kwa mtu mwenye uwezo mkubwa katika suala husika. Kwa mfano nguvu na uwezo wa Sinan katika usanifu wa majengo bila shaka ni mkubwa kuliko wasanii na vibarua wote walio Shiriki katika ujenzi wa msikiti wa Suleymaniye. Licha ya haya yote lakini Sinan alikuwa hana ufahamu mkubwa katika sanaa ya ujenzi wa kutumia marumaru kumpita mtaalamu katika soko hilo aliyekuwa akifanya kazi katika ujenzi ule. Lakini hili halimaanishi mapungufu kwa upande wa Sinan, kwani wasanii na vibarua wote walikuwa chini ya amri yake.

Hivyo si kwamba kwa sababu Khidhir – amani iwe juu yake – alikuwa mwalimu wa Musa – amani iwe juu yake – kwa muda ndio inamaanisha kuwa Khidhir alikuwa ni mbora kuliko Musa. Katika kiini cha mambo sehemu hii haihitaji ulinganishi wa nani mbora na nani dhaifu, kwani Musa na Khidhir – amani iwe juu yao – wote ni wapita njia katika mazingira tofauti yasiyolingana. Cha kuzingatia hapa ni kwamba viumbe wote, wakiwemo Mitume, ni dhaifu mbele ya elimu takatifu; na hii ndiyo yenye kuwafanya waziangalie tena elimu zao.

Pamoja na Mitume kuwa kwao wanadamu lakini wao ni watu waliochaguliwa na waliojaaliwa kupokea ufunuo matakatifu. Waja hawa wa Mwenyezi Mungu wa kipekee huwa hawatendi madhambi. Lakini kwa kuwa nao ni wanadamu na hivyo ni madhaifu mbele ya Mola wakati mwingine hukosea na kuteleza, kuteleza huku kunaitwa *dhalla*. Kwa kupitia kuteleza huku ambako kuna lengo la kutoa funza katika suala fulani kwa wanadamu, Mwenyezi Mungu huwapa ladha ya ubinadamu na hivyo kuwafunza kwa namna ambayo hatuifahamu. Hapa Musa – amani iwe juu yake – alitakiwa kuelewa udhaifu wa elimu ya mwanadamu ukilinganisha na ile ya Mola na hivyo kumfanya atambue uwepo wa daraja nyingi za elimu ambazo hazijafunuliwa kwake. Utambuzi wake huu ni kwa ajili ya kutoa mfano muhimu kwa wanadamu wote mpaka siku ya mwisho.

Kwa hakika licha ya nguvu na mamlaka makubwa ya utume waliokuwa nao lakini Mitume hao walikuwa wakiyafahamu yale tu waliyojaaliwa







na Mwenyezi Mungu kuyafahamu katika mambo yasiyoonekana (*ghayb*). Kwa kuwa elimu ya ladunni ni zawadi hivyo wao huyafahamu yale tu waliyofunuliwa na hubakia hawayafahamu yale yaliyofichwa. Imetajwa katika Gulistan ya Sheikh Sadi kwamba siku moja mtu mmoja alimuuliza Yaqub – amani iwe juu yake:

*“Wewe ni Mtume mwenye hekima na mwenye moyo wa utambuzi... Uliwezaje kuhisi harufu ya shati la Yusuf – amani iwe juu yake – pindi lili-pokuwa likiletwa kwako tokea mbali kama Misri, lakini ulishindwa kumu-ona pindi alipokuwa anarushiwa ndani ya kisima kilichokuwa karibu yako?”*

*“Sehemu ya elimu takatifu tuliyojaaliwa huwa ni kama mshindo wa radi. Ukweli huwa wazi kabisa wakati fulani na kubakia umefichwa wakati mwingine”*

Maneno aliyoyatumia Musa – amani iwe juu yake – pindi alipokuwa anatafuta elimu kutoka kwa Khidhir – amani iwe juu yake – yalikuwa ni ‘elimu uliyopewa’. Haya yanamaanisha kwamba elimu ni lazima itoke kwa Mwenyezi Mungu na si kwa wanadamu. Humpa sehemu ya elimu yeyote amtakaye na kwa kiwango akitakacho. Sehemu ya elimu hii huitoa kwa kupitia sababu fulani, na wakati mwingine huifunua moja kwa moja kwenye moyo wa mja wake.

Kingine cha kuzingatia ni kwamba, pindi mtu aliyefunga anapokula chochote kwa kusahau swaumu yake huendelea kuwepo. Vivyo hivyo upingaji wa Musa – amani iwe juu yake – kwa Khidhir – amani iwe juu yake – haukufanya safari yao iishie pale. Lakini Musa – amani iwe juu yake – ndiye aliyekataa kuendelea kupata elimu hii kwa kusema yafuatayo kwa aibu na hofu bila ya kulazimika kuyasema:

*“Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami...”* (al-Kahf, 76). Aliweka mwenyewe sharti hivyo akalazimika kutoendelea kupata zaidi sehemu ya elimu ile.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema, *“Rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya Musa. Kama angeliweza kuen-ndelea kuwa na subira juu ya mambo yale Mwenyezi Mungu angelitufahamisha mambo mengi zaidi (ya kustaajibisha na yasiyo ya kawaida)”* (Muslim, Fadail, 170; Bukhari, Tafsir, 18/2). Kwa hiyo subira ni jambo la lazima katika njia hii.





Maelezo mengine kutoka kwa wasufi kuhusiana na kukutana kwao ni kwamba: Imesimuliwa kwamba yule kijana aliyekuwa na Musa – amani iwe juu yake – pindi alipokuwa katika safari yake ya kumsaka Khidhir – amani iwe juu yake – alikuwa ni Yusha Ibn Nun ambaye alikuwa mpwa wa wake, na pia alikuwa mtu mkubwa miongoni mwa maswahaba wake. Baada ya Musa – amani iwe juu yake – kufariki yeye ndiye aliyechukua nafasi yake. Vile vile Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alimchagua Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – afuatane naye wakati wa hijra; yeye alikuwa ni mbora zaidi miongoni mwa maswahaba zake na alifahamika kama “wa pili kati ya wawili ambao watatu wao alikuwa Mwenyezi Mungu”. (Bukhari, Ashabu'n-Nabi, 2). Mifano hii inaonyesha umuhimu wa kujenga urafiki wa kweli katika njia ya imani, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu peke yake.

Mfano huu peke yake wa Musa – amani iwe juu yake – unatupatia ufahamu mzuri kuhusiana na ubora wa elimu ya *ladunni*.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

*“Bila shaka ninaviona vitu ambavyo hamvioni na ninavisikia vitu ambavyo hamvisikii. Anga imetoa sauti kali na hivyo ndivyo inavyotakiwa...kwani hakuna alama ndogo kama inchi nne ambayo malaika hajapata kuweka paji lake la uso kwa ajili ya kumsujudia Mwenyezi Mungu. Ninaahidi kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba kama mngelizifahamu siri ninazozifahamu mimi mngelicheka kidogo sana na kulia sana...Mngeliyaacha majumba yenu na kukimbilia kwenye tambarare kwa ajili ya kumuomba Mwenyezi Mungu kwa sauti za juu”.*

*Baada ya kuyasikia haya msimuliaji wake ambaye ni Abu Dharr al-Ghifari – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisema, “Nilitamani kweli kweli kuwa mti ambao unakatwa!” (Ibn Majah, Zuhd, 19).*

Maswahaba wengine waliziweka hisia zao za hofu na udhalili mbele ya uhalisia wa *ladunni* katika maneno yafuatayo:

“Natamani lau kama ningelikuwa kipande cha tende ambacho ndege wanakidonoa”, alisema Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye alikuwa na wasiwasi mkubwa alitamani kuwa “kipande cha jani...au asiwe kitu chochote!” Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alitamani kuwa “jani katika mti wowote mkuu kuu.”





Kilichowafanya wainame mbele ya Nguvu na Utukufu wa Mwenyezi Mungu ni kutambua kwao udhaifu na udhalili walio nao, na hofu iliyokuwa nyoyoni mwao.

*Swahaba mwingine ambaye aliathiriwa na utukufu wa unaopatikana kwa kuwa pamoja na Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – alikuwa ni Harithah ibn Malik al-Ansari – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Siku moja Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – alimuuliza:*

*“Ewe Harithah, uliamka katika hali gani?”*

*“Nikiwa Muumini wa kweli” alijibu.*

*“Kila ukweli huja na uthibitisho wake, Harithah. Ni upi uthibitisho wa imani yako” Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – aliuliza.*

*“Baada ya kuiacha dunia mchana wangu ukawa umechomwa na usiku wangu ukawa haulaliki. Ilikuwa ni kana kwamba ninakiona kwa uwazi kiti cha enzi cha Mola wangu. Ni kana kwamba ninawaona wakazi wa peponi wakitembeleana na watu wa Motoni wakilaaniana”.*

*Kwa mara nyingine tena Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – alimuongelea Harithah kwa kusema, “Yeyote anayetaka kumuona mtu ambaye Mwenyezi Mungu ameumulika moyo wake amuangalie Harithah” (Ibn Hajar, al-Isabah, 1,289).*

*Kitendo hiki kilielezwa na Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – katika lugha ya upendo kama ifuatavyo:*

*“Harithah anamuomba Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – ruhusa ya ‘...kuelezea kile alichokiona’ na anaanza kama ifuatavyo:*

*‘Mjumbe wa Mwenyezi Mungu...Ngoja sasa hivi nianze kutoa picha ya siku ya kiama, kiama ambacho watu wanaamini kitatokea hapo kesho. Niache nifunue siri za kufufuliwa. Niamuru na mimi nitachana mapazia ya siri hizi...ili lulu ya hekima takatifu zilizo ndani yangu zing’ae kama jua angani...*

*Niamuru ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na mimi nitawaweka wazi wale walioweza kubakia kuwa kama dhahabu na lulu katikati ya uchafu na ubaya wa dunia na wale waliojing’atua kwenye kutu ya ukafiri...*





*Niruhusu niwafahamishe watu ubaya wa aina saba wa unafiki katika nuru isiyoweza kuzimika ya utume...*

*Niache nimuonyeshe kila mtu mavazi watakayoyavaa waasi siku ya kiama. Niache niwafanya wasikie sauti za ngoma ambazo zitaviringishwa kwa ajili ya Mitume...*

*Niruhusu niwaonyeshe bwawa la Kawthar lenye nishati na lenye kutiririka ili rasha rasha zake ziweze kufikia nyuso zao na sauti yake iweze kufika masikioni mwao.*

*Tafadhali niruhusu nikuonyeshe roho zenye kiu zikikimbia huku na kule karibu na bwawa hilo...Mabega yao yanasuguana na yangu. Kelele zao zinayaenea masikio yangu...*

*Wakazi wa peponi wenye furaha wanakumbatiana na kupeana mikono mbele ya macho yangu.*

*Makelele ya malalamiko ya watu wa Motoni na vilio vyao vya masikitiko vinakaribia kunifanya kuwa kiziwi!*

*Hizi ni dalili ninazodhihirisha kutoka ndani ya moyo wangu. Ningelise-ma zaidi kama nisingelihofia kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana na amani ziwe juu yake – angeliweza kunikemea’*

*Alikuwa akiyasema haya kwa kuwa alikuwa amezama kwenye dimbwi la kiroho. Alikuwa amepotea ndani ya raha za hali ya juu; alikuwa na udhibiti mdogo wa utambuzi wake. Alikuwa tayari kutoa siri zote.*

*Ili kumuamsha kutoka kwenye hali hii Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana na amani ziwe juu yake – alisema, ‘Dhibiti hisia zako na unyamaze’. Kisha akaongezea yafuatayo huku akivuta kola ya Harithah:*

*‘Rudisha akili yako! Shika ugwe wa ulimi wako kwani uko katika kilele cha kuyasema mambo ambayo hutakiwi kuyasema. Kioo cha roho yako kimepasuka na kutoka nje na hifadhi yake. Lakini kamwe usisahau kuwa kuziweka kwako wazi siri ulizopewa ni kutokana na kushindwa kwako kuzihimili. Moja ya jina la Mwenyezi Mungu ni Sattar, Mwenye kusitiri. Kuwa makini na hilo na usitoe muhanga furaha yako kwa kutolizingatia jina hili.’”*

*Kama ambavyo kila chembe katika ulimwengu inadhihirisha usawa mtakatifu mbele ya ubainifu wa ulimwengu wa kiroho, ndivyo ambavyo*





mtu anahitajika kuchunga usawa na kiasi. Kutokana na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kuwa mfano bora kwa umma wake katika masuala yote kamwe hakuwahi kutoka kwenye mipaka ya viwango wa wastani hata pale alipokuwa katika kilele cha imani.

Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akifikwa na hali ngumu ya kiroho ambayo ilikuwa ikimfanya ashindwe kuivumilia kwa muda mrefu. Hasa alikuwa akipata shida sana wakati ufunuo mtakatifu na kupelekea kutokwa na matone ya jasho kama lulu. Pindi ufunuo huo ulipokuwa ukifikia kwenye kilele chake alikuwa akisema:

“Mambo ya kiroho yamenisonga sana ewe Aisha. Njoo uongee na mimi kidogo”<sup>17</sup> na kisha anarejea katika mazingira ya kibinadamu.

Kinyume chake pindi alipokuwa anatekwa na hisia za kidunia alikuwa akisema, “Ewe Bilal, tuite kwa ajili ya swala ili tuweze kuburudika!” (Abu Dawud, Adab, 78).

Pamoja na kujiwekea mazingira mazuri katika ulimwengu wake wa ndani lakini pia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiwafanyia kiasi watu waliokuwa wamemzunguka. Alikuwa makini ili asije akaweka wazi siri za ndani alizokuwa amejaaliwa kuzifahamu na ambazo zilikuwa ziko nje ya utambuzi wa mwanadamu wa kawaida, isipokuwa kwa wale waliokuwa na uwezo wa kuzitambua. Kutokana na umuhimu wa suala hili Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – amesema, “Ongea na watu kwa namna ambayo watakuelewa” (Bukhari, ilm, 49); yani si kulingana na uwezo wako wa utambuzi bali uwezo wao.

Kuhusiana na mafumbo haya yenye kustaajabisha, Abu Hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaeleza namna alivyojizua kusimulia maneno kadhaa ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kuhofia kuwa watu wangelishindwa kuyaelewa.

“Nilijifunza buli mbili zilizojaa elimu kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Ya kwanza niliisambaza kwa watu. Na ya pili kama ningelisambaza basi koo langu lingelikatwa” (Bukhari, ilm, 42).

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Kuwapelekea hekima wale wasiostahili ni uonevu” (Darimi, Muqad-

<sup>17</sup> Rejea Munawi, *Fayzul-Qadir*, V, 228.





dimah, 34). Pia tunaweza kusema kuwa kuzuia hekima yenye manufaa na watu ni uonevu. Qur'an inasema:

“Yeye humpa hikima amtakaye; na aliye pewa hikima bila ya shaka amepewa kheri nyingi. Na hawakumbuki ila wenye akili” (al-Baqara, 269).

Sufi wakubwa wenye muelekeo bora hawakuwapa elimu hii wale wenye uelewa mdogo. Siri hizi za ndani ambazo watu wengi hushindwa kuzihimili hazina budi kufichwa. Hallaj Mansur ambaye alipewa siri hizi ambazo baadhi ya watu ndio waliojaaliwa aliwajibika kwa uhai wake baada kutoa muale mmoja tu wa siri hizo. Aliuawa.

Baada ya kuingia kwenye bahari ya kuutambua Umoja mtakatifu, Hallaj aligubikwa na raha ya hali ya juu na ubainifu mkubwa ndani ya moyo wake, hili lilimpelekea kudai ‘Ana’l-Haqq’, ‘Mimi ni Mtukufu’. Maneno haya yaliwapelekea watu kumhukumu kulingana na kiwango cha uelewa wao.

Watakatifu wengi pia walipitia hali ya kiroho aliyopitia Hallaj. Lakini hali hii haibakii sehemu moja (*tathbit*) wala si yenye mfanano kamili (*tashkhis*). Hii ni hali yenye kupita ambayo huwatokea watakatifu ambao katika kipindi cha *fana’fillah* au kuangamia kwa Mwenyezi Mungu hushindwa kujizuia na hivyo kupoteza udhibiti wa akili zao. Katika kipindi hiki ambacho udhibiti wa akili yake haupo mtu hawezi kulindwa na sheria, kwani anakuwa amevuka mipaka ya ulimwengu wa viwango vya nje, kwani sharti la kwanza la kukuwezesha kulindwa na sheria ya dini ni kufanya mambo yenye ‘mantiki’.

Kwa kuwa hali hizi ni matokeo ya kuingia kwenye haiba takatifu (*jazbah*), hivyo mtu aliyethirika na hali hiyo katika usufi huitwa *majzub*.<sup>18</sup> Ingawa hali hii yenye kuvuka viwango vya nje inaweza kupuuziwa na wale wenye utambuzi lakini watu wa kawaida hupelekea jambo hilo kutoweza kukubalika. Kuhusiana na kuuawa kwa Hallaj hakukusemwa bure kwamba

18. *Majzub* ni mtu ambaye ameleweshwa na Baraka kiasi kwamba akapoteza udhibiti wa akili yake, lakini ambaye moyo wake umeegemea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu moja kwa moja. Ingawa *majzub* anaweza akawa amezama kwenye hali ambayo inaweza kuonekana ni ngeni pindi itakapopimwa katika viwango vya kawaida vya maisha ya mwanadamu, lakini anakuwa amewapita watu wa kawaida wengi katika uzamivu wake kwenye utambuzi. Ni kana kwamba uwezo wake, utambuzi wake na akili yake imefikiwa na nguvu ya volti kubwa ambayo haizuiliki. Watu kama hawa ni mifano hai ya udhalili wa mwanadamu mbele ya ubainifu wa Mola wake.





‘Hallaj alikuwa sahihi na waliomuua pia walikuwa sahihi.’ Hivyo usawa umeshauriwa sana katika usufi ambao unachukulia hali ya kuwa mwenye haiba (*jazib*) ni bora kuliko ile ya kufanyiwa haiba (*majzub*).

Imesimuliwa kwamba Abu’l-Harith ambaye ndiye aliyemning’iniza Hallaj alimsogelea Hallaj kwa mbele kwa ajili ya kutekeleza hukumu na kumpiga kikatili usoni, alisababisha uso na pua yake kuvunjika na kububujikwa na damu. Pale pale Sheikh Shibli ambaye alisimama pale alipiga ukelele na kuzimia kwa sababu isiyofahamika.

Ubainifu ulioshuhudiwa kwa Hallaj ni hali ya akili iitwayo *hal*, pindi hali inapopita, Mtukufu huwa Mtukufu na maada huwa maada. Sheikh Shibli anasema:

*“Hallaj na mimi tulipitia hali moja. Waliniita mwendawazimu na kuniacha. Kwa upande wa Hallaj walimchukulia kuwa alikuwa na akili timamu na hivyo wakamnyonga.” Anaelezea zaidi:*

*“Baada ya Hallaj kuhukumiwa nilienda kwenye kaburi lake wakati wa usiku na kumswalia mpaka asubuhi. Niliomba, ‘Mola wangu...Hallaj alikuwa mja wako muaminifu na mwenye busara, mja ambaye aliamini katika upweke wako. Kwa nini umemfanya aingie kwenye mateso haya?’*

*Kisha nikashika na usingizi na kulala. Nikaota ndoto ambayo ndani yake niliona siku ya kiama imefika na nilimsikia Mola akisema:*

*“Tunaweka kwenye mateso hayo kwa sababu ameisambaza siri yetu kwa wasiostahili!”*

Hivyo imeeleweka kwamba kisichotakiwa si kupata siri za ukweli wa mambo kwa kuangamia kwa Mola bali ni kuzisambaza kwake kwa watu, jambo ambalo linaweza kusababisha watu kukosa utulivu. Hivyo ni kosa kubwa kujumuisha baadhi ya matukio kama haya yaliyosababishwa na kushindwa kuzingatia viwango vya kawaida na hivyo kuwaongelea vibaya watakatifu na wafuasi wa mwenendo wa kisufi. Kuwaongelea vibaya vipenzi vya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kushindwa kuthamini juhudi zao kunatokana na ujinga na kutoona mbali. Ni jambo lisiloingia akilini kwa muumini kutowatambua watu hawa.

Hivyo kanuni ya msingi katika njia ya kiroho ni kushikamana vilivyo na viwango vitukufu bila ya kukataa ukweli wa kuwepo kwa siri takatifu.





Pia ni jambo la msingi kutotoa siri za ndani kati ya Mola na mja wake. Zote hizi ni hali zinazopitiwa kutokana na raha ya kiroho inayovuka akili ya kawaida. Pindi hali hii itakapopita na fahamu za kawaida kurudi hali ya kiroho hurejea katika hali yake ya kawaida.

Kutokana na ubainifu wa hali ya juu ulioziita roho zao, baadhi ya watakatifu walishawishika kuonyesha tabia isiyokuwa ya kawaida. Lakini pindi walipoamka kutoka kwenye hali hiyo waliendelea kwenda kwenye uelekea wa msingi.

Siku moja Junayd - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliulizwa, “Baadhi ya watakatifu huingia kwenye hali ya kiroho yenye kustaaajabisha na kuonyesha tabia isiyo ya kawaida. Una kipi cha kusema kuhusiana na hilo?”

“Waache wawe hivyo”, alijibu Junayd - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - “ili waweze kupata amani yao kwa Mwenyezi Mungu. Usiwalaumu isipokuwa juu ya yale ambayo sheria ya dini inayakataza moja kwa moja. Zingatia kwamba njia hii imeunguza maini yao, jitihada zao zimewapelekea kuchoka na kukauka, na wamepitia magumu mengi. Wanafanya hivyo si kwa sababu nyingine zaidi ya kuishinda hali ya kiroho iliyowaelemea. Na hakuna tatizo katika hilo.”

Dua aliyoiomba Hallaj muda mfupi kabla ya kunyongwa inatupa ufahamu juu ya usafi wa moyo aliokuwa nao na kiwango cha imani alichokuwa amefikia:

“Ewe Mwenyezi Mungu...Waja wako wamekusanyika kwa ajili ya kuniua mimi si kwa sababu nyingine zaidi ya utii wao Kwako na dini Yako. Wasamehe...kwani kama ungeliwajaalia kuzifahamu siri ulizonijaalia mimi kuzifahamu wasingelinifikiria vibaya. Na kama ungelizuia siri hizo zisinifikie mimi basi nisingelizifunua kwao. Wasamehe ewe Mola...kwani wananifanya nije kukutana na wewe!”

Imesimuliwa kutoka kwa wale walioshuhudia hali ya kiroho aliyokuwa nayo Hallaj akiwa amening'inizwa juu ya kiunzi cha miti ya kunyongea kwamba Iblis alimjia na kumwambia:

*“Wewe ulisema Ana<sup>19</sup> na mimi nilisema Ana. Inakuwaje unapata rehe-*

<sup>19</sup> Katika kiarabu neno *ana* ni rehema na amani zive juu yakea na kiwakilishi *mimi*.







*ma kwa kulitaja neno lile lile ambalo lilinganyia mimi nilaaniwe?”*

*“Kwa kusema kwako Ana ulijiona wewe ni bora kuliko Adam na hivyo ukajivuna”, Hallaj alijibu. “Lakini kwa upande mwingine mimi nilisema Ana'l-Haqq, na kwa kufanya hivyo nikajihilikisha kwa Mola. Kujivuna si chochote bali ni dalili ya Motoni. Lakini kujiepusha nayo na kujihilikisha kwa Mola ni kuashiria ‘udhalili’. Ndio maana malipo yangu ni rehema wakati yako ni laana.”*

Ibrahim ibn Fatiq anasimulia namna Hallaj alivyomshauri pindi alipokaribia kunyongwa:

*“Mwanangu, baadhi ya watu wamenitangaza mimi kuwa ni kafiri wakati wengine bado wanashawishika na utakatifu wangu. Lakini wale wanaonituhumu mimi kuwa ni kafiri wanapendwa zaidi na Mwenyezi Mungu na mimi kuliko wale wanaoniita mtakatifu’*

*‘Kwa nini unasema hivyo?’ nilimuuliza.*

*‘Wale wanaonitazama kama mtakatifu wanafanya hivyo kwa sababu ya manufaa yao ya tuhuma (husn-u zan). Lakini wengine wananiita kafiri kutokana na utii wao katika dini. Mtu ambaye ni mtii katika dini anapendwa zaidi na Mwenyezi Mungu kuliko yule aliye na mashaka.”*

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - ambaye alipata ubainifu mkubwa zaidi ya ule wa Hallaj amesema, “Kama Hallaj angelifahamu ubainifu kati yangu na Mola wangu, yeye mwenyewe angeligeuka na kunipiga mawe.”

Hizi na hali nyingine kama hizi ni udhihirisho wa kujihilikisha kwa Mola au *fana fillah* katika maneno. *Fana fillah* kunaielezwa na Mawlana Rumi kama ifuatavyo:

*“Pindi unauona mto wa usio na mwisho wa uhai yamwage ndani yake maji ya yaliyo ndani ya kikombe chako cha uhai. Je maji yataweza kuukimbia mto?”*

*Pindi maji ya yaliyo kwenye kikombe chake yanapochanganyika na maji ya mto, yanakuwa yameokolewa dhidi ya uwepo wake na kuwa maji ya mto. Kisha maji ya kwenye kikombe yanapoteza ubora na sifa zake na kubakia na dhati yake pekee. Pia hayatapungua wala kuchafuka wala kunuka.”*





Kwa kuwa hekima zao na hisia zao zote zinakuwa zimeelekezwa kwa Mwenyezi Mungu, kwa upande wa Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – pamoja na mfano wake, watu ambao wameingiza ndani ya nyoyo zao imani thabiti, Mola anakuwa kama macho yao yanayoangalia na mikono yao inayoshika.

Mfuasi mmoja wa Rumi anafafanua namna hali yake ya akili ilivyo-epusha uelewa wa watu wengi:

“Tumesikiliza mayowe ya raha za Mawlana Jalaladdin. Lakini hatuwezi kuona vina vya bahari ya amani alivyo zama ndani yake. Tunachoki-ona ni kile kilichoosha juu ya ufukwe kutokana maji ya mwisho wa kina cha bahari hiyo. Tulichokipata si mapenzi ya Mawlana, bali ni mayowe yaliyopaishwa na mapenzi yake. Hicho ndicho tunachojaribu kukielezea hapa kwa ndimi zetu zenye kitembe. Yeye ndiye aliyezama ndani ya bahari ya amani. Sisi tunabaki na sauti zilizotolewa na gharika la raha yake...na hasa hilo ndilo linalopatikana kwa Mawlana.”<sup>20</sup>

Hali ya raha na mapenzi ya kiroho ni bahari yenye kustaajabisha kiasi kwamba kilichopo chini yake hufahamika kwa wale tu waliozama ndani yake.

Vile vile Muhyiddin ibn Arabi ambaye aliweka katika maneno sayansi hii yenye kustaajabisha ingawa ilikuwa katika alama amesifiwa na watakatifu na wapita njia katika njia ya ufusi, wakati huo huo kutokana na ufanisi wake mkubwa alifikia kuitwa *Shaikhu'l-lAkbar*, Sheikh mkubwa. Wale walio mbali na ulimwengu wa elimu za siri walimtuhumu kuwa alikuwa kafiri kutokana na kushindwa kwao kufungua kifundo cha maajabu yake.

Ikiwa hakuna mtu aliye karibu ambaye anaweza kuzihimili siri hizo ni bora kubakia kimya. Ni muhimu kuongea na watu kulingana na upeo wa akili yao. Vinginevyo kuongelea hekima na *marifah* kwa mtu ambaye hawezi kukubaliana na msukumo wa kiroho uliopo ni sawa na kutoutendea kazi ukweli.

Hivyo Muhyiddin ibn Arabi amesema, “Wale wasio na msimamo kama wetu wasisome vitabu vyetu.”





Vile vile yapo hivyo maneno ya Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. “Nimeitoa siri hii kwa namna ambayo haifahamiki na wengi na kwa ufasaha...kwani yeyote atakayejaribu kuifafanua ataishia kuungua ulimi wake na msikilizaji wake ataishia kuwa na utambuzi uliungua.”

Ili kuzuia watu wenye uelewa mdogo wasije wakapotea njia Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - katika *Mathnawi* yake, yani kitabu kilichotolewa kwa ajili ya uelewa wa watu wenye viwango mbalimbali vya uwezo wa kuelewa mambo, ama ametumia misamiati mirahisi katika kuelezea siri za ndani, au amezificha katika alama ambazo zinaweza kueleweka na watu wakubwa katika imani. Hivyo amezungumzia mambo mengi ndani ya *Mathnawi* kiasi kwamba watu wengi wenye ufahamu mdogo wataweza kuelewa. Anasema:

“Vina vyangu si vina; bali ni bahari ya maana. Pia tashtiti yangu si tashtiti; bali ni yenye kuelimisha. Mafumbo yangu si rahisi, yamesheheni maneno mengi; bali ni yenye kuelekeza. Vyote hivi ni kwa ajili ya kufafanua siri na kuwawezesha watu kuzitambua vyema.”

Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia tukio alilolishuhudia:

*“Siku moja nilienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – nikamkuta akiongea na Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kuhusiana na Upweke wa Mwenyezi Mungu. Nikakaa nao. Lakini nilijihisi kama mtu asiyefahamu kiarabu; Ilikuwa ni vigumu kuelewa walichokuwa wakizungumzia.*

*‘Kile kilikuwa ni nini?’, baadae nilimuuliza Abu Bakr. ‘Je hivyo ndivyo namna wakati wote unavyoongea na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?’*

*‘Ndio, lakini si mara nyingi’ alijibu. ‘Pindi tunapokuwa peke yetu...’<sup>21</sup>*

Ikiwa mtu kama Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye kipaji chake ni cha hali ya juu, hawezi kuyaelezewa mazungumzo yaliyo katika lugha yake, mtu anaweza kupata ufahamu juu ya ugumu atakaokuwa nao mtu wa kawaida.

Hivyo kuyaweka mazungumzo hayo ya kiroho kwenye karatasi na

21 Kwa maelezo zaidi rejea Ahmed ibn Abdullah at-Tabari, *ar-Riyadu 'n-Nadrah*, II, 52.





kuwapelekea watu ni jambo lisilopendekezwa; kwani hili ni jambo kubwa mno. Lakini taarifa hizo zimeruhusiwa kuwafikia watu maalum wenye uwezo mkubwa ili kuhakikisha wanazitunza siri ili zisiwafikie umma. Ndio maana pindi linapotajwa jina la mtu anayedhaniwa kuwa amefikia daraja la juu ya kiroho linaambatanishwa na maneno *qaddas'Allahu sirrah*, yani 'Mwenyezi Mungu aitakase siri yake, au moyo wake, dhidi ya uchafu wote ulio nje ya roho.'

Kutokana na watu wengi kugubikwa na dunia ndio maana *tasawwuf* inawajibika kutumia upendo ambao ndio sababu ya uwepo wa ulimwengu. Ndio maana pia ikaitwa njia ya upendo na huruma. Lakini kwa kuwa upendo ni wenye kuleta raha, unaweza kupunguza nguvu ya maamuzi ya mtu na hatimae kumsababishia raha isiyozuilika.

Mfano mmoja wapo wa mapenzi hayo makubwa kati ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na Jafar Tayyar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ni kama ifuatavyo:

Siku moja Jafar Tayyar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa amerejea Madina kutoka Abyssinia huku akiwa pamoja na kundi la maswahaba. Pindi alipogundua kuwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa Khaybar aliamua kumfuata bila ya kuchukua muda hata kidogo kwa ajili ya kupumzika. Kuwasili kwake Khaybar kulimpa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – furaha kubwa mno, kiasi kwamba akasema:

“Sijui nifurahie kuanguka kwa Khaybar au kuwasili kwa Jafar?” (Ibn Hisham, as-Sirah, IV, 3).

Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliporejea kutoka kwenye *umratu'l-qada*<sup>22</sup> alijadiliana na ndugu zake kuhusiana na mtu atakayefaa kumlea Fatimah, yatima wa Hamza – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Mwishowe aliamua kumteua Jafar, na baada ya kumbusu kwenye paji lake la uso alisema:

“Wewe umefanana na mimi kimuonekano na kisilika!” (Bukhari, *Maghazi*, 43).

22. *umratu'l-qada* au umra ya fidia ni hijja ya *sunnah* ambayo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipanga kuitekeleza hapo kabla ndani ya mwaka wa amani ya Hudaybiyah lakini aliweza kuitekeleza katika mwaka uliofuatia.





*Jafar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliposikia kwamba ameteuliwa kutokana na furaha aliyokuwa nayo akawa kana kwamba amepoteza fahamu fahamu. Akaanza kuruka kama mtoto mdogo na kuzunguka kama mnyoo ulio kwenye moto. (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, I,108; Ibn Saad, IV, 35; Waqidi, II, 739).*

Hivyo kama ambavyo mtu mwingine angeliweza kujisikia raha kwa kusikia uteuzi huo na kuwa si yeye tena, pia anaweza kujivua na dunia na kuzama ndani ya ulimwengu wa kiroho. Hili ni jambo la kawaida. Cha muhimu ni kujitahidi kusimamia kwenye usawa na kuangalia mbele kwenye njia kuu na si kutoka nje ya viwango vinavyokufanya wewe kuwa mwanadamu hata katikati ya dhoruba kali ya raha.

Ili kuweza kubakia na usawa huu ulazimika kuongozwa na wale walio kwenye njia usufi, ambao wameunganisha sayansi za dhahiria na maisha ya kiroho.

Ikiwa watu waliopewa jukumu la kuongoza hawatafikia kwenye lengo na uwezo unaohitajika ndani ya sayansi za dhahiri, bado kutaendelea kuwa na hatari katika njia ya mapenzi ya kiroho. [Ili kuzuia hatari hii ndio maana katika baadhi ya matawi kama vile la Naqshibandiyya imekuwa desturi kwa walimu kupewa wanafunzi wenye uwezo wa aina moja katika sayansi za dhahiri, yote haya ni ili wajilinde wao wenyewe na watu wengine dhidi ya hatari kubwa iliyoongelewa.

Njia za mafunzo ya kiroho zilizotumiwa na watakatifu ni nyingi. Tawi la Naqshibandiyya ambalo ni miongoni mwa matawi maarufu katika matawi ya usufi, humfundisha mwanafunzi bila ya kumruhusu aangukie kwenye raha ya kiroho (*jazba*). Hili linagusiwa na maneno ya Abdulkhaliq Gujdawani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake:

“Kama Hallaj angelikuwa ameishi katika nyakati zetu na kupata mafunzo yetu, tungelikuwa tumemlinda dhidi ya kulewa kiroho (*sakr*).”

Hivyo kwa kuzingatia sheria ya dini hisia za kupindukia zinazooneka na katika baadhi ya matawi ya kisufi ambazo zinatokana na kuzidi kwa uzito wa ulevi wa kiroho si chochote bali ni kuteleza kwa ulimi.

Licha ya sifa walizonazo Mitume wote lakini ni wazi kwamba kila Mtume ana uwezo wa peke yake. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa watakatifu ukiwalinganisha wao kwa wao. Kwa mfano mtakatifu anaweza kuwa katika



hali ya jalali au jamali lakini ndani ya moyo wake anaweza kumfahamu Mwenyezi Mungu kwa namna tofauti ukimlinganisha na mtu wa kawaida ambaye anajitahidi kuwa karibu na Mola wake kwa kujiepusha na mambo ya kidunia yenye kupita. Wanatambua kwamba wao ni dhaifu mbele ya uwanja mpana wa elimu takatifu. Vyovyote iwavyo si tu watakatifu wote hawapo katika daraja moja la kiroho lakini pia hawalazimiki kutekeleza majuku ya aina moja. Wengine hurejea kwa watu pindi wanapofikia mwisho wa *sayr-u suluk*, safari yao ya kiroho. Huwa wanawajibika kuwafundisha watu wengine. Kama ambavyo kumekwishasemwa hapo kabla sawa na mwalimu anayemfundisha mtoto mdogo taratibu kuhusiana na mahusiano ya kijamii ndivyo ambavyo wao wanavyojifanya hawafahamu mengi miongoni mwa siri ambazo kiukweli wanazifahamu. Kujifanya hufahamu kwa namna hii kunaitwa *tajahul-i arifana*; yani 'ujinga ulio na busara'.

Kwa kuwa watakatifu wengine hawawajibiki kuufahamisha umma juu ya mambo mbalimbali basi hubakia katika hali ya hofu (*khayrah*) na kuendelea kuwa kimya. Ni kana kwamba ni mabubu mbele ya mmiminiko wa nguvu takatifu zilizoenea katika ulimwengu mzima. Hata hivyo kuna watakatifu wengine ambao wamepewa jukumu la kuwaongoza watu, hawa maneno yao ni kama maporomoko ya maji. Siri takatifu na hekima huanza kutiririka kutoka kwenye ndimi zao bila kukoma.

Kwa baadhi yao hali hizi ni zenye kutofautiana. Hupitia katika hali mbalimbali katika maisha yao. Mfano mmoja wapo wa hilo unajibainisha wenyewe katika maisha ya Muhammad Parisa - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake kama – kama ifuatavyo:

Kila baada ya swala ya *isha* Muhammad Parisa - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa akisimama kwenye uwanja wa msikiti kwa muda na kisha baada ya hapo alikuwa akirejea nyumbani kwake. Wakati mwingine shauku hiyo ilikuwa ikimjia kiasi kwamba akawa anasimama kwenye uwanja wa msikiti kimya kama vile ameganda mpaka adhana ya swala ya alfajir inamkuta pale pale huku akiwa katika hali ya hofu. Pindi alipokuwa akisikia adhana alikuwa akiingia msikitini tena.

Licha ya tofauti zilizopo kwenye maisha yao na hisia zao lakini pia watakatifu wana mitazamo tofauti kuhusiana na kifo. Wakati Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akikiangalilia kifo kama





sababu ya kukutana na Mola wake na kama usiku wa harusi kutokana na mapenzi yake makubwa juu ya Mola, Hasan Basri - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – yeye alikuwa akifikiria itakuwaje katika pumzi yake ya mwisho, hili lilitokana na hofu yake kubwa juu ya Mola.

Tunachoweza kukifahamu kuhusiana na elimu ya *ladunni* ni taswira ndogo sana iliyowekwa katika maneno kwa kadiri maneno yanavyoruhusu, na haya yanatokana na kile kilichodhihirika kutoka katika maisha ya Mitume na kusambaa kwake mpaka kwenye maisha ya watakatifu. Kwa kuwa ukweli kamili wa elimu hii upo kwa Mola, hivyo kuelewa kwa undani maana yake ni jambo lililo nje ya mipaka ya uelewa wetu.





**U**tambuzi wa kiroho ni uwezo wa kutambua kilichopo nyuma ya pazia, yani siri zilizo nje ya upeo wetu. Wale tu wenye kuweza kuan-galia ndani ya lulumizi ndio watakaoweza kuitambua lulu.



## 2.UTAMBUZI WA KIROHO (FIRASAH)

Firasah ni nuru ambayo Mola huzawadia nyoyo za waja wake vipenzi. Kwa maneno mengine, firasah ni kuingiziwa ndani ya moyo akili, kipaji, utambuzi, elimu ya kina na uelewa katika hali ya utambuzi wa kiroho. Kwa kupitia hisia na msukumo mzuri unaojitokeza ndani ya moyo mtu atakuwa na uwezo wa kutambua ukweli uliojificha wa vitu vinavyotokea na kutabiri na kutambua vyema fikra zinazopita kwenye nyoyo na akili za wengine.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

اتَّقُوا فِرَاسَةَ الْمُؤْمِنِ فَإِنَّهُ يَنْظُرُ بِنُورِ اللَّهِ

“Kuweni makini na macho ya muumini...kwani huangalia kwa nuru ya Mwenyezi Mungu” (Tirmidhi, Tafsir, 15). Bila shaka uwezo wa kuangalia kwa namna hii jambo ambalo linamuwezesha mtu kutazama kwa nuru ya Mola yenye mpenyo kumewekwa kwa ajili ya wale waliofanikiwa kuzitawala nafsi zao. Historia ya uislamu ina mifano mingi juu ya suala hili:

*Kutokana na masimulizi ya Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, siku moja alipokuwa njiani kuelekea kwa Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alimuona mwanamke mmoja. Alivutiwa na uzuri wake. Aliingia nyumbani kwa Othman huku akiwa katika hali ile, pindi Othman alipomuona tu Anas akasema:*

“Anas, umekuja hapa na alama za zinaa machoni mwako.” Huku Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akiwa amestaabishwa na maneno ya Othman akauliza:

“Je wahyi bado unaendelea kushuka baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu?” Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akajibu:







*“Hapana...hii ni busara na utabiri sahihi.”<sup>223</sup>*

Pia kunafahamika kwamba utabiri wa Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - katika mambo mengi ulikuja kuendana na maam-risho matakatiifu yaliyokuja hapo baadae. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – analithibitisha hili pale anaposema:

“Miongoni mwa watu walioishi kabla yenu kuna ambao walipokea ufunuo. Kama kuna mtu yeyote kama wao katika umma wangu kwa hakika atakuwa ni Omar.” (Bukhari, Ashabu’n-Nabi, 6).

Abu Abbas ibn Mahdi anaelezea:

*“Siku moja nilikuwa ninasafiri jangwani, nilikutana na mtu mmoja aliyekuwa mbele yangu kwa umbali mfupi. Mtu huyo alikuwa peku na hakuwa amevaa chochote kichwani, na pia hakuwa amebeba chupa ya maji. ‘Je atawezaji kuswali bila ya kuwa na maji?’ Nilifikiria mwenyewe; nadhani hana habari yoyote juu ya udhu wala swala. Kisha yule mtu akamgeukia ghafla na kumsomea aya ifuatayo ya Qur’an, ‘...Na jueni kwamba Mwenyezi Mungu anajua yaliyomo katika nafsi zenu’ (al-Baqara, 235). Mara nikapoteza fahamu na kuanguka chini. Pindi nilipopata fahamu nilitubia na kuen-delea na safari. Baada ya muda si mrefu nilikutana tena na mtu yule yule. Kwa mara hii nilipomuona nilivutiwa sana na kupatwa na shauku kubwa. Nikaamua kusimama. Kisha akageuka kama pale mwanzo na kusoma, ‘Naye ndiye anaye pokea toba kwa waja wake, na anasamehe makosa, na anayajua mnayo yatenda’ (as-Shura, 25). Baada ya hapo akatoweka kwenye macho yangu. Kamwe sikumuona tena.”*

Dhunnun-i Misri - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - anasimulia jambo kama hilo:

*“Siku moja nilimuona kijana mmoja aliyevaa mavazi yaliyochakaa na yaliyojaa viraka. Ingawa nafsi yangu ilitaka niachane naye lakini ilikuwa kana kwamba moyo wangu unakiri utakatifu wake. Pindi nilipokuwa nim-etekwa kimawazo kati ya nafsi na moyo yule kijana aligundua siri yangu. Baada ya kuniangalia alisema:*

*‘Usiniangalie ewe Dhunnun ili uone ni namna gani nguo zangu zimechakaa. Siku zote lulu hujificha ndani ya lulumizi!’ Kisha akaondoka mbele ya macho yangu.”*

23 Qushayri, ar-Risala, uk.238





Kijana mmoja ambaye alikuwa na *sobah* kwa mtakatifu Abdulkhaliq

Gujdawani kwa mara ya kwanza na ambaye alificha imani yake ya kikiristo alimuuliza juu ya maana ya ndani ya maneno ya Mtume yasemayo, “Kuweni macho juu ya mtazamo wa muumini...kwani hutazama kwa nuru ya Mwenyezi Mungu”. Jibu lake lilikuwa: “Ondoa kizuizi kiunoni mwako na uingie kwenye muislamu!”

Kutokana na kuguswa kwake na maneno yale ya wazi kijana yule alitamka maneno ya *tawhid* mbele ya Sheikh mkubwa na kuwa muislamu pale pale.

Vile vile imepokewa kwamba Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliona mbele kwamba kijana ambaye alijifanya ni muislamu alikuwa ni myahudi na kwamba angeliingia kwenye uislamu muda si mrefu.

Hivyo kuona mbele ni zawadi takatifu ambayo inaweza kuongezeka ama kupungua kutegemeana na kiwango cha imani na uchamungu uliopo ndani ya moyo.





**W**ema na jitihada ni bora kuliko matendo magumu mengi ya utambuzi wa kiroho na karamah. Pia hatuna budi kufahamu kwamba utambuzi wa kiroho na karamah ambavyo havipelekei kuongezeka kwa utii kwenye maamrisha ya dini si chochote bali janga na maangamizi. (Mawlana Khalid Baghdadi).



### 3. UDHIBITI WA KIROHO (TASARRUF) NA KARAMAH

Kutokana na kuwa na uwezo mkubwa pindi Mola anapotaka kitu chochote husema tu 'kuwa' (*Kun*) na kisha kinakuwa. Pamoja na hili kulingana na uwezo mtakatifu Mwenyezi Mungu wakati huo huo amewajaalia baadhi ya waja wake kuwa na udhibiti juu ya baadhi ya mambo. Lakini cha msingi ni kwamba udhibiti huu hauwezi kufanya kazi bila ya kibali cha 'Muumba'. Hivyo kulingana na udhibiti huu watu hawa ni njia tu kama ilivyo kwa malaika wakuu wanne.

Miongoni mwa malaika hawa, kwa mfano Jibril – amani iwe juu yake – amepewa jukumu la kupeleka ufunuo kwa Mitume, Mikail – amani iwe juu yake – amepewa jukumu la kuongoza na kudhibiti matukio ya kiasili, Izrail – amani iwe juu yake – amepewa jukumu la kutoa roho za viumbe na Israfil – amani iwe juu yake – jukumu la kupuliza baragumu ili kuashiria mwanzo wa siku ya kiyama.

Bila shaka Mwenyezi Mungu ana uwezo wa kuyatekeleza majukumu yote haya bila ya kuwahitaji malaika. Lakini bado kwa kupitia uwezo wake aliwapatia majukumu na mamlaka hayo. Uwezo wa malaika unatoka kwa Mola. Yeye ndiye anayewapa nguvu waliyonayo. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa viumbe wote.

Vile vile Mwenyezi Mungu Mtukufu amewapatia Mitume wake mamlaka maalum. Miongoni mwa mamlaka hayo ni yale aliyopewa nabii Suleiman – amani iwe juu yake, yeye alipewa ufahamu wa lugha za wanyama na amri juu ya upepo na majini.

Mjumbe Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye ni imam wa Mitume wote, pia alipewa uwezo wa kipekee, uwezo ambao baadhi ya watu katika umma wake walivuna sehemu yake kwa kadiri walivyoruhusiwa na Mola. Pia kumekuwa kukiripotiwa mara kwa mara mamlaka





waliyokuwa wamepewa baadhi ya watakatifu wakubwa kama vile Abdulqadir Jilani na Ahmed ar-Rufai wakati wakiwa hai na baada ya kufa kwao.

Mamlaka ya kiroho hailetwi na nguvu ya mtu yeyote. Bali mamlaka hayo huja kutokana na ubainifu wa sifa ya Mola ya 'Muumba'. Hivyo mamlaka hayo si jambo la kawaida tu. Tofauti ipo katika hali yake ya kustaajabisha, na kwamba si kila mtu anajaaliwa kuwa mamlaka hayo.

*Karamah* ambayo ni aina ya mamlaka ya kiroho ni jambo lililo nje ya uwezo wa kawaida wa kibinadamu, mamlaka hayo hayawezi kuelezewa na kanuni za asili, na Mola amewapa watakatifu kutokana na imani zao thabiti, uchamungu na elimu ya kiroho. Hii ni *karamah* ya kawaida. Kwani *karamah* ya kweli kama ambavyo imeelezewa na watakatifu ni kuishi katika msimamo (*istiqamah*) bila ya kubadilika badilika. Kwa upande wa mamlaka ya kiroho watakatifu wema wanatofautiana na wanadamu wengine katika utambuzi, kufikiria na hata tabia.

Kama ilivyoelezewa kwenye maana iliyotangulia *karamah* kama ambavyo inadhihirika kwa watakatifu ipo katika aina mbili:

1. *Karamah* ya kiroho: Hii inahusiana na kusonga mbele katika kutafuta elimu za mambo ya dhahiri na ya kiroho, tabia njema na ubora wa kuabudu, yote haya ni ili kufikia kwenye daraja la kiroho ambalo litatoa uhakika wa kupokea maana ya ndani ya aya, "Basi, simama sawa sawa kama ulivyo amrisha" (Hud, 112). Hii inamaanisha *istiqamah*; yani kutoyumba katika njia iliyonyooka. Kwa mfano maneno ya hekima yanayotoka kwenye kinywa cha mtakatifu huwa yanakuwa katika hali ambayo hayaumizi hisia za yeyote, hata pale yanapotolewa kwa ajili ya kumuonya msikilizaji.

Haiwezekani kufikia kwenye hali hii kwa kupitia kwenye kufikiria na kutafakari kimantiki. Huwa Mwenyezi Mungu Mtukufu anampa hali hii yule aliyemteua.

2. Yenye kuhusu maisha (*Kawni*) na *karamah* rasmi: Hizi zinaashiria matukio ya kustaajabisha ambayo hutokea kwenye dunia hii, kama vile kuhama kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine (*tayy-i makan*), kuwafanyawanyama watekeleze mahitaji binafsi na kadhalika.

Wataalamu wa kweli katika usufi huwa hawazingatii sana katika aina hii ya *karamah*. Hata hivyo kubainisha aina hii ya *karamah* si sharti la utakatifu. Pia Mola huwajaalia aina hii ya *karamah* waja wake anaowacha-





gua. Vyovyote iwavyo lakini sufi hawaipi kipaumbele aina hii ya *karamah* mpaka pale inapowalazimu, kwani huambatana na kusifiwa na kutukuzwa na watu. Kisha baada ya hapo wajinga hutarajia kila kitu kutoka kwa mtakatifu.

Hata kama watu wataitazama zaidi aina ya pili ya *karamah*, lakini ya kwanza ndiyo bora zaidi. Ni jambo la kawaida kwa sufi kwamba ‘*Karamah* kubwa zaidi ni msimamo’. Jitihada za mja ambaye hana msimamo huwa hazina maana.

Mawlana Khalid-i Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Msimamo na jitihada ni bora kuliko utambuzi wa kiroho na *karamah* za aina nyingi. Na pia ifahamike kwamba utambuzi wa kiroho na *karamah* ambayo haipelekei kuwa mtii wa maamrishi ya dini si chochote bali ni janga na maangamizi”

*Karamah* ina lengo tukufu; kuwashtusha washuhudiaji, hivyo kuwashawishi wawe na msimamo. Lakini uislamu unatoa fadhila nyingi kutoka kwa Mola, huwafanya wanadamu waweze kutekeleza wajibu wao. Hali hii itaendelea mpaka siku ya mwisho. Kwa upande mwingine mambo makubwa ya kustaaajibisha ni yenye madhara kwa namna fulani. Ndio maana Mitume hawatendi miujiza wala watakatifu kudhihirisha *karamah* mpaka pale inapokuwa hakuna jinsi.

Kwa ujumla *karamah* ya kweli huleta athari mbili:

- 1) Huifunza nafsi.
- 2) Huupusha moyo dhidi ya tabia na matendo mabaya na kuupamba kwa msukumo wa kiroho.
- 3) Huufanya moyo kuzitambua siri na hekima za mambo.

Kwa upande mwingine moja wapo ya njia muhimu ya kubainisha *karamah* ni *Ism-i Azam* ambalo ni jina tukufu kuliko majina yote ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, jina ambalo huwafunulia waja wake kama siri. Tungelipenda kugusia kwa ufupi juu ya maudhui ya *Ism-i Azam* kwa kiwango ambacho itachukua nafasi muhimu katika mjadala wa zawadi takatifu.





*Ism-i Azam* ni moja ya majina ya Mola ambayo yanafanya dua ikubalike pale linapotajwa ndani yake. Lakini bado jina hilo linabakia kuwa siri miongoni mwa majina mengi ya Mwenyezi Mungu, na maneno mengi yamesemwa kuhusiana na hili. Maneno yenye nguvu zaidi miongoni mwa yote ni yale yaliyosema kwamba *Ism-i Azam* ni ‘Mwenyezi Mungu’, jina la Dhati ya Mola, na jina ambalo linayaunganisha majina mengine yote katika upeo wake.

Katika suala hili tuangalie tukio lifuatalo lililotokea kati ya Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na Bedui:

*Siku moja masikini mmoja wa kibedui alimuomba sadaka Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Kutokana na kutokuwa na chochote cha kumpa kwa wakati ule Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alichota mchanga mkononi mwake na kuumba dua na kisha kuupulizia hewa yake na kisha kuuweka kwenye mikono ya yule bedui huku ukiwa umebadilika na kuwa dhahabu. Yule bedui alistaajabishwa na jambo lile. Alianza kumsihi Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – amfahamishe ni namna gani alifanya vile na ni dua gani aliyoiomba kwenye mchanga ule. Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alimwambia dua ile ilikuwa ni al-Fatha huku akiwa ametulia kabisa. Huku akiwa na furaha ya hali ya juu bedui yule akachota mchanga mkononi mwake na kuusomea surat al-Fatha na kisha kupulizia ndani yake. Lakini alishangazwa kuona kuwa ule mchanga ulibakia kuwa mchanga. Hivyo akamuuliza tena kuhusiana na hekima iliyopo kwenye suala hili, naye akajibu kwa kusema:*

“Hii ni tofauti ya nyoyo.”

Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - naye anasimulia tukio kama hili kama ifuatavyo:

*“Siku moja mtu mmoja aliongozana na Yesu – amani iwe juu yake – katika safari yake. Njiani aliona mifupa imekusanyika pembezoni mwa barabara na hivyo akamuomba Mtume amfundishe *ism-i Azam* analolifahamu ili aweze kuirudisha ile mifupa kwenye uhai!”*

*“Uko nje ya fikra zako”, Yesu – amani iwe juu yake – alijibu. “Ili kuweza kutaja *ism-i Azam* na kumfufua maiti unahitaji pumzi safi kuliko mvua na utumishi wenye hadhi kubwa zaidi ya malaika. *Ism-i Azam* linahitaji ulimi safi na moyo uliotakasika...mtu mwenye roho isiyochafuliwa na mambo ya*





*haram na ulio mbali na maasi na madhambi kama malaika. Mtu atakub-aliwa maombi yake pale tu atakapokuwa na roho safi. Mola humfanya mtu huyo azione hazina Zake. Unaweza ukawa umeshikilia fimbo ya Musa mikononi mwako. Lakini je una nguvu alizonazo kiasi kwamba ukaweza kuigeuza na kuwa joka kubwa na kulidhibiti? Hata Musa mwenyewe ali-pata hofu pindi fimbo yake ilipogeuka na kuwa joka kubwa kiasi kwamba Mola akamtuliza kwa kumwambia, “Usiogope, Musa’ (an-Naml, 10). Hivyo hakuna faida ya kujifunza ism-i Azam analolifahamu Yesu wakati huna pumzi kama aliyonayo yeye!”*

*Lakini mtu yule mjinga aliendelea kung’ang’ania. “Kwa kuwa sina nguvu kama hizo, je huwezi angalau kuisomea ile mifupa pale ili uihuishie?”*

*Kutokana na kustaajabishwa kwa kuona bado mtu yule mjinga anang’ang’ania, Yesu – amani iwe juu yake – akasema, “Je kuna hekima gani katika kuisisitiza kwake ewe Mola wangu? Kwa nini mtu huyu mjinga ameegemea kwenye mjadala? Anataka kuihuisha mifupa wakati angelita-kiwa kuuhuisha moyo wake ambao umekufa na kubakia mifupa. Badala ya kuomba kwa ajili ya yeye kuhuishwa, anataka kuihuisha mifupa. Ni ujinga wa namna gani huu!”*

Hivyo waja wema wa Mwenyezi Mungu ni wale ambao wamefikia kwenye hatua hii ya ukomavu. Pindi *karamah* inapokuwa imeingia kwa mtakatifu hisia zake za kushukuru kutokana na baraka za Mola huongeze-ka zaidi. *Karamah* huwapa msukumo katika majukumu waliyonayo. Lakini watakatifu wa kweli *karamah* yao haiwafanyi wakajiona wako salama kabisa kwa maisha yao ya kesho akhera. Kinyume chake hujawa na hisia za udhalili na unyenyekevu mbele ya Mola, na hivyo huziweka pembeni nafsi zao zaidi ya ilivyokuwa hapo kabla. Kwa kuwa kamwe hawawezi kuwa na uhakika juu ya kutoangukia kwenye majivuno na mitihani, jambo hili linawafanya waendeleo kuwa na hofu wakati wote.

Mwisho wa kustaajabisha wa Balam Ibn Baura, mtu ambaye Mwenyezi Mungu alimfunulia ism-i azam, unatupatia mazingatio mengi. Waiz-rael walimtambua mtu huyu kama mwanachuoni na mtakatifu. Lakini kadiri muda ulivyosogea aliangukia kwenye majivuno na kudanganywa na mambo ya kidunia na hatimaye akapoteza hadhi yake ya kuheshimiwa; na hata akafa kafiri. Suala lake linazungumziwa ndani ya Qur’an kama ifuatavyo:





“Na wasomee khabari za yule ambaye tulimpa Ishara zetu, naye akajivua nazo. Na She’ani akamuandama, akawa miongoni walio potea. Na tungelitaka tungeli mtukuza kwa hizo Ishara, lakini yeye aliushikilia ulimwengu na akafuata pumbao lake. Basi mfano wake ni mfano wa mbwa. Ukimhujumu hupumua na kutoa ulimi na ukimwacha pia hupumua na kutoa ulimi. Huo ni mfano wa kaumu wanao zikanusha Ishara zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari.” (al-Araf, 175-176).

Hivyo kumpenda kupita kiasi mtakatifu ambaye ana mamlaka juu ya *karamah* limekuwa ni jambo la hatari mno. Imekuwa hatari zaidi pale mtakatifu anapokuwa hapendi kuweka wazi *karamah* yake. Lakini vyovyote iwavyo *karamah* sio kiwango cha mwisho cha daraja za kiroho na haidhihirishi kwa namna yoyote ile kiwango cha juu cha imani ya mtakatifu. Wale waja wema wanatambua vyema kwamba hakuna mtu aliyepewa uhakika wa furaha ya kesho akhera isipokuwa Mitume. Watu wengi huingia peponi baada ya kuukaribia Moto kwa inchi moja; na wengine wengi huzamishwa kwenye mashimo ya Moto huku wakiwa wamebakisha hatua moja ili waingie peponi. Hivyo muumini hana budi kushikamana na mwenendo bora katika maisha yake yote:

“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie Yakini” (al-Hijr, 99).

Kama ilivyo kwa mambo mengine yote, kipimo chetu kikubwa kulin-gana na baraka takatifu zinazotujia kama *karamah* ni Qur’an na *Sunnah*. Hivyo ukweli wa *karamah* unasimama kama kithibitisho cha kweli kisi-chopingika.

Baadhi ya ushahidi kutoka ndani ya Qur’an kuhusiana na ukweli wa *karamah* ni kama ifuatavyo:

Asaf ambaye alikuwa mshauri wa Suleiman – amani iwe juu yake – alimhakikishia kwamba angeliweza kukileta kiti cha Balqis ‘kwa mpepeso wa jicho” (an-Naml, 40) na maneno yake yakawa kweli.

Zakariyya – amani iwe juu yake – alipewa jukumu la kumlea Mariam - amani iwe juu yake, Mariam ambaye alijitolea kukaa hekaluni kwa ajili ya kuabudu. Kila alipokuwa akiingia ndani ya hekalu alikuwa akimkuta Mariam amezungukwa na aina mbalimbali za Vyakula. Pindi alipokuwa akimuuliza juu ya mahali vinapotoka vyakula vile alikuwa akipokea jibu lifuatalo:







“Kutoka kwa Mwenyezi Mungu...” (Al-i imran, 37). Aya za 24 na 25 kutoka katika surat Al-Imran ambazo zinadhihirisha zaidi namna Mariam – amani iwe juu yake – alivyolishwa moja kwa moja na Mwenyezi Mungu Mtukufu zinathibitisha zaidi juu ya ukweli wa *karamah*.

Ushahidi kutoka katika *Sunnah* ni mwingi zaidi: “Kuna watu watatu walioongea wakati angali wachanga”, Mtume aliyeathirika – rehma na amani ziwe juu yake – amesema. “Yesu mwana wa Mariam, mtoto aliye kuwa amepewa Jurayj na mtoto mwingine.” Kisha aliendelea kufafanua.<sup>24</sup>

Hadith nyingine inaelezea juu ya wasafiri watatu waliokwama kwenye pango walilokuwa wamepumzikia ndani yake wakati wa usiku; jiwe kubwa liliporomoka na kuja kuziba sehemu ya kutokea. Ili kuweza kutoka kila mmoja wao aliomba kwa kutaja jema alilokuwa amelifanya kwa ajili ya kutafuta radhi za Mola pekee, na matokea yake lile jiwe likajisogeza kidogo kidogo mpaka likatoa njia ya kutokea.<sup>25</sup>

Anas - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea:

“Siku moja usiku *Usayd ibn Khudayr na Abbad ibn Bishr* walikuwa wakitembea karibu na Mtume – rehma na amani ziwe juu yake. Pindi walipoachana naye waliona taa za aina mbili mbele yao zikiwamulikia njia. Na pindi walipotengana, taa moja ilimfuata mmoja wao na nyingine kumfuata mwingine.” (Bukhari, Salat, 79; Masajid, 78, Manaqib, 28, Manaqibu'l-Ansar, 13).

Tukio jingine lenye kuthibitisha *karamah* ya swahaba ni pale Hubayb - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipokuwa amekamatwa na washirikina na kufanya mateka. Katika majira ambayo hakukuwepo na matuna Hubayb - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alionekana akila zabibu zilizoiva vizuri. (Bukhari, Jihad, 170; Maghazi, 10,28).

Pia imesimuliwa kwamba wakati Omar - radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipokuwa anahutubia watu juu ya *mimbar* mara alisema, “Kwenye mlima, Sariya, kwenye mlima!” Wakati alipokuwa anayasema maneno haya ambayo hayakuwa na uhusiano na kile alichokuwa anakizungumzia Sariya alikuwa katikati ya vita akiliongoza jeshi la waislamu katika sehemu yenye umbali wa mwezi mmoja kutoka Madina. Lakini

24. Rejea Muslim, Birr, 8.

25. Rejea Bukhari, Adab, 5; Anbiya, 53; Dhikr, 100.





Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyafanya maneno haya yasikike kwake. (Ibn Hajar, al-Isabah, II, 3).

Maisha ya maswahaba yalikuwa kama hivyo.

Kinyume na *karamah* tunaweza kuona matendo mengine magumu yenye kustaajabisha kutoka kwenye mikono ya watu fulani ambao wanaweza kuwa makafiri au ambao wanajifanya kuwa watakatifu, matendo haya kimuonekano huwa sawa na *karamah* halisi. Matendo haya ya kustaajabisha na ambao hayatokani na utakatifu yanaitwa *istidraj*.

Matendo haya hutokana na mazoezi fulani ya kiroho. Kwa maneno mengine ni kwamba inawezekana kukubaliana na uwepo wa nguvu fulani zinazoihusisha roho kwa kupitia ushawishi usio wa kidini. Kwa mfano Hindu fakirs wanafahamika kwa kuwa kwao na nguvu za kiroho hasa kwa kupitia kwenye kujizuia. Wakati mwingine nguvu hizi hutokana na mazingaumbwe au kukusanya *khuddam*<sup>26</sup> kutoka kwa majini. Kuyatofautisha matendo haya na *karamah* ya kweli ni suala linalohitaji elimu. Tunaweza kuona kuwa maisha ya watu wenye *istidraj* hayaendani na viwango vya *taqwa* au uchamungu. Huwa yanakosa kushikamana na *Sunnah* ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Hili ni jambo la kwanza la kuzingatia katika suala hili. Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amesema:

“Pindi utakapomuona mtu anapaa angani na huku maisha yake hayaendani na Qur’an na *Sunnah* usidanganyike kwani hiyo ni *istidraj*.”

Hata hivyo mtu aliyejaaliwa na Mola kuwa na mamlaka juu ya *karamah* kamwe asingeljaribu kujionyesha. Kwa kuwa watakatifu wa kweli hawana kasoro ya kujionesha, huidhihirisha *karamah* yao pale inapokuwa hakuna budi. Badala yake hujipamba na mwenendo mwema wa kimaadili kiasi kwamba watu wengine wanaweza kuwaiga. Tunaweza kulinganisha jambo hili na ukweli kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiishi kulingana na mazingira ya kawaida ya kibinadamu ili kuwa mfano kwa umma wake na alidhihirisha miujiza kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu pale tu ilipobidi. Waja wema wa Mola huwa

26 Kwa kupitia visomo fulani unaweza kumuweka jini chini ya amri yako na kumtumia kama mtumishi. Jini wa aina hiyo anaitwa *khuddam*, mtumishi. *Khuddam* hutekeleza amri za yule aliyeungana naye kwa kadiri ya uwezo wake.





hawatoki kwenye mwenendo wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – hata kwa urefu wa sharubu. Haya peke yake yanatosha kutofautisha kati ya *karamah* na *istidraj*.

Firauni alikuwa mmoja wa watu waliokuwa na mamlaka juu ya *istidraj*. Katika kipindi chake chote cha miaka mia nne (kulingana na baadhi ya mapokezi) alichoiishi hapa duniani hakuwahi kuugua hata kichwa. Meno yake yote yalikuwa kamili wakati wa kifo chake. Pia inasemekana kwamba pindi alipokuwa akisafiri na farasi wake kuelekea chini ya vilima miguu ya mbele ya farasi wake ilikuwa ikiongezeka urefu.

*Istidraj* humfanya kafiri ajivune na kujiona na mwisho wake huwa mbaya sana. Pindi Firauni alipoona Musa – amani iwe juu yake – ameichapa bahari nyekundu na hivyo bahari kujigawa na kutengeneza njia kavu kwa ruhusa ya Mola, aliwageukia askari zake na kupiga kelele:

“Angalieni! Bahari imejitenga kutokana na utukufu wangu!” Hakutambua kwamba kama angelimruhusu farasi wake kuelekea kwenye ile njia bahari nyekundu ingelimmeza yeye na watu wake ndani ya vina vya bahari.

Pia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ametufahamisha kwamba Dajjal naye atadhihirisha namna nyingi za *istidraj* ili aweze kuwadanganya watu.

Pia kuna wakati matokeo ya *istidraj* yanakuwa tofauti kabisa na vile mtu alivyotarajia. Hizi zinaitwa *ikhanah*, usaliti wenye kudhalilisha. Muongo mmoja aitwaye Musaylamah ambaye alidai kuwa mtume siku moja alitema mate kwenye kisima kwa lengo la kuongeza maji yake. Lakini kwa mshangao aliona kisima chote kikikauka.

Kama ambavyo iliwezekana kwa *karamah* na *istidraj* kusambaa katika kipindi cha Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na maswahaba, basi ubainifu wake katika nyakati zilizofuata ni jambo lenye kuwezekana pia. Utambuzi wa kiroho na *karamah* zinazobainishwa na baadhi ya watakatifu kwa lengo la kuwaongoza watu wenye kuwafuata ni jambo lenye kufanyika kwa kupitia baraka za Mtume wanayemfuata; hivyo wakati huo huo zinakuwa na muendelezo wa miujiza yake.

Ni ukweli wa kihistoria usiopingika kwamba utambuzi wa kiroho na *karamah* zilizodhihirika katika kipindi cha maswahaba na nyakati zilizowafuatia ziliwangoza wengi kuelekea kwenye uongofu. Watu wen-





gine wengi wa pembeni wamefikia kukiria kwamba, ‘Kama dini hii ina watakatifu kama hawa, si jambo la kuuliza ni vipi atakuwaje Mtume wao’, kiasi kwamba wakafikia kumthibitisha Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kama kitovu cha kila *karamah*.

### **Baadhi ya matukio ya utambuzi na *karamah***

Ili kumuabudu Yeye pekee na kujituma hapa duniani, Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ndiye Muumba na mtawala wa ulimwengu amewafanya wanadamu kuwa wawakilishi wake (*khalifah*). Jambo hili linathibitishwa na Qur’an kama ifuatavyo:

وَ إِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلٰٓئِكَةِ اِنِّىْ جَاعِلٌ فِى الْاَرْضِ خَلِيْفَةً

“Na pale Mola wako Mlezi alipo waambia Malaika: Mimi nitamweka katika ardhi Khalifa (mfwatizi), wakasema: Utaweka humo atakaye fanya uharibifu humo na kumwaga damu, hali sisi tunakutakasa kwa sifa zako na tunakutaja kwa utakatifu wako? Akasema: Hakika Mimi nayajua msiyo yajua.” (al-Baqara, 30).

‘Uwakilishi’ wa mwanadamu unabeba maana zifuatazo:

“Nitampatia baadhi ya mamlaka kutokana na nguvu na sifa zangu; na na yeye kama muwakilishi wangu atakuwa na mamlaka juu ya viumbe vyangu katika kuifanyia kazi sheria yangu kwa niaba yangu. Lakini hatakuwa mtendaji mkuu; hataifanyia kazi sheria kwa niaba yake na kwa ajili yake. Yeye atakuwa wakala na kaimu wangu tu. Atawajibika kutekeleza matakwa Yangu, amri Zangu na sheria Zangu. Na wale watakaokuja baada yao watalazimika kuendelea na jukumu hilo hilo kama ilivyokuwa kwa waliowatangulia, jambo ambalo litadhihirisha siri ya kwamba, ‘Naye ndiye aliyekufanyeni makhalifa wa duniani...’ (al-Anam, 165)” (Elmalili, Hak Dini, 1, 299-300)

Vyote miujiza waliyokuwanayo Mitume na amri na *karamah* zinazoonekana kwa watakatifu vinatoa mwangaza juu ya mwanadamu kuwa kwake muwakilishi wa Mola. Miongoni mwa matukio mengi ya ubainifu wake baadhi yake ni haya yafuatayo:





*Mansur ibn Abdullah anasimulia yafuatayo kumhusu Abu Abdullah Ibn Jalla: "Siku moja Ibn Jalla alinisimulia jambo moja kuhusiana na yeye:*

*'Nilikuja Madina huku nikiwa sina chochote mfukoni. Nikaenda kwenye kaburi tukufu la Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Baada ya kumtolea salamu nilisema, 'Mimi nipo katika umasikini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, na nimekuja kama mgeni wako.'*

*Baada ya muda mfupi nilishikwa na usingizi na kulala. Ndani ya ndoto Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alinipatia kipande cha mkate. Nikala nusu yake. Na pindi nilipoamka nilikuta ile nusu nyingine ipo pembeni yangu."<sup>27</sup>*

Tukio jingine la kuzingatia na ambalo lilitokea baada ya kufariki kwa Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – limesimuliwa na al- Utbi kama ifuatavyo:

*"Nilikuwa nimekaa karibu tukufu na kaburi la Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, mara bedui mmoja akaja na kusema yafuatayo kwa sauti ambayo niliweza kuisikia:*

*'Rehema na amani ziwe juu yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Nilimsikia Mwenyezi Mungu Mtukufu akisema, '...Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangeli kujia, wakamwomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.' (an-Nisa, 64). Hivyo nimetubia madhambi yangu na kuomba msamaha na nimekuja kukuomba uniombe kwa Mola wangu badala yangu.'*

*Kisha akasoma shairi zuri na kuondoka. Baada ya muda mfupi nilishikwa na usingizi. Ndani ya ndoto nilimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye aliniambia 'mtafute yule bedui na umpe habari njema kwamba Mwenyezi Mungu amemsamehe.'" (Ibn Kathir, Tafsir, 1, 532).*



*Pindi vita vilipopamba moto wakati wa vita vya Gallipoli meja wa jeshi*

<sup>27</sup> Rejea Kalabazi, *Taarruf, iliyotafsihiwa na S. Uludag, uk. 214*





Lutfi Bey alipiga ukelele, “Njoo ewe Muhammad! Kitabu chako kimepotea!”<sup>28</sup>, huku akiomba msaada wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa shauku kubwa. Pia maombi hayo yamebainika katika tukio lifuatalo:

*Ulikuwa mwaka 1928...ilikuwa imepita miaka thelathini kamili tokea upatikane ushindi pale Gallipoli.*

*Cemal Ogut Effendi wa Alasonya ambaye alikuwa mtu mwenye elimu na hekima alikuwa katika hijja ndani ya Madina, mahali ambapo alikuwa na bahati ya kukutana na watu wengi muhimu. Miongoni mwa watu hao alikuwepo msimamizi wa kaburi tukufu la Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Wakati huo huo mtu huyo alikuwa ni kipenzi cha watu wa Uthmainiyya, mapenzi yake alikuwa akiyadhihirisha katika kila fursa aliyokuwa akiipata. Baada ya mazungumzo mafupi Cemal Ogut Effendi alishindwa kujizuia na hivyo akamuuliza juu ya sababu iliyompelekea kuwapenda watu wa dola ya Uthmainiyya.*

*Mtu mzima yule alimwambia maneno yafuatayo bila kusita huku uso wake ukiwa unang’aa:*

*“Kumbukumbu yangu moja tu ambayo nitakwambia itatosha kuwa kishawishi cha kupelekea mimi kuwapenda watu wa dola ya Uthmainiyya kwa ajili ya uislamu. Itakuwa ni mwaka 1915 ambao ndani yake mwana-chuoni mmoja kutoka India alikuja kwa ajili ya hijja. Utajiri wa nafsi ya mtu yule haukuhitaji ushahidi zaidi; alikuwa mtakatifu katika kila nyanja. Nilimuona kwa mara ya kwanza karibu na kaburi la Mtume Mkuu – rehema na amani ziwe juu yake; aliwasili hapa baada ya kumaliza hijja yake. Alionekana ni mwenye huzuni sana. Nilidhania machozi yaliyokuwa yakitiririka kutoka kwenye macho yake yasingelikuja kuisha. Ilibidi nimuulize juu ya sababu ya huzuni yake. Hivyo nilimuuliza. Alianza kulia zaidi na kusema:*

*‘Baada ya miaka mingi ndio sasa hivi nimepata fursa ya kumtembelea mtu mtukufu kuliko wanadamu wote hapa duniani na kesho akhera. Lakini nafsi yangu inaniambia kuwa atakuwa hayupo katika sehemu yake ya kawaida. Je ni kwamba jicho la moyo wangu limepofuka? Ni kwa nini siwezi kuhisi uwepo wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake? Nimekuwa*





*nikisumbuliwa na fikra hizi tokea siku ya kwanza kutia mguu wangu ndani ya Madina!*

*Usiku ule ule nilipata bahati ya kumuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ndani ya ndoto. Niliyakumbuka maneno ya yule mwanachuoni wa kihindi. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – hakuniacha kwenye wasi wasi. ‘Anachokihisi ni cha kweli’, alisema. ‘Sasa hivi siko Madina. Moyo wangu usingeliweza kuvumilia kuwaacha watoto wangu kwenye tabu peke yao katika uwanja wa mapambano. Sasa hivi ninawasaidia.’”<sup>29</sup>*

*Kukiri kwa Generali wa kiingereza aliyeitwa Ian Hamilton baada ya kushindwa pale Gallipoli ni ushahidi tosha juu ya maneno yaliyotangulia: “Hatukushindwa na nguvu ya kiwiliwili ya waturuki; nguvu yao ya kiroho ndiyo iliyotushinda. Hawakuwa wamebakia na risasi hata kidogo za kuweza kutushambulia. Lakini tuliona vikosi vikiwasili kutoka angani kwa macho yetu.”*

Matukio kama haya yanatokana na amri ambazo Mwenyezi Mungu huwapa Mitume yake baada ya kuiaga dunia. Mitume huendelea kuishi ndani ya makaburi yao kwa namna ambayo haiwezi kutambulika kwa kutumia viungo vyetu vya fahamu. Hadith ifuatayo inalithibitisha hili kwa uwazi kabisa:

Aws Ibn Aws – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - amesimulia kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

*“Siku bora kuliko masiku yote ni siku ya ijumaa. Hivyo fanyeni hima kunitumia salamu nyingi katika siku hiyo, kwani salamu zenu huletwa moja kwa moja kwangu.” Baada ya kuyasikia haya maswahaba waliuliza:*

*“Ni vipi salamu zetu zitaletwa kwako baada ya wewe kufa na kuto-bakiza chochote katika kiwiliwili chako?”*

*“Mwenyezi Mungu Mtukufu amejaalia miili ya Mitume isioze chini ya ardhi.” (Abu Dawud, Salat, 201; See, Nasai, Juma, 5).*

Hali hii ya kuwa hai pia inawahusu mashahidi kama ambavyo imeelezwa ndani ya Qur’an:

29. Kutoka kwenye gazeti la Zaman la tarehe 18 machi 2001.





“Wala kabisa usiwadhania walio uliwa katika Njia ya Mwenyezi Mungu kuwa ni maiti. Bali hao ni wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi” (Al-ilmran, 169).

Kwa mtazamo huo kuwa kwake Mtume hai ni kuzito zaidi ya masha-hidi.

Ubainifu wa amri na *karamah* za watakatifu ambao ndio warithi Mitume umeendelea mpaka leo. Ifuatayo ni mifano michache juu ya hili:

Ubaydullah Ahrar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alihama Asia ya kati (*tayy-i makan*) kwa ajili ya kushika nafasi yake katika kuit-waa Istanbul. Suala hili limesimuliwa na mjukuu wake aliyeitwa Khawaja Muhammad Qasim:

*“Ilikuwa ni Alhamisi mchana pindi Ubaydullah Ahrar alipoagiza aan-daliwe farasi wake. Alimpanda farasi wake kisha akatoka nje ya Samarkand. Mawlana Sheikh ambaye alikuwa mwanafunzi wake maarufu alimfuata baada ya muda mfupi. Baada ya muda mfupi alirejea na kuwaambia wen-gine kwamba farasi wa Ubaydullah Ahrar alienda kushoto na kisha kulia na kisha akatoweka kwenye macho yangu. Baadae alirejea Samarkand na kusalimiwa na wanafunzi wake ambao walikuwa na shauku ya kufahamu sababu ya safari yake ya ghafla.*

*‘Mehmed Khan ambaye ni Sultan wa Waturuki aliomba msaada wangu’ alielezea, ‘Ndio maana nikaenda kumsaidia. Na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu Mtukufu tulipata ushindi.’”*

*Khawaja Abdulhadi ambaye alikuwa mjukuu wa Ubaydullah Ahrar na ambaye miaka michache baadae alikuja Istanbul kutokea Samarkand anasimulia yafuatayo:*

*“Pindi nilipoenda Istanbul nilimtembelea Sultan Bayazid II ambaye baada ya kunielezea muonekano wa babu yangu alinielezea yafuatayo:*

*‘Siku moja baba yangu aliniambia yafuatayo: Katikati ya mapambano makali ya Istanbul nilimuomba Mola anitumie qutb ya muda kwa ajili ya msaada. Muda si mrefu akajitokeza katika muonekano huu na huu akiwa juu ya farasi mweupe na kunihakikishia kwamba nisihofia chochote kwani ushindi ni wetu.*







*gua kaftani yake na kuniambia niangalie ndani yake. Ndani ya mikono ya kaftani yake niliona jeshi kubwa likitiririka kama mafuriko makubwa.*

*'Jeshi hili limekuja kunisaidia', alisema, baada ya hapo aliongezea, 'sasa panda juu ya kile kilima na kisha upige ngoma mara tatu na kisha uliamrishe jeshi lako lishambulie'.*

*Nilifanya kama alivyonielekeza. Na yeye pia alishiriki kwenye mapambano yale pamoja na jeshi lake. Hatma ya Istanbul ikapatikana..."<sup>30</sup>*

Hivyo ni ukweli wa kihistoria kwamba Sultan Mehmed alipata msaada wa kiroho kwa ukamilifu wake. Hasa tukio maarufu ni msaada wa kiroho na kimwili alioutoa Aksemseddin - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake.

Moja ya tukio linaloashiria amri ya kiroho ya Aziz Mahmud Hudayi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ni hili lifuatalo:<sup>31</sup>

*Ulikuwa ni mwaka 1975. Muda wa swala ya zuhr ulikuwa umekaribia pindi kijana mmoja mnene na mweusi na aliyekuwa na muonekano wa kirafiki alipowasili katika kaburi la mtakatifu mkubwa. Kwa bahati mbaya akakutana na Muharrem Effendi ambaye alikuwa imam wa msikiti wa Aziz Mahmud, mtu ambaye alimfikishia shida yake.*

*"Tafadhali bwana", alisema. "Nimekuja kumuona Aziz Mahmud Hudayi. Je inawezekana nikamuona sasa hivi? Je sasa hivi yuko hapa?"*

*Huku akistaajabishwa kuulizwa swali kama lile Muharrem Effendi alinyamaza kidogo na kisha akasema, "Ndio mwanangu. Aziz Mahmud Hudayi yupo."*

*Huku akionekana amefurahishwa na kusikia maneno yale alimuomba imam "Tafadhali niruhusu nikamuone!"*

*Alipoona bado kijana yule hajaelewa imam alirudia maneno yake ya awali akitumaini kuwa yule kijana angelitambua kuwa walikuwa wamesimama pembeni ya kaburi alilotaka kuliona.*

<sup>30</sup> Nililisikia tukio hili mimi mwenyewe kutoka kwa Muharrem Kir Effendi ambaye alikuwa mwanafunzi mwenzangu katika (Shule ya) Imam Hatip Lise.

<sup>31</sup> Rejea Mawlana Sheikh, Manaqib Khawaja Ubaydullah-i Ahrar, 4b-5a; Majdi Mehmed, Khadaiqu's-Shaqaiq, uk. 272-273; Molla Jami, Nafakhatu'l-Uns, uk. 764-765.





“Kwa hakika Aziz Mahmud Hudayi yupo hapa”, alisema. Lakini yule kijana bado alirudia ombi lake.

“Kama ni hivyo basi niruhusu nimuone. Ninataka kumuona.”

Ili kufikia muafaka Muharrem Effendi alimuuliza, “Mwanangu, je unamfahamu kweli Aziz Mahmud Hudayi?”

Kutokana na kuchoshwa kwake na maswali haya yaliyoonekana hayana maana pamoja na usumbufu wa imam usioelezeka katika kumzuia asimuone Sheikh, kijana yule ambaye usafi wa moyo wake ulikuwa ukiendana na muonekano wake alisema:

“Ninamfahamu Aziz Mahmud Hudayi kwa undani. Yeye mwenyewe alinialika kuja hapa. Nilimuahidi ningelikuja na yeye analifahamu hili fika.”

Mwishowe Muharrem alitambua kwamba suala lile lilikuwa ni muhimu na lenye kustaajibisha.

“Ulimuahidi vipi kwamba ungelikuja?” alimuuliza kwa shauku. Yule kijana akaanza kumuelezea:

“Nilikuwa miongoni mwa makanda waliodondoshwa kwenye mapambano kutoka kwenye ndege, mapambano hayo yalikuwa katika kipindi cha shughuli za amani za Cyprus za 1974. Katikati ya mapambano makali kati ya vikosi vyetu vilivyokuwa ufukweni mwa bahari na wagiriki wa Cyprus waliokuwa wakijaribu kutufukuzia mbali na ngome zao katika milima ya Besparmak tulishuka chini kwa kutumia maparachuti. Lakini upepo mkali ulisababisha kila mtu ashukie sehemu yake mbali kabisa na pale walipotarajia kushukia. Mimi nilishukia katikati ya maadui. Nilijikuta nipo katikati ya mapambano makali ya kurushiana risasi kati ya pande zote mbili. Pindi nilipokuwa nimesimama pale huku nimeduwaa na bila kujua la kufanya alitokea mtu mmoja mrefu na aliyekuwa na muonekano wa kubembeleza. Aliniangalia kwa tabasamu zuri na kuniambia:

‘Unafanya nini hapa mwanangu? Huu ni upande wa maadui. Kwa nini umekuja hapa peke yako?’

‘Baba’, nilisema, ‘sikushuka mwenyewe hapa...nilidondoshwa hapa na upepo.’

Mtu mzima yule aliyekuwa na sura yenye kung’aa alitingisha kichwa





*kidogo na kusema, 'Na mimi pia nimekuja kupambana. Nilitumwa kuja hapa muda mrefu kabla yako. Ninalifahamu eneo hili kama mgongo wa kiganja changu. Umetoka kwenye platuni ipi? Njoo...ngoja nikupeleke kwenye platuni yako!'*

*Hivyo nilimfuata nyuma huku risasi zikipita juu ya vichwa vyetu. Lakin ni mtu yule mkubwa alikuwa akitembea kana kwamba anatembea kwenye barabara iliyo na utulivu. Nilishangazwa na mwenendo wake kwa ujumla. Njiani aliniuliza maswali mengi mno; jina langu, nilikotoka na kadhalika. Niliyajibu maswali yote, na mimi nikamuuliza swali.*

*'Na wewe unaweza kuwa nani, Baba?'*

*'Wananiita Aziz Mahmud Hudayi', alijibu.*

*'Baba', niliongezea, 'umenifanyia fadhila kubwa. Pindi nitakaporejea nyumbani kwa amani ningelipenda nikutembelee kutokana na kuthamini msaada wako. Je unaweza kuniachia anuani yako?'*

*'Njoo Uskudar na kisha uniulizie', alisema. 'Mtu yeyote atakuonyesha nilipo!' Hiyo ndiyo anuani aliyonipa.*

*Muda si mrefu tulifikia kwenye platuni yetu. Nilibusu vichwa vya watu wakubwa kwa upendo na heshima. Kisha nikaagana nao na kuungana na kamanda wangu.*

*Mara baada ya kamanda wangu kuniona sijadhuriwa hata kidogo na wakati aliona isingeliwezekana mtu akaingia katikati ya mapambano yale makali na akatoka bila ya kudhurika, aliniuliza:*

*'Umewezaje kuja hapa?'*

*'Baba mmoja mzuri ndiye aliyenileta hapa', nilijibu.*

*Baada ya mapambano kusitishwa nilirejea nyumbani. Lakini nilishindwa kujizuia kuifikiria fadhila kubwa niliyoipata kutoka kwa Aziz Mahmud Hudayi; hivyo nimekuja Uskudar kwa ajili ya kumtembelea ili kuonyesha shukurani. Watu niliowauliza wamenielekeza hapa na kuniambia kuwa yeye ni mtu mtukufu”.*

*Yule kijana akatulia kidogo na kuvuta pumzi, kisha akarudia ombi lake la pale awali:*

*“Hivyo ndivyo tulivyokutana. Sasa tafadhali niruhusu nionane naye.*





*Huku akiwa ametekwa na maneno ya kijana yule Muharrem Effendi hakuweza kusema chochote kwa kijana yule na hivyo kubakia ameduwaa. Akajitahidi kurudisha hali yake ya awali na kuweza kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:*

*“Mwanangu...Aziz Mahmud Hudayi hayuko hai kimwili. Yeye ni mtakatifu mkubwa ambaye aliishi kati ya 1543 na 1628. Lazima atakuwa amekuuta uje hapa kwa ajili ya kumsomea Fatha. Kaburi lake lile pale...”*

*Baada ya kijana yule mtiifu na mwaminifu kusikia habari zile alihuzunika sana. Lilibakia kaburi la mtakatifu ambaye alikuja kumtembelea na ambaye alimuokoa maisha yake. Pale ndipo alipoitambua amri ya kiroho aliyokutana nayo katika mapambano yale makali. Alianza kulia. Alilia kwa dakika kadhaa huku akiwa ameziba uso wake kwa mikono.*

*Hakuwa peke yake katika kulia. Na imam pia alikuwa akilia...*

*Moja ya kumbukumbu za mtakatifu Mahmud Sami Ramazanoglu ambazo tulizisikia moja kwa moja katika moja ya sohbah zake ni hii ifuatayo:*

*Dada wa Mahmud Sami ambaye alikuwa nyuma kwa miaka miwili alikuwa kilema wa miguu yote miwili. Karibu na walipokuwa wakiishi lilikuwepo kaburi la mtakatifu aliyefahamika kwa jina la Kaplanci Baba, kaburi lake lilikuwa likitembelewa na watu mara kwa mara. Siku moja na yeye alienda kulitembelea kaburi lake huku akiwa ameongozana na mama yake na dada yake mdogo, walikesha pale kaburini. Pindi walipokuwa kati-kati ya usingizi waliamshwa na makelele ya yule dada yake ambaye kilema. Mama yake alimkimbilia ili kumuuliza tatizo lilikuwa ni nini. Huku akiwa na wasiwasi yule msichana alielezea kwamba mzee mmoja alinyanyuka kutoka kaburini na kuminya miguu yake miwili. Sami Effendi ambaye ndiye aliyesimulia hii kumbukumbu alisema kwamba kuanzia siku ile mpaka mauti yalipomfika dada yake aliweza kutembea bila ya kuhisi maumivu hata kidogo kwenye miguu yake.*

*Matukio yaliyoelezewa na mengine kama hayo ni baraka takatifu za mamlaka ya amri za kiroho ambazo Mwenyezi Mungu amewajaalia baadhi ya waja wake. Lakini isisahaulike kwamba mtendaji kabisa ni Mwenyezi Mungu mwenyewe. Msaada aliowapa waja wake kwa kupitia malaika na watakatifu umekuwa ukiendelea mpaka leo.*





**N**doto ya kweli aiotayo muumini ni moja ya arobaini na sita ya utume. (Bukhari, Tabir, 26; Muslim, Ruya, 6).



#### 4. NDOTO ZA KWELI

Ndoto za kweli ni miongoni mwa zawadi takatifu, zinachukuliwa ni moja ya njia za kutambua uhalisia wa mambo yasiyoonekana. Pindi mtu anapokuwa amelala muunganiko wake na dunia hupungua sana na hisia za kiroho zilizo ndani yake huimarishwa. Mawingu ya nafsi ambayo huziba utukufu husambaa na kuruhusu muonekano mzuri. Kutazama ndani ya ulimwengu usioonekana kwa namna hii kumefanywa kuwezekane kwa baadhi ya watu wema. Uthibitisho wa kile kilichoonekana ndani ya ndoto hizi huja baadae baada ya kuamka.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

“Bishara njema (*Mubashshirat*) peke yake ndizo zinazoachwa baada ya utume”, baada ya kuyasema hayo maswahaba waliokuwepo pale walimuuiliza juu ya maana hasa ya hizo bishara njema.

“Ndoto ya kweli”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alijibu. (Bukhari, Tabir, 5; Muslim, Salat, 207-208).

*Mubashshirat* huonekana pindi nyoyo za waumini zinapokuwa na uwezo wa kupokea ufunuo wa kiroho na bishara njema wakati wa ndoto.

Katika kufafanua maana ya maneno ‘bishara njema ndani ya maisha ya duniani’ kama ilivyokuja katika aya “Wao wana bishara njema katika maisha ya dunia na katika Akhera...” (Yunus, 64), Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

“Hizo ni ndoto za kweli ambazo muislamu huziona au hufanya azi-one.” (Tirmidhi, Ruya, 3).

Kuna aina tatu za ndoto:

**1. Ndoto za kishetani:** Hizi ni ndoto zinazosababishwa na shetani ili



kumuingizia mtu hofu, mahangaiko na huzuni; kama ndoto ambazo ndani yake mtu hujiona akidondoka kutoka kwenye mlima au huona majanga na shida ambazo humpelekea kukata tamaa. Ndoto hizi hazina maana. Pindi mtu atakapoota ndoto kama hizo yenye kuchanganya na ambazo hawezi kuzikumbuka vizuri asimuhadhithie mtu yeyote na badala yake atafute ulinzi wa Mwenyezi Mungu ili amlinde dhidi ya ushawishi wa shetani.

Abu Said al-Khudri – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisimulia kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alisema: “Pindi mmoja wenu atakapoota ndoto ambayo ataifurahia basi na afahamu kwamba ndoto hiyo inatoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo hana budi kumshukuru Mwenyezi Mungu na kuisimulia kwa wengine.”

Kutokana na masimulizi mengine ni kwamba:

“Aliyeiota hana budi kuwasimulia wale anaowapenda. Pindi atakapoota ndoto ambayo itamchukiza, basi hiyo inatoka kwa shetani. Hivyo hana budi kuomba ulinzi wa Mwenyezi Mungu dhidi ya ubaya wake na asimimulie yeyote. Kwa njia hiyo ndoto hiyo haitaweza kumdhuru.” (Bukhari, Tabir, 3,46; Muslim, Ruya, 3).

Pia imesimuliwa zaidi katika hadithi nyingine kama ifuatavyo:

“Pindi mtu atakapoota ndoto mbaya basi ateme mate upande wake kushoto mara tatu na kisha ajikinge kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya ubaya wa shetani mara tatu na abadilishe mlalo kutoka upande mmoja na kulalia mwingine.” (Muslim, Ruya, 5).

**2. Ndoto zinazosababishwa na mazingira yanayokuzunguka:** Hizi ni ndoto zinazohusiana na hisia na matukio ya mtu ya kila siku; kama vile kuota kuwa unakunywa maji mengi baada ya kula chakula chenye chumvi nyingi kabla ya kulala au kuota tatizo ambalo lilikuwa likikushughulisha mno ndani ya siku ile. Ndoto hizi hazina ufafanuzi. Hazina maana.

**3. Ndoto za kweli:** Ndoto hizi hukumbukwa vizuri kabisa. Hizi huwa ni ufunuo kutoka kwa Mola na huwa kama bishara njema au tahadhari. Malaika maalum hupokea taswira hizo kutoka kwenye ubao uliohifadhiwa (*lawh-i mahfuz*) na kuziingiza kwenye roho ya mtu wakati amelala kwa amri na ruhusa ya Mola.





Ndoto za kweli ni mwangaza utokao kwenye ubao uliohifadhiwa ambao unarusha mwanga kwenye mambo yajayo. Hatua za mwanzo za utume wa Mjumbe Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – zilibeba ndoto za kweli ambazo zilibakia kwa takriban miezi sita.

Mtume aliyebariwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Kadiri muda unavyosogea<sup>32</sup> ndoto za muumini hukaribia kuwa za uhakika zaidi (hutokea kama zilivyoonekana). Ndoto ya kweli anayoita muumini ni moja ya arobaini na sita ya utume...na ile itokayo kwa Mtume kamwe haiwi ya uongo.”<sup>33</sup>

“Ndoto zipo katika aina tatu: Aina ya kwanza ni ndoto za kweli, yani bishara njema. Aina ya pili ni hofu na huzuni inayosababishwa na shetani. Na aina ya tatu ni vitu vinavyotokana na mtu mwenyewe. Yeyote atakayeona kitu kibaya katika ndoto basi asiwahadithie wengine...hana budi kusi-mama upesi na kuswali.” (Bukhari, Tabir, 26; Muslim, Ruya, 6).

“Ndoto za kweli zaidi ni za wale wenye kusema ukweli zaidi.” (Muslim, Ruya, 6)

“Ndoto za kweli zaidi kuliko zote ni zile zinazootwa karibia na asubuhi.” (Tirmidhi, Ruya, 3/2274)

Ndoto za kweli zinahitaji kutafsiriwa na wajuzi; alama zake zinahitajika kutafsiriwa. Kutafsiri ndoto ni kama kipaji kutoka kwa Mungu. Kuna nyakati baada ya swala Mtume aliyebariwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akisikiliza na kutafsiri ndoto za baadhi ya maswahaba zake na kuwafahamisha mambo yajayo yaliyoashiriwa na ndoto zao.

Bila shaka kutafsiri ndoto ni sayansi maalum inayosimamia kwenye kanuni maalum. Wale wenye utambuzi wa sayansi hii wanaitwa *muabbir*, yani mfasiri. Vitabu vingi vimeandikwa kuhusiana na tafsiri za ndoto kwa

32. Kulingana na wanachuoni wa *hadith*, maneno ‘kadiri muda unavyosogea’ yanaweza kuashiria ikwinoksi au kufungwa kwa muda ama wakati kikikaribia kiamu au wakati wa alfajiri karibia na kuchomoza kwa jua.

33. Kuhusiana na suala kwamba ndoto za kweli ni moja ya arobaini na sita ya utume, inasemekana kwamba Mtume aliyebariwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliota ndoto za kweli wakati wa miezi sita ya miaka yake ishirini na tatu ya utume; na kipindi cha miezi sita ni rehema na amani ziwe juu yake na moja ya arobaini na sita ya miaka ishirini na tatu.



faida ya watu wote. Miongoni mwa vitabu maarufu ni kazi za Ibn Sirin na Muhyiddin Arabi - Mwenyezi Mungu azitakase siri zao. Vitabu vyao vimekuwa vikinukuliwa katika vitabu vingine vingi vinavyohusiana na kutafsiri ndoto mpaka leo hii. Vyovyote iwayo lakini kutafsiri ndoto kwa kuchukua taarifa kutoka kwenye kazi hizo ni njia nzuri sana; kwani ari ya kutafsiri ndoto inatokana na utambuzi wa kiroho (*kashf*). Hivyo mfasiri hana budi kuwa na amri ya kiroho. Kinyume na hivyo mtu ataweza kuingia kwenye hatari ya kutoa tafsiri za uongo kama alivyosema Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake:

“Ndoto huwa ya kweli kama ilivyosemwa na mfasiri wa mwanzo.” (ibn Majah, Tabir, 7). Hivyo hatutakiwi kuwasimulia ndoto zetu wale wasio na ujuzi. Na wajuzi katika sayansi hii wamesema kwamba ‘tafsiri ya kwanza ndio sahihi na hufutilia mbali tafsiri zijazo’.

Kulingana na kile kilichoelezewa ndani ya waraka wa *Mizanun-Nufus*,<sup>34</sup> sayansi ya kutafsiri ndoto imegawanyika katika sehemu mbili: ile ya dhahania (*anfusi*) na ile isiyo ya dhahania (*afaqi*). Mtu yeyote wa kawaida anaweza kuwa na uwezo wa *anfusi* katika kutafsiri ndoto; yani mtu yeyote anaweza kupata ujuzi huu kwa kukusanya tafsiri mbalimbali zilizoandaliwa hapo mwanzoni na wataalamu wa kiroho kutoka kwenye vitabu vyao au kwa kusikia kutoka kwao. Kwa njia hii ndoto nyingine zinazoendana na hizo huweza kutafsiriwa kwa msaada wa tafsiri zilizotangulia.

Kila kitu kinachoonekana ndani ya ndoto ni kama neno katika lugha. Kwa maneno mengine ni kwamba kila moja ni kama lugha inayohusiana na ndoto husika. Maana iliyohusishwa na lugha ya ndoto na kile kilichooonekana ndani yake inategemeana na uhusiano wa mbali. Tunaweza kusema kwamba uhusiano huu una msingi wake. Kwa mfano nyoka huchukuliwa kuashiria adui; na maana hii chanzo chake ni masimulizi ya Adam – amani iwe juu yake. Hivyo kila tabia anayoionyesha nyoka huchukuliwa kuashiria aina fulani ya uadui. Kwa mfano kama nyoka ataonekana kuwa amekufa au ametulia hii itatafsiriwa kama njia.

Kwa upande mwingine kuna mambo mengi ya kuzingatia katika kutafsiri ndoto; kama vile siku husika, usiku wake au majira ya mwaka ambayo ndani yake ndoto iliotwa. Kwa mfano wakati kudhihirika kwa



34. Ulioandikwa na Hafiz Hulusi Effendi, ambaye ni *mudarris* mkuu wa msikiti wa Bayezid, waraka huo ulitolewa mwaka 1305 (AH) ndani ya Istanbul.





ndoto iliyootwa wakati wa kipupwe kunachelewa lakini ndoto iliyootwa karibia na kupambazuka hujidhihirisha haraka sana. Lakini mara nyingi tafsiri kama hizo huwa na mapungufu kwa kuwa huwa hazizingatii mazingira tofauti tofauti ya muotaji.

Sayansi ya kutafsiri ndoto isiyo ya dhahania huwa haiendani na tabaka la wenye uwezo (*khawass*) na wakati wote inahitaji msaada wa utambuzi wa kiroho (*kashf*), kama ambavyo kutenganisha ndoto tukufu (*rahmani*) dhidi ya zile za kishetani (*shaytani*) kunavyohitaji msukumo wa kiroho. Kwa kuongezea ni kwamba, kwa kuwa wanadamu wanatofautiana wao kwa wao kitabia basi hata ndoto moja iliyootwa na watu wawili tofauti inaweza kubeba maana mbili tofauti. Ili kulitambua hili unahitaji amri ya kiroho.

Hili linatukumbusha namna siku moja watu wawili walivyomjia Ibn Sirin na kumwambia kuwa wote waliota kwamba wanatoa hotuba juu ya mimbar. Ibn Sirin alimwambia mmoja wao kwamba angelikuja kutekeleza ibada ya hijja na mwingine kwamba angelikuja kunyongwa. Baada ya muda mfupi tafsiri zote zikaja kuwa za kweli.

Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea:

“Siku moja niliota miezi mitatu ikidondokea chumba changu. Nikamsimulia ndoto hiyo baba yangu Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Alinyamaza kimya bila kunipa jibu. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipofariki na kuzikwa ndani ya chumba changu ndipo aliposema, hiyo ndiyo ile miezi mitatu uliyoita!” (Muwatta, Janaiz, 30).

Pindi *Muhajirun* walipowasili Madina wengi wao waliambiwa wawachague ndugu zao katika *Ansar*. Othman ibn Mazun – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliangukia kwenye familia ya Ummu’l-Ala al-Ansariyya – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Walimchukua mara moja na kuishi naye katika nyumba yao. Muda mfupi baadae alishikwa na maradhi. Familia ile ilisimamia matibabu yake lakini hayakusaidia kitu, kwani aliaga dunia baada ya muda mfupi. Baada ya hapo Ummu’l-Ala alimuona Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ndani ya ndoto akiwa na bomba lililokuwa likitiririsha maji. Upesi aliisimulia ndoto yake kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake, Mtume alisema:





“Hayo ni matendo yake ambayo yanatiririka kwa ajili yake.” (Bukhari, Tabir, 13, Janaiz, 3, Shahadat, 30, Manaqibu’l-Ansar, 46)

*Mwanamke mwingine alikuwa amekuja kwa Mtume – rehemana amani ziwe juu yake – ili amtafsirie ndoto yake aliyoota kwamba nguzo ya katikati ya nyumba yake ameanguka mbele yake. Mtume aliyebarikiwa – rehemana amani ziwe juu yake – alimuuliza ikiwa alikuwa ameolewa ama la, na kama alikuwa ameolewe basi mume wake alikuwa wapi. Yule mwanamke alimwambia kwamba mumewe alikuwa amesafiri lakini alikuwa bado hajarejea. Mtume aliyebarikiwa – rehemana amani ziwe juu yake – alimwambia kwamba mume wake angelirejea salama kabisa na wangelikuja kulifurahia sana jambo hilo. Ile ndoto ilikuja kujidhihirisha vile vile kama ilivyotafsiriwa.*

*Yule mwanamke aliota ndoto kama ile katika kipindi cha ukhalifa wa Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – wakati mume wake yuko safarini. Wakati huu alienda kwa khalifa ili atafsiriwe ndoto yake. Kama ilivyokuwa kwa Mtume aliyebarikiwa – rehemana amani ziwe juu yake – na Siddiq – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – naye alimuuliza yule mwanamke baadhi ya maswali. Kisha akamwambia kwamba mumewe alikuwa amekufa njiani.*

*Huku akiwa amechanganyikiwa yule mwanamke alisema, “Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana amani ziwe juu yake – aliitafsiri ndoto hiyo hiyo kwamba mume wangu angelirudi salama!”*

*“Kweli”, alimjibu. “Huo ni ufunuo alikuwa amepewa na huu ndio niliopewa mimi.” Muda si mrefu habari za kifo cha mumewe zilifika Madina.*

Hivyo kuzitafsiri ndoto kwa usahihi ni jambo gumu mno na kuna wakati haliwezekani bila ya kuwa na amri ya kiroho, kwani ulimwengu wa ndoto unadhahirisha vitu ambavyo viko nje ya upeo wa mwanadamu, vitu vyenye kustaajabisha na visivyoingia akilini.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ametufahamisha ndani ya Qur’an namna alivyomjaalia Yusuf – amani iwe juu yake – kipaji juu ya sayansi hii.<sup>35</sup> Pindi Yusuf – amani iwe juu yake – alipokuwa gerezeni alisikiliza ndoto za aliyekuwa mwoka mikate na msambazaji wa vinywaji katika kasri. Yule





mwoka mikate alimsimulia kwamba aliota akiwa amebeba sinia la mikate na kuona kundi la ndege limetua juu yake na kuanza kula ile mikate yote. Yusuf – amani iwe juu yake – alimtaarifu kwamba angelikuja kunyongwa na kundi la ndege lingekuja kudonoa juu ya kichwa chake. Kwa upande mwingine yule msambazaji wa vinywaji alimwamba Yusuf – amani iwe juu yake – kwamba aliota akimhudumia mfalme kama msambazaji wa vinywaji kama hapo kabla, ndoto Mtume alimtafsiria kuwa ilikuwa inaashiria ‘kurejea kwake ndani ya kasri na kuwa msambazaji wa vinywaji.’ Funuo hizi zilikuja kudhihirika muda si mrefu kama zilivyotafsiriwa.

Kama tulivyoona kwenye maneno yaliyotangulia, sayansi ya kutafsiri ndoto imeegemea hasa kwenye utambuzi wa kiroho (*kashf*). Kwa sababu hii mfasiri wa ndoto hana budi kuwa na daraja la kiroho. Ilisemekana kwamba Celeleddin Okten ambaye alikuwa na hazina kubwa ya elimu katika miaka aliyokuwa Istanbul katika Shule ya elimu ya juu ya Imam Hatip Lise alikuwa akionyesha ujuzi mkubwa katika kutafsiri ndoto. Alikuwa akisema kwamba ndoto zingeliweza kutafsiriwa na watu waliokuwa na nyoyo safi na kwamba usahihi wa tafsiri ulitegemea uchamungu wa mfasiri.

Wakati wa ujana wake Celeleddin Okten - Mwenyezi Mungu amrehemu – alikuwa akifundisha masomo ya dini katika shule za elimu ya juu; huku akiishi maisha ya kitakatifu kwa moyo safi. Ndipo kwa miaka ile akawa maarufu kwa kutafsiri ndoto kwa usahihi. Pindi alipokuwa akimaliza kutoa baadhi ya mifano ya uzoefu wake katika kutafsiri ndoto alikuwa akiongeza:

“Ndipo ukafika wakati ambao mapazia yakashushwa...kwani masomo ya dini yaliondolewa na serikali na mimi nikateuliwa kuwa mwalimu wa falsafa. Na pindi nilipoanza kuogelea ndani ya bahari pana ya falsafa chemchem zote za moyo wangu zilikauka.”

Ndoto nyingine ya kweli inayofahamika kwa watu wengi ni hii ifuatayo:

*Siku moja Imam Busiri ambaye ni mshairi maarufu wa Qasidah-i Burda alipokuwa njiani kuelekea nyumbani kwake alikutana na mzee mmoja aliyekuwa amejaaliwa imani ya hali ya juu.*

“Busiri!” yule mzee aliniita. “Je ulimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ndotoni usiku wa kuamkia leo?”





*“Hapana, sikumuona”, Busiri alijibu. Yule mzee aliondoka bila ya kusema chochote. Lakini swali hili liliwasha moto wa mapenzi aliyokuwa nayo moyoni mwake juu ya Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake.*

*Usiku wake Imam alimuona ndotoni Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake. Pindi alipoamka alihisi moyo wake ukiwa na furaha na amani isiyoelezeka. Baada ya pale aliandika mashairi mengi yaliyokuwa yanaelezea utukufu wa Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – ili watu watakaoyasoma waweze kuzama kwenye bahari ya mapenzi juu ya Mtume.*

*Lakini muda mfupi baadae alipooza upande mmoja wa mwili wake. Alishindwa kutembea, na alipata ugumu katika kusogeza hata kidole chake. Baada ya pale ndipo alipoandika Qasidah-i Burda ambayo ndani yake alitafuta ponyo kutoka kwa Mola. Usiku wa ile siku aliyomaliza kuandika qasidah aliota ndoto ambayo ndani yake alikuwa akimsomea Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – kile alichokiandika; na kutokana na furaha aliyokuwa nayo Mtume baada ya kusikia mashairi yale aligonga ule upande wa mwili uliokuwa umepooza. Itakuwa ni kutokana na mapenzi ndio maana alipoamka alijiona amepona kabisa, baada ya hapo alimshukuru sana Mwenyezi Mungu Mtukufu.*

*Wakati alipokuwa njiani kuelekea msikitini kwa ajili ya swala ya alfajiri asubuhi yake alikutana na Sheikh Abu’r-Raja - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - ambaye alimuomba amsomee qasidah ambayo ndani yake anam-sifu Mbora wa viumbe – rehema na amani ziwe juu yake.*

*“Nina mashairi mengi ya namna hiyo. Ni lipi unalolitaka?” Imam Busiri alimuuliza.*

*“Lile ulilolisoma mbele ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu”, Sheikh Abu’r-Raja alisema. “Nimegundua kuwa alifurahi sana baada ya kulisikia.”*

*Imam Busiri alistaajabishwa na maneno yale kwani alikuwa akifahamu kuwa hakuna yeyote aliyekuwa ameisikia qasidah ile.”<sup>36</sup>*

*Kuna matukio mengi ndani ya ulimwengu wa kiislamu ambayo ndani yake siri nyingi zinazohusu mambo yasiyoonekana (ghayb) zinawekwa*





wazi kwa watu wema kwa kupitia utambuzi wa kiroho, kuona mbali, ufunuo au ndoto za kweli. Lakini tamko lifuatalo linabakia kutawala:

“Sema: Hapana katika mbingu na ardhi ajuaye ya ghaibu isipo kuwa Mwenyezi Mungu” (an-Naml, 65). Hivyo aya hii inahitaji maneno zaidi ya ufafanuzi.

Ukweli ni kwamba kiini cha ufafanuzi huu kiko ndani ya *hadith al-qudsi*, “...na pindi ninapompenda ninakuwa kama ulimi wake anaongelea, moyo wake anaotambulia mambo, masikio yake anayosikilizia, macho yake anayotazamia, mikono yenye kushikia na miguu yenye kutembelea...” (Bukhari, Riqaq, 38). Kitovu cha utambuzi wa kiroho na ufunuo ni roho ambayo Mola amempulizia mwanadamu. Macho yaliyowekwa kwenye kichwa yanaweza kuonekana na njia ya kuonea mambo ya nje peke yake; lakini ukiingalia ‘nuru takatifu’ iliyowekwa kwenye macho hayo inaweza kuwezesha kuona yale yaliyo nyuma ya pazia kwa kadiri atakavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kwa namna hiyo tunaweza kuona kwamba Mwenyezi Mungu ndiye anayeweka wazi mambo yasiyoonekana; kinyume chake ni kwamba mwanadamu hana uwezo wa kuona, kusikia wala kuyafahamu yale yaliyobakia nyuma ya pazia. Ni kwa kupitia rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu ndipo mwanadamu anapokuja kuyafahamu yale yaliyokuwa yamefichwa.

Kwa hakika Mwenyezi Mungu ametufahamisha ndani ya Qur’an kwamba Yeye hutufunulia baadhi ya taarifa juu ya vile visivyoonekana: “Hizi ni khabari za ghaibu tunazo kufunulia...” (Al-i Imran, 44)

Baada ya kuyasema hayo ni kwamba mambo yasiyoonekana yapo katika namna mbili; yale yasiyoonekana kabisa na yale yasiyoonekana kwa kiwango fulani.

Yale mambo yasiyoonekana isipokuwa kwa Mola peke yake yanaitwa mambo yasiyoonekana kabisa. Haya yanahusiana na kuona kitu ambacho hakiko ndani ya uwezo wa kibinadamu. Kinachoweza kuonekana ndani yake ni kile kilichowekwa wazi na Mola. Hivyo kuweza kuona kitu ambacho hakionekani kabisa ni kulingana na vile Mola alivyoridhia.

Kwa upande mwingine vile vitu ambavyo vinaonekana kwa kiwango fulani pekee ni vitu ambavyo baadhi ya watu wanavifahamu na wengine hawavifahamu. Kwa mfano mtu mwenyewe ndiyo mwenye kuweza kufa-





hamu fika kwamba ni kiasi gani cha fedha anacho mfukoni mwake na si mtu mwingine. Baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakawa hayaonekani na hivyo kutofahamika kwa baadhi ya watu yanaweza kuwa ni jambo rahisi kwa wengine.

Kwa upande wa waja watakatifu wa Mola yale yasiyoonekana kabisa yapo upande wa yale yanayofahamika kwa Mola pekee. Na katika hayo Mola humruhusu mja kuyafahamu kwa kadiri atakavyo.

Hata kama watakatifu watakuwa na uhakika kiasi juu ya mambo waliyoyaona au waliyotabiri kuwa yatatokea lakini kamwe hawajitangazii kwa watu kwamba wao wana amri juu ya utambuzi wa kiroho na uoni wa mbele. Kuna wale watu ambao ukiwaangalia usoni upesi mno utamkumbuka Mola. Ndimi zao hutoa lulu za hekima. Huwa hawaongei wao wenyewe bali hufanywa waongee. Lakini bado huwa wanyenyekevu mbele ya baraka za Mola na hutambua fika kwamba mwanadamu ni dhaifu na anaweza kudondokea kwenye kujiona na kuvuka mipaka kwa urahisi. Bila shaka hisia za kujiona peke yake hatari mno. Pindi hatari hii inapokuja kuwa tishio Mwenyezi Mungu huweza kumuacha mtu bila ya msaada wowote ili kumuonya.

Utambuzi wa kiroho, kuona mbele na ndoto za kweli si chochote bali ni rehema za Mola alizowajaalia waja wake wema kwa kuwafunulia yale mambo yasiyoonekana.





---

# SURA YA NNE

---

## Baadhi ya Maswali Kuhusiana na Usufi

- A- KUOMBEA (TAWASSUL)
- B- KUTAFUTA BARAKA (TABARRUK)
- C- KUTEMBELEA MAKABURI





“...Hakika kwa kumkumbuka Mwenyezi Mungu ndio nyoyo hutua.” (ar-Rad, 28)





## Baadhi ya maswali kuhusiana na usufi

**E**nyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia! (*al-Maidah*, 35)



### A. KUOMBEA (TAWASSUL)

Kila njia na chombo ambacho kinampeleka mja kwenye lengo lake la kuumbwa kinachukuliwa kuwa ni sababu (*wasilah*). Kuomba au kutafuta *tawassul* ni kitendo cha kutumia sababu hizi ili kupata ukaribu wa Mola. Kwa ufasaha zaidi, hii inahusiana na kuomba kitu kwa Mola kwa kupitia Majina yake mazuri, Qur'an, matendo mema, Mitume na watakatifu, kwa matumaini ya kuongeza uwezekano wa kukubaliwa kile kilichoombwa, kujikinga kwake na kutafuta msaada wa kupata kitu unachokitaka au kuki-fukuza kitu ambacho hukitaki.

Aya ya 35 ya surat al-maidah inasema :

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَابْتَغُوا إِلَيْهِ الْوَسِيلَةَ

“Enyi mlio amini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na tafuteni njia ya kumfikilia!”

Neno *wasilah* limetajwa kama lilivyo; inamaanisha bila mipaka yoyote. Hivyo njia ambazo mtu anatakiwa kuzitumia ili kupata ukaribu na Mola ni matendo mema kama vile swala, swaumu na kupambana katika njia yake (*jihad*). Baadhi ya wajuzi wameongezea kwamba kuwa chini ya mafunzo ya *murshid* kwa lengo la kujipamba na mwenendo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ni moja wapo ya sababu.

Namna ambayo watakatifu na wanachuoni wanaitumia kuwaelekeza watu katika njia ya Mola si ya kichungaji. Njia inayotumika ni ile ya kufahamisha na kutadharisha. Wao ni kama viongozi wenye kuwaongoza wasafiri katika njia iliyoharibika. Kinyume chake ni kwamba ukatoliki una





achungaji ambao ndani yake mchungaji anakuwa ni njia ya lazima kati ya mwanadamu na Mungu. Uislamu unalikata hili; yani kati ya mola na mwanadamu hatakiwi wa watatu. Mtu anaweza kumgeukia mola wake yeye mwenyewe wakati wowote ule na kumuabudu haraka iwezekavyo.

Vyovyote iwavyo lakini kuna maneno tofauti yaliyosikika kuhusiana na jukumu la *murshid*, amechukuliwa kama mchungaji kwamba yupo kati ya Mola na mwanafunzi aliye katika njia ya kiroho. Lakini hatuna budi kukumbuka kwamba katika uchungaji mtu hawezi kutekeleza majukumu yake ya utumishi bila ya kuingiliwa na mchungaji. Huu ni mkanganyiko uliotokana na uharibifu wa ukiristo. Hivyo kamwe majukumu ya wanachuoni na watakatifu hayawezi kulinganishwa na yale ya wachungaji.

Kwa hiyo upingaji unaoendana na jambo hilo si sahihi na hauna mashiko, na unatokana na kuileta mbele maana halisi ya neno *tawassul*. Hili linavuka hali halisi ya kuombea. Kwa namna yoyote ile upingaji wa namna hiyo unaletwa na wale walio nje ya mwenendo wa kisufi, watu wasioweza kuelewa msimamo wa *murshid-i kamil* wa kweli. Mara nyingine kuhukumu huku kunasababishwa na tabia mbaya ya baadhi ya wafuasi wa matawi ya kisufi ambao wanashindwa kuziingiza nyoyoni mwao kanuni za kisufi. Lakini bado hii haiwezi kuwa dharura. Kama ambavyo haingii akilini kuzipinga harakati zote kutokana na makosa na wakati mwingine nia mbaya za baadhi ya wafuasi wake, ndivyo ilivyo makosa kuingiza makosa binafsi kwenye harakati nzima. Hivyo ni jambo lisiloingia akilini kuyazingatia makosa ya wachache juu ya jambo tukufu wanalodai kuwakilisha. Kwa mfano hakuna mtu mwenye utambuzi mzuri ambaye ataweza kuuona uislamu unawajibika kwa makosa ya waislamu.

Kama ilivyoashiriwa hapo kabla, *murshid* wa kweli huwangoza watu katika njia ya kiroho sawa na jukumu linalotekelezwa na wanachuoni katika sayansi za mambo ya dhahiri. Hii haimaanishi yeye kuwa kati ya Mola na mja wake. Bali inahusiana na *Murshid* kutumia uzoefu na utaalamu wake katika kumtahadharisha mfuasi wake kuhusiana na njia ya kuelekea kwa Mola wake na kuimulika njia ili kuhakikisha anavipita vikwazo kwa usalama bila ya kupatwa na hatari yoyote. Kama ambavyo chombo tunachokichukua kwa ajili ya safari haiwi ndio tumemaliza bali ni sababu tu, na kiongozi wa kiroho ni mwalimu ambaye anaufunza moyo wa mwanafunzi wake na kuupamba kwa maadili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mjumbe





wake. Inaweza ikafikia wakati mwanafunzi akawa na maendeleo makubwa kiroho hata akafikia kumpita mwalimu wake ambaye ndiye aliyemfungulia upeo mpya hapo mwanzoni; hili ni sawa na lile lililotokea kati ya Shams Tabrizi na Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – pindi ukilinganisha kwa nje.<sup>1</sup>

Hivyo licha ya umuhimu na thamani yake lakini *murshid* kamwe si mwisho ya safari, bali ni njia tu.

Kwa msingi huo kutafuta uongofu ni kushikamana vilivyo na *murshid-i kamil*, ambaye si mwingine bali muumini aliyekomaa na mwenye uzoefu mkubwa na kumfanya kuwa kiongozi na hivyo kutafuta msaada wake kati-ka kupita kwenye njia nyembamba ambayo kinyume chake mtu anaweza kuharibikiwa na hivyo kupotea kabisa. Kwa maana nyingine, kutafuta usaidizi ni kuweka wazi mapenzi yako kwa Mola na kuomba kukubaliwa naye kwa kupitia wale ambao Mola anawapenda; hivyo yote hii ni jitihada ya kuhakikisha maombi yanakubaliwa. Kinyume chake si kuunasibisha utukufu kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

“Mshirikisheni Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake - katika dua zenu”, Imam Malik – rehema za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – amesema.

Vivyo hivyo ndivyo yasemavyo maneno ya Imam Jazari - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake: “Washirikisheni Mitume na watu wema kama njia ya kufanya dua zenu zijibiwe.”

Imam Subki ameandika yafuatayo katika *Shifau’s-Saqam* yake:

“Kuomba kwa kupitia kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kumeruhusiwa katika hali zote. Kumtumia Mtume kama njia ya kupitishia maombi kuliwezekana hata kabla ya kuumbwa kwake na baada ya kuumbwa kwake. Vivyo hivyo inawezekana baada ya kufariki kwake na kuelekea kwenye *Barzakh*, kama itakavyokuwa pindi atakavyofufuliwa kwenye uwanja wa hesabu na peponi.”

1. Shams Tabrizi ambaye alivumbua bahari ya kiroho iliyokuwa imejificha kwa Rumi, alikuwa kama muale wa moto unaosubiri kuwasha bahari ya petrol. Hilo ndilo lililokuwa jukumu na mamlaka yake. Pindi alipowasha hiyo bahari alikutana na mlipuko mkubwa wa kiroho kiasi kwamba yeye mwenyewe akajikuta yupo katikati ya moto wenye kunguruma.





Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

“Kulikuwa na vita kati ya wayahudi wa Khaybar ba kabila la Ghatafan, ndani ya vita hivyo wakati wote wayahudi walikuwa wakishindwa. Mwishoni waliomba, ‘Ewe Mola...tunakuomba ushindi kwa jina la Mtume uliyehidi atakuja karibu na saa za mwisho’. Baada ya dua hiyo wakawashinda Ghatafan vibaya sana. Lakini pindi Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomleta Mjumbe wake – rehema na amani ziwe juu yake - ambaye walimtumia kama njia ya maombi yao wayahudi hao walikataa utume wake na kitabu alichokuwa amefunuliwa. Baada ya hapo Mwenyezi Mungu mtukufu akasema:

وَكَاثُوا مِنْ قَبْلِ يَسْتَفْتِحُونَ عَلَى الَّذِينَ كَفَرُوا  
فَلَمَّا جَاءَهُمْ مَا عَرَفُوا كَفَرُوا بِهِ فَلَعْنَةُ اللَّهِ عَلَى الْكَافِرِينَ

‘Na kilipo wajia Kitabu kitokacho kwa Mwenyezi Mungu kinacho thibitisha waliyo nayo - na wao walikuwa wakitafutia ushindi kuwashinda makafiri - yalipo wajia yale waliyo kuwa wakiyajua waliyakanusha. Basi laana ya Mwenyezi Mungu juu ya wakanushao!’” (al-Baqara, 89) (Qurtubi, II, 27; Wahidi, Asbabu'n-Nuzul, uk. 31).

Baada ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kuiaga dunia Madina ilikubwa na njaa kali. Wakazi wa pale waliufikiria ushauri wa Aisha – rehema na amani ziwe juu yake – kwamba watoboe tundu kwenye dari lililopo juu ya kaburi la Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ili kusiwe na kizuizi kati yake na anga.

Waliamua kufanya kama walivyokuwa wameshauriwa. Muda si mrefu wapakata mvua kubwa. Madina ikawa imejawa na majani yenye kijani kibichi na ngamia wakawa na nyama nzuri kabla ya hapo mwanzo. Mwaka ule ulijulikana kama *Amul-Fatk*, yani mwaka wa wingi. (Danmi, Muqaddimah, 15).

*Kulikuwa na mtu ambaye alikuwa akienda kwa Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kwa ajili ya kumuomba amkidhie haja zake; lakini Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa akimpuuzia. Baadae yule mtu akakutana na Ibn Hunayf – radhi za Mwe-*





nyezi Mungu ziwe juu yake – na kumlalamikia juu ya hali ile, lakini aliambiwa:

“Chukua udhu na uswali raka mbili ndani ya msikiti na kisha usome dua ifuatayo:

‘Ewe Mwenyezi Mungu...Ninakuomba na kukugeukia Wewe kwa jina la Mtume Muhammad – rehemana na amani ziwe juu yake, Mtume wa rehemana. Ewe Muhammad! Ninamgeukia Mola wako kwa kupitia jina lako...yashughulikie mahitaji yangu!’ na kisha taja lile unalolihitaji.”

Yule mtu akafanya kama alivyoelekezwa na kisha akaenda kwenye mlango wa Othman ibn Affan – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Mlinzi wake akamshika mkono na kumpeleka kwa Othman, Othman akamkaribisha akae kwenye kochi karibu yake.

“Unahitaji nini?” kisha alimuuliza. Yule mtu akamwambia alichokuwa akihitaji. Shida yake ikatatuliwa mara moja. Alipokuwa anaondoka Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisema:

“Kwa nini hukutuambia muda wote huo kama ulikuwa unahitaji kitu? Rudi kwetu kama utahitaji chochote hapo baadae!”

Yule mtu akaamua kwenda kwa Ibn Hunayf kwa ajili ya kumshukuru. Pindi nilipomuona alisema, “Mwenyezi Mungu akupe kila lililo la kheri! Alilitambua nililoliendea kabla ya kuongea naye!”

“Ninakuhakikishia kwamba nilichokushauri hakikutokana na mawazo yangu binafsi. Kimetokana na kile nilichokishuhudia hapo kabla. Siku moja kipofu mmoja alimuendea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana na amani ziwe juu yake – na kumuomba, ‘Muombe Mwenyezi Mungu aniondoshee huu upofu katika macho yangu. Kwani maisha ni magumu kwa kipofu!’

‘Kuwa na subira kama unataka...hiyo itakuwa bora kwako’, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana na amani ziwe juu yake – alimshauri.

‘Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, sina mtu wa kunishika mkono na kunipeleka ninapotaka kwenda’, alijibu. ‘Jambo hili linaniweka kwenye shida kubwa. Tafadhali...Niombe niponywe!’ Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemana na amani ziwe juu yake – akamwambia:





*'Nenda na uchukue udhu na kuswali raka mbili. Kisha uombe: Ewe Mwenyezi Mungu...Ninakuomba na kukugeukia Wewe kwa jina la Mtume Muhammad – rehema na amani ziwe juu yake, Mtume wa rehema. Ewe Muhammad! Ninamgeukia Mola wako kwa kupitia jina lako...Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie aniombee!'* (Tirmidhi, Daawat, 118; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, IV, 138).

*Kulingana na mapokezi ya Hakim, pindi yule mtu alipomaliza maombi yake akawa si kipofu tena.*(Hakim, Mustadrak, 1707-708)

Utbah ibn Ghazwan – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - anasimulia maneno yafuatayo kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake:

“Pindi mmoja wenu atakapopoteza kitu katika sehemu ambayo hakuna mtu au akawa hana jingine la kufanya zaidi ya kuomba msaada basi na aite ‘Waja wa Mwenyezi Mungu...nisaidieni!’, kwani Mwenyezi Mungu ana waja ambao hamuwezi kuwaona”. (Haythami, Majmau’z-Zawaid, X, 132; Imam Nawawi, al-Adhkar, 201)

Imam Nawawi ambaye ndiye aliyesimulia maneno hayo ameongezea uzoefu wake binafsi kama ifuatavyo:

“Mtu ambaye nilipokea hii *hadith* kutoka kwake aliniambia kwamba na yeye aliwahi kupatwa na shida kama ile na akathibitisha kwamba kutokana na kufanya kama alivyoshauri Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alifanikiwa katika jambo lake. Nilistaajabu kwa kiasi fulani. Baadae ngamia aliyekuwa akimilikiwa na huyu mtu aliye karibu yangu alikimbia. Ingawa alikuwa anaweza kupatikana lakini kila alipokuwa anasogelewa alikuwa akikimbia. Hivyo nikamsimulia hii *hadith*. Na baada ya kuifanyia kazi yule ngamia alirejea na kusimama kwa utulivu na kumwezesha mmiliki wake kushika kamba zake bila ya shida yoyote”

Katika mapokezi ya Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, Mjumbe Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

“Zaidi ya malaika walinzi, Mwenyezi Mungu Mtukufu ana malaika kadhaa hapaa ardhini ambao wanaandika kila kitu kwa kiasi cha kudondoka kwa kila jani. +





basi na aite ( عِبَادِ اللَّهِ ) ‘Waja wa Mwenyezi Mungu...nisaidieni!’” (Haythami, Majmau’z-Zawaid, X, 132)

Pia imepokewa kwamba Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – mwenyewe katika dua zake alikuwa akisema: “Kwa fadhila za Mtume wako na mitume waliotangulia...” (Haythami, Majmau’z-Zawaid, X, 132)

Katika *hadith* nyingine Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – anaelezea yafuatayo:

“Ewe Mola...Ninaomba msamaha wako kwa kupitia kwa Muhammad! Aliomba Adam – amani iwe juu yake – baada ya kutambua kosa lake lililompelekea kufukuzwa peponi.

Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akamuuliza:

‘Umefahamu vipi Muhammad wakati bado sijamuumba?’<sup>2</sup>

Adam – amani iwe juu yake – akasema, ‘Pindi uliponiumba na kunipulizia roho itokanayo na Wewe nilitazama juu na kuona maneno La ilaha ill’Mwenyezi Mungu Muhammadun Rasulullah yameandikwa kwenye nguzo za kiti cha enzi. Kuanzia pale nikatambua kwamba usingelitaja jina lile baada ya jina lako kama asingelikuwa kipenzi chako kikubwa ukilinganisha na viumbe vyako vyote.’ Baada ya hapo Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema:

‘Umesema kweli Adam! Kwa hakika yeye ndiye kipenzi changu kikubwa kati ya viumbe vyote! Hivyo niombe kwa kupitia yeye; na kwa kuwa ume-fanya hivyo ninakusamehe. Kama si Muhammad wewe usingeliumbwa!’ (Hakim, Mustadrak, II, 672).

2. Kutokana na kuwa peke yake Mola aliumba masiwa; yani kitu chochote tofauti na Yeye, kwani alitaka kufahamika na watu na majini kwa kadiri ya uwezo wao. Cha kwanza kuumbwa kilikuwa ni nuru ya Muhammad. Ndio maana Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema, “Nilikuwa Mtume hata wakati Adam yupo kati ya roho na mwili.” (Tirmidhi, Manaqib, 1). Ukiachana na suala kwamba nuru ya Muhammad, yani dhati ya Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake, ilikuwa ndiyo ya kwanza kuumbwa, lakini kujitokeza kwake hapa duniani ilikuwa ishara ya mwisho wa mnyororo wa utume. ‘Muhammad ambaye alikuwa bado hajaumbwa’ kama ilivyo hapo juu ni ‘nafsi’ ya Mtume na siyo dhati yake, yani nuru ya Muhammad.





Katika maneno mengine kulingana na taratibu za dua zilizoshauriwa katika uislamu, dua zote hazina budi kuanza na kuishia na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na kisha kumswalia Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kumswalia (*salawat*) Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – ni kumuomba kwa Mwenyezi Mungu badala yake. Kuna msingi kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu kamwe hakatai *salawat'us-sharifah* ambaye kimsingi ni dua mbele ya Mwenyezi Mungu; ndio maana tunazipamba dua zetu kwayo, mwanzoni na mwishoni. Tunaweza kusema kwamba kuziminya dua zetu katikati ya salamu hizo mbili ambazo matarajio ya kukubalika kwake ni makubwa mno, ni kuhakikisha kuwa dua hizo nazo zinajibiwa.

Kwa hakika siku moja Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alimuona mtu mmoja ambaye baada ya swala ya faradhi alikuwa anaomba dua bila kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na kumswalia Mjumbe wake.

“Mtu yule amefanya haraka”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - alisema kabla ya kumuita na kumpa ushauri:

“Pindi mtu anapotaka kuomba dua, kwanza amshukuru na kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumswalia Mtume wake...na kisha baada ya hapo aombe anachokitaka.” (Tirmidhi, Da'awat, 64/3477).

Kuomba dua ikubaliwe kwa kupitia utukufu wa Mitume, watakatifu na waja wema wa Mwenyezi Mungu ni jambo jema mbele ya Mwenyezi Mungu, na ni moja ya njia bora katika kuvuta rehema za Mwenyezi Mungu na kuhakikisha dua inajibiwa. Lakini dua inaelekezwa kwa Mwenyezi Mungu peke yake. Kuwataja waja vipenzi kwa Mola katika dua ni njia tu ya kufanya dua hiyo ijibiwe.

Hivyo kuomba kwa kupitia watu wema si chochote kingine isipokuwa ni kuyafanya matendo yao na tabia zao njema ziwe sababu ya kujibiwa dua zako. Hata hivyo matendo hayo ndiyo yaliyowafanya wawe wema mbele ya Mola.

Hivyo hata Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - mwenyewe alikuwa akiomba msaada au ushindi<sup>3</sup> kwa kupitia masikini







miongoni mwa *Muhajirun*, na alikuwa akisema, “Waleteni wadhaifu wenu kwangu; kwani kwa sababu ya wadhaifu wenu ndio maana mnakuzwa na kusaidiwa.” (Abu Dawud, Jihad, 70; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, V, 198).

Ni hakika kwamba kuwafanya kama njia watu hawa waliovunjika nyoyo lakini wema, ambao wanaridhika na utajiri wa nyoyo zao licha ya kutokuwa na nguvu ya kifedha ambayo ingeliwafanya wame na nafasi kati-ka jamii, ni jambo ambalo lingelipelekea maombi kukubaliwa kwa haraka.

Kuhusiana na kuwatafuta watu waliovunjika nyoyo na walio na huzuni kama njia ya kukuwezesha kupata radhi za Mola hatuna budi kuzingatia kifuatacho cha Malik Ibn Dinar:

*“Pindi Musa – amani iwe juu yake – alipokuwa anamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliuliza, ‘Nikutafute wapi ewe Mola?’*

*‘Nitafute karibu na watu waliovunjia nyoyo’ Alijibu. (Abu Nuaym, Hilyah, II, 364).*

Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - anasimulia kwamba wakati wa ukame mkali uliotokea katika kipindi cha ukhalifa wa Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, yeye Omar alimchukua mjomba wa Mtume Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – na kumuweka pembeni yake na kumfanya kuwa njia pindi alipokuwa anamuomba Mola kwa ajili ya mvua, aliomba:

“Mola wangu...Tulikuwa tukimtumia Mtume wetu kama njia na Wewe ulikuwa ukitupa mvua! Sasa hivi tumemfanya mjomba wa Mtume wetu kuwa njia. Tunaomba utushushie mvua!” Muda si mrefu mvua ikanyesha na wakazi wakapata maji ya kutosha. (Bukhari, Istisqa, 3).

Masimulizi mengine yanamuonyesha Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akilia huku akiomba kwa unyenyekevu na kwa hisia kama ifuatavyo:

“Mola wangu...Vyote mawingu na maji viko upande wako. Yatume mawingu na utushushie mvua!” Muda mfupi baada ya dua mawingu mazito yenye rehema yalijikusanya juu na kushusha mvua kubwa. Kuto- kana na baraka hii tukufu Omar- radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliwakusanya watu na kuwaambia maneno yafuatayo:

“Enyi watu! Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe





juu yake – alikuwa akimheshimu na kumpenda mjomba wake Abbas kama baba na alikuwa akikichukulia kiapo kilichotolewa na mjomba wake kama kiapo alichokitoa yeye mwenyewe. Hivyo watu! Shikamaneni na heshima ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa nayo juu ya mjomba wake...Mtumieni kama njia katika kumuomba Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kuondoa matatizo mbalimbali yatakayokusibuni.” (Hakim, Mustadrak, III, 377).

Kuna masimulizi zaidi kutoka kwa Ibn Abdilbarr ambayo yanamulika zaidi katika suala hili:

*“Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alitoka nje huku Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akiwa pembeni yake na kuomba, ‘Ewe Mwenyezi Mungu...Tunatafuta ukaribu na Wewe (taqarrub) kwa kupitia mjomba wa Mtume wetu na tunahitaji atuombe (istishfa). Muangalia yeye kwa ajili ya Mjumbe wako kama ulivyowaangalia mayatima wawili kwa ajili ya wema wa wazazi wao.’<sup>4</sup> Tumekuja kwako kwa ajili ya kutubia na kuomba uombezi!’ kisha huku akiwa amewageukia watu waliokuwepo pale alisoma yafuatayo kutoka kwenye Qur’an:*

*“Nikasema: Ombeni msamaha kwa Mola wenu Mlezi; hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe. Atakuleteeni mvua inyeshe mfululizo. Na atakupeni mali na wana, na atakupeni mabustani na atakufanyieni mito” (Nuh, 10-12).*

*Kisha na Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – naye akasimama na kuomba. Machozi yalikuwa yakitiririka mfulululizo kutoka kwenye macho yake kama chemchem yenye kutiririsha maji yake. Mara mvua iliyokuwa ikisubiriwa kwa muda mrefu ikanyesha, watu wakaanza kumpongeza kwa kumwambia, ‘Hongera mbeba birika (saqi) wa Nyumba tukufu!’ (ibn Abdilbarr, Istiab, II, 814-815).*

Kisa kilichotangulia ni ushahidi tosha wa swahaba kuomba kwa

4. Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaitaja aya ya Qur’an ambayo khidhir anamuelezea Musa – amani iwe juu yake – sababu iliyompelekea kukarabati ukuta uliokuwa unakaribia kuanguka: “Na ama ukuta, huo ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini. Na chini yake ilikuwako khazina yao; na baba yao alikuwa ni mtu mwema. Basi Mola wako Mlezi alitaka wafikie utu uzima na wajitolee khazina yao wenyewe, kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Wala mimi sikutenda hayo kwa amri yangu. Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria” (al-Kahf, 82).





kupitia swahaba mwingine. Lakini hili limepelekea baadhi ya watu kudai kwamba kuomba kwa kupitia mtu mwema kunawezekana endapo mtu huyo bado yupo hai lakini kuomba kwa kupitia yeye pindi anapokuwa amefariki ni jambo lisiloruhusiwa. Lakini kufanya maombezi hayo yawe ni kwa kipindi ambacho Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa hai pekee ni wazo lisiloelezea ukweli wa mambo. Maneno ya Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambayo yanaelezea namna walivyokuwa wakiomba kwa kupitia Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – yanahusisha kipindi alichokuwa hai na baada ya kufa kwake. Vyovyote iwavyo lakini sababu pekee iliyowafanya wamchague Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kuwa njia ya kupitishia maombi yao si nyingine bali kwa kuwa yeye alikuwa ni mjomba wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Kwa kuwa Abbas alikuwa na udugu na Mtume ndio maana walimchagua, kwa hiyo njia ya waliyoita-futa ni ile ile ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – mwenyewe. *Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa baadhi ya watakatifu wakubwa; kuwatumia kama njia* hata baada ya kufa kwao ni jambo linalowezekana na wakati mwingine linapendekezwa zaidi.<sup>5</sup>

Moja ya mifano mizuri juu ya hili ni huu ufuatao:

Ilikuwa ni kawaida kwa wanachuoni na watu wengine kutembelea kaburi la Imam mkubwa Abu Hanifah na kumtumia kama njia ya kupitishia maombi yao, suala lililoonekana ni lenye manufaa. Mmoja wao ni Imam Shafii ambaye baadae alisema:

“Pindi nilipohisi kuhitaji kitu nilikuwa nikiswali raka mbili. Kisha nilikuwa nikilitembelea kaburi la Abu Hanifah mahala ambapo nilikuwa nikiomba kwa Mwenyezi Mungu. Na kutokana na utukufu wake shida yangu ilikuwa ikishughulikiwa.”<sup>6</sup>

Pia kwa upande mwingine matendo mema yanaweza kuwa njia ya kupitishia maombi. Katika *hadith* Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - anasimulia kisa cha wasafiri watatu:

*“Marafiki watatu ambao walifikwa na mvua wakati wakiwa safarini*

5. Kwa maelezo zaidi juu ya mada hii rejea Zekeriya Guler, “Vesile ve Tevessul Hadislerinin Kaynak Degeri”, Jarida la taaluma la ILAM, toleo la II, n. 1, uk. 83-132.
6. al-Haytami, al-Khayratu'l-Hisan, uk. 94.





waliingia pangoni kwa ajili ya kupumzika kwa usiku mzima. Lakini baada ya pale jiwe kubwa likaporomoka kutoka mlimani na kuziba sehemu ya kutokea. Mmoja wao akashauri, 'Hatuna njia nyingine zaidi ya kumuomba Mwenyezi Mungu kwa kupitia amali zetu njema; hakuna mwingine kinyume na Mwenyezi Mungu ambaye anaweza kutunusuru na hili.'

Wa kwamba alitumia namna alivyowahudumia wazazi wake kama njia. Lile jiwe likasogea kidogo, lakini halikutoa njia ya kuwezesha kutoka. Wa pili alitumia hofu, usafi wake wa moyo na wema wake kama njia. Lile jiwe likasogea kidogo tena ingawa halikutoa uwazi wa kuwawezesha kutoka. Kisha wa tatu akatumia uchungaji wake wa haki za wengine kama njia. Kisha lile jiwe likasogea lote na kuwawezesha kutoka nje ya pango."<sup>7</sup>

Jambo lingine la msingi la kuwezesha maombi kupokelewa na kujibiwa ni majina mazuri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Hivyo ni jambo la kawaida kumuomba Mola kwa kurudia rudia Majina yake matukufu.

Qur'an inasema:

"Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri kabisa, basi muombeni kwa hayo..." (al-Araf, 180).

Katika suala hili Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiomba kwa kutumia maneno yafuatayo: "Mola wangu... Ninakuomba kwa kupitia jina Lako ambalo ni tukufu, bora, lililotakasika na ambalo unalipenda zaidi kuliko mengine! Hilo ni jina ambalo unajibu dua pindi itakapombwa kwa kupitia jina hilo, hutoa pindi kinapohitajika kitu, hutoa rehema zako pindi zinapohitajika na huonyesha njia pindi unapombwa msaada kwa kupitia Jina hilo."

Baada ya hapo Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alimuuliza Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

"Je unafahamu ewe Aisha kuwa Mwenyezi Mungu amenifundisha Jina lake ambalo pindi anapombwa kwa kupitia jina hilo hujibu maombi?"

"Wazazi wangu watolewe fidia kwa ajili yako ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu! Tafadhali nifundishe hilo jina", alisisitiza, kiasi kwamba Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:





“Hupaswi kufundishwa jina hilo!” Kisha Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akasogea pembeni na kukaa peke yake kwa muda. Baada ya muda mfupi akarejea na baada kumbusu Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kichwani akarudia:

“Tafadhali ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu...Nifundishe hilo jina!”

“Sipaswi kukufundisha hilo jina ewe Aisha kwani haitakuwa sawa kwa wewe kuomba kitu cha kidunia kwa kupitia jina hilo!” Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea kilichofuata baada ya pale kama ifuatavyo:

“Kisha nikanyanyuka na kuchukua udhu na baada ya hapo nikaswali raka mbili. Baada ya hapo nikamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kama ifuatavyo: ‘Ewe Mola wangu...Ninakutaja na kukuomba Wewe kama Mwenyezi Mungu...kama Mwingi wa rehema (ar-Rahman), Mwenye kurehemu (ar-Rahim), Mwema (al-Barr). Ninakuita kwa majina yote ninayoyafahamu na nisiyoyafahamu. Ninakuomba unisamehe na kunirehemu.” Pindi nilipomaliza maombi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alitabasamu na kusema:

“Kwa hakika umelitaja lile jina katika maombi yako!” (Ibn Majah, Dua, 9)

Anas ibn Malik – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia kifuatacho:

“Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alimsikia mtu akiomba, ‘Ewe Mola wangu...Utukufu ni wako pekee! Hakuna Mungu isipokuwa Wewe! Wewe uko peke yako bila ya mshirika yeyote! Wewe ndiye mpaji (al-Mannan). Wewe ndiye Muumba wa mbingu na ardhi (al-Badi’). Utukufu na heshima ni vyako...’Kisha mtu yule akataja shida yake. Baada ya pale Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:

‘Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mtu huyu ameomba kwa kutumia jina la Mwenyezi Mungu tukufu kuliko yote. Hilo ndilo jina la Mwenyezi Mungu ambalo kwa kupitia jina hilo mtu hupata chochote atakacho na hujibiwa dua atakayoiomba kwa kupitia jina hilo.’ (Ibn Majah, Dua, 9; Nasai, Sahw, 58)

Kwa hiyo ni wazi kwamba kuomba kwa kupitia majina mazuri ya Mola





ni sehemu ya *sunnah* ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

Baadhi ya wanachuoni wamesema kwamba hakuna tofauti kimaana kati ya maneno ya kisufi ya *tawassul*, *istianah*, *istighathah*, *istishfa*, *tashajfu*, *tawajjuh* na *tabarruk*, maneno ambayo yanaashiria kutafuta msaada.<sup>8</sup> Yanaashiria shauku ya kupata msaada wa kiroho (*himmah*) kutoka kwa watakatifu ambao wana amri ya kiroho wakiwepo na wasipowepo. Kuomba *himmah* kutoka kwa waja wema wa Mola wanaoaminika kuwa na amri ya kiroho ni kumuomba kuwa kama sababu (*wasilah*) katika njia ya kuelekea kwenye lengo kuu. Na mafanikio yake hupatikana kutokana na dua na msimamo wa kiimani.

Neno *himmah* lenye kumaanisha msaada wa kiroho mara nyingi linatumika sambamba na msaada unaotolewa na waja wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kinyume chake maneno yanayotumika kuashiria msaada wa Mola ni *nusrah* na *tawfiq*, maneno yenye kumaanisha msaada na usaidizi mtakatifu.

Kimsingi ni kwamba Mwenyezi Mungu peke yake ndiye anayeweza kusaidia. Hivyo ingelikuwa si jambo la kawaida kuchukulia kwamba kutafuta sababu katika dua ni sawa na kuomba msaada kwa mwingine. Mola pekee ndiye anayeombwa msaada wakati wote.

Qur'an iko wazi juu ya suala hili:

وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ

“...Na haupatikani ushindi ila kutoka kwa Mwenyezi Mungu” (al-Anfal, 10)

“Akikunusuruni Mwenyezi Mungu hapana wa kukushindeni, na akikutupeni ni nani, basi, baada yake Yeye ataye kunusuruni? Na Waumini wamtegemee Mwenyezi Mungu tu” (Al-i imran, 160)

Abdullah ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anakumbuka ushauri ufuatao aliopewa siku moja na Mtume aliyebarikiwa akiwa nyuma ya farasi wake:

“Ngoja nikufundishe maneno machache kipenzi change. Chunga





*maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu ili na Yeye aweze kukuan-galia na kukulinda wewe. Yafanye matamano yako yote yawe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu kwanza katika mambo yako yote ili Mwenyezi Mungu awe mbele yako. Kama unataka kuomba kitu muombe Mwenyezi Mungu. Kuna unatafuta usaidizi utafute kwake. Na tambua kwamba hata kama ulimwengu mzima ungelikusanyika kwa ajili ya kukunufaisha wewe basi wasingeliweza kuzidisha katika kile alichokukadiria Mwenyezi Mungu. Na kama ulimwengu mzima ungelikusanyika kwa ajili ya kukudhuru wewe basi wasingeliweza kufanikisha hilo zaidi ya kiwango alichokikadiria Mwenyezi Mungu” (Tirmidhi, Qiyamah, 59).*

Kwa kuwa waislamu wote wanauthamini ukweli huo, wanaendelea kurudia maneno hayo ndani ya al-Fatiha pindi wanapoisoma katika kila rakaa ndani ya kila swala:

إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ

“Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada”

Kwa hakika kuhusiana na msaada mtakatifu alioupata Mtume aliye-barikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – katika vita vya badr, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema, “...Na wewe hukutupa, walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliye tupa” (al-Anfal, 17); hii inamaanisha kwamba mfanyaji wa kweli na mtoaji wa msaada wa kiroho na rehema ni Mola pekee.

Dua zilizoombwa kwa moyo safi na shauku ya kupata ukaribu wa Mola bila ya kuwa na nia yoyote ya *shirk* ya *kufr*, na dua ambayo ime-ambatanishwa na watu wema bila shaka kuna matumaini makubwa ya kupata rehema za Mola. Hii husaidia kuleta mandhari ya kiroho ambayo yataongeza msukumo. Kila kitu hutokea kwa ruhusa ya Mola pekee. Mtu uliyempitishia maombi yako si mtendaji na Mwenyezi Mungu pekee ndiye mwenye kutoa msaada unaotafutwa.

Kuwaomba moja kwa moja watu wema ama wakiwa hai au wakati wa kutembelea makaburi yao na kuwaita kwa kusema, “Fulani! Niponye! Nikidhie haja yangu”, maneno ambayo watu wengi wanayatumia ni kosa kubwa mno na ni jambo ambalo linaweza kufungua milango ya *shirk*. Ingawa tafsiri nyingi zinaweza kutolewa kwa ajili ya kuondokana na maneno hayo, hivyo mtu hana budi kujizuia na maneno hayo kabisa ili kue-





puka kudhuru kiini cha imani ya upweke wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Maneno kama hayo ambayo humhusu Mola pekee yakitumiwa kinyume yataweza kuleta tabu katika ulimwengu huu.<sup>9</sup>



9. Wale waliosema kwamba maneno hayo yanaweza kutumika wamependekeza kwamba kila neno miongoni mwa maneno hayo halina budi kuchukuliwa kama tashbihi ya kimantiki (*majaz-i aqli*), aina ya maneno katika sayansi ya balagha. Tashbihi ya kimantiki ni pale kitendo kinaponasibishwa na mtu ambaye siye mtendaji halisi lakini badala yake kinanasibishwa na sababu yake inavyoonekana na kubainika katika nyakati na nafasi. Mfano mzuri wa matumizi ya tashbihi ya kimantiki ndani ya Qur'an ni katika aya isemayo, "Na itakapo toa ardhi mizigo yake" (az-Zilzal, 2), hapa kitendo cha 'kutoa mizigo' kimenasibishwa na ardhi ambayo ndipo mahali ambapo kitendo hicho kitatokea, wakati mfanyaji wake halisi ni Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani Yeye atakayetoa hiyo mizigo ndani ya ardhi. Hivyo bado mtendaji hapa ni Mwenyezi Mungu licha ya Yeye kutotajwa moja kwa moja.

Kwa hiyo sufi wanashikilia na kuamini kwamba mtu ambaye wanaomba kwa kumpitia yeye kiuhalisia si mtendaji, kwani mtendaji wa kweli ni Mola; na Mola pekee ndiye wanayemuomba msaada. Wanakubaliana kwamba mawazo mengine yaliyo kinyume na haya yanaweza kupelekea kwenye shirki.

Kuhusiana na hili Muhammad Abu Zahra anasema:

"Maneno ya waislamu wa kawaida na wasio na hekima hayana budi kutafsiriwa kulingana na maana zake za karibu zaidi. Badala ya kuwakataza kabisa wasitembelee kaburi la Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – ni vyema uwape maelekezo yanayofaa. Kuwaelezea na kuwataarifu ni bora kuliko kuwahukumu kwa shirk. Hakuna shaka kuwa Mwenyezi Mungu anaweza akaiihifadhi *tawhid* yao mpaka siku ya mwisho. Katika siku zake za mwisho Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – aliwapa waumini bishara njema kwamba shetani amepoteza matumaini kabisa ya kuja kuabudiwa tena katika ardhi hizi. Hivyo Ibn Taymiyya apumzike sehemu nzuri kutokana na jitihada yake ya kuhuisha *tawhid*" (Abu Zahra, Ibnu Taymiyya, uk. 326).

'*Meded ya Rasulallah*' (tusaidie ewe Mtume), neno ambalo linakaririwa mara kwa mara katika fasihi ya kiislamu, ni ombi analopelekewa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa matumaini ya kupata maombizi yake siku ya kiamaa. Kulichukulia jambo hili kama shirk si rehema na amani ziwe juu yakea kwani kila muumini anaamini kwamba hata hayo maombezi ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – yatafanyika kwa ruhusa ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.







**H**eshima inayooneshwa kwenye kumbukumbu yenye kuvutia ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – inatokana na uwepo wa mapenzi yanayohisiwa juu yake.



## **B. KUTAFUTA BARAKA (TABARRUK)**

*Tabarruk* ni kuomba Baraka kutoka kwa mwingine. Ni kupata manufaa na msukumo wa kiroho kwa kupitia kitu kingine.

### **Kutafuta baraka kutoka kwenye chakula kilichobaki**

Kutumia chakula kilichobakizwa na watakatifu kumekuwa ni njia iliyotumiwa kwa ajili ya kupata baraka. Kinyume na watu wengi wanavyofikiria hili si jambo lisilo sahihi (*bidah*). Fasihi ya *hadith* na historia ya waislamu inathibitisha mengi katika suala hili wakati wa uhai wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake.

Katika nyakati na sehemu mbalimbali na wakati wa harakati za Hundaybiyah, maswahaba walitafuta manufaa ya kiroho kutoka kwa mabaki yaliyobarikiwa ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

Jabir – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

“Watu walikuwa wamechoka kutokana na kiu katika siku ya Hundaybiyah, hivyo wakaenda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye wakati ule mbele yake kulikuwa na chombo cha maji kilichotengenezwa kwa ngozi. Watu walipomsogelea ndio alikuwa ametoka kuchukua udhu.

‘Mna shida gani?’ Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliuliza.

‘Hakuna maji yaliyobaki kwa ajili ya kunywa wala kuchukulua udhu isipokuwa haya machache yaliyo mbele yetu’, walielezea.

Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu akaingiza mkono wake ndani ya kile chombo. Mara maji yakaanza kutiririka kutoka kwenye vidole vyake; vilikuwa ni kama chemchem yenye kurusha maji yake. Wote tukanywa na kuchukua udhu kwa kutumia maji yale.”





“Siku ile mlikuwa wangapi?” Jabir – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliulizwa.

“Kama tungelikuwa laki moja yale maji yangelikutosha; lakini kwa wakati ule tulikuwa elfu moja na mia tano kwa ujumla.” (Bukhari, *Manaqib*, 25).

Bila shaka maji yaliyotiririka kutoka kwenye vidole vya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake - ni bora zaidi na yanatibu zaidi kuliko yale ya *zamzam*, kwani maji haya yanatiririka moja kwa moja kutoka kwenye mikono mitakatifu ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

Kutokana na *hadith* nyingi tumefahamishwa kwamba pindi Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa akimaliza kunywa maziwa kwenye chombo kilichojaa maziwa alikuwa akiwapatia maswahaba zake waliokuwa karibu yake yale yaliyobakia ili aweze kuhamisha msukumo wa kiroho, manufaa ambayo yangelikuwa yameingia kwenye maziwa yale moja kwa moja bila ya kupungua chochote.

Sahl Ibn Sad – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anathibitisha kama ifuatavyo:

“Wakati fulani Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipewa kikombe cha kinywaji. Akanywa sehemu ya kinywaji kile. Upande wake wa kulia kulikuwa na mototo na ule wa kushoto walikuwepo maswahaba zake wakubwa. Kisha akamgeukia yule mtoto kwa upole na adabu na kumuuliza:

‘Je unaweza kuniruhusu kuwapa hiki kinywaji wakubwa zako kwanza?’

Lakini mtoto yule mwerevu alitoa jibu lenye kustaajibisha. ‘Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu’, alisema, ‘Kamwe siwezi kufikiria kumpa mwingine mgao ulionipatia!’

Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akampa mtoto yule kile kikombe.” (Bukhari, *Ashribah*, 19)

Asma bint Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaeleza:

“Wakati nilipokuwa na ujauzito wa Abdullah ibn Zubayr nilihama pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu





yake. Pindi tulipofika Madina nilisimama sehemu karibu na Quba mahali ambapo ndipo nilipojifungulia. Kisha nikamsogelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – pamoja na mwanangu. Akamchukua yule mtoto mikononi mwake na kuagiza kipande cha tende. Baada ya kukitafuna kidogo akakiweka kwenye mdomo wa Abdullah. Hiki kilikuwa ndicho cha kwanza kukitumia Abdullah. Kisha Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – akamuombea yule mtoto baraka tele.<sup>10</sup>

Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa mgeni wao, Abu Ayyub al-Ansari na familia yake walikuwa wakimpa chakula walichokiandaa. Pindi mabaki yalipokuwa yakirejeshwa Abu Ayyub alikuwa akitafuta ile sehemu ya chakula iliyoguswa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na kula kwa ajili ya *tabarruk*. (Muslim, Ashribah, 170-171)

Jabir – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - anasimulia nyakati za ugumu walizopitia kabla ya vita vya Handak wakati walipokuwa wanachimba mahandaki:

*“Tulipokuwa tukichimba mahandaki katika masiku kabla ya vita vya Handak tulifikia kwenye muamba mgumu sana. Baadhi ya maswahaba walienda kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kumwambia kwamba wamekutana na muamba mgumu ambao hawawezi kuuvunja.*

*‘Nitashuka chini mwenyewe’ Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – aliwaambia. Kisha akanyanyuka. Akafunga jiwe kwenye tumbo lake kutokana na njaa. Ilikuwa ni siku ya tatu tokea wapate chochote. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akakamata sururu na kuugonga ule mwamba, pale pale ukapasuka na kugeuka na kuwa kama mchanga.*

*‘Naomba niende nyumbani ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu’, baada ya pale nikaomba. Baada ya kuruhusiwa nilienda nyumbani na kutokana na hali niliyomuona nayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu nilimwambia mke wangu, ‘Je kuna chochote kwa ajili ya kula?’*

*‘Kuna shayiri kidogo na mwana mbuzi’, mkewe alisema.*

*Hivyo nikamchinja yule mwana mbuzi na kuandaa shayiri. Tukaweka*

10 Rejea Bukhari, Aqiqah, 1.





nyama ndani ya chungu. Mkate ulipokuwa unakaribia kuiva na chungu kilipokaribia kuchemka nikamkimbilia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu na kusema:

*'Nina chakula ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Tafadhali twende wewe na baadhi ya maswahaba...'*

*'Huko kuna kiasi gani cha chakula?' akauliza. Nikamwambia kiasi tuli-chokuwa nacho. Kisha akasema, 'Ni kizuri na kingi...Mwambie mkeo asiepue chungu kutoka kwenye moto na auache mkate kwenye tanuru mpaka tufike!'*

*Kisha akawageukia maswahaba zake na kuita kwa sauti ya juu, 'Enyi watu wa mahandaki; njooni...Jabir ametuandalia chakula!' Kila mtu aliyekuwapo pale akaenda.*

*Huku akiwa amejawa na wasiwasi alikimbilia kwa mke wake na kusema, 'Angalia kilichotokea sasa...Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anakuja pamoja na kundi lote la Ansar, Muhajirun na wengine kama hao!'*

*'Je Mjumbe wa Mwenyezi Mungu aliuliza kuna kiasi gani cha chakula?' mkewe aliuliza.*

*'Ndio' nilijibu.*

*'Basi usiwe na wasiwasi', alimtuliza, 'kwani yeye anajua zaidi yako!'*

*Baada ya muda mfupi wakawasili. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akawaambia waingie bila ya kusukumana. Maswahaba wakaingia kumi kumi. Kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akaanza kuigawa nyama na kuweka kipande cha nyama juu yake na kumpa kila swahaba aliyekuwa anasubiria; na kila wakati alipomaliza kugawa alikuwa akifunika chungu na tanuru. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akarudia zoezi lile mpaka kila swahaba aliyekuwapo pale akala na kutosheka. Mwishoni mwa zoezi lile kukawa na chakula kimebaki. Kisha akamgeukia mke wangu na kumwambia 'kula hiki na kingine uwapatie majirani zako; kwani kwa hakika njaa imemshika kila mtu!' (Bukhari, Maghazi, 29; Muslim, Ashribah, 141)*

Yafuatayo ni masimulizi mengine:

*Pindi Mtume aliyebilikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – alipore-*





*jea kutoka kwenye harakati za Taif alifika Jirannah, sehemu iliyokuwa kwenye njia ya kutoka Makka mpaka Madina. Pale akawapatia Abu Musa al-Ashari na Bilal – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – chombo kilichokuwa na maji ambayo baadhi yake aliyatumia na kuwaambia:*

*“Kunyweni haya maji na mengine mjipige nayo kwenye nyuso zenu na vifua. Kuna bishara njema kama mtafanya hivyo”. Waliyachukua maji yale kufanya kama walivyoshauriwa. Nyuma ya pazia Ummu Salamah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye alikuwa ni mke wa Mtume akaita:*

*“Mpeni sehemu ya maji hayo mama yenu naye”. Kisha maswahaba wawili wakampelekea Ummu Salamah baadhi ya yale maji. (Bukhari, Maghazi, 56)*

### **Kutafuta Baraka kutoka kwenye mali**

Ni jambo lisilopingika kwamba kitu ambacho kinaamsha kumbukumbu ya kipenzi cha mtu huwa kinazidisha mapenzi juu yake pale kinapomletea hisia za kumkumbuka. Hii ni sifa ya mwanadamu. Pia ime-thibitika katika historia kwamba kuzama sana katika hisia hizo kunaweza kumpelekea mtu kuingia katika shirk.<sup>11</sup> Na wakati huo huo ni jambo la kawaida kujawa na mapenzi ya kukipenda kitu analichonacho kipenzi chako. Cha msingi ni kujitahidi kutovuka mipaka.

Mfano wa dhahiri uliotajwa ndani ya Qur'an katika kuonyesha mvuto wa kiroho unaotokana na mali ya mtu ni shati la Yusuf – amani iwe juu yake. Pindi lilipochukuliwa kutoka misri kwa ajili ya kupelekwa kwa Yaqub – amani iwe juu yake – licha ya kuwa Canaan lakini Yaqub – amani iwe

<sup>11</sup> Ukweli ni kwamba katika historia ya dini kuabudia miungu ya masanamu ni jambo lililotokea baada ya watu kuvipa utukufu vitu vilivyokuwa vimeachwa na mashujaa waliokufa, huu ni upotoshaji wa kihistoria ambao ulitokana na kukithirisha ada hii ya kawaida. Kwa kuwa ni vigumu kuelewa mambo yaliyojifisha watu wengi walifikia kumnasibisha muumba na vitu vinashikika, na hivyo kufikia kuabudia masanamu. Ni kweli kwamba ubainifu wa kiroho unaweza ukafanywa kwenye vitu vinavyoshikika. Lililo la rehema na amani ziwe juu yakea ni kuvitumia vitu hivi kwa namna ambayo itakupa msukumo wa kumfikia muweza. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anapokuja kufahamika pamoja na uwezo wake. Hili linaenea kwenye uhalisia wote wa dhahania.



juu yake – aliweza kuhisi harufu yake; na pindi shati lile lilipopanguswa kwenye macho yake yasiyoona aliweza kuona tena.<sup>12</sup>

Kwa hiyo msukumo huu wa kiroho uliotokana na kitu cha mtu humfanya *murshid* aweze kumuivisha mwanafunzi wake kiimani. Pia hili ni jambo lenye kuongeza mshikamano wa kiroho. Wakati huo huo hili jambo lililoshauriwa na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – juu ya kupeana zawadi.

Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa na maswahaba zake katika makao makuu ya Banu Saidah alim-uomba Sahl Ibn Sad – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ampatie kikombe cha maji. Kutokana na maneno yafuatayo ya Abu Hazim – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – lazima Sahl atakuwa amekienzi kikombe kile katika maisha yake yote:

“Sahl alichukua kikombe na kutoka nacho nje; na sisi tukakitumia kwa kukinywea maji. Baadae Omar ibn Abdulaziz akamsisitiza ampatie kile kikombe kama zawadi. Naye akafanya hivyo” (Bukhari, Ashribah, 30).

Sahl ibn Saad – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

*“Siku moja mwanamke mmoja alimletea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – joho na kumwambia kuwa ameamua kumpa kama zawadi. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – akaikubali ile zawadi na kulivaa lile joho. Lakini baada ya hapo swahaba akasema:*

*‘Uzuri ulioje wa joho hilo, ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, unaweza kunipatia mimi?’*

*‘Bila shaka’, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alijibu na huku akimpa yule swahaba joho. Baada ya Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – kuondoka maswahaba wengine wakamsema yule swahaba.*

*‘Ulichokifanya si sawa’, walisema. ‘Mjumbe wa Mwenyezi Mungu alilipokea lile joho kwa kuwa alikuwa analihitaji. Na kisha baada ya hapo ukamuomba huku ukifahamu fika kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu huwa hakatai kutoa chochote anachoombwa’*





*‘Nilichohitaji ni kuvuna baraka zake za kiroho (tabarruk) kwa kuwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa amelivaa’, yule swahaba alielezea. ‘Na ninatarajia kuwa nikifa hii ndiyo itakayokuwa sanda yangu’ (Bukhari, Adab, 39)*

Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

*“Kulikuwa hakuna kitu kinachowapendeeza maquraish kama kulala juu ya sarir. Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipowasili Madina na kukaa kwa muda kwenye nyumba ya Abu Ayyub alimuuliza ikiwa walikuwa nayo. Lakini ikawa hanayo.*

*Baada ya Asad ibn Zurarah kutoka Ansar kusikia kuhusu suala lile alimtumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – sarir iliyozungukwa na majani makavu na iliyotengezewa kwa mwaloni na kufumwa kwa kitani.*

*Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akaitumia sarir ile kwa kipindi chote alichokuwa ndani ya nyumba ya Abu Ayyub na baada kuhamia kwenye chumba chake kilichokuwa pembezoni mwa msikiti. Baada ya kufa kwake alioshwa na kufunikwa sarir hii pindi alipolazwa kwa ajili ya kuswaliwa.*

*Baada ya pale watu wakawa wanaomba waazimwe ile sarir kwa ajili ya kubebea miili ya maiti zao ili ipate baraka zake za kiroho. Maiti za Abu Bakr na Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – nazo zilibebeba kwenye sarir hiyo hiyo mpaka makaburini. (Balazuri, Ansabul-Ashraf, I, 525)*

Tukio kama hilo ni hili lifuatalo:

*Abu Hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye ndiye swahaba aliyesimulia idadi kubwa ya hadith kupita wenzake, alikuwa bega kwa bega na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – huku akifuatilia kila kitendo na mwenendo wake. Siku moja alilalamika kwa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwamba anashindwa kukumbuka mengi miongoni mwa yale anayoyasema licha ya kuyahifadhi kichwani mwake pindi ayasikiapo.*

*“Tandika joho lako chini”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alisema kabla ya kumuomba na kufanya kana kwamba anakusanya vitu kwa mikono yake na kutupia kwenye lile joho lililotandikwa.*





Kisha akasema, “Nyanyua joho lako”. Baada ya pale Abu Hurayrah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akajaaliwa kumbukumbu imara ambayo ilimfanya asisahau chochote alichokisikia kuanzia pale. (Tirmidhi, *Manaqib*, 46)

Swahaba mwingine aliyekuwa akifahamika kwa jina la Firas naye alitaka kumiliki kitu kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake. Siku moja alimuona Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akila kwenye sahani mbele yake; hivyo akaamua kumuomba ile sahani kama zawadi kwake. Kwa kuwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kamwe hakatai ombi la yeyote aliamua kumpa Firas ile sahani.

Mara kwa mara Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa akienda nyumbani kwa Firas na kumuomba alete ‘...ile sahani takatifu’. Kisha alikuwa akijaza maji ya zamzam ile sahani iliyowahi kuguswa na mikono mitakatifu ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake, na kisha alikuwa akinywa yale maji na yaliyobaki kujipiga nayo usoni mwake. (Ibn Hajar, *al-Isabah*, III, 202)

Abu Juhafah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – naye amesimulia yafuatayo:

Katika joto kali la mchana Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alitoka na kwenda kwa Bathah, mahali ambapo alichukua udhu na kuswali swala za *Dhuhur* na *al-asir* kwa raka mbili mbili. Mbele yake kulikuwa na mkuki mfupi. Mara watu waliokuwa pale wakanyanyuka na kuanza kushika mikono ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na kuifutia kwenye nyuso zao. Na mimi pia nikaushika mkono wake na kuuweka usoni mwangu; kwa hakika mkono wake ulikuwa wa baridi kuliko theluji na ulikuwa ukinukia vizuri kuliko maski. (Bukhari, *Manaqib*, 23)

Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia namna maswahaba walivyokuwa wakishindana katika kupata vipande vya nywele za Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwa matumaini ya kupata baraka ndani yake:

“Baada ya kumpiga mawe shetani, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alichinja mnyama wake na kunyoa







nywele zake. Kinyozi akashika kishungi cha nywele za upande wake wa kulia na kukikata. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akamuita Abu Talha na kumpa kile kishungi. Kisha kinyozi akashika nywele za upande wake wa kushoto. ‘Zikate’, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akamwambia; na yeye akafanya vile. Pia akampa Abu Talha kile kishungi cha pili na kumwambia ‘zigawanye kwa watu!’” (Muslim, Hajj, 323-326)

Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anathibitisha namna maswahaba walivyokuwa wakijikusanya kumzunguka Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – pindi alipokuwa ananyoa ile kuhakikisha hakuna hata unywele mmoja unaodondoka chini bila ya kuokotwa na mtu. (Muslim, Fada'il, 75)

Kwa hakika maswahaba hawakutafuta baraka kwenye nywele za Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – peke yake lakini pia walitafuta baraka hizo kwenye vitu vyake binafsi. Walikuwa wakiendelea na mwenendo huu mpaka katikati ya mapambano makali ya vita. Moja ya mfano mzuri wa suala hili unasimuliwa na Khalid ibn Walid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye alihifadhi kwenye *imamah* yake vinywele vichache vya Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – kama kumbukumbu.

Imesimuliwa kwamba pindi nywele za Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake – zilipokuwa zinakatwa Khalid ibn Walid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aling'ang'ania awe mkingaji wa nywele zile. “Tafadhali nipatie mimi hizo nywele ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu”, aliomba. “Usimchague yeyote juu yangu katika hili...wazazi wangu watolewe fidia kwa ajili yako!”<sup>13</sup>

Baada ya kupata zile nywele za Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – alizokuwa akizitamani mno, alizipangusia kwenye macho yake na kuziweka mbele ya kofia yake ndani ya *imamah*. Kuanzia pale kamwe hakuwahi kukutana na maadui akashindwa. Khalid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisema, “kila nilipokuwa nikizielekezea

13. Wakati huo Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alikuwa anayalinganisha makosa ya Khalid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - wakati wa Uhud, Handak na Hudaybiyah na alivyo sasa. (Ibn Saad, II, 174).



*hatimaye sehemu hiyo ilikuwa ikichukuliwa!”<sup>14</sup> (Waqidi, III, 1108; Ibn Athir, Usd’ul-Ghabah, II, 111)*

*Wakati fulani katikati ya mapambano makali katika vita vya Yamamah Khalid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipoteza imamah yake. Kisha akawaagiza askari zake waitafute. Licha ya kuitafuta lakini hawakufanikiwa kuiona popote. Hivyo Khalid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akaawagiza tena waitafute. Baada ya kuitafuta kwa kina waliipata na kuikuta ni kuukuu na imechakaa, walishangazwa na jambo lile. Haikuwaingia akilini ni kwa nini kamanda wao asisitize kukitafuta kitu kama kile kisicho na thamani yoyote. Ili kuwafanya waelewe Khalid – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – aliwaelezea kama ifuatavyo:*

*“Nywele za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – zilikuwa zinakatwa na huku maswahaba wanazigombania. Na mimi pia nikafanikiwa kupata vinywele vichache na kuviweka kwenye imamah*

14. Hikmet Atan anathibitisha tukio la karibuni linalohusiana na baraka zilizotokana na nywele na ndevu za Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake: “Mwaka 1983 nilimsikia Ali Yucel Efendi akisimulia tukio lifuatalo: ‘ilikuwa ni wakati nilipokuwa imam katika msikiti mkuu wa Suluova pindi imam mwingine kutoka katika kijiji cha jirani alipokuja kwangu na kusema, ‘Kuna kitu kimetokea lakini hakiningii akilini’, alisema hivyo kabla ya kuanza kunielezea yafuatayo. ‘Hivi karibuni watu kutoka katika kijiji cha jirani walinjia na idadi kubwa ya vitabu. ‘Baba yetu amefariki muda si mrefu na ametuachia hivi vitabu’, walisema, ‘lakini hatuwezi kuvisoma. Wewe ni mwanachuoni, hivyo wewe unaweza kunufaika navyo. Hivyo tumefikiria tukuletee kama zawadi’. Hivyo nikavichukua vile vitabu na kwenda nyumbani. Kisha nikakaa mbele ya jiko lililokuwa likiwaka kwa nguvu kisha nikaanza kuvichunguza vile vitabu. Ndani yake kulikuwa na barua na bahasha za imam aliyekuwa amefariki. Nilifikiria kwamba zilikuwa ni zake binafsi hivyo nikaamua kuzirushia ndani ya lile jiko na kuanza kuungua vibaya mbele yangu. Lakini mara tu baada ya kufanya vile jiko lilifanya ‘tissss’ na kuzimika. Kutokana na kuogopesha na kitendo kile nilikimbilia nje. Baadae ndipo nilipopata ujasiri wa kuingia tena ndani.”
- “Hivyo nikamwambia *hodja* kwamba ndani ya bahasha moja miongoni mwa zile bahasha kulikuwa na unywele wa Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake”, Ali Efendi aliendelea. Baada ya muda si mrefu nilimuona tena *hodja* ambaye aliniuliza pale pale, “Ulijuaje kuwa kulikuwa na unywele wa Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – ndani ya moja ya bahasha zile?” Watu waliokuwa wamenipatia vile vitabu walikuja tena baadae na kusema, ‘Tulikuwa hatufahamu kwa wakati ule lakini tumegundua kwamba kulikuwa na unywele wa Mtume aliyebarikwa – rehema na amani ziwe juu yake – ndani ya bahasha zile. Je unaweza kuturudishia?’.





*hii. Nywele hizo ziliniletea baraka kiasi kwamba hakuna vita nilivyopigana huku nimevaa imamah hii isipokuwa nilishinda. Siri ya ushindi wangu si kingine zaidi ya kumpenda Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake.” (Haythami, Majmau’z-Zawaid, IX, 349)*

Matukio hayo yaliyojidhihirisha mbele ya macho ya maswahaba ni ushahidi zaidi kwamba maada inaweza kuwa chanzo cha baraka. Ufunguo wake ni kuwa na moyo ulioamka ambao unaweza kupokea utukufu utokao kwenye kitu husika kwa sharti kwamba mtu havuki mipaka.

Watu wema waliotangulia – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – waliendeleza mwenendo wa maswahaba wa kutafuta baraka. Ifuatayo ni mifano michache:

Ibn Sirin anasema:

“Pindi nilipomfahamisha Ubaydah kwamba ninao unywele wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake - niliourithi kutoka kwa mama au familia ya Anas, kutokana na furaha kubwa iliyompata alisema: ‘Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba kuwa na unywele wake mmoja tu kunanipendezea kuliko dunia nzima na vilivyomo.” (Bukhari, Wudu, 33)

Abdullah ambaye ni mtoto wa Ahmed ibn Hanbal anasimulia yafuatayo:

“Mama yangu alikuwa akishikilia unywele wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na kuuweka mdomoni mwake na kuubusu. Wakati mwingine alikuwa akiuweka juu ya kope za macho yake. Kuna wakati mwingine alikuwa akiudumbukiza kwenye kikombe cha maji na kunywa maji yake; na kisha alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu kwa kupitia Baraka za unywele ule amponywe maradhi yaliyokuwa yanamsumbua. Pia ninakumbuka wakati ambao alichukua kikombe alichokitumia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na kukiosha ndani ya ndoo na kunywea maji ndani yake. Pia alikuwa akinywa maji ya zamzam na kupitisha maji kwenye mikono na uso wake.” (Dhahabi, Siyari Alami’n-Nubalam Beirut, 1986-1988, XI, 212)

Abdullah huyo huyo siku moja alimuuliza baba yake ambaye ni Ibn Hambal ikiwa ilikuwa inaruhusiwa kugusa kinundu cha mimbari ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – (ambayo alikuwa akiiegemea pindi alipokuwa anatoa hotuba) na chumba cha Mtume kwa lengo la kupata baraka.





“Sioni tatizo katika hilo”, lilikuwa ndilo jibu lake. (Dhahabi, Siyar, XI, 212)

Qadi Iyad anathibitisha kwamba “Ibn Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alionekana akisugua uso wake kwenye sehemu ya mimbari ambayo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiitumia kukalia.”<sup>15</sup>

Tukio lifuatalo lililoripotiwa kuwa lilitokea kati ya Imam

Ahmed ibn Hanbal na Imam Shafii – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yao – ni moja ya mifano mizuri katika suala hili. Anayesimulia ni mwanafunzi wa Imam Shafii anayeitwa Rabi ibn Sulayman:

*“Siku moja Imam Shafii alinipatia Barua na kuniagiza niipeleke kwa Ahmad Ibn Hambal na kurudisha majibu. Hivyo nikaichukua ile barua na kuelekea Baghdad. Nilikutana na Imam wakati wa swala ya alfajir na kuswali nyuma yake. Baada ya pale pindi Imam alipotoka pale mihrab nilimpatia ile barua na kusema:*

*‘Hii ni barua iliyotumwa kutoka Misri kutoka kwa ndugu yako Imam Shafii’*

*‘Je unafahamu kilichoandikwa?’ aliuliza.*

*‘Hapana’, nilijibu. Kisha Imam akaifungua ile barua na kuisoma. Mara akawa anabubujikwa na machozi.*

*‘Barua inasemaje?’ nilimuuliza kwa shauku.*

*Akaanza kuelezea, ‘Anasema kwamba katika ndoto alimuona Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye alimua-giza amuandikie barua Ahmad Ibn Hambal na kumtumia salamu zake; na amuambie kwamba atakabiliwa na mtihani mkubwa, mtihani ambao atatakiwa adai kwamba Qur’an imeumbwa. Mwambia kwamba asije akakubali kwa namna yoyote ile, kwani Mwenyezi Mungu atalitukuza jina lake na kulifanya libakie mpaka siku ya mwisho’*

*‘Uzuri ulioje wa habari hizo’, nilisema. Kutokana na furaha Imam akavua shati lake na kunipatia; na baada ya kupokea lile shati kama majibu ya barua ile nilirejea Misri. Pindi nilipompata Imam Shafii lile shati alisema:*





*'Sitaki kukuudhi kwa kulichukia hilo shati. Lakini labda unaweza kuli-dumbukiza ndani ya maji na kunipatia hayo maji ili wote tuweze kupata baraka (barakah)''<sup>16</sup>*

Vipande vya ndevu za Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – vimekuwa vikitunzwa na kulindwa kwenye mimbari za misikiti mbalimbali duniani kote, na imekuwa kama rehema kwa waislamu wote, na upepo mwanana unaovuma kutokea wakati wake mpaka wakati wetu. Kuheshimu kumbukumbu nzuri ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ni jambo lenye kuimarisha mapenzi na utii juu yake ndani ya moyo. Watu wengi waliokuwa wakimtii Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – walipata Baraka nyingi za kiroho zilizotokana na hizi kumbukumbu.

Uzuri wa dola ya Uthmainiyya ambao ulibakia kwa takriban karne sita na ambao haufananishwi na dola nyingine za kiislamu, ulifikia kwenye hatua hiyo kutokana na heshima yake kubwa juu ya vitu vya kiroho. Katika kutambua uzuri wa dola ya Uthmainiyya mtu anaweza kukumbuka tukio maarufu ambalo Othman Gazi alibakia macho usiku kucha kutokana na kuona kwamba haitakuwa heshima kuweka mguu wake juu ya sakafu ya chumba ambacho ndani yake kulikuwa na nakala ya Qur'an, na pia tunaweza kukumbuka wakati ambao Sultan Salim kutokana na uchamungu wake alipeleka Istanbul amana takatifu za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na kujenga ngome ya *huffaz* kwa ajili ya kusoma Qur'an pembeni yake usiku na mchana, utaratibu huu haukukoma mpaka pale dola ilipoanguka.

Suala kwamba amana takatifu likiwemo joho la Mtume aliyebarikiwa vipo mpaka leo na muislamu yeyote anaweza kuviona, kunaleta njia kwa ulimwengu mzima wa kiislamu kuweza kupata Baraka.



<sup>16</sup> Rejea Ibnul-Jawzi, Manaqibu'l-Imam Ahmed ibn Hanbal, uk. 609-610.



**N**liwakataza kutembelea makaburi. Lakini sasa hivi mnaweza kuyatembelea, kwani kuyatembelea makaburi kutawakumbusha juu ya akhera. (Tirmidhi, Janaiz, 60; Muslim, Janaiz, 106)

*Makaburini ni shule za hekima na kutembelea makaburi kunatoa mafunzo bora kuhusiana na kuyatafakari mauti.*



### C. KUTEMBELEA MAKABURI

Katika safari yake ya maisha mwanadamu hutetemeka kati ya pande mbili zenye kuvutana; furaha ya kuishi na hofu ya kufa. Bila ya kufahamu fika hali halisi ya uhai na kifo kutakuwa hakuna uelewa wa hali halisi ya mwanadamu na siri ya kustaajabisha ya kuumbwa kwake.

Uelewa wa mwanadamu ambao umekwama kati ya mafumbo mawili ‘la kuja hapa duniani na kuondoka hapa duniani’ hauna budi kujipandisha ili kufikia kwenye uelewa wa sawa na wa kweli kuhusiana na dunia na hivyo kuweza kufanya mambo yake kulingana na uelewa huo. Baada ya hapo ndipo atakapoweza kujinasua kutoka kwenye kivuli cha udanganyifu cha maisha ya dunia na kuingia kwenye safari ya kiroho ya kuelekea kwenye ulimwengu wa kweli.

Kwa muumini kifo ni njia ya kukutana na Mola wake na ni mapito ya furaha na ya kuvutia ambayo yanatoka kwenye hali moja na kuelekea kwenye nyingine. Kwa kafiri na muovu kifo ni maumivu na udhalili ambao unamletea dhoruba ya adhabu itokayo kwenye mashimo ya Moto.

Kibarua kigumu kwa mwanadamu ni pale anapoanza kutatua fumbo gumu lililopo chini ya ardhi. Mazingira ya ardhi ya waliokufa huwa haitoi siri zake mpaka mtu mwenyewe afanye jitihada kubwa, atafute, awe na moyo safi na awe na utambuzi wa kiroho katika uhalisia wa kifo usiopingika.

Bila shaka mwanadamu ana washauri muhimu wawili katika maisha yake. Mmoja anaongea, wakati mwingine amekaa kimya. Mshauri mwenye kuongea ni Qur’an. Na yule mwenye kutoa ushauri kutokana na ukimya wake ni kifo. Ndio maana katika historia yote waislamu wamekuwa wakiweka makaburi katikati ya miji, pembezoni mwa barabara na katika viwanja vya misikiti ili wawape wale wanaoishi fursa ya kutosha ya kunu-





faika na ushauri wa kimya wa kifo. Majani yaliyopendekezwa yalikuwa ni yale ya kijani kama ya mvinje wenye kudumu ili kuwa kama alama ya akhera, alama ya maisha yasiyo na mwisho.

Kifo hakina lugha; lakini kuna maana kubwa iliyofichikana ndani ya kimya chake kikubwa! Kwa sasa makaburi ni makazi ya mama, baba, watoto, wapenzi, marafiki na wema ambao walipata ukazi huo baada ya kumaliza muda wao juu ya ardhi.

Kuhusiana na mazingira ya kaburini ambayo yataendana na namna mtu alivyoishi hapa duniani kulingana na maamrisho ya Mola, Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – anasema:

“Kaburi ni ama bustani la peponi au shimo la Moto” (Tirmidhi, Qiya-mat, 26). Hii inaashiria uhusiano wa karibu kati ya matendo katika maisha ya hapa duniani na maisha ya kesho akhera.

*Othman – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alikuwa anapo-simama karibu na kaburi analia mpaka ndevu zake zinaloa machozi. Siku moja mtu mmoja alimuuliza, “Hulii pindi unapokumbuka akhera na Moto; lakini unamwaga machozi pindi unapojiwa na fikra ya kaburi!”*

*“Ninalia kwa kuwa nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – re-he-ma na amani ziwe juu yake – akisema, ‘Kaburi ni kituo cha kwanza cha akhera. Kama mtu ataweza kukipita vizuri basi yaliyobaki yatakuwa mepe-si. Kinyume chake yaliyobaki yatakuwa magumu na mazito zaidi. Hakuna kitu ninachokiona kinatisha na kuhuzunisha kama kaburi!” (Tirmidhi, Zuhd, 5/2308; Ahmed, I, 63-64)*

Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - anasimulia kwamba siku moja mwanamke mmoja wa kiyahudi alimjia na baada ya kuongelea habari za adhabu za kaburi akamwambia, “Namuomba Mwenyezi Mungu akulinda dhidi ya adhabu yake!”

Baada ya pale Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alim-uuliza Mtume aliyebarikiwa – rehemu na amani ziwe juu yake – kuhusiana na adhabu ya kaburi.

“Ndio”, alisema. “Adhabu ya kaburi ni kweli”

“Kuanzia siku ile sikumuona tena Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – akiswali bila ya kujilinda dhidi ya adhabu





ya kaburi”, Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alisema. (Bukhari, Janaiz, 87; Muslim, Masajid, 123).

Bara – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

“Tulikuwa na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake - katika mazishi. Huku akiwa karibu na kaburi alilia mpaka machozi yake yakalowesha udongo uliokuwa chini yake. Kisha akasema, ‘Ndugu...jiandaeni vjema na kile kitakachotufika (kifo) sisi sote!’” (ibn Majah, Zuhd, 19)

Hatuna budi kutambua kuwa maeneo ya makaburi ni shule za hekima na mafunzo na kuyatembelea makaburi kunatoa mafunzo mazuri juu ya tafakuri ya mauti. Katika kuonyesha heshima mara kwa mara Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiyatembelea makaburi ya maswahaba zake waliotangulia na kuwaombea kheri.

Pindi alipokuwa akiyatembelea makaburi ya mashahidi wa Uhud alikuwa akisema, “Amani iwe juu yenu kutokana na yale mliyoyafanyia subira! Uzuri ulioje kwenu juu ya ardhi ya akhera!” (Tabari, Jamiul-Bayan, xm, 186; Ibn Kathir, Tafsir, II, 529)

Vile vile alikuwa akiyatembelea makaburi ya Baqi mara kwa mara; baada ya kuwatolea salamu waliokufa alikuwa akisema: “Amani iwe juu yenu enyi wakazi wa ardhi ya waumini! Mwenyezi Mungu akipenda na sisi tutakuja kuungana na nyinyi. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atujaalie ustawi na amani sisi na nyinyi” (Muslim, janaiz, 104)

Siku moja pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa amelala katika chumba cha Aisha katikati ya usiku aliletewa maagizo matakatifu na Jibril – amani iwe juu yake: Mwenyezi Mungu alikuwa akimuagiza ayatembelee makaburi ya Baqi na kuwaombea dua wale waliozikwa pale. Hivyo Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – akanyanyuka taratibu bila ya kutoa sauti ili asije akamuamsha Aisha. Lakini Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - alikuwa bado hajalala; na kutokana na shauku ya kutaka kujua alipokuwa anaelekea Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – aliamua kumfuata kwa siri. Baada ya kumuona Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anaingia makaburini na huku anatokwa na machozi kwa ajili ya ustawi wa wale waliozikwa pale, mara hisia zake za mwanzo za udadisi zikageuka







na kuwa aibu. Alisimama pale kwa muda huku akimuangalia Mtume aliyebarikwa – rehemu na amani ziwe juu yake – kwa mbali namna alivyokuwa akiomba. Kisha akarejea upesi kwenye chumba chake na kujifunika na kujifanya kana kwamba muda wote alikuwa amelala. Lakini kutokana na namna alivyokuwa akivuta pumzi kwa haraka kutokana na kukimbia kwake, Mtume aliyebarikwa – rehemu na amani ziwe juu yake – alielewa kilichotokea, hivyo akasikitika:

“Je ulikuwa unahofia kwamba Mwenyezi Mungu na Mjumbe wake wangeliveza kukukosea?” (Muslim, janaiz, 103). Kwa kusema vile pia alikuwa anaashiria kuwa mwenendo wake ulikuwa wakati wote unaangaliwa na Mola.

Simulizi lifuatalo limetolewa na Muadh ibn Jabal – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

*“Pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – aliponiagiza kwenda Yemen kuwa gavana alinisindikiza mpaka kwenye viunga vya mji wa Madina kwa ajili ya kuniaga. Nilikuwa pembezoni mwa kipando changu na yeye alikuwa pembeni yangu. Baada ya kunipa ushauri alisema:*

*“Huwezi jua ewe Muadh, unaweza usinione tena baada ya mwaka huu. Lakini labda utatembelea msikiti wangu na kaburi langu...”*

*Niliyaposikia maneno hayo ya utengano na yenye kuhuzunisha niligubikwa na machozi.*

*‘Usilie’, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehemu na amani ziwe juu yake – alinibembeleza. Kisha alisema yafuatayo huku akiwa ameyaelekeza macho yake Madina:*

*‘Walio karibu mno na mimi miongoni mwa watu ni wale ambao popote walipo wanashikamana na uchamungu wao kwa Mwenyezi Mungu’” (Ahmad, V, 235; Haythami, IX, 22)*

Dawud ibn Abi Salih anaelezea yafuatayo:

*“Siku moja Marwan alimuona mtu mmoja akiwa ameuweka uso wake kwenye jiwe la kaburi la Mtume – rehemu na amani ziwe juu yake. Akashika skafu ya shingoni ya yule mtu na kusema kwa hasira, ‘Unafikiri unafanya nini?’*



*Yule mtu akageuka nyuma; na hakuwa mwingine bali alikuwa ni Abu Ayyub al-Ansari – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Huku akimuangalia Marwan, swahaba yule aliyekuwa akiheshimika sana alisema:*

*“Ninalifahamu fika ninalolifanya. Nimekuja kumtembelea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na sio jiwe. Siku moja nilimsikia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akisema, ‘Msihofie juu ya majaliwa ya dini pindi mtu mweledi anapotekeleza majukumu yake. Lakini pindi Mtu asiye mweledi atakapoanza kushughulikia mambo ya dini hakuna hofu atakayohisi mtu wala machozi atakayotoa mtu ambayo yatatosha!’” (Ahmed ibn Hanbal, V, 422).*

Tukio lililopita ni la swahaba ambaye anapangusia uso wake kwenye jiwe la kaburi la Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – pindi alipomtembelea.

Si kwamba Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akitembelea makaburini mara kwa mara lakini pia aliwaasa maswahaba zake na waislamu wote wafanye kama yeye:

“Niliwakataza kutembelea makaburi. Lakini sasahivi mnaweza kufanya hivyo, kwani kuyatembelea makaburi kutawakumbusha juu ya akhera” (Tirmidhi, Janaiz, 60; Muslim, Janaiz, 106).<sup>17</sup>

Kuyatembelea makaburi hutoa mafunzo kwa watembeleaji na ni sababu aliyekufa kupata rehema; kwani maiti iliyozikwa hulilia kusaidiwa kama mtu aliyezama kwenye mchanga.

Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

“Siku moja Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alipopita karibu na makaburi mawili alisema yafuatayo kuhusiana na makaburi yale, ‘Wote wanaadhibiwa lakini si kutokana na dhambi ya aina moja. Mmoja anaadhibiwa kwa sababu ya kugombanisha watu na mwingine kwa sababu ya kutochunga mkojo wake wakati wa kukojoa.’

17. Wakati wa kipindi cha ujinga watu walikuwa wakijivuna na maiti wao kwamba maiti hawa wana daraja tukufu, na walikuwa wakitembelea makaburi yao kwa msingi huu. Ili kuondoa ushirikina huu mara ya kwanza Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikataza watu kuyatembelea makaburi. Lakini baada ya mabaki ya ushirikina huu kuisha kabisa aliamua kuondoa katazo lile na kuwashauri watu wafanye hivyo kwa lengo la kukumbuka kifo na si vinginevyo.





Hivyo akaomba aletewe tawi la kijani la mtende. Kisha akaligawa mara mbili na kuviweka vipande vyake katika makaburi yale kila moja, kisha akasema, ‘Inatarajiwa kwamba watapunguziwa adhabu kwa muda ambao matawi haya yatakuwa bado hayajakauka’ “ (Muslim, Taharat, 111).

Qurtubi ameifasiri *hadith* hiyo kama ifuatavyo:

“Maneno ‘muda ambao matawi haya yatakuwa bado hayajakauka’ yanaendana na ukweli kwamba huwa matawi yanamtukuza Mola kwa muda ambao bado ni ya kijani. Hivyo wanachuoni wamesema kwamba kupanda miti makaburini na kusoma Qur’an makaburini huleta faida kwa waliozikwa pale. Ikiwa kama hata kupanda mti tu kunapunguza adhabu ya maiti, nani ajuaye ni kwa kiasi gani atafaidika kutokana na kisomo cha Qur’an” (Qurtubi, Tafsir, X, 267).

Hasa kuisoma Surat Yasin ni njia inayotumika sana na kutekelezwa na watu wengi ili kumuwezesha maiti aweze kunufaika na rehema takatifu itokanayo na kuisoma Qur’an. Hadith inasema:

“Yasin ni moyo wa Qur’an. Kama mtu ataisoma kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu peke yake na kwa tamaa ya akhera, kwa hakika atasamehewa madhambi yake. Wasomeeni maiti zenu Yasin” (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, v, 26).

“Pindi mmoja wenu anapofariki msimcheleweshe kumzika. Na pindi mnapokuwa mmemzika mmoja wenu amsomee al-Fatiha upande wa kichwa chake na sehemu ya mwisho (aya mbili za mwisho) ya al-Baqara upande wa miguu yake” (Tabarani, al-Mucamu’l-Kabir, XII, 340; Daylami, Musnad, 1,284; Haythami, Majmau’z-Zawaid, III, 44).

Ala ibn al-Lajlaj ameripoti kwamba kabla ya baba yake ambaye ni swahaba kufariki aliacha wosia ufuatao:

“Pindi mtakaponiweka ndani ya kaburi semeni *Bismillah wa ala sunnati Rasu-lillah*<sup>18</sup> na kisha mnifunike kwa udongo. Upande wa kichwa changu nisomeeni al-Fatiha na sehemu ya mwisho ya al-Baqara. Mimi mwenyewe nilishuhudia hili likifanywa na Abdul-lah ibn Omar.” (Bayhaki, as-Sunanu’l-Kubra, IV, 56)

18. Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mtukufu na juu ya *sunnah* za Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake.





Hatuna budi kuzingatia wosia wa mwisho wa swahaba Amr ibn As – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

“Pindi mtakaponiingiza ndani ya kaburi subirini pembeni yangu kwa muda wa kumchinja ngamia na kukata nyama yake, ili uwepo wenu uweze kuimarisha moyo wangu ili uweze kuzoea maisha mapya na niweze kuandaa majibu nitakayotakiwa kuyatoa kwa wajumbe wa Mola wangu” (Muslim, iman, 192).

Imam Nawawi ambaye ameitaja *hadith* hiyo ndani ya kitabu chake anasimulia zaidi yafuatayo kutoka kwa Imam Shafii – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

“Kusoma sehemu ya Qur’an kaburini ni suala linaloshauriwa (*mustahab*). Lakini kuisoma Qur’an yote ni bora zaidi” (Nawawi, Riyadu’s-Salihin, 293)

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema yafuatayo kama ambavyo imepokewa na Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake:

“Maiti ndani ya kaburi ni kama mtu anayekaribia kugharikishwa na maji ya bahari, huwa anaogopa na anaomba msaada. Huwa anatarajia dua kutoka kwa baba yake, mama yake, watoto na marafiki zake wa karibu. Dua anayoisubiria huwa ni bora kwake kuliko dunia na vyote vilivyomo ndani yake. Bila shaka Mwenyezi Mungu huwapa wakazi wa makaburini thawabu mfano wa mlima kwa kupitia baraka za dua za walio hai. Zawadi bora ambayo mtu aliye hai anaweza kumpatia maiti wake ni dua kwa ajili ya msamaha juu yake na kutoa sadaka kwa ajili yake” (Daylami, Musnad, IV, 103/6323; Ali al-Muttaqi, XV, 694/42783; XV, 749/42971)

Imeripotiwa kutoka kwa Othman ibn Affan – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – kwamba pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipokuwa akimaliza kuzika alikuwa akisubiri pembezoni mwa kaburi na kusema:

“Muombeeni msamaha ndugu yenu na muombeni Mwenyezi Mungu amjaalie ayajibu kwa usahihi maswali atakayoulizwa ndani ya kaburi... kwani sasa hivi anaulizwa” (Abu Dawud, janaiz, 67-69/3221)

Jabir ibn Abdullah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:





*“Pindi Saad ibn Muadh – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipofariki tulienda pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – kwa ajili ya kutekeleza wetu wetu wa mwisho. Baada ya kuongoza swala ya maiti na kumzika ndani ya kaburi lake, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – aliendelea kuleta tasbihat kwa kitambo zaidi; na sisi tukafanya vile. Kisha Mtume wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akatoa takbir.*

*“Kwa nini ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu ulileta tasbih na kisha takbir?’, baadhi wa maswahaba waliuliza.*

*“Kabla ya Mwenyezi Mungu kulipanua kaburi hili, mwanzo lilimbana na kumbana zaidi mja huyu mwema’, alijibu” (Ahmad ibn Hanbal, ill, 360).*

Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

*“Siku ambayo Saad alizikwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – huku akiwa amesimama karibu na kaburi lake alisema:*

*“Kama kungelikuwa na mtu ambaye asingelitakiwa kujaribiwa kaburini”, kisha Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akaendelea, “kwa hakika angelikuwa ni Saad. Lakini kaburi lilimbana mpaka pale Mwenyezi Mungu alipolipanua.” (Tabarani, Mujam’ul-Kaabir, X, 334).*

Kama ambavyo tunaweza kuelewa kutokana na yaliyotangulia, kuyatembelea makaburi, kuwaombea msamaha waliozikwa ndani yake, kutoa sadaka kwa niaba yao na kuwasomea Qur’an ni sababu ya rehema kwa maiti. Ndani ya Qur’an Mwenyezi Mungu anatuagiza tuwaombe waumini ambao wametangulia mbele za haki kama ifuatavyo:

*“Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na ndugu zetu walio tutangulia kwa Imani, wala usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa walio amini. Mola wetu Mlezi! Hakika Wewe ni Mpole na Mwenye kurehemu” (al-Hashr, 10)*

Lakini pindi tunapoyatembelea makaburi hatuna budi kujichunga dhidi ya mambo yaliyozushwa (*bidah*). Ingawa wanachuoni wa kiislamu wamejitahidi kusema na kuandika mengi kwa ajili ya kuwalinda waislamu wasije wakajiingiza katika kuvuka mipaka na matendo mengine yasiyoruhusiwa pindi wanapotembelea makaburi, lakini yote hayo yamedhihirika mpaka leo.



Kusafisha utembeleaji wa makaburi dhidi ya kuvuka mipaka na matendo mengine maovu, suala lenye kuchanganya vichwa vya wale wenye elimu ndogo ya dini, ni suala gumu kueleweka. Kutokana na mwanadamu kushindwa kuelewa mambo magumu kwa wepesi kumepelekea suala la kutembelea makaburi kuwa kama *shirk*, angalau kulingana na baadhi ya watu shirki imekuwa ni katika kuwasha mishumaa na kuning'iniza vitambaa kwenye kaburi na kuomba msaada moja kwa moja kutoka kwa mtu aliyelazwa pale. Huu ni ubainifu wa kasoro sawa na wakiristo wanavyo-unasibisha uungu kwa Yesu – amani iwe juu yake - kutokana na kushindwa kumuelewa Mungu vilivyo. Kwa upande mwingine uvukaji mipaka huu umepelekea utembeleaji wa makaburi ulinganishwe na *shirk*.

Katika kuwaelewesha waislamu namna ya kuliendelea jambo hili uislamu umeweka kanuni ya katikati katika kutembelea makaburi. Kama ilivyokwihatajwa hapo kabla maneno na vitendo vya kufanya pindi tunapoyatembelea makaburi vimewekwa wazi na Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – na kufuatwa na Maswahaba, hivyo kuweka wazi njia sahihi ya kushikamana nayo wakati wa kutembelea makaburi. Hivyo kuepusha kuangukia kwenye uvukaji wa mipaka na makosa.

Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anaelezea:

*“Saad ibn Ubadah – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake - ambaye mama yake alikuwa amefariki muda si mrefu alikuja kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – na kuuliza:*

*‘Ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mama yangu alifariki wakati mimi nikiwa sipo. Je itamnufaisha yeye pindi nitakapotoa sadaka kwa niaba yake? Na pindi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake - alipojibu ‘ndio’, Saad alisema:*

*‘Basi shuhudia ewe Mjumbe wa Mwenyezi Mungu kuwa ninatoa bustani yangu ya matunda kwa jina la mama yangu.’” (Bukhari, Wasaya, 15)*

Abdurrahman ibn Abi Amra anasimulia kwamba mama yake alihidi kumuacha mtumwa huru usiku lakini aliahirisha mpaka kesho yake asubuhi. Lakini hakufanikiwa kufika asubuhi, alifariki usiku wake. Hivyo akaenda kwa Qasim ibn Muhammad na kumuuliza kama ingelimumfaisha mama yake pindi angelimuacha mtumwa huru kwa jina lake. Qasim akasema:





“Saad ibn Ubadah amewahi kumuendea Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na kumuuliza, ‘Mama yangu amefariki. Je itamnufaisha ikiwa nitamuacha huru mtumwa huru kwa jina lake?’ swali ambalo Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – alijibu ‘Ndio’”. (Muwat-taa, Itq, 13)

Abdurrahman ambaye ni mtoto wa Abu Bakr – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alifariki ghafla huku akiwa usingizini. Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alitoa sadaka nyingi kwa niaba ya kaka yake aliyefariki. (Muwattaa, itq, 13)

Ibn Abbas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – anasimulia:

*“Siku moja mtu alimjia Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – na kumuuliza, ‘Mama yangu amefariki wakati wa mwezi wa kufunga. Je ninaweza kufunga badala yake?’*

*Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema, ‘Kama mama yako angelikuwa anadaiwa, je usingelimlipia deni lake?’*

*‘Ningelifanya hivyo’, alijibu, kisha Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – akasema:*

*‘Mwenyezi Mungu anastahiki zaidi kulipwa deni lake’” (Muslim, Siyam, 155)*

Masimulizi mengine kama hayo yanamripoti Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akiuliza, “Kama mama yako angelikuwa anadaiwa na wewe ukamlipia deni lake, je hiyo ingelikuwa sahihi?” baada ya mtu yule kukubali kwamba ingelikuwa sahihi basi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – akasema, “Basi funga kwa ajili ya kufidia funga ya mama yako”. (Muslim, Siyam, 156)

Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – ambaye ndiye taa yetu yenye kutuongoza amesema:

“Matendo yote ya mja husitishwa pindi anapokufa isipokuwa matatu: Sadaka ambayo kwayo watu wanaendelea kunufaika (sadaqah-i jariyah), elimu yenye manufaa na mtoto mwema ambaye anawaombea wazazi wake.” (Mus-lim, Wasiyyah, 14)

Maneno haya yanaonyesha malipo ambayo muumini aliyefariki huvu-



na kutokana na sadaka aliyotoa wakati wa uhai wake na ambayo inaendelea hata baada ya kufa kwake, na cha zaidi ni kwamba anafaidika na dua na sadaka zilizotolewa na vipenzi vyake na ndugu zake walio hai kwa kumkusudia yeye.

Kwa hakika ni jambo muhimu kuendelea kutoa sadaka kwa niaba ya waislamu waliokufa na kuelekea akhera. Kulingana na *hadith* iliyotangulia kitabu cha matendo ya muislamu huwa hakifungwi ikiwa bado sadaka yake inaendelea katika maisha. Kutoa sadaka kwa niaba ya muumini aliyetangulia akhera ni miongoni mwa matendo mema ambaye warithi wake na marafiki zake wa kweli wataweza kuyafanya.

Kulipa madeni ya maiti peke yake ni jambo jema ambalo limependekezwa na Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – mwenyewe. Swali la kwanza ambalo Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alikuwa akiliuliza kabla ya kumswalia maiti lilikuwa ni kuhusiana na uwepo wa madeni kwa maiti, na baada ya madeni kushughulikiwa ndipo alipokuwa akimswalia maiti. Ni rehema iliyoje katika maelekezo haya kulingana na kurekebisha majukumu ambayo maiti aliyaacha.

Ukilinganisha na fidia anayotakiwa muislamu kulipa kwa ajili zile fungu alizoshindwa kuzilipa wakati ule na baadae kumempelekea Imam Muhammad kutoa hukumu (*ijtihad*) ijulikanayo kama *isqat-i salat*, hukumu ambayo warithi wa maiti ya kiislamu wanaweza kulipa fidia kwa ajili ya swala za faradhi alizoshindwa kuziswali katika maisha yake. Kulingana na hukumu yake fidia hiyo inaweza kulipwa kwa kila swala ya faradhi aliyoshindwa kuitekeleza; ama kumlisha masikini kwa kila siku au kutoa kiasi sawa cha pesa. Sadaka hii haina budi kupelekwa kwa masikini bila ya kupunguzwa chochote au kubadili kiwango kinachohitajika. Katika hukumu ya Imam Muhammad tunaweza kupata faida tatu:

- a) Kushawishi utoaji wa sadaka, jambo ambalo linampatia faida hata mtoaji.
- b) Huleta furaha kwa wahitaji na kupelekea wale waliopewa wamuombee dua maiti.
- c) Kutarajia rehema na msamaha wa Mola.







Lakini leo hii suala la *isqat*<sup>19</sup> limepelekwa mbali na malengo yake ya asili, jambo hili limebadilishwa na kuwa *dawr*<sup>20</sup>, jambo lenye kupingana na imani ya uislamu.

Suala la *dawr* limewekwa katika hali ya ulaghai. Jambo hili linaleta picha kuwa ibada fulani imelipiwa fidia kwa sadaka jambo ambalo kiuhalisia si kweli. Kinachofanyika ni kwamba kiasi fulani cha fedha kili-chokudusiwa kufidia deni la maiti juu ya swala za faradhi<sup>21</sup> alizoshindwa kuziswali wakati wa uhai wake kinawekwa katikati, kiasi kwamba badala ya kutolewa moja kwa moja kwa muhitaji, kinakuwa kinazunguka kati ya pande mbili; mtoaji kwenda kwa mpokeaji na kisha kinarudi tena kwa mtoaji kwa kujirudia rudia, na kwa kila mzunguko kile kiasi cha sadaka kilichokusudiwa huongezeka. Kumpa mpokeaji kiasi kidogo cha fedha kwa nia ya kukichukua na kisha kumpa tena na hasa pale wapokeaji wanapokuwa wengi kwa lengo la kuongeza kiasi hicho si chochote bali uzushi mbaya; na watu wanaohusika huwa wanajidanganya wenyewe. Cha kushangaza hasa ni namna matajiri wengi wanavyojiingiza kwenye utaratibu huu na kutarajia matokeo mazuri. Jambo hili si chochote bali upuuzi ambao kwa nje tu ni jambo lisiloingia akilini kwani ni mbinu ya kumlaghai Mola.

19. *Isqat* ni kumuondolea maiti mzigo wa madeni ya swala zake, funga zake, ahadi zake, n.k kwa kuwapatia masikini fedha kulingana na matendo hayo kama fidia. (Hayrettin Karaman, Ebediyet Yolcusunu Ugurlarken, uk. 81-85).
20. Kinyume na kuwapa fedha masikini, *dawr* ni kuweka kiasi fulani cha fedha kwenye kitambaa na kumpatia masikini ili naye akurudishie; na kasha mzunguko huu huendelea mpaka deni litimie. Utaratibu huu wa kizushi haukuwepo wakati wa Mtume aliyebariwa – rehemu na amani ziwe juu yake – wala maswahaba, wala wakati wa kipindi cha tabiin ambao walikuja baada yao. *Isqat* iliruhusiwa katika kipindi cha mwisho wa karne ya pili baada ya hijra, na *dawr* kuja baadae katika karne ya tano. Kuenea kwa *dawr* katika zama hizi kwa hoja kwamba imetokana na uislamu ni jambo baya lenye kushawishi ugumu na uvuvi katika utekelezaji wa amali njema. Kwa hiyo hatuna budi kuachana na desturi ya *dawr* na badala yake tutoe sadaka moja kwa moja kwa ajili ya maiti na kumuomba Mola amsamehe madhambi yake. Kwa namna hii tutakuwa tumetekeleza jambo la *sunnah* na wakati huo huo tutakuwa tumehakikisha kuwa sadaka inamfikia mhitaji. (Hayrettin Karaman, Ebediyet Yolcusunu Ugurlarken, uk. 81-85).
21. Madeni ya swala za faradhi hapa yanahusiana na zile swala ambazo maiti alishindwa kuziswali au zile alizoziswali bila ya kuzingatia masharti yake kama vile usafi wa moyo na utulivu. Na haya hayahusiki kwa njia yoyote ile na zile swala alizoziacha mtu kwa makusudi na kutarajia kuwa atalipiwa fidia.



**Ewe Mola! Jaalia nia zetu ziendane na radhi zako! Tulinde dhidi ya maangamizi ya wale waliopiga mbizi ndani ya dunia na matokeo yake kuzama ndani ya tope! Mola wetu, mwingi wa rehema! Yapambe na kuyajaza maisha yetu na vifo vyetu baraka, rehema, uzuri uliowapa waja wako wema na juu hayo yote tujaalie tuje kukutana na wewe!**

**Ewe Mola! Tujaalie tuutazame ulimwengu kwa jicho la mapenzi matakatifu, tuutazame kwa hisia na utambuzi wa kiroho; kwa hofu ya utambuzi na furaha ya imani...Na tujaalie tuufanye uwe moshi wa rehema mbele yako kwa kupitia machozi ya majuto ambayo yanatiririka kutoka machoni mwetu, kwa jina safi na amani ya moyo!**

**Amin...**





---

# SURA YA TANO

---

**Ushauri kutoka kwa  
watu wema**





"Tambua"



**T**ahadhari na ushauri wa watu wema vinatokana  
na Qur'an na maneno ya Mtume.



## Ushauri kutoka kwa watu wema

Waja wema wa Mola ambao wamefikia kwenye daraja la ukamilifu katika elimu ya dhahiri na ya siri kwenye mwenendo wa kisufi, ni wale waliobahatika kupokea heshima ya kuwa 'warithi wa Mitume'. Wao ni mfano wa mwenendo bora wa kiutumbe na uongofu uliosambaa katika nyakati zote. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba wao ni viongozi kwa ajili ya wale wasiobahatika kuishi katika zama za Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake - na maswahaba zake. Hadith inasema:

“Wanachuoni (walio na ukamilifu wa ndani na nje) ni warithi wa Mitume.” (Abu Dawud, Ilm, 1).

Kutokana na kuwa kwao wapokezi wa ubainifu mzito wa majina matakatiifu ya Mwingi wa rehema na Mwenye kurehemu, huruma na upole huwa sehemu ya tabia zao. Kutokana na kujifungua kwao pingu za nafsi ambazo huwapelekea kutothamini kingine chochote zaidi ya nafsi, waja hawa waliokomaa wanakuwa wamefikia kwenye ukarimu usio na mwisho, hivyo kumfikiria kila mtu badala ya nafsi zao. Hivyo maisha yao ambayo wameyatoa kwa ajili ya kuwaongoza wengine huendelea hata baada ya kufa kwao. Matokeo ya kuzidhibiti nafsi zao huwapelekea kuwa madaraja ya kuwafikisha wao na umma wote kwa Mola ambaye ndiye wanayetafuta uongofu wake. Wao ni waalimu wa watu wote wanaosubiria kuokolewa, pia ni mashujaa ambao wamebeba jukumu la kuwaongoza watu wamuelekee Muumba wao.

Tahadhari na ushauri wa watu wema vinatokana na Qur'an na maneno ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake; kwani yeye ni kitovu cha





munufaa ya kiroho. Maneno yao, tahadhari zao na ushauri wao wa kiimani ni cheche zitokazo kwenye kitovu hicho. Hivyo ni muhimu kushikamana na mikusanyiko ya watu wema; kwani wanawakilisha miaka ishirini na tatu ya utume wa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake, katika maneno yao, matendo yao na hisia zao.

Mtakatifu hupukutisha uwezo wake katika kumpenda Mola kama nondo anavyouzunguka moto bila ya kujizuia, hivyo Mola anakuwa macho yake yanayoona na masikio yake yanayosikia. Kwani wakati wote yupo chini ya ubainifu wa mapenzi na upole wa Mola, nafsi yake huungua kama karatasi inavyoangua chini ya lenzi iliyomulikwa mwanga wa jua. Hivyo anakuwa kitovu cha mapenzi kwa wengine ambao wanamfuata. Maonyo na ushauri wake huwa kama tiba ya nyoyo zilizojeruhiwa.

Maonyo na maneno ya ushauri yanayotoka kwenye vinywa vya watu wema ambao wamefikia kwenye upeo wa juu ya kiimani yana thamani kubwa na ushawishi mkubwa katika kutuma wito wa kuamsha nyoyo za wajinga, tofauti na ule ushauri wa wale wasiotenda yale wanayoyasema. Hivyo kila mtu hana budi kuthamini ushauri wao mwema kama hazina iliyopotea na kila mtu hana budi kuyafuata maneno yao kwa mapenzi na moyo safi. Ifuatayo ni mifano kadhaa kutoka kwenye ushauri wa watu wema, mifano ambayo inatoa mwangaza mzuri katika njia ya furaha ya milele:



### **Hasan Basri - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (642-728)**

Mwana wa Adamu! Muumini wa kweli huamka asubuhi akiwa na hofu, hata kama ni mtu wa ihsan. Hili linamfaa kwa namna yoyote ile. Muumini huamka tena usiku unaofuata kwa hofu. Wakati wote huwa kati-kati ya hofu ya vitu viwili:

1. Madhambi yaliyopita: Kamwe hawezi kuwa na uhakika kuwa Mola atamfanya nini kutokana na madhambi hayo.

2. Maisha yajayo: Aishi vipi na atakufa vipi? Wakati wote hutafakari juu ya majibu ya maswali haya ambayo hana majibu yake.

Wanadamu! Qur'an ni tiba kwa waumini, muongozo kwa watu wema.





Yeyote atakayeifuata ataongozwa katika uongofu na katika njia iliyonyooka. Yeyote atakayeipa mgongo ataishia kwenye maangamizi.

Mwana wa Adam! Utakufa peke yako, utafufuliwa peke yako na utahesabiwa peke yako!



**Malik ibn Dinar - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (alifariki 748)**

Hakuna tena raha katika ardhi isipokuwa katika vitu viwili:

1. Kukutana na kuzungumza na ndugu.

2. Kuamka kwa ajili ya swala ya tahajjud na kugubikwa na utajo mtakatifu na kuisoma Qur'an wakati huo wa usiku.



**Jafar-i Sadiq - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (699-766)**

Zifanye siri amali zako njema na zifanye siziwe na thamani machoni mwako; kwani kama utazichukulia kuwa hazina thamani, hazitokupelekea kwenye kujivuna. Na kama utazifanya kuwa siri zitarekebisha kasoro zake na kuongeza thamani yake. Kwa kuharakisha kufanya amali njema utaweza kuzifikia bila kuchelewa. Kinyume chake nafsi yako inaweza ikadhoofika na kukufanya uahirishe; au kuachana nazo kabisa, jambo ambalo ni baya zaidi.

Kama utasikia jambo baya kuhusiana na ndugu yako, jitahidi kujishawishi kuwa lazima atakuwa na nyudhuru. Na kama utashindwa kupata nyudhuru basi chukulia kwamba nyudhuru ipo kwa namna ambayo huwezi kuielewa na hivyo jitahidi kuficha kasoro yake!



**Sufyan-i Sawri - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (713-777)**

Kutafuta elimu kuwa kwa lengo la kupata uchamungu juu ya Mwenyezi Mungu, kutekeleza maamrishi Yake na kumuogopa Yeye. Ubora wa elimu unatokana na uwezo wake wa kumfanya awe na hisia hizi. Yakikosekana malengo haya elimu itakuwa katika daraja lisilofaa.



Kwenda Khorasan kwa ajili ya kufikisha daawa ni bora kuliko kuishi karibu na mji wa Makka.

Sharti la kwanza la elimu ni kutafuta njia za kuipata elimu hiyo. Pindi itakapokuwa imepatikana na kuchukuliwa, matendo hufuatia...na kisha ukimya na tafakari...na baada ya hapo kinafuata kuutazama ulimwengu kwa kupitia jicho la hekima.



**Junayd Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (alifariki 909)**

*Sohbah* pamoja Mwenyezi Mungu, yani kuwa pamoja Naye, inatokana na mwenendo mzuri na muendelezo wa mtazamo bora.

*Sohbah* pamoja na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – inatokana na kushikamana na *Sunnah* yake.

*Sohbah* pamoja na watakatifu inatokana na heshima na huduma.

*Sohbah* pamoja na familia inatokana na maadili mazuri.

*Sohbah* pamoja na ndugu inatokana na kutabasamu na kuwachangamkia wakati wote.

Na *sohbah* pamoja na jamii inatokana na dua na huruma.



**Imam Ghazzali - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (alifariki 1111)**

Ewe mwanangu, uhuishe moyo wako kwa hizi amali tatu za ibada; Usiuruhusu moyo na akili yako ikaelekea mahali pengine pindi usomapo Qur'an, pindi umtajapo Mola wako na pindi utekelezapo ibada ya swala. Pindi ushikamanapo na amali hizi tatu usiuruhusu moyo wako na akili yako vikaelekea sehemu nyingine hata kwa kitambo kifupi. Usisahau kuwa upo mbele ya Mwenyezi Mungu! Kama utaruhusu akili yako ihame wakati uso wako umeelekea *qiblah*, thamani ya unachokifanya itapungua. Uelekeze uso wako kwenye Al-Kaaba ambayo ndiyo ndilo hekalu la kwanza ambalo uislamu ulizaliwa juu yake, na ufunge vyema moyo wako pamoja na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Na kama unataka kuungana na watu wenye hekima







kijaze kimya chako kwa tafakari, ufanye mtazamo wako uwe ni kwa ajili ya kupata mazingatio na fanya tamaa yako iwe ni kufanya ibada. Sifa hizi tatu ndizo alama za watu wenye hekima.

Jichunge dhidi ya kuvunja haki za wengine! Hata deni dogo mno huweza kuzuia amali nyingi za ibada zisilipwe! Kamwe Mtume aliyebarikwa – rehemu na amani ziwe juu yake – hakuwa anamswalia maiti ambaye deni lake halijalipwa. Lengo lake lilikuwa ni kuwafanya matajiri waingiwe na huruma na hivyo kuwafutia maiti madeni yao. Lakini Mwenyezi Mungu Mtukufu humsaidia yule mwenye kukopa kutokana na shida iliyomfika kwa lengo la kulipa hilo deni. Hata kama atafariki huku akiwa katika jitihada za kulilipa deni hilo bila ya mafanikio, Mwenyezi Mungu atamsaidia kesho akhera.

Mwanadamu hana budi kumshukuru Mola kwa Majaribu; kwani licha ya ukafiri na madhambi lakini hakuna majaribu ambayo hayaji na wema ambao haufahamiki. Mwenyezi Mungu anajua kilicho bora kwako zaidi ya wewe ujuavyo! Kuna vitu vingi ambavyo unavichukulia kuwa vibaya wakati ni vyenye heri kwako. Na kuna vitu ambavyo unavichukulia kuwa ni vizuri wakati ni vyenye shari kwako. Upande salama zaidi ni kuridhika kwa kila litakalokufika na kushukuru bila ya kujali upo katika hali gani.

Mwanangu...Kama kungelikuwa na kitu cha kuwa makini nacho zaidi kingelikuwa ni kuwa makini na mtu unayefanya naye urafiki. Fahamu kuwa kikapu kilichojaa matufani yaliyoiva vizuri hakiwezi kuligeuza tufani moja lililooza na kuwa zuri; na vilevile tufani moja lililooza haliwezi kuoza matufani mengine. Hivyo wakati wote fuatana na watu wema!

Rafiki mzuri ni kama mtu anayeza mafuta ya waridi; ama utanunua kutoka kwake au atakupatia kidogo, au angalau atakupangusia mafuta hayo hali ya kuwa utakuwa karibu yake. Mtu huwa pamoja na yule anayempenda. Siku ya kiama utafufuliwa pamoja na yeyote uliyekuwa ukimpenda na kufanya urafiki naye hapa ardhini. Hivyo shikamana na kufuatana na wanachuoni na watu wema ambao wanaifanyia kazi elimu yao!

Mwanangu, kila kitu katika maisha kimepangwa na Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu amewafanya baadhi kuwa matajiri na wengine masikini, baadhi wenye afya na wengine madhaifu, baadhi wajuzi na wengine wajinga. Hii ndiyo njia pekee ya kuleta utulivu katika dunia. Pindi unapowaona watu walio chini yako usiwe jeuri na kuwatenga! Kwani





ungeliweza kuwa katika nafasi yao na wao wakawa katika nafasi yao. Lifikirie hili na ufanye urafiki na masikini! Jitahidi kukaa nao kwa upole! Linda heshima ya kuwa mwanadamu na muislamu! Hii ndio njia pekee ya kukupelekea kwenye furaha. Kama unataka amani hapa duniani na kesho akhera basi usimfanyie mtu yeyote kitu kibaya! Pindi umuonapo kijana, jiambie mwenyewe ‘ana madhambi machache kuliko yangu’; na pindi umuonapo mtu aliyezeeka, jiambie ‘ana thawabu nyingi kuliko mimi na ni mwema kuliko mimi kwa namna ambayo siifahamu’. Watazame kwa fikra hizi! Pindi umuonapo mwanachuoni jifikirie kwamba ‘ana elimu ambayo itamuokoa’; na pindi umuonapo mjinga fikiria kwamba ‘atasamehewa kwa lile asilolifahamu!’ Hata pale unapomuona kafiri fikiria kwamba ‘kama Mwenyezi Mungu atamjaalia uongofu basi atasamehewa madhambi yake yote na ataenda mbele ya Mola kama kinda la njiwa...lakini ni nani ajuaye nitakuwa katika hali gani katika pumzi yangu ya mwisho?’ na hivyo tafakari juu ya mwisho wako! Kadiri unavyojifahamu mwenyewe na kadiri unavyojitazama mwenyewe ndivyo daraja lako mbele ya Mola linavyopanda.

Wasaidie ndugu zako katika dini ewe mwanangu kwa kadiri uweza-vyo; kwani Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

“Yeyote atakayemkidhia haja ndugu yake katika dini, Mwenyezi Mungu atamkidhia haja zake.” (Bukhari, Mazalim, 3).

Na katika hadith nyingine Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – amesema: “Yeyote atakayesitiri aibu ya muislamu mwenzake, Mwenyezi Mungu atasitiri aibu zake hapa duniani na kesho akhera.” (Muslim, Birr, 72).

Mtu mwenye busara anapaswa kujiambia yafuatayo: Mtaji pekee nilionao ni uhai wangu; sina kingine. Mtaji huu ni wenye thamani kubwa mno kiasi kwamba kila pumzi inayotoka ndio imeenda, hairejei tena. Pumzi zina idadi maalum na kila wakati zinapungua. Hivyo wekeza katika kila pumzi na chukulia kana kwamba utakufa kesho. Kilinde kila kiungo chako dhidi ya madhambi na shikamana na uchamungu!

Mola wangu...Tujaalie tuwe na mwisho wenye furaha! Tujaalie tupate radhi zako na sura yenye ufahari (*jamal*)! Usituondoshee ustawi, usiku au mchana! Tujaalie uchamungu na uzielekeze imani na matarajio yetu Kwako! Tujaalia msimamo katika njia ya haki! Wewe pekee ndiye unayestahili kuabudiwa! Ninakutukuza dhidi ya upungufu wa aina yoyote ile!





Mimi ni miongoni mwa wale waliozidhulumu nafsi zao kwa kushindwa kukutumikia kwa namna unavyostahili Utukufu Wako!

Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu wote; na salamu na amani ziwe juu ya Muhammad Mustafa ambaye ndiye fahari na furaha ya ulimwengu!



**Abdulqadir Jilani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (1077-1166)**

Mwanangu! Uchamungu ndio unaouhitaji. Jitahidi kukamilisha masharti ya uchamungu ili moyo wako utakasike dhidi ya utatanishi wa ndani na tabia mbaya...na uwe umeshikamana na wema.

Wakati unapata mazuri ya dunia usiwe kama yule anayeokota kuni katika giza la usiku bila ya kuwa na uhakika juu ya kile anachokiokota. Tahadhari ikiwa jambo fulani linaruhusiwa au haliruhusiwi, ni halali au haramu. Jaalia jua la *tawhid* na uchamungu viangazie kwenye matendo yako yote.

Mwanangu, kama utaiweka Qur'an kwenye matendo, itakuinua mpaka kwenye daraja la Qur'an; na kukuinua mpaka kwenye kiti chake cha enzi. Na kwa upande mwingine, kuifanyia kazi Sunnah kutakufanya uwe karibu na Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake, Mjumbe ambaye msaada wake wa kiroho utakuhakikishia kuwa hautengwi na nyoyo za watakatifu hata kidogo. Yeye ndiye anayeziimarisha nyoyo za watakatifu.

Chakula cha haramu huua moyo ewe mwanangu, wakati chakula cha halali huufufua. Kuna matonge ya chakula ambayo yatakufanya ushikamane na dunia na mengine ambayo yatakufanya ushikamane na akhera. Pia kuna mengine ambayo yataelekeza tamaa yako kwa Muumba wa mbingu na ardhi.

Mwanangu...Kuwa rafiki wa yule anayekusaidia kupambana na nafsi yako! Fuatana naye! Usiwe rafiki wa yule anayechochea matamanio ya nafsi yako! Kwanza kabisa idhibiti nafsi yako; jinufaishe mwenyewe na kuinyoosha nafsi yako...na kisha shikamana na wengine. Usiwe kama mshumaa ambao unaangazia sehemu wakati wenyewe unayeyuka!



Ewe ambaye unatarajia kufanya matendo mema katika njia ya Mwenyezi Mungu! Kuwa na moyo safi! Kinyume chake utakuwa umejichosha bila ya kupata chochote.

Watu hawaongolewi kwa maneno matupu; bali kwa imani ya kweli na shauku ndani ya moyo. Yote haya hupatikama kwa kupitia kujitenga, ibada, utajo mtakatifu, kujizuilia na maovu na tafakari. Kinyume chake hakutakuwa na matokeo mazuri ambayo yataweza kumnyanyua mtu kiimani. Ulimi na moyo, maneno na dhati na nje na ndani ya muumini aliye katika njia ya Mola havina budi kuwa vimoja na kupaza sauti moja.



#### **Ahmed ar-Rifai - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (1118-1182)**

Marafiki...Jaribu kuwa karibu na waja wema wa Mola; kwani kumpenda mja mwema ni kumpenda Mola na kumfanyia uadui ni kumfanyia uadui Mola.

Endelea na *dhikr* ya Mola; kwani *dhikr* ni sumaku ambayo inakuvuta kwake, na ni kamba imara inakuunganisha naye. Wale ambao wanaendeleza utajo wao mtakatifu wana hali nzuri pamoja na Mola; na yeyote aliye katika hali nzuri na Mola wake anakuwa yupo pamoja naye wakati wote. Dhikr hutulia moyoni kwa kupitia baraka za sohbah, kwani mtu huwa katika njia moja na rafiki yake na hupelekwa popote pale njia ile inapoelekea.

Tafakuri ilikuwa ndio amali ya kwanza ya Mtume Mtukufu – rehemu na amani ziwe juu yake. Kabla ya hapo hakukuwa na matendo ya lazima, ibada zake zilihusiana na kutafakari juu ya uumbaji na baraka za Mwenyezi Mungu. Hivyo shikamana na tafakuri na ifanye iwe njia ya kuimarisha imani yako.

Kuwa makini usiwe kama chekeche ambalo linaruhusu sehemu nzuri ya unga kupita na kuacha makapi. Msiruhusu nyoyo zenu zikajawa na uongo na uovu wakati maneno ya hekima yanatiririka kutoka kwenye ndimi zenu, kinyume na hayo aya isemayo **“Je! Mnawaamrisha watu mema na mnajisahau nafsi zenu, na hali nyinyi mnasoma Kitabu? Basi je, hamzingatii?”** (al-Baqarah, 44) itawashitaki.

Zisafisheni nyoyo zenu kikamilifu, kwani usafi wa moyo ni muhimu





zaidi kuliko usafi wa nguo. Hata hivyo Mwenyezi Mungu hutazama moja kwa moja kwenye moyo wa mtu, na si mavazi yake. Jichunge na mipaka ya usawa na usimtafute mwingine yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu.

Marafiki...Mlango uko wazi kwa yule mwenye kuugonga kwa unyenyekevu na utulivu; na anaruhusiwa kuingia ndani. Yule atakayeingia na huzuni atakaribishwa kwa heshima.



### **Abdulkhaliq Gujdawani - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (alifariki 1189)**

Mwanangu...Wosia wangu ni kwa wewe kuongozwa na elimu, mwenendo mwema na uchamungu katika mambo yote! Soma maneno ya watu waliopita na ufuate njia ya *Ahl-i Sunnah wa'l-Jamaah!*. Jifunze sheria (*fiqh*) na *hadith* na uhome ujinga na ukaidi! Hakikisha unawali swala za faradhi katika jamaa! Jitenge na umaarufu kwa kadiri uwezavyo; kwani umaarufu huja na balaa. *Usitamani vyeo vya watu na wakati wote jishushu! Usichukue jukumu lililo nje ya uwezo wako! Usiingilie mambo ya watu ambayo hayakuhusu!* Usijihusishe na watu wakaidi! Kua na uwiano sawa katika mambo yako yote! Usivunje uwiano huo na kugeuzia masikio yako kwenye sauti zenye kuvutia zisizo na umuhimu, kwani sauti hizo hudhoofisha moyo na kuzaa unafiki ndani yake! Lakini usikatae kabisa sauti zenye kuvutia, kwani wito wa adhana na kisomo cha Qur'an vinahuisa moyo.

Kula kidogo, ongea kidogo na lala kidogo; na wakimbie wajinga kama paa anavyomkimbia simba! Tafuta uswahiba wakati wa dhiki na kaa mbali na wanachuoni ambao wanapitisha hukumu kwa ajili ya maslahi yao na kwa kufanya hivyo wakaweza kuidhoofisha dini kwa kupitia matajiri wenye kiburi na wajinga! Kula chakula cha halali tu, jiweke mbali na vitu vyenye mashaka na weka mbele uchamungu katika ndoa yako! Kinyume chake utaikumbatia dunia na kujiangamiza mwenyewe!

Usicheke sana; hasa kuwa makini usiwe na kicheko cha chini kwa chini! Kwani kucheka sana kunaua moyo. Lakini usijitenge kabisa na tabasamu.

Muangalie kila mtu kwa huruma; usimdharau mtu yeyote. Usifanye mambo kwa ajili ya kuonyesha wasifu wako wan je, kwani wasifu wa nje



huficha maangamizi ya ndani. Usijihusishe na mabishano. Usiombe chochote kutoka kwa mtu yeyote; ridhika na ulichonacho na fanya kuridhika kwako kuwe ndio utajiri wako. Linda utu wako!

Endeleza utii wako kwa wale waliochangia katika maendeleo na mafunzo yako. Wahudumia kwa hali na mali na shirikiano nao katika shida! Wakashifishaji wao kamwe hawatapata amani! Usiiegemeo dunia na wajinga ambao wanafanya jitihada kwa ajili ya dunia!

Wakati wote moyo wako utakuwa laini na mnyenyekevu, mwili wako utakuwa tayari kutekeleza jukumu la utumishi na macho yako yatakuwa ni yenye kutoa machozi. Mola ajaalie matendo yako yawe mema, maombi yako yawe ni ya kutafuta ulinzi, mavazi yako yawe ya staha, watu wema wawe rafiki zako, elimu ya dhahiri na ya kificho iwe kwako na msikiti uwe nyumba yako!



#### **Fariduddin Attar – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (1119-1220)**

Kubali msamaha wa wale wanaokuudhi. Mwenyezi Mungu hampendi yule anayewaudhi watu. Sifa hiyo haimfai mtu wa dini. Kuumiza moyo wa mwingine kwa dhuluma ni sawa na kuumiza moyo wako mwenyewe. Yule mwenye kuweza kutambua kasoro zake huwa anakuwa ana uwezo fulani katika moyo wake.

Dalili za upumbavu ni kuchunguza kasoro za wengine bila ya kuanzalia kasoro zako mwenyewe...na kutarajia ukarimu wakati umepanda mbegu za ubakhili ndani ya moyo wako.

Yule asiyewaridhisha watu kwa kupitia maadili yake hana thamani mbele ya Mola.

Watembelee wagonjwa, kwani huo ni mwenendo wa Mtume. Kama unaweza mkidhie mtu kiu chake kwa maji. Wahudumie watu katika mikusanyiko. Wahudumie yatima ili Mwenyezi Mungu akufanye uheshimike. Fahamu kuwa kilio cha yatima, hata kama ni nusu sekunde, hutikisa kiti cha enzi. Dhalimu ambaye anamliza yatima atakuwa kuni za Moto wa Jahannam. Yule mwenye kumpa yatima furaha anakuwa amefungua milango ya akhera kwa ajili yake.





Chochote unachokitoa katika njia ya Mwenyezi Mungu ndicho chako. Kwani kwa vile vilivyobakia utaulizwa juu yake.



**Muhyiddin Ibn Arabi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (1165-1240)**

Kama utauzoesha moyo wako kumkumbuka Mwenyezi Mungu, basi moyo wako utapata utambuzi unaotokana na nuru ya *dhikr*. Nuru hiyo ndiyo inayofungua macho ya moyo.

Kaa na waja wa Mwenyezi Mungu kwa huruma na upendo. Tawanya huruma yako kwa viumbe vyote. Usiseme, 'haya ni magugu tu, hayana uhai wala manufaa'. Ukweli ni kwamba wana manufaa ambayo wewe huyatambui. Kiache kiumbe na kuwa na huruma juu yake, kwani Mola wake anakihurumia pia.

Usimrudishe mtu yeyote mikono mitupu. Mtulize hata kwa maneno mema na umfanyie wema. Fikiria kwamba siku moja utakutana na Mola.

Usikubali mtu yeyote akakufanya mtumwa kwa kipande cha mng'ao wa kidunia. Wewe ni mja wa Mwenyezi Mungu pekee, Mwenyezi Mungu ambaye amekubali uwe mja wake.

Onyesha upendo kwa waja wema wa Mwenyezi Mungu kwa kuwalisha na kuwakidhia haja zao. Tambua kwamba katika umoja wao waumini wote ni kama mwili mmoja.

Jizoeshe kuwa katika jamaa. Jaribu kutoa machozi kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu. Shikamana na kamba ya Mwenyezi Mungu na fanya mambo yanayomridhisha Yeye.



**Mawlana Rumi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (1207-1273)**

Mwenyezi Mungu Mtukufu amewatuma Mitume na watakatifu kuja hapa duniani kama rehema. Ndio maana wakati wote wanawashauri watu bila ya kuchoka. Na kwa wale wanaoziba masikio yao dhidi ya mawaidha yao, huwaombea, 'Ewe Mola, wahurumie watu hawa, na usifunge milango ya rehema katika nyuso zao!'

Chunga matendo yako na uzingatie mawaidha ya watakatifu! Wasikilize



ili uokolewe kutokana na hofu; na uwe katika amani na usalama wa kiroho!

Tambua kwamba adabu ya kiroho ni kama imani inayotulizana ndani ya mwili. Kwa watakatifu, hiyo ni nuru ya jicho na moyo. Kama unataka kukiponda kichwa cha shetani, tambua kuwa hii ndiyo silaha unayohitaji.

Fungua macho yako na uitazame Qur'an ambayo ni maneno ya Mwenyezi Mungu, kuanzia juu mpaka chini! Kila aya yake inamfundisha na kumfunza mtu katika maadili ya kiroho.

Toa kila ulichonacho, mwili wako, roho yako na mali zako kwa ajili ya moyo wako uliokabatiwa! Ukarabati moyo ili uweze kutoa mwangaza ndani ya giza kubwa la kaburi.

Kuwa pamoja na watu wema hata kwa kitambo kifupi tu kuna thamani kubwa kuliko hata kipindi chote cha maisha yako. Unywele unaodondoka kutoka kwake ni wenye thamani kama lulu. Lakini kuna watu walio kinyume na hayo, watu ambao kukaa kwao mbali na watu hawa ni bora zaidi kwao kuliko utajiri wote wa hapa duniani.

Niluambia moyo wangu, 'Usipendeele kuwa mbele, na badala yake kuwa mwenye ukarimu. Usiwe mwiba wenye kuchoma. Kama hutaki kudhuriwa na yeyote basi usiwe mtu mwenye kuongea, kufikiria na kufundisha uovu. Jitahidi kufanya matendo mema bila ya kujali upo katika hali gani.



**Ibrahim Dasuki - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – (alifariki 1277)**

Unachohotaji mwanangu ni dua za watakatifu; hitajio la kuwa chini ya msaada wao wa kiroho ni kwa faida yako.

Wewe ambaye umeisoma na kuihifadhi Qur'an usijisifu kuwa umefanikiwa! Badala yake jiangalie: Je unaweza kuifanyia kazi kwa ufanisi au la?

Mwanangu! Kuwa mkimya na jizuia kujihusisha na maneno ya kipuuzi na mabishano yasiyo na maana! Chagua usafi wa moyo na usiisikilize nafsi yako wakati wa kutekeleza matendo mema kwa moyo safi!

Ongozana na yule aliyekusanya kwa pamoja Sheria (*Shariah*) na haki (*haqiqah*) katika mambo yake. Kamwe usisahau kwamba watu hao ndio watakaoweza kukusaidia mno katika njia hii!







Ninatamani ewe mwanangu uwe ni mwenye kushikamana na Sunnah wakati wote na kujipamba na maadili ya kiroho ambayo ni muhimu sana!

Huna budi kuwa mwerevu! Usiwe muoga ambaye anakwepa hata kivuli chake mwenyewe! Vumilia hata kama utapata tabu kiasi gani!

Jaza mapenzi ya Mola wako ndani ya moyo wako; kuwa naye hata wakati wa raha.

Kama unatafuta watu wa kuwateta wachague wazazi wako; kwani wao wanastahili zaidi kukuchukulia malipo ya matendo yako mema kuliko mtu mwingine yeyote.

Mwenyezi Mungu Mtukufu huzitazama nyoyo za waja wake mara sabini na mbili kila siku. Hivyo ufanye moyo wako uwe safi na wenye kung'aa; kwani ndipo mahali panapoangaliwa na Mola.

Usijidanganye ewe ndugu kwa kufikiria kuwa umefanikiwa katika jambo fulani kwa juhudi zako binafsi. Pindi unapofunga, Mwenyezi Mungu ndiye aliyekufanya ufunge; na pindi unaposwali, Mwenyezi Mungu ndiye aliyekufanya ufanye hivyo. Hivyo ndivyo ilivyo kwa amali zako nyingine. Kama umefikia katika daraja la uchamungu au kama umejaaliwa kupata chochote, kiroho au kitu chenye kushikika, ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu amejaalia ukipate kitu hicho.

Jichunge na kusema 'Mimi' ewe mpendwa, hata kama umefanya matendo mema mengi sawa na matendo ya wanadamu wote na majini. Kwani Mwenyezi Mungu huwadunisha wale waliojiona wao ni bora zaidi ya wengine! Jambo hili daima hushusha daraja la kiroho la mtu...wakati wote liweke kichwani jambo hili!



### **Bahaaddin Naqshiband - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (1318-1389)**

Njia yetu ni njia ya uongofu kama ilivyoonyeshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu; hiyo ni njia iliyoambatana na kushikamana na Sunnah na kuwafuata maswahaba. Hivyo njia yetu inazaa malipo makubwa katika muda mfupi.

Njia yetu ni ile ya *sobah* na upendo, kama ilivyokuwa njia ya maswa-



haba. Wema na baraka zinapatikana katika kuwa pamoja na kuwa pamoja kunapatikana kwa kupitia *sohbah*. Utengano unatokana na hatari ya umaarufu; na umaarufu ni janga.

Wale wenye kusafiri katika njia yetu hawana budi kuwa na vitu vitatu:

Cha **kwanza** ni kufuata utaratibu aliouweka Mwenyezi Mungu Mtu-kufu; yani hawana budi kuzama katika utii, nje na ndani. Hawana budi kutekeleza maamrishi yote ya Mwenyezi Mungu na kujiweka mbali na makatazo Yake; na kuondoa kila kitu ndani ya moyo isipokuwa Mwenyezi Mungu, hawana budi kufanya mambo yao bila ya kutoka kwenye njia Yake.

Cha **pili** ni kumfuata Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Huku ni kumfuata yeye na kumpenda katika mambo yako yote.

Cha **tatu** ni kuwatii watu wema ambao wamekufungua macho.

Hakuna wema unaopatikana katika chakula kilichoandaliwa au kupatikana kwa ujinga, bila ya kujitambua au kwa hasira; kwani shetani na nafsi hupata nafasi ndani yake. Kama kitaliwa basi kitaleta madhara yanayoweza kuharibu mfukumo na amani ya kiroho. Wema hupatikana katika chakula kilichoandaliwa na kuliwa bila ya ujinga na kikiwa katika fikra za Mwenyezi Mungu. Sababu inayowapelekea watu washindwe kukusanya nguvu ya kutosha ya kufanya wema na matendo mema ni kwa kuwa hawako makini katika kujihadhari na haramu, mambo yenye kutia mashaka na haki za wengine katika kula na kunywa. Vyovyote iwavyo lakini ukweli ni kwamba kuwa na amani na utulivu wakati wa swala na kuiswali kwa unyenyekevu na upole kunategemeana na kula chakula cha halali, kukiandaa kana kwamba unakiandaa huku ukiwa mbele ya Mwenyezi Mungu na kukila kana kwamba unakila mbele ya Mwenyezi Mungu. Mwili ulio-stawishwa kwa chakula cha haramu hauwezi kupata raha wakati wa swala.

Maneno ya Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – yasemayo, “Swala ni kupaa kwa muumini” (Suyuti, Sharhu ibn Majah, i, 313) yana-husika na swala iliyo sawa. Pindi mtu anapotamka takbira ya kufungulia swala hana budi kuwa katika hali ya utulivu na hisia za kuwa mbele ya Mola, na kufikiria juu ya utukufu wa Mola. Hana budi kuboresha hali hii kiasi cha kupoteza uhibitibi binafsi (*istighraq*). Kilele chake kimedhihirika kwa kipenzi wetu Mtume – rehema na amani ziwe juu yake.

Ukweli wa kusema ‘hakuna Mungu isipokuwa Allah’ ni kutoruhusu kitu kingine chochote tofauti na Mwenyezi Mungu kutawala ndani ya





moyo. Kutii sheria ya kiislamu, yani kutekeleza maamrisho na kujizuia na makatazo ni kuachana na haramu, mambo yenye kutia mashaka na hata baadhi ya vitu vilivyoruhusiwa; yani kuwa mbali vile vitu vilivyoruhusiwa (*rukhsah*) lakini katika mazingira fulani tu, na badala yake kuvitumia pale tu inapobidi. Si tu kwamba hiyo ni nuru na usafi, bali pia ni chombo chenye kumpandisha mtu mpaka kwenye madaraja ya uchamungu; mada-  
raja ambayo hayapatikani isipokuwa kwa kupitia njia hizi. Wengi mion-  
goni mwa watu wanaoshindwa kufikia kwenye madaraja hayo ni kutokana  
na sababu kwamba watu hao wanashindwa kuchunga mipaka hiyo. Na  
matokeo yake hushindwa kupata uongofu wa Mola wao kwa wepesi.



**Mawlana Khalid Baghdadi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake -  
(alifariki 1826)**

Ninakushauri kwa kupitia uendelevu katika kumuabudu Mwenyezi Mungu na uchamungu, usimdhuru yeyote popote pale utakapokuwa na uwe makini hasa juu ya vitukufu viwili (*Haramayn-i Sharifayn*).

Usisengenye hata kama na wewe umesengenya. Usichukue mali ya mtu kwa nguvu. Chukua kile tu ulichoruhusiwa na sheria na ukitumie katika njia ya wema. Usitumie fedha kwa ajili ya kuiridhisha nafsi yako wakati ndugu zako wana njaa na wanahitaji. Kamwe usidanganye. Usimdharau mtu yeyote. Kamwe usijifikirie kuwa wewe ni bora kuliko wengine.

Tumia nguvu zako zote kwa ajili ya kufanya matendo ya ibada, kimwili na kiroho. Lakini wakati huo huo ishawishi nafsi yako kwamba haujafanya chochote chenye thamani; kwani katika matendo yote ya ibada kinachozingatiwa ni nia na nia nzuri itaweza kupatikana kwa kupitia moyo safi. Itakuwaje wewe usihitaji usafi wa moyo wakati wale walio wabora zaidi yako waliuhitaji? Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba mimi binafsi siamini kuwa nimetenda amali yoyote yenye thamani tokea nizaliwe; hilo limekubaliwa mbele ya Mola ili kunifanya niepukane na dhima ya kuulizwa mbele ya Mwenyezi Mungu.

Kama hujioni kuwa wewe ni muflisi katika amali zote za wema basi tambua kuwa upo katika sehemu ya mwisho ya ujinga. Lakini pindi utakapotambua kuwa wewe ni muflisi basi usikate tamaa na rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu.





### **Musa Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake - (1918-1999)**

Uzuri wa moyo na ukamilifu wa kiimani kwa muumini hudhahirika katika tabia yake. Miongoni mwa dalili kuu za tabia hii ni:

Kuwa mnyenyekevu wakati wote, kutambua thamani ya kila muda na pumzi ipitayo na kutoruhusu vipite hivi hivi, kuwapenda waja wa Mwenyezi Mungu na kuwa na mahusiano mema, kushirikiana na wengine kulingana na kiwango cha imani zao, kuficha kasoro zao, kuwa makini kuhusiana na halali na haramu na kuiona ni kubwa mno dhambi ambayo inachukuliwa na wengine kuwa ni ya kawaida; kwani kuifanya dhambi kuwa ni kitu cha kawaida ni sawa na kumdharau Mola.

Ili kuendana na matakwa ya Mola wetu hebu tupambe nyakati za alfa-jiri kwa dua na utajo mtakatifu. Tutangulize kutoa huduma zetu kwenye familia zetu na wakubwa wetu. Na tupunguze muda tunaoutumia pamoja na wale wanaoipenda dunia na badala yake tuwe pamoja na watu wema. Na tutoe huduma zetu kwa usawa kwa miongoni mwa ndugu zetu na wenye kuhitaji. Na cha muhimu zaidi tuwe makini katika kuchunga halali na haramu. Na tuwe makini katika mahusiano yetu ya kijamii ili tusije tukatoka katika jukumu letu kuu la kumtumikia Mola.

Makosa, usahaulifu na udhaifu wakati wote hutokea katika nyakati ambazo umejiweka mbali na *dhikr*. Wale wenye kuendeleza hali ya kiroho ya *dhikr* huwa hawaathiriwi na huzuni na majoji yatokanayo na dunia; huwa hawana hata furaha kubwa ya kidunia kama wengine. Nafasi yake hujazwa na hali ya kiroho yenye kuendelea, ukarimu na huruma juu ya viumbe wengine. Kwa maneno mengine tunaweza kusema kwamba huu ni upendo; upendo wenye kuendelea. Mwenyezi Mungu humdidimiza mja aliye karibu yake ndani ya bahari ya upendo. Baada ya hapo mtu huwapenda wale tu wanastahili kupendwa; na upendo huo ni kwa kadiri atakavyowezeshwa na Mola.

Kila mtu hana budi kuona kwamba kuitumikia jamii inayomzunguka kwa ajili ya Mola ni jukumu lenye thamani kubwa. Mtu mwenye kufanya kazi kwa ajili ya kuboresha maisha ya kijamii na kuleta usawa na maendeleo anakuwa ana nafasi tukufu katika jamii hiyo; na atakuwa na malipo makubwa kesho akhera. Kumesemwa katika hadith kwamba:





## سَيِّدُ الْقَوْمِ خَادِمُهُمْ

“Yule mwenye kuwatumikia watu ndiye mbora wao.” (Daylami, Musnad, II, 324)

Wengi wetu licha ya kuwa na amali njema nyingi lakini wanapuuzia kujipamba na tabia ya ‘*sattaru’l-uyub*’, yani tabia tukufu ya kusitiri kasoro za wengine. Na kwa namna hiyo hawawezi kuendelea kiroho kwa kiwango wanachotarajia. Hivyo kusamehe na kuficha kasoro za wengine ni moja wapo ya sifa muhimu ya maadili mema. Kama ambavyo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasitiri na kusamehe makosa mengi tunayoyafanya sisi waja wake, hivyo na sisi hatuna budi kuwa ni wenye kusamehe. Wale tu walio-guswa na upendo mtakatifu ndio wenye kufahamu namna ya kusamehe.

Maarifa yote yanaegemea kwenye uwezo wa kuwa karibu na Mola, licha ya kuwa katikati ya ghasia za dunia na mihangaiko ya kila siku; hii ni hali bora ambayo ni zawadi itokayo kwa Mola. Kama tungelitafakari vyema juu ya jukumu muhimu lililo mbele yetu tungelijichunga dhidi ya ulaghai unaotokana na dunia.

Moja wapo ya zawadi kubwa ambayo Mola anaweza kumpa mja wake ni kumfanya atambue udhaifu wake mwenyewe. Labda mafanikio makubwa niliyowahi kuyapata katika njia ya kiroho yalikuwa ni kuweza kwangu kuona kasoro zangu mwenyewe. Nilitambua ufilisi wangu kuele-kea kwa Mola, kwa namna hiyo sikuweza tena kuwa na uwezo wa kuona na kufuatilia kasoro za mtu mwingine. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kutokana na kulithamini kwangu jambo hilo...

**Ewe Mola! Tujaalie sehemu ya moto wa upendo unaowaka ndani ya nyoyo za waja wako vipenzi! Tujaalie uwezo wa kuweza kujiongoza wenyewe kwa kupitia tahadhari na ushauri wa watu wema waliotupatia msaada wa kiroho!**

**Amin...**







---

# SURA YA SITA

---



## Simulizi za kisufi na mafunzo yake

Elimu ya kweli  
Kanuni katika mafunzo ya kiroho  
Ibrahim ibn Adham na mtoto wa paa  
Kutoitia doa njia ya Mola  
Karamah  
Kuziathiri nyoyo za wajinga  
Mlango wa rafiki  
Kutii, Kuhudumia, Kushauri  
Kuwahudumia viumbe  
Kuwaheshimu watu wema  
Utashi mbele ya Mola  
Adabu  
Adabu katika kuhudumia  
Adabu...Hata iweje  
Maadili na huduma ya mtu mwema  
Waache wanaokufa wafahamu, sio walio hai!  
Usimdharau mtu yeyote!  
Usimlaumu yeyote!  
Kuwachangamkia mayatima  
Urafiki  
Lengo la urafiki  
Kujisalimisha moja kwa moja  
Kupokea maombi ya muumini  
Majzub na tiba ya moyo wenye maradhi  
Sura kama malaika  
Hali ya moyo wakati wa sadaka  
Matendo mema ambayo yanakifikia kiti cha enzi  
Kumtambua Mola wakati wote  
Karim ndiye ninayemuhitaji  
Jukumu la mtangulizi  
Kuhudhuria mwaliko wa Mola  
Umuhimu wa Halal  
Kipato cha halali

MUKHTASARI



"Adab yâ hû"





**W**atu wema ambao hufikia katika kiini cha uswahaba kwa kupitia kwa Mola hubakia kuwa maswahaba wa wanadamu wote milele.



## Simulizi za kisufi na mafunzo yake

Usufi kama ambavyo umekwisha gusiwa katika sura zilizotangulia ni sayansi isiyojihusisha sana na maneno katika kumkomaza mtu kiimani; bali imejawa na uzuri na msukumo ambao unaakisi katika maisha kutokana na nyoyo njema za watu wema. Uzuri huu ambao tokea hapo kabla umekuwa ukisambazwa chini ya jina la ‘simulizi’ umechukua nafasi muhimu katika kukomaza imani juu ya Mola, kueneza maadili mema, kuamsha chemchem za upendo mtakatifu na huruma ndani ya nyoyo za watu na kustawisha hisia tukufu kama vile upendo, huruma na ukarimu. Simulizi zilizosimuliwa mara kwa mara ndani ya Qur’an ni taswira yenye kumchochea mwanadamu kuelekea kwenye ukomavu wa kiroho katika safari yake ya maisha; na kwa kuwa simulizi zenyewe zimechukuliwa kwenye maisha halisi ya watu husika, hivyo zinakuwa ni zenye kuleta ufanisi mkubwa.

Kutokana na kushawishika na njia hii tukufu na kutokana na kuwa na nia ya kweli katika lengo letu la kusambaza ukweli wa usufi si tu kama ulivyoandikwa katika maandishi, bali pia cha muhimu zaidi ni kuusambaza kulingana na namna ulivyodhihirika katika maisha halisi ya watu wema katika sura zilizotangulia. Tunachokusudia katika sura hii ni kutoa mifano mizito zaidi kuhusiana na simulizi hizo. Pia tutafafanua zaidi mafunzo ya msingi yanayopatikana katika simulizi hizi, na pia tahadhari na mazingatio tunayohitajika kuyachukua. Kwa usupi lengo letu juu ya hicho kinachofuatia ni kumpatia msomaji matone machache kutoka kwenye bahari pana ya maadili na wema utokao kwenye nyoyo za sufi mbalimbali.





### **Elimu ya kweli**

Mtukufu Sami Effendi alikuwa ndio ametoka kumaliza shahada yake ya sheria katika chuo kikuu cha Daru'l-Funun

ndani ya Istanbul. Baada ya mtu mwema mmoja kugundua mwenendo wake wa sawa na kutojiona kwake alimwambia:

“Elimu hii iko sawa pia, lakini huna budi kutafuta namna ya kusoma elimu ya kweli ewe mwanangu. Acha tukuandikishe katika shule ya hekima, mahali ambapo utapokea mafunzo ya sayansi za moyo na siri za akhera”, baada ya maneno hayo akaongezea:

“Ukweli ni kwamba sifahamu namna wanavyomfundisha na kumuelekeza mtu. Lakini ninachofahamu ni kwamba somo la kwanza la elimu hii ni kutoumiza na somo la mwisho ni kutoumizwa”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Bila shaka kutoumiza ni rahisi. Lakini kutoumizwa mara nyingi ni suala lililo nje ya udhibiti wa mtu; kwani ni suala linalohusiana na moyo wa mtu. Hivyo kujizuia dhidi ya kuumizwa na kuvunjwa moyo kutawezekana baada ya kuwa ni mtu usiyethiriwa na sumu na mishale yenye kuchoma kutoka kwa wanadamu. Uimara wa uwezo huu wa kustahamili hayo yote unategemeana na kiwango alichofikia mtu katika kuisafisha nafsi na kuutakasa moyo. Pindi Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alipopigwa mawe Taif alijiwa na malaika na kuhakikishiwa kuwa kwa tamko moja tu angeliweza “...kugonganisha milima miwili inayoizunguka Taif na kuwaangamiza wakazi wake”.

Lakini kutokana na Mtume Mtukufu – rehema na amani ziwe juu yake – kuwa rehema kwa walimwengu wote si tu kwamba alikataa suala lile bali aligeukia Taif na kuwaombea wakazi wake uongofu.

Vile vile licha ya kupigwa mawe hadi kufa Hallaj ambaye alikuwa kipenzi mkubwa wa Mtume kabla ya kufa alisikika akiomba, “Mola wangu... Hawafahamu kitu; hivyo wasamehe wao hata kabla ya kunisamehe mimi!”

Huu ni msimamo ambao hupatikana kwa kupitia elimu ya kweli; msimamo huu upo ndani ya moyo wa mtu aliyetakaswa kwa kupitia mafunzo ya kiroho.





Pindi Abu'l-Qasim al-Hakim alipoulizwa kuhusiana na sifa za moyo uliotakasika (*qalb-i salim*) alijibu kama ifuatavyo:

“Moyo uliotakasika una sifa tatu: Ni moyo usioumiza, moyo usioumizwa na moyo wenye kutenda wema kwa ajili ya kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu bila ya kukubali kitu chochote kutoka kwa watu kama fidia. Muumini huweza kufika mbele ya Mola wake kwa heshima (wara), ikiwa hajamuumiza yeyote; kwa utii, ikiwa aliuelekeza moyo wake kwa Mola wake pekee na kuulinda dhidi ya kuumiza na mtu yeyote; na usafi wa moyo, ikiwa hakumshirikisha Mola wake na chochote katika ibada zake”

Mshairi amelizungumzia suala hili kwa uzuri zaidi kama ifuatavyo:

*Lengo la mwanadamu na jini kwenye bustani ya ardhi  
Ni kutoumiza, bali ni kutii, na kutoumizwa!*



### **Kanuni katika mafunzo ya kiroho**

Shah Naqshiband – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anatoa maelezo ya kina kuhusiana na kile alichokutana nacho pindi alipokuwa anawasaidia wengine katika kuzitakasa nyoyo zao na kuzisafisha nafsi zao:

“Huwa tunawafundisha wanafunzi kwa kutumia njia bora kwa kadiri iwezekanavyo; yani kulingana na hali zao. Kuna wakati tunapendekeza njia ya ushawishi (*jazbah*), na wakati mwingine njia ya taratibu (*suluk*). Tunafahamu kwamba wengi huja kwetu huku wakiwa na mbegu za upendo ndani ya nyoyo zao, wakati huo huo wengine wengi hawana mbegu hizi au mbegu zao zimeachwa zikaoza kutokana na tabaka zito la nafsi na tamaa za kidunia. Hivyo jukumu letu ni kung’oa tamaa hizi za nafsi na badala yake kupandikiza mbegu za upendo, na pia jukumu letu kuhakikisha kuwa mbegu hizi zinastawi na kuwa vimelea vya nyoyo safi vilivyonyeshelzewa mvua ya ukweli chini ya miale ya jua la *marifatullah*.

Tufundisha dhikr ni sawa na kumpa mtu jiwe gumu sana. Cheche za upendo zitaweza kuwaka kulingana na juhudi za mwanafunzi katika kuli-tumia jiwe hilo”





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Maradhi ya mwili huja katika aina mbalimbali na tiba mbalimbali; pia hivyo ndivyo yalivyo maradhi ya nafsi na moyo. Hivyo watakatifu wenye utambuzi na umakini huchunguza na kutibu maradhi ya mtu ya kiroho kulingana na hali yake husika. Wakati huo huo watu kama Ibrahim Adham wanashauriwa:

“kuachana na taji na kiti cha enzi”, wakati kinyume chake kabisa wengine kama vile Sultan Mehmed wanaambiwa:

“Utajilaumu mwenyewe kama utaliacha taji lako na baada ya hapo akaja kulichukua mtu asiyefaa”

Baadhi hujaribiwa kwa maji na wengine kwa moto. Haijalishi jaribio litakuwa ni lenye kuchosha kwa kiasi gani lakini kuyatibu maradhi ya kiroho kama ilivyo kwa maradhi ya kimwili kunahitajika imani juu ya daktari na ufanisi mkubwa katika kutumia tiba iliyopendekezwa; na zaidi. Kupuuzia kumeza dawa kwa ajili ya maradhi ya kimwili kunaweza kusababisha madhara zaidi kadiri muda unavyosogea; Vivyo hivyo kupuuzia kuchukua dawa husika kwa ajili ya kutibu maradhi ya moyo kunaweza kupelekea kupata hasara ya milele.



### **Ibrahim ibn Adham na mtoto wa paa**

Mwanzoni Ibrahim ibn Adham alikuwa mfalme wa Balkh ambaye alikuwa na matumizi makubwa katika anasa ndani ya kasri. Sufi wa wakati ule walikuwa wakimuasa mara kwa mara ili aokoke na mtindo wake mbaya wa maisha na kuhuisha moyo wake. Kulingana na masimulizi maarufu, pindi alipokuwa amelala kitandani mwake alisikia sauti ngeni zikimfikia kutoka juu ya dari. Kutokana na kushindwa kulala alitoa kichwa chake nje ya dirisha na kufoka:

“Ni nini kinaendelea huko?” Alijibiwa kwa jawabu la kushangaza.

“Ninatafuta ngamia wangu aliyepotea”, yule mtu alisema.

“Unafikiria nini”, Ibrahim alijibu kwa ukali, “unatafuta ngamia wako juu ya dari?” Wakati huu jibu likawa ni lenye kustaajibisha:





“Unafahamu vyema kuwa ni ujinga ulioje kutafuta ngamia aliyepotea juu ya dari, lakini kamwe hufikirii ni ujinga ulioje kutafuta furaha ya milele ndani ya maisha ya kifahari na ubadhirifu kama hayo unayoishi wewe!”

Ukilinganisha na maneno ambayo alikwisha yasikia hapo kabla, maneno haya yalimuacha Ibrahim kwenye fadhaa kubwa. Lakini licha ya hayo ilichukua masiku machache kwa yote hayo kusahaulika na kuendelea na mtindo wake ule ule wa maisha bila ya mabadiliko yoyote.

Siku nyingi zikapita ndipo siku moja Ibrahim akaamua kutoka nje ya kasri kwa ajili ya kwenda kuwinda paa wadogo pamoja na kundi la watu. Kuna wakati akawa anaendesha peke yake kwa ajili ya kutafuta windo zuri. Ndipo akasikia mnong’ono katika sikio lake. ‘Amka’, sauti ile ilisema. Haku-tilia maanani. Lakini sauti ile ilikuwa ikijirudia tena na tena. Mara sauti ile ikaenea na ikawa inakuja kutoka kila mahali:

“Amka kabla kifo hakijakuamsha”, ilisikika.

Ibrahim ibn Adham alipigwa na butwaa na kupata hofu. Lakini mara mtoto wa paa mdogo mwenye kuvutia alijitokeza mbele ya macho yake yaliyokuwa yakidadisi, na mara akaanza taratibu kusahau sauti zile. Akajituliza na kwa shauku kubwa akamlenga yule paa mpole kwa mshale wake kwa lengo la kumchoma. Ilibakia inchi moja kwa yeye kuruhusu mshale uchomoke. Lakini paa yule huku akiwa amemtazama Ibrahim kwa huzuni alinong’ona:

“Je Mwenyezi Mungu aliye mwingi wa rehema aliniumba ili uje kuniwinda ewe Ibrahim?”

Huku akiwa ameduwaa Ibrahim akaanza kutetemeka kuanzia kichwani mpaka chini. Huku macho yake yakiwa yamejawa na machozi aliteremka juu ya farasi wake na kusujudu chini kwa majuto makubwa na kuomba:

“Mola wangu ambaye rehema na heri zako hazina mwisho! Kwa muda mrefu nimepoteza pumzi zangu katika anasa na fahari! Uoshe moyo wangu kwa rehema zako ewe Mwenyezi Mungu, na usiache chochote isipokuwa mapenzi yako!”

Macho ya Ibrahim ibn Adham yakaamka katika ulimwengu mwingine kabisa; akajikuta akiangalia kwenye ulimwengu wa kiroho. Mtazamo huu





mzuri ukafuta akilini mwake fikra zote za uzuri alizokuwa akizishabikia hapo kabla. Kaftani ya kiufalme aliyokuwa akiivaa kila siku asubuhi kwa umakini mkubwa, na fahari ya kuwa sultani wa Balkh ikiwa imepoteza mvuto na umuhimu. Vyote hivyo vikawa kama ziada ambayo angeliweza kuishi bila kuwa nayo.

Huku macho yake yakiwa bado yana machozi ya toba na moyo wake ukiwa unaungua kwenye moto wa majuto, Ibrahim ibn Adham akaondoka pale alipokuwepo na kuingia kwenye pori. Alitembea masafa marefu kabla ya kukutana na mchungaji aliyekuwa amevalia joho la sufi kama ilivyokuwa kawaida yao. Akamsogelea yule mchungaji na kumbadilishia lile joho lake la sufi kwa kaftani yake iliyokuwa ikivutia. Pindi tu Ibrahim alipolivaa lile joho alihisi ahueni kubwa. Wakati ule mchungaji alikuwa akistaajabu. “Sultani wetu amechanganyikiwa”, alijifikiria kichwani mwake. Lakini kinyume na kupoteza fahamu ndio alikuwa amepata fahamu. Alikuwa ameenda kuwinda paa ili aweze kuamshwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kupitia paa huyo.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Pindi mnapokabiliwa na chagua kati ya hapa duniani na akhera, wale watakachangua akhera huwa ni masultani wa milele waliozawadiwa zawadi zisizo na mwisho. Kwa wale wataochagua dunia, hata kama machoni wataonekana ni wafalme lakini kiuhalisia wao ni omba omba wa maisha wa milele, maisha ambayo kamwe hawatayapata hata kama wataomba kwa kiasi gani. Hii ndiyo siri ambayo Ibrahim ibn Adham alikuja kuifahamu; na pindi alipoipata siri hiyo alijitolea muhanga unaotakiwa ili kuwa sultani wa milele. Kama maonyo aliyoyapata katika njia yake ya kufikia kwenye maamuzi haya yalitokana na johari ya usafi wa moyo aliyokuwa nayo mpaka wakati ule.





### **Kutoitia doa njia ya Mola**

Njia ya usufi ni njia yenye kung'aa kutokana na nuru ya Mola ambayo hairuhusu doa lolote. Wale wenye kuweza kuona dhati yake na kutambua utukufu wa njia hii kamwe hawawezi kuona kitu chenye kuingiliana na mwangwi wa uislamu.

Darasa la kiroho la Shah Naqshiband – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – lilizungukwa na idadi kubwa ya wanafunzi kutoka katika nyanja zote za maisha. Wanachuoni wakubwa wa Bukhara kama vile Khawajah Yusuf wakati wote walikuwa na shauku ya kuhudhuria madarasa yake. Lakini bado umaarufu wa Shah Naqshiband ulikuwa ni suala walilotofautiana baadhi ya wanachuoni, wanachuoni ambao walianza kumzungumzia vibaya, wakidai kwamba mafundisho yake yalikuwa yakienda kinyume na misingi ya uislamu. Wakaja kukutana na Shah Naqshiband na kumuelezea wasiwasi wao juu ya mafundisho yake.

“Sikilizeni wakati tukiwaelezea njia yetu”, Shah Naqshiband aliwaambia. “Pindi mtakaposikia jambo linaloenda kinyume na Qur’an na Sunnah basi liwekeni wazi na sisi tutaachana nalo!”

Kisha wanachuoni wale wakamsikiliza Shah Naqshiband alipokuwa akiwaelezea kuhusiana na mwenendo wa kisufi na kuwataka watafakari kwa kina kuhusiana na maneno yake, hawakuweza kupata kitu chochote cha kupinga.

“Inaonekana njia yenu si nyingine bali ni njia iliyonyooka (*sirat-i mustaqim*). Hamtasikia tena tukiipinga njia hiyo”, walihitimisha.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kinachoeleweka kutoka katika kisa kilichotangulia ni kwamba mwenendo wa kweli wa kisufi unakubaliana na Qur’an na Sunnah na unahitaji umakini mkubwa katika kuendana nao. Huku akiwashauri wanafunzi wake juu ya kuwa wapole pale wanapokutana na watu wasiozungumzia vyema njia hii, pia Shah Naqshiband anasisitiza juu ya umuhimu wa kuendelea kutumia Qur’an na Sunnah pindi wanapokabiliana na





wanachuoni wanaoushuku mwenendo wao, yeye aliwapa nafasi wataje vipengele vya usufi ambavyo vinaenda kinyume na Qur'an na Sunnah ili aweze kukubaliana nao. Hivyo ni jambo la msingi kwa wafuasi wengine wa mwendendo huu wajipambe na mwenendo kama huu ili wasije wakachafua kile kilichotakasika. Hatuna budi kutambua kwamba wanachuoni waliotajwa katika kisa hicho ni wanachuoni wema na si wanachuoni waovu (*ulama bi's-suu*) ambao wanaitumia vibaya elimu yao na nyoyo zao kwa uovu, si wale wanachuoni wanaoenda kinyume na maamrishi ya Mola kwa kushindwa kuchunga vipimo vya usafi wa moyo na uchamungu, pia hawa si wale wanaopinga maneno ya watu wema na maneno ya Qur'an pamoja na kuuza aya za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili ya kupata faida ndogo ya dunia.



### **Karamah**

Siku moja Shah Naqshiband aliombwa na wanafunzi wake aonyeshe karamah, kisha akawajibu kwa kusema:

“Karamah yetu ipo wazi. We angalia: Tunaweza kusimama kwa miguu yetu na kutembea juu ya ardhi licha ya mzigo mzito wa madhambi tulioubeba mabegani mwetu. Je kunaweza kuwepo kwa karamah zaidi ya hiyo?”

Kisha akawakumbusha wanafunzi wake kwamba msingi wa mwendendo wa kisufi si karamah bali ni msimamo (*istiqamah*), alisema:

“Hata kama ungelikuwa uingie kwenye bustani na kusikia miti iki-sema jani moja baada ya jingine, ‘Karibu ewe mtakatifu wa Mola’ lakini bado usingelitakiwa kushughulishwa na maneno hayo ama kwa ndani au kwa nje. Badala yake ungelitakiwa kuongeza unyenyekevu wako katika kumtumikia Mwenyezi Mungu”

Baada ya pale baadhi ya wanafunzi wake wakasema:

“Haijalishi ni kwa kiasi gani unajaribu kuificha lakini kuna wakati huwa unadhihirisha baadhi ya karamah”

“Hicho unachokishuhudia si kingine bali ni karamah ya wanafunzi wangu”, alijibu guzo ile kubwa ya staha.







Sheikh alikuwa makini mno katika kuufanya siri msimamo wake wa kiroho kiasi kwamba hakumruhusu mwanafunzi wake aliyetitwa Husamaddin Khawajah Yusuf aandike maneno na karamah zake pindi alipokuwa hai.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Watu wema waliotangulia waliweza kubakia katika msimamo wao wa kiimani si kwa kuzingatia karamah kama kiwango cha imani bali waliegemea kwenye msimamo. Katika kuonyesha karamah hakuna ulazima wa mtu kuwa na thamani kubwa kuliko ile ya ndege anayepaa au samaki anayeogelea; na kwamba marifah ya kweli hayahusiani na kuiga kwa urahisi kile ndege au samaki wanachokifanya. Bali ni kuishi katika maadili na msimamo na kujitolea kwa ajili ya Mola peke yake na kuwa na shauku kubwa ya kumtumikia yeye. Hilo ndilo lililoshauriwa na watu wema waliotangulia katika kila fursa waliyoipata na ndivyo walivyokuwa wakiishi.



### **Kuziathiri nyoyo za wajinga**

Kwenye siku tukufu katika mwaka wa 1340 AH kulikuwa na tukio maalum lililojumuisha usomaji wa Qur'an na *mawlid* ndani ya msikiti wa Ayasofya ndani ya Istanbul. Msikiti ulijaa sana. Ndani yake walikuwepo wanachuoni mbalimbali na wanafunzi, pamoja na makundi ya *huffaz* (walioihifadhi wa Qur'an) wakubwa wa wakati ule, walikuwa wakisoma Qur'an na *mawlid* mbele ya watazamaji waliokuwa na ari kubwa.

Karibu na mimbar alikuwa amekaa Adil Bey wa Beylerbeyi, huyu alikuwa ni mtu wa imani mwenye utambuzi mkubwa wa kiroho. Baada ya muda mfupi alizidiwa na hali ya mbinyo wa kiroho; ilikuwa ni kitu cha kustaajabisha, kwani sehemu kama ile ambayo Qur'an ilikuwa ikisomwa ilikuwa iwe ya mwisho katika sehemu ambazo mtu angeliweza kupatwa na mbinyo wa kiroho wa namna ile. Adil Bey akaangalia huku na kule. Muda si mrefu akagundua kuwa aliyekuwa amekaa mkabala na yeye alikuwa ni



mtu mjinga na mwenye moyo mgumu. Walikuwa wamegeukiana. Adil Bey akagundua kuwa sababu ilikuwa ni ubaya uliokuwa ukimfikia kutoka kwenye moyo wa mtu yule. Akabadilisha sehemu upesi. Alipata nafuu ingawa hakuweza kuondokana na hali ile mara moja.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kama ambavyo watu wema wanasababisha amani na utulivu kwenye nyoyo za watu ndivyo ambavyo watu wabaya wanavyosababisha udhaifu na uchovu na ugumu wa moyo. Kuingia kwenye bustani humfanya mtu apate harufu nzuri ya maua, wakati kuwa karibu na uchafu humfanya mtu achafuke. Kuhusiana na wale ambao nyoyo zao zimeoza na hivyo zinachotoa ni ushawishi mbaya, Mwenyezi Mungu amesema:

“Na unapo waona wanaoziingilia Aya zetu, basi jitenge nao mpaka waingilie mazungumzo mengine. Na kama Shet’ani akikusahaulisha, basi baada ya kutanabahi usikae pamoja na watu madhaalimu” (al-Anam, 68)

Uzito wa amri hiyo tukufu upo wazi kwa waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu ambao wanaongozwa na nyoyo safi. Kadiri moyo unavyokuwa msafi ndivyo viwango vya imani vinavyoongezeka; jicho huanza kuona siri zilizopo nyuma ya pazia na kuupata ukweli uliojificha kwa wengi. Mfano mzuri tunaweza kuupata kwa Seyfi Baba:

Seyfi Baba ambaye alikuwa akimpenda sana Sami Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa ni mtu mwenye utambuzi mkubwa wa kiroho. Siku moja aliiacha nyumba yake iliyokuwepo kwenye kitongoji cha istambul kilichoitwa Topkapi kwa ajili ya kwenda kumtembelea Sami Effendi kama ilivyokuwa kawaida yake. Lakini pindi alipoingia tu kwenye nyumba ya Sami Effendi alizimia na kuanguka chini. Mtu aliyekuwa amemfungulia Seyfi Baba alimwagia maji kwenye uso wake na kumfanya arudiwe na fahamu:

“Hatuna budi kumuita daktari”, yule mtu alishauri, lakini alizuiwa na Seyfi Baba ambaye alisema:

“Hakuna haja ya daktari ewe mwanangu, kwani hali hii haihusiani na





matibabu ya hospitalini. Watu waasi na sehemu zenye uasi mkubwa nilizopitia nilipokuwa njiani kuja hapa ziliniathiri na pindi nilipofika hapa nilikubwa na hali safi ya kiroho...Lakini moyo wangu haukuweza kuivumilia hali hiyo. Kwa msaada wa kipenzi changu Sami Effendi na baraka za hali ya kiimani iliyopo hapa nitapona wakati wowote.”

Hivyo kama ambavyo uovu wa mtu ulivyo na athari kwenye moyo wa mtu ndivyo wema utokao kwa mtu mwema unavyoweza kumtuliza na kumfanya arudi katika hali yake ya awali. Hivyo watu wenye mtazamo sahihi hawana budi kujiweka mbali na watu waovu kwa kadiri wawezavyo, na badala yake wawe karibu na watu wema. Mara kwa mara Daud – amani iwe juu yake – alikuwa akimuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu dua ifuatayo:

“Mola wangu...pindi utakaponiona nikielekea kwenye mkusanyiko wa watu waovu vunja mguu wangu kabla sijafanikiwa kufika ili nisije nikaungana nao. Nitafurahi sana kama utanifanyia hivyo!”



### **Mlango wa rafiki**

“Andaeni vipando vyetu”, siku moja Abu Said Nishaburi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliwaagiza wanafunzi wake. “Tunaenda mjini.”

Maandalizi yalikamilika, kisha Sheikh akifuatana na kikundi cha wanafunzi wake walianza safari. Muda mfupi baadae wakawa wamewasili katika kijiji kimoja ndani ya Nishapur.

“Hiki kijiji kinaitwaje?” Sheikh aliuliza.

“*Dar-i Dost*”, wakazi wa pale walimjibu, maneno haya yanamaanisha ‘mlango wa rafiki’.

Kisha Sheikh akaamua wapumzikie pale. Baada ya siku kupita baadhi ya wanafunzi wake walisema:

“Ewe mwalimu, tulidhania tunaenda mjini. Je hatuendelei na safari?”

Abu Said – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye moyo wake ulikuwa umejaa funguo za siri za kiroho nyingi anaelezea yafuatayo:





“Huchukua safari ndefu na yenye tabu kwa mpenzi kufikia kwenye mlango wa kipenzi chake. Kwa kuwa tumeshafika kwenye mlango wa rafiki hapa, ni wapi pengine tunapoweza kwenda?”

Waliishia kuishi pale kwa miaka arobaini na kubainikiwa na matukio mengi ya kiimani. Wana kijiji wengi walifurahia uwepo wa Sheikh na hivyo kutubia mambi yao na kisha kuungana na kundi la wanafunzi wake. Alichokimaanisha Sheikh pale aliposema ‘mlango wa rafiki’ kilikuwa ni kwamba: ili kuweza kuziteka nyoyo...kwa kufungua mlango wa kasri la rafiki kuliwezekana pale mtu alipokuwa na funguo: yani moyo ambao tayari umeshatekwa.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kuufungua mlango wa ‘rafiki’ kidogo kwa kuudhibiti moyo wakati wote kumekuwa ndio tamaa ya waja wema ambao nyoyo zao zinaungua kwa mapenzi juu ya Mola wao na taji lililo kwenye vito vya matendo mema ambayo huwawezesha kufikia kwenye makutano ya milele. Kwa mfano Shah Naqshiband – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa akifanya juhudi kubwa katika kuwafundisha wengine kwa umakini mkubwa kiasi kwamba alikuwa akiyachukulia matatizo ya wanafunzi wake ni kama matatizo yake mwenyewe, bila ya kujali kuwa matatizo yale yalionekana ni madogo kiasi gani. Kila alipokuwa akimtembelea yeyote alikuwa akiulizia kuhusiana na matatizo binafsi ya yule aliyemtembelea, kisha yale ya familia yake na hata ya vipando na kuku wake. Kisha alikuwa akijitahidi kumridhisha mtu yule. Kama kulikuwa na chakula kilichokuwa kikigawanywa kwenye mkusanyiko, Sheikh alikuwa akiwahudumia waandaaji yeye mwenyewe kwa mikono yake.



### **Kutii, Kuhudumia, Kushauri**

Mtu mwema mmoja ambaye alikuwa akifanya *sohbah* mara kwa mara na Dawud-i Tai siku moja alimshauri Maruf-i Karhi dhidi ya ‘...kuachana na amali, kwani humsogeza mtu karibu na radhi za Mola.”





“Unamaanisha nini hasa unaposema amali?” Maruf-i Karhi aliuliza.

“Kubakia katika hali ya kumtii Mola katika hali yoyote ile na kuwahudumia na kuwashauri waislamu”, yule mtu alijibu.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Amali ndogo iliyotekelezwa kwa utii na unyenyekevu ni yenye thamani zaidi mbele ya Mwenyezi Mungu kuliko milima ya amali zilizotekelezwa bila ya sifa hizo. Kumtumikia Mwenyezi Mungu kunaanzia kwenye utii na unyenyekevu. Licha ya hayo, je Shetani hakufukuzwa mbele ya Mola kutokana na kukataa kwake kutii na kunyenyekea kwa Mola wake? Je ilikuwa ni kutokana na upungufu wa amali?

Kwa upande mwingine kuhudumia ni jambo lenye thamani kubwa kiasi kwamba Mitume yote na watakatifu walishikamana nako, na hawakuacha kuhudumia watu hata pale walipokuwa wagonjwa au walipokuwa juu ya vitanda vyao vya mauti. Kwa watu wenye hekima hii ndiyo njia bora ambayo mtu anahitajika kuifuata katika kuhudumia. Kwa ufupi kuhudumia ni nembo ya huruma na wema wa mtu.

Muumini aliyekomaa ni mtu mwenye kuhudumia, ni askari wa moyo ambaye baada ya kuweka pembeni thamani ya mwili anajiweka katika mstari wa mbele wa jeshi la wahudumu. Huwa yuko pembezoni mwa mgonjwa na mwenye matatizo, wakati wote yupo karibu na waombolezaji, pia yupo pamoja na walio na huzuni, waliokata tamaa na waliotengwa.

Kinyume na hayo, kushauri ni sifa inayowahusu mabingwa; kwani kile kinachosemwa huleta ushawishi kulingana na namna kinavyofanyiwa kazi na msemaji. Hivyo si sawa kwa kila mmoja kutoa ushauri. Wanaostahili ni wale walioshikamana na mwenendo na maadili ya kiutumbe. Kukwepa jukumu hili licha ya kujaaliwa uwezo wa kufanya hivyo ni jambo lenye lawama na kuwajibika; kwani Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Dini ni kutoa nasaha (*nasihah*)”. (Bukhari, iman, 42)

Hivyo kujiweka mbali na jukumu la kushauri ni sawa na maangamizi





kulingana na tahadhari tukufu iliyotolewa katika surat al-Asr. Kutosikiliza ushauri ni sawa tu hilo; kwani sababu ya maangamizi.

Hivyo watu walio katika njia ya Mola hawana budi kukubali kwamba kutii, kuhudumia na kushauri ni viwango visivyopingika na hivyo kujipamba na sifa hizo kutamuwezesha mtu kupata radhi za Mola.



### **Kuwahudumia viumbe**

Mtu mwema mmoja alimuona katika ndoto Pertevniyal Valide Sultan ambaye alikuwa mdhamini wa msikiti wa Aksaray Valide ndani ya Istanbul muda mfupi baada ya kufariki kwake, alimuona akiwa katika madaraja ya juu huko akhera.

“Je ni kutokana na msikiti uliujenga ndio maana Mwenyezi Mungu akakunyanyua mpaka kwenye daraja hili?” alimuuliza.

“Hapana”, alijibu.

“Basi ni kwa amali ipi?” yule mtu aliuliza kwa shauku.

“Ilikuwa ni siku ya mvua na matope mengi”, alianza kuelezea. “Tulikuwa njiani kuelekea kwenye msikiti wa Ayyub Sultan, mara tukamuona mtoto wa paka aliyekonda akiwa anatapatapa huku akipumua kwa shida ndani ya kidimbwi cha maji kilichokuwepo pembezoni mwa barabara. Nikaamuru rukwama isimamishwe na kisha nikamwambia *baji* aliyekuwa karibu yangu, ‘Nenda ukamtoe yule mtoto wa paka kwenye maji...asije akaghariki ndani ya maji’.

Huku akisita kushuka kwenye rukwama ile alisema, ‘Lakini kama tutatoka nje tutachafuka mikono yetu na nguo zetu!’

Hivyo bila ya kutaka kuumumiza moyo nilitoka mwenyewe nje ya rukwama na kisha nikajikokota kwenye yale matope na kumtoa yule mtoto wa paka pale kwenye dimbwi. Kiumbe yule dhaifu alikuwa akitetemeka. Huku nikimuonea huruma nilimuweka kwenye paja langu na kumpatia joto, na sikumruhusu aondoke mpaka pale aliporudiwa na fahamu zake.

Ni kutokana na huruma ile ndogo ndio maana Mwenyezi Mungu akanijaalia kufikia kwenye daraja hili la juu”





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Njia yenye kung'aa ambayo inaelekea kwenye anga za ukomavu wa kiroho na ukamilifu inapitia kwenye daraja la huruma na huduma. Hivyo kila muislamu hana budi kufanya huruma na huduma kuwa ni sehemu ya sifa zake za kipekee.



### **Kuwaheshimu watu wema**

Musa Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasimulia yafuatayo:

“Kilikuwa ni kipindi cha hijja. Huku nikuwa pamoja na Sami Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – tulikuwa tumefikia kwenye nyumba ya Abdussattar Effendi wa Turkistan ndani ya kitongoji cha Makka kina-choitwa Jiyad kilichokuwepo karibu na al-Kaaba. Chumba alichokuwemo Sami Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – kilikuwa juu ya mtaa, wakati vyumba vyetu vilikuwepo pembezoni mwa nyumba.

Miongoni mwa siku zile siku moja mchana Sami Effendi alikuja mlan-  
goni mwetu na kusema, “Inaonekana kuna mtu nje anahitaji chochote kwa  
ajili ya kula.”

Upesi nikaandaa chakula na kukiwahisha nje. Lakini sikumuona mtu  
yeyote. Nikarudi ndani na kufikiria kwamba labda alishindwa kusubiri  
hivyo akaamua kuondoka. Zilipopita dakika kumi Sami Effendi akaja tena  
kwenye mlango wa chumba chetu.

“Yule muhitaji amerudi na anasubiria hapa nje”, alisema.

Wakati huu nilipotoka nje na chakula nilifanikiwa kumuona yule ali-  
yekuwa na shida: alikuwa ni mbwa aliyeonekana kuchoka na huku akiwa  
anatweta kutokana na njaa. Upesi nikamuwekea kile chakula mbele yake.  
Alionekana kuwa na njaa sana, kwani alikila chakula chote.





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Hiyo ndiyo adabu na unyenyekevu kwa wazee wa kiroho. Sami Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – hakumchukulia mbwa kama ‘mbwa’ bali alimchukulia kama mtu. Mara nyingi alikuwa akiwaongelea wanyama kama ‘waja wa Mwenyezi Mungu’ na si ‘wanyama’.

Uzuri wa mwenendo bora kuelekea kwa viumbe kwa ajili ya Muumba huwa ni sawa na kumuhusisha Muumba Mwenyewe; kwani huu ni uzuri wa moyo uliotakasika ambao umeshikamana na Mola. Kwa upande mwingine, kuwa na moyo uliotakasika ni sawa na kuwa na uswahaba wa kweli usio na mipaka. Nyoyo zilizotakasika hudunda kwa raha juu ya Mola, kwani ndipo mahali unapobainika ustadi mzuri wa ukarimu na huruma.



### **Utashi mbele ya Mola**

Kulitapaka tetesi kwamba Sheikh Muhammad Nuru'l-Arabi, ambaye alikuwa Sufi wa karne ya 19, alikuwa akikataa uwepo wa uwezo fulani (irada-i juziyyah) ndani ya wanadamu. Sultani wa dola ya Uthmaniyya aliyeitwa Abdulmecid akamtaka Sheikh alipeleke suala lake katika kasri wakati wa moja ya masomo ya huzur. Hivyo sheikh akawasili pale na kuambiwa atoe maelezo kuhusiana na suala lile, Sheikh alisema:

“Mtu huwa na kiwango fulani cha uwezo wa kuamua jambo; na hiyo ndio sababu ya kuwajibika kwake kwa Mola...lakini si kila mmoja na si kila wakati. Kwa mfano mimi nina uwezo fulani wa maamuzi na uhuru wa kuchagua lakini nimekuja kwa sababu ya amri ya Sultani. Hata kama ningelitaka kuondoka nisingeliweza, kwani hilo lipo nje ya mamlaka yangu. Wanasema ‘Njooni’ na sisi tunakuja...wanasema ‘ondokeni’ na sisi tunaondoka. Hili linamaanisha kwamba uwezo wangu wa maamuzi hapa hauna maana kuhusiana na uchaguzi wa baadhi ya mambo. Vivyo hivyo ninapokuwa mbele ya Sultani ninakuwa na mipaka katika vitu ninavyovifanya. Kwa namna hiyo hiyo kuna baadhi ya watu ambao wakati wote hutambua uwepo wao mbele ya Mola. Kutokana na watu wengi kutambua kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ni yupo kila mahali na kwamba anaangalia kila kitu, hujichukulia kuwepo mbele ya Mola wao pale tu







wanapotekeleza ibada ya swala. Lakini kuna baadhi ya watu ambao wamefikia kwenye daraja fulani la kiroho, watu hawa huishi huku wakitambua fika kwamba wapo mbele ya Mola wao wakati wote. Sasa ni juu yako kumua ikiwa watu hao wana uwezo wa maamuzi ama hawana!”

Kutokana na kuvutiwa na maneno ya Sheikh Sultani alimzawadia Sheikh zawadi nyingi.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Mja hutumia utashi aliopewa na Mwenyezi Mungu Mtukufu. Ingawa utashi wa Mola hutawala kila jambo lakini radhi zake huwa juu ya wema. Lengo la mwalimu ni kumpatia mwanafunzi elimu ambayo itamuwezesha kufanya vizuri katika fani yake. Hakuna atakachoweza kufanya mwalimu endapo mwanafunzi atafeli. Vile vile jukumu la daktari ni kuhakikisha kuwa mgonjwa anatibiwa; hivyo mgonjwa hana wa kumlaumu zaidi na nafsi yake endapo atapuuzia kumeza dawa alizopewa. Daktari hatolauliwa kuhusiana na upuuziaji huo.

Kwa upande mwingine, kusalimisha utashi wako kwa Mola ambaye uko mbele yake kuna malipo makubwa zaidi ya kile ulichopewa. Pia tunaweza kusema kwamba kama mtu atasalimisha kwa moyo safi uoni wake mbele ya uoni wa Mola usio na mipaka, mikono yake mbele ya mikono ya Mola isiyoweza kuhimiliwa, ulimi wake mbele ya sifa Yake ya kuongea na kusikia kwake mbele ya kusikia kwa Mola kusio na mipaka, fahamu zake na utambuzi wake utakuwa katika hali ya kipekee kabisa. Kwa ufupi ni kwamba hatojutia kile alichokitoa. Vile vile kila kitu kitakachokuwa kikimpata kwake kitakuwa ni baraka zitokazo kwa Mola. Hivyo kutokana na waja wake wema ambao wakati wote wanatambua kuwa wapo mbele ya Mola wao na ambao wameweza kusalimisha utashi wao kwake, Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema yafuatayo kwa sitiari katika *hadith al-qudsi*:

“Nitakuwa macho yao yenye kuangalia, masikio yao yenye kusikia na mikono yao yenye kushika” (Bukhari, Riqaq, 38)





## Adabu

Dawud-i Tai anasimulia:

“Nilikaa na Abu Hanifah kwa muda wa miaka ishirini. Niligundua kwamba kwamwe sikupata kumuona ameacha kichwa wazi au kuweka miguu yake juu, ama pembezoni mwa wengine au akiwa peke yake. Siku moja nilimuuliza kwamba kulikuwa na tatizo gani kuweka miguu yako juu pindi unapokuwa peke yako.

“Ni bora kuwa na adabu pindi unapokuwa mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu” alisema.



## Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:

Pindi watu wanapokuwa mbele ya mtu mwenye daraja la juu huwa hawawi kama ambavyo wanatarajiwa wawe, na huwa wanakuwa makini katika kudhihirisha tabia inayoendana na mazingira waliyomo. Tunaweza kusema kwamba kuwa karibu na mtu wa namna hiyo kunahitaji kuwa na tabia njema. Kwa kuwa watu wema wanatambua kwamba wakati wote wapo mbele ya Mola wao, hivyo hawapuuzii tabia njema. Hivyo adabu huyagubika maisha yao yote, kwani wana nyoyo za hekima ambazo kwa kupitia nyoyo hizo wanaona na kuhisi kwa uhakika kwamba wanaangaliwa na Mola wao mpendwa katika sehemu zote na nyakati zote. Wameshikamana na siri ifuatayo:

وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنْتُمْ

“Naye yu pamoja nanyi popote mlipo...” (al-Hadid, 4); na kwa namna hiyo wanaishi huku wakitambua kuwa wako mbele ya Mola wakati wote.

Tunachojaribu kusema hapa ni kwamba kimsingi wakati watu wengine wanahisi kwamba wapo mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati wa swala pekee, watu ambao huwa na adabu hali ya kuwa wapo ndani ya swala kutegemeana na uzito wanaouhisi, wakati huo huo kuna watu wengine walio wema zaidi, watu ambao kila tabia na mwenendo wao upo kati-





ka misingi ya adabu, hawa ni watu ambao wanaendeleza mfumo huu hata pale wanapokuwa nje ya swala. Katika kuwasifu watu hao Qur'an inasema:

الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ

“Ambao wanadumisha Sala zao” (al-Maarij, 23). Si tu kwamba hawapuuzii swala zao, lakini pia wapo katika hali ya kuswali hata pale wanapokuwa nje ya swala. Hili linadhihirisha uwezo wao wa kuendelea kujitambua kuwa wako mbele ya Mola wao ndani na nje ya swala.



### **Adabu katika kuhudumia**

Abu Abdullah Rugandi anasema:

“Kamwe usiidharau huduma yoyote unayoipata. Hata hivyo huduma ni huduma; na inawezekana kitu ambacho kinaonekana hakina umuhimu kwako kikawa kikubwa sana kwa Mola kwa sababu usizozijua. Hatufahamu ni huduma ipi ambayo ndani yake tunaweza kukutana na radhi za Mwenyezi Mungu. Hivyo endelea kuhudumia mpaka ukidhi haja yako na haja yako haipaswi kuwa kitu kingine chochote zaidi ya radhi za Mwenyezi Mungu. Baraka na manufaa utakayoweza kuyapata njiani vinapaswa kukuongezea ari yako kuelekea kwa Mola na kuzidisha huduma yako.”



### **Mafunzo tunayoyapata kutokana na kisa hiki:**

Hakuna umuhimu wa kutoa huduma hivi hivi bila ya kuwa na moyo safi na katika ubora wa hali ya juu kwa kadiri iwezekanavyo. Hivyo watu ambao wanashikana mikono kwa ajili ya kutoa huduma hawana budi kupewa motisha, na motisha hiyo isiwe kutokana na kuhudumia tu bali kutokana kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Kutoa huduma kwa ajili ya kusifiwa na watu ni suala lililompelekea mtu kwenye furaha ya milele. Ingawa watu hao wanaweza kuishia kwenye kupata sifa kutoka kwa watu





lakini rehema za Mola hutolewa kwao na badala yake kupata ghadhabu za Mwenyezi Mungu. Kuhudumia hakutakiwi kutiwe motisha na tamaa ya kupata sifa na radhi za binadamu katika hii Ardhi. Lakini hakuna budi kuhamasishwe na tamaa ya kukamilisha amali ambazo zitamuwezesha mtu kupata ufalme wa kiroho huko akhera.

Hivyo mja hana budi kuiona kila fursa ya kuhudumia kama hazina iliyopotea na kupatikana. Inawezekana kwamba huduma ambayo inaonekana ni ndogo hapa duniani ikawa imeficha malipo makubwa kuliko mbingu na Ardhi. Katika kujaribu usafi wan yoyo za waja wake na kuona ni wapi nyoyo zao zinapoelekea Mola huficha mambo mengi yanayotafutwa katika tone.



### **Adabu...Hata iweje**

Ibn Ata – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anaelezea:

“Wale waliosogea mbele katika njia ya kiroho waliweza kufanya hivyo si kutokana na swala na funga zao. Walifanikiwa kusonga mbele kutokana na kutekeleza wajibu pamoja na matendo na tabia zao njema. Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – amesema:

“Atakayekuwa karibu na mimi zaidi miongoni mwenu siku ya kiama ni Yule atakayekuwa na tabia na maadili mema zaidi.” (Tirmidhi, Birr, 71)



### **Mafunzo yatokanayo na kisa hiki:**

Mshairi anasema:

*Adabu...taji kutoka kwa Mungu,*

*Livae usije ukapatwa na shida.*

Mshairi mwingine mwenye hekima anasema:

*Niliomba na kutafuta kuwa miongoni mwa wenye imani*

*Wanasema yote yamekubaliwa kwa kupitia adabu hata iweje.*





Mashujaa wa kweli katika adabu na maadili Mitume na watakatifu, na pia wale waliofahamu namna ya kufuata nyayo zao na kuweza kuji-pamba na mwenendo wao. Nguzo ya maadili si kitu kilichoshikamana na ukomavu katika dini. Maadili ni kuiokoa nafsi yako dhidi ya sifa za kiun-yama na badala yake kuipamba kwa sifa za kiubinadamu. Kuwa muislamu ni kushikamana na maadili ya kiislamu, kudhihirisha uzuri wake katika mwenendo na vitendo.

Pindi Qur'an inapotazamwa kwa hekima na busara si vigumu kuiona kwamba maudhui yake ni adabu na maadili. Hata visa vilivyosimuliwa vinapelekea kupata ukamilifu wa tabia.

Mawlana Rumi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Imani ni nini?” moyo wangu uliuliza. Akili yangu iliinama na kuninong'oneza kwa sikio, ‘Imani si kingine bali adabu’. Watu wabaya sit u kwamba wanajidhuru wao wenyewe bali kwa kupitia ubaya wao inaweze-kana wakaiwasha moto dunia nzima.”



### **Maadili na huduma ya mtu mwema**

Ahmed Ar-Rifai – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa akimsalimia kila mtu aliyekuwa akikutana naye. Pindi alipokuwa akisikia kuwa kuna mgonjwa ama kijijini au mjini alikuwa akiharakisha kwenda kumtembelea. Pindi alipokuwa akikutana na kipofu njiani alikuwa akim-shika mkono na kumpeleka kule alipokuwa akielekea. Pindi alipokuwa akikutana na mtu mzima alikuwa akimsaidia kubeba mizigo yake na kuwasimuliwa wale walio karibu yake msemu ufuatao kutoka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake:

“Yeyote atakayemheshimu na kumsaidia mtu mzima atajaaliwa na Mwenyezi Mungu kupata mtu ambaye atamheshimu na kumsaidia wakati wa utu uzima wake.” (Tirmidhi, Birr, 75)

Pindi alipokuwa akirejea kutoka kwenye safari ndefu alikuwa akienda moja kwa moja kwenye pori na kukata kuni na kisha kuzibeba juu ya punda wake na kisha kuwasambazia wajane na masikini.





Alikuwa akiwakimbilia watu waliokuwa na upungufu wa akili na walemavu na kufua nguo zao na kukaa nao kwa ajili ya kusikiliza matatizo yao. Kisha alikuwa akiwapakulia chakula kwa mikono yake na kuwaomba wamuombe. Alikuwa akiwaambia wanafunzi wake:

“Kuwatembelea watu hawa wenye matatizo si tu jambo lenye kupendekezwa (*mustahab*) bali ni wajibu (*wajib*)”

Siku moja watoto kadhaa waliokuwa wakicheza mtaani walikutana naye. Kutokana na kuogopeshwa na muonekano wake wa wasiwasi walikimbia. Lakini Ahmed Ar-Rifai – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akawakimbilia upesi na kuwakumbatia kwa mapenzi mmoja baada ya mwingine, kisha akawaomba msamaha kwa kusema:

“Kama mnavyoweza kuona watoto mimi mtu niliye katika shida kama nyinyi. Naomba mnisamehe...kwani sikukusudia kuwatisha!”



### **Mafunzo yatokanayo na kisa hiki:**

Njia ya hekima ya kiroho ambayo mu anaifuata ili apate radhi za Mola na funguo ya kukutana naye ni kama karatasi nyeupe isiyoandikwa kitu chochote. Wino unaotumika kuandikia kwenye karatasi hii pia ni mweupe na inaweza kusomwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu peke yake. Kwa mantiki hiyo watu wema hujitahidi katika maisha yao wasije wakadondosha doa jeusi hata kidogo katika kipande hicho cha karatasi, kiasi kwamba wanajizua kuumumiza hata siafu na hujipamba na mwenendo bora na huduma kwa Mola wao kwa kadiri wawezavyo, yote haya ni ili wapate radhi zake. Kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:

إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ التَّوَّابِينَ وَيُحِبُّ الْمُتَطَهِّرِينَ

“Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao tubu na huwapenda wanao jisafisha” (al-Baqarah, 222)



### **Waache wanaokufa wafahamu, sio walio hai!**

Katika kipindi cha mwanzo wa uislamtu mtu mmoja asiye kuwa akifa-





hamika alikuwa akiweka mfuko wa chakula katika milango ya baadhi ya masikini. Jambo hili liliendelea kwa muda mrefu mpaka ikifikia siku moja asubuhi masikini wakaamka lakini hawakukuta chochote kilichoachwa milango mwao. Huku wakiwa wanafikiria sababu iliyopelekea hali kuwa vile mara Madina ikatikiswa na habari za kifo cha Zayn'al-Abidin – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye alikuwa mjukuu wa Ali – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake. Habari zile zilimhuzunisha kila mtu.

Furaha iwaendee mashujaa wa kweli ambao wakati wanajitahidi kuboresha hali za watu kwa kupitia huduma bora wanazozitoa lakini pia wanatafuta radhi za Mola na si kufurahisha nafsi zao.



### **Usimdharau mtu yeyote!**

Imepokewa kwamba siku moja Yesu – amani iwe juu yake – alitoka nje na mji pamoja na mtu mmoja aliyechukuliwa kuwa ni mtu mwema na ambaye alikuwa akiheshimiwa na waizraeli. Mtu mwingine ambaye alikuwa na madhambi mengi na ambaye alikuwa akifahamika kwa ufisadi wake aliwafuata nyuma huku akiwa amejawa na hisia za majuto kutokana na matendo yake. Pindi waliposimama mahali kwa ajili ya kupumzika yule muovu alikaa sehemu nyingine huku moyo wake ukimuuma, pale alipokuwepo akatafuta ulinzi wa rehema za Mwingi wa rehema na kutubia kama ifuatavyo:

“Ewe Mola...Nisamehe kwa baraka za Mtume yule!”

Pindi yule mtu aliyeonekana kuwa mwema alipofanikiwa kusikia dua yake alimdharau na kumpuuzia na kisha akaomba dua yake:

“Mola wangu...Usinifufue pamoja na mtu yule katika siku ya kياما!”

Kisha Mola akamfunulia Yesu – amani iwe juu yake – yafuatayo:

“Wafahamishe waja wangu wawili kwamba nimeshapokea maombi yao wote. Nimemsamehe mja wangu aliyekuwa akijuta na nimemfanya awe miongoni mwa watu wa peponi. Na kwa huyo mwingine ambaye alionekana kuwa mwema nimemuweka mbali na pepo kutokana na kuto-taka kuwa pamoja na mtu ambaye nimeshamsamehe.”





**Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kumdharau mja yeyote wa Mwenyezi Mungu nje ya wale ambao tayari wameshakutana na ghadhabu za Mwenyezi Mungu ni sawa na kuua moyo. Ni nyoyo za mawe ambazo zipo mbali na mapenzi ya Mola ndizo zinazoweza kujiingiza kwenye mauaji haya. Pale utakapomdharau mtu si kwamba utamfanya awe chini bali wewe ndiye utakayejishusha chini na kujitengenezea maangamizi. Kwa hakika Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Kumdharau na kumchukia ndugu yako wa kiislamu kunatosha kuwa dhambi.” (Muslim, Birr, 32)

Mshairi mmoja analielezea hili kwa ufasaha kabisa kama ifuatavyo:

*Usiwadharau waovu*

*Kwani hazina nyingi zimejificha katika maharibiko*



**Usimlaumu yeyote!**

Khamdun Qassar – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Pindi umuonapo mlevi akipepesuka njiani kuwa makini usimlaumu... kwani inawezekana siku moja na wewe ukajikuta katika hali kama yake!”



**Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Mwenendo wa kisufi umejikita katika huruma na upendo; hauruhusu kubeza, kudharau na kuumiza hisia za wengine. Mola anatufunulia kwam-ba mja wake ni mwujiza utokao kwenye nguvu zake zisizo na mipaka. Hivyo hatuna budi kumuangalia muovu kama kito kilichoangukia kwe-nye matope na ambacho kinangojea kuokotwa. Kudharau kunamaanisha kukizamisha zaidi kito hicho ndani ya matope. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema yafuatayo katika kuwaamrisha waja wake wajikinge dhidi ya tabia hii yenye kuangamiza:

“Enyi mlio amini! Wanaume wasiwadharau wanaume wenzao, wala







wanawake wasiwadharau wanawake wenzao. Huenda hao wakawa bora kuliko wao” (al-Hujurat, 11).

Kuliko kupima madhambi ya wengine, jambo ambalo limekatazwa na Qur’an, mtu hana budi kupima na kuangalia madhambi yake mwenyewe. Pia imegundulika kwamba watu ambao wanatumia muda mwingi katika kuwafuatilia wengine kwa dharau wameishia kuangukia kwenye hali kama za watu hao. Ndio maana kuna msemo usemao, “Mcheke mwenzako, na wewe upatwe na kilichompata.”



### **Kuwachangamkia mayatima**

Sari-i Saqati anasimulia:

“Katika siku ya eid nilimuona Maruf-i Karhi akikusanya mbegu za tende njiani. Nikamuuliza alikuwa anataka kuzifanyia nini mbegu zile, naye akanijibu:

‘Nilimuona mtoto mdogo akilia pale. Pindi nilipomsogelea na kumuuliza sababu ya kulia kwake aliniambia kwamba yeye ni yatima ambaye hana nguo wala midoli ya kuchezea kama walivyo wenzake. Kabla ya kumaliza maneno yake akaanza kulia tena. Hali yake iliumiza moyo wangu sana. Ndipo nilipoamua kukusanya hizi mbegu unazoziona. Baada ya hapa nitaziua na fedha nitakayoipata nitanunulia mavazi na midoli kwa ajili yake.’

Maneno yake yaligusa moyo wangu pia, hivyo nikamsihi Sheikh aniruhusu ‘...nimshughulikia mimi yule mtoto.’ Aliniruhusu nifanye hivyo kutokana na wema wake, hivyo nikamchukua yule mtoto na kumpeleka sokoni na kumnunulia mahitaji yake.”

Sari-i Saqati anaelezea zaidi athari aliyopata moyoni mwake kutokana na amali hii:

“Baraka zilizotokana na kumhudumia yatima yule ziliingiza nuru ndani ya moyo wangu kiasi kwamba nikawa na ari kubwa ya kiimani ambayo sijapata kuwa nayo hapo kabla.”





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kuwachangamkia na kuwasaidia mayatima ni jambo linalopendekezwa mno na uislamu, kwani malipo yake ni makubwa mno. Ahadi ifuatayo ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – kwa wale wanaotekeleza jambo hili inatosha kuziweka nyoyo kwenye mzubao:

“Yule mwenye kumlinda yatima wake au yatima wa mwingine atakawa na mimi peponi *kama hivi*”. Malik ibn Anas – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipokuwa anasimulia *hadith* hii aliashiria kwa vidole vyake kitendo alichokionyesha Mtume pale aliposema ‘kama hivi’, alikigusisha kidole chake cha shahada pamoja na kidole kinachofuatia. (Muslim, Zuhd, 42)

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Mtu atakapohenga henga kichwa cha yatima kwa ajili ya Mwenyezi Mungu atakapa thawabu kumi kwa kila unywele unaofikiwa na mkono wake.” (Ahmed ibn Hanbal, Musnad, V, 250)

‘Kuhenga henga nywele za yatima’ kunamaanisha kusimamia mahitaji yake yote, yawe ni ya kimwili au ya kiroho.



### **Urafiki**

Sahl ibn Ibrahim anaelezea:

“Tulikuwa na urafiki na Ibrahim ibn Adham. Siku moja nilipatwa na maradhi makubwa, Ibrahim akatumia kila alichokuwa nacho kuhakikisha kwamba afya yangu inarejea. Baada ya muda nikaanza kupona taratibu. Kuna wakati nilijisikia kula baadhi ya vitu hivyo nikamuomba kama angeliweza kunipatia. Kwa kuwa wakati ule alikuwa hana kitu, aliamua kuuza punda wake ili aweze kuninunulia vitu nilivyokuwa nikivihitaji. Baadae nilipopata nafuu na kuweza kunyanyuka ndipo nilipolifahamu hili. Nilitaka kwenda mahali, hivyo nikamuomba aniazime punda wake. Nilipomuuliza juu ya mahali alipokuwa punda wake alinijibu:

“Tumemuza”

Kwa kuwa nilihisi uzito wa safari yangu ungeliveza kuniathiri kiafya, nikamuuliza:

“Sijui nifanye nini sasa?”





“Usipate tabu ndugu yangu”, akasema. “Nitakubeba mgongoni mwanangu!”. Mwishowe akanibeba mgongoni mwake na tukakatiza vijiji vitatu.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Katika nyakati nzuri kila mtu ni rafiki. Lakini urafiki wa kweli hujidhihirisha katika nyakati za shida na thamani yake huwezi kuilinganisha na chochote. Hivyo siri ya utukufu imegemea katika kuendelea kuwa rafiki wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mjumbe wake na watu wema, katika shida na tabu ndani ya maisha yako.

Kujitolea muhanga na uhisani hasa kwa waislamu wenye shida ni suala linalovuta rehema za Mola ambaye ni mwingi wa rehema na mwenye kurehemu waja wake, na ambaye amemtuma Mjumbe wake – rehema na amani ziwe juu yake – si kwa lengo jingine kinyume na kuwa rehema kwa walimwengu wote. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Mwenyezi Mungu huwahurumiwa watu wenye huruma na upole.”  
(Abu Dawud, Adab, 58)



### **Lengo la urafiki**

Abdullah ibn Mubarak – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa safarini pamoja na mtu aliyekuwa na tabia mbaya. Safari yao ilipofika mwisho na kila mtu kwenda njia yake, Abdullah ibn Mubarak alianza kulia. Rafiki zake wakamuuliza sababu ya kulia kwake kwa upole:

“Licha ya safari ndefu”, alielezea huku macho yake yakiwa yawezungukwa na machozi, “Sikuweza kurekebisha tabia hata moja ya rafiki yangu pindi tulipokuwa njiani. Sikumsaidia aweze kuboresha tabia yake. Na sasa siwezi kumsaidia bali ninafikiria kwamba makosa yangu ndiyo yaliyopelekea kushindwa kwangu kuwa msaada kwake...Ikiwa kasoro zangu ndizo zilizopelekea kushindwa kumsahihisha, itakuwaje kesho akhera pindi tutakapofufuliwa?” Kisha akaendelea kulia kwa masikitiko.





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Urafiki hauna budi kujengwa katika misingi ya malengo ya kiroho. Hivyo kufanya urafiki na kuwa karibu na watu wema hakuna budi kuwa kwa lengo la kufaidika kutoka kwao na kufanya urafiki na watu walio dhafifu kiimani hakuna budi kuwa kwa lengo la kuwasaidia kiroho. Urafiki uliojengwa kwa lengo la kupata raha na kutojijusisha na manufaa ya kiroho utampelekea mtu kukosa furaha hapa duniani na kesho akhera. Hautakiwi kupuuzia hata athari ndogo iliyotokana na urafiki wa aina hiyo; kwani tabia na matendo hutoka kwa rafiki mmoja na kwenda kwa mwingine.

Kama katika kuboresha hali zao njia zote hazitazaa matunda, basi njia ya kufuatwa ili kuwasahihisha watu hawa dhidi ya kasoro zao si kuumizi hisia zao kwa kuwalaumu. Badala yake mtu anahitajika kujiuliza mwenyewe, kwani huenda tatizo likawa upande wake. Kwani ikiwa kasoro na makosa yetu ndivyo vilivyopelekea mtu akashindwa kumsahihisha mwingine, hilo linamaanisha kwamba kesho akhera tutajibu kuhusiana na hilo. Lengo si kuwa kama pazia bali ni kufunua mapazia yote na kudhihirisha ukweli.



### **Kujisalimisha moja kwa moja**

Qur'an inatuelezea namna Mwenyezi Mungu alivyomuamuru Musa – amani iwe juu yake – kama ifuatavyo:

“Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepindukia mipaka...” (Taha, 24).

Kwa kuwa Musa – amani iwe juu yake – hakumfikiria mtu yeyote ambaye anaweza kumuachia familia yake na kondoo, aliuliza:

“Vipi kuhusu familia yangu na kondoo wangu ewe Mola?”

Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akamkumbusha Mjumbe wake juu ya kuwa kwake mbora wa walinzi, kwa kusema:

“Unataka nini kingine ewe Musa baada ya kunipata Mimi? Kimbilia kwenye kutekeleza agizo langu! Jikurubishe na kujisalimisha kwangu! Kama nikitaka ninaweza kumuweka mbwa mwitu akulindie kondoo wako na malaika wakulindie familia yako! Ni kipi kinachokusumbua ewe Musa? Ni nani aliyekuoka pindi mama yako alipokuweka kwenye mto? Na ni





nani aliyekuunganisha na mama yako baada ya pale? Kumbuka wakati ulipomuua mtu kwa bahati mbaya na Firauni akawa anatafuta kichwa chako...Ni nani aliyekulinda dhidi yake wakati ule?”

Musa – amani iwe juu yake - akawa wakati wote huo anasikiliza kwa umakini na kujibu kila swali kwa kusema:

“Wewe, Wewe, Wewe, Mola wangu!”

### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Bila shaka Musa – amani iwe juu yake – alikuwa katika kilele cha unyenyekevu kama walivyo Mitume wote. Lakini kwa kuwa Mitume huwa ni mifano ya kuigwa na wanadamu Mola huwafanyia mambo mengi ya muhimu ili sisi tuweze kupata mazingatio kwa kupitia wao pindi tutakapokutana na hali kama zao. Funzo tunalolipata katika simulizi iliyotangulia ni kwamba hakuna sababu inayokubalika mbele ya amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu ambaye ndiye Mola wa walimwengu wote. Baraka na ulinzi hupatikana kutoka kwake pindi unapotekeleza amri yake. Kama mja atajitahidi kutekeleza amri zake kwa ajili ya kupata radhi zake, basi ataona kwamba Mola anamsaidia katika hali yoyote anayokutana nayo. Mlinzi Mkuu ndiye aliyemnyanyua Musa – amani iwe juu yake – katika kasri la Firauni, na ndiye aliyemzamisha Ibrahim – amani iwe juu yake – ndani ya bustani la mawaridi katikati ya moto mkubwa wa Namrut, na ndiye aliyewalaza watu wa pangoni zaidi ya miaka mia tatu ili kuwalinda dhidi ya madhalimu na ndiye aliyemlinda Muhammad Mustafa – rehema na amani ziwe juu yake – dhidi ya matishio mengi kama vile kumficha dhidi ya macho ya upelelezi ya maadui zake ndani ya pango la thawr. Mshairi anasema:

*Sitarajii msaada wa yeyote, Mola ndiye mlinzi wangu,  
Ninamuamini Yeye, 'Kwani Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi bora'  
Sayri*



### **Kupokea maombi ya muumini**

Ilikuwa ni siku ambayo Maruf-i Karhi alikuwa kwenye fungu isiyo ya wajibu. Wakati alipokuwa anakatisha sokoni mchana alimuona mbeba maji akiomba:





“Mwenyezi Mungu amtibu yeyote atakayekunywa maji haya kwa baraka na rehema zake!” Hivyo Maruf akavutiwa na wito ule na kuamua kuvunja funga yake na kunywa yale maji.

“Kwa nini umevunja funga yako?” walimuuliza wale waliokuwa karibu yake.

“Ili niweze kupata baraka za maombi ya yule mtu”, alijibu.

Baada ya Maruf-i Karhi kufariki rafiki yake alimuona kwenye ndoto; na baada ya kulikumbuka lile tukio, alimuuliza, “Mwenyezi Mungu alikutibu vipi?”

“Kutokana na baraka za maombi ya mbeba maji Mola wangu ameni-samehe na kunitibu kwa huruma.”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kuna watu wengi waliotengwa na jamii ambao nyoyo zao zipo na Mola wao wakati wote, na ambao wakati mwingine maombi yao yanaweza kuwa ya thamani kubwa kuliko malipo ya matendo ya wajibu. Lakini hatuna budi kufahamu kwamba funga za sunnah zilizovunja kwa lengo la kupata wema mkubwa zaidi zinatakiwa zilipwe baadae, kwani kukamilisha funga iliyokatizwa ni lazima (wajib) hata kama mwanzoni ilikuwa si ya wajibu. Tukio lililotangulia linaashiria kwamba ni jambo jema kuchagua kitu cha muhimu zaidi juu ya kile chenye umuhimu mdogo. Kwani kuna wakati ambao vitu vinavyoonekana ni vidogo vinaweza kuzungukwa na manufaa makubwa. Kwa upande mwingine ni kwamba namna iwezekanavyo kuwepo hazina zilizochimbiwa ndani ya majengo yaliyohamwa, ndivyo ambavyo kunaweza kuwepo kwa watu ambao licha ya kuonekana kana kwamba wametelekezwa kwa nje, lakini kwa ndani wanaweza kuwa lulu zenye thamani kubwa. Hivyo hatuna budi kujihadhari dhidi ya kuwapuu-zia watu wa namna hiyo. Maneno yafuatayo yanalielezea hili kwa ufasaha zaidi:

*Uone kila usiku kuwa ni Qadr, kila mtu ni Khidr,*

*Unaangaliwa, mbingu nane zinakusubiri.*

*Sayri*

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:





“Je niwafahamishe kuhusiana na watu wa peponi? Hao ni wale ambao watu wengi wanawapuuzia, kwa kuwa ni madhaifu na wanaonekana kuwa madhaifu; lakini lau kama wangelipia kwamba ‘hiki na kile kitatokea’, kwa hakika Mwenyezi Mungu angelijaalia viapo vyao kuwa vya kweli.

Je niwafahamishe kuhusiana na watu wa motoni? Hao ni wale walio na nyoyo ngumu, makatili, madhalimu na wenye kujivuna, wale ambao wanatembea kwa kiburi” (Bukhaii, Aymaxi, 9; Muslim, Jannah, 47)



### ***Majzub na tiba ya moyo wenye maradhi***

Bayazid-i Bistami – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alimkuta daktari akiandaa dawa akamuuliza:

“Daktari, je una dawa ya maradhi yangu?”

“Una maradhi gani?” daktari alimuuliza.

“Dhambi”, alijibu.

Huku akiwa amenyong’onyea na kunyoosha mikono yake pande zote alisema, “Sifahamu dawa ya maradhi ya dhambi?”

Muda si mrefu *majzub* mmoja kijana aliyekuwepo karibu yao na ambaye aliyasikia mazungumzo yao aliwakatisha na kusema:

“Ninafahamu baadhi ya dawa za maradhi yako!”

“Niambie ewe kijana”, Bayazid alimsihi kijana yule huku akionekana kuwa ni mwenye furaha. Licha ya kijana yule kuonekana mwendawazimu lakini ukweli ni kwamba kijana yule alikuwa ni mtu mwenye hekima. Hivyo akaanza kuelezea vitu vinavyotakiwa katika kutengeneza dawa ya kutibu madhambi:

“Chukua dirham kumi za mizizi ya majuto na dirham kumi za toba! Ziweke kwenye sinia la moyo wako na kisha uziponde kwa nyundo ya *tawhid*. Kisha chekecha kwa chekecheo la wema na ukande mchanganyiko huo kwa machozi. Baada ya hapo upike kwenye jiko la upendo! Kisha utapata mchanganyiko ambao utautumia kwa kupima vijiko vitano kwa siku. Fanya kama nilivyokuelekeza muda si mrefu maradhi yako yatatoweka!”





Bayazid-i Bistami akavuta pumzi na kusema:

“Huzuni iwe juu ya wale wanaodhania kwamba wewe umechanganyikiwa na kujiona wao ni wenye ak ili!”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Pindi mtazamo wa mtu mbele ya Mola unapokuwa muhimu kuliko muonekano kwa watu, njia za ukomavu na hekima huwa pana. Kisha uoni, usikivu na hisia za mtu huanza kuzama kwenye kina cha ajabu. Watu wengi wa namna hii huwa watu wa namna ya Uways al-Qarani, yani watu ambao wanapuuziwa na watu na kuonekana wamechanganyikiwa. Lakini ukweli ni kwamba kwa kuwa amefikia kwenye urafiki wa kipekee na Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mjumbe wake ndio maana anaonekana kama hivyo.

Tukio lililotangulia pia linaashiria baraka za amri takatifu isemayo, “kuweni pamoja na wakweli!” (at-Tawbah, 119). Kama tulivyoona kwenye maneno ya hekima ya kijana yule, dawa inayotolewa na watu wema huwa ni tiba ya nyoyo zenye maradhi, pamoja kuziunganisha na Mola huku zikiwa na afya na imara zaidi. Cha zaidi ni kwamba suala kwamba Bayazid-i Bistami anaomba dawa ya moyo licha ya kuwa na moyo uliohuika na ulio imara kiimani, linadhihirisha unyenyekevu wake na cha zaidi alichochewa na lengo la kutoka kutibu moyo wa yule daktari.



### **Sura kama malaika**

Tulikuwa tumeongozana na marehemu Sami Effendi pamoja na baba yangu Musa Effendi – Mwenyezi Mungu azitakase siri zao, baba yangu alikuwa akimsindikiza Sami Effendi ambaye alikuwa akirejea Istanbul kutoka Bursa. Tulikuwa tunataka kupanda kivuko cha magari cha Yalova tukiwa tunataka kwenda upande wa pili wa bahari ya Marmara, tulikuwa tunakaribia kujipanga katika mstari pamoja na magari mengine. Mhudumu aliyekuwepo pale na ambaye alipewa jukumu la kuhakikisha kuwa magari yote yapo katika mistari iliyonyooka mara alimuona Sami Effendi na Musa Effendi wakati alipokuwa anatuelekeza kuliweka gari letu katika sehemu







husika. Alipatwa na mshangao kisha akatulia kidogo. Kisha akatusogelea karibu. Pindi alipoangalia ndani ya gari kwa ukaribu zaidi alivuta pumzi kwa nguvu na kusema:

“Mola ni mwema, dunia ni yenye kustaajabisha sana! Kuna sura kama malaika...na kuna sura nyingine kama Namrut...”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Tukio hilo linaonyesha kwamba dalili ya kuwa ‘rafiki’ wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni kwa moyo na uso kumulikwa na nuru yake tukufu. Watakatifu ni wale ambao pindi mtu anapowaona humkumbuka Mola wao kwa kuwa njia yao ni njia ya Mola. Hawa ni watu wenye kufuata nyayo za Mtume Muhammad Mustafa – rehema na amani ziwe juu yake, Mtume ambaye ndiye kiongozi wetu wa kutuelekeza kwenye haki. Kwa hakika uso na muonekano wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – vili-kuwa vikimkaribisha mtu kwa Mola wake bila ya hata kutumia maneno ya kumkaribisha mtu. Abdullah ibn Salam – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – ambaye ni mwanachuoni mkubwa miongoni mwa mayahudi, pindi alipomuona Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – kwa mara ya kwanza alikiri:

“Sura kama ile haiwezi kuongopa.” Hili peke yake lilitosha kumshawishi kuingia ndani ya uislamu. (Tirmidhi, Qiyamah, 42; Ahmed ibn Hanbal, Musnad, V, 451)

Hivyo kila mahali mja anapoenda huacha kiasi fulani cha mvuto kisi-choisha, ama uwe mzuri au mbaya; tabia na msimamo wake huongea na hukutana na macho ya wengi yaliyo na mazingatio na yasiyo na mazingatio. Si jambo geni kuona namna watu wanavyopenda mwenendo wa mtu katika jamii na kuamua kuufuata.

Hatuna budi kutambua kuwa ulimwengu ndicho chanzo cha furaha, furaha ambayo ni ubainifu wake mkubwa unamhusu mwanadamu. Watu wema na waliokomaa kiimani ambao wanahusika katika furaha hii takatifu huwa ni watu ambao kamwe hawafutwi katika historia; kwani maisha yao huendelea hata baada ya kufa kwao, haya ni malipo yatokanayo na kuishi kwao katika mwenendo ambao unafaa kuigwa na wanadamu wote.





### **Hali ya moyo wakati wa sadaka**

Musa Effendi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasimulia:

“Tulikuwa safarini pamoja na Sami Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake. Tulipofika mahali fulani ndani ya mji wa Urgup mtu mmoja alisimamisha gari letu na kuomba hela ya sigara. Licha ya kuwepo upinzani wa kimya kimya wa wasafiri wengine, Sami Effendi alisema:

‘Kwa kuwa anaomba hiyo hela hatuna budi kumpe anachokitaka,’ na alihakikisha yule mtu anaipata ile hela. Baada ya kupokea ile hela, yule mtu aliyekuwa mwerevu mara akabadilisha nia yake na kusema:

‘Sasa hivi nitaenda kununua mkate kwa hii hela.’ Kwa mbali alionekana kuwa ni mwenye furaha.”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Matendo yaliyotendwa kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu hupata njia ya kuingia ndani ya moyo na kuboresha mwenendo wa mtu. Hivyo cha muhimu katika sadaka si hali ya ndani ya mpokeaji bali ni hali ya ndani ya mtoaji. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Siku moja mtu mmoja aliahidi katika nafsi yake kwamba angelitoa sadaka. Wakati wa usiku akaondoka nyumbani kwake huku ameshikilia sadaka mkononi, bila ya kujua alimpa mwizi ile sadaka. Siku iliyofuata mtaani kukawa na maneno ‘...ni jambo la kustaajabisha kwamba jana usiku mwizi alipewa sadaka!’

Baada ya yule mtu kuyasikia maneno hayo akasema, “Ahsante Mola wangu. Kwa hakika nitatoa sadaka nyingine’

Kisha akaondoka tena nyumbani kwake huku ameshikilia sadaka mkononi mwake na bila kujua akaiweka mikononi mwa malaya. Siku iliyofuata watu wakawa wanasema kwamba ‘malaya alipewa sadaka!’

“Ahsante Mola wangu kwa kunijaalia kutoa sadaka ijapokuwa ni kwa Malaya, kwa hakika nitatoa tena sadaka,’ yule mtu alisema.

Usiku wake akatoka tena huku akiwa ameshikilia sadaka mkononi mwake na bila kujua alimpatia sadaka ile tajiri. ‘Ni nini kinaendelea?’ walistaajabu watu wa mji. ‘Wakati huu tajiri ndiye aliyepewa sadaka!’





‘Ahsante Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kutoa sadaka ijapokuwa nilimpa mwizi, malaya na tajiri!’

Kutokana na usafi wa moyo wake, mtu yule aliambiwa yafuatayo ndani ya ndoto:

“Sadaka uliyompa mwizi inaweza ikamfanya ahisi aibu kutokana na kuiba kwake na ikamfanya aachane na wizi. Sadaka uliyompa Malaya inaweza ikamfanya aachane na umalaya na kuishi maisha ya wema. Na tajiri anaweza akapata fundisho kutokana na sadaka yako na kuamua kutoa mali yake kwa ajili ya kuwasaidia wasiojiweza!” (Bukhari, Zakat, 14; Muslim, Zakat, 78)

Kwa kuwa ushawishi wa sadaka iliyotolewa ni mkubwa na unalingana na usafi wa moyo wa mtu, hivyo mtoaji hana budi kuwa katika hali ya kuonyesha shukurani kwa Mola.



### **Matendo mema ambayo yanakifikia kiti cha enzi**

Siku moja mwanafunzi wa Dawud-I Tai ambaye alikuwa akimhudumia Sheikh alisema, “Nimepika nyama. Je ungelipenda nikuletee kidogo?”

Pindi alipomuona mwalimu wake amenyamaza kimya aliamua kuleta sahani iliyojaa nyama na kuiweka mbele yake. Lakini bila hata ya kukiangalia chakula kilichokuwa mbele yake Dawud-I Tai – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – aliuliza:

“Vipi kuhusu yatima fulani na fulani ewe mpendwa?”

Yule mwanafunzi akavuta pumzi kidogo na ili kuashiria kwamba walikuwa hawana mahitaji ya kutosha alijibu kwa kusema “Hali yao ni ile ile mwalimu”

“Kama ni hivyo wapelekee hiki chakula!” Sheikh yule mkubwa alimshauri.

“Lakini umepita muda mrefu tokea ule nyama ewe mwalimu”, mwanafunzi yule alisema kwa upole kwa lengo la kumtaka mwalimu wake ale kile chakula. Lakini bado alishikilia msimamo wake ule ule na kusema:

“Kama nikikila hicho chakula kitakuja kutoka. Lakini kama watakila mayatima kitapita mpaka kwenye kiti cha enzi cha Mola!”





### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kama ilivyo vigumu kwa jua kuacha kutoa joto ndivyo ilivyo vigumu kwa wanadamu wenye imani ya juu kuacha kuhisi huruma juu ya wengine na kutohisi chochote katika maumivu na matatizo yao. Huruma ni hazina tukufu iliyoenea ulimwenguni kote. Na nyoyo za watu wema ndizo zilizo na sehemu kubwa ya hazina hiyo ya huruma. Machoni mwao wanapendezewa na malipo yanayowangojea baada ya kujitenga na matamaniao ya kidunia yenye kupita na kuzipamba nafsi zao kwa matendo mema ambayo si kwamba yanastawisha nafsi peke yake bali pia ni ya milele. Faida kubwa ambayo mwanadamu anaweza kuipata katika ardhi ni kwa kupitia matendo mema. Vitu vingine ni amana alizopewa mwanadamu kwa muda mfupi, hili linathibitishwa na tukio lifuatalo:

Siku moja familia ya Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – ilichinja kondoo. Baada ya sehemu ya nyama yake kutolewa sadaka Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – aliuliza ili afahamu ni kiasi gani cha nyama kilichobakia.

“bega peke yake”, Aisha – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alitoa taarifa.

“Hilo linamaanisha kuwa yote ni ya kwetu isipokuwa bega moja!”, Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – alisema. (Tirmidhi, Qiyamah, 33)



### **Kumtambua Mola wakati wote**

Abdulqadir Jilani – Alalh aitakase siri yake – anasimulia hali iliyowahi kumkuta yeye binafsi:

“Siku moja mwanga ulijitokeza mbele ya macho yangu na muda si mrefu ukaenea mahali pote. Huku bado nikitafuta ili nijue ni nini kilikuwa kimetokea mara nikasikia sauti kutoka kwenye ule mwanga:

‘Mimi ni Mola wako ewe Abdulqadir’, ilisema. ‘Nimevutiwa sana na matendo mema ambayo umeshayafanya mpaka sasa, na nimefanya kila lililo la haramu kuwa halali kwako!’

Lakini pindi maneno yale yalipomalizika tu nikagundua kuwa sauti ile ilikuwa ikitoka kwa Shetani aliyelaaniwa na hivyo nikasema:





‘Nenda zako ewe kiumbe fedhuli! Mwanga unaouonyesha si chochote bali ni kiza kikuu kwangu!’

‘Nimekukosa tena kwa kupitia hekima uliyopewa na Mola wako, alisema. ‘Lakini mpaka leo hii nimeweza kudanganya maelfu ya watu kwa kutumia hila hii!’ Kisha ule mwanga ukatoweka.

Kisha nikanyanyua mikono yangu na kumshukuru Mola wangu huku nikifahamu fika kwamba ile ilikuwa ni rehema kutoka kwake.”

Mtu mmoja aliyemsikia akisimulia tukio hili alimuuliza, “Ulijuaje kuwa sauti ile ilikuwa ni ya shetani?” Abdulqadir Jilani – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – akajibu:

“Pale aliposema, ‘nimefanya kila lililo la haramu kuwa halali kwako”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Katika nyakati zote na sehemu mbalimbali kumekuwepo watu ambao hujaribu kupotosha dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu. Wakati ambao jambo hili lenye kuangamiza linapokuwa zito zaidi muumini hana budi kujitahidi kuweza kutofautisha kati ya zuri na baya, kosa na sahihi. Leo hii tukio kama hilo lipo, kuna watu wanaofahamika kuwa ni wanachuoni lakini wanajitahidi kubadilisha mambo ya haramu katika uislamu na kuyafanya yaonekane ni halali na kinyume chake, na wakati huo huo wakiharibu mshikamano wa kijamii. Hivyo tabia na maamuzi mazuri ya Abdulqadir Jilani – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – yana umuhimu mkubwa kwetu sote. Bila shaka njia yake ya maamuzi iko wazi: Kamwe Mola hampi mtu kitu ambacho hakuwahi kumpa hata Mtume. Je shetani na wale wanaojifanya ni wanachuoni wanaweza kuwa na utambuzi mkubwa katika halali na haramu, jema na baya kuliko Mitume? Haiwezekani! Mwenyezi Mungu anatuma tahadhari kali kwa watu wanaofikiria kinyume na hayo:

“Sema: Ati ndio mnamfundisha Mwenyezi Mungu Dini yenu, na hali Mwenyezi Mungu anayajua ya katika mbingu na ardhi, na Mwenyezi Mungu anajua kila kitu?” (al-Hujurat, 16)





### ***Karim* ndiye ninayemuhitaji**

Bayazid-i Bistami anaelezea:

“Siku moja nilitaka kuvuka upande mwingine wa Tigris. Nipofika karibu na ufukwe pande zote mbili za mto ziliungana ili kurahisisha njia. Pindi nilipopata fahamu nilijisemea moyoni:

“Kwa hakika siwezi kudanganywa na jambo hili; kwani watu wa meli humvusha mtu kuelekea kwenye upande mwingine kwa nusu ya sarafu. Lakini kwa kuungana kwako unaniomba miaka yangu thelathini ya matendo mema! Samahani lakini siwezi kupoteza amali ambazo nimeziandaa kwa ajili ya siku ya kiama kwa ajili ya kupata thamani ndogo zaidi ya nusu ya sarafu! *Karim* (Mwingi wa ukarimu) ndiye ninayemuhitaji, na si *karamah*.”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

*Karamah* ambayo ndiyo inayopendwa na nafsi ina tatizo kubwa kwa watakatifu. Malipo ya kuipuuzia *karamah* ni ama uchovu wa muda mfupi, gharama ndogo kutoka mfukoni au kutotambulika mbele ya macho ya watu. Lakini malipo ya kuikumbatia *karamah* yanaweza kuwa malipo yako yote ya mpaka wakati huo na kufilisika kiimani, jambo linamfanya mtu akose kitu cha kwenda nacho huko akhera. Isipokuwa kwa zile *karamah* ambazo zimejidhihirisha kuwa zimetoka kwa Mola, watakatifu wamekuwa wakizikumbatia *karamah* hizi ambazo ni muhimu katika kutambulika na kukubalika katika jamii, lakini wakati wote huegemea katika kupata radhi za Mola ambaye ni *Karim*.

Yafuatayo ni maneno yenye maana kubwa kuhusiana na suala hili na yametolewa na Sahl ibn Abdullah at-Tustari:

“Kubadilisha tabia mbaya kwa tabia nzuri ndio *karamah* kubwa kuliko zote. Kwa hakika baadhi ya *karamah* ni midoli anayobembelezewa mtoto mwenye kulia. Watakatifu kamwe hawaitaki *karamah* hii; wajinga peke yao ndio wanaoitaka. Huwa wanajifurahisha wao wenyewe na wengine kwa kupitia *karamah* hiyo.”

Hivyo nukta muhimu zaidi kupita zote ni:

“...simama sawa sawa kama ulivyo amrishwa” (Hud, 112).





### **Jukumu la mtangulizi**

Siku moja Imam Abu Hanifah alimuona mtoto akitembea kwenye matope. Baada ya kumuonyeshea tabasamu la huruma alisema:

“Kuwa makini mpendwa usije ukateleza na kuanguka!”

Yule mtoto akamgeukia Imam huku macho yake yakiwa yanang’aa kwa ufahamu na kumpa jibu lifuatalo ambalo hakulitarajia:

“Kwangu mimi kuanguka si kitu ewe Imam. Bali wewe ndiye unayetakiwa kuwa makini...kwani kama utateleza basi wale wote wanaokufuata na kuegemea kwenye kila neno lako wataanguka na itakuwia ugumu sana katika kuwasaidia wanyanyuke!”

Imam akaanza kulia baada ya kutekwa na maneno ya busara ya mtoto yule. Aliwageukia wanafunzi wake na kusema:

“Kama mtapata dalili madhubuti kuhusiana na jambo fulani basi msifuate hukumu yangu. Hiyo ni dalili ya ukomavu katika uislamu...na kwa njia hii ndipo mapenzi na ukaribu wenu utakapodhihirika...” (Khashiyat’u Ibn Abidin, I, 217-219, Dimashq, 2000)



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kuwa mbele katika njia ya haki huwa ni jambo lenye baraka ingawa pia huwa na kuwajibika kukubwa. Waliotangulia huwashawishi wengine kwa kupitia tabia zao nzuri; lakini bado kasoro na makosa yao yanaweza kutafsiriwa vibaya na kuonekana kuwa ni sahihi na hatimaye watu kushikamana nayo. Hivyo maimamu wakubwa kama Abu Hanifah si tu kwamba walilitambua suala hili muhimu wakati wa kupitisha maamuzi, bali pia waliishi ndani ya misingi ya kiuchamungu. Baada ya Imam Abu Hanifah kuondoa doa dogo la uchafu kutoka kwenye shati lake, aliulizwa:

“Kulingana na hukumu uliyoiipitisha kuhusiana na suala hilo ni kwamba kiasi cha uchafu kilichopo kwenye shati lako hakikufanyi ushindwe kuswali. Kwa nini umejihangaisha hivyo?”

“Hiyo ilikuwa ni hukumu, lakini huu ni uchamungu!”, Imam alijibu.

Hicho ndicho kiwango pekee ambacho kinatosha kubadilisha wajibu wa aina zote juu ya Muumba na viumbe na kuwa sababu ya furaha katika maisha ya akhera!





### **Kuhudhuria mwaliko wa Mola**

Hasan Basri – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – anasema:

“Kondoo wapo makini zaidi ya wanadamu, kwani pindi mchungaji anapowaita, huacha kula na kumsikiliza. Tunaweza kusema nini kuhusiana na mtu ambaye anashindwa kuchukua mazingatio katika hili na kubakia kuwa kiziwi kwenye mwaliko wa Mola?”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Mwaliko unaweza kuwa wa aina nyingi. Kama mwaliko unatoka kwa mtu usiyempenda ni tofauti na ule unaotoka kwa rafiki yako kipenzi. Hivyo hatuna budi kuitikia mwaliko wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa moyo safi na wenye kutiririkiwa na furaha ya unyenyekevu. Hatuna budi kuzipima nyoyo zetu ili kuona ikiwa zinapata shauku na raha pale adhana inaposikika mara tano kwa siku. Mawlana Rumi analielezea jambo hili kwa vizuri zaidi kama ifuatavyo:

“Yakusanye matendo yako! Kwa kuwa Mola wako anakuamrisha, basi geuza kichwa chako kuwa miguu kama ikibidi, na kisha ukimbie...kwani mwaliko wake humtukuza mwanadamu, humuongeza imani na baraka za milele!”



### **Umuhimu wa Halal**

Siku moja mwanafunzi mmoja wa Abu Abbas Nihawandi – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – ambaye alikuwa tajiri alimuuliza Sheikh juu ya mtu aliyekuwa akistahili zaidi kupokea sadaka zake.

“Yeyote ambaye moyo wako umemridhia”, Sheikh alimshauri.

Yule mwanafunzi aliuchukua ushauri huu na kuuweka moyoni na kuondoka. Njiani alikutana na kipofu ambaye alikuwa akiomba omba mtaani. Kutokana na kuvutiwa na mtu yule, yule mwanafunzi alitoa pochi yake iliyojaa sarafu za dhahabu na kumpa yule mtu. Yule kipofu aliipapasa ile pochi kwa mikono yake na kuondoka zake kwa furaha. Siku iliyofuatia akawa anatembea kwenye mtaa ule ule, yule mwanafunzi akafanikiwa







kusikia mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kati ya yule kipofu aliyem-saidia siku iliyotangulia na kipofu mwingine.

“Jana mtu mmoja alinipa pochi iliyojaa dhahabu”, yule mtu alikuwa akimwambia rafiki yake. “kisha nikaenda kwenye kilabu ya pombe na kulewa...”

Yule mwanafunzi akaenda kwa Abu Abbas - Mwenyezi Mungu aita-kase siri yake – huku akiwa ameghadhibika. Alikuwa ndio anataka kum-simulia kitendo kile lakini bila hata ya kupewa fursa ya kuongea Sheikh alimpa sarafu aliyokuwa ameipata baada ya kuuza taqiyah yake na kum-wambia yule mwanafunzi:

“Mpe sarafu hii yeyote wa kwanza kukutana naye!”

Mwanafunzi yule akaondoka sehemu ile bila ya kuweza kuzung-umza chochote, ili aweze kutekeleza jukumu tukufu alililokuwa amepewa. Akampa ile sarafu mtu wa kwanza kukutana naye ili kuendana na ombi la sheikh wake. Lakini alimfuatilia yule mtu kwa shauku kubwa. Mara mtu yule akaishia kwenye viunga vya mji, mahali ambapo aliingia kwe-nye nyumba iliyotelekezwa. Kisha akatoa mfukoni mwake ndege mdogo aliyekufa na kumuweka chini. Pindi alipotaka kuondoka eneo lile yule mwanafunzi alimsogelea na kumwambia:

“Tafadhali niambie ukweli. Vipi kuhusiana na yule ndege mdogo ali-yekufa ambaye umemuacha pale?”

Alipoona ameulizwa na yule mwanafunzi ambaye ndiye aliyempa ile sadaka alianza kuelezea kwa kigugumizi:

“Nilikosa kitu cha kuulisha familia yangu kwa siku saba. Mimi na mke wangu tulikuwa tukijitahidi kuvumilia kwa kadiri ya uwezo wetu, lakini watoto wetu hawakuweza kuvumilia tena...Na kuwaomba watu ni jambo nisiloweza kulifanya. Nilipokuwa ninaumiza kichwa nilipata ndege mdogo ambaye alikuwa anakaribia kuoza na ambaye alikuwa hafai kuliwa. Kwa kuwa nilikuwa na shida kubwa nilifikiria kumchukua na kumpeleka kwa wanangu kwa ajili ya kumla. Lakini kichwani mwangu nilikuwa nikimuomba Mola anisaidia...Na pale ndipo ulipotokea wewe na kunipa ile sarafu. Na baada ya pale nilimshukuru Mola na kuja hapa kwa ajili ya kumtupa huyu ndege aliyekufa. Na sasa hivi nina nia ya kwenda sokoni kwa ajili ya kununua chochote cha kula...”

Huku akiwa ameduwaa yule mwanafunzi hakuchelewa akaamua





kwenda moja kwa moja kwa Sheikh. Kabla ya kusema chochote Sheikh alisema:

“Mwanangu, inaonekana hukuwa makini kuangalia ikiwa kipato chako kilikuwa kimechanganyika na halal au la. Ndio maana sadaka yako ikapotelea kwenye pombe ingawa ulikuwa makini katika kumtafuta mtu sahihi. Namna unavyoichuma mali ndivyo inavyotumika. Sababu iliyopelekea sarafu yangu moja kuangukia kwenye mikono ya mtu mwema, kinyume na pochi yako iliyojaa dhahabu ambayo iliangukia kwenye mikono ya mlevi, ni kwamba sarafu yangu ilitokana na mafuta ya bega...kwa maneno mengine, ilikuwa ya halali”



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Kila kitu hupata na kupoteza thamani yake kulingana na sifa yake nzuri au mbaya. Ukweli huu unahusiana moja kwa moja na halali na haramu. Kuna msemu wa zamani unaohusiana na utajiri na mali na ambao unatoa maana ya ndani ya ukweli huo:

“Kinachotoka kwa *Hayy*, huenda kwa *Hu*” (*Haydan gelen huya gider*)

Msemu huu una maana mbili. Ya kwanza ni kwamba, kile kinachotoka kwa *Hayy* (Aliye Hai) au Mola, hurejea kwa *Hu*, yani huyo huyo Mola. Maana ya pili ni ‘njoo kwa wepesi na uende kwa wepesi’; yani, kipato kilichopatikana kwa njia zisizoruhusiwa hupotea pasipo na faida. Kwa ufupi ni kwamba wakati halali inazaa halali, pia haramu huzalisha haramu nyingine. Maneno yafuatayo ya Abu Bakr Warraq – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – yanaliezeza hili kwa upana zaidi:

“Pindi ninapoamka asubuhi huwa ninawaangalia watu wanaonizunguka na kuwatambua wanaoishi kwa halali na wanaoishi kwa haramu”.

“Kwa namna gani?” aliulizwa.

“Pindi ninapomuona mtu ambaye anapoamka tu asubuhi anajiingiza kwenye mazungumzo ya upuuzi, anasengenya na kulaani, basi ninatambua kuwa hali hii inasababishwa na haramu anayotumia. Na yeyote anayeamka asubuhi na kujishughulisha na utajo wa Mola na kuomba toba kwa majuto, huweza kufanya hivyo kutokana na halali anayoitumia. Halali na haramu hudhihirika kwenye tabia za watu kulingana na sifa walizonazo”





### **Kipato cha halali**

Imam Abu Hanifah alikuwa ni mtu mwenye mali nyingi, alikuwa akipata kipato chake kwa kupitia biashara. Kutokana na kuwa kwake mwanachuoni aliyetingwa na mambo mengi alikuwa akiendesha biashara zake kwa kupitia kwa wawakilishi wake na yeye binafsi alikuwa akikagua mahesabu ili aone kama biashara ilikuwa ikiendana na viwango vya halali. Alikuwa makini mno katika suala hili kiasi kwamba siku moja kabla ya kumtuma mwenzi katika biashara aliyetitwa Hafs ibn Abdurrahman ili aende akauze vitambaa, alimshauri kwa kumwambia:

“Kaziuze hizi kwa bei ya chini, kwani vitambaa hivi vina kasoro kidogo.”

Hafs aliishia kuviuza vitambaa vile kwa bei aliyokuwa ameshauriwa na Imam, lakini alisahau kuwafahamisha wateja juu ya kasoro za bidhaa walizokuwa wamezinunua. Baada ya Imam kugundua vile alimuuliza Hafs ikiwa alikuwa akimfahamu mteja ili aweze kuwasiliana naye. Lakini ikatokea kwamba Hafs hakuwa anamfahamu yule mtu. Kutokana na kuhofia kwamba kipato kile ni chenye kutia wasiwasi Imam Abu Hanifah alitoa sadaka fedha zote zilizokuwa zimepatikana kwa kupitia mauzo yale. Kiwango cha uchamungu cha Imam kilimzidishia baraka katika mauzo yake yote, kifedha na kiroho.



### **Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:**

Ili kufahamu kama mtu fulani ni mwema na mwenye moyo safi huna budi kutazama amali anazozitekeleza kama ziko katika kiwango kizuri cha kiroho. Hasa mtu hana budi kuangalia ikiwa tabia zake zinaendana na maadili ya uislamu ama la, na ikiwa kipato chake kinapatikana kwa kupitia njia za halali ama la. Pindi Omar – radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – alipomsikia mtu akimsifu mtu mwingine alimuuliza ikiwa alikuwa amefanya hata kimoja wapo kati ya vitu vitatu ambavyo vingeliweza kuthibitisha sifa zake:

“Je umewahi kuishi naye jirani, kusafiri naye au kufanya naye biashara?”

Mtu yule alipotoa jibu hasi kwa maswali yote matatu Omar - radhi za





Mwenyezi Mungu ziwe juu yake – akaendelea kwa kusema:

“Kama ni hivyo basi usimsifu, kwani humfahamu vizuri!”

Hivyo Sufyan-i Sawri – Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – amesema:

“Uchamungu wa mtu unategemeana na kiwango cha uhalali katika kipato chake.”

Siku moja aliombwa aelezee faida ya kuswali katika jamaa, katika safu ya kwanza.

“Kwanza angalia mahali unapopatia mkate wako ewe ndugu” alijibu. “Tkiwa kipato chako ni cha halali kuwa huru kuswali kwenye safu yoyote utakayo...hakuna tatizo.”

Marehemu Musa Effendi - Mwenyezi Mungu aitakase siri yake – alikuwa akisimulia uzoefu wake katika kuelezea uzito wa kuhakikisha kwamba kipato chako kinatokana na njia za halali na kinawekwa mbali na uharibifu wa haramu:

“Tulikuwa na jirani. Mwanzoni alikuwa si muislamu lakini baadae aliingia kwenye uislamu. Siku moja nilipomuuliza juu ya kitu kilichomshawishi aingie kwenye uislamu alinielezea yafuatayo:

“Niliingia kwenye uislamu kutokana na maadili ya kibiashara ya jirani yangu katika ardhi anayeitwa Molla Rebi ndani ya Acibadem. Molla Rebi alikuwa ni mtu ambaye kipato chake kilitokana na kuuza maziwa. Usiku mmoja alikuja nyumbani kwetu huku akiwa na chombo kilichojaa maziwa na kusema:

‘Haya...maziwa haya ni yenu!’

‘Kwa nini iwe hivyo?’ niliuliza. ‘Sikumbuki kama nilihitaji maziwa kutoka kwako!’

Hapo ndipo mtu yule aliyebarikiwa alipoanza kuelezea:

‘Ng’ombe wangu mmoja aliingia kwenye ardhi yako na kula na mimi nilikuja kulitambua hilo baadae. Kwa sababu hiyo maziwa haya ni yako. Pia nitaendelea kukuletea maziwa yake mpaka mfumo wake wa kumeng’anya chakula usimame...kwa maneno mengine, mpaka majani na magugu aliyoyala kutoka kwenye ardhi yako yaishe kabisa kwenye mfumo wake.’

‘Usiseme hivyo rafiki yangu, majani ni majani. Sikudai chochote...’ alisema. Lakini Molla Rebi hakuyachukulia maneno yale kuwa ni jibu.





‘Hapana kabisa’ alisema. ‘Maziwa haya ni yako bila shaka!’ Hivyo akakiweka kile chombo cha maziwa kwenye mikono yangu na kuendelea kuniletea kwenye siku zilizofuatia mpaka mfumo wa mmeng’enywa wa yule ng’ombe ulipokoma.

Nilivutiwa sana na tabia yake. Matokeo yake mapazia ya ujinga yali-yokuwa yamefunika macho yangu yakafunuka na jua la uongofu likamulika ndani ya moyo wangu. Nikajifikiria kichwani mwangu, ‘...dini inayosababisha maadili kama hayo lazima itakuwa ni dini tukufu; na hakuna mtu atakayeweza kutilia shaka usahihi wa dini inayowanyanyua watu kiimani kiasi hicho.’ Hivyo nikaitaja *kalima-i tawhid* na kuwa muislamu.”

Mafunzo haya ya hekima yanadhihirisha umuhimu na tahadhari ambayo hatuna budi kuitambua kuhusiana na kutafuta kipato cha halali na kujiepusha na kila lenye kusababisha haramu. Kwani vipato vya halali ni moja wapo ya nguzo kuu za uchamungu. Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema:

“Mfanyabiashara muaminifu yuko katika daraja la Mitume, watu wema (*siddiq*) na mashahidi.” (Tirmidhi, Buyu, 4).

Mfanyabiashara mwenye moyo safi ambaye amepata bahati ya kutajwa pamoja na Mitume, watu wema na mashahidi huwa sababu ya amani na baraka kwa watu wanaomzunguka na yeye mwenyewe hupata furaha ya hapa duniani na kesho akhera. Na wale ambao ni waathirika wa tamaa ya kidunia hupewa umasikini katika maisha ya milele, hata kama wataonekana kuishi katika maisha yenye kuvutia kiasi gani hapa ardhini.

Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – anasema tena:

“Utafikia wakati ambao hakuna mtu atakayezingatia ikiwa kipato chake ni cha halali au cha haramu.” (Bukhari, Buyu, 7,23)

Hivyo katika masiku na miaka hii ambayo hatari alizozitaja Mtume – rehema na amani ziwe juu yake – zinatapakaa kwa kasi, na wakati ambao hatari hizo hazionekani zikimuachilia mtu licha ya mtu huyo kujitahidi kujiepusha nazo, kushikamana na halali linakuwa ndilo suala la msingi na kuwa amali kubwa kuliko amali zote za ibada.





Nyoyo zilizofanikiwa kutekeleza amali hii na kubakia kwenye msimamo katika hali ya utii na unyenyekevu kwenye amri za Mwenyezi Mungu Mtukufu huwa ni chanzo cha wema na uongofu, kama waridi ambalo linapitia kwenye miba mingi kabla ya kuchanua. Kinyume chake nyoyo zilozama kwenye haramu na vitu vyenye kutia mashaka zinakuwa zimejiweka miongoni mwa miba huku zikizuia uwezo wa kuchanua; na kwa namna hiyo zimekuwa tuta la uovu na tabia mbaya.

**Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu atulinde sote!**

**Amin...**





**T**isawwuf ni raha...wale tu wenye kuidiriki ndio ndio wanaoweza kufahamu.



## MUKHTASARI

### Katika neno

Kunapatikana hekima kubwa katika ufunuo ufuatao kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu mpaka kwa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake:

“Ameuteremsha Roho muaminifu (Qur’an), Juu ya moyo wako, ili uwe katika Waonyaji.” (as-Shuara, 193-194)

Kiini cha hekima zote kimegemea kwenye ukweli kwamba elimu zote, hasa elimu na hekima takatifu, zinaweza kustawi katika ulimwengu wa kiroho. Kwa maneno mengine ni kwamba elimu hudhihirisha maana yake na uzuri wake wa ndani kwa kupitia nyoyo zilizojava mapenzi, furaha na shauku. Suala hili linabainika katika nukuu ifuatayo ya mtazamo wa kisufi:

“Elimu ni suala la msingi lakini lengo la kuipata si linguine bali kwa ajili ya kutenda amali njema. Jambo hili limegemea katika siri ya kushikamana na amri za Mola wakati wote (*tazim li-amrillah*) na kuwahurumia viumbe wake wote (*shafqah li-khalqillah*) Kinyume na hayo elimu si chochote bali mzigo usio na faida.”

Hivyo elimu yote iliyoandikwa ni kama mbegu. Kama haitapanda na kinyume chake ikabakia ghalani itabakia kuwa mbegu, haitajalisha itapitiwa na miaka mingapi. Vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa elimu isiyopandwa ndani ya ulimwengu wa kiroho na badala yake ikawa imebakia kwenye safu za vitabu kabatini. Kinyume chake mbegu zilizopandwa katika ardhi hustawi kulingana na uwezo wake wa ndani na nyingi huishia kuwa safu za miti mingi. Mbegu za elimu zilizopandwa ndani ya udongo wa moyo hukua na kuwa mabustani ya imani na baada ya hapo ndipo matunda ya





elimu na hekima huwa tayari kwa ajili ya kuchumwa.

Ndio maana Qur'an tukufu iliteremshwa kwenye moyo wa Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – na maswahaba wakasoma maonyo na maamrisha matakatifu si kutoka kwenye mistari ya vitabu bali moja kwa moja kutoka kwenye moyo wa Mtume – rehema na amani ziwe juu yake. Kwa kufanya hivyo nyoyo na macho yao yaliweza kumulikwa na ubainifu mwingi wa neno takatifu uliopo ndani ya moyo huo mtakatifu, mahali ambapo uhalisia wa mambo, siri na hekima zake hupatikana. Maswahaba walishikamana katika kumuamini Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake – kwa kufuata mwenendo wake bora. Kwa msingi huo mwenendo wa kisufi umekuwa ni kuuweka uislamu hai kiimani kwa kusambaza utambuzi uliomulikwa na chanzo ambacho ni Mtume aliyebarikiwa – rehema na amani ziwe juu yake – mpaka kwenye nyoyo za watakatifu na hatimae kufikia kwenye miaka na karne zijazo.

Hivyo upande wa kisheria wa uislamu ndio nguzo kuu ya jengo hili, vipengele vyake vya uchamungu husimama kama visaidizi vilivyojengwa kuzizunguka nguzo, visaidizi hivi ni vyenye kulifanya jengo hilo lipendeze na kuvutia. Kwa kuviunganisha vipengele vyote hivi, *tasawwuf* si tu inaelezea misingi ya matendo mema na tabia njema, bali inakwenda mbali zaidi kwa kufunua siri za mwanadamu, maisha na ulimwengu, na kumuwezesha mwanadamu aweze kutambua wajibu wake juu ya vile vitu alivyopewa kuvisimamia, Licha ya kuwa na ubora huu unaolingana na maswali ya mapenzi matakatifu (*mahabatullah*) na elimu (*marifatullah*), pia mwenendo wa kisufi ni kama dirisha ndani ya moyo ambalo limefunguka kuelekea mbinguni.

Kama tulivyokwishataja hapa awali *tasawwuf* imebeba uislamu ulio hai kulingana na vipimo vya wema na uchamungu ulio ndani ya moyo pamoja na tafakuri, kujizuia na maovu, kujisalimisha na mapenzi. Lakini kiini cha yote haya si cha kuelezewa sana kwani cha msingi kuyaweka yote hayo ndani ya maisha yetu kwa kadiri tuwezavyo. Ilikuwa ni jambo la kawaida kwa watu wema kumaliza ushauri wao na hekima zilizolenga kuboresha nyoyo za watu kwa kupitia uzuri na maadili matakatifu kwa maneno yafuatayo:

“Ni rahisi kusema na rahisi kusikiliza...lakini ni vigumu mno kuyafanyia kazi uliyoyasema au uliyoyasikia!”







Ukizingatia nukta hii pia kuandika ni rahisi kama ilivyo kusoma mistari iliyoandikwa; ingawa ni vigumu kuishi kulingana na mambo hayo kama mwenendo bora wa maisha yetu. Kutaja maagizo ya ‘kuwa na subira’ ni jambo gumu kwa ulimi unaolitaja; lakini ni mzigo kwa masikio ambayo yanasikia na macho ambayo yanayasoma maagizo hayo. Lakini pindi unapokuja wakati wa kuyafanyia kazi maagizo hayo baada ya kuwa tayari mtu ameshachoshwa na tabu na magumu mbalimbali, watu wengi huona watapata tabu zaidi na matokeo yake huchagua njia ya kuyapuuza. Kwa hiyo cha msingi hapa si kujifunza wala kufundisha elimu hiyo ya *tasawwuf* lakini ni kuyachukulia kama mambo muhimu ambayo yatahuisha nyoyo zetu.

Mwenyezi Mungu Mtukufu ndani ya Qur’an anawaalika waja wake kwenye matendo mema kama ifuatavyo:

“Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni ni nani miongoni mwenu mwenye vitendo vizuri zaidi. Na Yeye ni Mwenye nguvu na Mwenye msamaha...” (al-Mulk, 2)

Cha msingi ni kwamba aya hii ya Qur’an haikutoa maneno kama vile ‘mwenye elimu zaidi’ au ‘mwingi wa maneno’ au hata ‘mbora zaidi katika kusikiliza’, lakini imesema ‘mwenye vitendo vizuri zaidi’, vitendo ambavyo si vingine isipokuwa amali njema.

Hivyo lengo kuu la msingi la usufi ni kustawisha petali za moyo kwa kupitia hekima, uchamungu na upendo ili kuhakikisha kuwa mwanadamu anaungana na Mola wake kabla ya kuzama katika jangwa la ujinga ambalo ndio maisha ya hapa duniani. Kuutambua na kuufanyia kazi uhalisia huu ni sawa na kuutambua na kuishi katika mwenendo wa kisufi. Kwani wakubwa katika *tasawwuf* wanasema:

“*Tasawwuf* ni ladha...wale tu wenye kuionja ndio wenye kuweza kuitambua!”

Hivyo kiini cha mwenendo wa kisufi kama tulivyokwishajaribu kuelezea kinahusiana na kumtumikia Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kadiri iwezekanavyo na kufanya maandalizi ya makusudi kwa ajili ya maisha ya akhera. Kwa ufupi *tasawwuf* ni kuishi kiutumishi kwa kadiri ya uwezo wako, kwani Mola amemuumba mwanadamu si kwa lengo lingine bali kumtumikia yeye. Kwa hiyo usufi unahusiana na kuondoa vikwazo vili-





vyopo kwenye njia ya kati mwanadamu na utumishi na kupata sababu za kumuwezesha kuwa mtumishi. Usufi hufunika majeraha ya wengi na kuufanya udongo mkavu kuwa na mabustani ya maua yenye kupendeza na kuvutia, na pia hugeza moyo mpweke kuwa kasri lenye kuvutia. Kwa ufupi ni kwamba, wakati tunapokuwa tunasafiri katika njia hii ya utengano kuelekea kwenye ulimwengu wa makutano, *tasawwuf* inakuwa ni njia ili-yopakwa dhahabu ambayo inampatia mwanadamu funguo za kumuwezesha kuwa 'mtumishi bora' mbele ya Mola.

Jukumu linalotungoja si lingine bali kuitupilia mbali nafsi na mambo yake yote na kuendesha maisha ya udhalili mbele ya utukufu wa Mola. Hii ni hali inayomuingizia mtu hisia za udhalili na uaminifu kwa Mola, hisia zenye kuendelea mpaka kuunyanyua moyo mpaka kwenye kilele cha ukamilifu wa imani. Nyoyo zinazoishi kwenye kasri la udhalili kamwe haziwezi kuanguka kwenye genge la uovu kwa udhalili na aibu; kinyume chake huzipandisha kwenye vilele vya mbingu kulingana na viwango vya unyenyekevu na kwa kiwango ambacho zimezikandamiza nafsi. Shairi lifuatalo linalielezea jambo hili kwa uzuri zaidi:

*Kwa kudondoka kwenye ardhi kwa unyenyekevu mbegu hubarikiwa,  
Kwa rehema za Mwingi wa rehema unyenyekevu huo hupanda.*

**Ewe Mola...Tujaalie tuwe miongoni mwa wale uliowasifu kama 'watumishi bora'! Zijaalie nyoyo zetu ambazo tunajitahidi kuzilinda dhidi ya nafsi na matamano yake ziwe ndani ya mazingira ya unyenyekevu utokanao na rehema zako! Yapatanishe maneno yetu pamoja na nyoyo zetu na nyoyo zetu pamoja na maneno yetu! Ndani ya nyoyo zetu stawisha chipukizi za ukweli ambao tumejaribu kwa unyenyekevu kuuweka katika maneno chini ya sifa yako ya Usemi! Tujaalie tuwe miongoni mwa vipenzi vyako na waja wako wema; na utufufue pamoja nao! Tujaalie kuwa na mtazamo na mwenendo unaouridhia na usituache tufanye matendo kinyume na yale unayoyaridhia! Zipatanishe hisia zetu zote na kudura yako! Tuweke mbali na mtazamo na mwenendo ambao Wewe huupendi! Tujaalie tuongoze maisha yetu katika njia iliyonyooka kupita njia zote mpaka katika pumzi zetu za mwisho! Jaalia kazi yetu dhalili na dhaifu iwe sababu ya wema, uongofu, hekima, ukweli na elimu takatifu!**





## Bibliografia

Abdurrahman Güzel, Mustafa Tatçı, **Yunus Emre**, Ankara, 1991.

Abdülbaki Gölpınarlı, **Mesnevi ve Şerhi**, İstanbul, 1973-1974.

Abdulqadir Jilani, **al-Fathu'r-Rabbani**, (kilichotafsiriwa na Yaman Arikan), istanbul, 1987.

Abdulkarim al-Jili, **İnsan-ı Kamil**, (kilichotafsiriwa na Abdülaziz Mecdi Tolun; kilichoandaliwa na Selçuk Eraydın, Ekrem Demirli, Abdullah Kartal) istanbul, 1998.

Abdulmajid Zindani, **Kuran'da İlmi Mucizeler** (kilichotafsiriwa na Resul Tosun), İstanbul, 1995.

Abu Dawud, Sulayman ibn Ashas as-Sijistani, **Sunanu Abi Dawud**, I-V, istanbul, 1992.

Abu Nasr as-Sarraj at-Tusi, **al-Luma** ( kilichotafsiriwa na Hasan Kamil Yılmaz), istanbul, 1996.

Ajluni, ismail ibn Muhammad, **Kashfu'l-Khafa**, I-II, Beirut (hakina tarehe).

Adem Ergül, **Kalbi Hayat**, istanbul, 2000.

Ahmad ibn Hanbal, **al-Musnad**, I-IV, istanbul, 1992; **Kitabu'z-Zuhd** (kilichochapwa na Muhammad Said Basyuni Zaghlul), Beirut, 1986.

Ahmed Davudoğlu, **Sahih-i Müslim Tercüme ve Şerhi**, I-XII, İstanbul, 1979.

Ahmed ar-Rifai, **Onların Alemi** (kilichotafsiriwa na Abdülkadir Akçiçek), istanbul, 1996.

Ahmed Taşgetiren, **Altın Öğütler**, istanbul, 1992.

Ali ibn Husayn Waiz Kashifi, **Rashahat Aynu'l-Hayat** (kilichohaririwa na Ali Asghar Muiniyan), I-II, Tehran, 1977.

Ali Can Tatlı, **Zühhd Açısından Dünya Nimetleri**; istanbul, 2005.





Ali Himmet Berki, **Açıklamalı Mecelle: Mecelle-i Ahkam-ı Adliye**, istanbul, 1982.

Ali Özek, Hayrettin Karaman, Ali Turgut, Mustafa Çağrıç, İ. Kafi Dönmez, Sadreddin Gümü, **Kuran-ı Kerim ve Türkçe Açıklamalı Meali**, Saudi Arabia, 1992.

Asad Sahib, **Maktubat-ı Mawlana Khalid**, (kilichotafsiriwa na Dilaver Selvi, Kemal Yıldız), Istanbul, 1993.

Balazuri, **Ansabu'l-Ashraf**, Misri, 1959.

Baydawi, Abu Said Nasruddin Abdullah ibn Omar, Anwaru't-Tanzil wa **Asraru't-Tawil**, I-IV, Beirut, (hakina tarehe).

Bayhaki, Abu Bakr Ahmed ibn al-Husayn, **as-Sunanu'l-Kubra** (hakina tarehe),

Darul-Fikr; **Kitabu'z-Zuhdi'l-Kabir**, Beirut, 1996.

Bukhari, Abu Abdillan Muhammad ibn Ismail, **al-Jamiu's-Sahih**, I-VIII, Istanbul, 1992.

Darimi, Abu Muhammad Abdullah ibn Abdirrahman, **Sunanu'd-Darimi**, I-II, Istanbul, 1992.

Daylami, Abu Shujaa Shiruyah ibn Shahridar, **al-Firdaws bi-Ma'suri'l-Khitab**, Beirut, 1986.

Elmalılı Muhammed Hamdi Yazır, **Hak Dini Kuran Dili**, Istanbul, 1971.

Ethem Cebecioğlu, **Tasavvuf Terimleri ve Deyimleri Sözlüğü**, Ankara, 1997.

Fariduddin Attar, **Tadhkiratu'l-Awliya** (kilichoandaliwa na Süleyman Uludağ), istanbul, 1985.

Ferit Devellioğlu, **Osmanlıca-Türkçe Ansiklopedik Lügat**, Ankara, 1997.

Ghazzali, Abu Hamid Muhammad ibn Muhammad, **Ihya-u Ulumi'd-Din**, I-VI, Beirut, 1990.

Hakim, Abu Abdillan Muhammad ibn Abdillan an-Nisaburi, **Mustadrak**





**ala's-Sahihayn**, I-V, Beirut, 1990.

Hasan Basri Çantay, **Kuran-ı Hakim ve Meal-i Kerim**, I-III, İstanbul, 1996.

Hasan KamilYılmaz, **Anahatlarıyla Tasavvuf ve Tarikatlar**, İstanbul, 2000.

Hayat Neşriyat ilmi Araştırma Merkezi Meal Heyeti, **Kuran-ı Kerim ve Muhtasar Meali**, istanbul, 2001.

Hayrettin Karaman, **Ebediyet Yolcusunu Uğurlarken**, Ankara, 1999.

al-Haythami, Hafiz Nuraddin Ali ibn-Abi Bakr, **Majmau'z-Zawaid wa Manbau'l-Fawaid**, I-X, Beirut

Ibn Ataullah Iskandari, **al-Hikamul-Ataiyyah** ( kilichotafsiriwa na Saffet Yetkin), Ankara, 1963.

Ibn Hajar al-Asqalani, Shihabuddin Ahmed ibn Ali, **Hadyu's-Sari Muqad-dimatu Fathu'l-Bari Sharhi Sahihi'l-Bukhari**, I-XXVIII, (hakina tarehe); al-Isabah fi Tamyizi's-Sahabah, Misri, 1379; Munabbihat, İstanbul, 1960.

Ibn Hibban, Abu Khatim al-Busti, **al-Ihsan bi Tartibi Sahihi Ibn-i Hibban**, I-X, Beirut, 1987.

Ibn Hisham, **as-Siratu'n-Nabawiyah**, Beirut, 1992.

Ibn Jawzi, Abu'l-Faraj Abdurrahman ibn Ali ibn Muhammad, **Manaqibu'l-Imam Ahmed ibn Hanbal** (kilichoandaliwa na Abdullah ibn Abdulmuh-sin at-Turki), Cairo, 1409.

Ibn Kathir, Imaduddin Abu'l-Fida, **Tafsiru Qurani'l-Azim**, I-IV, Beirut, 1988; **al-Bidayah wa'n-Nihayah**, I-XV, Cairo, 1993; **as-Siratu'n-Nabawiyah**, I-IV, Cairo, 1964.

Ibn Majah, Abu Abdillah Muhammad ibn Yazid al-Qazwini, **Sunanu Ibn Majah**, İstanbul, 1992.

Ibnu Abdilbarr, Abu Omar Yusuf ibn Abdullah ibn Muhammad, **al-Istiab fi Marifati'l-Ashab**, I-IV, Cairo (hakina tarehe).

Ibnu'l-Asir, Muhammad ibn Abdulkarim ibn abdulwahid as-Shaybani, **al-Kamil fi't-Tarih**, I-XIII, Beirut, 1965.

Ibrahim Canan, **Hadis Ansiklopedisi**, I-XVIII, İstanbul, (hakina tarehe).





İlhan Armutçuoğlu, **Kaside-i Bürde Manzum Tercümesi**, Konya, 1983.

Imam Malik, **Muwattaa**, I-II, Istanbul, 1992.

Ismail Fenni Ertuğrul, **Vahdet-i Vücut ve İbn-i Arabi** (kilichoandaliwa na Mustafa Kara), istanbul, 1991.

İsmail Hakki Bursevi, **Ruhu'l-Beyan**, I-IX, istanbul; Kenz-i Mahfi, istanbul, 1727.

Kadir Mısıroğlu, **Külliyat**, Sebil Yayınevi.

Kalabazi, Taj u'l-Islam Abu Bakr Muhammad ibn Ishaq Bukhari, **at-Taaruf li Madhhabi Ahli't-Tasawwuf**, (kilichotafsiriwa na Süleyman Uludağ), istanbul, 1992.

M. Aziz Lahbabi, **İslam Şahsiyetçiliği** (kilichotafsiriwa na İ. Hakki Akın) ö istanbul, 1972.

Mahir İz, **Tasavvuf**, istanbul, 1969; **Yılların İzi**, istanbul, 1975.

Mahmud Sami Ramazanoğlu, **Külliyat**, Erkam Yayınlan.

**Majmuul-Hadith**, Damascus Maktabatu'z-Zahiriyah Library, no: 59.

Maqdisi, Izzuddin Abdussalam, **Sırların Çözümü ve Hazinelelerin Anahtarları**, (kilichotafsiriwa na Hayri Kaplan), istanbul, 2001.

Mawlana Sheikh, **Manağib-i Khawajah Ubaydullah-i Ahrar**, Bayazid, Maktaba ya taifa, Bayazid Section, no: 3624.

Mecdi Mehmed, **Hadaiku's-Şakaik**, Istanbul, 1853.

Mehmed Doğan, **Büyük Türkçe Sözlük**, istanbul, 1994.

Mehmed Niyazi, **Çanakkale Mahşeri**, istanbul, 1999.

Molla Jami, **Nafakhatu'l-Uns**, (kilichorahisishwa na Abdülkadir Çiçek), istanbul, 1981.

Muhammad Abid al-Jabiri, **Arap-İslam Kültürünün Akıl Yapısı**, istanbul, 1999.

Muhammad ibn Abdullah al-Hani, **Adab**, istanbul, 1995.

Muhammad Abu Zahra, **İbnu Taymiyyah Hayatuhu wa Asruhu wa Fikruh**, Beirut, (hakina tarehe).





Muhammad Asad, **Kuran Mesajı**, (kilichotafsiriwa na Cahid Koytak, Ahmet Ertürk), Mil, Istanbul, 1999.

Muhammad Fuad Abdulbaqi, **al-Mujamu'l-Mufahras li Alfazi'l-Qurani'l-Karim**, Cairo, 1988.

Muhammad Hamidullah, **İslam Müesseselerine Giriş**, Istanbul, 1981.

Muhammad Salih az-Zarqan, **Fakhruddin ar-Razi ve Arauhu'l-Kalamiyya wal-Falsafiyya**, Beirut, 1963.

Muhammed Esad Erbili, **Mektubat**, (kilichorahisishwa na H. Kamil Yılmaz, İrfan Gündüz), istanbul, 1983; **Risale-i Esadiyye**, Dersaadet, 1924.

Munawi, Muhammad Abdurrauf, **Fayzu'l-Qadir Sharhu'l-Jamii's-Saghir**, I-IV, Beirut, 1994.

Mundhiri, Abdulazim ibn Abdulqawi, **at-Tarhib wa't-Tarhib**, I-IV, Cairo, 1934.

Muslim, Abu'l-Husayn ibn Hajjaj al-Qushayri, **al-Jamiu's-Sahih**, I-III, Istanbul, 1992.

Mustafa Kara, **Metinlere Günümüz Tasavvuf Hareketleri**, istanbul, 2002.

Nasai, Abu Abdirrahman Ahmed ibn Shuayb, **Sunanu'n-Nasai**, I-VIII, istanbul, 1992.

Nawawi, Abu Zakariyya Yahya ibn Sharaf, **Riyadu's-Salihin**, Beirut; **Riyazu's-Salihin** (kilichotafsiriwa na kufafanuliwa na Yaşar Kandemir, İsmail Lütü Çakan, Raşit Küçük), I-VIII, istanbul, 1997; Sharhu Sahih-i Muslim, I-XVIII, Misri, 1981.

Necip Fazıl Kisakürek, **Veliler Ordusundan 333**, istanbul, 1976; **Reşahat (Şeyh Safiyyüddin)**, istanbul, 1995.

Nurettin Topçu, **M evlana ve Tasavvuf**, istanbul, 1998.

Osman Nuri Topbaş, **Külliyat**, Erkam Yayınları.

Ömer Rıza Doğrul, **İslamiyetin Geliştirdiği Tasavvuf**, istanbul, 1948.

Qurtubi, Abu Abdillan Muhammad ibn Ahmed, **al-Jami li Ahkam'i'l-Quran**, I-XX, Beirut, 1985.

Qushayri, Abdulkarim, **ar-Risalatü'l-Qushayriyyah**, Beirut, 1990.





Razi, Fakhruddin Muhammad ibn Omar, **Mafatihul-Ghayb (at-Tafsiru'l-Kabir)**, I-XXXII, Beirut, 1990.

Roger Garaudy, **İslam'ın Vaad Ettikleri** (kilichotafsiriwa na Nezih Uzel), Istanbul, 1983.

Rudani, Imam Muhammad ibn Muhammad ibn Sulayman, **Jamu'l-Fawaid**, (kilichotafsiriwa na Nairn Erdoğan), Istanbul, 1996.

Sadık Dâna, **Külliyat**, Erkam Yayınları.

Sayyid Sharif Jurjani, **Kitabu't-Tarifat**, Beirut, 1990.

Selçuk Eraydın, **Tasavvuf ve Tarikatlar**, Istanbul, 1994.

Suat Yıldırım, **Kuran'da Uluhiyyet**, istanbul, 1987.

Subqi, Taqiyyuddin Abu'l-Hasen Ali, **Shifau's-Saqam fi Ziyarati Khayri'l-Anam**, Misri, 1318.

Suyuti, Abu'l-Fadl Jalaladdin Abdurrahman ibn Abi Bakr, **al-Jamiu's-Saghir**, Misri, 1306; Sharhu's-Sudur bi Sharhi Hali'l-Mawta wa'l-Qubur, istanbul, 1986; **Sharhu ibn Majah**, Karachi, (hakina tarehe).

Süleyman Ateş, **İslam Tasavvufu**, Ankara, 1972.

Süleyman Uludağ, **Tasavvuf Terimleri Sözlüğü**, istanbul, 1991.

Şefik Can, **Mesnevi Tercümesi**, I-VI, istanbul, 1997.

Sheikh Ashraf Ali Tanawi, **Hadislerle Tasavvuf** (kilichoandaliwa na Zaf-erullah Davudi, Ahmed Yıldırım), istanbul, 1995.

Sheikh Sadi Shirazi, **Bostan**, istanbul, 1995.

Shihabuddin Ahmed ibn Hajar al-Haytami al-Makki, **Khayratul-Hisan fi Manaqibi'l-Imam'l-Azam Abi Hanifati'n-Numan**, Beirut, 1983.

at-Tabarani, al-Hafiz Abu'l-Qasim Sulayman ibn Ahmed, **al-Mujamu'l-Kabir**, I-XXV, 1983.

Tabari, Abu Jafar Muhammad ibn Jarir, **Jamiu'l-Bayan an Tawili Ayi'l-Quran**, Beirut, 1995.

Tahanawi, Muhammad Ala ibn Ali, **Kashshafu Istilahati'l-Funun**, Beirut, 1861.







Tahiru'l-Mevlevi, **Şerh-i Mesnevi**, I-XIV, İstanbul, 1963-1973.

Tirmidhi, Abu İsa, Muhammad ibn İsa, **Sunanu't-Tirmidhi**, I-IV, İstanbul, 1992.

Waqidi, **Maghazi**, Misri, 1948.

Zekeriya Güler, “**Vesile ve Tevessül Hadislerinin Kaynak Deęeri**”, Jarida la taaluma la ILAM, January-June, 1997, tol. 2, na. 1, uk. 83-132.





# YALIYOMO

Dibaji .....7

## SURA YA KWANZA

USUFI NI NINI? ..... 13

A. ASILI YA USUFI..... 13

B. TAFSIRI YA USUFI ..... 30

1. Mwenendo wa kisufi unawakilisha mfano wa maaadili (*akhlaq*) na adabu (*adab*)..... 31

2. Mwenendo wa kisufi unahusiana na kuutakasa moyo na nafsi... 34

3. Mwenendo wa kisufi ni mapambano ya kiroho yasiyoisha. .... 37

4. Usufi unamaanisha usafi wa moyo (*ikhlas*)..... 38

5. Usufi unamaanisha kusimama kwa ushupavu katika njia iliyonyooka (*istiqamah*)..... 41

6. Mwenendo wa kisufi ni (*rida*) na kujisalimisha (*taslimiyyah*) ..... 44

C. MADA YA USUFI..... 49

D. LENGU LA USUFI ..... 51

E. ULAZIMA WA KUFUATA USUFI..... 54

F. UHUSIANO KATI YA USUFI NA FIKRA NYINGINE ZA KIELIMU .....70

1. USUFI NA FIKRA NYINGINE ZA KIISLAMU ..... 70





a. Usufi na Thiolojia.....	71
b. Usufi na ufafanuzi wa Qur'an ( <i>Tafsir</i> ) .....	73
c. Usufi na maneno na matendo ya Mtume aliyebarikiwa- rehema na amani ziwe juu yake - ( <i>Hadith-Siyar</i> ) .....	76
d. Usufi na sheria ya kiislamu ( <i>fiqh</i> ).....	78
2. USUFI NA SAYANSI ASILIA.....	81
3. USUFI NA FASIHI .....	86
4. USUFI NA SANAA.....	89
a. Musiki .....	89
b. Usanifu majengo .....	91
c. Kaligrafia .....	93
5. USUFI NA FALSABA.....	96
G. ELIMU YENYE MANUFAA .....	101

### SURA YA PILI

Mafunzo ya Usufi ( <i>Sayr Suluk</i> ).....	113
A. NAFSI (NAFS) NA UTAKASO WAKE (TAKZIYA).....	118
1. UHALISIA WA NAFSI .....	118
2. UTAKASO WA NAFSI.....	123
a. Utakaso kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.....	127
b. Utakaso kutoka kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu – rehema na amani ziwe juu yake .....	129
c. Mtu kuitakasa nafsi yake mwenyewe .....	131
3. HALI ZA NAFSI .....	139
a. Nafsi yenye kuamrisha maovu ( <i>an-nafsu'l-ammara</i> ).....	139
b. Nafsi yenye kujilaumu ( <i>an-nafsu'l-lawwama</i> ).....	146
c. Nafsi iliyopokea ufunuo ( <i>an-nafsu'l-mulhama</i> ).....	149





d. Nafsi tulivu ( <i>an-nafsu'l-mutmainna</i> ) .....	152
e. Nafsi iliyoridhia ( <i>an-nafsu'r-radhiya</i> ) .....	155
f. Nafsi iliyoridhiwa ( <i>an-nafsul-mardhiyya</i> ) .....	158
g. Nafsi kamilifu ( <i>an-nafsu'l-kamila</i> )/ nafsi safi ( <i>an-nafsu's-safiya</i> ).....	160
<b>B. MOYO NA UTAKASO WAKE .....</b>	<b>162</b>
1. TABIA YA MOYO .....	162
2. AINA ZA NYOYO .....	169
a- Nyoyo ambazo zinafuata lengo na heshima ya kuumbwa kwake. ....	169
b- Nyoyo zilizopigwa muhuri na kufa .....	172
c. Nyoyo zenye maradhi na zisizozingatia mambo .....	174
3. UTAKASO WA MOYO .....	178
a. Chakula cha halali .....	178
b. Toba na dua .....	183
c. Kuisoma Qur'an na kutii maamrishi yake.....	188
d. Kufanya ibada kwa umakinifu wa hali ya juu ( <i>khushuu</i> ) ...	193
e- Kuhuisha nyakati za usiku .....	204
f- <i>Dhikrullah</i> na <i>Muraqaba</i> .....	208
g- Upendo juu ya Mtume Mtukufu – rehemu na amani ziwe juu yake – na <i>Salawat-u Sharifa</i> .....	214
h. Kutafakari juu ya mauti .....	222
i. Kukaa pamoja na watakatifu na watu wema.....	229
j. Kujipamba na maadili mema .....	240
4. KUUTAZAMA ULIMWENGU KWA MOYO SAFI.....	247
<b>C. KANUNI ZA MSINGI ZA MAFUNZO YA KISUFI.....</b>	<b>253</b>
<b>D. MURSHID-IKAMIL NA NJIA ZA KUONGOKA KIROHO .....</b>	<b>261</b>
1. MURSHID-IKAMIL .....	261





2. NJIA ZA MWONGOZO WA KIROHO.....	271
a. <i>Mahabbah</i> (Upendo) na <i>Rabitah</i> .....	271
b. Mkusanyiko wa kiroho ( <i>Sohbah</i> ).....	281
c. Huduma .....	288
d. Utegemezi wenye kupendekezwa ( <i>Tawajjuh</i> ).....	295
e. Maombi (Dua) .....	300
E. UPEKEE WA USUFI .....	304
1. NAMNA YA MUONGOZO NA REHEMA.....	304
2. NAMNA YA UPOLE NA UPENDO.....	315

### SURA YA TATU

MARIFATULLAH NA MALIPO MATAKATIFU .....	329
A. MARIFATULLAH AU KUMFAHAMU ALLAH .....	329
1. DHATI TAKATIFU .....	329
2. SIFA TAKATIFU NA UBAINIFU WAKE.....	339
3. KUMFAHAMU MOLA NA UBAINIFU WAKE KWAWENYE HEKIMA .....	367
1. ELIMU YA <i>LADUNNI</i> .....	375
2. UTAMBUZI WA KIROHO ( <i>FIRASAH</i> ) .....	406
3. UDHIBITI WA KIROHO ( <i>TASARRUF</i> ) NA <i>KARAMAH</i> .....	409
4. NDOTO ZA KWELI.....	427

### SURA YA NNE

BAADHI YA MASWALI KUHUSIANA NA USUFI .....	439
A. KUOMBEA ( <i>TAWASSUL</i> ).....	439
B. KUTAFUTA BARAKA ( <i>TABARRUK</i> ).....	455





C. KUTEMBELEA MAKABURI..... 468

**SURA YA TANO**

USHAURI KUTOKA KWA WATU WEMA ..... 483

**SURA YA SITA**

SIMULIZI ZA KISUFI NA MAFUNZO YAKE ..... 503

Elimu ya kweli ..... 504

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 504

Kanuni katika mafunzo ya kiroho..... 505

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 506

Ibrahim ibn Adham na mtoto wa paa ..... 506

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 508

Kutoitia doa njia ya Mola..... 509

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 509

Karamah ..... 510

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 511

Kuziathiri nyoyo za wajinga..... 511

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 512

Mlango wa rafiki ..... 513

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 514

Kutii, Kuhudumia, Kushauri ..... 514

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 515

Kuwahudumia viumbe..... 516

Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:..... 517

Kuwaheshimu watu wema..... 517



Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	518
Utashi mbele ya Mola.....	518
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	519
Adabu.....	520
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	520
Adabu katika kuhudumia .....	521
Mafunzo tunayoyapata kutokana na kisa hiki: .....	521
Adabu...Hata iweje .....	522
Mafunzo yatokanayo na kisa hiki: .....	522
Maadili na huduma ya mtu mwema .....	523
Mafunzo yatokanayo na kisa hiki: .....	524
Waache wanaokufa wafahamu, sio walio hai! .....	525
Usimdharau mtu yeyote!.....	525
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	526
Usimlaumu yeyote!.....	526
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	526
Kuwachangamkia mayatima .....	527
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	528
Urafiki.....	528
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	529
Lengo la urafiki .....	530
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	530
Kujisalimisha moja kwa moja.....	531
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	531
Kupokea maombi ya muumini .....	532
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	533







Majzub na tiba ya moyo wenye maradhi.....	534
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	534
Sura kama malaika.....	535
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	536
Hali ya moyo wakati wa sadaka .....	536
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	537
Matendo mema ambayo yanakifikia kiti cha enzi .....	538
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	539
Kumtambua Mola wakati wote .....	539
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	540
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	541
Jukumu la mtangulizi.....	542
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	542
Kuhudhuria mwaliko wa Mola .....	543
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	543
Umuhimu wa Halal .....	543
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	545
Kipato cha halali.....	546
Mafunzo yanayopatikana katika kisa hiki:.....	547
MUKHTASARI .....	549
BIBLIOGRAFIA .....	553



